

Minhajil Muslim

Kimeandikwa:

Sheikh Abubakar Jabir-al-Jazair

Kimetafsiriwa:

Japo la Wanavyuoni wa Kiislamu

Minhajil Muslim

Tafsiri ya *Minhajil Muslim*

©Bright House Ltd.

Kimefasiriwa Toka Kiarabu:

Jopo la Masheikh

Kimehaririwa na:

Hassan Mnjeja, Said Bawazir,
Yusuf Rajab, Khatib Giragiza,
Yassir Salim na Khalfan Njama.

Typesetting:

Ally Said Abdallah.

Kimechapishwa:

Kauthar Printers,
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam.

Haki Zote Zimehifadhiwa Hairuhusiwi Kupiga Chapa Kitabu hiki kwa Jinsi Yoyote
ile Bila Idhini ya Wachapishaji kwa Maandishi

Yaliyomo:

Yaliyomo.....	3
Utangulizi (Kiswahili).....	6

Mlango wa Kwanza: Katika Itikadi8

Mada ya 1	Kumuamini Allah Mtukufu.....	9
Mada ya 2	Kamuamini Uungu wa Allah Kwa Kila Kitu.....	15
Mada ya 3	Kuamini Uungu wa Allah Kwa Watu.....	26
Mada ya 4	Kuamini Majina Yake Na Sifa Zake Tukufu.....	30
Mada ya 5	Kuamini Malaika juu Yao Amani.....	36
Mada ya 6	Kuamini Vitabu vya Allah.....	42
Mada ya 7	Kuamini Qur'an Tukufu.....	47
Mada ya 8	Kuamini Mitume wa Allah.....	53
Mada ya 9	Kuamini Utume wa Mtume.....	59
Mada ya 10	Kuamini Siku ya Mwisho.....	74
Mada ya 11	Adhabu za Kaburi na Raha Zake.....	86
Mada ya 12	Kuamini Hukumu na Uwezo wa Allah.....	90
Mada ya 13	Kumpwekesha Allah Katika Ibada.....	97
Mada ya 14	Kinahusu Wasilah.....	103
Mada ya 15	Mawalii wa Allah.....	110
Mada ya 16	Wajibu wa Kuamrisha Mema.....	123
Mada ya 17	Wajibu wa Kuwapenda Maswahaba.....	131

Mlango wa Pili: Katika Adabu na Heshima143

Mada ya 1	Adabu za Nia.....	144
Mada ya 2	Adabu na Allah.....	148
Mada ya 3	Adabu na Maneno ya Allah.....	155
Mada ya 4	Adabu na Mtume.....	160
Mada ya 5	Adabu na Nafsi.....	166
Mada ya 6	Adabu na Viumbe,.....	178
Mada ya 7	Adabu za Undugu kwa Ajili ya Allah.....	222
Mada ya 8	Adabu za Kukaa na Kikao.....	228
Mada ya 9	Adabu za Kula na Kunywa.....	232

Minhajil Muslim

Mada ya 10	Adabu za Kumkaribisha Mgeni.....	238
Mada ya 11	Adabu za Safari.....	242
Mada ya 12	Adabu za Kuvaa.....	249
Mada ya 13	Adabu za Mambo ya Maumbile.....	255
Mada ya 14	Adabu za Kulala.....	258

Mlango waTatu: Tabia.....263

Mada ya 1	Tabia njema na Maelezo Yake.....	264
Mada ya 2	Tabia ya Kusubiri na Kuvumilia Maudhi.....	268
Mada ya 3	Tabia ya Kumtegemea Allah Mtukufu.....	273
Mada ya 4	Tabia ya Kuwafadhilisha Wengine.....	279
Mada ya 5	Tabia ya Uadilifu na Unyoofu.....	285
Mada ya 6	Tabia ya Huruma.....	290
Mada ya 7	Tabia ya Kuona Haya.....	294
Mada ya 8	Tabia ya Kufanya Wema.....	298
Mada ya 9	Tabia za Ukweli.....	302
Mada ya 10	Tabia ya Utoaji na Ukarimu.....	307
Tabia ya 11	Unyenyekevu na Kukiponda Kibri.....	313
Mada ya 12	Tabia Mbaya, Dhulma, Hasadi n.k.....	318

Mlango wa Nne: Kuhusu Mambo ya Ibada.....334

Mada ya 1:	Kuhusu Tohara.....	335
Mada ya 2:	Adabu za Kukidhi Haja.....	339
Mada ya 3:	Udhu.....	343
Mada ya 4:	Kuoga Janaba.....	353
Mada ya 5:	Tayammam.....	360
Mada ya 6:	Kupaka Juu ya Khofu Mbili na Bandeji.....	364
Mada ya 7:	Hukumu ya Hedhi na Nifasi.....	367
Mada ya 8 :	Katika Swala.....	373
Mada ya 9:	Hukumu ya Jeneza.....	450
Mada ya 10:	Kutoa Zaka.....	474
Mada ya 11:	Katika Funga.....	497
Mada ya 12:	Kinahusu Hijja na 'Umra.....	523
Mada ya 13:	Ziara katika Msikiti wa Mtume.....	552
Mada ya 14:	Udhhiya na 'Aqiqa.....	561

Mlango wa Tano: Katika Muamalaat.....	570
Jihadi.....	571
Katika Mashindano ya Kulenga Shabaha.....	600
Katika Kuuza na Kununua (Biashara).....	607
Kuhusu Mikataba.....	638
Katika Jumla za Hukumu.....	676
Ndoa Talaka, Rejea, Khulu, Lliaani	713
Mirathi.....	777
Yamini na Nadhiri.....	828
Kuchinja.....	838
Jinai na Hukumu zake.....	854
Ukadhi.....	901
Utumwa.....	914



Utangulizi:

Bismillahir Rahmanir Rahiim

Shukrani zote anastahiki Allah ambaye kwa neema zake matendo mema yanatimia; na Sala zetu na Salamu zimwendee mbora wa viumbe Muhammad ﷺ na Ahli zake na Sahaba zake wote.

Kutokana na maombi mengi na mapenzi ya ndugu zetu Waislamu katika kutaka kufahamu Dini yao, na utamaduni wake uliojikita katika fani mbalimbali za Elimu kutoka katika marejeo yake makuu. Kutokana pia na uhaba mkubwa uliopo wa vitabu vilivyofasriwa katika lugha ya Kiswahili. Tumeona kuwa tukitafsiri kitabu hiki katika lugha hii. Kitabu ambacho kimekusanya Maarifa mapana ya Elimu nyingi juu ya Uislamu na Sheria zake.

Elimu iliyopo katika kitabu hiki ni kama mfumo au kanuni zinazo jumuishia mambo yote muhimu anayopaswa kuyajua Muislamu Mwema kuhusu Itikadi, Adabu, Maadili, Ibada, Maingiliano na Matengamano mbalimbali na nduguze.

Kitabu hiki *Minhajil Muslim* ni kitabu miongoni mwa vitabu rejea. Mtunzi wa kitabu hiki ni Mwanazuoni *Al-Alaama* Sheikh, Abubakar al-Jazair. Kitabu hiki kimekusanya mengi anayoyahitaji Muislamu katika Dini yake.

Njia aliyotumia Mtunzi wa kitabu hiki ni mfumo wa kati na kati katika kutimiza mambo ya Dini. Katika Itikadi hakutoka nje ya itikadi ya watu wema waliotangulia (*as-salafu as-swalih*) kwani hiyo ndiyo Itikadi ya Mtume ﷺ, Maswahaba wake na wanaofuata baada yao.

Katika masuala ya *Fiqhi* na haswa katika *Fiqh* ya ibada na muingiliano na watu mwandishi alitegemea maneno ya Maimamu waliobobea kama vile Imam Hanifa, Malik, Shafii na Ahmad (Rehema za Allah ziwaendee wote).

Lugha iliyotumika katika kitabu hiki cha *Minhajil Muslim* ni lugha nyepesi na inayofahamika. Ni matarajio yetu kuwa Waislamu wengi wataweza kukipata kitabu hiki na kufaidika nacho. Hili ndilo la muhimu zaidi kulifanyia kazi. Yote yaliyomo ndani ya kitabu hiki miongoni mwa: Hukumu, Maelezo, Adabu, Maadili

na kadhalika ni ya kufanyiwa kazi ili yaweze kuwaunganisha Waislamu wema na Wacha Mungu katika njia ambayo itakusanya nguvu zao, fikra zao na mwisho roho zao na hisia zao katika kusimamisha Sheria bora za Kiislamu na Maadili yake mazuri.

Kazi ya kufasiri kitabu hiki imefanywa na jopo la Masheikh weledi wa lugha ya Kiarabu na Kiswahili. Wameifanya kazi hii kwa uhodari na uaminifu mkubwa.

Washiriki wa Jopo hili ni hawa wafuatao:

1. Sheikh Muharram Juma Doga (B.A.) Chuo cha Sharia ya Kiislamu
2. Sheikh Twaha Suleyman Bane (B.A.) Chuo cha Sharia ya Kiislamu
3. Sheikh Omar Ally Kama (B.A.) Chuo cha Sharia ya Kiislamu
4. Sheikh Abdallah S. Ramadhan (B.A.) Chuo cha Hadithi Tukufu
5. Sheikh Amran S. Kilemile (B.A.) Chuo cha Lugha ya Kiarabu
6. Sheikh Hashim A. Rusaganya (B.A.) Chuo cha Da'wa na Usul
7. Sheikh Khatibu Mussa Giragiza (M.A.) Chuo cha Lugha ya Kiarabu
8. Dr.Hamdun I.Sulayman (PhD)

Kitabu hiki kimehaririwa na Khatib Giragiza, Yusuf Rajab, Ust. Hassan Mnjeja, Ust. Said Bawazir na Ust. Yassir Salum.

Katika chapa hii ya 2013 kitabu hiki kimehaririwa tena kwa mara ya pili na Ust. Said Bawazir na Yassir Salim. Pia tumeamua kukichapisha katika kitabu kimoja, sio kama chapa zilizopita katika vitabu vitatu kwa lengo la kuwarahisishia wasomaji wetu.

Chapa hii ya 2013, tumekiboresha kitabu kwa kuweka aya zote zilizotumika kwa kiarabu na kukipangilia kwa mpangilio mzuri wenye kuvutia.

Allah awape kheri duniani na kesho akhera kwa kazi hii tukufu waliyofanya. Allah ndiye mbora wakukusudiwa naye Ndiye Muongozaji kwenye njia ya kheri.

Yassir Salim

Wabillah Tawfiq

Mlango wa Kwanza
Itikadi



Mada ya Kwanza

Kumamini Allah Mtukufu

Muislamu anamwamini Allah Mtukufu kwa maana anakubali kuwepo kwa Allah Aliye Mtukufu na kwamba Yeye ni Mwenye kuumba Mbingu na ardhi, Mwenye kujua mambo yasiyoonekana (*ghaib*) na yanayoonekana (*dhahiri*). Naye ni Bwana wa kila kitu na Mmiliki wake. Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye, na Hana Mola mwingine isipokuwa Yeye. Allah ni Mwenye Kusifiwa na kila sifa ya ukamilifu na ni Mwenye kuepukana na kila sifa ya upungufu. Hayo ni kutokana na mwongozo wa Allah kabla ya kila kitu. Haya ni kwa hoja za kunukuliwa na kwa hoja za kiakili zifuatazo:

Hoja za Kunukuliwa

1) Kujieleza Allah Yeye Mwenyewe kuhusu kuwepo kwake, Ubwana wake kwa viumbe, Majina yake na sifa zake, na hayo yamo katika Kitabu chake kitukufu. Allah aliyeshinda na kutukuka anajielezea kwa kauli yake:

إِنَّ رَبَّكُمْ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ
عَلَى الْعَرْشِ يُغْشَى اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ
مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

“Hakika Mola Mlezi wenu ni Mwenyezi Mungu aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akatawala juu ya Kiti cha Enzi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazo tumika kwa amri yake. Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (7:54).

Kauli Yake Allah pale Alipomwita Mtume wake Musa عليه السلام kwenye ukingo wa jangwa lililo kuliani katika eneo lililobarikiwa kwenye mti:

يَمْوَسَىٰ إِنَّي - أَنَا اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٢٨﴾

“...Ewe Musa! Hakika Mimi ni Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.....’ (28:30)

Kauli yake Allah

أَنَا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدْنِي وَأَقِمِ الصَّلَاةَ لِذِكْرِي ﴿٢٠﴾

“Hakika Mimi ndiye Mwenyezi Mungu. Hapana mungu ila Mimi tu. Basi niabudu Mimi, na ushike Swala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi.” (20:14).

Kauli Yake katika kuitukuza Nafsi yake na kuyataja Majina yake na sifa zake:

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿٥٩﴾

“Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mwenye kuyajua yaliyo fichikana na yanayo onekana. Yeye ndiye Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu..” (59:22).

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ

الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٥٩﴾

“Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake, Mwenye nguvu, Anaye fanya analo litaka, Mkubwa, Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayo mshirikisha nayo.” (59:23)

Na kauli yake:

هُوَ اللَّهُ الْخَلِيقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي
السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٤﴾

“Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, Muumbaji, Mtengenezaji, Mtia sura, Mwenye majina mazuri kabisa. Kila kilioko katika mbingu na ardhi kinamtakasa, naye ni Mwenye kushinda, Mwenye hikima” (59:24).

Kauli yake katika kuisifu Nafsi yake:

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿٢﴾ مَلِكِ يَوْمِ
الدِّينِ ﴿٣﴾

“Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote; Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Mwenye Kumiliki Siku ya Malipo.” (1:2-4)

Kauli yake akituambia sisi Waislamu:

إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ ﴿١٧﴾

“Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi..” (21: 92).

Katika aya ya Surat Al-Muuminun:

وَأَنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاتَّقُونِ ﴿٥٢﴾

“Na kwa yakini huu Umma wenu ni Umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi nicheni Mimi”. (23:52)

Kauli yake katika kubatilisha madai ya kuwepo Mola asiyekuwa Yeye mbinguni na ardhini:

لَوْ كَانَ فِيهِمَا ءِاهَةٌ إِلَّا اللَّهُ لَفَسَدَتَا ۗ فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا

يَصِفُونَ ﴿٢٢﴾

“Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subhana ‘Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu, Bwana wa A’rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua..” (21: 22).

2) Mitume na Manabii wapatao laki moja na ishirini na nne elfu kutoa habari ya kuwepo Allah Mtukufu na Uungu Wake kwa viumbe vyake na ameviumba viumbe vyote na hufanya atakavyo kwa viumbe hivyo. Na kutoa habari juu ya majina yake na sifa zake Allah. Hapana Nabii wala Mtume yeyote isipokuwa amesema naye Allah Mtukufu au amempelekea mjumbe au ametia katika moyo wake jambo ambalo linathibitisha kwamba hayo ni maneno ya Allah na ufunuo wake kwake.

Kwa hali hii ya kutolewa habari kwa idadi hii kubwa ya wateule wa viumbe (Mitume) na wasafi kuliko watu wengine, akili inaona haiwezekani idadi hii inaweza kusema uongo. Kama inavyoona haiwezekani kuwafikiana idadi hii juu ya uongo na kutoa habari kwao kwa jambo walilolijua, na kulihakikisha na kutaka usahihi wake, na kuwa na yakini. Kwani wao ni miongoni mwa wabora wa watu na watakasifu wao kwa nafsi na wenye akili zenye nguvu kuliko watu wote, na wa kweli wao kwa mazungumzo.

3) Kuamini mabilioni ya watu na kuitakidi kwao juu ya kuwepo kwa Allah na kumwabudu Yeye na kumtii Yeye. Desturi ya kibinaadamu inakubali na kusadiki habari za mtu mmoja au wawili, sembuse kuamini kwa umma na idadi ambayo haihisabiki miongoni mwa watu, pamoja na kushuhudia kwa akili na maumbile juu ya usahihi wa kitu walichoamini na wakakitolea habari kitu hicho na wakakiabudu na wakajiweka karibu nacho.

4) Kutoa habari kwa mamilioni ya wanazuoni kuhusu kuwepo kwa Allah, Sifa Zake, Majina Yake, na Ubwana Wake, na Uwezo Wake juu ya kila kitu. Kwamba wao kwa ajili hiyo wamemuabudu na wamemtii wakapenda na wakachukia kwa ajili Yake.

Hoja za Kiakili:

1) Kuwepo kwa Ulimwengu na viumbe vingi vya aina mbalimbali. Vyote hivi vinashuhudia kuwepo kwa Muumba wa viumbe hivyo, Ambae ni Allah kwani hakuna yeyote ulimwenguni aliyedai kuviumba hivyo na kuvifanya vipatikane isipokuwa Yeye. Kama ambavyo akili ya kibinadamu inavyoona haiwezekani kupatikana kitu chochote bila ya kupatikana mwenye kukipatisha. Bali pia akili inaona haiwezekani kupatikana kitu kidogo bila kuwepo mwenye kukipatisha na hilo ni kama chakula bila ya kuwepo mpishi mwenye kukiandaa kwa kukipika, au kuwepo tandiko ardhini pasina mtandikaji sasa vipi kwa hivi viumbe vikubwa mno miongoni mwa mbingu na vilivyokusanya miongoni mwa sayari na jua, mwezi na nyota?

Wakati vyote hivyo vimetofautiana maumbo, ukubwa, umbali na mwenendo. Ardhi na vitu vilivyoubwa humo miongoni mwa binaadamu na majini na wanyama, vilivyo katika jinsia zake na kimoja kimoja vinavyotofautia na rangi na lugha, pamoja na kutofautisha katika kutambua na kufahamu. Na vitu vilivyowekwa ardhini miongoni mwa madini yenye rangi na faida mbalimbali na vitu vilivyopitishwa ardhini miongoni mwa mito, na sehemu kavu zilizozungukwa na bahari, na vitu alivyoviotisha katika ardhi yake, miongoni mwa mimea na miti yenye matunda yenye kutofuatiana aina zake, na ladha zake na harufu zake, na sifa zake na faida zake.

2) Kuwepo kwa maneno yake Allah mikononi mwetu, kwani tunayasoma, tunayazingatia na kufahamu maana yake. Hiyo ni dalili ya kuwepo kwake Allah kwa sababu haiwezekani maneno kuwepo bila ya mwenye kuyazugumza, na kupatikana kauli bila ya msemaji. Kwa hiyo tunapouona ukweli kwamba maneno Yake Allah yamekusanya sheria madhubuti mno ambazo ndiyo kwa mara ya kwanza zimeanza kufahamika katika historia ya mwanadamu na kukusanya kanuni zilizotengenezwa vyema zinazohakikisha kheri nyingi kwa binaadamu. Kama ambavyo imekusanya ndani yake nadharia za kweli za kisayansi na mengi katika mambo ya ghaibu na matukio ya Kihistoria. Haikushindwa pamoja na urefu wa

zama, hukumu yoyote katika hukumu zake na kuleta faida zake zilizokusudiwa. Hali hii itaendelea kuwa hivyo hata pale zitapohitilafiana zama na mahala. Isitoshe haikubatilika hata dhana ndogo katika dhana hizo za kisayansi na haikukosekana ghaibu yoyote katika yale ambayo imeelezea Qur'an katika mambo ya ghaibu.

3) Kuwepo kwa mpangilio huu mzuri wenye kuonekana katika njia hizi za kimaumbile katika uumbaji na utengenezaji, uanzishaji au uendelezaji wa viumbe hai vyote vilivyo katika ulimwengu huu. Kwani vyote hivyo ni vyenye kufuata na vyenye kufungika kwenye njia hizi, haviwezi kutoka nje ya njia hizi kwa hali yoyote ile.

Kwa mfano:

Mwanadamu anafungamanisha matone yake ya manii (mbegu zake za uzazi) katika mfuko wa uzazi kisha zinaupitia mfuko ule hatua ya ajabu hakuna yeyote anayehusika katika hatua hiyo, isipokuwa Allah. Baada ya hatua hizo anatoka binadamu aliyekamilika. Hatua hizi pia zinapatikana katika kuumba kwake Allah na uendelezaji wake, kuanzia uchanga, utoto, ujana hadi utu uzima, uzee wa makamo na uzee sana. Hizi ni njia kuu kwa wanaadamu na wanyama, na ndizo hizo hizo kwa miti na mimea.

Mfano mwingine ni nyota zilizoko juu na sayari za mbinguni, kwani vyote hivyo ni vyenye kufuata vile ambavyo vimefungamanishwa navyo katika kamba hizo; wala havitoki nje ya njia hizo, lau kama ingetokea ukatoka mkusanyiko wa sayari nje ya mizunguko yake basi ungeliharibika ulimwengu na yangekoma mambo ya uhai huu.

Kwa hoja hizi za kiakili na kimantiki zilizo nakiliwa na zilizosikika, Muislamu amemuamini Allah na ameuamini Ubwana wake kwa kila kitu, na Uungu Wake kwa viumbe wa mwanzo na wa mwisho. Juu ya msingi huu wa Imani na yakini hujengeka maisha ya Muislamu katika mambo yote.



Mada ya Pili

Kuamini Uungu wa Allah juu ya kila kitu

Muislamu anaamini Uungu wa Allah kwa kila kitu na kwamba Yeye hana mshirika katika Uungu Wake kwa viumbe vyote. Hilo kwanza linatokana na uongofu wa Allah kwa Muislamu. Pili ni kwa hoja za kunukuliwa na hoja za kiakili zifuatazo:

Hoja za Kunukuliwa:

1) Allah anaelezea Uungu wake na Anasema katika kujisifu Yeye Mwenyewe:

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾

“Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote;...” (1:2).

Na akasema katika kuthibitisha Uungu wake:

قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ قُلِ اللَّهُ

“Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu na ardhi? Sema: Mwenyezi Mungu..” (13:16).

Na amesema katika kubainisha Uumbaji na Uungu Wake:

رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۗ إِن كُنْتُمْ مُوقِنِينَ ﴿٧﴾ لَا إِلَهَ

إِلَّا هُوَ تَعَالَى عَنِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ يُعَلِّمُ مَن يَشَاءُ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَا تُكْتُمُونَ ۗ ﴿٨﴾

“Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilio baina yao, ikiwa nyinyi mna yakini. Hakuna mungu ila Yeye; anahuisha na anafisha-Mola Mlezi wenu na Mola Mlezi wa baba zenu wa mwanzo.” (44:7-8).

Amesema katika kukumbusha ahadi ambayo ameichukua kwa binaadamu wakiwa bado migongoni mwa baba zao kuwa waamini Uungu Wake na wamuabudu Yeye wala wasimshirikishe na chochote:

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِنْ بَنِي آدَمَ مِنْ ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَأَشْهَدَهُمْ عَلَىٰ
أَنْفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ قَالُوا بَلَىٰ شَهِدْنَا أَنْ تَقُولُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّا
كُنَّا عَنْ هَذَا غَافِلِينَ ﴿٧٢﴾

“Na pale Mola wako Mlezi alipo waleta katika wanaadamu kutoka migongoni mwao kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao, akawaambia: Je, Mimi si Mola Mlezi wenu? Wakasema: Kwani! Tumeshuhudia. Msije mkasema Siku ya Kiyama sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo.” (7:172).

Na amesema katika kusimamisha hoja dhidi ya Washirikina na kuwalazimisha waikubali hoja hiyo:

قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٨٦﴾ سَيَقُولُونَ
لِلَّهِ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٨٧﴾

“Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa A’rshi Kuu? Watasema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Sema: Basi je, hamwogopi?” (23: 86-87)

2) Ni maelezo, kushuhudia na kukiri kwa Mitume kuhusu Uungu Wake katika kuumba. Nabii Adam عليه السلام amesema katika dua yake:

قَالَ رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ
الْخَاسِرِينَ ﴿٣١﴾

“Wakasema: Mola wetu Mlezi! tumejidhulumu nafsi zetu, na kama hutusamehe na kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika..” (7:23)

Na Nabii Nuhu عليه السلام amesema katika kumshitakia Allah:

قَالَ نُوحٌ رَبِّ إِنَّهُمْ عَصَوْنِي وَاتَّبَعُوا مَنْ لَمْ يَزِدْهُ مَالُهُ وَوَلَدُهُ إِلَّا خَسَارًا ﴿٧١﴾

“Nuh’u akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika hao wameniasi, na wamemfuata yule ambaye mali yake na wanawe hawakumzidishia ila khasara.” (71:21).

Na amesema:

قَالَ رَبِّ إِنَّ قَوْمِي كَذَّبُونِ ﴿١١٧﴾ فَأَفْتَحَ بَيْنِي وَبَيْنَهُمْ فَتَحًا وَجَّيْتُ وَمَنْ مَعِيَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٨﴾

“Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika watu wangu wamenikanusha. Basi hukumu baina yangu na wao kwa hukumu yako, na uniokoe mimi na walio pamoja nami, Waumini..” (26:117-118).

Na Nabii Ibrahim عليه السلام amesema katika kuiombea Makkah, mji mtukufu wa Allah, na kuiombea nafsi yake na kizazi chake:

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا وَاجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ إِلَّا صَنَامًا ﴿١٢٥﴾

“Na Ibrahim alipo sema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ujaalie mji huu uwe wa amani, na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu..” (14:35).

Na amesema Nabii Yusuf, rehema na amani ziwe juu yake na juu ya Mtume wetu, katika kumsifu Allah na kumuomba Yeye:

﴿ رَبِّ قَدْ آتَيْتَنِي مِنَ الْمَلِكِ وَعَلَّمْتَنِي مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَنْتَ وَلِيِّ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ ﴾

“Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika umenipa utawala, na umenifunza tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema..” (12:101).

Na Nabii Mussa عليه السلام amesema katika baadhi ya maombi yake:

﴿ قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي ﴿٢٥﴾ وَيَسِّرْ لِي أَمْرِي ﴿٢٦﴾ وَأَحِلْ لِي غُضْفَةَ مِن لِسَانِي ﴿٢٧﴾ يَفْقَهُوا قَوْلِي ﴿٢٨﴾ وَاجْعَلْ لِي وَزِيرًا مِّنْ أَهْلِي ﴿٢٩﴾ ﴾

“(Musa) akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu, Na unifanyie nyepesi kazi yangu, Na ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu, Wapate kufahamu maneno yangu. Na nipe waziri katika watu wangu” (20:25-29).

Na Nabii Harun عليه السلام alisema kuwaambia wana wa Israel:

﴿ وَلَقَدْ قَالَ لَهُمْ هَارُونُ مِنْ قَبْلُ يَنْقَوْمِ إِنَّمَا فُتِنْتُمْ بِهِ وَإِنَّ رَبَّكُمُ الرَّحْمَنُ فَاتَّبِعُونِي وَأَطِيعُوا أَمْرِي ﴾

“Na hakika Harun alikwisha waambia kabla yake: Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmetiwa mtihanini tu kwa kitu hiki. Na kwa yakini Mola wenu Mlezi ni Arrahmani, Mwingi wa Rehema. Basi nifuateni mimi, na t’iini amri yangu!” (20:90).

Na Nabii Zakaria عليه السلام amesema katika kutaka kuhurumiwa:

قَالَ رَبِّ إِنِّي وَهَنَ الْعَظْمُ مِنِّي وَأَشْتَعَلَ الرَّأْسُ شَيْبًا وَلَمْ أَكُنْ
بِدُعَاؤِكَ رَبِّ شَقِيًّا ﴿١٩﴾

“Akasema: Mola wangu Mlezi! Mafupa yangu yamedhoofika, na kichwa kinameremeta kwa mvi; wala, Mola wangu Mlezi, sikuwa mwenye bahati mbaya kwa kukuomba Wewe..” (19:4)

Na akasema katika maombi yake,

وَزَكَرِيَّا إِذْ نَادَى رَبَّهُ رَبِّ لَا تَذَرْنِي فَرْدًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِينَ ﴿٨٩﴾

“Na Zakariya alipo mwita Mola wake Mlezi: Mola wangu Mlezi! Usiniache peke yangu, na Wewe ndiye Mbora wa wanao rithi.” (21:89).

Na Nabii Issa عليه السلام amesema katika jibu lake kwa Allah:

مَا قُلْتُ هُمْ إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِهِمْ أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ

“Sikuwaambia lolote ila uliyo niamrisha, nayo ni: Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi.....” (5:117).

Na akasema Nabii Isa عليه السلام hali ya kuwaambia watu wake wana wa Israel:

أَعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ إِنَّهُ مَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ
عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنْصَارٍ ﴿٧٦﴾

“...Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.” (5:72).

Na Nabii wetu Muhammad, Chuo cha Sharia ya Kiislam amani ziwe juu yake pamoja na ndugu zake na maswahaba zake, alikuwa akisema wakati wa shida:

“Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah ambaye ni: Mkubwa, Mpole. Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah Mola wa Arshi iliyo kubwa kabisa. Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah Mola wa mbingu na Mola wa ardhi iliyo tukufu kabisa.” (al-Bukhari na Muslim).

Mitume wote hawa na wengine wasiokuwa hawa, rehema za Allah na amani Zake ziwashukie, walikuwa wakitambua na kukubali Uungu wa Allah wakiomba kwa Uungu huo. Nao ni watu waliokamilika mno kwa maarifa na waliokamilika sana kiakili na ni wenye kusema kweli na wenye kumjua zaidi Allah na Sifa zake kuliko viumbe vyake vyote vilivyoko katika ardhi hii.

3) Kuamini kwa mabilioni ya wanazuoni na watu wenye hekima kuhusu Uungu wa Allah juu yao na juu ya kila kitu na kuukubali kwao Uungu huo na kuitakidi kwao kuhusu Uungu, huo ni itikadi isiyo na shaka.

4) Kuamini kwa mabilioni ya watu wenye akili na watu walio wema Uungu Wake kwa viumbe vyote.

Hoja za Kiakili:

Miongoni mwa hoja za kiakili na za kimantiki zilizo salama juu ya Uungu Wake Allah ni hizi zifuatazo:-

1) Kupwekeka Kwake (kuwa pekee) kwa Kuumba kila kitu. Kwani miongoni mwa mambo yasiyokuwa na mjadala kwa kila mtu ni kwamba hakuna aliyedai Kuumba na Kuanzisha, au kufanya kazi hizo mbili au kuziweza isipokuwa Allah. Kiumbe chochote kitakavyo kuwa kiwe kidogo au kidhaifu kazi yake ni kubwa

hata kama ungalikuwa unywele katika mwili wa mwanaadamu au mnyama au unyoya mdogo ulioko katika ubawa wa ndege au jani lililoko katika tawi la mti sembuse kuumba mwili unaokua au kilicho hai katika miili au mwili mkubwa au mdogo miongoni mwa miili.

Ama Allah Amesema katika kuthibitisha kuwa Uumbaji una muhusu Yeye na si mwingine ila Yeye tu:

﴿أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ﴾

“...Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (7:54.)

Na amesema:

﴿وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ﴾

“Na hali Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni nyinyi na hivyo mnavyo vifanya!” (37:96)

Allah Amejisifu Mwenyewe kwa Uumbaji Wake kwa kusema:

﴿الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَجَعَلَ الظُّلُمَاتِ وَالنُّورَ ثُمَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُونَ﴾

“Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliye umba mbingu na ardhi, na akafanya giza na mwangaza. Tena baada ya haya walio kufuru wanawafanya wengine sawa na Mola wao Mlezi.” (6:1)

Na akasema:

﴿وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ؕ وَلَهُ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ﴾

“Na Yeye ndiye anaye anzisha uumbaji, kisha ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake. Naye ndiye mwenye mfano bora katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.” (30:27).

Basi hivi haukuwa Uumbaji Wake kwa kila kitu kuwa ni dalili ya kuwepo Kwake na kuwepo Uungu Wake? Kwanini isiwe hivyo? Sisi ewe Mola wetu juu ya hilo ni wenye kushuhudia.

2) Ni kupwekeka Kwake katika kutoa riziki. Kwani hakuna mnyama yeyote mwenye kutembea katika ardhi au mwenye kuogelea katika maji, au mwenye kujisitiri ndani ya matumbo ila Allah ni Mwenye Kuumba riziki yake na Mwenye Kumwongoza kujuwa namna ya kuipata na kunufaika nayo.

Kuanzia kwa sisimizi kama kiumbe hai mdogo zaidi mpaka kwa binadamu ambaye ni mkamilifu zaidi na aliye juu zaidi ya aina za viumbe wengine. Vyote hivyo ni vyenye kumhitaji Allah katika kupatikana kwao, kutengenezwa kwao, katika kupata chakula chao na riziki zao. Allah Peke Yake Ndiye Mwenye kuvifanya viwepo na kuvitengeneza na ni Mwenye kuvilisha na kuvipa riziki.

Hizi zifuatazo ni aya zinazo thibitisha kuhusu ukweli huo ulivyo. Allah amesema:

فَلْيَنْظُرِ الْإِنْسَانُ إِلَى طَعَامِهِ ﴿٢٤﴾ أَنَا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ﴿٢٥﴾ ثُمَّ
شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقًّا ﴿٢٦﴾ فَأَنْبَتْنَا فِيهَا حَبًّا ﴿٢٧﴾ وَعَيْنًا وَقَضْبًا ﴿٢٨﴾
وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا ﴿٢٩﴾ وَحَدَائِقَ غُلْبًا ﴿٣٠﴾ وَفَيْكِهَةً وَآبًا ﴿٣١﴾

“Hebu mtu na atazame chakula chake. Hakika Sisi tumemimina maji kwa nguvu, Tena tukaipasua pasua ardhi kwa nguvu, Kisha tukaotesha humo nafaka, Na zabibu, na mimea ya majani, Na mizaituni, na mitende, Na bustani zenye miti iliyo songana baraabara, Na matunda, na malisho ya wanyama” (80:24-31)

Na amesema Allah:

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ مَهْدًا وَسَلَكَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا وَأَنْزَلَ مِنَ
السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِّن نَّبَاتٍ شَتَّى ﴿٥٣﴾ كُلُوا وَارْعَوْا
أَنْعَامَكُمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَبْصَارِ ﴿٥٤﴾

“Ambaye amekufanyieni ardhi kuwa tandiko, na akakupitishieni humo njia, na akakuteremshieni kutoka mbinguni maji. Na kwa hayo tukatoa namna mbali mbali za mimea. Kuleni, na mchunge wanyama wenu. Hakika katika hayo zipo ishara kwa wenye akili.” (20: 53-54)

Na amesema:

وَأَرْسَلْنَا الرِّيحَ لَوَاقِحَ فَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَسْقَيْنَاكُمُوهُ وَمَا أَنْتُمْ
لَهُ بِمُحْسِنِينَ ﴿٢٢﴾

“Na tunazipeleka pepo za kupandishia, na tunateremsha kutoka mbinguni maji, kisha tukakunywesheni maji hayo. Wala si nyinyi mnayo yaweka..” (15:22).

Na amesema:

﴿ وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا
وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٦﴾ ﴾

“Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.” (11:6).

Minhajil Muslim

Na ikithibitika bila ya kuwepo mpinzani kwamba hapana yeyote mwenye kutoa riziki ila Allah basi hili linakuwa ni hoja ya kuthibitisha Uungu Wake kwa viumbe Vyake.

3) Ushahidi mwingine ni umbile la kibinaadamu lililo salama linalokiri na kutoa ukelele wa kukubali hayo. Kwani kila mwanaadamu ambaye umbile lake halikuharibika anahisi ndani ya moyo wake kwamba yeye ni dhaifu hana uwezo mbele ya Mwenye Mamlaka, Tajiri, Mwenye Nguvu. Na kwamba mwanadamu yuko chini ya atakavyo Allah na usimamizi Wake kwake (Mwanadamu) kwa namna ambavyo amesema waziwazi bila ya kusita kwamba Yeye ni Allah. Na ukiwa ukweli huu ulio salama haupingi au kumtilia shaka kila mwenye umbile salama. Basi Yeye anataja ziada katika kuthibitisha kutokana na kukubali kwa wakubwa wa Mushrikina ukweli huu ambao ni Uungu Wake Allah kwa viumbe na kwa kila kitu. Allah amesema:

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ خَلَقَهُنَّ الْعَزِيزُ

الْعَلِيمُ ﴿٩﴾

“Na ukiwauliza: Nani aliye ziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Kaziumba Mwenye nguvu, Mjuzi.” (43: 9).

Na Amesema:

قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٨٦﴾ سَيَقُولُونَ

لِلَّهِ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٨٧﴾

“Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa A’rshi Kuu? Watasema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Sema: Basi je, hamwogopi?” (23:86-87).

4) Kupwekeka Kwake Allah kwa kumiliki kila kitu, na kufanya kwake atakavyo kusikokuwa na mipaka katika kila kitu, na kupanga Kwake kila kitu kunajulisha juu ya Uungu Wake. Kwa sababu miongoni mwa yasiyokubali mjadala kwa

wanaadamu wote ni kwamba mwanadamu ambaye ni sawa na wengine miongoni mwa viumbe hai vilivomo katika ulimwengu huu, hamiliki kitu chochote kwa dalili kwamba yeye anapokuja ulimwenguni kwa mara ya kwanza anakuja akiwa uchi, kichwa wazi, nyayo tupu (Pekupeku).

Wakati anapotoka dunia anatoka hana kitu ukiacha sanda anayositiriwa nayo mwilini mwake. Hivyo basi itakuwaje iwe sahihi kusema kwamba mwanadamu ni mwenye kumiliki kitu? Katika ulimwengu huu? Na ikiwa ni sahihi kuwa mwanadamu si mwenye kumiliki kitu katika ulimwengu huu hali ya kuwa yeye ni mtukufu wa viumbe vyote, basi atakuwa nani mwenye kumiliki? Jawabu ni kuwa Mwenye kumiliki ni Allah Peke Yake bila mjadala wowote ule, na bila shaka yoyote ile.

Kama ni hivyo basi naapa kwa Jina la Allah kuwa hizo ndizo sifa za Uungu ambazo ni Kuumba, Kutoa riziki, Kumiliki, na Kupanga mambo. Tokea kale wakubwa wa Mushirikina wameshayakubali hayo na Qur'ani imeyaeleza hayo katika sura zake nyingi.

Amesema Allah:

قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّنْ يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَمَنْ
يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيتِ وَيُخْرِجُ الْمَمِيتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَنْ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ
فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ فَعَلًا أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٣١﴾ فَذَلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمْ الْحَقُّ فَمَاذَا
بَعَدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ فَأَنَّى تُصْرَفُونَ ﴿٣٢﴾

“Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Au ni nani anaye miliki kusikia na kuona? Na nani amtoaye hai kutoka maiti, na akamtoa maiti kutoka aliye hai? Na nani anaye yadabiri mambo yote? Watasema: Allah, Mwenyezi Mungu. Basi sema: Je! Hamchi? Basi huyo ndiye Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu wa haki. Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu? Basi huwaje mkageuzwa?.” (10:31-32).

Mada ya Tatu

Kuamini Uungu wa Allah wa Watu wa Mwanzo na wa Mwisho

Muislamu anaamini Uungu wa Allah kwa watu wote wa mwanzo na wa mwisho, na kwamba hakuna Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye tu, na hayo ni kwa Hoja zilizonakiliwa kutoka kwenye Qur'an na sunna na hoja za kiakili. Kabla ya yote ni uongofu wa Allah kwa mwanadamu, kwani mwenye kuongozwa na Allah basi ndiye mwenye kuongoka na mwenye kupotezwa na Allah hakuna wa kumuongoa.

Hoja za Kunukuliwa:

1) Ushahidi wake Allah na ushahidi wa malaika wake na watu wenye elimu juu ya Uungu Wake kama alivyosema katika Sura ya *Aal Imran*;

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ لَا
إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٨﴾

“Mwenyezi Mungu, na Malaika, na wenye ilimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana mungu ila Yeye, ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana mungu ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hikima.” (3:18).

2) Ni kuthibitisha kwa Allah kuhusu Uungu Wake katika aya zaidi ya moja kutoka kwenye kitabu chake kitukufu, aliposema:

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ لَا تَأْخُذُهُ سِنَّةٌ وَلَا نَوْمٌ ﴿٢٥٥﴾

“Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala..” (2:255)

Na amesema,

وَاللَّهُمَّ إِلَهٌ وَاحِدٌ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٣﴾

“Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapana mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu..” (2:163).

Na amesema kumwambia Mtume wake Musa عليه السلام:

إِنِّي أَنَا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدْنِي وَأَقِمِ الصَّلَاةَ لِذِكْرِي ﴿٢٠١٤﴾

“Hakika Mimi ndiye Mwenyezi Mungu. Hapana mungu ila Mimi tu. Basi niabudu Mimi, na ushike Swala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi..” (20:14).

Na amesema kumwambia Mtume wetu Muhammad ﷺ:

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ۗ

“Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake.” (47: 19).

Na akasema hali ya kuielezea nafsi yake:

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَالِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۗ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿٢٢٠﴾ هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْقَدُّوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهِمُّ الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ۗ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٢٢١﴾

“Yeye ndiye Mwenyezi Mungu, ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mwenye kuyajua yaliyo fichikana na yanayo onekana. Yeye ndiye Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake, Mwenye nguvu, Anaye fanya analo litaka, Mkubwa, Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayo mshirikisha nayo.” (59: 22-23).

3) Ni maelezo ya Mitume Yake Rehema za Allah na amani ziwashukie) kuhusu Uungu Wake na kuwataka watu wao wamtambue na kumuabudu Peke Yake pasi na mwingine (asiyekuwa yeye). Hakika Nuhu **عليه السلام** alisema:

يَقَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ

عَظِيمٍ

“...Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu.” (7:59).

Na kama Nuhu, Hud, Swaleh na Shuaib (Rehema za Allah na amani yake ziwafike) hapana yeyote miongoni mwao ila alisema:

“Enyi watu wangu muabudini Allah hamna nyinyi muabudiwa mwingine asiyekuwa Yeye.”

N akasema Musa **عليه السلام** kuwaambia wana wa Israil:

قَالَ أَغَيَّرَ اللَّهُ أَبْغَيْكُمْ إِلَهًا وَهُوَ فَضَّلَكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ

“Akasema: Je, nikutafutieni mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na Yeye ndiye aliye kufadhilisheni juu ya viumbe vyote?” (7:140).

Nabii Yunus عليه السلام alisema katika kumtakasa Mola wake:

أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٢١﴾

“...Hapana mungu isipo kuwa Wewe Subhanaka Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.” (21:87).

Na Mtume wetu Muhammad ﷺ alikuwa akisema katika Tahiyatu yake katika Swala:

“Ninashuhudia kwamba hakuna Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah Peke Yake Hana mshirika.”

Hoja za Kiakili

1) Hakika kuthibiti bila upinzani kuwa Allah ndiye Muumba yaani Bwana wa viumbe, hili linatulazimisha kuamini kuwa ni yeye tu Mwenye haki ya kuabudiwa. Kuabudiwa Mola Ambaye anayehuisa, Anayefisha, Anayetoa na Anayezuia, Anayenufaisha, Anayedhuru, Yeye Ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa na viumbe. Ni mwenye kuwalazimisha wamuabudu Yeye kwa kumtii, kumpenda, kumtukuzi, kumtakasa, kujipendekeza Kwake na kumuogopa.

2) Ikiwa kila kitu miongoni mwa viumbe ni chenye kulelewa na Allah kwa maana kwamba kila kitu ni miongoni mwa jumla ya vile Alivyoviumba na Akavipa riziki na Akavipangia mambo yake na Akafanya Atakavyo katika hali zake na mambo yao. Basi hivi inaingia akilini kwa viumbe vyake kumuabudu asiyekuwa Yeye, miongoni mwa viumbe Vyake, vyenye kumhitaji. Na ikiwa ni batili kuwepo kwa alieumbwa, basi italazimika kuwa mwenye kuumba viumbe ndiye Mola wa kweli na Mwenye kuabudiwa na si vinginevyo.

Kule kusifika Kwake kwa sifa za ukamilifu usio na mipaka kama kuwa Kwake Yeye ni Mwenye Nguvu, ni Mwenye Kuweza, ni wa Juu kabisa ni Mkubwa, ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona, ni Mwenye Kutambua (mambo), ni Mwenye Kulazimisha kuabudiwe na kuwa nyoyo za waja wake zimpende na kumtukuzi na wavizoeshi viungo vyao juu ya kumtii Allah na kufuata aliyotuamrisha.

Mada ya Nne

Kuamini Majina ya Allah na sifa zake

Muislamu anaamini yale aliyonao Allah miongoni mwa Majina yake Mazuri na Sifa zake za juu na wala Muislamu hamshirikishi Allah na mwingine asiyekuwa Yeye katika Majina na sifa hizo. Na wala Muislamu hayafanyii *taawili* (tafsiri) Majina hayo ni Sifa hizo. Wala hafananishi sifa za Allah na sifa za viumbe kwa kusema vipi Allah ana uhai na ni vipi Allah anaona na kusikia. Hayo kufanywa na Muislamu ni muhali na hayatakiwi.

Muislamu anathibitisha kwa Allah yale aliyojithibitishia Mwenyewe na akayathibitisha Mtume Wake miongoni mwa Majina na Sifa zake. Muislamu ana mkatalia Allah sifa alizozikataa Mwenyewe na akazikataa Mtume wake, za kuepukana na kila aibu na upungufu kwa ujumla na kwa mchanganuo. Na hilo ni kwa hoja zilizokaliwa vitabuni na za kiakili nazo ni:

Hoja za Kunukuliwa:

1) Ni kueleza Mwenyewe kuhusu Majina Yake na Sifa Zake pale Aliposema:

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا ۖ وَذُرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ ۚ
سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٨٠﴾

“Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanao haribu utakatifu wa majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda..” (7:180).

Na Akasema;

قُلِ ادْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ أَيًّا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۚ وَلَا
تَجْهَرُوا بِصَلَاتِكُمْ وَلَا تَخَافُوهَا ۚ وَابْتَغِ بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١٨١﴾

“Sema: Mwombeni Allah (Mwenyezi Mungu), au mwombeni Rahman (Mwingi wa Rehema), kwa jina lolote mnalo mwita. Kwani Yeye ana majina mazuri mazuri. Wala usitangaze Sala yako kwa sauti kubwa, wala usiifiche kwa sauti ndogo, wali shika njia ya kati na kati ya hizo.” (17:110).

Kama Alivyojisifu Mwenyewe kwamba: Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona, Mjuzi, Mwenye Hekima, Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda, Mpole, Mwenye Kutambua, Mwenye Kushukuru, Mwenye Kuvumilia, Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu. Yeye Amezungumza na Mtume Mussa na Amelingana sawa sawa juu ya Arshi Yake. Yeye Anawapenda walo wema, na Amewaridhia waumini na mengineyo yasiyokuwa hayo (yaliyotajwa) miongoni mwa sifa zake za Dhati, kama Kuja Kwake na Kushuka Kwake miongoni mwa yale aliyoyateremsha katika kitabu Chake na akayatamka hayo Mtume Wake Muhammad ﷺ.

2) Kuyaeleza hayo Mtume Wake Muhammad ﷺ katika yale yaliyopokelewa toka kwake kwa njia sahihi miongoni mwa habari sahihi na hadithi za wazi kama anavyosema:

“Allah Anawacheka watu wawili: mmoja wao anamuua mwenzake kisha wote wanaingia peponi.” (Bukhari na Muslim)

Na kauli yake Mtume ﷺ.

“Wataendelea watu kutiwa katika Jahannamu, huku ikisema jee kuna nyongeza? Mpaka hapo Allah atapoweka humo mguu wake.”

Na katika mapokezi mengine:

“Ataweka unyayo wake, na hapo itajikusanya Jahannamu yenyewe kwa yenyewe na itasema basi basi.” (Bukhari na Muslim).

Kauli yake Mtume ﷺ:

“Mola wetu Anateremka kwenye uwingu wa Dunia kila usiku. Pale inaposalia theluthi ya mwisho ya usiku na Anasema: Nani Ananiita Nimjibu? Nani Ananiomba Nimpe? Nani Ananitaka msamaha Nimsamahe?” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake:

“Hakika Allah anafurahi zaidi anapotubia mja wake kuliko anavyofurahi mmoja wenu anapo muona mnyama wake aliyekuwa amepotea.”

Na kauli yake kwa mjakazi alipomuuliza:

“Allah yuko wapi?’ Akasema, ‘Yuko juu’. “Na mimi ni nani? Akajibu, ‘Wewe ni mjumbe wa Allah.’ Akasema: “Mwache huru kwani yeye ana imani.”

Na kauli yake:

“Allah Siku ya Qiyama, Ataishika ardhi na Ataikunja mbingu kwa Mkono Wake wa Kuume, kisha Atasema: “Mimi Ndie Mfalme, wako wapi walodai ufalme wa Ardhi?” (Bukhari).

3) Kukiri kwa wanazuoni wema wa kale kama vile maswahaba, Ta’abiina, na Maimamu wanne, (Allah awawie radhi wote) juu ya sifa za Allah, na kutozipa tafsiri potofu, au kuzikanusha au kuzitoa katika dhahiri yake. Kwani haikuthibiti kuwa kuna swahaba yeyote aliyeipa tafsiri potofu Sifa miongoni mwa Sifa za Allah au kuipinga au akasema kuwa dhahiri yake sio iliyokusudiwa. Bali walikuwa wanaamini maana inayofahamika kutoka katika sifa hiyo kama ilivyo, na wanaichukulia dhahiri yake, hali wanaelewa kuwa Sifa za Allah sio sifa za viumbe miongoni mwa viumbe Wake. Imamu Maliki رضي الله عنه alilulizwa kuhusu Kauli ya Allah.

الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَى ﴿٥﴾

“Arrahmani alal-Arshi stawaa.” (20:5).

Akasema:

“Kulingana” kunaeleweka, na namna ya kulingana huko hakueleweki, na kuliulizia hilo ni uzushi.”

Imam Shafii (Allah Amrehemu) anasema:

“Nimemuamini Allah na kilicho kuja kutoka kwa Allah, kama alivyokusudia Allah, na nimemuamini Mtume wa Allah na kila kilicho kuja kutoka kwa Mtume wa Allah, kama alivyokusudia Mtume wa Allah.”

Imam Ahmad (Allah Amrehemu) alikuwa akisema kutokana na kauli za Mtume ﷺ zisemazo kuwa:

“Hakika Allah Anateremka kwenye mbingu ya Dunia na kwamba Allah siku ya kiama Ataonekana na kwamba Allah Anafurahi, anacheka, Anakasirika, Anaridhia, Anaona karaha na Anapenda, alikuwa akisema: “Tunayaamini, na tunayakubali, si kwa namna wala kwa maana fulani.” Anakusudia kuwa sisi tunaamini kuwa Allah Anaona, Naye Yuko juu ya Arshi Yake tofauti na viumbe wake. Lakini hatuelewi namna ya kushuka kwake, wala kuona kwake, wala kulingana kwake, wala maana hasa ya hiyo. Bali maana yake hiyo tunaiacha katika elimu ya Allah kwa Aliyoyasema na Aliyomletea Mtume Wake ﷺ. Hatumpingi Mtume wa Allah na wala hatumpi sifa zaidi ya zile Alizojisifia Mwenyewe, na Alizomsifia Mtume Wake bila ya mpaka wala kikomo. Nasi twaelewa kuwa hakuna kilicho Mfano Wake Naye ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kuona.”

Hoja za Kiakili:

1) Allah Amejisifu kwa Sifa Nyingi, na Amejiita kwa Majina mengi, na hakutukataza kumsifu wala kumwita kwayo, na wala hakutuamuru kubadilisha maana zake na kuyapa tafsiri tofauti, au kuyachukulia kinyume na yalivyo. Je hivi inaingia akilini kusemwa kuwa sisi kama tutamsifu kwa sifa hizo tutakuwa tumemfananisha na viumbe vyake na kuwa kwa hiyo inatulazimu tuzitafsiri sifa hizo tofauti na zilivyo,

na tuzichukulie kinyume na dhahiri yake? Hata kama, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeziacha Sifa Zake na tumezipinga, tumeyapotosha Majina Yake, huku tukielewa kuwa Yeye Amewakemea wenye kupotosha Sifa Zake na Majina yake kwa kauli yake aliposema:

وَذُرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِمْ سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٨٠﴾

“...Na waacheni wale wanao haribu utakatifu wa majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda..” (7:180).

2) Hivi anayeikataa sifa miongoni mwa Sifa za Allah kwa kuhofia kushabihisha (kumfananisha Allah na viumbe) si anafanya hivyo baada ya kumfananisha na viumbe kisha akahofu kufanana huko na kukimbilia kukataa na kukana kuthibiti kwa sifa hizo kwa Allah na kufanya hivyo ni kukataa Sifa za Allah ambazo Amejithibitishia Mwenyewe juu ya Nafsi Yake. Na mtu kwa kufanya hivyo huwa amekusanya makosa mawili makubwa:

Kwanza: Kufananisha.

Pili: Kuzikataa na kuzikana sifa hizo. Hivi haingii akilini kuwa ni sahihi kuwa Allah Asifiwe kwa kutumia Sifa Alizojisifia yeye Mwenyewe na Alizomsifia Mtume Wake? Pamoja na kuamini kuwa Sifa Zake Allah Aliyetukuka hazifanani na sifa za viumbe, kama ilivyo Dhati Yake haifanani na dhati ya viumbe wake.

3) Kwa hakika kuamini sifa za Allah na Kumsifu kwazo hakuna maana kuwa ni kumshabihisha (kumfananisha) na viumbe, kwa sababu akili hazikatai Allah kuwa na Sifa za Dhati Yake ambazo hazifanani na sifa za viumbe, Hazikutani (hazifanani) isipokuwa katika jina tu, (kwa mfano Allah anaona na Mtume anaona na lakini kuona kwa Allah siyo sawa na kuona kwa Mtume) kwa hiyo Allah Akawa na Sifa Zake Yeye tu na kiumbe akawa na sifa zake yeye tu. Muislam anapoziamini Sifa za Allah, na akamsifu kwazo kamwe haamini, na wala haimpitii akilini mwake kuwa Mkono wa Allah kwa mfano unafanana na mkono wa kiumbe kwa maana yoyote ile, isipokuwa jina tu la mkono. Na hayo yanatokana na utofauti wa Muumba na kiumbe katika Dhati Yake, Sifa Zake na Matendo Yake.

Allah Amesema:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۝ اللَّهُ الصَّمَدُ ۝ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ۝ وَلَمْ
يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ ۝

“Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa Pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana naye hata mmoja. .” (112:1-4)

Na Amesema:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ۝

“...Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.” (42: 11).



Mada yaTano

Kuamini Malaika

Muislamu anaamini kuwepo Malaika wa Allah, na kwamba wao ni viumbe bora kuliko viumbe Wake wengine, na kuwa wao ni waja waliokirimiwa miongoni mwa waja wake. Amewaumba kwa nuru, kama Alivyomuumba Mwanaadamu kwa udongo mgumu kama kigae, na Amemuumba jini kwa moto usio na moshi. Kwa Allah Amewapa kazi, nao wanazitekeleza kuna wengine kazi zao ni kutunza taarifa za matendo ya waja na waandishi wa matendo yao. Wengine ni watunza pepo na neema zake, na wengine ni watunza moto na adhabu zake na wengine wanamtakasa Allah usiku na mchana hawachoki. Na kwamba Allah Ametofautisha kati yao katika ubora, kwa hiyo miongoni mwao kuna Malaika waliokurubishwa na Allah kama vile Jibril, Mikail na Israfil na miongoni mwao kuna wenye daraja ndogo chini ya hapo. Yote hayo yamethibiti kwa hoja za kunakiliwa na za kiakili zifuatazo:-

Hoja za Kunukuliwa:

1) Amri Yake Allah ya kuamini Malaika, na kueleza Kwake kuhusu habari zao pale aliposema:

وَمَنْ يَكْفُرْ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ وَالْيَوْمِ الْأَخِيرِ فَقَدْ ضَلَّ

ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١٣٦﴾

“...Na anaye mkataa Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Akhera, basi huyo amekwisha potelea mbali..” (4:136)

Kauli yake Allah:

مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِلَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَرُسُلِهِ وَجِبْرِيلَ وَمِيكَالَ فَإِنَّ اللَّهَ

عَدُوٌّ لِلْكَافِرِينَ ﴿١٣٧﴾

“Aliye kuwa adui wa Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Mitume wake na Jibril na Mikail, basi hakika Mwenyezi Mungu ni adui wa makafiri.” (2:98).

Na kauli ya Allah:

لَنْ يَسْتَنْكِفَ الْمَسِيحُ أَنْ يَكُونَ عَبْدًا لِلَّهِ وَلَا الْمَلَائِكَةُ الْمُقَرَّبُونَ
وَمَنْ يَسْتَنْكِفْ عَنْ عِبَادَتِهِ وَيَسْتَكْبِرْ فَسَيَحْشُرُهُمْ إِلَيْهِ جَمِيعًا ﴿٩٨﴾

“Masih hataona uvunjifu kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu, wala Malaika walio karibishwa. Na watakao ona uvunjifu utumwa wa Mwenyezi Mungu na kufanya kiburi, basi atawakusanya wote kwake..” (4: 172).

Na kauli yake Allah:

وَالْمَلِكُ عَلَىٰ أَرْجَائِهَا وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ ثَمَنِيَّةٌ ﴿١٧﴾

“Na Malaika watakuwa pembezoni mwa mbingu; na wanane juu ya hawa watakuwa wamebeba Kiti cha Enzi cha Mola wako Mlezi..” (69:17).

Na kauli yake Allah:

وَمَا جَعَلْنَا أَصْحَابَ النَّارِ إِلَّا مَلَائِكَةً ﴿٣١﴾

“Na hatukuwafanya walenzi wa Motoni ila ni Malaika....” (74:31).

Na kauli Yake:

وَأَلْمَلَيْكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ﴿٢٣﴾ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ
فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٤﴾

“Na Malaika wanawaingilia katika kila mlango. (Wakiwaambia) Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyo subiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera” (13 :23-24)

Na kauli yake Allah:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَأِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً ۗ قَالُوا أَتَجْعَلُ فِيهَا
مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدِّمَاءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ وَنُقَدِّسُ لَكَ ۗ قَالَ
إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

“Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyoyajua” (2:30).

2) Taarifa iliyotolewa na Mtume ﷺ kuhusu Malaika aliposema katika dua yake wakati anaswali Swala za usiku:

“Ewe Mola Wangu Bwana wa Jibril, Mikaili, na Israfil, Muumba wa mbingu na Ardhi, Mwelewa wa siri na dhahiri. Wewe ndiye Mwenye hukumu kati ya waja zako katika kile walichokhitilafiana, niongeze kwa idhini yako katika kile walichokhitilafiana miongoni mwa haki, hakika yako unamuelekeza umtakaye katika nia ilionyooka.”(Muslim)

Kauli yake ﷺ,

“Imepiga ukelele mbingu, na ina haki ipige ukelele, kwani haina sehemu ya eneo la ukubwa wa vidole vinne isipokuwa juu yake kuna Malaika mwenye kusujudu” (Ahmad).

Katka kauli yake:

“Baitil-Maamuur kila siku wanaingia Malaika sabini alfu, kisha hawarejei humo tena.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake:

“Inapofika siku ya Ijumaa husimama kwenye mlango wa kila msikiti Malaika wanaandika wanaoingia wa kwanza wa pili mpaka anapokaa Imamu wanakunja mafaili na wanakuja sikiliza Khutba.” (Ameipokea Bukhari na Malik).

Na kauli yake:

“Wakati mwengine Malaika humuona akiwa amejifananisha na watu kisha akanielewesha nami nikafahamu yale anayoyasema.” (Bukhari).

Na kauli yake:

“Wanapeana zamu kwenu malaika usiku na mchana.” (Bukhari).

Na kauli yake:

“Malaika wameumbwa kwa nuru, na majini wameumbwa kwa moto usio na moshi na Adamu ameumbwa kwa alichowaeleza yaani udongo.” (Muslim)

3) Idadi kubwa ya masahaba رضي الله عنهم waliwaona Malaika siku ya vita ya Badr. Pia masahaba walimuona Jibrilu (Malaika mtunza Wahyi wakiwa wengi kwa zaidi ya mara moja. Kwani nyakati zingine alikuwa anakuja akiwa katika hali ya

mtu mwenye sura nzuri (*Duhyatul-kilbiy*) kwa hiyo alikuwa wanamuona, na miongoni mwa matukio mashuhuri zaidi ni yale yaliyoelezwa katika hadihti ya Umar Ibni Khattab رضي الله عنه aliyoipokea Imam Muslim. Katika maelezo hayo mna kauli ya Mtume ﷺ, "Mwamjua nani muulizaji? Wakasema, "Allahu wa Rasuulahu a'lam" akasema huyo ni Jibrilu amewajia ili awafundishe Dini yetu." (Muslim)

4) Imani ya maelfu na mamilioni ya waumini na wafuasi wa Mitume katika kila enzi na kila mahali ya kuamini kuwepo kwa Malaika na kuyakubali yaliyoelezwa na Mitume kutoka kwa Malaika bila yakuwa na shaka wala kubabaika.

Hoja za Kiakili:

1) Akili haioni kizuizi cha kuwepo Malaika na wala haikatai kuwepo kwao. Kwani akili haikatai isipokuwa kile kinacholazimisha kukutana vinyume viwili kwa pamoja. Kama vile kitu kuwa kipo na wakati huo hupo hakipo kwa wakati mmoja, au vitu vinavyopingana, kama vile kuwepo kiza na nuru (usiku na mchana) kwa pamoja. Kwa kuaminika kuwepo kwa Malaika hakulazimishi kuwepo kitu katika hivyo vilivyotajwa.

2) Ikiwa miongoni mwa visivyo kubali mjadala kwa wenye akili wote ni kwamba athari (dalili/alama) ya kitu inajulisha juu ya kuwepo kwa kitu hicho. Basi Malaika wana athari (alama) nyingi zinazo hukumu kuwepo kwao na miongoni mwa hizo ni:

Kwanza: Kufika wahyi (ufunuo) kwa Manabii na Mitume, kwani mara nyingi ulikuwa unawafikia kwa kupitia kwa Roho Muaminifu (Jibril Juu yake amani). Malaika mwenye dhamana ya wahyi, na hii athari iko wazi haipingiki, na hiyo inathibitisha na kusisitiza juu ya kuwepo kwa Malaika.

Pili: Kufa kwa viumbe kwa kushikwa roho zao. Hii ni athari iliyo wazi na inajulisha juu yakuwepo kwa Malaika wa kifo na wasaidizi wake.

Amesema:

﴿ قُلْ يَتَوَفَّنَا مَلَكُ الْمَوْتِ الَّذِي وُكِّلَ بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴾

“Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti aliye wakilishwa juu yenu; kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu Mlezi.”(32:11)

Tatu: Kuhifadhiwa mwanadamu na maudhi ya majini na mashaitwani na shari zao kwa muda wa uhai wake wote. Huku akiwa anaishi kati yao na wanamuona wakati yeye hawaoni, na wanaweza kumuudhi na wala yeye hawezi hata kuondoa shari yao. Hiyo ni dalili ya kuwapo Malaika wanaomuhifadhi mwanaadamu na wanaomlinda. Amesema Allah:

لَهُ مُعَقِّبَاتٌ مِّنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ

“Kila mtu analo kundi la malaika mbele yake na nyuma yake linamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu.....” (13: 11).

3) Kutokukiona kitu kwa udhaifu wa macho au kukosa maandalizi kamili ya kukiona kitu hakukatai kuwepo kwa kitu hicho. Kwani kuna vitu vingi katika ulimwengu huu lakini macho matupu yanashindwa kuviona na vinaonekana vizuri kwa kutumia vyombo vya kukuzia.



Mada ya Sita

Kuamini Vitabu vya Allah

Muislamu anaviamini vitabu vyote alivyoviteremsha Allah, na nyaraka alizowapa baadhi ya Mitume wake. Muislamu anaamini kwamba yaliyomo katika vitabu hivyo na nyaraka hizo ni maneno ya Allah aliyoyapeleka kwa Mitume wake. Ili waifikishe sheria Yake na Dini Yake kwa wanaadamu na kwamba kubwa ya vitabu hivi ni vinne navyo ni: “Qur’ an Tukufu” Iliyoteremshwa kwa Mtume wetu ﷺ, “Tourati” iliyoteremshwa kwa Mtume wa Allah Mussa عليه السلام, “Zaburi” iliyoteremshwa kwa Mtume wa Allah na mja wake Dawud عليه السلام na Injili kwa Mtume wa Allah na mja wake Issa عليه السلام.

Qur’ ani Tukufu ndicho kikubwa cha vitabu hivi na kinachoviongoza vyote na kuzitengua baadhi ya sheria za vitabu hivyo na hukumu zake. Hayo yamethibiti kutokana na hoja za kunukuliwa (kutoka katika vitabu vitakatifu) na hoja za kiakili zifuatazo:

Hoja za Kunukuliwa:

1) Allah ameamuru kuviamini Vitabu vyake kwa kusema:

يَتَأْتِيَا الَّذِينَ ءَامَنُوا ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ؕ وَالْكِتَابِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَيَّ
رَسُولِهِ ؕ وَالْكِتَابِ الَّذِي أَنْزَلَ مِن قَبْلُ

“Enyi mlio amini! Muaminini Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Kitabu alichokiteremsha juu ya Mtume wake, na Kitabu alichokiteremsha kabla yake....” (4:136).

2) Kauli Yake Allah:

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴿١﴾ نَزَّلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ
مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَأَنْزَلَ التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ ﴿٢﴾

“Mwenyezi Mungu, hakuna mungu ila Yeye Aliye Hai, Msimamizi wa yote milele. Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati na Injili.” (3:2-4).

Kauli yake Allah:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ
وَمُهَيِّمًا عَلَيْهِ فَاحْكُم بَيْنَهُم بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ عَمَّا
جَاءَكَ مِنَ الْحَقِّ لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَا جَا^ط وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ
لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ لِيَبْلُوَكُمْ فِي مَا آتَاكُمْ فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرَاتِ
إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿١٨﴾

“Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda. Basi hukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamaniao yao ukaacha Haki iliyo kujia. Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea sharia yake na njia yake. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli taka ange kufanyeni nyote umma mmoja, lakini ni kukujaribuni kwa aliyo kupeni. Basi shindaneni kwa mambo ya kheri. Kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo yenu nyote, na atakuja kuwaambieni yale mliyo kuwa mkikhitalifiana.” (5:48)

Na kauli Yake Allah:

وَأَتَيْنَا دَاوُدَ زُبُورًا ۝

“...na Daud tukampa Zaburi..” (4:163)

Na Kauli Yake Allah:

وَأَنَّهُ لَتَنْزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ۝ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ۝ عَلَى قَلْبِكَ
لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ۝ بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُبِينٍ ۝ وَأَنَّهُ لَفِي زُبُرِ
الْأُولَىٰ ۝

“Na bila ya shaka hii ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ameuteremsha Roho muaminifu, juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji, Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi. Na hakika bila ya shaka haya yamo katika Vitabu vya kale.” (26: 192-196).

Na kauli Yake Allah:

إِنَّ هَذَا لَفِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ۝ صُحُفِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ ۝

“Hakika haya yamo katika Vitabu vya mwanzo, Vitabu vya Ibrahimu na Musa.” (87:18-19).

3) Mtume ﷺ ameeleza habari hizi katika hadithi nyingi, miongoni mwa hizo ni kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika si vingine kubaki kwenu katika waliopita kama vile kati ya saa ya Alasiri mpaka kuzama jua wamepewa watu wa Taurati “Taurati” wakati wakitumia mpaka nusu ya mchana, kisha wakashindwa, kisha wakapewa Qiratwa Qiratwa, (aina ya malipo) kisha wakapewa watu ‘Injili’ wakitumia mpaka ikaswaliwa Alasiri, kisha wakashindwa wakapewa Qiratwa

Qiratwa Qiratwa kisha mkapewa Qur'an" mkaitumia mpaka jua likazama, mkapewa Qiratwa mbili mbili, kisha akasema mtu katika Ahlul Kitabu: ni wachache wa matendo kuliko sisi lakini wamepewa malipo mengi. Allah akasema: "Je, katika haki zenu nimedhulumu kitu gani?" Wakasema: "Hapana akasema hiyo ni fadhila yangu nampa ninaye mtaka." (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

"Nabii Daudi عليه السلام alipewa uwezo wa kusoma Zaburi alikuwa anaamuru kupambanua Mnyama wake, na akapambwa na akawa anaisoma Zaburi kala hajakamilika kupambwa mnyama wake, na alikuwa hali isipokuwa kutokana na kazi ya mkono wake (yaani jasho lake)." (Bukhari)

Na kauli yake Mtume ﷺ

"Husda inaruhusiwa katika vitu viwili tu: navyo ni (1) Na mtu aliyepewa Qur'an na Allah akawa anaisoma usiku na mchana .(2) Na mtu aliyepewa mali na Allah akawa anaitumia katika heri." (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

"Nimewaachia vitu ambavyo kama mtashikamana navyo hamtapotea baada yangu navyo ni: kitabu cha Allah na sunna ya Mtume wake ﷺ." (al-Hakim na Malik).

Na kauli ya Mtume ﷺ,

"Msiwasadiki Ahlulkitabi na wala msiwapinge na semeni: tumekiamini (kitabu) tulichoteremshiwa na (kitabu) mlichoteremshiwa, na Mungu wetu na Mungu wenu ni mmoja nasi Kwake tumejisalimisha." (Bukhari).

4) Imani ya mamilioni ya wataalamu na wenye hekima na waumini wa kila zama na kila mahala, na kuamini kwao kusiko na wasi wasi kuwa Allah Ameteremsha

vitabu Alivyowapelekea Mitume Wake ambao ni watu bora katika viumbe Wake na Ameweka humo Alichokitaka miongoni mwa Sifa zake na habari zake za ghaibu na ufafanuzi wa sheria yake na Dini yake, na ahadi njema kwa wamchao na onyo kwa wanao muasi.

Hoja za Kiakili:

1) Udhaifu wa mwanadamu, na mahitaji yake kwa Mola wake katika uzima wa mwili wake na roho yake ililazimu kuteremsha vitabu vilivyobeba sheria na kanuni zitakazo mthibitishia mwanadamu ukamilifu wake, na kile anacho kihitaji katika uhai wake wa duniani na uhai wake wa akhera.

2) Mitume ndio walio kati, kati ya Allah (Muumba) na waja wake (viumbe) Mitume ni waadamu sawa na wanadamu wengine wanaishi kwa kipindi kisha wanakufa, kama ujumbe wao usingekuwa katika vitabu maalumu ungalikuwa unapotea kwa kufa kwao, na watu baada yao wanalibaki bila ya ujumbe wala Mtume. Kwa hiyo lengo la utume linalipotea na kwa ajili hiyo hali ililazimisha kuteremshwa vitabu vya Allah.

3) Kama angalikuwa Mtume si anayelingania watu wamuamini Allah, angelikuwa hana kitabu chenye kueleza sheria, muongozo na kheri kutoka kwa Allah ingalikuwa rahisi kumuona kuwa ni mwongo kisha kukataa ujumbe wake. Hivyo hali hii nao imesababisha kuteremshwa kwa vitabu vya Allah ili iwe hoja dhidi ya watu.



Mada ya Saba

Kuiamini Qur'ani Tukufu

Muislamu anaamini kuwa Qur'ani Tukufu ni kitabu cha Allah Alichokitegemea kwa mbora wa viumbe wake, na mbora wa Mitume wake na Mjumbe Wake ambaye ni Mtume wetu Muhammad ﷺ kama Alivyoteremsha vitabu vingine kwa waliotangulia miongoni mwa Mitume. Na kwamba hakumu za kitabu chake zimetengua hukumu zingine zilizo katika vitabu vilivyoteremka kutoka mbinguni vilivyotangulia. Kama utume wake pia ndiyo uliyofunga mlango wa kuendelea kwa utume baada yake.

Muislamu anaamini pia kuwa Qur'an Tukufu ni kitabu kilichokusanya sehemu kubwa ya sheria za Allah na Aliyekitegemea Amechukua dhamana ya kumpa maisha bora duniani na akhera mwenye kukifuata na akamuahidi adhabu atakayekipuuza akiwa hakukifuata na akamuahidi adhabu atakayekipuuza akawa hakukifuata kwa kumpa maisha magumu duniani na akhera. Kwamba hicho ni kitabu pekee ambacho Allah amechukua dhamana ya usalama wake kwa kukiepusha na upungufu au ziada yoyote au kubadilishwa aya au kuharibiwa aya yoyote au sura yoyote na kuwa kitabaki kama kilivyoteremshwa mpaka hapo Allah atakapokichukua mwisho wa maisha ya duniani. Yamethibiti hayo kwa hoja zifuatazo:

Hoja za Kunukuliwa:

1) Allah ameeleza hayo aliposema:

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿١﴾

“Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.” (25:1).

Na kauli yake Allah:

خُنْ نَقْصُ عَلَيْكَ أَحْسَنَ الْقَصَصِ بِمَا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ هَذَا الْقُرْآنَ
وَإِنْ كُنْتَ مِنْ قَبْلِهِ لَمِنَ الْغَافِلِينَ ﴿٣﴾

“Sisi tunasimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Qur’ani hii. Na ijapo kuwa kabla ya haya ulikuwa miongoni mwa wasio jua.” (12:3).

Kauli yake Allah:

يَأْهَلِ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ كَثِيرًا مِمَّا
كُنْتُمْ تُخْفُونَ مِنَ الْكِتَابِ وَيَعْفُو عَنْ كَثِيرٍ قَدْ جَاءَكُمْ
مِّنَ اللَّهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُّبِينٌ ﴿٥﴾ يَهْدِي بِهِ اللَّهُ مَنِ اتَّبَعَ
رِضْوَانَهُ سُبُلَ السَّلَامِ وَيُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِهِ
وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٦﴾

“Enyi Watu wa Kitabu! Amekwisha kujieni Mtume wetu anaye kufichulieni mengi mliyo kuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anaye samehe mengi. Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na Kitabu kinacho bainisha. Mwenyezi Mungu huwaongoa wenye kufuata radhi yake katika njia za salama, na huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye nuru kwa amri yake, na huwaongoa kwenye njia iliyo nyooka..” (5:15-16).

Kauli Yake:

قَالَ أَهْبِطًا مِنْهَا جَمِيعًا ۖ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۖ فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي هُدًى فَمَنِ اتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشْقَى ﴿١٢٣﴾ وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكًا وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى ﴿١٢٤﴾

“Akasema: Ondokeni humu nyote, hali ya kuwa ni maadui nyinyi kwa nyinyi. Na ukikufikieni uwongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika. Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.” (20:123-124).

Na kauli yake Allah:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِالذِّكْرِ لَمَّا جَاءَهُمْ ۖ وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ ﴿٤١﴾ لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ۖ تَنْزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

“Kwa hakika wanayo yakataa mawaidha haya yanapo wajia (wataangamia), na haya bila ya shaka ni Kitabu chenye nguvu na utukufu. Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye hikima, Msifiwa.” (41:41-42).

Na kauli ya Allah:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٩﴾

“Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda”. (15:9)

Minhajil Muslim

2) Maelezo ya Mtume Wake ﷺ ambaye ndiye aliyeteremshiwa Qur'an amesema:

“Elewa mimi nimepewa kitabu (yaani Qur'an) na mfano wake pamoja: (na mfano wa kitabu ni hadithi) (Abu Dawud na Ahmad).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mbora wenu ni yule aliyejifundisha Qur'an na kisha akaifundisha.” (Abu Dawud na Tirmidhi na Ibn Majah).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Haifai kufanya husda isipokuwa katika hali za namna mbili: Mtu ambaye Allah amempa Qur'an naye anaisoma usiku na mchana, na kwa mtu ambaye Allah amempa mali akawa anaitoa usiku na mchana.” (Bukhari)

Na kauli yake ﷺ:

“Hakuna katika Mitume isipokuwa kila mmoja wao amepewa hoja ambazo kwa hoja hizo walimuamini watu ama hoja niliyopewa mimi ni Qur'an yaani wahyi aliouleta Allah kwangu, kwa hiyo nataraji kuwa zaidi yao kwa wafuasi Siku ya Qiyama.” (Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Lau kama Nabii Mussa au Nabii Issa wangelikuwa hai wangelazimika kunifata.” (Abu Ya'ala)

3) Kuamini kwa mabilioni ya Waislamu kuwa Qur'an ni Kitabu cha Allah na ni Wahyi wake alioupeleka kwa Mtume wake na itikadi yao isiyo na wasi wasi kwa kuamini hivyo pamoja na kuisomakwao Qur'an na kuihifadhi kwa walio wengi wao na kuyatumia yaliyomo miongoni mwa sheria na hukumu zake.

Hoja za Kiakili:

1) Qur'an imekusanya Elimu mbali mbali pamoja na kuwa aliyeteremshiwa Qur'an hiyo hajui kusoma wala kuandika wala hakupata kwenda chuoni. Elimu hizo ni kama zifuatazo:-

- a) Elimu za kimaumbile.
- b) Elimu za kihistoria.
- c) Elimu za Kisheria na kanuni.
- d) Elimu za kivita na kisiasa.

Kupatikana elimu za aina hizi ni dalili zenye nguvu kuwa Qur'an ni maneno ya Allah na ni wahyi wake. Kwa sababu akili haikubali kuwa elimu kama hizi anaweza kuzijua mtu asiyejua kusoma wala kuandika.

2) Kutamba kwa Allah Aliyeiteremsha Qur'an na kuwaambia wanaadamu kuwa walete mfano wa Qur'an kwa kauli Yake:

قُلْ لِّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨٨﴾

“Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur’ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao..” (17:88).

Kama Alivyowatambia wasanii wao walete sura kumi tu mfano wa Qur'an bali walishindwa kuleta hata sura moja. Basi hii ni hoja kubwa kabisa inayothibitisha kuwa Qur'an ni Maneno ya Allah na kamwe si maneno ya mwanaadamu.

3) Kuwamo katika Qur'an habari nyingi za ghaibu, na ambazo baadhi yake zimeonekana baada ya kuelezwa na Qur'an na zimedhihiri kwa sura ile ile iliolezwa na Qur'an bila tofauti yoyote.

4) Kama wanaamini kuwa Allah ameteremsha vitabu vingine kwa asiyekuwa Muhammad ﷺ kama vile Tourati kwa Nabii Mussa, na Injili kwa Nabii Issa (ziwe juu yao amani), kwa nini wapinge kuwa Qur'an hakuiteremsha Allah, ambaye Yeye ndiye aliyeviteremsha vitabu vilivyotanglia? Na je kiakili, hivi akili inasema ni muhali kuteremka Qur'an? Hapana bali akili inaona kuwa ni lazima na kuwa ni wajibu.

5) Nimezifuatilia taarifa zilizotolewa na Qur'an na nimezikuta kama ilivyoelezwa sawa sawa, pia nilivyofuatilia habari zake nimezikuta kama zilivyozisimulia sawa sawa, kama pia nilivyofuatilia kukumu zake na sheria zake na kanuni zake nikakipata kila kilichotakiwa miongoni mwa amani, ubora na heshima na elimu na ufahamu. Haya yanathibitishwa na historia ya utawala wa makhalifa waongofu Allah awawie radhi.

Sijui ni hoja gani tena zaidi ya hii inayotakiwa ili kuthibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Allah na ni wahyi Wake Aliouteremsha kwa mbora wa viumbe Wake, mwisho wa Mitume na Wajumbe wake wote?



Mada ya Nane

Kuamini Mitume (Ziwe juu yao amani)

Muislamu anaamini kuwa Allah amechagua Mitume kutokana na watu na akawapelekea Wahyi (ufunuo) wa sheria zake na akawapa jukumu la kuutangaza Wahyi huo ili kukataa hoja za watu dhidi Yake Siku ya Kiama. Akawatuma kwa hoja za wazi na Akawaimarisha kwa kuwapa miujiza kuanzia kwa Mtume wake Nuhu na kumalizia kwa Muhammad ﷺ. Na kwamba Mitume ni wanadamu yanawapata mengi miongoni mwa mambo ya kibinadamu, wanakula, wanakunywa, wanaumwa, wanapona, wanasahau, wanakumbuka, wanakufa na wanapata uhai. Wao Mitume ni wakamifu zaidi katika viumbe vya Allah kwa ujumla, na wabora wao bila ya upinzani. Na kwamba haikamiliki imani ya mja isipokuwa kwa kuwaamini na kuwakubali hao wote kwa ujumla wao na kwa mmoja mmoja. Hayo yamethibiti kwa hoja zilizonukuliwa na hoja za kiakili zifuatazo:-

Hoja za Kunukuliwa:

1) Kueleza Kwake Allah katika Qur'an kuhusu Mitume Wake na kupewa kwao utume na namna walivyofikisha ujumbe wao.

Na kauli Yake Allah:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ
فَمِنْهُمْ مَن هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَن حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ فَسِيرُوا فِي
الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكذِبِينَ ﴿١٦﴾

“Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao ulio wathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanao kanusha..” (16:36).

Na kauli yake Allah,

اللَّهُ يَصْطَفِي مِنَ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا وَمِنَ النَّاسِ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ

بَصِيرٌ ﴿٧٥﴾

“Mwenyezi Mungu huteuwa Wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona..” (22:75).

Na Kauli yake Allah:

﴿ إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ وَأَوْحَيْنَا

إِلَى إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَعِيسَى وَأَيُّوبَ

وَيُونُسَ وَهَارُونَ وَسُلَيْمَانَ وَءَاتَيْنَا دَاوُدَ زَبُورًا ﴿١١٣﴾ وَرُسُلًا قَدْ

فَصَّصْنَا لَهُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ وَرُسُلًا لَمْ نَقْضُصْهُمْ عَلَيْكَ وَكَلَّمَ اللَّهُ

مُوسَى تَكْوِيمًا ﴿١٦٤﴾ رُسُلًا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لَعَلَّ النَّاسَ عَلَى

اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٦٥﴾

“Hakika Sisi tumekuletea wahyi wewe kama tulivyo wapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio kuwa baada yake. Na tulimpelekea wahyi Ibrahim na Ismail na Is-haka na Yaakub na wajukuu zake, na Isa na Ayub na Yunus na Harun na Suleiman, na Daud tukampa Zaburi. Na Mitume tulio kwisha kukuhadithia kabla yake, na Mitume wengine hatukukuhadithia. Na Mwenyezi Mungu alinena na Musa kwa maneno. Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.” (4:163-165).

Na kauli Yake:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ
النَّاسُ بِالْقِسْطِ^ط

“Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu....” (57: 25).

Na Kauli Yake:

﴿ وَأَيُّوبَ إِذْ نَادَىٰ رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ الضُّرُّ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴾

“Na Ayyubu, alipo mwita Mola wake Mlezi, akasema: Mimi yamenipata madhara. Na Wewe ndiye unaye rehemu kuliko wote wanao rehemu” (21: 83).

Kauli Yake:

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ الطَّعَامَ
وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ^ط

“Na hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakenda masokoni...” (25:20).

Kauli Yake:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ تِسْعَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ^ط فَسَعَلَٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ إِذْ جَاءَهُمْ
فَقَالَ لَهُ فِرْعَوْنُ إِنِّي لَأَظُنُّكَ يَمُوسَىٰ مَسْحُورًا ﴿١١﴾

“Na kwa yakini tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi. Waulize Wana wa Israili alipo wafikia, na Firauni akawaambia: Hakika mimi nakuona wewe Musa umerogwa!.” (17:101).

Kauli Yake:

وَإِذْ أَخَذْنَا مِنَ النَّبِيِّينَ مِيثَاقَهُمْ وَمِنْكَ وَنُوحٍ وَإِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ
وَعِيسَىٰ ابْنَ مَرْيَمَ ۗ وَأَخَذْنَا مِنْهُم مِّيثَاقًا غَلِيظًا ﴿٧﴾ لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ
عَنْ صِدْقِهِمْ وَأَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٨﴾

“Na tulipo chukua ahadi kwa Manabii na kwako wewe, na Nuhu na Ibrahim na Isa mwana wa Mariamu, na tulichukua kwao ahadi ngumu, Ili (Mwenyezi Mungu) awaulize wakweli juu ya ukweli wao. Na amewaandalia makafiri adhabu chungu.” (33: 7-8).

2) Maelezo ya Mtume Muhammad ﷺ ya kujitangaza na Mitume wenzake miongoni mwa Manabii na Mitume katika kauli yake:

“Allah hakumpeleka Nabii isipokuwa Nabii huyo amewahadharisha watu wake na mwenye jicho moja mrongo mno naye ni, “Masihi Dajjali.” (Bukhari).

Kauli yake: Na wakati Abu Dharr alipouliza idadi ya Mitume akasema:

“Ni laki moja na Ishirini na nne elfu, katika hao Mitume mursali ni mia tatu na kumi na tatu...” (Ibn Hibban).

Kauli yake:

“Naapa kwa jina la yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi kwake kama Nabii Mussa angalikuwa hai angenifuata” (Imamu Ahmad).

Na kauli yake:

“Pindi Mtume alipoambiwa ewe mbora wa viumbe, kwa unyenyekevu wake Mtume ﷺ akajibu mbora ni Mtume Ibrahimu.”

Na kauli yake:

“Haistahiki kwa mja kusema: mimi Muhammad ni bora kuliko Nabii Yunus Ibni Matta”. (Ahmad na pia katika sahihi mbili).

Katika maelezo yake Mtume ﷺ kuhusu Mitume wengine siku ya usiku wa miiraji, pale walipokusanywa huko *Masjidil Maqdis* na akaswali nao akiwa Imam wao, kama alivyowakuta mbinguni Nabii Yahya na Nabii Issa, Yusuf, Idris, Haruna na Mussa na Ibrahimu na akaeleza habari zao na hali zao alivyoziona.

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Na hakika Nabii wa Allah Daud alikuwa anakula kutokana na kazi ya mkono wake.” (Bukhari na Muslim).

3) Imani ya Mabilioni ya wanadamu wakiwemo Waislamu na wasiokuwa Waislamu Mayahudi na Manaswara katika kuwaamini Mitume wa Allah na kuwakubali kwao utume wao bila ya wasiwasi na kuamini kwao kuwa Mitume ni wakamilifu na kuwa wameteuliwa na Allah.

Hoja za Kiakili:

1) Uungu Wake Allah na Huruma Zake Zinalazimisha kupeleka Mitume kutoka kwake kwenda kwa viumbe Wake ili wawajulishe viumbe hao kuhusu Mola wao na wawaelekeze kufanya yale ambayo yanaonyesha ukamilifu wa kibinadamu na yanayowapeleka kwenye maisha bora ya duniani na akhera.

2) Kuwa Yeye Allah Ameumba viumbe ili wamuabudu, pale aliposema:

﴿ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴾

**“Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.”
(51:56).**

Kwa lengo hili la Allah inalazimisha kuteua Wajumbe na kuwatuma ili kuwafundisha waja ili wajue namna ya kumuabudu na kumtii kwa sababu hayo ndiyo majukumu aliyowaambia. Aliwapeleka Manabii ili watu siku ya kiama wasiseme: “Sisi Ewe Mola wetu haukuwa tunajua namna ya kukutii ili tukutii, na wala namna ya kukuasi ili ujiepushe na maasi, leo kwako hakuna kosa, hivyo usituadhibu” wasije wakapata hoja juu ya Allah. Hii ni nani sababu inayolazimisha kupeleka Mitume ili kusiwe na hoja juu ya viumbe.

Amesema:

لَكِنِ اللَّهُ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ وَالْمَلَكُ يَشْهَدُونَ
وَكَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٥٦﴾

**“Lakini Mwenyezi Mungu anayashuhudia aliyo kuteremshia wewe. Ameyateremsha kwa kujua kwake - na Malaika pia wanashuhudia. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.”
(4:166).**



Mada ya Tisa

Kuamini Utume wa Muhammad ﷺ

Muislamu anaamini kuwa Nabii asiyejua kusoma wala kuandika ni Muhammad Ibni Abdillahi Ibni Abdil Mutwalib wa kizazi cha Hashim, Muarabu wa kabila la Ki-Quraishi, anayetokana na kizazi cha Nabii Ismail, mtoto wa Nabii Ibrahim Amani iwe juu yake.

Yeye ni mja wa Allah na ni mjumbe wake alimtuma afikishe ujumbe wake kwa watu wote wekundu, weusi na weupe. Kwa Utume wake na kwa Ujumbe wake amefunga ujumbe usiendeleo tena; hakuna Nabii wala mjumbe, baada yake. Allah Alimpa nguvu kwa kumpa miujiza, na amemfanya bora zaidi ya mitume wengine kama alivyo ufanya bora umma wake na kuwa zaidi ya umma nyingine. Allah Ametuamrisha kumpenda na ametuwajibisha kumtii, na kuufuata ni lazima. Amempa mambo ambayo hakupewa Mtume mwengine asiyekuwa yeye, miongoni mwa hayo ni: *Wasila, Kauthar, Birika* na *Maqamu-Mahmud*, na haya yamethibiti kwa hoja zifuatazo zilizonukuliwa kutoka katika vitabu vya Allah.

Hoja za Kunukuliwa:

1) Ushindi wa Allah na ushindi wa Malaika wake kwake ﷺ wakithibitisha utume wake, kama ulivyopokelewa katika Qur'an:

“Lakini Allah Anashuhudia kwa aliokuteremshia amekuteremsha kwa Elimu yake na malaika pia wanashuhudia hivyo na atosha Allah kuwa shahidi.” (4:166)

2) Taarifa ya Allah kuwa ujumbe wa Muhammad ni kwa watu wote, na kuwa amehitimisha Utume kwa kumleta Mtume wake Muhammad na kumtii na kumpenda ni wajibu, na kuwa Muhammad ndiyo mwisho wa Mitume. Haya ni kwa kauli Yake aliposema:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ الرَّسُولُ بِالْحَقِّ مِنَ رَبِّكُمْ فَآمِنُوا خَيْرًا لَكُمْ وَإِنْ
تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا

“Enyi Watu! Amekwisha kujieni Mtume huyu na haki itokayo kwa Mola wenu Mlezi. Basi aminini, ndiyo kheri yenu. Na mkikanusha basi hakika viliomo mbinguni na duniani ni vya Mwenyezi Mungu tu. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye hikima.” (4:170).

Na kauli Yake:

يَتَأَهَّلَ آلِ كَتَبٍ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ عَلَىٰ فَتْرَةٍ مِّنَ الرُّسُلِ أَنْ
تَقُولُوا مَا جَاءَنَا مِن بَشِيرٍ وَلَا نَذِيرٍ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَشِيرٌ وَنَذِيرٌ وَاللَّهُ عَلَىٰ
كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٧٠﴾

“Enyi Watu wa Kitabu! Bila ya shaka amekujilieni Mtume wetu akikubainishieni katika wakati usio kuwa na Mitume, msije mkasema: Hakufika kwetu mbashiri wala mwonyaji. Basi amekujieni mbashiri na mwonyaji. Na Mwenyezi Mungu anao uweza wa kila kitu.” (5:19).

Kauli Yake:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٧١﴾

“Na Hatukukupeleka ila uwe rehema kwa viumbe wote.” (21:107).

Kauli Yake:

هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ
وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا مِن قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٦٢﴾

“Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasio jua kusoma, awesomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.” (62:02).

Kauli Yake:

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ

“Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu..”(48:29).

Kauli Yake:

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿٢٥﴾

“Ametukuka aliye teremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote..” (25:01).

Kauli Yake:

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رُّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ۗ وَكَانَ
اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٣﴾

“Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.” (33:40).

Kauli Yake:

أَقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَنْشَقَّ الْقَمَرُ ﴿٥٤﴾

“Saa imekaribia, na mwezi umepasuka” (54:1).

Kauli Yake:

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١٠٨﴾

“Hakika tumekupa kheri nyingi.” (108:1).

Kauli Yake:

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿٩٣﴾

“Na Mola wako Mlezi atakupa mpaka uridhike.” (93:5).

Kauli Yake:

عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٩﴾

“...Huenda Mola wako Mlezi akakunyanyua cheo kinacho sifika..” (17:79)

Kauli Yake:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ ﴿٥٩﴾

“Enyi mlio amini! Mt’iini Mwenyezi Mungu, na mt’iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi....” (4:59)

Na kauli Yake:

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ
أَقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنْ
اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرْتَصُّوا حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا
يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٢﴾

“Sema: Ikiwa baba zenu, na wenenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyo yachuma, na biashara mnazo ogopa kuharibika, na majumba mnayo yapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu.” (9-24).

Na kauli Yake:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

“Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu....” (3:110).

Na kauli Yake:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُونَ الرَّسُولُ
عَلَيْكُمْ شَهِيدًا

“Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu....” (2:143).

Minhajil Muslim

Na kauli Yake:

“Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Yeye Allah”

Na kauli Yake:

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ

“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu...” (3:31).

1) Taarifa za Mtume Muhammad ﷺ kuhusu utume wake na kuwa utume wake ndio mwisho wa utume na kwamba ni wajibu kumtii. Na kuwa utume wake ni kwa watu wote kama alivyosema Mtume ﷺ.

“Mimi na Nabii wala si urongo, mimi ni mtoto wa Abdi-I-Muttwalib.” (Bukhari na Muslim).

Kauli yake:

“Mimi ni mja wa Allah na Mwisho wa Manabii, na hakika Nabii Adamu ameumbwa kwa udongo wa mwamba”. (Bukhari katika Taarikhii, na Ahmad na Ibn Hibban ameisahihisha).

Na kauli yake:

“Mfano wangu na mfano wa Mitume waliopita kabla yangu ni sawa na mfano wa Mtu aliyejenga nyumba akaitengeneza vizuri na akairembesha isipokuwa mahala pa nafasi ya tofali moja, watu wakawa wanazunguka nyumba hiyo na wanaipenda na wanasema kwa nini halikuwa kwa tofali hili? Basi mimi ndiye hilo tofali nami ni mwisho wa Manabii.” (Bukhari, Muslim).

Mtume ﷺ pia amesema,

“Namuapia yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake kuwa hawi muumini kamili mmoja wenu mpaka anipende mimi zaidi kuliko mtoto wake na mzazi wake na kuliko watu wote” (Bukhari).

Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Kila mmoja wenu ataingia peponi isipokuwa atayekataa wakamuuliza nani atakayekataa ewe Mjumbe wa Allah?’ Akasema:”Atakayenitii ataingia peponi na atakayeniasi atakuwa amekataa”. (Bukhari).

Na kauli yake:

“Hakika Utume na Unabii umekwisha, hakuna Mtume baada yangu wala Nabii.” (Ahmad na At-Tirmidhi ameisahihisha.)

Na kauli yake:

“Nimefadhilishwa kuliko Mitume wengine kwa mambo sita: nimepewa ufasaha wa mazungumzo, na nimenusuriwa kwa adui kuingiwa na uoga, na nimehalalishiwa ngawira na imefanywa kwangu ardhi kuwa msikiti na itwahaarika na nimetumwa kwa viumbe wote, na utume umehitimishiwa kwangu.” (Muslim, At-Tirmidhi).

“Atakaye nitii basi amentii Allah na atakayeniasi basi amemuasi Allah na atakayemtii amiri wangu basi amenitii na atakayemuasi Amiri wangu basi ameniasi.” (Bukhari).

Na kauli yake:

“Hakika ya pepo imekatazwa kwa Mitume wote mpaka kwanza niingie mimi, na imekatazwa kwa umati wote mpaka waingie umma wangu.” (Ameipokea Daraqutny na ina njia zengine zinazoifanya iwe katika daraja la Hassan.).

Minhajil Muslim

Na kauli yake:

“Ikifika Siku ya Kiyama nitakuwa Imamu wa manabii na mtowa khutuba wao na muomba shufaa wao na wala sijifakhiri.” (At-Tirmidhi na Ibn Majah, Ahmad).

Na kauli yake ziwe juu Amani:

“Mimi ni bwana wa watoto wa Adam Siku ya Kiyama, na wa kwanza kufufuliwa Siku ya Kiyama, na wa mwanzo kuomba, na wa mwanzo kukubaliwa ombi lake.” (Muslim).

4) Ushahidi wa taurati na Injili unashuhudia kutumwa kwake na utume wake. Pia na kubashirikwa Mtume Musa na Issa (juu yao Amani). Amesema Allah Mtukufu katika maneno aliyoyaeleza Nabii Issa:

وَإِذْ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ يَبْنِي إِسْرَائِيلَ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُولٍ يَأْتِي مِنْ بَعْدِي اسْمُهُ أَحْمَدٌ فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ مُبِينٌ ﴿١٧٠﴾

“Na Isa bin Mariamu alipo sema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninaye thibitisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakaye kuja baada yangu; jina lake ni Ahmad! Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi ulio dhaahiri!” (61:06).

Amesema Allah:

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُمْ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ وَهُمْ لَهُمُ

الطَّيِّبَاتِ وَمُحَرَّمَ عَلَيْهِمُ الْخَبِيثَاتِ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ
عَلَيْهِمْ

“Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao.....” (7:157).

Na imekuja katika Taurati:

“Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye anawaambia yote ninayomwamuru na asiyeyafuata maneno yake anayoyazungumza kwa jina langu, mimi ndiye nitakaye muadhibu kwa kosa hilo.” (Kum:Taurati 18:18).

Kwa hiyo biashara hizi zilizothibiti ndani ya Taurati mpaka leo ni ushahidi wa kutosha kwa utume wa nabii wetu na ujumbe wake na uwajibu wa kumfuata na ulazima wa kumtii. Na ni hoja dhidi ya Myahudi hata kama wanapotosha na kuupinga ukweli, kwani kauli yake: **“Nitawawekea nabii”**, bila ya shaka inathibitisha unabii na Utume wake Mtume Muhammad ﷺ kwani anayeelezwa hapa ni Mussa عليه السلام naye ni Nabii na ni Mtume ﷺ, na atayekuwa mfano wake atakuwa Nabii na Mtume-Rasul. Na kauli yake kuwa katika **“ndugu zao”** ni wazi kabisa kuwa huyo ni Muhammad ﷺ.

Na kauli yake:

“Nami nitatia maneno yangu kinywani mwake” anakusudiwa nabii wetu Muhammad ﷺ kwa sababu yeye ndiye anayeyasoma maneno ya Allah na anayahifadhi nayo ni Qu’ani Tukufu.

Na kauli yake:

“Atawaeleza kila kitu”,

pia ni ushahidi, kwasababu Nabii Muhammad ameyaelezea mambo ya ghaibu asoyaeleza Nabii asiyekuwa yeye, kwani ameeleza baadhi ya yaliokuwa na yatakayokuwa mpaka Siku ya Kiyama”.

Na yamekuja katika Taurati maelezo yafuatayo:

“Ewe Nabii Sisi Tumekupeleka kuwa Mbashiri na Mkhofishaji, na kinga kwa wasiojuu kusoma na kuandika. Wewe ni mja wangu na Mjumbe Wangu, nimekuita mutawakil-hauna tabia mbaya wala nzito na wala haukuwa kama mpiga kelele sokoni, na ovu haliondolewi kwa ovu jingine, lakini anasamehe na kufuta makosa ya aliyemkosea na haliendelezi kosa mpaka watu wasema” “Hakuna Mola mweuye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah.” Na atafungua kupitia kwake macho yasiyoona, na masikio yasiyosikia na nyoyo zilizofunikwa.” (Bukhari).

Na imekuja pia katika Taurati:

“Wamenishambulia si kwa ajili ya Allah, na wamenikasirisha kwa kutetea wanavyo viabudia ambavyo ni batili, nami ninawashambulia kwa kutumia watu (taifa) ambao hawajui kusoma wala kuandika”.

Kwa hiyo kauli yake kuwa: Kwa Taifa la wasiojua kusoma ni tamko la wazi kuwa Mtume ni Muarabu, kwani yeye kaba ya utume alikuwa katika ujahili hata Mayahudi walikuwa wanawaita Waarabu kuwa ni watu wasio jua kusoma na kuandika, kama pia ilivyo kuja katika Taurati kauli yake:

“Fimbo itaendelea kuwepo kwa yahudha, mwenye kutoka katika kizazi chake mpaka atakapokuja mwenye yote, naye ndiye anayesubiriwa na mataifa”.

Kwa hiyo Mayahudi, walikuwa wanamsubiri Mtume ﷺ zaidi kuliko watu wote, kwa kukiri kwao wao wenyewe nani waliyemsubiri katika mataifa asiye kuwa

Mtum wetu Muhammad ﷺ. Isipokuwa roho mbaya na husuda waliyonayo ndicho kilichowanyima imani ya kumkubali na kumfuata yeye na wafuasi wake. Kama alivyosema Allah katika *Suratil-Baqarah*:

وَكَاثُوا مِنْ قَبْلُ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا
عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٨٩﴾

“...na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri - yalipo wajia yale waliyo kuwa wakiyajua waliyakanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu juu ya wakanushao!” (2:89).

Kama zilivyokuja ndani ya Injili biashara zifuatazo:-

1) Katika masiku hayo alifika Yohana mbatizaji akitowa wito na mawaidha huku akibashiri ujio wa Nabii katika bara la Mayahudi akisema:

“Leteni toba kwa sababu umekaribia ufalme wa mbinguni.”
(Marko :01:15)

Kwa hiyo neno lake: *“Umekaribia ufalme wa Mbinguni”*. Ni biashara ya kuja kwa Muhammad ﷺ pia kukaribia Utume wake, kwani yeye ndie aliyetawala na kuhukumu kwa Sheria ya mbinguni.

2) Akawapa mfano mwengine akisema:

“Ufalme wa mbinguni unafanana na mbegu moja ya khardan alioichukuwa mwanadamu akaipanda shambani mwake ikiwa ndogo kuliko mbegu zote, lakini ilipokuwa ikawa kubwa kuliko mbegu zote”

Aliyekusudiwa hapo ni Muhammad na wafuasi wake.

3) *“Naondoka kwa sababu nisipoondoka hatawajia huyo (Palqrit) ama nikiondoka nitamtuma kwenu, na akishafika huyo ataeleza ulimwengu kosa lake.” (Yohana 16:07).*

Hivi maelezo hayo katika Injili hayakuwa bayana katika ubashiri wa ujio wa Muhammad ﷺ?”

Nani huyo Palqrit kama si Muhammad? Na nani aliyuonya ulimwengu kwa kosa lake kama si yeye? Kwa sababu yeye ndiye aliyetumwa huku ulimwengu ukiwa unaogelea ndani ya bahari ya maovu na uharibifu, na ushirikina umeota mizizi mpaka kwa Ahlil Kitab. Na ni nani huyo aliyekuwa baada ya kuondoka kwa Nabii Issa akawaita watu kumuamini Allah Bwana wa mbingu na ardhi asiyekuwa Muhammad?

Hoja za Kiakili:

- 1) Kuna pingamizi gani kwa Allah kumtuma Muhammad ﷺ na kumfanya Mjumbe, wakati tayari kabla yake amekwisha watuma mamia ya wajumbe na maelfu ya Manabii? Na ikiwa akili na sheria havioni kizuizi cha kutumwa kwa Muhammad, wanaokataa ujumbe wake na kuukufuru utume wake wanafanya hivyo kwa kutumia hoja gani?
- 2) Mazingira yaliyotawala kipindi cha kupewa kwake Utume ﷺ yalikuwa yanahitaji ujumbe kutoka mbinguni. Mjumbe atakaye wafundisha upya binadamu namna ya kumjua muumba wao.
- 3) Uharaka wa kuenea kwa Uislamu katika pande zote za ulimwengu, na maeneo mbalimbali katika miji, na jinsi watu wanavyopokea Uislamu, na kuuona kuwa ndio dini bora kuliko dini zengine, ni hoja ya ukweli wa utume wake ﷺ.
- 4) Usahihi wa misingi aliyokuja nayo Mtume ﷺ na ukweli na kufa kwake na kudhihiri kwa matokeo yake ambayo ni mazuri yenye baraka ni ushahidi kuwa yanatoka kwa Allah na kuwa alieyaeleza ni Mtume wa Allah na Nabii wake.
- 5) Miujiza iliyotokea mikononi mwake na matukio yasiyokuwa ya kawaida ambayo akili inayaona ni muhali bali haiwezekani kutokea kwa asiyekuwa Mtume na Nabii wa Allah.

Hapa nataja baadhi tu ya miujiza hiyo kama ilivyopokelewa katika hadithi sahihi za Mtume ﷺ zinazofanana na hadithi *mutawatir* ambazo hazipingi isipokuwa aliye na akili dhaifu au asiye na akili kabisa.

a) Kupasuka kwa mwezi Al-Wailid Ibn Mughira na wengine miongoni mwa makafiri wa Makkah walimtaka Mtume ﷺ Muujiza – utaohibitisha dai lake la unabii na Utume. Kwa hiyo mwezi ulipasuka kwa ajili yake ukawa vipande viwili: kipande kimoja kikawa juu ya mlima na cha pili chini ya mlima, na Mtume ﷺ akawaambia: “Shuhudieni! Baadhi yao wakasema: “Tumeuona mwezi kati ya mianya miwili ya mlima (mlima wa Abii Qubaiisi)”

Maquraishi waliwauliza watu wa miji mingine, “Je wameona mapasuko wa mwezi?” Nao wakawaeleza kama walivyoona na katika hili ikashuka kauli ya Allah:

أَفْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَادْشَقَّ الْقَمَرُ ﴿١﴾ وَإِنْ يَرَوْا آيَةً يُعْرَضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ

مُسْتَمِرٌّ ﴿٢﴾ وَكَذَّبُوا وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ۖ وَكُلُّ أُمَّرٍ مُّسْتَقَرٌّ ﴿٣﴾

“Saa imekaribia, na mwezi umepasuka! Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Huu uchawi tu unazidi kuendelea. Na wamekanusha na wamefuata matamanio yao. Na kila jambo ni lenye kuthibiti.” (54: 1-3).

b) Jicho la Qatada lilipatwa na maumivu Siku ya Uhud mpaka likaangukia kwenye kitefute (sehemu ya chini ya jicho) chake, Mtume ﷺ akalirejesha kwenye nafasi yake na likawa zuri mno kuliko awali.

c) Kumwa macho kwa Ali Ibn Abi Twalib رضي الله عنه Siku ya Khaibara akayapulizia Mtume ﷺ yakapona yakawa kama vile hayakuwa na maumivu yoyote kabisa.

d) Ugoko wa Ibn Hakam ulivunjika katika vita vya Badri Mtume ﷺ akaapulizia basi wakati huo huo akapona na hakuwa na maumivu tena.

e) Mti kushuhudia Utume wake: Mtu mmoja Muarabu alimsogelea Mtume, na Mtume ﷺ akamuuliza yule mtu:

“Ewe bedui (yaani Mwarabu wa shamba) unakwenda wapi? Yule mtu akajibu, ‘Ninakwenda iliko familia, yangu.’ Mtume akasema, ‘Waonaje ukaenda kwenye kheri?’ Yule mtu akauliza: ‘Ni kheri ipi hiyo?’ Akasema: ‘Ukiri kwa moyo wako na utamke kwa ulimi wako kuwa hakuna Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah Peke Yake. Yule mtu akasema: ‘Nani anayekushuhudia kwa hayo uyasemayo?’ Mtume ﷺ akamwambia, ‘Mti ule’, ‘Anaushiria mti ulio kingoni mwa jangwa, mti ukaja ukichana ardhi mpaka ukasimama mbele yake na akautaka utoe ushahidi mara tatu mti ule ukashuhudia kama alivyosema Mtume ziwe juu yake Rehma na Amani.’ (Sunani Darami).

f) Kigogo cha mtende kumlilia Mtume ﷺ kwa sauti walioisikia walipokuwa msikitini kwake. (Muslim).

Hayo yalitokea wakati alipokiacha Mtume ﷺ kigogo hicho baada ya kukitumia kwa mimbari yake aliyokuwa anayotolea khutuba, pale aliojengewa mimbari na akaacha kupanda juu ya kile kigogo. Basi kikalialia kwa mapenzi na hamu ya Mtume ﷺ, ilisikika sauti yake kama sauti ya ngamia aliye na mimba ya miezi kumi, na hakikunyamaza mpaka pale Mtume ﷺ alipokiendea, na akauweka mkono wake Mtukufu juu yake na hapo kikanyamaza.

g) Dua yake Mtume ﷺ aliyo muombea mfalme Kisra ili usambaratike ufalme wake na kweli ukasambaratika.

h) Dua yake Mtume ﷺ aliyomuombea Ibnu Abbas ili aifahamu dini, matokeo yake Ibnu Abbas akawa ni bahari ya elimu kwa Umma huu.

i) Kuongezeka kwa chakula kichache kwa dua yake ﷺ. Kwa vibaba viwili tu vya shairi (ngano) wakila na kutosheka watu zaidi ya thamanini.

j) Kuongezeka kwa maji machache kwa dua yake Mtume ﷺ siku ya vita vya Hudaibia. Watu walikumbwa na matatizo ya kiu na Mtume alikuwa na kiriba

(chombo) kidogo tu cha maji ya kutawadhia, na watu wakamuendea aliko, na wakamwambia hatuna maji isipokuwa uliyonayo ndani ya kiriba chako kidogo hiki. Mtume ﷺ akaweka mkono wake ndani ya kile kiriba cha maji yakawa yanafurika kutoka kati ya vidole vyake kama vile chemchem watu wakanywa na wakatawadha. Walikuwa watu alfu moja na mia tano.

k) Tukio la Israa na Miiraji kutoka Masjidil Haram (Makkah) mpaka *Masjid-Aqswa Baitil Maqdis*- mpaka mbingu ya saba mpaka *Sidratil-Muntaha* na akarudi usiku ule na joto la alipolala bado halijapoa.

l) *Qur'anul Karim*, kitabu ambacho ndani yake mna khabari za waliopita kabla yetu na habari za watakaokuja baada yetu na hukumu za yalio kati yetu. Ndani yake mna muongozo na nuru. Kwa kweli Qur'an ndio muujiza mkubwa wa Mtume ﷺ na alama ya kudumu ya Unabii wake. Kwa kudumu huko imekuwa ni dalili yenye kuendelea na hoja ya kudumu juu ya viumbe mpaka mwisho wa dunia. Kwa hiyo Qur'an tukufu ni miongoni mwa miujiza mikubwa aliyopewa Mtume ﷺ na ni ubainifu mkubwa aliyopewa, na kuhusu Qur'an Mtume ﷺ anasema:

“Miongoni ma manabii waliotumwa hakuna nabii yeyote ila alipewa miujiza ambao kwayo watu walimuamini. Ama mimi miujiza niliopewa ni wahyi (ufunuo) alioniteremshia Allah. Hivyo nataraji nitakuwa na wafuasi wengi zaidi ya Mitume wengine Siku ya Kiama.” (Bukhari na Muslim).



Mada ya Kumi

Kuamini Siku ya Mwisho

Muislamu anaamini kuwa maisha haya ya duniani yana wakati wa mwisho wake, maisha haya yatakoma, kisha yanakuja maisha ya pili ndani ya nyumba ya akhera na hapo Allah Atawafufua viumbe na atawakusanya Kwake wote ili awape mahesabu yao. Awalipe waliofanya mema wapate neema ya kudumu kwa kuishi peponi, na awalipe waliofanya maovu adhabu yenye kudhalilisha kwa kuingizwa motoni.

Muislamu anaamini pia kuwa haya yatatanguliwa na alama za kiamama vile kuozeza kwa masihi muongo, Yaajuja na Ma'ajuja, kuteremka kwa Issa عليه السلام, kuibuka mnyama, kuchomoza jua kutoka Magharibi na alama nyingine.

Kisha litapulizwa baragumu mpulizo wa kufa viumbe vyote kisha mpulizo wa kufufua na kisha kusimama mbele ya Bwana wa viumbe wote. Kisha vitatolewa vitabu, na kuna atakayepokea kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, na kuna atakayepokea kwa mkono wa kushoto. Itawekwa mizani na itapita hisabu na itatandikwa njia (*swiratwa*) na hapo kisimamo kikubwa kitamalizika kwa kuingia peponi watu wa peponi, na kuingia motoni watu wa motoni. Hayo yanathibitishwa kwa hoja za Qur'an zifuatazo:-

Hoja za Kunukuliwa:

1) Maelezo ya Allah kuhusu pale aliposema:

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾

“Kila kilioko juu yake kitatoweka. Na atabakia Mwenyewe Mola wako Mlezi Mwenye utukufu na ukarimu.” (55:26-27)

Na kauli Yake

وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّن قَبْلِكَ الْخُلْدَ أَفَإِنَّ مَتَّ فَهُمْ الْخَالِدُونَ ﴿٢٨﴾

“Nasi hatukumjaalia mwanaadamu yeyote kabla yako kuwa na maisha ya milele. Basi je! Ukifa wewe, wao wataishi milele?” (21:34).

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ ۗ وَنَبَلُّوكُم بِالشَّرِّ وَالْحَيْرِ فِتْنَةً ۗ وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٤﴾

“Kila nafsi itaonja mauti; na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa.” (21:35).

Na kauli Yake:

رَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَنْ يُبْعَثُوا ۗ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۗ

وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٦٧﴾

“Walio kufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwani? Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mliyo yatenda. Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu..” (64:7).

Na kauli Yake:

أَلَا يَظُنُّ أُولَٰئِكَ أَنَّهُمْ مَبْعُوثُونَ ﴿٤٦﴾ لِيَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٤٧﴾ يَوْمَ يَقُومُ النَّاسُ لِرَبِّ

الْعَالَمِينَ ﴿٤٨﴾

“Kwani hawadhani hao kwamba watafufuliwa Katika Siku iliyo kuu, Siku watapo msimamia watu Mola Mlezi wa walimwengu wote?” (83: 4-6).

Na kauli Yake:

وَتُنَادِرُ يَوْمَ الْجُمُعِ لَا رَبَّ فِيهِ ۗ فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ ﴿١٠٢﴾

“Na uhadharishe na Siku ya Mkutano, haina shaka hiyo. Kundi moja litakuwa Peponi, na kundi jengine Motoni.” (42-07)

Na kauli Yake:

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ۖ وَأُخْرِجَتِ الْأَرْضُ أَنْقَالَهَا ۖ وَقَالَ
الْإِنْسَانُ مَا هَٰذَا ۖ يَوْمَئِذٍ تُخْبِرُ أَخْبَارَهَا ۗ بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَىٰ لَهَا ۗ
يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ النَّاسُ أَشْتَاتًا لِيُرَوْا أَعْمَالَهُمْ ۗ فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ
حَيْرًا يَرَهُ ۗ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ۗ

“Itakapo tetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake! Na itakapo toa ardhi mizigo yake! Na mtu akasema: Ina nini? Siku hiyo itahadithia khabari zake. Kwa sababu Mola wake Mlezi ameifunulia! Siku hiyo watu watatoka kwa mfarakano wakaonyeshwe vitendo vyao! Basi anaye tenda chembe ya wema, atauona! Na anaye tenda chembe ya uovu atauona!” (99:1-8).

Na kauli Yake:

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ رَبُّكَ أَوْ يَأْتِيَ بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ ۗ
يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِنْ قَبْلُ أَوْ
كَسَبَتْ فِي إِيْمَانِهَا حَيْرًا ۗ قُلِ أَنْتُمْظِرُونَ إِنَّا مُنْتَظِرُونَ ۗ

“Wanangoja jengine ila wawafikie Malaika, au awafikie Mola wako Mlezi, au zifike baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi? Siku zitakapo fika baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi, kuamini hapo hakutomfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake, au amefanya kheri katika Imani yake. Sema: Ngojeni, nasi pia tunangoja.” (6:158).

Kauli Yake:

❖ وَإِذَا وَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ أَخْرَجْنَا لَهُمْ دَابَّةً مِّنَ الْأَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ أَنَّ النَّاسَ

كَانُوا بِعَاقِبَتِنَا لَا يُوقِنُونَ ﴿٢٧﴾

“Na itapo waangukia kauli juu yao, tutawatolea mnyama katika ardhi atakaye wasemeza, ya kuwa watu walikuwa hawana yakini na Ishara zetu..” (27:82).

Kauli Yake:

حَتَّىٰ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُمْ مِّن كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ ﴿٢٨﴾

وَأَقْرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ فَإِذَا هِيَ شَاخِصَةٌ أَبْصَرُ الَّذِينَ كَفَرُوا يَتَوَيْلَنَا قَدْ

كُنَّا فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَذَا بَلْ كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٢٩﴾

“Mpaka watapo funguliwa Juju na Maajuju wakawa wanateremka kutoka kila mlima; Na miadi ya haki ikakaribia. Hapo ndipo yatapo kodoka macho ya walio kufuru (na watasema:) Ole wetu! Bila ya shaka tulikuwa tumeghafilika na haya, bali tulikuwa wenye kudhulumu.” (21:96-97).

Na Kauli Yake:

❖ وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا إِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ ﴿٣٠﴾ وَقَالُوا

ءِإِلٰهَتُنَا خَيْرٌ أَمْ هُوَ ۗ مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا ۗ بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُونَ ﴿٣١﴾

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٣٢﴾ وَلَوْ نَشَاءُ

لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْأَرْضِ يَخْلُفُونَ ﴿٣٣﴾ وَإِنَّهُ لَعِلْمٌ لِّلسَّاعَةِ فَلَا

تَمْتَرْنَ بِهَا وَأَتَّبِعُونَ ۗ هَذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٣٤﴾

“Na alipo pigiwa mfano Mwana wa Mariamu, watu wako waliupiga ukelele. Wakasema: Miungu yetu kwani si bora kuliko huyu? Hawakukupigia mfano huo ila kwa ubishi tu. Bali hao ni watu wagomvi! Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa tuliye mneemesha na tukamfanya ni mfano kwa Wana wa Israili. Na tungeli penda tungeli wafanyia miongoni mwenu Malaika katika ardhi wakifuatana. Na kwa hakika yeye ni alama ya Saa ya Kiyama. Basi usiitilie shaka, na nifuatani. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka.” (43:57-61).

Na Kauli Yake:

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ
ثُمَّ نُفِخَ فِيهِ أُخْرَىٰ فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ ﴿٥٧﴾ وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا
وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجَاءَ بِالنَّبِيِّينَ وَالشُّهَدَاءِ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ وَهُمْ لَا
يُظْلَمُونَ ﴿٥٨﴾ وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٥٩﴾

“Na litapulizwa barugumu, wazimie waliomo mbinguni na waliomo katika ardhi, isipo kuwa aliye mtaka Mwenyezi Mungu. Kisha litapulizwa mara nyengine. Hapo watainuka wawe wanangojea. Na ardhi itang’ara kwa Nuru ya Mola wake Mlezi, na Kitabu kitawekwa, na wataletwa Manabii na mashahidi, na patahukumiwa baina yao kwa haki, wala hawatadhulumiwa. Na kila nafsi italipwa kwa yale iliyo yafanya, na Yeye anayajua sana wanayo yatenda..” (39:68-70).

Na Kauli Yake:

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَإِنْ كَانَ
مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا وَكَفَىٰ بِنَا حَاسِبِينَ ﴿٦١﴾

“Nasi tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumuwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali tutaileta. Nasi tunatosha kuwa washika hisabu.” (21:47).

Na Kauli Yake:

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ نَفْخَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٧﴾ وَحُمِلَتِ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً
 وَاحِدَةً ﴿١٨﴾ فَيَوْمَئِذٍ وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ﴿١٩﴾ وَأَنْشَقَّتِ السَّمَاءُ فَهِيَ يَوْمَئِذٍ وَاهِيَةٌ ﴿٢٠﴾
 وَالْمَلَكُ عَلَى أَرْجَائِهَا ﴿٢١﴾ وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ ثَمَنِيَةٌ ﴿٢٢﴾
 يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَى مِنْكُمْ خَافِيَةٌ ﴿٢٣﴾ فَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ
 فَيَقُولُ هَؤُلَاءِ أَقْرَبُوا كِتَابِيَّةً ﴿٢٤﴾ إِنِّي ظَنَنْتُ أَنِّي مُلَاقٍ حِسَابِيَّةً ﴿٢٥﴾ فَهُوَ فِي
 عِيشَةٍ رَاضِيَةٍ ﴿٢٦﴾ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿٢٧﴾ قُطُوفُهَا دَانِيَةٌ ﴿٢٨﴾ كُلُوا وَاشْرَبُوا
 هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ ﴿٢٩﴾ وَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِشِمَالِهِ
 فَيَقُولُ يَلِيَّتِي لِمَ أُوتِ كِتَابِيَّةً ﴿٣٠﴾ وَلِمَ أُدْرِمَ مَا حِسَابِيَّةً ﴿٣١﴾ يَلِيَّتَهَا كَانَتْ
 الْقَاضِيَةَ ﴿٣٢﴾ مَا أَغْنَىٰ عَنِّي مَالِيَّةٌ ﴿٣٣﴾ هَلَكَ عَنِّي سُلْطَانِيَّةٌ ﴿٣٤﴾ خَذُوهُ
 فَعُلُوهُ ﴿٣٥﴾ ثُمَّ الْجَحِيمَ صَلُّوهُ ﴿٣٦﴾ ثُمَّ فِي سِلْسِلَةٍ ذَرْعُهَا سَبْعُونَ ذِرَاعًا
 فَاسْلُكُوهُ ﴿٣٧﴾ إِنَّهُ كَانَ لَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ ﴿٣٨﴾ وَلَا تَحْضُ عَلَىٰ طَعَامِ
 الْمَسْكِينِ ﴿٣٩﴾

“Na litapo pulizwa barugumu mpulizo mmoja tu, Na ardhi na milima ikaondolewa, na ikavunjwa kwa mvunjo mmoja, Siku hiyo ndio Tukio litatukia. Na mbingu zitapasuka, kwani siku hiyo zitakuwa dhaifu kabisa. Na Malaika watakuwa pembezoni mwa mbingu; na wanane juu ya hawa watakuwa wamebeba Kiti cha Enzi cha Mola wako Mlezi. Siku hiyo mtahudhurishwa - haitafichika siri yoyote yenu. Basi ama atakaye pewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, atasema: Haya someni kitabu changu! Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu. Basi yeye atakuwa katika maisha ya kupendeza, Katika Bustani ya juu, Matunda yake yakaribu. Waambiwe: Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyo tanguliza katika siku zilizo pita. Na ama atakaye pewa kitabu chake katika mkono wake wa kushoto, basi yeye atasema: Laiti nisingeli pewa kitabu changu! Wala nisingeli jua nini hisabu yangu. Laiti mauti ndiyo yangeli kuwa ya kunimaliza kabisa. Mali yangu hayakunifaa kitu. Madaraka yangu yamenipotea. (Pasemwe): Mshikeni! Mtieni pingu! Kisha mtupeni Motoni! Tena mtatizeni katika mnyororo wenye urefu wa dhira sabiini! Kwani huyo hakika alikuwa hamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, Wala hahimizi kulisha masikini.” (69:13-34).

Na Kauli Yake:

فَوَرَبِّكَ لَنَحْشُرَنَّهُمْ وَالشَّيَاطِينَ ثُمَّ لَنُحْضِرَنَّهُمْ حَوْلَ جَهَنَّمَ جِثِيًّا ﴿٦٩﴾ ثُمَّ لَنَنْزِعَنَّ مِنْ كُلِّ شِيعَةٍ أَيُّهُمْ أَشَدُّ عَلَى الرَّحْمَنِ عِتِيًّا ﴿٧٠﴾ ثُمَّ لَنَخْنُقُ أَعْلَمُ بِالَّذِينَ هُمْ أَوْلَىٰ بِهَا صِلِيًّا ﴿٧١﴾ وَإِنْ مِّنكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا كَانَ عَلَىٰ رَبِّكَ حَتْمًا مَّقْضِيًّا ﴿٧٢﴾ ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوْا وَنَذَرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثِيًّا ﴿٧٣﴾

“Basi naapa kwa Mola wako Mlezi! Kwa yakini tutawakusanya wao pamoja na mashet’ani; kisha tutawahudhurisha kuizunguka Jahannamu, nao wamepiga magoti! Kisha kwa

yakini tutawatoa katika kila kundi wale miongoni mwao walio zidi kumuasi Arrahmani, Mwingi wa Rahema..Tena hakika Sisi tunawajua vyema zaidi wanao stahiki kuunguzwa humo. Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia. Hiyo ni hukumu ya Mola wako Mlezi ambayo lazima itimizwe. Kisha tutawaokoa wale walio mchamngu; na tutawaacha madhaalimu humo wamepiga magoti.” (19:68-72).

2) Maelezo ya Mtume ﷺ katika kauli yake,

“Hakitasimama kiama mpaka mtu atapita kwenye kaburi la mwengine na aseme: Natamani nineipata mimi nafasi yake hii.”
(Ahmad, Bukhari na Muslim).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Atatoka Dajali katika umati wangu atakuwa kwa muda wa siku arobaini kisha Allah atamtuma Nabii Issa bin Mariam akifanana na Urwa bin Masudi, atamtafuta dajali kisha atamuua. Baada ya hapo itapita miaka saba bila kuwa na uadui baina yao. Kisha Allah atautuma upepo wa baridi kutokea upande wa Sham. Hatabaki juu ya Ardhi mtu yeyote mwenye angalau chembe ndogo ya imani ila upepo huo utaingiana umchukue, na hapo watabaki duniani watu waovu tu wakiwa wepesi wa mwanzo kama ndege, ndoto zao kama za wanyama mwitu hawajui matendo mema wala hawakatai na kuyaacha maovu. Hapo atajitokeza shetani katika sura ya mwanadamu kisha atamwambia: ‘Mbona haujibu? “Nao watamuuliza: ‘Kwani unatuambia tufanye nini?’” Basi atawaamrisha waanze kuabudu mizimu, na kwa kukubali hilo watakuwa wanapata malipo ya kupata chakula na maisha yao yatabadilika yawe mazuri sana. Kisha litapigwa baragumu la kwanza hapana yeyote atakaye lisikia ila atageuza shingo yake ili apate kusikia vizuri, na wa kwanza kusikia ni mfuga ngamia atakuwa anahudumia ngamia wake. Akaendelea kusema Mtume ﷺ basi mtu huyo atakufa kisha watu wote watakufa. Kisha itashuka mvua kama

Minhajil Muslim

umande, kwa mvua hiyo miili ya watu itanza kuota kisha itapulizwa baragumu jingine, basi watu wote watasimama huku wakiangalia kipi kitachotokea. Kisha itasemwa Enyi watu njooni kwa Mola wenu, na Malaika wataamrisha wa wasimamisha watu ili wauliwe. Kisha itasemwa watoeni watu wa kwenda mtoni. Itaulizwa: kutoka katika ngapi? Itajibiwa kila elfu moja toeni watu mia tisa tisini na tisa. Hiyo ndivyo siku itakayowafanya vijana kuota mvi kwa matisho yake. Na hiyo ndiyo siku ambayo siri zote zitawekwa wazi.” (Ameipokea Muslim).

Na Kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakitasimama kiama isipokuwa kwa watu Wenye shari kuliko watu wote.” (Muslim).

Na katika kauli yake Mtume ﷺ:

“Na muda ulio kati ya pulizo mbili za parapanda ni Arubaini kisha Allah akateremsha maji kutoka mbinguni watu, wataota kama zinavyoota mboga mboga, kila kitu katika mwili wa mwanaadamu kitaoza isipokuwa mfupa wa mgongo na kwa mfupa huo ndio utaanzia kuumba mtu siku ya kiama.”

Na kauli yake Mtume ﷺ katika hutuba yake alisema:

“Enyi watu hakika nyinyi mtafufuliwa mkiwa uchi tena miguu wazi, mkiwa na alama nyeupe kwa ajili ya udhu jueni kuwa kiumbe wa kwanza kuvalishwa nguo nabii Ibrahimu عليه السلام Wataletwa watu katika umati wangu watawekwa katika kundi la watu wa kushoto, nami nitasema Ee Mola wangu hao ni watu wangu naye Mola atasema: “Hakika wewe hujui mambo waliyoyazusha baada yako.” (Ahmad).

Na kauli yake:

“Hataruhusiwa mja kunyanyua nyayo zake Siku ya Kiama mpaka Aulizwe mambo manne: Umri wake ameumaliza katika nini? Na elimu Yake ameifanyia nini? Na mali yake ameipata vipi? Na ameitumia Vipii? Na mwili wake ameuchakaza kwa vipi?” (At-Tirmidhi)

Na kauli yake Mtume ﷺ:


“Birika yangu ukubwa wake ni mwendo wa mwezi, maji yake meupe kuliko maziwa, harufu yake ni nzuri kuliko miski, glasi zake ni kama nyota za mbinguni atakayekunywa maji hayo hapatwi na kiu tena.” (Bukhari, Muslim, Ibn Majah, At-Tirmidhi)

Na kauli yake Mtume ﷺ: Kwa mama Aisha رضي الله عنها wakati alipo ukumbuka moto akalia Mtume akamuuliza:

“Nini kinachokuliza? Akasema mama Aisha: “Nimeukumbuka moto ndio maana nalia.” Kisha akauliza, “Hivi mtazikumbuka familia zenu siku ya Kiyama.” Mtume ﷺ akajibu: ‘Ama sehemu tatu hakuna mtu atakaye mkumbuka mwenzake: Katika mizani mpaka aelewe mizani yake imekuwa nyepesi au uzito, na wakati wa kupeperusha nyaraka mpaka aelewe wapi kitatua kitabu chake kuliani, kushotoni au mgongoni mwake? Na kwenye njia wakati inapowekwa juu ya moto mpaka aivuke.” (Abu Dawud)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Kila nabii ana dua aliyowaombea watu wake nami dua yangu nimeiweka iwe uombezi wangu kwa umma wangu Siku ya Kiama.”

Na kauli yake Mtume 

“Mimi ni bwana wa watoto wa Adam sisemi hilo kwa kujifakhiri nami ni wa mwanzo litaempasukia kaburi siku ya kiama sijifakhiri, nami ni muombaji wa kwanza, nami ni wa kwanza kukubaliwa ombi lake Siji fakhiri; na bendera ya sifa njema iko mikononi mwangu siku ya kiyama sisemi hivyo kwa kuji fakhiri.” (Muslim).

Na kauli yake:

“Na atakayeomba pepo mara tatu, pepo itasema ewe Mola wangu muingize peponi; na atakayejulinda na moto, mara tatu, moto utasema ewe Mola wangu mlinda huyo na moto.” (At-Tirmidhi, na Ibnu Majah).

3) Imani ya mamilioni ya manabii, na mitume, na watu wenye hekima na wanazuoni na watu wema miongoni mwa waja wa Allah wanaoamini Siku ya Mwisho na yote yaliyo kuja katika siku hiyo.

Hoja za Kiakili:

1) Kuwepo uwezekano wa Allah wa kuwarejesha viumbe baada ya kufa. Kwa sababu kuwarejesha kwa mara ya pili si kugumu kama kuumba kwa mara ya kwanza na kuwaleta duniani kwa mara ya kwanza bila ya mfano uliotangulia.

2) Hakuna kisicho ingia akilini katika mambo ya kufufuliwa na malipo kwa sababu akili haikatai isipokuwa jambo la muhali (yasiowezezana) kama vile vinyume viwili kukutana pamoja au kukutana viwili vinaotenguana, na kufufua na malipo si miongoni mwa hayo.

3) Hekima zake Allah zilizo wazi katika matendo yake kwa viumbe wake. Yaliyo bayana katika kila nyanja miongoni mwa nyanja za maisha zinasema ni muhali kukosekana kufufuliwa viumbe baada ya kufa kwao, na kwisha kwa muda wa maisha ya dunia na kulipwa kwa matendo yao ya kheri au ya shari.

4) Kuwepo kwa maisha ya duniani na vilivyomo miongoni mwa neema na matatizo, ni dalili ya kuwepo kwa maisha mengine ambao ni maisha yaliyo na uadilifu, kheri na ukamilifu. Maisha bora zaidi, kiasi cha kuwa maisha haya ya duniani na vilivyo ndani yake miongoni mwa raha na matatizo ukiyalinganisha na maisha ya akhera ni sawa na kulinganisha ghorofa kubwa au bustani miongoni mwa bustani kubwa na kipande kidogo kilichochoywa kwenye kipande cha karatasi.



Mada ya Kumi na Moja

Adhabu na Neema za Kaburini

Muislamu anaamini kuwa, neema na Adhabu za Kaburini, na Maswali ya Malaika wawili ndani ya Kaburi ni vya kweli, kwa hoja za kunukuliwa na za kiakili zifuatazo:

Hoja za Kunukuliwa:

1) Taarifa za Allah kuhusu hayo:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ يَتَوَفَّى الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ
وَأَدْبَرَهُمْ ۗ وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٥٠﴾ ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيكُمْ
وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلْمٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٥١﴾

“Na laiti ungesi ona Malaika wanapo wafisha wale walio kufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao, na kuwaambia: Ionjeni adhabu ya Moto! Hayo ni kwa sababu ya yale yaliyo kwisha tangulizwa na mikono yenu, na hakika Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja.” (8:50-51).

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ
شَيْءٌ ۗ وَمَنْ قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ ۗ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي
غَمْرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنفُسَكُمُ ۗ الْيَوْمَ
تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنتُمْ عَنْ
آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٥٢﴾ وَلَقَدْ جَعَلْنَا فِرْدَوْىٰ كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ

وَتَرَكْتُمْ مَا حَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ ۗ وَمَا نَرَىٰ مَعَكُمْ شُفَعَاءَ كُفَّ الَّذِينَ
 زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَاءَ ۗ لَقَدْ تَقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ عَنْكُمْ مَا كُنْتُمْ
 تَزْعُمُونَ ﴿٩٤﴾

“Nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye mzuliya uwongo Mwenyezi Mungu, au anaye sema: Mimi nimeletewa wahyi; na hali hakuletewa wahyi wowote. Na yule anaye sema: Nitateremsha kama alivyo teremsha Mwenyezi Mungu. Na lau ungesi waona madhaalimu wanavyo kuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyooshea mikono wakiwambia: Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyo kuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyo ya haki, na mlivyo kuwa mkizifanyia kiburi Ishara zake. Nanyi mlitujia wapweke kama tulivyo kuumbeni mara ya kwanza. Na mkayaacha nyuma yenu yote tuliyo kupeni, na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu kwenu. Yamekatika makhusiano baina yenu, na yamekupoteeni mliyo kuwa mkidai.” (6:93:94).

Na kauli Yake:

لَا تَعْلَمُهُمْ سَنُعَذِّبُهُمْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَىٰ عَذَابٍ عَظِيمٍ ﴿١٠١﴾

“...Sisi tunawajua. Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa.” (9:101).

Na kauli Yake:

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا ۖ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ
فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

“Wanaonyeshwa Moto asubuhi na jioni. Na itapo fika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!” (40: 46).

Na kauli Yake:

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي
الْآخِرَةِ ۖ وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ ۗ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ﴿٢٧﴾

“Mwenyezi Mungu huwatia imara wenye kuamini kwa kauli ya imara katika maisha ya dunia na katika Akhera. Na Mwenyezi Mungu huwaacha kupotea hao wenye kudhulumu. Na Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo..”(14:27).

2) Taarifa ya Mtume ﷺ kuhusu hayo ni kauli yake:

“Hakika mja anapowekwa kaburini mwake, na jamaa zake wakaondoka, hakika anausikia mkito wa viatu vyao, na hapo wataamjia Malaika wawili watamkalisha kitako na watamuuliza, Ulikuwa unasema nini kuhusu mtu huyu Muhammad ﷺ?” Ama Muislamu atasema: “Nashuhudia kuwa yeye ni mja wa Allah, na Mjumbe wake”, Ataambiwa aiangalie nafasi yake motoni, badala yake amekubadilishia Allah makazi peponi na ataziona nafasi zote mbili. Ama mnafikiri au kafiri Malaika watamuuliza: “Ulikuwa unasema nini kuhusu mtu huyu?” Atajibu: “Sijui nilikuwa ninasema wanayoyasema watu wengine, basi ataambiwa hukujua wala hukufuata, hapo atapigwa kwa nyundo ya chuma pigo la nguvu atapiga ukelele ambao atausikia kila aliye karibu naye isipokuwa wanaadamu na majini.” (Bukhari).

Kauli yake Mtume ﷺ:

“Mmoja wenu anapofariki anaoneshwa makazi yake asubuhi na jioni kama ni mtu wa motoni basi atakuwa miongoni mwa watu wa motoni na ataelezwa: Haya ndio makazi yako mpaka atakapokufufua Mola wako Siku ya Kiama.” (Bukhari)

Na kauli yake Mtume ﷺ: Katika dua yake:

“Ewe Mola wangu mimi ninajilinda kwako na adhabu ya Kaburi, na fitna za uhai na za kifo, na fitna za Masihi Dajjali.” (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ: wakati alipopita kwenye makaburi mawili akasema:

“Hakika hawa waliomo katika makaburi haya wanaadhibiwa na hawaadhibiwi kwa kosa kubwa”, kisha akasema, ‘ni kweli ama mmoja wao alikuwa kazi yake ni uchochezi, ama mwengine alikuwa hajiepushi na mkojo wake.’ (Bukhari).

Hoja za Kiakili:

1) Kuamini kwa mabilioni ya wanazuoni na watu wema na waumini wengine katika umma wa Muhammad ﷺ na Umma zingine zilizotangulia wote waliamini adhabu ya kaburi na neema zake na yote yaliyopokelewa kuhusu hilo. Mtu yeyote mwenye imani kuhusu Allah na Malaika wake na siku ya mwisho yanalazimisha imani yake hiyo aamini adhabu ya kaburi na neema zake na kila kilichotajwa kuhusu habari za kaburini, kwa sababu yote ni ghaibu. Kwa hiyo, atayeamini sehemu moja kiakili inamlazimu kuamini sehemu nyengine.

2) Adhabu ya kaburi au neema yake, au kinachotokea kaburini kama vile maswali ya Malaika wawili si miongoni mwa mambo yasiyokubalika kiakili au kuyaona kuwa ni muhali, bali akili salama inayakubali hayo na kuyashuhudia.

3) Aliyelala akiwa usingizini anaweza akaota ndoto inayomfurahisha akaona raha na kuneemeka kwa athari ya ndoto hiyo ndani ya nafsi yake usingizini jambo ambalo likamuhuzunisha au kumsikitisha akisha amka akalaumu kwanini ameamka.

Minhajil Muslim

Kama mtu anavyoweza kuota kitu anachokichukia akajihisi vibaya kwa ndoto hiyo na akahuzunika, jambo ambalo litamfanya amshukuru atayemuamsha katika usingizi huo. Kwa hiyo neema au adhabu ndani ya usingizi ni kweli inatokea kwenye roho na hayo si miongoni mwa mambo anayoyahisi mwanadamu wala kuyaona kwa macho yetu, lakini hakuna mtu anayeyapinga kuwa hayapo. Kama hali ni hiyo inakuwaje mtu kujipinga kuwepo adhabu ya kaburini na neema zake?



Mada ya Kumi na Mbili

Kuamini hukumu ya Allah na Qadar yake

Muislamu anaamini hukumu ya Allah, Qadar Yake, Hekima Yake na Utashi Wake, Hakitokei katika ulimwengu – hata matendo ya waja ya khiari yao isiokuwa baada ya Allah kuyakadiria. Muislamu anaamini Allah ni Muadilifu katika Hukumu Yake na Makadirio Yake, ni Mwenye Hekima katika Matendo Yake na Mipango Yake. Hekima Yake inafata baada ya Kutaka Kwake. Anachokitaka Allah kinakuwa na asichokitaka hakiwi, na hakuna hila wala nguvu isipokuwa kwa Allah. Haya yamethibiti kwa hoja za kiakili na za kunakili kama zifuatazo:

Hoja za Kunukuliwa:

1) Allah ameeleza haya aliposema:

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٥٤﴾

“Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo.” (54: 49).

Na kauli Yake:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنْفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَنْ نَبْرَأَهَا إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٥٧﴾

“Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi..” (57:22).

Na kauli Yake:

وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا عِنْدَنَا خَزَائِنُهُ وَمَا نُنزِّلُهُ إِلَّا بِقَدَرٍ مَّعْلُومٍ ﴿٢١﴾

“Na hakuna chochote ila asili yake inatokana na Sisi; wala hatukiteremshi ila kwa kipimo maalumu..” (15:21).

Na kauli Yake:

وَكُلِّ إِنْسَانٍ أَلَزَمْتَهُ طَيْرُهُ فِي عُنُقِهِ ۖ وَخُجِرُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَمَةِ كِتَابًا
يَلْقَاهُ مَنْشُورًا ﴿١٣﴾

“Na kila mtu tumemfungia a’ mali yake shingoni mwake. Na Siku ya Kiyama tutamtolea kitabu atakacho kikuta kiwazi kimekunjuliwa.” (17:13).

Na Kauli Yake:

مَا أَصَابَ مِنْ مُصِيبَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يُؤْمِنْ بِاللَّهِ يَجِدْ قَلْبَهُ عِندَ اللَّهِ
بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١﴾

“Haufiki msiba wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu huuongoa moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu..” (64:11).

Na kauli Yake:

* وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ ۗ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۗ
وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٌ فِي ظُلْمَتٍ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ
وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾

“Na ziko kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinacho bainisha.” (6:59).

Na Kauli Yake:

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٨١﴾

“Wala nyinyi hamtataka isipo kuwa atake Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote. .” (81:29).

Na kauli Yake:

إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ أُولَٰئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُونَ ﴿٢١﴾

“Ama wale ambao wema wetu umewatangulia, hao watatenganishwa na hayo.” (21:101)

Na Kauli Yake:

وَلَوْلَا إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَاءَ اللَّهُ لَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ ۗ إِنَّ تَرَنَ أَنَا
أَقَلَّ مِنْكَ مَالًا وَوَلَدًا ﴿٣٩﴾

“Na lau kuwa ulipo ingia kitaluni kwako ungesi sema: Mashaallah! Alitakalo Mwenyezi Mungu huwa! Hapana nguvu ila kwa Mwenyezi Mungu. Ikiwa unaniona mimi nina mali kidogo na watoto kuliko wewe.” (18:39).

Na Kauli Yake:

وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا اللَّهُ ۗ

“Wala hatukuwa wenye kuhidika wenyewe ingeli kuwa Mwenyezi Mungu hakutuhidi..” (7:43).

2) Maelezo ya Mtume ﷺ kuhusu hayo katika kauli yake:

“Hakika mmoja wenu linakusanywa umbile lake ndani ya tumbo la mama yake kwa siku arobaini akiwa tone la maji ya mbegu, kisha linakuwa pande la damu kama hivyo, kisha pande la nyama kama hivyo hivyo, kisha anapelekewa Malaika na anampulizia roho na anaamrisha mambo manne; aandike riziki yake, muda wake wa kuishi, kazi yake na atakuwa mwema au muovu na naapa kwa yule ataye hakuna Mola isipokuwa Yeye hakika mmoja wenu atafanya matendo ya watu wa peponi mpaka itakuwa kati yake na pepo hakuna ila umbali wa dhiraa moja tu na hapo kitamtangulia kitabu na atafanya matendo ya watu wa motoni na ataingia moto, na hakika ya mmoja wenu atafanya matendo ya watu wa motoni mpaka itakuwa hakuna umbali kati yake na moto ila dhiraa moja tu, na hapo kitamtangulia kitabu akafanya matendo ya watu wa peponi na ataingia peponi.”(Muslim).

Na Kauli ya Mtume ﷺ akimwambia Abdallah Ibn Abbasi:

“Ewe kijana hakika mimi nitakufundisha maneno: “Muhifadhi Allah kwa kutii ari zake nae atakuhifadhi; muhifadhi Allah Utamkuta kila uendako na unapoomba muombe Allah, ukitaka msaa mtake Allah, na elewa lau kama umma ungalijikusanya ili ukunufaishe basi hautakunufaisha ila kwa kile tu alichokuandikia Allah tu, na lau kama watajikusanya ili wakudhuru basi hawangalikudhuru ila kwa kile alichokuandikia Allah tu, kalamu zimekwishamaliza kuandika na nyaraka zimekwishakauka wino ulioandikiwa.” (At-Tirmidhi amesema ni sahihi)

Na kauli ya Mtume ﷺ:

“Cha kwanza alichokiumba Allah ni Kalamu na akaiambia andika, ikasema ewe Mola niandike nini? Akasema:”Andika makadirio ya kile kitu mpaka Kiama kitakaposimama.”(Ahmad na Abu Dawud).

Na kauli ya Mtume ﷺ:

“Walijadiliana nabii Adam na nabii Mussa Nabii Mussa akasema. ‘Ewe Adam wewe ndie Baba yetu umetupa khasara, kwa kututoa peponi.’ Nabii Adam naye akasema: “Wewe ndiye Mussa aliyekuteua Allah kwa kusema Naye na akakuandikia Taurati kwa Mkono wake, unanilaumu kwa jambo alilolikadiria Allah juu yangu kabla hajaniumba kwa miaka Arobaini. ‘Kwa hoja hiyo Adamu akamshinda Mussa.” (Muslim).

Na kauli ya Mtume ﷺ:

“Katika maana ya Imani ni kumuamini Allah, Malaika Zake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Mwisho na kuamini Uwezo Wake wa Kheri Yake na Shari Yake.” (Muslim).

Na kauli ya Mtume ﷺ:

“Fanyeni kazi kwani kila mtu amerahisishiwa kufanya alichoumbiwa.” (Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika ya nadhiri haibadilishi hukumu ya Allah.” (Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ kwa Abdillahi Ibni Qaisi:

“Ee Abdalah Ibni Qaisi hutaki nikuelimishe neno ambalo ni miongoni mwa hazina ya peponi? Sema Hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Allah.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Kwa mtu aliyesema: Akitaka Allah na ukataka wewe Mtume, Akamwambia sema, ‘Akitaka Allah Peke Yake.’ (Ahmad and Ibn Majah).

3) Kuamini kwa mamia ya mamilioni ya watu katika Umma wa Muhammad ﷺ miongoni mwa wanazuoni, wenye hekima wafanya mema na wengineo kuhusu kuthibiti kwa hukumu ya Allah na Qadar Yake, Hekima Yake na Utashi Wake, na kwamba kila kitu kinatanguliwa na Elimu Yake, na kinaendeshwa na Qadari Yake, na hakiwi katika Ufalme Wake isipokuwa anachokitaka na asichokitaka hakiwi, na kwamba kalamu iliandika makadirio ya kila kitu mpaka kitakaposimama Kiyama.

Hoja za Kiakili:

1) Akili hazikatai chochote kinachohusu hukumu, Qadari, Utashi, Hekima, na Kupanga kwa Allah, bali akili inalazimisha kuwepo kwa hayo yote, kutokana na dalili zake za kuyafanya hayo zilizojitokeza hapa duniani..

2) Kumkubali Allah kunalazimisha kuamini Hukumu Yake, Uwezo Wake, Hekima Yake na Utashi Wake.

3) Ikiwa muhandisi, msanifu majengo anachora juu ya karatasi ndogo mchoro wa jengo la ghorofa na akaliwekea muda maalum wa kukamilika kwa ujenzi wake. Kisha akaingia katika ujenzi, na mpaka muda aliyopanga kukimalizika, tayari na ule mchoro ulio kwenye karatasi umekamilika na kuwa nyumba, kama alivyoichora juu ya karatasi bila ya kupungua kitu hata kidogo, na bila kuzidi. Kama mwanaamu ana uwezo wa kupanga jambo na likawa kama alivyolipanga inakuwaje watu wapinge kuwa Allah hawezi kuandika makadirio ya kila kitu ulimwenguni mpaka Kiama kitapofika. Kisha kwa ukamilifu wa Uwezo Wake, na Elimu Yake juu ya kila kitu hayo aliyoyakadiria yakatokea kama alivyokadiria katika kiwango chake na aina yake na muda wake na pahala pake. Yote hayo ikizingatiwa kuwa Yeye ana uwezo wa kufanya jambo lolote.



Mada ya Kumi na Tatu

Tauhid katika Ibada

Muislamu anauamini Uungu wa Allah kwa viumbe wa mwanzo na wa mwisho, na Uumbaji Wake kwa viumbe wote, na kwamba hakuna Mola asiyekuwa yeye, na hakuna mlezi zaidi yake. Kwa sababu hiyo Muislamu Ibada zake zote anazielekeza kwa Allah tu, ibada ambazo Allah Ameziamrisha kwa waja wake wamuabudu kwa kufanya ibada hizo. Kwa hiyo Muislam haelekezi chochote katika ibada hizo kwa asiyekuwa Allah kwa hiyo anapomba anamuomba Allah, na anapotaka msaada anamtaka Allah, na anapoweka nadhiri hamuwekei asiye kuwa Allah kwa hiyo anayeyaelekeza kwa Allah tu matendo yake yote ya ndani kama vile khofu, matarajio, kutegemea, kupenda, kutukuza, na matendo ya dhahiri, kama vile Swala, Zaka, Funga, Hija na Jihadi hayo yote anayafanya kwa hoja za kunukuliwa na za kiakili zifuatazo:

1) Amri ya Allah kuhusu hilo:

إِنِّي أَنَا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدْنِي وَأَقِمِ الصَّلَاةَ لِذِكْرِي ﴿١٤﴾

“Hapana mungu ila Mimi tu. Basi niabudu Mimi, na ushike Sala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi.” (20:14).

Na kauli yake Allah:

وَإِنِّي فَأَرْحَمُونَ ﴿٤٠﴾

“...na niogopeni Mimi tu.” (2:40).

Na kauli Yake:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ
تَتَّقُونَ ﴿١٤﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ

السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَكُمْ ۗ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أُندَادًا
وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢١﴾

“Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka. (Mwenyezi Mungu) ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua.” (2:21-22).

Na kauli Yake:

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

“...Basi jua ya kwamba hapana mungu ila Mwenyezi Mungu.” (47:19)

Na kauli Yake:

وَإِمَّا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٦﴾

“Na Shetani akikuchochea kwa uchochezi wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua..” (41:36)

Na kauli Yake:

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٣﴾

“Mwenyezi Mungu, hapana mungu isipo kuwa Yeye. Na juu ya Mwenyezi Mungu nawategemee Waumini..” (64:13).

2) Maelezo yake Allah kuhusu hayo aliposema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطُّغُوتَ
فَمِنْهُمْ مَن هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَن حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ

“Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo alio waongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao ulio wathibitikia upotovu.” (16: 36).

Na kauli Yake:

فَمَن يَكْفُرْ بِالطُّغُوتِ وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَى
لَا انفِصَامَ لَهَا وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

“... Basi anaye mkataa Shetani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua..” (2:256).

Na kauli Yake:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا
فَاعْبُدُونِ

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu..” (21:25).

Na katika kauli Yake:

قُلْ أَفَغَيْرَ اللَّهِ تَأْمُرُونِي أَعْبُدُ أَيُّهَا الْجَاهِلُونَ ﴿٦٤﴾

“Sema: Je! Mnaniamrisha nimuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, enyi majaahili?” (39: 64).

Na kauli Yake:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada.” (1:5).

Na kauli Yake:

يُنزِلُ الْمَلَكَةَ بِالرُّوحِ مِنْ أَمْرِهِ عَلَى مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ أَنْ أَنْذِرُوا أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاتَّقُونِ ﴿٢٠﴾

“Huwateremsha Malaika na Roho kwa amri yake juu ya amtakaye katika waja wake ili nyinyi muonye kwamba hapana mungu ila Mimi, basi nicheni Mimi..” (16:2).

3) Maelezo ya Mtume ﷺ kuhusu hayo katika kauli yake kwa Muadh Ibn Jabali رضي الله عنه wakati alipomtuma Yemen akamwambia,

“Na kiwe cha mwanzo unachowalingania watu kuwa wampwekeshe Allah.” (Bukhari na Muslim).

4) Na kauli yake pia:

“Ewe Muadhi unaelewa nini haki ya Allah ilio juu ya waja?” Akasema: “Allah na Mjumbe wake ndio wanaoelewa akasema wamuabudu na wasimshirikishe kwa chochote.”

Na kauli Yake kwa Abdallah Ibni Abbasi رضي الله عنه:

“Ukitaka kuomba basi muombe Allah na unapotaka msaada mtake Allah.”

Katika kauli yake kwa aliyemwambia mtu.

“Mungu akipenda na wewe ukipenda.” Mtume akamwambia sema:
“Akipenda Allah Peke Yake.”

Na katika kauli yake:

“Kubwa mno ninalo hofia juu yenu ni shirki ndogo, Wakauliza ‘kwani shirki ndogo ni nini Ewe Mjumbe wa Allah’: Akasema: ‘Ni riya.’ Kwani atasema Allah kesho Siku ya Kiama akishawalipa waja kwa matendo yao, “Nendeni kwa wale mliokuwa mkifanya ibada ili wakuoneni mliokuwa duniani ili muone watawapeni malipo gani?” (Ahmad)

Na kauli yake:

“Je, na hawakuwa wanawahalalishia alichokiharamisha Allah nanyi mnakihalalisha na wanaharamisha alichokihalalisha nanyi mnakiharamisha?” Wakasema, ‘Ndio.

Akasema: “Basi huko ndiko kuwaabudu’, na hayo amemwambia Adiyi bin Hatim wakati alipolisoma neno lake Allah:

اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرَهْبَتَهُمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ

“Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu....” (9:31)

Na Adiyi alisema,

“Ee Mjumbe wa Allah hatukuwa tunawaabudu.” (At-Tirmidhi).

Na kauli yake:

“Mie sio wa kutakiwa uwokovu bali Allah ndiye anayetakiwa.”
(Atwabarani) aliyasema hayo Mtume ﷺ wakati waliposema baadhi ya masahaba kuwa ‘twendeni tukamuombe Mtume atuokoe na manafiki huyu (kwa mnafiki aliyekuwa anawaudhi)’.

Na kauli yake:

Na atakayeapa kwa asiye kuwa Allah atakuwa amemshirikisha.”
At-Tirmidhi na Ahmad).

Na kauli yake:

“Hakika zindiko, hirizi na tiwala (Yaani dawa za mwanamke za kupendwa na mume) yote hayo ni ushirikina” (Ahmad, Abu Dawud, na Ibn Majah).

Hoja za Kiakili:

- 1) Allah Kuwa Kwake Peke yake katika kufanya kazi za Kuumba, Kutoa riziki, Kuendesha na Kupanga, Upekee huu unalazimisha kuwa Yeye ndiye wa kuabudiwa peke na kuwa hana mshirika na yeyote au chochote katika kuabudiwa huko.
- 2) Viumbe wote wameumbwa na Yeye, na wanamhitajia Yeye. Kwa hali hiyo hakuna anayefaa kuabudiwa pamoja naye.
- 3). Kama anayeombwa dua au kutakiwa kuokoa au kuombwa kuepusha balaa au uadui, na hawezi wala hamiliki uwezo wa kujibu dua aliyoombwa wala kuokoa wala kuinga, basi hafai kuombwa na kumuomba ni batili. Pia hafai kumuwekea nadhiri ya kumtegemea. Kwa hali hiyo anabaki Allah ndiye wa kuabudiwa kwani Yeye Pekee ndiye Mwenye Uwezo wa kuyafanya hayo yote.

Mada ya Kumi na Nne

Wasila

Muislamu anaamini kuwa Allah anapenda matendo yaliyo mema na yale yanayofaa zaidi na mazuri sana. Ama katika waja wake Anaowapenda ni wale wafanyao mema.

Muislamu pia anaamini kwamba Allah amewataka waja wake kujisogeza kwake, na kujipendekeza kwake na kutumia wasila wake. Hayo ndiyo yanayomfanya mja awe karibu na Allah. Kwa kujisogeza Kwake kwa matendo mema na maneno mazuri. Kwa hiyo Muislamu anamuomba Allah kujikurubisha Kwake kwa Majina Yake yaliyo mazuri, na Sifa Zake za juu, na anamuamini Yeye na Mjumbe wake ﷺ anapenda Yeye na mjumbe wake na anawapenda watenda mema na Waumini wote. Mja huyu anajikurubisha kwa kuswali Swala za faradhi na kwa kutoa Zaka, na Kufunga, na Kuhiji, pamoja na kuswali Swala za sunna. Kama anavyojikurubisha kwake kwa kuyaacha ya haramu, na kujiepusha na yaliyokatazwa. Hamuombi Allah kupitia cheo cha yeyote miongoni mwa viumbe wake, wala tendo la mja miongoni mwa waja zake. Kwa sababu cheo cha mtu si miongoni mwa chumo lake litakalomuwezesha amuombe Allah kwa kulitumia hilo, au alitangulize mbele kuwa ni kikurubisho kwa Mola. Allah hakuweka kwa waja zake sheria ya kujisogeza Kwake kwa kutumia kisicho kuwa matendo yao na usafi wa roho zao, kwa imani na kufanya matendo mema. Haya yamethibiti kwa hoja za kunukuliwa na kiakili zifuatazo:

Hoja za Kunukuliwa:

1) Maelezo yake Mola kuhusu hilo alisema:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعِزَّةَ فَلِلَّهِ الْعِزَّةُ جَمِيعًا ۖ إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ
الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ ۗ وَالَّذِينَ يَمْكُرُونَ السَّيِّئَاتِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۖ وَمَكْرُ
أُولَئِكَ هُوَ يَبُورُ ﴿١٠٣﴾

“Mwenye kutaka utukufu basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye hupanda neno zuri, na a’ mali njema Yeye huitukufa. Na wanao panga vitimbi vya maovu watapata adhabu kali. Na vitimbi vya hao vitaondokea patupu..” (35:10)

Na kauli Yake:

يَتَأْتِيهَا الرُّسُلُ كُلُّوَا مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَأَعْمَلُوا صَالِحًا إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٤١﴾

“Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa mnayo yatenda” (23:51).

وَأَدْخَلْنَاهُ فِي رَحْمَتِنَا إِنَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٥﴾

“Na tukamuingiza katika rehema yetu. Hakika yeye ni miongoni mwa watenda mema..” (21:75).

Na kauli Yake:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَأَبْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ وَجَاهِدُوا فِي سَبِيلِهِ

لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ ﴿٣٥﴾

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na tafuteni njia ya kumfikilia. Na wanieni kwa juhudi kwa ajili yake ili mpate kuokoka..” (5:35).

Na kauli Yake:

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ

غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٠٤﴾

“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuatani mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu.” (3:31).

Na kauli Yake:

رَبَّنَا آمَنَّا بِمَا أَنْزَلْتَ وَاتَّبَعْنَا الرَّسُولَ فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴿٣١﴾

“Mola wetu Mlezi! Tumeyaamini uliyo yateremsha, na tumemfuata huyu Mtume, basi tuandike pamoja na wanao shuhudia.” (3:53).

Na kauli Yake:

رَبَّنَا إِنَّا سَمِعْنَا مُنَادِيًا يُنَادِي لِلْإِيمَانِ أَنْ ءَامِنُوا بِرَبِّكُمْ فَءَامَنَّا رَبَّنَا فَاغْفِرْ
لَنَا ذُنُوبَنَا وَكَفِّرْ عَنَّا سَيِّئَاتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ الْأَبْرَارِ ﴿١٩٣﴾

“Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumemsikia mwenye kuita akiitia Imani kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi; nasi tukaamini. Basi tusamehe madhambi yetu, na utufutie makosa yetu, na utufishe pamoja na watu wema” (3:193).

Na kauli Yake:

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا ۖ وَذَرُوا الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ ۚ
سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٨٠﴾

“Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanao haribu utakatifu wa majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda..” (7:180).

Na kauli Yake:

كَلَّا لَا تُطِيعُهُ وَأَسْجُدْ وَاقْتَرِبْ ﴿١٩﴾

“Hasha! Usimt’ii! Nawe sujudu na ujongee!” (96:19).

2) Maelezo ya Mtume wake ﷺ kuhusu hayo aliposema:

“Hakika Allah ni mzuri kwa hiyo hakubali isipokuwa matendo na maneno mazuri.” (Muslim).

Na kauli Yake:

“Jitambulisha kwa Allah wakati wa Neema atakutambuwa wakati wa matatizo.” (At-Tirmidhi).

“Na hakujikurubisha Kwangu mmoja wenu kwa kitu Nikipendacho zaidi kuliko kile nilichokiwajibisha juu yake, na mja ataendelea kujikurubisha kwangu kwa Ibada za sunna mpaka nitampenda.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli Yake Allah katika hadithi aliyoipokea kutoka kwa Mola wake.

“Kama atajikurubisha Kwangu kiasi cha shubiri Nitakaribia kwake kiasi cha dhiraa, na Akijikurubisha kwangu kiasi cha dhiraa Nitakaribia kwake kiasi cha upana wa vitanga viwili ya mikono, na Akinijia anatembea kwa miguu Nitamjia mbio.” (Bukhari)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Katika kisa cha watu wa pangoni ambao jiwe lilifunika mlango wao wa kutokea pale alipotawasali mmoja wao kwa wema alioufanya kwa wazazi wake, na wa pili kwa kuacha alichokiharamisha Allah, na watatu kwa kuirejesha amani kwa muhusika pamoja na kuipenda, walifanya hivyo baada ya

kuambiana kuwa: “Angalieni katika matendo mema mliyoyafanya na muombeni Allah kwayo huenda akawapatia njia ya kutoka wakaomba na wakajikurubisha kwa Allah, naye akawaondolea lile jiwe, na wakatoka pangoni wakiwa salama” (Bukhari na Muslim).

Na kauli Yake:

“Mja anakuwa karibu mno na Mola wake anapokuwa katika sijida.”

Na kauli yake:

“Ewe Mola wangu ninakuomba kwa kila jina lako ulilojiita au Umeliteremsha ndani ya Kitabu Chako, au umemfundisha yoyote miongoni mwa viumbe wako, au umelibakisha kwako katika Elimu yako ya Ghaibu uifanye Qur’ani Tukufu kirutubisho cha moyo wangu na nuru ya kifua changu, na kuondoa huzuni yangu, na kitulizo cha wasiwasi wangu na huzuni yangu.” (Ahmad)

Na kauli yake:

“Mtu huyu ameomba kwa jina la Allah ambalo Allah hakuombwa kwalo isipokuwa atatowa, na hakuitwa kwalo isipokuwa atajibu.” (At-Tirmidhi na Ibn Majah).

3) Habari za Mitume zilizopokelewa katika Qur’an zinazoeleza kuwa wakifanya walivyokuwa wakifanya tawasul, na kwamba hatawasali kwao kulikuwa kwa kuyatumia majina yake ‘Allah na kwa Sifa Zake na kwa Imani na kufanya hizo Yusuf عليه السلام amsema katika kujikurubisha kwa Allah:

* رَبِّ قَدْ آتَيْتَنِي مِنَ الْمَلِكِ وَعَلَّمْتَنِي مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ ۚ فَاطِرَ
السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَنْتَ وَلِيِّ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۖ تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحَقْنِي

بِالصَّالِحِينَ ﴿١٠٧﴾

“Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika umenipa utawala, na umenifunza tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema.” (12:101).

Nabii Yunus عليه السلام amesema,

أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠١﴾

“...Hapana mungu isipo kuwa Wewe Subhanaka Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.” (21:87).

Na Mussa عليه السلام amesema:

قَالَ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَاغْفِرْ لِي فَغَفَرَ لَهُ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٦﴾

“Akasema: Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu; basi nisamehe. Akamsamehe; hakika Yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.” (28: 16)

وَقَالَ مُوسَىٰ إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ مِنْ كُلِّ مُتَكَبِّرٍ لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٢٧﴾

“Na Musa akasema: Mimi najikinga kwa Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi anilinde na kila mwenye jeuri asiye iamini Siku ya Hisabu” (40:27).

Ibrahim عليه السلام na Ismail عليه السلام wamesema:

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ

السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

“Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipo inyanyua misingi ya ile Nyumba wakaomba: Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi..” (2:127).

Adamu na Hawa wamesema:

قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿١٢٧﴾

“Wakasema: Mola wetu Mlezi! tumejidhulumu nafsi zetu, na kama hutusamehe na kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika.” (7:23)

Hoja za Kiakili:

1) Kujitosheleza kwa Allah, na kuhitajia kwa mja ni jambo linalolazimisha mja mwenye mahitaji ajisogeze karibu na Allah Tajiri Aliyeshinda kwa njia ya tawasuli, ili mja huyo fakiri na dhalili aweze kusalimika na kile anachokiogopa, na akakipata kile anachokipenda.

2) Kutokujua kwa mja nini anachokipenda Allah Aliyetukuka na nini Anachokichukia katika matendo na maneno ni jambo linalolazimisha kuwa kujikurubisha kuwe kwa kile Alichokiweka Allah tu na Akakibainisha kwa Mjumbe wake miongoni mwa maneno mazuri na matendo mema yanayo fanywa. Na maneno mabaya na matendo mabaya yaepukwe na kuachwa.

3) Ni kwamba cheo cha mtu mwingine ambacho siyo chako wala siyo wewe uliyesababisha kipatikane, ni jambo lisiloruhusu mtu mwingine kufanya tawasuli ya kumuomba Allah kwa kukitumia cheo hicho. Kwani cheo cha mwenzako (hata kama cheo hicho kikubwa sana) hakiwezi kutumiwa na mtu mwingine kwa tawasuli ya kumuomba Allah na kujikurubisha kwake. Isipokuwa kama mtu huyo alichangia au kusababisha kupatikana kwa cheo cha huyo mwenzake kwa njia ya kumsaidia kwa kutumia nguvu yake au kutoa mali mpaka akafikia kupata cheo hicho. (Kama vile kumfadhili mtu kwa kumsomesha mpaka yule mtu akawa shekhe au mtalaamu tena mcha Mungu) hapo si vibaya kukitumia cheo chake kwa kutawasuli kwa Allah kwa kukitaja cheo kile. Kwani ni miongoni mwa kazi alizozifanya kwa kutoa mali yake au nguvu yake, lakini pia iwe alifanya kazi hiyo kwa nia ya kutaka radhi ya Allah tokea mwanzo wa kufanya kwake kazi hiyo ya ufadhili.

Mada ya Kumi na Tano

Mawalii wa Allah na karama zao na Mawalii wa Shaitwani na mazingaombwe yao

1) Mawalii wa Allah:

Muislamu anaamini kuwa Allah ana mawalii, waja zake aliowatenga kwa ibada Yake na Anawatimia katika kumtii Yeye na Anawapa heshima ya kumpenda, na Akawapa karama zake. Kwa huyo Yeye ni mtawala wao na Anawapenda na ana ukaribu nao. Nao ni wapenzi wake, wanampenda, wanamtukuza, wanatekeleza amri yake na wanaacha kwa katazo lake. Wanapenda kwa penzi lake na wanachukia kwa kuchukia kwake wanapomuomba anawapa na wanapotaka msaada anawasaidia na wanapojilinda kwake anawalinda.

Muislamu anaamini mawalii kwamba wao ndio wenye imani kamilifu na wacha-Mungu, na ni wenye karama na ishara njema duniani na akhera. Muislamu pia anaamini kuwa kila Muumini mcha-Mungu huyo ni walii wa Allah isipokuwa wanatofautiana daraja zao kulingana na ucha-Mungu mkubwa zaidi ya mwengine, basi na daraja yake kwa Allah inakuwa kubwa zaidi na karama zake ni nyingi zaidi. Kwa hiyo Mabwana wa mawilii wa Allah ni Mitume na Manabii, na baada ya wao ni Waumini, na kwamba karama anazozipitisha Allah mikononi mwao kama vile, chakula kichache kuwa kingi, au kuponya maumivu na magonjwa, au kuingia katika bahari au kutoungua kwa moto na yanayofanana na hayo nayo ni katika miujiza isipokuwa muujiza una ambatana na upinzani wakati karama haina upinzani na wala haina uhusiano. Na kwamba karama kuwa mno ni kutokutetereka katika kumtii Allah kwa kuyafanya yaliyoamrisha na sheria, na kujiepusha na yaliyokatazwa na kuharamishwa. Hiyo yamethibiti kwa hoja zifuatazo:-

Hoja za Kunukuliwa:

a) Taarifa Zake Allah kuhusu mawilii zake na karama zao katika kauli Yake:

“Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika. Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu.

لَهُمُ الْبَشَرَىٰ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۗ لَا تَبْدِيلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۗ
ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٤﴾

“...Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hapana mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu. Huko ndiko kufuzu kukubwa.” (10:64).

Na kauli Yake:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ط

“Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walio amini. Huwatoa gizani na kuwaingiza mwangazani.” (2:257).

Na kauli Yake:

وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ ۗ إِنِ أَوْلِيَآؤُهُ إِلَّا الّٰمْتَنِقُونَ وَلٰكِن كَثُرْهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٤﴾

“... Wala wao hawakuwa ndio walinzi wake, bali walinzi wake hawakuwa ila wacha-Mngu tu. Lakini wengi katika wao hawajui.” (8:34).

Na kauli Yake:

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِمِ ۗ وَهَمَّ بِهَا لَوْلَا اَنْ رَّءَا بُرْهَانَ رَبِّهٖ ۗ ط

“Na hakika yule mwanamke alimtamani, na Yusuf angeli mtamani lau kuwa hakuona ishara ya Mola wake Mlezi.....” (12:24).

Na kauli Yake:

كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ وَجَدَ عِنْدَهَا رِزْقًا ۖ قَالَ يَمْرُؤُا أَنَّىٰ لَكَ هَٰذَا ۖ
قَالَتْ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ۖ إِنَّ اللَّهَ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٧﴾

“...Kila mara Zakariya alipo ingia chumbani kwake alimkuta na vyakula. Basi alimwambia: Ewe Maryamu! Unavipata wapi hivi? Naye akasema: Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.” (3:37).

Na kauli Yake:

وَإِنَّ يُونُسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣٩﴾ إِذْ أَبَقَ إِلَى الْفُلْكِ الْمَشْحُونِ ﴿١٤٠﴾ فَسَاهَمَ
فَكَانَ مِنَ الْمُدْحَضِينَ ﴿١٤١﴾ فَالْتَقَمَهُ الْحُوتُ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿١٤٢﴾ فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ
الْمُسْتَجِيبِينَ ﴿١٤٣﴾ لَلَبِثَ فِي بَطْنِهِ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٤٤﴾

“Na hakika Yunus alikuwa miongoni mwa Mitume. Alipo kimbia katika jahazi lilio sheheni. Akaingia katika kupigiwa kura, na akawa katika walio shindwa. Samaki akammeza hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa. Na ingeli kuwa hakuwa katika wanao mtakasa Mwenyezi Mungu, Bila ya shaka angeli kaa ndani yake mpaka siku ya kufufuliwa..” (37:139-144).

Na kauli Yake:

فَنَادَاهَا مِن تَحْتِهَا أَلَّا تَحْزَنِي قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ تَحْتَكِ سَرِيًّا ﴿١٥٦﴾ وَهَزَيْتَ إِلَيْكَ يَجْدَعُ
الْخَلَّةَ تُسْقِطُ عَلَيْكَ رَطْبًا جَنِيًّا ﴿١٥٧﴾ فَكُلِّي وَاشْرَبِي وَقَرِّي عَيْنًا ۖ فَأِمَّا تَرِينٌ مِّنَ
الْبَشَرِ أَحَدًا فَقُولِي إِنَّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَنِ صَوْمًا فَلَنْ أُكَلِّمَ الْيَوْمَ إِنْسِيًّا ﴿١٥٨﴾

“Pakatangazwa kutoka chini yake: Usihuzunike! Hakika Mola wako Mlezi amejaalia chini yako kijito kidogo cha maji! Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu. Basi kula, na kunywa, na litue jicho lako. Na pindi ukimwona mtu yeyote basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu.” (19: 24-26).

Na Kauli Yake:

قُلْنَا يَنْتَازُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿٦٩﴾ وَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ

الْأَخْسَرِينَ ﴿٧٠﴾

“Sisi tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim! Wao walimkusudia maovu, lakini Sisi tukawafanya wao ndio walio khasiri.” (21:69-70).

Na kauli Yake:

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ أَصْحَابَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿٩١﴾ إِذْ أَوَى

الْفِتْيَةُ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا

رَشَدًا ﴿٩٢﴾ فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿٩٣﴾ ثُمَّ

بَعَثْنَاهُمْ لِنَعْلَمَ أَيُّ الْحِزْبَيْنِ أَحْصَىٰ لِمَا لَبِثُوا أَمَدًا ﴿٩٤﴾

“Bali unadhani ya kwamba wale Watu wa Pangoni na Maandishi walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara zetu? Vijana hao walipo kimbilia kwenye pango walisema: Mola wetu Mlezi! Tupe rehema itokayo kwako, na tutengezee uwongofu katika jambo letu. Tukayaziba masikio yao kuwalaza humo pangoni kwa muda wa miaka kadhaa wa kadhaa. Kisha tukawazindua ili tujue ni lipi katika makundi mawili lililo hisabu sawa muda walio kaa.” (18:9-12).

b) Maelezo ya Mtume ﷺ kuhusu mawalii wa Allah na karama zao aliposema kauli yake katika hadithi aliyoipokea kutoka kwa Mola swake.

“Atakayeninyanyasia walii wangu nimemtangazia vita, na hakujisogeza Kwangu mja kwa kitu nikipendacho zaidi kama kufanya kile Nilichokiwajibisha juu yake na ataendelea kujisogeza kwangu mja wangu kwa kutenda matendo ya sunna mpaka Ninampenda, na nikishampenda basi Ninakuwa sikio lake analosikilizia, na jicho lake analoonea na mkono wake anaoshikia, na mguu wake anaotembelea, na kama ataniomba (wallahi) Nitampa na akinitaka ulinzi nitamlinda.”

Na kauli Yake:

“Mimi ni Mwenye kulipiza kwa walii zangu kwa yeyote atakaye wafanyia ubaya kama anavyolipiza simba mwenye hasira.” Na kauli yake: “Hakika Allah ana watu kama watamuapia Allah angaliwatakasaa.” (Bukhari, Muslim).

Na katika kauli yake:

‘Kulikuwa na mama mmoja alikuwa anamnyonyesha mwanawe akamuona mtu juu ya farasi aliyevaa vazi la kheri, akasema: “Ewe Mola wangu mfanye mwanangu awe kama mtu huyu.” Yule mtoto akamwangalia yule mtu huku ananyonya kisha akasema: Ewe Mola wangu usinifanye kama yeye.” (Bukhari na Muslim).

Kwa hiyo kutamka mtoto mdogo anayenyonya ni karama kwa mtoto na mzazi wake.

Na katika Kauli Yake:

“Kuhusu kisa cha Juraiji Mcha Mungu na mama yake aliposema Mama yake kuwa: “Ewe Mola wangu usimuue Juraiji mpaka umuoneshe nyuso za makahaba, na Allah akamkubalia ombi lake zikiwa ni karama kutoka kwake Allah kwa mama wa Juraiji, na

mwanawe Juraiji—akasema wakati walipomtuhumu kuwa yule mtoto wa zinaa aliyezaliwa ni wa Juraiji, Juraiji alipomuuliza yule mtoto anayenyonya: ‘We mtoto baba yako nani?’ Mtoto akajibu: ‘Baba yangu ni mchungu mbuzi.’ (Bukhari).

Kwa hiyo kusema kwa mtoto yule anayenyonya ilikuwa ni karama kwa Juraiji kutokana na ucha-Mungu wake:

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Kuhusu wale watu watatu wa pangoni ambao liliwafunika jiwe wakamuomba Allah na kutawasili kwake kwa matendo yao mema, na Allah akawapokelea na akawafungulia mpaka wakatoka wakiwa salama ni karama” (Bukhari na Muslim).

Na katika kauli yake:

“Katika kisa cha mtawa na kijana mna maelezo haya: Yule kijana amempiga jiwe mnyama aliyewazuia watu kupita njia, akampiga kwa jiwe akafa na wauu wakapita tukio hilo kwa mtoto ni karama, na kwa njia mbali mbali mfalme ametaka kumuua yule kijana bila ya mafanikio kama vile kumuangusha kutoka kwenye kilele cha mlima mrefu na akamtupa baharini akatoka anatembea wala hakufa, haya yote ni karama kwa yule kijana Muumini mfanya mema.” (Muslim).

c) Visa vya mawalii na karama walivyovipokea na kuviona maelfu ya maulamaa havina idadi. Baadhi ya hivyo kwa mfano: Malaika walikuwa wakimsalimia Imran Ibn Huswain رضي الله عنه. Na kuwa Salman al-Farisi na Abudardai walikuwa wana kula katika sahani ikawa sahani au chakula kilichokuwa ndani ya sahani kikatamka SubhanaLlaahi. Na kuwa Khubaibu رضي الله عنه ametekwa na Mushirikina wa Makka akawa analetewa Zabibu anakula kipindi ambacho Makka hakuna zabibu.

Baraa Ibn ‘Azib رضي الله عنه alikuwa anapo kula kiapo kwa Allah katika jambo, basi Allah atamjibu kama alivyoomba. Hata ilipofika siku ya Qaadisiya akala kiapo

kwa Allah awawezeshe Waisamu kupata ushindi dhidi ya Mushirikina na awe wa kwanza katika vita hiyo, kufa shahidi, basi ikatokea hivyo hivyo kama alivyoomba.

Na kwamba Umar Ibnil Khatwab siku moja alikuwa anatoa khutba akiwa juu ya mimbari ya Mtume ﷺ, ghafla akasikika anasema: “Ewe Saria kimbilia mlimani! Alikuwa anamuelekeza kiongozi wa vita anayeitwa: Saria na Saria akaisikia sauti ya Umar akakimbilia mlimani pamoja na jeshi, na kwa kufanya kwao hivyo ulipatikana ushindi, na maadui zake Mushirikina wakashindwa. Na Saria akarudi akamueleza Umar na maswahaba wengine sauti ya Umar رضي الله عنه aliyoisikia.

Na ‘Alaa Ibn Hadhrami رضي الله عنه alikuwa anasema katika dua yake: **“Ya ‘Alim ya Hakim, Ya ‘Aliyyu ya ‘Adhim”** na anajibiwa mpaka amefikia kuingia baharini pamoja na kikosi cha askari kilichokuwa pamoja nae wala havikuroa vitu vilivyo kuwa juu ya farasi wao.

Kulikuwa na mtu mmoja anamnyanyasa Hasaan al-Basri basi akaomba dua dhidi yake yule mtu akafa hapo hapo. Kuna mtu moja wa kabila la Nnakhai alikuwa na punda akafa punda wake wakiwa njiani katika safari basi yule mtu akatawadha akaswali raka mbili kisha akamuomba Allah amrudishie uhai Punda wake Allah akapokea dua ile Punda akapata uhai tena akabeba mizigo kisha wakaendelea na safari. Na mengine yasiyokuwa haya katika karama nyingi ambazo hazina idadi na ambazo zimeshuhudiwa na maelfu ya watu.

2) Mawalii wa Shaitwani:

Kama Muislamu anavyo amini kuwa Shaitwani anawapenzi katika wanaadamu aliowatawala na akawasahaulisha kumkumbuka Allah, akawashawishi watende mabaya, na akawapambia maovu. Akawafanya wawe viziwi haki wasiisikilize, na wakawa vipofu hoja za haki wasizione, kwa hiyo wanamtii yeye tu. Anawachochea kufanya shari, na kuwavuta kwenye uharibifu kwa kuwapambia kwao, akawambia huo uovu ndio wema, na wema ndio uovu. Pia wakatambua hivyo. Kwa hiyo wakawa dhidi ya mawalii wa Allah au kinyume chao kwani wale wamempenda Allah na hawa ni maadui zake. Wale wamempenda na wamemridhia na hawa wamemkasirisha na kumchukiza, basi iko juu yao laana ya Allah na ghadhabu zake. Hata kama zitajitokeza Alama zisizokuwa za kawaida kwao kama vile kuruka angani, au kutembea juu ya sakafu ya maji. Kwa sababu kutokea matendo kama hayo ya kifanywa na maadui wa Allah maana yake Allah

anawavuta kidogo kidogo, au wanafanya hayo kwa msaada wa shaitwani kwa wapenzi wake, na hayo yanathibitishwa kwa hoja zifuatazo:-

a) Maelezo ya Allah kuhusu mawalii wa shetani aliposema:

ط وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ الطَّانُغُوتُ يُخْرِجُونَهُمْ مِنَ النُّورِ
ط إِلَى الظُّلُمَاتِ أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

“Lakini walio kufuru, walinzi wao ni Mashet’ani. Huwatoa kwenye mwangaza na kuwaingiza gizani. Hao ndio watu wa Motoni, na humo watadumu..” (2:257).

Na kauli Yake:

ط وَإِنَّ الشَّيَاطِينَ لَيُوحُونَ إِلَى أَوْلِيَآئِهِمْ لِيُجَدِّدُواكُمْ وَإِنَّ
ط أَطَعْتُمُوهُمْ إِنَّكُمْ لَمُشْرِكُونَ ﴿١٢١﴾

“...Na kwa yakini mashet’ani wanawafunza marafiki zao kubishana nanyi. Na mkiwafuata basi hapana shaka nyinyi mtakuwa washirikina.” (6:121).

Na kauli Yake:

ط وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا يَمَعَشَرَ الْجِنَّ قَدِ اسْتَكْبَرْتُمْ مِنَ الْإِنْسِ وَقَالَ أَوْلِيَآؤُهُمْ
ط مِنَ الْإِنْسِ رَبَّنَا اسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ وَبَلَّغْنَا أَلْجَلَّتْ لَنَا قَالِ
ط النَّارُ مَقْوَنُكُمْ خَالِدِينَ فِيهَا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٢١﴾

“Na ile Siku atapo wakusanya wote awaambie: Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika wanaadamu. Na marafiki zao katika wanaadamu waseme: Mola Mlezi wetu! Tulinufaishana sisi na wao. Na tumefikia ukomo wetu ulio tuwekea. Basi Mwenyezi Mungu atasema: Moto ndio makaazi yenu, mtadumu humo, ila apendavyo Mwenyezi Mungu. Hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye hikima, na Mwenye kujua..” (6:128).

Na kauli Yake:

وَمَنْ يَعِشْ عَنِ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقِصْ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ
﴿١٦﴾ وَإِنَّهُمْ لَيَصُدُّونَهُمْ عَنِ السَّبِيلِ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُّهْتَدُونَ ﴿١٧﴾

“...na atakayepuuza utajo wa Allah Tutamsaliti na ‘shaitwani atakuwa ndiye rafiki yake na mashaitwani watawapoteza njia huku wakidhani kuwa wameongoka.” (43:36-37).

Na kauli Yake:

إِنَّا جَعَلْنَا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٦﴾

“...Hakika Sisi tumewafanya Mashet’ani kuwa ni marafiki wa wasio amini..” (7: 27).

Na katika kauli Yake:

فَرِيقًا هَدَىٰ وَفَرِيقًا حَقَّ عَلَيْهِمُ الضَّلَالَةُ ۗ إِنَّهُمْ اتَّخَذُوا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ
دُونِ اللَّهِ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُّهْتَدُونَ ﴿١٧﴾

“Hali ya kuwa kundi moja amelihidi, na kundi jengine limethibitikiwa na upotofu. Kwa hakika hao waliwafanya mashetani kuwa ndio marafiki walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, na wanadhani kuwa wao wameongoka.” (7:30).

Na kauli Yake:

﴿ وَقِيضْنَا لَهُمْ قُرْنَاءَ فَزَيُّوهُم مَّا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أَمْرٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ إِنَّهُمْ كَانُوا خَاسِرِينَ ﴾

“Na tukawawekea marafiki, na wakawapambia yaliyo mbele yao na nyuma yao. Basi ikawathibitikia kauli wawe pamoja na mataifa yaliyo pita kabla yao, miongoni mwa majini na watu. Hakika hao wamekuwa ni wenye kukhasirika.” (41:25).

Na kauli Yake:

﴿ وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا ﴾

“Na tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam! Walimsujudia isipo kuwa Iblisi. Yeye alikuwa miongoni mwa majini, na akavunja amri ya Mola wake Mlezi. Je! Mnamshika yeye na dhuriya zake kuwa marafiki badala yangu, hali wao ni adui zenu? Ni ovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu.” (18: 50).

2) Maelezo ya Mtume ﷺ kuhusu hayo katika kauli yake wakati alipoiona kimondo iliyorushwa ikitoa mwanga akasema kuwaambia maswahaba wake:

“Na kabla ya Uislamu tukio kama hili mlikuwa mnalisemaje?” Wakasema, “Tulikuwa tunasema kuwa kuna mtu mkubwa atakayekufa au atakayezaliwa.”

Mtume ﷺ akasema:

“Kimondo hakirushwi kwa kufa, au kuzaliwa yoyote, lakini Mola wetu Aliyetukuka anapo hukumu jambo humsabihi Malaika wabeba Arshi kisha humsabihi viumbe wa mbinguni ambao wanao wafuatia kisha wanaofuatia, itaendelea hivyo tasbihi mpaka itawafikia walio katika uwingu huu wa dunia kisha walio mbinguni watawauliza wanaobeba Arshi: “Mola wetu amesema nini?” Nao watawaeleza alichosema, kisha walio kila uwingu watataka waelezwe mpaka taarifa zitawafikia walio katika uwingu wa Dunia, hapo mashaitwani watatega masikio ili wasikie na hapo ndipo wanaporushiwa vihenga vya moto nao na habari walizozipata huwapa viongozi wao, anachokileta kama kilivyo hicho ni sahihi lakini wao wanaongeza ya kwao...” (At-Tirmidhi, Muslim na, Ahmad).

Na kauli yake Mtume ﷺ wakati alipoulizwa kuhusu makuhani Mtume ﷺ akasema:

“Hao si chochote” Wakasema: “Ndio wanatuambia maneno wakati mwengine yanakuwa kama walivyosema.” Mtume ﷺ akasema neno hilo ndilo lile la kwanza ambalo wanalolipora majini na kuliweka masikioni mwa kiongozi wao na wanaliongezea mengine pamoja na ya urongo.” (Bukhari na Muslim)

Na kauli yake:

“Hakuna yeyote miongoni mwenu isipokuwa ana rafiki ambaye ni Shaitwani.” (Muslim).

Na kauli yake:

“Hakika Shaiwani anatembea katika mishipa ya mwanadamu kama inavyotembea damu katika mishipani m-baneni kwa kuwabana njia zake kwa funga.” (Bukhari na Muslim).

3) Mambo mengi wanayoyaona na kuyashuhudia Malaika ya wanadamu kuhusu hali za ajabu za kishetani kila zama na mahala zikitokea kwa ‘mawalii wa mashetani’. Baadhi yao wanawaletea aina mbalimbali za chakula na vinywaji, na baadhi yao wanawatimizia kazi zao, na kuna wengine wanaonyesha na kuwaeleza mambo ya ghaibu kuhusu siri na undani wa baadhi ya mambo. Na wengine wanawakinga zisiwafikie silaha. Wengine shetani kwake anajitokeza katika sura ya mtu mwema na hasa mtu anapokuwa anamuomba mtu mwema ili apate kumdanganya na kumpoteza ili apate kumshirikisha Allah na kumuasi. Kuna mashetani wengine wanaweza wakampeleka nchi ya mbali, au kumletea watu au mahitaji kutoka mbali, na mengi yasio kuwa hao miongoni mwa matendo ambayo kufanyika kwake kunawapa nguvu mashetani, maafiriti wa kijini na wengineo wachafu.

Na hali hizi za kishetani zinapatikana zikiwa ni matokeo ya roho mbaya ya kibinadamu kwa sababu ya mambo mbalimbali mabaya anayoyafanya ya ufisadi na ukafiri na maasi ambayo yako mbali na haki yako mbali na kheri, imani na wema. Mpaka manadamu huyo kwa ubaya wa nafsi yake, roho yake inakuwa sawasawa na roho za mashetani ambazo zimeumbiwa ubaya na shari, na hapo urafiki na mapenzi kati ya shetani na mwanaadamu vitakamilika na wanapelekeana mawasiliano wao kwa wao, na wanatumikiana. Kila mmoja anakifanya kilicho katika uwezo wake ndio maana wanapokuja ambiwa habari za siku ya kiamama,

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا يَمَعَشَرَ الْجِنِّ قَدِ اسْتَكْبَرْتُمْ مِنَ الْإِنسِ^ط
وَقَالَ أَوْلِيَاؤُهُمْ مِنَ الْإِنسِ رَبَّنَا اسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ

“Na ile Siku atapo wakusanya wote awaambie: Enyi makundi ya majini! Hakika nyinyi mmechukua wafuasi wengi katika wanaadamu. Na marafiki zao katika wanaadamu waseme: Mola Mlezi wetu! Tulinufaishana sisi na wao.....” (6:128).

Ama tofauti iliopo kati ya karama za mawalii wa Allah na hali za kishetani, inajitokeza katika mwenendo na tabia za mtu mhusika, kama atakuwa miongoni mwa waumini na wacha-Mungu na akawa ni mwenye kushikamana na sheria ya

Minhajil Muslim

Allah, kwa dhahiri na siri basi kitachofanyika kitakuwa ni karama kutoka kwa Allah.

Kama atakuwa ni miongoni mwa watu wabaya waovu walio mbali na ucha-Mungu, waliozama ndani ya maasi na ndani ya ukafiri na ufisadi basi yanayotokea kwake yasiyo ya kawaida yanakuwa ni istid-raji:

(Yaani Allah anampa uwezo wa kufanya hayo ili azidi kuwa jeuri na kuzidisha maasi au anafanya hayo kwa msaada wa shetani).



Mada ya Kumi na Sita

Kuamini Wajibu wa Kuamrisha Mema na Kukataza Maovu

1) Kuamini Wajibu Wa Kuamrisha Mema na Kukataza Maovu:

Muislamu anaamini kuwa kuamrisha mema na kukataza maovu ni wajibu, juu ya kila Muislamu aliye baleghe, mwenye akili timamu mwenye kuweza. Muislamu aliyelielewa zuri akaliona limeachwa au amelielewa ovu na akaliona litafanywa na akaweza kuliamrisha au kuliondoa kwa mkono wake au ulimi wake.

Hilo ni miongoni mwa makubwa yaliyo wajibishwa kidini baada ya kumuamini Allah, Allah Amesema,

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ
وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ

“Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu.” (3:110).

Na hayo yamethibitishwa kwa hoja za kunukuliwa na za kiakili zifuatazo:-

a) Hoja za Kunukuliwa:

1) Amri yake Allah alipoamrisha watu kufanya kazi ya kuamrisha mema na kukataza maovu kwa kusema:

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ
وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

“Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio walio fanikiwa.” (3:104).

2) Na maelezo Yake kuhusu waliopata nusra Yake kuwa wao wanaamrisha mema na wanakataza maovu aliposema:

الَّذِينَ إِذَا مَكَتَهُمْ فِي الْأَرْضِ أَخَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوْا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا
بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ وَاللَّهُ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ ﴿٢٤١﴾

“Wale ambao tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Swala, na wakatoa Zaka, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote.” (22:41).

Na kauli Yake:

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ
عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
أُولَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

“Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humt’ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hikima..” (9:71).

Na kauli Yake kuhusu wali wake Luqman عليه السلام alipokuwa Luqman anamuonya mwanawe:

يَبْنِي أَقْبِرَ الصَّلَاةَ وَأْمُرَ بِالْمَعْرُوفِ وَأَنَّهُ عَنِ الْمُنْكَرِ وَأَصْبِرَ عَلَيَّ مَا أَصَابَكَ
إِنَّ ذَلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿٧١﴾

“Ewe mwanangu! Shika Swala, na amrisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayo kupata. Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa...”(31:17).

Na kauli ya Allah akieleza janga lililowafika wana wa Israil,

لُعِبَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَى لِسَانِ دَاوُدَ وَعِيسَى ابْنِ
مَرْيَمَ ذَلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿٧٨﴾ كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ
عَنْ مُنْكَرٍ فَعَلُوهُ لَبِئْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٧٩﴾

“Walilaaniwa walio kufuru miongoni mwa Wana wa Israili kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryamu. Hayo ni kwa sababu waliasi na wakawa wanapindukia mipaka. Walikuwa hawakatazani maovu waliyo kuwa wakiyafanya. Hakika ni maovu yalioje mambo waliyo kuwa wakiyafanya!” (5:78-79).

Kauli Yake Allah katika aliyoyaeleza kuhusu wana wa Israil kuwa Allah Aliwasalimisha wanaoamrisha mema na wanaokataza maovu na aliwahilikisha waliyoacha kufanya hivyo:

فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِمُ أَجْمِئَتِنَا الَّذِينَ يَنْهَوْنَ عَنِ السُّوْءِ وَأَخَذْنَا الَّذِينَ
ظَلَمُوا بِعَذَابٍ بَئِيسٍ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿١٦٥﴾

“Basi walipo yasahau waliyo kumbushwa, tuliwaokoa walio kuwa wakikataza maovu, na tukawatesa walio dhulumu kwa adhabu mbaya kwa vile walivyo kuwa wakifanya upotovu.” (7:165).

3) Na Mtume ﷺ ameamrisha hilo katika kauli yake:

Minhajil Muslim

“Atakayeliona ovu miongoni mwenu basi aliondoe kwa mkono wake, na asipoweza kuliondoa kwa mkono aliondoe kwa ulimi wake, na asipoweza alichukie kwa moyo wake na huo ndio udhaifu wa Imani.” (Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Na amrیشانeni mazuri na katazaneni maovu, na msipofanya hivyo Allah Atawaleta adhabu kutoka kwake kisha mtamuomba na hatawajibu.” (Abu Dawud na Ahmad)

4) Maelezo yake Mtume ﷺ:

“Hakuna watu waliofanya maovu na kati yao wapo wanaoweza kuwakataza na hawakufanya hivyo, isipokuwa Allah atawaadhibu wote kwa adhabu kutoka kwake” (Tirmidhi)

Na kauli yake kwa Abi Thaalabah Al-Khushaniyi alipomuuliza tafsiri ya neno la Allah,

“Na hata wadhuru aliyepotea kama mtaongoka.”

Akasema Mtume ﷺ:

“Ewe Thaalaba amrisha mema na kataza maovu, kama utaona watu wamezidisha ubakhili na matamano, dunia inafuatwa na inaonwa bora, na kila mmoja anaona kuwa rai yake ndio sahihi, basi hapo iokoe nafsi yako, na waache wasiojua, kwani nyuma yenu kutakuwa na fitna kama kipande cha usiku wa kiza, kipindi hicho atayeshikamana na mfano wa mlichoshikamana nacho kama hivi (yaani Dini) atapata malipo ya watu khamsini miongoni mwenu. 'Akasema: "Bali khamsini miongoni mwao Ewe Mjumbe wa Allah." Akasema: "Hapana bali miongoni mwenu kwa sababu ninyi mnapata wasaidizi katika kheri na wao hawatopata wa kuwasaidia.” (Al-Hakim).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakuna Nabii aliyetumwa na Allah kabla yangu isipokuwa katika umma wake kulikuwa na waambata na wafuasi wanaofuata mwenendo wake na wanaofuata amri yake, khalafu baada yao watakuja watu wanaosema wasio yafanya na wanafanya yasio amrisha basi ataye pigana nao kwa mkono wake, huyo ni muumini na atakaye pigana nao kwa ulimi wake huyo ni muumini na atakayepigana nao kwa moyo wake huyo ni muumini na wasio kuwa hao wamakundi matatu hawatakuwa na imani hata kiasi cha chembe ya khardali.” (Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu jihadi bora, akasema;

“Ni kusema haki mbele ya mtawala dhalimu.” (Ibnu Majah Nasaai na Ahmad).

b) Hoja za Kiakili:

1) Imethibitishwa kwa uzoefu na kwa kushuhudia kuwa ugonjwa kama utaachwa bila ya kutibiwa utaenea mwilini na utakuwa mgumu kutibiwa baada ya kujizatiti mwilini na kuwa sugu. Basi hivyo hivyo ovu kama litaachwa bila ya kuondolewa, si muda mrefu watu wataizowea na atalifanya mkubwa na mdogo wao. Na hapo si rahisi tena kuliondoa na hao ndipo watapostahiki adhabu ya Allah kwa waliyoyafanya. Adhabu ambayo lazima ije, kwa sababu hiyo ndiyo Sunna ya Allah (yaani kanuni yake),”

وَلَنْ يَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ تَحْوِيلًا ﴿٤٣﴾

“...Basi hutapata mabadiliko katika mtindo wa Mwenyezi Mungu...” (35: 43).

2) Imethibiti kwa kushuhudia kwa macho kuwa endapo nyumba itaachwa, bila ya kusafishwa na kuondolewa uchafu haitafaa kwa kuishi kama hali hiyoitaachwa iendelee. Kwani harufu yake itakuwa mbaya sana, na hewa yake itaingia sumu, na vimelea vitasambaa humo ndani kutokana na muda mrefu wa kurundikana uchafu huo. Hivyo hivyo kikundi cha waumini kama maovu kati yao yataachwa

bila ya kuondolea, na bila ya kuamrisha mema si muda mrefu watakuwa na roho mbaya na nafsi zenye kupenda maovu. Hawajui ni lipi zuri na baya hawalioni, na kwa ajili hiyo atakuwa hawafai kuishi, na hapo atawahilikisha Allah kwa namna na njia atakayo na adhabu ya Mola wako ni kali, na Allah ni Mshindi Mwenye Mateso.

3) Imefahamika kwa njia ya kuona kuwa nafsi ya binadamu inapozowea ovu kwa muda mrefu huwa zuri ovu hilo kwa nafsi hiyo, na nafsi hiyo inazoea shari na kuwa ndio tabia yake na hiyo ndiyo inaonyesha kuna haja ya kuwepo tabia ya kuamrisha mema na kukataza maovu. Pia wema kama utaachwa bila ya kuamriwa hautachukua muda watu watazowea kuacha wema na kuufanya wema huo kuonekana ni ovu. Na ovu ni hivyo hivyo kama hapakuharikishwa kuondolea hautachukua muda utasambaa, na kuzoelewa, na kuwa kwa wafanyaji si ovu tena bali hakuna zuri kama hilo. Na huko ndiko kupotoka kwa busara na kufilisika kiakili. Allah apishe mbali. Kwa ajili hii Allah na Mjumbe wake wakaamuru kuamrisha mema na kukataza maovu ni jambo la wajibu kwa Waumini ili kuendeleza usafi wao na kufaa kwao. Pia kuitunza heshima ya daraja lao kati ya Umma na Mataifa.

c) Adabu za Kuamrisha Mema na Kukataza Mabaya.

1) Muamrishaji awe na uhakika wa yale anayoyaamrisha kuwa ni mema kisheria na kuwa watu wameacha kuyafanya, kisha aelewe ukweli wa baya analo kataza na analo taka kuliondoa. Na iwe kisha limefanywa hasa kwa uhakika na kuwa ni miongoni mwa yanayo katazwa na sheria miongoni mwa maasi na mambo yaliyoharamishwa.

2) Awe mcha Mungu asije akalifanya lile analolikataza, na kuliacha analoamrisha na hiyo ni kutokana na kauli ya Allah:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٦١﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ

تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٦٢﴾

“Enyi mlio amini! Kwa nini mnasema msiyo yatenda? Yanachukiza vikubwa mno kwa Mwenyezi Mungu kuwa mnasema msiyo yatenda..” (61:2-3).

Na kauli Yake:

﴿ أَتَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴾

“Je! Mnawaamrisha watu mema na mnajisahau nafsi zenu, na hali nyinyi mnasoma Kitabu? Basi je, hamzingatii?” (2:44).

3) Awe na tabia nzuri mvumilivu anaamrisha kwa upole na anakataza kwa upole, asihamaki kwa baya linalomfika linalo sababishwa na kazi anayoifanya kwa aliyokataza na asikasirike anapofikwa na kero kutoka kwa anaowalingania, bali asubiri na kusamehe kwani Allah anasema:

﴿ يَبْنِيْ اِقْبِرِ الصَّلٰوةَ وَاْمُرْ بِالْمَعْرُوْفِ وَاَنْتَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَاَصْبِرْ عَلٰى مَا اَصَابَكَ ط

﴿ اِنَّ ذٰلِكَ مِنْ عَزْمِ الْاُمُوْرِ ﴾

“Ewe mwanangu! Shika Swala, na amrisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayo kupata. Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.” (31:17).

4) Asitumie ujasiri wa kujua siri za watu kama njia ya kuelewa maovu kwa sababu hatakiwi alielewe ovu kwa kumpekuwa mtu nyumbani mwake au kumfunua nguo ili aelewe ndani mna nini, au kutoa mfuniko ili ajue ndani mna nini. Kwani muweka sheria Allah ameamrisha watu kupendana na kusitiriana na amekataza kupekuana na kuwafanyia watu upekuzi. Amesema Allah:

﴿ وَلَا تَجَسَّسُوْا

“... Wala msipelelezane...” (49: 12).

Na amesema Mjumbe wa Allah:

“Wala msipelelezane” (Bukhari).

Na amesema Mtume ﷺ

“Ataye msitiri Muislamu Allah atamsitiri duniani na akhera.”
(Muslim).

5) Kabla ya kuanza kumuamrisha mtu kwa lile analotaka kumuamrisha anatakiwa amjulisha jema ni lipi. Kwa sababu kuacha kwake kulifanya yawezekana kuwa kumetokana na kutokulielewa kuwa hilo ni miongoni mwa mazuri kama atavyomjulisha anayetaka kumkataza ovu kuwa alilolifanya ni ovu, kwa sababu inawezekana kulifanya kwake kunatokana na kutolijua kuwa hilo ni ovu.

6) Aamrishe na akataze kwa wema na endapo aliyeacha kutenda mema hakubadilika na mtenda maovu hakuacha basi atampa mawaidha kwa maneno ya kuulanisha moyo wake. Kwa kumuelezea hoja zilizo kuja katika sheria zinazohusu kufanya au kuacha. Kama bado hayajatekelezwa atatumia maneno ya kulaumu na kukemea, yasipofaa basi ovu ataliondoa kwa mkono wake. Na kama atashindwa basi ataomba msaada Serikalini au kwa jamii inayomzunguka.

7) Kama atashindwa kuondoa ovu kwa mkono wake na ulimi wake (yaani kwa maneno) kwa kuhofia usalama wake au mali zake au heshima yake akawa hawezi kuvumilia kwa yanayomfika basi atatosheka kuondoa uovu huo kwa moyo wake kufuatia kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakayeliona ovu miongoni mwenu basi aliondoe kwa mkono wake na asipoweza...” Hadithi.



Mada ya Kumi na Saba

Kuamini Wajibu wa Kuwapenda Masahaba wa Mtume ﷺ na Ubora Wao.

Kuwaheshimu Viongozi wa Waislamu na Kuwatii Wanaoongoza Mambo ya Waislamu

Muislamu anaamini wajibu wa kuwapenda masahaba wa Mtume ﷺ na Aali zake, na kuamini ubora wao juu ya watu wengine katika Waumini, na kwamba masahaba wanazidiana ubora, na ukubwa wa daraja kulingana na kutangulia kwao katika Uislamu.

Wabora wao ni makhalifa ambao ni Abubakar, Umar, 'Uthman, na Ally رضي الله عنه wanafatia kwa ubora wale kumi waliyobashiriwa pepo, nao ni wale makhalifa kisha Twalha Ibnu Ubaidillahi, Zubair Ibnul Awwami, Sa'adi bnu Abil Waqqas, Said Ibnu Zubair, Abu Ubaidah Aamiri Ibnu Jarrah na Abdur-Rahmani Ibnu 'Aufi. Kisha maswahaba walioshiriki katika vita vya Badri, kisha wabashiriwa pepo ambao si katika wale kumi kama vile Fatima Zahra-a na Wanawe Hassan na Hussein, Thabit Ibnu Qaisi, Bilali Ibnu Rabah na wengineo. Kisha waliohudhuria mkataba wa Ridhwan nao walikuwa masahaba elfu moja na mia nne رضي الله عنه.

Muislamu anaamini uwajibu wa kuwaheshimu maimamu wa Kiislamu na kuwawekea adabu, na hao ndio viongozi wa dini na bendera za muongozo kama vile wasoma Qur'an, wataalamu wa fiqhi, wataalamu wa hadithi, na wafasiri miongoni mwa taabiina na walio wafuasi wa (Allah wote awarehemu).

Muislamu anaamini uwajibu wa kuwatii wanaotawala mambo ya Waislamu na kuwaheshimu na kushirikiana nao katika jihad na kuswali nyuma yao, na uharamu wa kuwa dhidi yao. Kwa hiyo Muislamu mbele ya hawa wote waliotajwa anakuwa na adabu maalumu kwao. Ama Maswahaba na Ahli Baiti na Mtume ﷺ Muislamu:

1) Anawapenda kwa vile Allah na Mtume wake ﷺ anawapenda, kwa sababu Allah ameelewa kuwa anawapenda na wanampenda. Kwa kauli Yake Allah aliposema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ
وَيُحِبُّونَهُمْ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ
وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ؕ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ ؕ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٥٤﴾

“Enyi mlio amini! Atakaye iacha miongoni mwenu Dini yake, basi Mwenyezi Mungu atakuja leta watu anao wapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri, wanapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anaye laumu. Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu na Mwenye kujua..” (5:54).

Na Mtume wa Allah ﷺ amesema:

“Allah Allah Maswahaba zangu msiwafanye shabaha baada yangu, atayewapenda basi amewapenda kwa penzi langu, na atayewachukia basi amewachukia kwa chuki yangu. Atayewaudhi hao ameniudhi mimi na atayeniudhi mimi amemuudhi Allah, na atakae muudhi Allah bila shaka ataingia motoni.” (At-Tirmidhi).

2) Muislamu anaukubali ubora wao juu ya Waumini wengine na Waislamu wengine kwa kauli yake Allah Aliyetukuka alipokuwa anawasifu:

وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ
رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ
خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ؕ ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٥٥﴾

“Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa..” (9:100).

Na amesema Mjumbe wa Allah ﷺ:

“Msiwatukane Maswahaba zangu kwani hakika mmoja wenu hata kama angalitoa dhahabu kama mlima wa Uhudi sadaka asingalifikia kibaba alichotoa mmoja wao.” (Abu Dawud).

3) Muislamu anatakiwa kuona kuwa Abu Bakari Swiddiqi ndiye mbora wa Maswahaba wa Mtume ﷺ na walio chini yao moja kwa moja. Wanaomfuatia katika ubora ni Umar, Uthman kisha Ally (Allah awawie radhi wote), na hao ni kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Kama ningalikuwa ninateua kutoka kwenye Umma wangu rafiki mpenzi basi Abubakari angekuwa ndiye rafiki yangu mpenzi lakini yeye ni ndugu yangu na swahaba wangu.” (Bukhari).

Na kauli yake Ibn Umar رضي الله عنه:

“Tulikuwa tunasema na Mtume ﷺ bado yupo hai: Abubakari kisha Umar, kisha Uthman, kisha Ally, Mtume ﷺ yakamfikia hayo tunayoyasema hakuyapinga.” (Abu Dawud)

Na kwa kauli yake Ally رضي الله عنه:

“Mbora wa umma huu baada ya Mtume wake ni Abubakari, Umar na kama ninalitaka ningalimtaja watatu – anakusudia Uthman. (Allah wote awawie radhi).”.

4) Azikubali sifa zao za pekee, na azitambue sifa zao nzuri kama vile sifa ya Abubakari, Umar na Uthmani. Katika kauli yake Mtume ﷺ kwa Mlima Uhud ulipotetemeka wakiwa juu yake:

Minhajil Muslim

“Tulia Uhud kwani si vingine juu yako kuna Mtume wa Allah, Swiddiqi, na mashahidi wawili.”

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa Ally:

“Kwani hauridhiki uwe kwangu katika nafasi ya Haruna kwa Mussa?”

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Fatuma ni bibi wa wanawake wa peponi.”

Na kwa kauli yake kwa Zubairi Ibnul -Awwam:

“Hakika kila Mtu ana wasaidizi na hakika ya wasaidizi wangu ni Zubairi Ibnul Awwam”.

Na dua yake kwa Hassan na Hussein:

“Ewe Allah wapende hao kwani mimi ninawapenda.”

Na kauli yake kwa Jafari Ibnu Abi Twalib رضي الله عنه:

“Umefanana na umbile langu Tabia zangu.” (Bukhari).

Kauli yake kwa Abdillahi Ibnu Umar:

“Hakika ya Abdallah ni mtu mwema.”

Kauli yake kwa Zaidi Ibnu Haritha:

“Wewe ni ndugu yetu na maula wetu” (Bukhari)

Kauli yake kwa Bilal Ibnu Rabaha:

“Nimeusikia mlio wa viatu vyako mbele yangu peponi.”

Na kauli yake kuhusu Salim maula Abi Hudhaifa, Abdillahi Ibnu Masud, Ubayyi Ibni Masuud, Ubayyu Ibni Ka’abi na Muadhi Ibnu Jabal:

“Watakeni watu wanne wakusomeeni Qur’an nao ni Abdiillah Ibni Masuud, Salim maula wa Abi Hudhaifa, Ubayyu Ibni Kaab na Muadhi Ibni Jabal.” (Bukhari).

Na kauli yake kuhusu Aisha **رضي الله عنها**:

“Ubora wa Aisha kwa wanawake wengine ni kama ulivyo ubora wa mkate kwa mchuzi na aina nyingine ya chakula.” (Bukhari).

Na kauli yake kuhusu Answari:

“Lau kama Answari atapita Jangwa fulani au njia ya Mlimani, Basi mimi nitapita watakapopita Answari, na kama isingekuwapo hijra basi mimi ningalikuwa miongoni mwa answari.” (Bukhari).

Na amesema:

“Hakuna atayewapenda answari isipokuwa atakuwa Muumini. Na hakuna ataye wachukia isipokuwa atakuwa ni mnafikiki, atakayewapenda Answari Allah atampenda na atakaye wachukia Answar Allah atamchukia.” (Bukhari).

Na kauli yake kuhusu Saad Ibni Muadhi:

“Arshi imetikisika kwa kufa Saad Ibni Muadhi.” (Bukhari)

*“Na kama sifa nzuri ni za Usaidi Ibni Hudhwairi alipokuwa ndani ya nyumba ya Mtume **ﷺ** pamoja na mmoja wa Maswahaba wa Mtume **ﷺ** ndani ya usiku wa kiza, walipotoka ghafla wakaikuta nuru mbele yao wakawa wanatembea katika nuru hiyo na alipoagana waliagana pamoja na nuru ile.” (Bukhari).*

Na kauli yake kwa Ubayyi Ibni Kaabi: Allah ameniamrisha nikusomee aya hii:

لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Hawakuwa walio kufuru.” (98:1).

Minhajil Muslim

Akasema: “na amenitaja? Akasema: ‘Ndio’, Ubayyu kalia.” (Ahmad).

Na kauli yake kuhusu Khalid Ibnil Walidi:

“Ni upanga miongoni mwa panga za Allah zilizochomolewa kwenye Ala yake.” (Bukhari).

Na kauli yake kuhusu Hasan:

“Mtoto wangu huyu ni Bwana, na Nataraji Allah atatia sahihi kati ya makundi mawili miongoni mwa Waislamu kupitia kwake.” (Bukhari).

Na kauli yake kuhusu Abu Ubaida,

“Kila umma una mtunza siri na mtunza siri wetu sisi Waislamu ni Abu ‘Ubaid Ibnil Jarrah, Allah awawie radhi hao wote.” (Bukhari).

5) Muislamu asiwe anayatajaja mabaya yao, na asizitajaje tofauti zilizo tokea kati yao, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Msiwatukane maswahaba zangu.”

Na kauli yake:

“Msiwafanye shabaha baada yangu.”

Na kauli yake:

“Atakayewakasirisha wao atakuwa amenikasirisha na atayenikasirisha mimi atakuwa amemkasirisha Allah na atakaye mkasirisha Allah atakuwa ameikaribia adhabu yake.”

6) Muislamu aikubali heshima ya wake zake Mtume ﷺ na kuwa wao wako safi wametakaswa, na awaombe radhi ya Allah pia aone kuwa mbora wa wote ni Khadija binti Khuwailid

النَّبِيُّ أَوْلَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنفُسِهِمْ وَأَزْوَاجُهُ أُمَّهَاتُهُمْ

“Nabii ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao. Na wake zake ni mama zenu.” (33: 6).

Ama Mamamu wa Waislamu miongoni mwa wasoma Quran, wataalamu wa hadithi na wataalamu wa fiqhi anatakiwa:-

1) Muislamu awapende na awaombee rehema kwa Allah na kuwaombea maghfira, na autambue ubora wao, kwa sababu wao wametajwa katika Qur’an:

وَالسَّابِقُونَ الْأَوْلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ
بِإِحْسَنِ رِضَى اللَّهِ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ

“Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye ...” (9:100).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Wabora wenu ni wale walio katika karne yangu kisha wale ambao wanao wafuatia” (Bukhari na Muslim).

Na sehemu kuwa ya wasoma Quran, hadithi, fiqhi na wataalamu wa tafsiri walikuwa katika kipindi hicho cha hizi Karne tatu ambazo Mtume ﷺ amethibitisha ubora wao na Allah Amewasifu wale wanaowaombea maghfira waliotangulia kwa imani katika kauli Yake:

رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ

“...Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani...” (59:10)

Kwa hiyo yeye anawaombea maghfira Waumini wanaume na wanawake.

2) Asiwataje ila kwa kheri, asiitoe kasoro rai au kauli yao ila kwa mazuri pia aelewe kuwa wao walikuwa wanajitahidi kwa moyo wao wote – kwa Ikhlaswi. Aione bora rai yao kuliko rai ya waliokuja baada yao, akitanguliza walichokikubali wao kuliko walio kuja baada yao miongoni mwa wanawazuoni na wataalamu wa fiqhi, tafsiri na hadithi, na asiache kuitumia kauli yao ila kwa kufuata kauli ya Allah au kauli ya Mtume wake au Maswahaba wa Mtume, (Allah wote awawie radhi).

3) Walichokiandika Maimamu wanne: Malik, Shaafii, Ahmad na Abu Hanifa, na maoni yao, na waliyoyasema miongoni mwa masuala ya Dini, fiqhi na sheria hayo yamechukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Allah na Sunna ya Mtume wake ﷺ na hawakuleta ya kwao ila ni walichokifahamu kutoka kwenye asili mbili hizi, au waliyoyanyambua kutoka humo, au yameashiriwa au kuonyeshwa katika vitabu hivyo viwili.

4) Muislamu aone kuwa inafaa kukichukuwa na kukitumia kilichoandikwa na mmoja wa hawa wanawazuoni wakubwa miongoni mwa Masuala ya Fiqhi na Dini. Kuwa kuyatumia ni kuitumia sheria ya Allah kwa muda wa kuwa halikuingiwa na tamko la wazi sahihi kutoka katika kitabu cha Allah au sunna ya Mtume wake ﷺ. Kwani haliachwi kufuatwa neno la Allah au la Mtume wake kwa neno la mmoja katika viumbe wake yeyote awe na hayo ni kufuatia kauli yake Allah:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْدِمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ

“Enyi mlio amini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu...” (49:1).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakayefanya tendo lisilokuwa miongoni mwa yale tuliyoyaamrisha basi aliolifanya halikubaliwi.” (Bukhari na Muslim).

Kauli yake Mtume ﷺ:

“Ninaapa kwa yule nafasi yangu iko Mikononi mwake hawi muumini wa kweli mmoja wenu mpaka pale yanapokuwa matakwa yake yanaenda kulingana na nilicho kuja nacho.” (Nawawi Hasan Swahili).

5) Muislamu aelewe kuwa wao Maimamu ni wanadamu wanaokosea, anaweza mmoja wao akakosea na kuacha sahihi katika masuala miongoni mwa masuala, si kwa kukusudia–hapana lakini kwa kughafilika au kusahau au kutolifahamu. Na kwa sababu hii hatakiwi Muislamu kuwa mbaguzi na mng’ang’anizi wa rai ya mmoja wao na kuibezwa rai ya mwengine, bali anaruhusiwa kuichukua rai ya yeyote miongoni mwao, na hawezi kuiacha kauli yao ila kama itapingana na kauli ya Allah (*Subhanahu wa Taala*) au kauli ya Mtume ﷺ.

6) Awakubalie udhuru katika masuala tanzu ya Dini waliyotofautiana, na aone kuwa tofauti zao hazikutokana na ujinga wao, wala kutetea rai zao. Bali ima aliye kwenda kinyume haikumfikia hadithi, au ameona kuwa hadithi hiyo imefutwa, au ameona inapingana na hadithi nyingine iliyomfikia na akaona hiyo ndio bora zaidi kuitumia au ameelewa katika hadithi hiyo asichokielewa mwenzake. Kwa sababu inawezekana kutofautiana ufahamu katika tamko moja, na kila moja, akalichukulia kulingana na alivyolifahamu yeye.

Mfano wa haya ni lile neno alilolifahamu Imam Shaafi, (*Allah Amrehemu*), kuhusu kubatilika udhu kwa kumshika tu mwanamke kutoka katika kauli yake Allah:

وَإِنْ كُنْتُمْ مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا
بِأَيْدِيكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِّنْهُ

“...Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni vumbi lilio safi, na mpake nyuso zenu na mikono yenu...” (5:6).

Imam Shaafii ameelewa kubatilika udhu, wakati Maimamu wengine hawakuelewa hivyo akasema: “*Utalazimika udhu kwa kumgusa mwanamke*” yaani kuingilia kimwili, kwa hiyo wao hawakuona wajibu wa udhu kwa kushikana kugusa tu, bali lazima kuwe na kiwango cha ziada kama vile kukusudia na kupatikana hisia za matamanio.

Anaweza akasema msemaji: kwa nini Imam Shaafii hakuiacha kauli yake ili aende sanjari na Maimam wengine, na akalikata shina la khilafu (tofauti) katika Umma? Jibu ni kwamba: Haijuzu - hairuhusiwi - kwake kuelewa kitu katika sheria kuelewa kusiko kuwa, kisha akaacha kwa kuogopa kufuata rai au ufahamu wa Imamu mwingine. Na akawa anafuata kauli ya watu na kuacha kauli ya Allah kufanya hivyo ni miongoni mwa madhambi makubwa mbele ya Allah. Kwa hiyo endapo uelewa wake unapingana na hoja ya wazi katika Qur’ani au sunna sahihi ingalazimika kufuata tamko hilo na kuacha alivyofahamu yeye kutoka katika hivyo hata isiyokuwa hoja bayana. Kwa sababu kama lingalikuwa wazi hata watu wa kawaida, wasingali tofautiana katika tamko hilo hali itakuwaje kwa Maimamu:?

Ama Viongozi wa Mambo ya Waislamu ni kwamba:

1) Muislamu aone wajibu wa kuwatii. Na hiyo ni kwa kauli Yake Allah:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ ط

“Enyi mlio amini! Mt’iini Mwenyezi Mungu, na mt’iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi....” (4:59).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Muwe wasikivu na watiifu kwa viongozi wenu hata kama amiri wenu atakuwa ni mtumwa kutoka Uhabeshi na hata kama ana kichwa kama zabibu”. (Bukhari).

Na kauli yake:

“Mwenye kunitii mimi amemtii Allah; na mwenye kuniasi mimi amemuasi Allah; na atakayemtii Amiri wangu atakuwa ameniasi mimi.” (Bukhari).

Lakini Muislamu asione wajibu wa kuwatii viongozi katika mambo ya kumuasi Allah, kwa sababu kumtii Allah kunatanguliza mbele kisha inafatia kuwatii wao kwa kauli yake:

وَلَا يَعْصِيَنَّكَ فِي مَعْرُوفٍ ٧

“...wala hawatakuasi katika jambo jema...” (60:12).

Na kwa sababu Mtume ﷺ amesema:

“Hakika si vingine kutii si wajibu ila katika jema tu.” (Bukhari, Muslim).

Na amesema pia Mtume ﷺ:

“Hakuna kumtii kiumbe katika amri ya kumuasi Muumba.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake:

“Hakuna utiifu katika kumuasi Allah: (Bukhari, Muslim).

Na amesema pia Mtume ﷺ:

“Yawajibika juu ya mtu Muislamu kutii amri iwe katika anachokipenda au katika anacho kichukia kwa muda wa kuwa haamrishiwi kufanya maasi, na kama ataamrishiwa kufanya maasi basi hakuna kusikia wala kutii.” (Bukhari, Abu Dawud, Timrmidhy, na Muslim).

2) Muislamu aone vibaya kuwa dhidi ya viongozi, au kutangaza uasi dhidi yao, kwa sababu kufanya hivyo ni kuigawa baraka ya umoja ya utiifu juu ya kiongozi wa Waislamu. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Anayechukia kitu kwa amri yake avumilie, kwa sababu atayekuwa dhidi ya kiongozi Shibri moja atakufa kifo cha kijahilia.” (Bukhari, Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kumdhalilisha kiongozi Allah atamdhalilisha.” (Hadith Hassan At-Tirmidhi).

Minhajil Muslim

3) Muislamu awaombe viongozi wake kwa Allah wawe viongozi wema wenye kuyafanya yaliyo sahihi na wenye kuwafikishwa kutenda haki na wenye kulindwa na shari na kutoingia katika makosa. Kwa sababu wema wa umma uko katika wema wao, na uharibifu wa umma uko katika kuharibika kwa viongozi wao, na awape nasaha bila ya kuwadhalilisha au kufanya dharau, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Dini ni kunasihiana. Tukauliza, “Kwanini?” Akasema: “Kwa Allah (kitabu chake), na kwa wajumbe wake, na kwa viongozi wa Waislamu na kwa watu wote.” (Muslim).

4) Muislamu apigane jihadi nyuma yao na aswali nyuma yao, hata kama wamekuwa mafasiki (waovu) au wamefanya yaliyo haramu ambayo hayawatoi katika Uislamu na kuwaingiza katika ukafiri, kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa aliye muuliza kuhusu kuwatii viongozi wabaya;

“Wasikilizeni ni watiini kwani si vingine wao watabeba majukumu yao, nanyi mtabeba majukumu yenu.” (Muslim).

Na kwa kauli yake Ubada ibni Swami رضي الله عنه:

“Tumemuahidi Mtume wa Allah kuwa wasikivu na kuwa watiifu tukiwa katika furaha au katika dhiki, tukiwa katika hali nzito au nyepesi, na tusigombane na viongozi kwa nia ya kuwatoa katika uongozi ila tu pale watakapoonekana wakifanya kwa wazi matendo ya kikafiri na kwenda kinyume na hoja za wazi zilizomo katika Qur’an na hadithi.” (Muslim).



Mlango wa Pili
Heshima na Adabu



Mada ya Kwanza

Adabu za nia

Muislamu anaamini ukubwa wa hatari ya nia, pia anaamini umuhimu wake kwa matendo yake mengine ya kidini na kidunia, kwa sababu matendo yote yanakwenda kulingana na nia. Kulingana na nia, matendo yanakuwa na nguvu au udhaifu, yanakuwa sahihi au yanaharibika. Imani hii ya Muislamu ya kuona ulazima wa nia kwa matendo yote, na ulazima wa kuisahihisha hiyo nia imechukuliwa kutoka kwenye neno la Allah:

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ .

“Na hawakuamrisha ila wamuabudiye Allah hali ya kumtakasia Dini.” (Al-Bayyina:5).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika kila matendo yatalipwa kulingana na nia na hakika kila mtu atalipwa alichonuwia.” (Bukhari, Abu Dawud, At-Tirmidhi na An-Nasai).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika Allah haangalii sura zenu wala mali zenu, bali anaangalia nyoyo zenu na matendo yenu.” (Muslim na Ahmad).

Kwa hiyo kuangalia nyoyo ni kuangalia nia. Kwa saabu nia ndicho kitu kinachomfanya mtu atende na kinachomsukuma kwenye kufanya jambo.

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kutia nia ya kufanya jema na akawa hakulifanya anaandikiwa jema moja.” (Ahmad).

Kwa hiyo kukusudia tu jema, hiyo ni sawa na kufanya jema na zitapatikana kwa hilo thawabu, na hayo yanatokana na nia nzuri.

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Watu wako aina nne, nao ni: Mtu ambaye Allah amempa elimu na mali kwa hiyo anatumia elimu yake katika kutoa haki ya mali yake: Na akatokea mtu akasema, ‘Allah kama angalinipa kama alichompa fulani nami ningalifanya kama anavyofanya, basi hao katika malipo wanalingana. Na mtu mwingine Allah amempa mali lakini hakumpa elimu, kwa hiyo anafanya ovyo ovyo katika mali yake, iwapo atatokea mtu akasema, Allah angalinipa mali kama alizompa yule nami ningalifanya kama anavyofanya basi hao katika malipo ya dhambi wanalingana.” (At-Tirmidhi)

Katika hadithi hii tumeona kuwa mwenye nia nzuri amelipwa malipo mazuri sawa na aliyetenda tendo jema, na malipo ya dhambi kwa nia mbaya kama malipo ya mwenye tendo baya na yote hayo yanarudi kwenye nia tu.

Na kauli yake Mtume ﷺ akiwa Tabuk:

“Madina kuna watu hatukuvuka bonde na wala hatukukanyaga mahala, panapo wakasirisha makafiri, na wala hatukutoa gharama za matumizi, na wala haikutupata njaa isipokuwa watu hao wameshirikiana nasi, nao wakiwa wako Madina. ‘Akaulizwa, ‘Vipi itakuwa hivyo Ewe Mtume wa Allah?’ Akasema, ‘Udhuru umewazuwia, kwa hiyo wameshiriki kwa nia zao nzuri.” (Abu-Daud, Bukhari).

Kwa hiyo nia nzuri ndio iliyofanya asiye shiriki katika mapigano apate malipo kama mpiganaji na asiyekuwa katika jihadi apate malipo ya Mujaahid.

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Wanapokutana Waislamu wawili wakauwana kwa panga zao basi muuaji na muuliwa wataingia motoni” pa kaulizwa: “Ewe Mtume

Minhajil Muslim

wa Allah ni sawa huyu amewa, lakini huyu aliyeliwa naye jee?” Akasema: “Kwa sababu yeye alitaka kumuua mwenzake.”
(Bukhari, Muslim).

Umeona nia mbaya imewaweka pamoja muuwaji na muuliwaji kwani kuua kunawajibisha moto, na muuliwa ambaye kama si nia yake mbaya angalikuwa mtu wa peponi lakini kutokana na ubaya wa nia yake naye amehukumiwa kwenda motoni.

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kuoa kwa mahari ya deni ambayo hana nia ya kuyalipa huyo ni mzinifu, na mwenye kukopa akiwa hana nia ya kulipa huyo ni mwizi.” (Ahmad, Ibnu Majah)

Yote haya yanasisitiza imani ya Muislamu kuhusu hatari ya nia na uzito wa jambo lake, na uzito wa umuhimu wake. Kwa sababu hiyo Muislamu matendo yake mengine anayajenga juu ya nia nzuri kama anavyotoa juhudi zake zote asifanye tendo bila ya nia au kwa nia isiyokuwa njema, kwa sababu nia ndio roho ya tendo, usahihi wa nia ndio usahihi wa tendo kwa Muislamu na uharibifu wa nia ndio uharibifu wa tendo, na tendo bila ya nia maana yake ni kuwa mtendaji anafanya tendo hilo kwa ria na kwa kujikalifisha tendo ambalo limelaaniwa.

Kama Muislamu anavyoamini kuwa nia ni nguzo ya matendo yote na sharti lake, kwa hakika Muislamu haoni kuwa nia si kutamka tu kwa ulimi, “Ewe Mola wangu nimenuwia kitu kadha” na kuwa ni mazungumzo ya nafsi tu, bali nia kwake ni kusafiri kwa moyo kuelekea kwenye tendo linaloafiki lengo sahihi, yaani kuleta maslahi au kuondoa madhara kwa wakati wa sasa au baadaye. Pia kwake ni utashi unaoelekea upande wa tendo kwa ajili ya kupata radi au kutekeleza amri yake Allah.

Muislamu anaamini kuwa tendo la halali kwa nia nzuri linabadilika na kuwa ni ibada yenye malipo na thawabu. Na kuwa ibada kama haina nia nzuri inabadilika na kuwa maasi yenye madhambi, na adhabu. Wakati huo huo haamini kuwa nia zuri inaathiri kitu katika maasi na kuyafanya yawe ibada. Kwa hiyo anaye msengenya mtu ili kumfurahisha mwengine huyo anamuasi Allah. Kamwe haitamfaa nia yake nzuri kama anavyofikiria. Anayejenga msikiti kwa mali ya haramu hapati

thawabu kwa kazi hiyo na anayefika katika sherehe za muziki na kukaa uchi, au anakata tiketi za bahati nasibu, kwa nia ya kuleta changamoto katika miradi ya kheri, au kwa faida ya jihadi na mfano wake huyo anamuasi Allah, anapata dhambi wala hapati thawabu. Yule anayejenga mabanda juu ya makaburi ya watu wema au anawachinjia au kuwawekea nadhiri kwa nia ya kuwapenda watu wema, huyo anamuasi Allah, anapata dhambi kwa tendo lake hilo. Hata kama nia yake ni nzuri kama anavyoiona. Kwa sababu nia nzuri haibadilishi jambo baya na kulifanya kuwa ibada isipokuwa kwa kilichokuwa halali kilichoruhusiwa kufanywa tu. Ama kilichokatazwa hakibadiliki kuwa ibada kwa hali yoyote ile iwayo.



Mada ya Pili

Kuwa Adabu na Allah

Muislamu anaona kuwa neema za Allah ambazo ni nyingi bila ya idadi, ziko pamoja naye tokea pale alipokuwa tone la maji ya mbegu ndani ya mfuko wa kizazi wa mama yake, na zitaendelea kuwa naye mpaka anakutana na Mola wake kwa sababu hiyo anatakiwa amshukuru Allah juu ya neema hizo kwa ulimi wake na kumsifu kwa sifa zinazolingana naye, na kwa viungo vyake kwa kuvidhalilisha katika kumtii Allah. Tendo hili kwa Muislamu ni adabu na Allah, kwani kupinga neema si adabu, pia si adabu kukataa fadhila za muhisani wako. Allah anasema,

وَمَا بِكُمْ مِّنْ نِّعْمَةٍ فَمِنَ اللَّهِ

“Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu...” (16:53).

Na Allah anasema:

وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَةَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا

“Na mkizihisabu neema za Mwenyezi Mungu, hamwezi kuzidhibiti...” (16: 18).

Kauli yake,

فَاذْكُرُونِي أَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوا لِي وَلَا تَكْفُرُونِ

“Basi nikumbukeni nitakukumbukeni, na nishukuruni wala msinikufuru.” (2:152)

Muislamu anaamini kuwa Allah anamjua na anamuona katika hali zake zote na kwa kuamini hilo moyo wa Muislamu unajaa woga kwa Allah hofu na heshima. Kwa hiyo anaona aibu kumuasi, na anastahi kumkhalifu Mola wake na kutoka

nje ya kumtii na hii kwa Muislamu ni adabu na Allah. Kwani si adabu Mteme wa kumuasi Bwana wake mbele yake, au kumfanyia mabaya na machafu huku anamuona na kumuangalia. Allah amesema:

مَا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿١٣﴾ وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿١٤﴾

“Mna nini hamweki heshima ya Mwenyezi Mungu? Na hali Yeye kakuumbeni daraja baada ya daraja?” (71:13-14)

Na Amesema:

وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُسْرُوبُونَ ﴿١٩﴾ وَمَا تُعْلِنُونَ ﴿٢٠﴾

“Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yaficha na mnayo yatangaza.” (16:19).

Na Allah amesema

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْءَانٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ
إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ
مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا
أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦١﴾

“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi..” (10: 61).

Muislamu anaamini kwa Allah anauwezo juu yake na yuko ndani ya Uwezo wa Allah na kuwa hawezi kumkimbia wala kuponyoka, wala hakuna pa kukimbilia isipokuwa Kwake, akimbilie Kwake, na ajitupe mbele yake, na amtegemee yeye tu. Hali hii kwa Muislamu ni adabu na Mola wake na Muumba wake.

Kwa sababu si adabu kumkimbia asiyekimbilika, wala kumtegemea asiyekuwa na uwezo, Amesema Allah,

إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا
إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾

“...Hapana kiumbe yeyote ila Yeye anamwendesha atakavyo. Hakika Mola wangu Mlezi yuko juu ya Njia Iliyo Nyooka..” (11: 56).

Na Allah Amesema:

كَذَلِكَ مَا أَتَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مُجْنُونٌ ﴿٥٠﴾

“Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae kwake.” (51:50).

Na amesema:

وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٣﴾

“...Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini.” (5:23).

Muislamu anaamini upole wa Allah katika mambo yake yote na huruma ya Allah kwake na viumbe wake wengine ana matumaini ya kupata nyongeza zaidi ya hayo kwani ananyenyekea kwa Allah na kumuomba na kujikurubisha kwake kwa kauli yake nzuri na vitendo vizuri. Hilo kwa Muislamu ni kufanya adabu na

Mola wake kwa vile si adabu kukata tamaa ya kupata rehema zaidi kutoka kwa Allah wala kukata tamaa ya hisani yake iliyowaenea viumbe wote na upole wake uliyo nadhimu ulimwengu.

Amesema Allah:

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ

“...Na rehema yangu imeenea kila kitu...” (7:156).

Na amesema:

اللَّهُ لَطِيفٌ بِعِبَادِهِ

“...Allah ni Mpole kwa waja wake...” (42:19).

Na amesema,

لَا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ

“...Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu...” (39:53).

Muislamu anaamini ukali wa adhabu ya Allah, na anaamini nguvu za adhabu zake, na uharaka wa kuhesabu kwake, kwa hiyo anajilinda na hayo kwa kumtii, na anajikinga nayo kwa kutomuasi na hii kwa Muislamu ni adabu na Allah. Kwa sababu kwa wenye akili si adabu kwa mja ambaye ni mnyonge asiye na uwezo, kufanya maasi na dhulma, Bwana Mwenye Nguvu na Muweza.

Anasema Allah,

وَإِذَا أَرَادَ اللَّهُ بِقَوْمٍ سُوءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُ وَمَا لَهُمْ مِنْ دُونِهِ مِنْ وَالٍ ﴿١١﴾

“...Na Mwenyezi Mungu anapo watakia watu adhabu hakuna cha kuzuia wala hawana mlinzi yeyote badala yake...” (13: 11.)

Na Allah anasema,

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١١﴾

“Hakika kutesa kwa Mola wako Mlezi ni kukali..” (85:12)

Na anasema tena:

وَاللَّهُ عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ ﴿٤﴾

“...Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kulipa.” (3:4).

Muislamu anapomuasi Allah na akaacha kumtii anaona kama vile adhabu ya Allah imekwisha mteremkia, na mateso yake yamemfikia, na anapomtii na kufuata sheria yake anaona kama vile ahadi ya Allah kuwa imekamilika, na joho la ridhaa yake Allah Amemvisha na hiyo kwa mja ni dhana nzuri kwa Allah, na miongoni mwa adabu na Allah ni kuwa na dhana nzuri kwake. Kwa sababu si adabu kwa mtu kuwa adhana mbaya kwa Allah akamuasi na kutoka katika utiifu wake akidhania kuwa Allah hamuoni, na hana adhabu kwa kosa alifanyalo.

Naye Anasema:

وَلَكِنْ ظَنَنْتُمْ أَنَّ اللَّهَ لَا يَعْلَمُ كَثِيرًا مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٢٢﴾ وَذَلِكُمْ ظَنُّكُمُ
الَّذِي ظَنَنْتُمْ بِرَبِّكُمْ أَرْدَاكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٢٣﴾

“Lakini mlidhani kwamba Mwenyezi Mungu hayajui mengi katika mliyo kuwa mkiyatenda. Basi hiyo dhana yenu mliyo kuwa mkimdhania Mola wenu Mlezi. Imekuangamizeni; na mmekuwa miongoni mwa walio khasiri. (41: 22-23)

Pia si adabu na Allah mtu akawa anamcha na kumtii Allah halafu akadhania hamlipi kwa matendo yake hayo mazuri, na kwamba hamkubalii ibada yake na utiifu wake na Allah Anasema:

﴿٥٢﴾ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَخَشِيَ اللَّهَ وَيَتَّقِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ

“Na wenye kumt’ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamwogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu.” (24: 52).

Na Allah anasema:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أَنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهٗ حَيٰوةً طَيِّبَةً
وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾

“Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.” (16:97).

Na Amesema:

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ مِثَالِهَا وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ
إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦٠﴾

“Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi. na afanyae ubaya hatalipwa ila sawa nao tu. Na wao hawatadhulumiwa.” (6:160).

Kwa ufupi Adabu ya mja Muislamu na Mola wake iko katika kumshukuru Mola wake kwa kumneemesha, kuona haya anaposhawishika kumuasi, kumtegemea na kutarajia Rehema zake, na kiogopa adhabu yake. Kuwa na dhana nzuri kwa Mola wake katika kutekeleza hadi zake, na kutimiza ahadi yake ya adhabu kwa amtakaye miongoni mwa waja wake, na kwa kadiri atavyoshikamana nao mwenendo huo na kudumu nao ndivyo itavyopanda daraja yake, na kuwa juu cheo chake, na kuwa kubwa karama zake na atakuwa miongoni mwa mawalii wa Allah na kituo cha rehema zake, na nyumba ya neema zake na huu ndio upeo wa anayoyatafuta Muislamu na katika maisha yake yote anayatamani hayo,

“Ewe Mola wetu tupe uwalii wako, na usitunyime matunzo yako, na utuweke karibu nawe mbele yako, Ewe Allah Ewe Bwana wa viumbe wote.”



Mada ya Tatu

Kuyaheshimu Maneno ya Allah

Muislamu anaamini kuwa maneno ya Allah (Qur'ani) ni Matakatifu, Mtukufu na bora kuliko maneno mengine yoyote. Muislamu anaamini kuwa Qur'ani ni maneno ya Allah ambayo hayafikiwi na batili mbele yake na nyuma yake. Atakayesema kwa kutumia "Qur'an" atakuwa mkweli, na atayehukumu kwa Qur'ani atakuwa mwadilifu, na kwamba watu wa Qur'an ni watu wa Allah, muhtasi wake; na wenye kushikamana nayo wameokoka, wamefaulu na wenye kuipuuza wamehiliki na wamepata hasara.

Kinachoongeza imani ya Muislamu ni utukufu wa Kitabu cha Allah, utakatifu wake na hadhi yake na yale yaliyopokewa toka kwa Mtume yanayohusu ubora wa Qur'an. Qur'an ambayo imeteremshwa kwa mtu bora, kwani aliyeletewa wahyi huo ni kiumbe mteule, Bwana wetu Muhammad, mwana wa Abdallah, Mtume wa Allah ﷺ, kama alivyosema:

"Isomeni Qur'ani hakika itakuja Siku ya Kiyama kumuombea aliyeisoma." (Muslim).

Na kauli yake:

"Mbora wenu ni yule aliyejifunza Qur'ani na akaifundisha." (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

"Watu wa Qur-ani ni watu wa Allah na mukhtasi wake." (Ahmad).

Na kauli yake:

"Nyoyo zinapatwa na kutu kama kinavyopata kutu chuma."

Akaulizwa:

*"Ewe Mtume wa Allah nini kisugulio chake kutu hiyo?"
Akasema: Kusoma Qur'ni na kukumbuka kufa kila wakati"*
(Baihaqi).

Alikuwa kwa Mtume ﷺ siku moja adui yake mkubwa huku anasema: “Ewe Muhammad nisomee Qur’an.” Mtume ﷺ akamsomea:

• إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَايَ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ
الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ ۗ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩٠﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka..” (16:90).

Kabla hajamaliza Mtume ﷺ kuisoma Aya hiyo, yule adui akamtaka arudie tena akiwa amevutiwa na ubora wa matamko yake, na utakatifu wa maana yake, na kuchukuliwa na uwazi wake, na kuvutwa kwa nguvu ya kuathiri kwake. Kipaji chake kikubwa kikamuinua kwenda kusajili kuitambua Qur’ani na kuuthibitisha utakatifu wa maneno ya Allah na Utukufu Wake, pale aliposema: Wallahi haya maneno yana utamu, na juu yake kuna uzuri, na chini yake yana utajiri na juu yake kuna matunda, na haya hayasemwi na mwanadamu.” (Ibnu Jariri Twabari).

Kwa sababu hiyo Muislamu pamoja na kuhalalisha halali na kuharamisha haramu, hushikamana na adabu zake na, kufuata tabia zake, pamoja na hayo Muislamu anaposoma Qur’an anachunga adabu zifuatazo:-

1) **Kuisoma akiwa katika hali ya ukamilifu zaidi** kama vile: Kuwa twahara, kuelekea Qibla na kukaa kwa adabu na unyenyekevu.

2) **Kuisoma taratibu bila ya haraka**, asiisome Qur’ani yote chini ya muda wa siku tatu, kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Atakayeisoma Qur’ani chini ya muda wa siku tatu havezi kuifahamu.” (As-habu Sunan).

Mtume ﷺ alimuamrisha Abdallah Ibn Umar رضي الله عنه aimalize kuisoma Qur’an yote ndani ya kila siku saba. Kama alivyokuwa Abdallah Ibn Masoud, Uthmani Ibn

Affaan na Zaidi Ibni Thabiti (Allah Awawie radhi) wanaikamilisha kila wiki mara moja.

3) **Wakati wa kuisoma awe mnyenyekevu**, aoneshe huzuni, na atoe machozi na kama hawezi basi aonyeshe kulia kufuatia kauli yake Mtume ﷺ:

“Isomeni Qur’ani na lieni, na msipolia jilizeni.” (Ibn Majah).

4) **Airembeshe sauti yake anaposoma Qur’ani**, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

”Ipambeni Qur’ani kwa sauti zenu.” (Ahmad, Ibn Majah, An-Nasai na Al-Hakim).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Si miongoni mwetu asiyeghani kwa Qur’an.” (Bukhari, Abu Dawud na Ahmad).

Na kwa kauli yake,

“Allah hakuruhusu kitu kama alivyomruhusu Mtume ﷺ kughani anapoisoma Qurani.” (Bukhari, Muslim na Ahmad).

5) **Kama anajihofia ria asiisome Qur’ani** kwa sauti au kama atakhofia kumshawishi anayeswali, kufuatia khabari iliyokuja kutoka kwa Mtume ﷺ:

“Anayesoma kwa sauti Qur’ani ni sawa na anayetangaza sadaka.”

Inafahamika kuwa ni sunna sadaka kutolewa kwa siri isipokuwa kama katika kuitangaza kuna faida inayokusudiwa, kama vile kuwashawishi watu wafanye kama hivyo, basi na kusoma Qur’anini vivyo hivyo.

6) **Aisome Qur’ani kwa kuizingatia na kuitafakari**, pamoja na kuiheshimu, na kuhudhurisha moyo na akili, na kuelewa maana yake na siri yake.

7) **Anapoisoma Qur’ani na akawa hana habari** nayo kufanya hivyo kunaweza kukasababisha kujilaani mwenyewe, kwa sababu kama atasoma:

لَعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦١﴾

“...*laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo..*” (3:61)

Au

أَلَا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٨﴾

“...*Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate walio dhulumu.*”
(11:18)

Na kwa yeye ni mrongo au dhalimu atakuwa amejilaani mwenyewe.

Na mapokezi yajayo yanabaini kiwango cha kosa la wenye kulipa mgongo Qur’ani wasio na habari nayo wanashughulika na kingine. Imepokewa kuwa imekuja katika Taurati Allah Anasema:

“Huoni haya yakujia barua kutoka kwa baadhi ya ndugu zako ukiwa njiani unatembea, unaenda pembezoni mwa njia na unakaa kwa ajili ya barua hiyo na unaisoma na unaizingatia kila herufi hakuna unachokiacha, na hiki kitabu changu nimekuteremshia, angalia vipi nimekufafanulia neno, na mara ngapi nimerudia rudia humo ili uzingatie kwa urefu wake na upana wake, halafu wewe unakipuza nimekuwa duni mno kwako kuliko baadhi ya ndugu zako”

“Ewe mja wangu wanakaa mbele yako baadhi ya ndugu zako unawaelekea kwa uso wako wote na unayasikiliza maelezo yake kwa moyo wako wote, kama atazungumza mzungumzaji au akakushughulisha utamuashiria nyamaza na hapa Mimi Ninakuelekea na kuzungumza nawe wanipuza kwa moyo wako wote, hivi Mimi umenifanya duni mno kuliko baadhi ya ndugu zako?”

8) Ajitahidi kuwa na sifa za wana Qur’ani ambao ni watu wa Allah na mukhtasari wake, na ajipe alama zao kama alivyosema Abdullahi Ibn Masuud رضي الله عنه anatakiwa msoma Qur’ani aeleweke kwa usiku wake wakati watu wamelala, na mchana wake wakati watu wanakula, na kwa kilio chake wakati watu wanacheka, na kwa hofu yake wakati watu wanafanya maringo, na kwa ukimya wake wakati watu wanasema ovyo, na kwa unyenyekevu wake wakati watu wanakibri, na

kwa huzuni yake wakati watu wana furahi. Amesema Muhammad Ibni Kaabi tulikuwa tunamjua msoma Qur'an kwa unjano wa rangi yake unaoashiria kukesha kwake na urefu wa Ibada zake za usiku. Na amesema Wahibu Ibn Wardi, Aliulizwa mtu fulani. 'Kwanini hulali? Akajibu: "Maajabu ya Qur'an yameufukuza usingizi wangu."

Na Dhu Nnuni ameimba:

Qur'an kwa ahadi na kemeo zake,
Zimezuwia usingizi, kucha jicho halilali,
Wameelewa kutoka kwa Mfalme Mtukufu Maneno Yake
Ufahamu unaozifanya nyoyo zidhalilike na kunyenyekea.



Mada ya Nne

Kuwa na Adabu na Mtume ﷺ

Muislamu ndani ya nafsi yake anahisi wajibu kamili wa kuwa na adabu kwa Mtume ﷺ kwa sababu zifuatazo:-

1) Allah Amemlazimisha kila Muislamu kumfanyia adabu na heshima Mtume ﷺ kwa tamko Lake la wazi pale Aliposema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْدِمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ط

“Enyi mlio amini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake...” (49:1).

Na Allah amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ
بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٢﴾

“Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyo semezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui.” (49:2).

Allah Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ

لِلتَّقْوَى ۗ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٣﴾

“Kwa hakika wanao teremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa uchamngu. Hao watakuwa na maghfira na ujira mkubwa.” (49:3).

Na Allah amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِنْ وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّى تَخْرُجَ إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٤٥﴾

“Hakika hao wanao kuita nawe uko nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili. Na lau wao wangeli ngojea mpaka uwatokee ingeli kuwa kheri kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira, Mwenye kurehemu.” (49: 4-5).

Na Allah amesema kuhusu utukufu wake:

لَا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا

“Msifanye wito wa Mtume ﷺ baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi...” (24:63)

Na amesema pia:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَإِذَا كَانُوا مَعَهُ عَلَىٰ أَمْرٍ جَامِعٍ لَمْ يَذْهَبُوا حَتَّىٰ يَسْتَأْذِنُوهُ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَأْذِنُونَكَ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ

“Hakika Waumini wa kweli ni walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na wanapo kuwa pamoja naye kwa jambo la kuwakuhusu wote hawaondoki mpaka wamtake ruhusa. Kwa hakika wale wanao kuomba ruhusa, hao ndio wanao muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake...” (24:62).

Na Allah amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَعِذُّونَكَ أَوْلِيَّكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ
فَإِذَا اسْتَعِذُّوكَ لِبَعْضِ شَأْنِهِمْ فَأَذَنَ لِمَن شِئْتَ مِنْهُمْ

“...Kwa hakika wale wanao kuomba ruhusa, hao ndio wanao muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na wakikuomba ruhusa kwa baadhi ya kazi zao, mruhusu umtakaye miongoni mwao...” (24:62).

Na Allah Amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نَجَّيْتُمُ الرُّسُولَ فَقَدِمُوا بَيْنَ يَدَيْ جَوْنِكُمْ صَدَقَةٌ
ذَلِكَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَأَطْهَرُ فَإِن لَّمْ تَجِدُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Enyi mlio amini! Mnapo sema siri na Mtume, basi tangulizeni sadaka kabla ya kusemezana kwenu. Hiyo ni kheri kwenu na usafi zaidi. Na ikiwa hamkupata cha kutoa, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu...” (58: 12).

2) Hakika ya Allah Amelazimisha juu ya waumini kumtii, na amewajibisha kumpenda akasema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرُّسُولَ وَلَا تَبْطُلُوا أَعْمَلَكُمْ

“Enyi mlio amini! Mt’iini Mwenyezi Mungu, na mt’iini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu..” (47:33).

Na amesema:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَنْ تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“...Basi nawatahadhari wanao khalifu amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu.” (24:63)

Na amesema Aliyetakasika,

وَمَا آتَاكُمْ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا

“...Na anacho kupeni Mtume ﷺ chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho..” (59:7)

Na Amesema tena:

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ

“...Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu...” (3:31).

Mtume ﷺ ambaye kumewajibika kumtii kwake, na kukaharamika kumuasi kwake ni lazima kufanya naye adabu katika hali zote.

3) Allah amempa madaraka akamfanya kiongozi na hakimu. Allah Amesema:

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِتَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ بِمَا أَرَاكَ اللَّهُ وَلَا تَكُنْ

لِلْخَائِبِينَ خَصِيمًا ﴿١٠٥﴾

“Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa haki ili upate kuhukumu baina ya watu kwa alivyo kuonyesha Mwenyezi Mungu. Wala usiwe mtetezi wa makhaaini..” (4:105).

Na amesema:

وَأَنْ أَحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ

“Na wahukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamano yao...” (5:49).

Na Amesema,

فَلَا وَرَيْكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي

أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٤٥﴾

“La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenykee kabisa.” (4:65).

Allah amesema,

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ

وَدَذَرَ اللَّهَ كَثِيرًا ﴿٣٣﴾

“Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.” (33:21).

Na kuwa na adabu na kiongozi na mtawala kunalazimishwa na sheria na kunakubaliwa na akili na mantiki salama ina hukumu hivyo.

4) Allah Amewajibisha kumpenda kwa kupitia ulimi wake Mtume ﷺ

“Naapa kwa ambaye nafsi yangu ipo mkononi mwako, hawi Muumini mmoja wenu mpaka niwe mpendwa mno kwake kuliko mtoto wake na baba yake na watu wote.” (Bukhari na An-Nasai).

Na unayewajibika kumpenda ni wajibu kumfanyia adabu, na lazima kuwa na heshima naye.

5) Uzuri wa umbile lake Mtume na tabia zake za pekee alizozawadiwa na Allah, na kile alichopewa na Allah cha ukamilifu wa nafsi na dhati, amekuwa mzuri wa viumbe na mkamilifu wao. Bila ya kipingamizi mtu mwenye hali kama hii vipi iwe

si wajibu kumfanyia adabu. Hivyo (tulivyo vitaja) ni sehemu tu ya inavyowajibisha heshima kwa Mtume ﷺ na kuna vingine vingi, lakini je adabu inakuwaje? Na inakuwa kwa kitu gani? Hili ndilo jambo linalotakiwa kueleweka.

Kumfanyia adabu Mtume ﷺ itakuwa kwa yafuatayo:-

- 1) **Kwa kumtii** na kufuata, nyayo zake, na kuzizingatia hatua zake katika njia zote za dunia na Dini.
- 2) **Lisitangulizwe** juu ya penzi lake, hadhi yake na taadhima yake penzi la kiumbe mwingine yoyote awaye.
- 3) **Kumpenda** aliyekuwa anampenda Mtume na kumchukia aliyekuwa anamchukia na kuridhika na alichokuwa anakiridhia, na kukasirika kwa alichokuwa anakikasirikia.
- 4) **Kuliheshimu** jina lake linapotajwa na kumswalia na kumtukiza na kuziheshimu sifa zake.
- 5) **Kumkubalia** kwa yote aliyoyaeleza yanayohusu Dini na dunia, na mambo ya ghaibu yanayohusu maisha ya dunia na akhera.
- 6) **Kuihuisha** Sunnah na mwenendo wake na kuidhihirisha sheria yake, na kuitangaza da'awa yake, na kuyatekeleza maagizo yake.
- 7) **Kuteremsha** sauti Kaburini kwake na msikitini kwake kwa yule ambaye Allah aliyemkirimu kumzuru na kupata heshima ya kusimama mbele ya Kaburi lake ﷺ na juu ya jamaa zake, na swahaba zake, na ampe amani nyingi mno.
- 8) **Kuwapenda** watu wema kwa vile Mtume amewapenda, na kuwachukia mafasiki kwa vile yeye amewachukia. Hizi ndio sehemu za adabu na heshima kwa Mtume ﷺ zinavyotakiwa ziwe. Muislamu siku zote anajitahidi kuyatekeleza hayo kwa ukamilifu na kudumu nayo kikamilifu kwa sababu ukamilifu wake upo katika kuyaeleza hayo na maisha yake bora yameunganishwa juu ya hayo na wa kuombwa ni Allah atuwafikishe kumuwekea adabu Mtume wetu ﷺ na watufanye kuwa katika wafuasi wake na watetezi wake na kundi lake, pia atupe utiifu kwake na asitunyime shufaa yake. Ewe Mola Wetu. Amin.

Mada ya Tano

Adabu na Nafsi

Muislamu anaamini kuwa ubora wa maisha yake katika dunia na akhera, yanakuwa mazuri kulingana na kiasi gani anavyoiheshimu nafsi yake hiyo na kulingana na kiasi gani ameitekeleza adabu na kuifanya iwe nzuri na kuitakasa. Kama ilivyo pia maisha yake mabaya yanatokana na uharibifu na uchafu wa nafsi yake, kwa hoja zifuatazo. Kauli Yake Allah:

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّاهَا ﴿٩١﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿٩٢﴾

“Hakika amefanikiwa aliye itakasa, Na hakika amekhasiri aliye iviza.” (91: 9-10).

Na Kauli Yake,

إِنَّ الَّذِينَ كَذَبُوا بِعَايَتِنَا وَاسْتَكْبَرُوا عَنْهَا لَا تُفَتِّحُ لَهُمْ أَبْوَابُ السَّمَاءِ
وَلَا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ حَتَّى يَلِجَ الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْخِيَاطِ ۗ وَكَذَلِكَ
نَجْزِي الْمُجْرِمِينَ ﴿٩١﴾ هُمْ مِّنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَمِن فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ ۗ
وَكَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٩٢﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَا
نُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٩٣﴾

“Hakika wale wanao zikanusha Ishara zetu na wakazifanyia kiburi hawatafunguliwa milango ya mbingu, wala hawataingia Peponi mpaka apite ngamia katika tundu ya sindano. Na hivi ndivyo tunavyo walipa wakosefu. Jahannamu itakuwa kitanda chao na juu yao nguo za moto za kujifunika. Na hivi ndivyo tunavyo walipa madhaalimu. Na wale wanao amini na wakatenda mema - hatumkalifishi mtu yoyote ila kwa kiasi cha uwezo wake - hao ndio watu wa Peponi. Wao wataidumu humo.” (7:40-42).

Na Kauli Yake:

وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُفٍ ﴿٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ﴿٣﴾

“Naapa kwa Zama! Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara, Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausia kwa haki, na wakausia kusubiri.” (103:1-3)

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Nyote mtaingia peponi isipokuwa atakayekataa”, Wakasema, “Ewe Mjumbe wa Allah nani atakayekataa?” Akasema, “Atakayenitii ataingia peponi na atakayeniasi atakuwa amekataa.” (Muslim).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Watu wote wanatoka mapema kuna anayeiuzua nafsi yake na kuiacha huru au kuihilikisha.” (Muslim).

Muislamu anaamini kuwa kinachoitoharisha nafsi na kuitakasa ni imani nzuri na matendo mema, na kinachoichafua na kuiharibu ni ovu la ukafiri na maasi. Amesema Allah,

وَأَقْبِرَ الصَّلَاةَ طَرَفِي النَّهَارِ وَزُلْفًا مِّنَ اللَّيْلِ

“Na shika Swala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana...” (11:114).

Na Amesema:

كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾

“Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hao walio kuwa wakiyachuma.” (83:14)

Na amesema Mtume wa Allah,

“Hakika Muumini anapofanya kosa huweka doa jeusi kwenye moyo wake, na kama atatubu kwa Allah na kuacha dhambi na akaomba radhi utasafika moyo wake. Na ama ataongeza maovu moyo wake wote utaenea madoa.” (Muslim)

Basi hiyo ndiyo kutu Alivyosema Allah,

كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾

“Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hao walio kuwa wakiyachuma” (83:14)

Mtume ﷺ amesema tena:

“Mche Allah popote ulipo na baada ya kufanya ovu tenda jema ambalo linalifuta, na ishi na watu kwa tabia nzuri: (Ahmad, Tirmidhi, al-Hakim).

Kwa sababu hii Muislamu anaishi akiwa katika kuielimisha nafsi yake kuitakasa na kuitoharisha. Kwani nafsi ndiyo kitu cha kwanza kinachotakiwa kuabudu. Kwa hiyo aifundishe tabia itayoitakasa na kuisafisha na uchafu wake, na aiepushe na kula kinachoichafua na kuiharibu, na kupambana na itikadi mbaya, na maneno na matendo mabaya usiku na mchana. Aifanyie mahesabu kila wakati, ailazimishe kufanya mema, aisukume kwa nguvu zake zote kwenda katika twaa, aiondoe kwa juhudi zake zote kwenye shari na uharibifu, na aitoe huko. Zifuatazo ni hatua za kufuata katika kuiabudisha nafsi na kuitakasa:

a) **Kutubu**

Maana ya kutubu ni kuacha madhambi na maasi na kujua kila dhambi alizozifanya, na kuazimia kutokurudia tena kwenye kosa hilo katika kipindi kijacho cha umri wake.

Hayo ni kwa Kauli Yake Allah:

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ آمَنُوا تَوْبُوا إِلَى اللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوحًا عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يُكَفِّرَ
عَنكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيُدْخِلَكُم جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يَوْمَ لَا
يُخْزِي اللَّهُ النَّبِيَّ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ

“Enyi mlio amini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli! Asaa Mola wenu Mlezi akakufutieni maovu yenu na akakuingizeni katika Pepo zipitazo mito kati yake, siku ambayo Mwenyezi Mungu hatamdhalilisha Nabii na walio amini pamoja naye...” (66:8).

Na Kauli Yake:

وَتَوْبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهُ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

“Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa..” (24: 31).

Mtume ﷺ amesema:

“Ee nyinyi watu tubuni kwa Allah mimi ninatubu kwa siku mara mia moja” (Muslim).

Na kauli yake:

“Atayetubu kabla jua halijachomoza kutoka Magharibi (Kiama) Allah hupokea toba yake.” (Muslim).

Na kauli yake:

“Allah hutandaza mkono wake kwa kupokea toba kwa anayefanya maovu usiku mpaka mchana, na kwa anayefanya maovu mchana mpaka usiku (vivyo hivyo) hadi kuchomoza jua upande wa Mashariki kutokea Magharibi yake.” (Imamu Muslim).

Na kauli yake:

“Wallahi Allah Anafurahi mno kwa toba ya mja wake Muumini kuliko mtu aliye jangwani, akiwa na mnyama wake juu ya mnyama huyo kuna chakula na kinywaji chake, kisha akalala na alipoamka akakuta ameshaondoka (ngamia amekimbia) akamtafuta hata akafikwa na kiu, kisha akasema nirudi pale mahala pangu ambapo nilikuwa, nilale mpaka nife. Akaweka kichwa chake kwenye dhira ya yake (akalalia mkono wake) ili afe akaamka akamkuta mnyama wake akiwa amerudi na chakula chake na kinywaji chake: basi Allah ana furaha kubwa zaidi kwa toba ya mja (Muumini) kuliko furaha za huyo kwa kurudi mnyama wake na chakula chake.” (Muslim na Ahmad).

Hadithi iliyopokewa kuwa Malaika alimpongeza Adam kwa toba yake wakati Allah alipompokelea toba yake:

b) Kuchunga Mipaka ya Allah

Maana yake: Muislamu aiweke nafsi yake katika hali ya kuchunga mipaka ya Allah, kujilazimisha na hali hiyo kila wakati miongoni mwa nyakati za uhai wake mpaka awe na yakini kuwa Allah Anamuona. Anazijua siri zake. Anayaona matendo yake na Anaisimamia kila nafsi kwa matendo yake. Naye kwa kufanya hivyo wakati wote atakuwa katika kuuona Utukufu wa Allah na Ukamilifu Wake. Huku akijiliwaza kwa kumtaja Kwake Allah, na akipata raha katika kumtii. Hivyo basi nafsi itapenda kuwa Naye itaelekea Kwake, itapuuzza kila kisichokuwa Allah. Hii ndiyo maana ya kuusalimisha uso uliyo katika kauli ya Allah:

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَاتَّبَعَ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ
حَنِيفًا ۗ وَاتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٢٥﴾

“Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliye usalimisha uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa mwema, na anafuata mila ya Ibrahim mwongofu?.” (4:125).

﴿ وَمَنْ يُسَلِّمْ وَجْهَهُ إِلَى اللَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ ۗ ﴾

“Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti...” (31:22).

Na hiyo ndiyo maana ya wito wake Allah katika kauli yake:

﴿ وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي أَنْفُسِكُمْ فَاحْذَرُوهُ ۗ ﴾

“...Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo katika nafsi zenu. Basi tahadharini naye...” (2:235).

﴿ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا ۝ ﴾

“...Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni.” (4:1).

Na kauli yake:

﴿ وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ ۗ ﴾

“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo” (10:61)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Muabudu Allah kama unamuona na kama haumuoni Yeye anakuona.” (Bukhari na Muslim).

Huo ndiyo utaratibu walioutumia waliotangulia wa mwanzo walio wema katika Umma huu, kwamba nafsi zao wamezilazimisha hayo mpaka wakaufikia uhakika na wakafikia daraja la kukurubishwa kwa Allah, na hizi hapa athari zinazowashuhudia:

Minhajil Muslim

1) Aliulizwa Aljunaid (Allah Amrehemu), “Nini kinachosaidia kuinamisha macho? Akasema: “Ni wewe kuelewa kuwa Allah anakuona kabla wewe hujamuona huyo anayeangaliwa mwanzo katika angalio lako kwake”.

2) Amesema Sufiani Thauriy:

“Muangalie sana yule ambaye hakuna kinachojificha Kwake na mtarajie mno mtekeleza ahadi, (Allah) na muogope sana Anayemiliki adhabu.”

3) Ibnu Mubarak alimwambia mtu, “Muone Allah ewe Fulani” Yule mtu akamuuliza namna ya kumwuona, naye akamwambia: “Daima uwe kama unamuona Allah Aliyeshinda na Kutukuka.”

4) Amesema Abdullah Ibni Dinari: Nilitoka na Umar Ibnul – Khattwab kwenda Makkah tukapumzika njiani akatujia mchungu kutoka mlimani, Umar akamwambia, “Ewe mchungu tuuzie mbuzi mmoja. Mchungu akasema, “Huyo amemilikiwa.” Umar رضى الله عنه akamwambia, “Mwambie bwana wako mbuzi ameliwa na mbwa mwitu.” Yule mtumwa akasema: “Allah yuko wapi?” Umar akalia na akaenda kwa bwana wake akamnunua yule mtumwa na akamwacha huru.”

5) Na imepokewa kuwa: Zulaikha alipokuwa faragha na Nabii Yusuf عليه السلام alisimama na akaufunika uso wa sanamu lake, Yusufu akamuuliza “Vipi wewe waona vibaya kuonwa na kisicho na uhai na nisione vibaya kuonwa na Mfalme Mwenye Nguvu?”

Badhi Yao wameimba katika Mashairi.

Kama utakuwa peke yako pahala siku moja katika maisha usiseme,
Niko peke yangu. Lakini sema juu yangu kuna Raqibu (mwangalizi).
Na wala usidhanie kuwa Allah anaghafilika hata saa moja.
Wala kuwa unachokificha kwa Allah hakionekani.
Kwani huoni leo yaondoka haraka,
Na kesho kwa wanaoisubiri iko karibu.

c) Kujihesabu Matendo Yako

Kama ilivyo kawaida Muislamu katika maisha haya anafanya kazi usiku na mchana ili akipate kitachompa maisha bora akhera na kumfanya awe na sifa ya kupata utukufu akhera. Na ili kupata ridhaa za Allah akhera, hapa duniani ndio mahala pa kufanya hayo inamlazimu, ayaangalie kwanza yale ya wajibu kama anavyoangalia mfanya biashara rasilimali yake-msingi—na sunna aziangalie kama anavyoziangalia mfanya biashara faida ya ziada kwenye rasilimali. Ayaangalie maasi na dhambi kama hasara katika biashara. Kisha mwisho wa kila siku ni kuifanyia mahesabu nafsi yake kwa kazi ya siku ile. Kama atagundua upungufu katika wajibu ailaumu na kuikemea na asimame wakati ule ule kupaunga palipo vunjika. Kama utakuwa wajibu unalipwa atalipa, la hakilipwi basi atakiunga kwa kuzidisha sunna na kama upungufu utakuwa katika sunna basi ataleta badala ya upungufu. Hii ndio maana ya kuihesabu nafsi. Nayo ni moja ya njia za kuitengeneza nafsi, na kuifundisha pia kuitakasa. Dalili za hayo ni hizi zifuatazo:

Na amesema Allah Aliyetukuka:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اتَّقُوا اللّٰهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ وَّاتَّقُوا
اللّٰهَ ۚ اِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿٥٩﴾

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayo yatanguliza kwa ajili ya Kesho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari ya mnayo yatenda.” (59:18).

Na amesema Aliyetukuka:

وَتُوبُوْا اِلَى اللّٰهِ جَمِيْعًا اِنَّهُۥ اَلْمُوْمِنُوْنَ لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُوْنَ ﴿٣١﴾

“...Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa.” (24:31).

Na amesema Mtume ﷺ,

“Mimi ninatubu kwa Allah na ninamuomba msamaha kila siku mara mia moja.” (Abu Dawud).

Na Umar رضي الله عنه amesema,

“Zihesabuni nafsi zenu kabla hamjapimwa.” Na alikuwa Umar رضي الله عنه unapomfika usiku anazipiga nyayo zake kwa bakora na anaiambia nafsi yake. *“Leo umefanya nini?”*

Abu Talha ilipomshughulisha Bustani yake na akakosa kuswali aliitoa sadaka. Na asingelifanya hivi isipokuwa kwa sababu ya kuihesabu nasi yake, kuilaumu na kuipa adabu.

Imepokewa kutoka kwa Haniff Ibnu Qais alikuwa anakuja kwenye taa na anakiweka kidole chake kwenye moto wa taa mpaka anauhisi moto, halafu anaiambia nafsi yake. *“We Haniff nini kilichokufanya kuyafanya (madhambi) uliyofanya siku kadhaa nini kilichokufanya ukayatenda makosa siku ile?”*

Imepokewa kuwa mcha-Mungu mmoja alikuwa anapigana vitani akajitokeza kwake mwanamke akiwa hana nguo akamuangalia, akainua mkono wake na akalipiga jicho lake akalipasua na akasema *“Wewe kwa nini umeangalia kinachokudhuru!”*

Mtu mmoja alipita kwenye chumba akauliza chumba hiki kimejengwa lini? Kisha akaielekea nafsi yake akasema, *“Kwa nini unaniuliza kisicho kuhusu basi nitakuadhibu kwa kufunga mwaka mzima”* Basi akafunga mwaka mmoja.

Na imepokewa kuwa kuna mcha-Mungu mmoja alikuwa anaenda kwenye kokoto za mawe yenye joto kali na anajigeuza geuza juu yake na anaiambia nafsi yake onja joto hili na ujue kuwa jahannamu kuna joto kali zaidi. Pia kuna mcha-Mungu mmoja aliinua kichwa chake na akamuona mwanamke ghorofani akamuangalia akaichukulia ahadi nafsi yake kuwa hataangalia juu tena katika uhai wake wote.

Basi hivi ndivyo walivyoishi wacha-Mungu wa umma huu waliopita wakizihesabu nafsi zao kwa kutotekeleza wajibu wake na wanazilaumu kwa uzembe wake na wanazilazimisha kumcha-Allah na wanazikataza ubinafsi wake. Walifanya hivyo kwa kuitumia kauli Yake Allah:

وَأَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوَىٰ ۗ فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ
الْمَأْوَىٰ ۝

“Na ama yule anaye ogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamania, Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake!” (79:40-41).

d) Jihadi ya Nafsi:

Maana yake: Muislamu anatakiwa aelewe kuwa adui yake mkubwa zaidi ya wote ni nafsi yake aliyonayo, na kwamba nafsi kimaumbile inapenda shari, na haipendi kheri, na inaamrisha maovu.

إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي ۗ

“Kwa hakika nafsi ni mno kuamrisha maovu...” (12:53)

Na inapenda starehe na kubaki katika raha, inapenda uvivu na kufanya matamania hata kama zitagharimu maisha yake na uhai wake.

Muislamu akiyaelewa haya atajiandaa kwa mapambano dhidi ya nafsi yake, kwa hiyo ataitangazia vita, na ataielekezea silaha, atapania kupambana na raha zake, na kupambana na matamania yake. Ikitaka raha, anaichokesha, ikitamani kitu anainyima, na inapozembea katika ibada au kheri anaiadabisha. Vivyo hivyo na kuilaumu, anailazimisha kukifanya ilichokiacha, na kukilipa asichokifanya, anaiadhibu hivi mpaka inatulizana na kuwa nzuri na kutoharika. Huo ndio upeo wa kupambana na nafsi.

Amesema Allah,

وَالَّذِينَ جَاهَدُوا فِينَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِينَ ۝

“Na wanao fanya juhudi kwa ajili yetu, Sisi tutawaongoa kwenye njia zetu. Na hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na watu wema.” (29: 69).

Muislamu anapopambana na nafsi yake kwa ajili ya Allah ili iwe nzuri, na kusifika, kutoharika na kutulizana na ili iwe na sifa ya kupata karama za Allah Aliyetukuka na ridhaa Yake. Katika jitihada hizo anaelewa kuwa hii ndio njia ya wacha-Mungu ndio njia ya waumini wa kweli. Kwa hiyo atapita nayo kwa kuwaiga wao na atafata nyayo zao. Kwani Mtume ﷺ aliposimama usiku kufanya ibada mpaka zikavimba nyayo zake tukufu na akaulizwa kuhusu hilo alisema,

“Hivi hamtaki niwe mwenye kushukuru? Wallah ni yapi mapambano makubwa zaidi ya mapambano haya?” (Bukhari na Muslim).

Ally رضي الله عنه anawaelezea masahaba wa Mtume ﷺ anasema:

“Wallahi Nimewaona maswahaba wa Muhammad ﷺ na wala sioni kuna kitu kinachofanana nao, walikuwa wanapofika asubuhi wanakuwa nywele tintim na vumbi tupu, rangi ya njano na usiku kucha walikuwa wanasujudu na wanasimama na walikuwa wanasoma kitabu cha Allah ili wapumzishe nyayo zao na nyuso zao. Na walikuwa anapotajwa Allah wanayumba kama unavyoyumba mti siku ya upepo mkali, yanatoka machozi macho yao mpaka nguo zao zinaroa.”

Na amesema Abu Darda رضي الله عنه:

“Kama si mambo matatu nisingependa kuishi hata siku moja: Kitu cha kufunga kwa ajili ya Allah kipindi cha jua kali, kumsujudia katikati ya usiku na kukaa na watu wanaochambua maneno mazuri kama wanavyoyachambua matunda.”

Umar رضي الله عنه alilaumu nafsi yake kwa kumkosesha Swala moja ya Alasiri katika jamaa na akatoa shamba lake sadaka kwa kosa hilo. Shamba lenye thamani ya dirham laki mbili.

Abdallah Ibni Umar رضي الله عنه alikuwa kama itamkosa Swala moja kwa jamaa basi atauhuisha usiku huo wote. Siku moja aliichelewesha Swala ya Magharibi mpaka zikachomoza nyota mbili akawaacha huru watumwa. Allah awasamehe watu ambao wengine wanawadhani kuwa ni wagonjwa, kutokana na kupambana na nafsi.

Mtume ﷺ anasema,

“Mbora wa watu ni yule mwenye umri mrefu na yakawa mazuri matendo yake.” (At-Tirmidhi)

Uwaisul-Qarni رضي الله عنه alikuwa akisema: “Huu ni usiku wa rukuu na hapo anauhusisha usiku wote kwa raka moja, na usiku unaofata anasema huu ni usiku wa sijida basi atauhuisha usiku wote kwa sijida moja.”

Thabiti al-Bannan amesema, “Nimewahi kuwaona watu mmoja wao anaswali mpaka anashindwa kufika kitandani pake isipokuwa kwa kutambaa na mwengine anasimama mpaka nyayo zake zinavimba kwa urefu wa kisimamo. Na anajitahidi katika ibada kwa kiasi kwamba kama itasemwa kuwa kiama kiko kesho asingepata cha kuongeza katika ibada. Na kinapofika kipindi cha baridi anapanda kwenye sakafu ya juu wakati wa usiku ili limpige baridi asipate kulala na kipindi cha joto kinapoingia anasimama chini ya sakafu ili joto limnyime usingizi.”

Kuna wengine walikuwa wanafariki wakiwa katika sijida. Mke wa Masruq amesema: “Masruq hataonekana isipokuwa atakutwa miguu yake imevimba, kwa kisimamo kirefu wallahi nilikuwa ninakaa nyuma yake naye anaswali ninalia kwa kumuhurumia”.

Kuna mwengine anapofika umri wa miaka arubaini anakunja godoro lake ili asipate kulala tena kwenye godoro.

Inaelezwa kuwa kulikuwa na mwanamke mcha-Mungu miongoni mwa wake wa wacha-Mungu anaitwa Ajarah alikuwa kipofu, unapofika wakati wa alfajiri anaomba kwa sauti yake ya huzuni. “Wacha-Mungu wamemaliza usiku wote wakishindana na kukimbilia kwako kwa kufanya ibada ili kupata rehema zako, na Ubora wa Maghfira Yako. Nina kuomba Wewe tu Ewe Mola wangu uniweke mwanzoni mwa kundi la mwanzo na uniinue na kuiweka katika pepo yako ya daraja la juu, na unitie katika kundi la waja zako wacha-Mungu. Wewe ni Mwenye Huruma zaidi ya wote wenye huruma na Mtukufu wa Watukufu, na Karimu wa makarimu Ewe Karimu. Kisha anasujudu anaendelea kuomba huku akilia na kutoa machozi mpaka alfajiri.”



Mada ya Sita

Kuwa na Adabu na Heshima kwa Viumbe

a) Kwa Wazazi Wawili:

Muislamu anaamini haki ya wazazi wawili iliyo juu yake na wajibu wa kuwafanyia wema, kuwatii, na kuwafanyia hisani. Si tu kwa sababu wao ni sababu ya kupatikana kwake, au wamemfanyia wema, kwa hiyo analazimika kulipa bali Allah Amelazimisha hivyo, na Amewajibisha juu ya mtoto awafanyie wema na hisani wazazi wake. Hilo Amelitaja pamoja na haki Yake Allah ya kuabudiwa Yeye Pekee.

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۗ إِمَّا يَبُلُغَنَّ عِنْدَكَ
الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أُفٍّ وَلَا تَنْهَرهُمَا وَقُلْ لَهُمَا
قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ وَأَخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ
أَرْحَمُهُمَا كَمَا رَبَّيْتَنِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾ ﴾

“Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemu wa hishima. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyo nilea utotoni..” (17:23-24).

Na pia Allah amesema:

﴿ وَوَصَّيْنَا الْإِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ وَهْنًا عَلَىٰ وَهْنٍ وَفِصْلَهُ فِي عَامَيْنِ
أَنَّ اشْكُرْ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ ﴿٢٣﴾ ﴾

“Na tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. (Tumemuusia): Nishukuru Mimi na wazazi wako. Ni kwangu Mimi ndiyo marudio” (31:14).

Na Mtume ﷺ amesema kumuambia mtu aliyemuuliza akisema!

“Nani mwenye haki zaidi kuwa na ushirikiano naye mzuri?” Akasema, “Mama yako!” Akauliza, “Kisha nani?” Akasema, “Mama yako.” Akauliza “Kisha nani?” Akasema, “Baba yako.” (Bukhari na Muslim)

Na Mtume ﷺ amesema,

“Hakika Allah ameharamisha juu yenu kuwaasi mama zenu na zuia na lete, na kuwazika wasichana wakiwa bado wazima na amefanya kuwa ni karaha kwenu kusemasema ovyo kuwa ombaomba na kutumia mali ovyo.” (Bukhari na Muslim).

Mtume ﷺ amesema:

“Je hamtaki niwaambieni dhambi kubwa katika madhambi makubwa?” Wakasema: “Tuambie Ewe Mjumbe wa Allah,.” Akasema, “Ni kumshirikisha Allah na kuwaasi wazazi wawili na alikuwa ameegemea, akakaa na akasema, “Eleweni pia kusema urongo na kutoa ushahidi wa urongo” na aliendelea kusema hivyo mpaka Abukakari akasema, “Laiti angalinyamaza.” (Bukhari na At-Tirmidhi).

Mtume ﷺ amesema:

“Mtoto hawezi kumlipa mzazi isipokuwa kama atamkuta amemilikiwa (mtumwa) akamnunua akamuacha huru.” (Abu Dawud, At-Tirmidhi, Ibn Majah na Imam Ahmad).

Na Abdallah Ibnu Masoud رضي الله عنه amesema:

“Nimemuuliza Mtume ﷺ ni tendo lipi linalopendwa zaidi na Allah?” Akasema: “Kuwapanyia wema wazazi wawili. Nikauliza, ”Kisha lipi?” Akasema: Kupigana jihadi katika njia ya Allah. Na alikuja mtu kwa Mtume ﷺ akimtaka amruhusu kushiriki vitani akamuuliza, ‘Je wazazi wako bado wako hai?’ Akajibu ndio.’ Akasema: “Jihadi yako ifanye juu yao (kwa kuwatii na kuwasaidia).” (Bukhari, Muslim na An-Nasai).

Na akaja mtu kwa Mtume ﷺ katika Ansvari akauliza,

“Ewe Mtume wa Allah ni kitu gani cha wema kilichobaki cha kuwapanyia wazazi wangu baada ya kufariki kwao?” Akasema:”Ndio, kuna mambo manne, kuwaombea dua, kuwatakia msamaha, kutekeleza ahadi zao, kuwakarimu rafiki zao, na kuunga undugu ambao hauna undugu usipokuwa kupitia kwao, hicho ndicho kilichobaki juu yako cha wema kwao baada ya kufariki kwao.” (Abu Dawud katika sahihi yake).

Na Mtume ﷺ amesema,

“Hakika wema mkubwa ni mtu kuwapanyia wema watu wapenzi wa baba yake baada ya kuondoka kwake.”(Muslim).

Muislamu anapoitambua haki hii kwa wazazi wawili na akaitekeleza kwa ukamilifu anakuwa katika kumtii Allah Aliyetukuka na kutekeleza wasia wake. Muislamu pia anajilazimisha kufuata adabu zifuatazo:

1) **Kuwatii kwa kila walichoamuru**, au kukikataza mradi kisiwe kumuasi Allah, na wala si kinyuume cha sheria Yake. Kwa sababu hakuna haki ya kumtii mja katika kumuasi Muumba kwa kauli Yake,

وَأِنْ جَاهِدَاكَ عَلَىٰ أَنْ تُشْرِكَ بِي مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا
وَصَاحِبَهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۚ وَاتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَىٰ

“Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwat’ii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anaye elekea kwangu...” (31:15).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Hakuna haki ya kutii kiumbe katika kumuasi Muumba”

2) **Kuwaheshimu**, kuwapa taadhima, kuwanyenyekea na kuwakirimu kwa lugha nzuri na matendo mazuri. Usiwakaripie, usinyanyue sauti yako juu ya sauti ya wazazi, usitembee mbele yao, usimtangulize juu ya mke wala watoto wako. Usiwataje kwa majina yao, bali waite baba, mama, usisafiri isipokuwa kwa ruhusa yao na ridhaa yao.

3) Kuwafanyia wema kwa kila kilicho katika uwezo wako, katika aina za wema na hisani, kama vile kuwalisha, kuwavisha, kuwatibu kuwaondolea kero, kujitolea muhanga kwa ajili yao.

4) Kuunga udugu ambao hakuna udugu huo isipokuwa kupitia kwao. Kuwaombea na kuwataki maghfira, kutekeleza ahadi zao na kuwaheshimu rafiki zao.

b) Kwa watoto

Muislamu anatambua kuwa mtoto anayo haki kwa baba yake. Baba anawajibika kumtekelezea mwanawe haki hizo, pia kuna adabu (heshima) anapaswa azitekeleze kwa mwanawe.

Haya yanapatikana katika: Kumchagulia mama yake, (kuchagua mchumba) kumpa jina zuri siku ya saba baada ya kuzaliwa, kumfanyia Akika, kumtahiri, kumhurumia, kumpa matumizi, kumlea vizuri, kumuelimisha, kumfundisha Dini–Uislamu–Kumzowesha katika kutekeleza wajibu wa dini na sunna zake. Akibaleghe amuolee au amuozeshe, kisha amkhiyarishe akitaka kuishi chini ya himaya yake au ajitegemee.

Hayo yote ni kwa hoja zifuatazo:

Kauli Yake Allah:

﴿ وَالْوَالِدَاتُ يُرْضِعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُنْمِ
الرِّضَاعَةَ وَعَلَى الْمَوْلُودِ لَهُ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ ﴾

“Na wazazi wanawake wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kaamili kwa anaye taka kutimiza kunyonyesha. Na juu ya baba yake chakula cha kina mama, na nguo zao kwa mujibu wa ada...” (2:233).

Na Allah amesema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قُوًا أَنفُسِكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ
عَلَيْهَا مَلَكٌ غَلَاظٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا
يُؤْمَرُونَ ﴿٦٦﴾

“Enyi mlio amini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrisha” (66:6)

Katika aya hizi ana amri ya kuilinda familia na moto, na hayo yatapatikana kwa kumtii Allah. Kumtii Allah kutalazimu kuelewa kuwa ni yapi yenye wajibu wa kumtii.

Kwa Mtoto kumtii Allah hakupatikani bila ya elimu na kwa kuwa mtoto ni sehemu ya familia ya mtu, basi aya hii ni hoja inayothibitisha uwajibu juu ya baba kumsomesha mtoto wake, kumlea, kumuepusha na ukafiri, maasi, shari na uharibifu. Mzazi kwa kumfanyia hivyo mtoto atakuwa anamlinda na moto.

Kwa kuwa katika aya ya kwanza kina mama wanatakiwa wawanyonyeshe watoto wao kuna hoja inayowajibisha matumizi ya mtoto juu ya baba. Kwa sababu yale matumizi yaliyo lazimika kumpa mama anayenyonyesha ni kwa sababu ya kumnyonyesha mtoto:

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ

*“...Wala msiwauwe wana wenu kwa kuogopa umasikini...”
(17:31)*

2) Kauli yake Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu Madhambi makubwa mno, naye akasema:

“Ni kumuwekea Allah mshirika wakati Yeye Ndiye Aliye kuumba na kumuua mwanao ili asile pamoja nawe, na kuzini na mke wa jirani yako.” (Bukhari, Muslim na An-Nasai).

Kwa hiyo kuzuia kuua watoto kunalazimisha kuwafanyia huruma, kuitunza miili yao, akili zao na roho zao. Katika kumfanyia mtoto Akika Mtume ﷺ amesema,

“Mtoto yuko rehani kwa Akika anayochinjiwa siku ya saba, atapewa jina siku hiyo na anyolewe nywele za kichwa chake.” (al-Hakim, At-Tirmidhi).

Mtume ﷺ amesema:

“Sifa za kimaumbile ni tano: Hitani, usafi wa sehemu za siri (kinena), kupunguza masharubu, kukata kucha na kunyowa nywele za kwapa.” (Bukhari, Muslim Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Majah)

Mtume ﷺ amesema:

“Wakirimuni watoto wenu, na wafundisheni tabia zuri, kwa sababu watoto zenu ni zawadi zenu.” (Ibnu Majah, Dhaifu).

Na Mtume ﷺ amesema:

“Toeni (wagawieni) sawa kati ya watoto zenu, kama ningalikuwa ninampendelea mtu basi ningeliwapendelea wanawake.” (Bukhari na Twabarani).

Mtume ﷺ amesema:

“Waamrisheni watoto Swala baada ya umri wa miaka saba na wapigeni kwa sababu ya kuacha Swala wakiwa na umri wa miaka kumi na watenganisheni katika kulala (wasilale pamoja).” (al-Hakim, At-Tirmidhi).

Na Imekuja katika Athar:

Minhajil Muslim

“Miongoni mwa haki za mtoto kwa baba ni: kumfundisha adabu nzuri na kumpa jina zuri.”

Na amesema Umar **رضي الله عنه**,

“Miongoni mwa haki za mtoto kwa baba amfundishe kuandika, kulenga shabaha na asimpe ila cha halali kizuri.”

Na yamepokewa kutoka kwake vile vile kauli:

“Oeni katika nyumba bora, hakika ya asili –silika – inarithisha.”

Mtu mmoja amewasimulia wanawe jinsi alivyo fanikiwa kumpata mama yao na bahati alioipata kwa kupata mke bora akasema:

“Hisani yangu ya kwanza kwenu ni uteuzi wangu wa yule mwenye asili nzuri na kujitunza kwake (kujihifadhi) kuko bayana.”

c) Kwa Ndugu:

1) Muislamu anaamini kuwa adabu (na heshima) anayotakiwa kuwafanyia ndugu ni sawa na ile anayowafanyia baba, mama na watoto. Kwa hiyo ndugu wadogo wanapaswa kuwahesimu wakubwa zao kama wanavyo waheshimu baba zao, na ndugu wakubwa kwa wadogo zao. Wanapaswa kuwahurumia wadogo zao kama wanavyo hurumiwa na baba zao. Wote wana haki na wajibu wa kuyatekeleza kwa ushahidi wa Hadithi zifuatazo:

“Haki za ndugu mkubwa kwa wadogo zao ni sawa na haki za mzazi kwa mwanawe.” (Baihaqy dhaifu).

2) Kauli yake Mtume **ﷺ,**

“Mfanyie wema mama yako na baba yako, dada yako na ndugu yako kisha wa chini yako.” (Bazzar Hasan, Al-Hakim).

d) Kati ya Mume na Mke:

Muislamu anazitambua adabu na heshima za pande mbili kati ya mume na mke wake na hizo ni haki za kila mmoja kwa mwenzake kwa kauli Yake Allah Aliyetukuka:

وَيُعَوِّلُهُنَّ أَحَقُّ بِرِدَّهِنَّ فِي ذَلِكَ إِنْ أَرَادُوا إِصْلَاحًا وَهِنَّ مِثْلُ الَّذِي

عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٨﴾

“...*Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.*” (2:228).

Aya hii tukufu imethibitisha kuwa kila mmoja kati ya mume na mke ana haki kwa mwenzake na inamuhusisha mwanaume kwa nyongeza ya kuwa na daraja la juu kwa mwanamke kwa mazingatio maalumu.

Na kauli yake Mtume ﷺ katika Hijja ya wadai (kuaga):

“*Eleweni kuwa mna haki juu ya wake zenu na wake zenu wana haki juu yenu.*” (At-Tirmidhi).

Isipokuwa haki hizi baadhi yake wanashirikiana mume na mke, na baadhi yake ni za mume tu au za mke tu.

Haki wanazoshirikiana Mume na Mke:

1) **Uaminifu:** Analazimika kila mmoja awe muaminifu kwa mwenzake, asimfanyie hiyana katika uchache wala wingi, kwa dogo wala kwa kubwa. Kwa sababu mume na mke wanafanana mno na ni watu waliounda ushirika. Hivyo basi ni lazima ukamilike uaminifu, kunasihiana, ukweli na usafi wa nyoyo kati yao, katika kila jambo linalohusu maisha yao kwa pamoja au liwe linamuhsu mmoja wao.

2) **Mapenzi na kuhurumiana** kila mmoja awe na kiwango kikubwa kwa mwenzake cha mapenzi maalumu na huruma pana kati yao kwa muda wa uhai wao ili kuthibitisha kauli Yake Allah Aliyetukuka pale aliposema,

وَمِنْ آيَاتِهِمْ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا

وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً

“Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu...” (30: 21).

Na kuithibitisha kauli yake Mtume ﷺ:

“Asiye na huruma kwa wenzake naye hafai kuhurumiwa.”
(Bukhari, Muslim na Abu Dawud).

3) Dhamana kati yao: Kila mmoja awe ni mdhamini wa mwenzake, asiwe na shaka naye hata kidogo katika ukweli wake, nasaha zake, na usafi wa moyo wake.

Kwa kauli Yake Allah:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ

“Hakika Waumini ni ndugu....” (49:10).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Hawi muumini kamili mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake (Muislamu) yale anayojipendelea yeye mwenyewe,”
(Bakhari, Muslim, At-Tirmidhi)

Uhusiano wa ndoa si zaidi ya uhusiano wa imani isipokuwa kwa dhamana umadhubuti na nguvu. Kwa sababu hiyo kila mmoja anahisi kuwa yeye na mwenzake ni kitu kimoja. Kama vivyo ndivyo basi vipi mtu asijiamini mwenyewe na akakosa kuinasihi nafsi yake? Au vipi mtu atajihadaa mwenyewe na kujidanganya.

4) Adabu kwa ujumla: kama vile upole katika ushirikiano, kuonyesha uso wa tabasamu, ukarimu wa maneno, heshima na kuishi vizuri kama Alivyoamrisha Allah,

وَعَاشِرُوهُمْ بِالْمَعْرُوفِ

“...Na kaeni nao kwa wema.” (4:19).

Na huko ndiko kuusiana kheri alikoamuru Mtume Mtukufu ﷺ katika kauli yake,

“Usianeni kwa wanawake kuwafanyia kheri.” (Bukhari).

5) Na huu ni muhtasari wa adabu na heshima za pande mbili (ushirika) kati ya mume na mke ambazo wanatakiwa kuzitekeleza kati yao ili kutimiza ahadi nzito zilizoashiriwa katika Kauli Yake Allah Aliyetukuka,

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أَفْضَىٰ بَعْضُكُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ وَأَخَذْنَ مِنْكُمْ

مِيثَاقًا غَلِيظًا ﴿٢١﴾

“Na mtachukua je na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi, na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti?” (4: 21).

Na kumtii Allah Aliyesema:

وَلَا تَسْأُوا الْفَضْلَ بَيْنَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٣٧﴾

“...Wala msisahau fadhila baina yenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayaona mnyo yatenda” (2:237).

Ama haki zinazomuhusu kila mmojawao juu ya mwenzake, na adabu zinazomlazimu kila mmojawao ni:

Haki za Mke Juu ya Mume:

1) Aishi naye kwa wema kwa kauli ya Allah,

وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ

“...Na kaeni nao kwa wema...” (4:19).

Amlishe kile anachokula amvishe kile anachovaa. Amfundishe adabu na heshima kama atahofia kumfanyia maasi kwa njia aliyoiamuru Allah kuwafundisha wanawake, kama vile kumuonya, bila ya matusi wala lugha mbaya. Kama atamtii,

Minhajil Muslim

basi ni kheri na asipomtii, iwe kwa kumuhama kitanda, na asipomtii basi iwe kwa kumpiga isipokuwa usoni. Tena kwa pigo lisiloumiza, lisilotoa damu na lisiloharibu, au kupoteza uwezo wa viungo vyake, kwa kauli yake Allah:

وَالَّتِي تَخَافُونَ نُشُوزَهُمْ فَعِظُوهُمْ وَأَهْجُرُوهُمْ فِي الْمَضَاجِعِ وَأَصْرِبُوهُمْ
فَإِنْ أَطَعْتَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِمْ سَبِيلًا

“...Na ambao mnachelea kutoka katika utiifu wanasihini, muwahame katika malazi na wapigeni. Wakikut’iini msiwatafutie njia ya kuwaudhi bure.” (4: 34)

Kauli yake Mtume ﷺ aliyomwambia mtu aliyemuuliza:

*“Ni zipi haki za mke wa mmoja wetu juu yake?” Akasema:
“Umpe chakula kama unachokula na umvishe kwa unachovaa, usimpige usoni usimwambie kwa lugha mbaya na wala usimuhame isipokuwa humo humo ndani.” (Abu Dawud, Hasan).*

Na kauli yake:

“Elewa!! Na haki zao juu yenu muwafanyie hisani katika vazi lao na chakula chao.”

Na Mtume ﷺ amesema,

“Muumini mwanaume asimbughudhi Muumini mwanamke kama atamchukia kwa tabia fulani atairidhia tabia nyingine.” (Muslim, Ahmad).

2) **Amfundishe mambo ya lazima katika mambo ya dini** yake kama hayaelewi, au amruhusu kwenda darasani akajifunze. Kwa sababu mahitaji yake ya kuitengeneza Dini yake na kuitakasa roho yake si tofuati na mahitaji yake ya chakula, na ya kinywaji ambayo ni lazima kumpa.

Kwa kauli Yake Allah:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قُوًا أَنفُسِكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ

“Enyi mlio amini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe...” (66: 6)

Na mke ni katika familia na kumuokoa kwake na moto ni kwa kumjaza imani na matendo mazuri. Na matendo mazuri hayapatikani bila elimu ili aweze kuyatekeleza na kuyafanya kama yanavyotakiwa kisheria. Kauli yake Mtume ﷺ,

“Zindukeni! Usianeni usia wa kheri kwa wanawake kwani si vingine hao kwenu ni wasaidizi.”

Na katika kumuusia kheri ni kumfundisha kitacho mtengenezea Dini yake na kumfundisha kitachomdhaminia usawa, haki na hali nzuri.

3) **Amlazimisha kufuata maadili ya Uislamu na adabu zake, amzuie** kwenda kichwa wazi au kuonesha mapambo yake, asimruhusu kuchanganyika na wasio kuwa maharim zake katika wanaume. Amuwekee ulinzi wa kutosha, na matunzo kamili, asikubali aharibike tabia au Dini yake. Asimpe nafasi ya kuacha kutekeleza amri za Allah na Mtume wake au kufanya maasi. Kwa sababu yeye ndiye muhusika wa kumchungu, na mwenye jukumu la kumtunza.

Kwa kauli Yake Allah,

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ

“Wanaume ni wasimamizi wa wanawake...” (4:34)

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Mwanamume ni mchungu katika familia yake.” (Bukhari na At-Tirmidhi).

4) **Afanye usawa kati yake na mke mwenzake**, kama anaye mke mwenzake, awafanyie usawa katika chakula, kinywaji, kivazi, makazi, na kulala. Asidhulumu kitu katika hivyo kwani Allah ameharamisha hayo, kwa kauli Yake:

وَأِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ
مَثْنَىٰ وَثُلَاثَ وَرُبْعًا

“Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia mayatima uadilifu, basi oeni mnao wapenda katika wanawake, wawili au watatu au wane...” (4:3).

Mtume ﷺ ameusia kuwafanyia kheri akasema:

“Mbora wenu ni mbora wenu kwa familia yake, nami ni mbora wenu kwa familia yangu.” (At-Tirmidhi, Ibn Majah, Darimi, Twabaran).

5) **Asiitoe siri yake**, na asitaje kasoro zake, kwani yeye ndiye anayetakiwa kuzihifadhi, kuzitunza na kuzilinda. Kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Hakika miongoni mwa watu wabaya mbele ya Allah kwa daraja Siku ya Kiama ni mwanamume anayekutana na mkewe na mke anayekutana na mume kisha anazisambaza siri”. (Muslim).

Pili: Haki za Mume Juu ya Mke:

Ni wajibu juu ya mke kumfanyia mumewe yafuatayo:-

1) **Kumtii isipokuwa katika kumuasi Allah. Kwa kauli Yake Allah:**

فَإِنْ أَطَعْنَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِنَّ سَبِيلًا

“... Wakikutiini msiwatafutie njia ya kuwaudhi bure...” (4:34).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Mume anapomuita mkewe Kitandani kwake na akawa hakumkubalia akalala hali amemkasirikia, Malaika watamlaani mpaka asubuhi.” (Muslim na Abu Dawud).

3) **Kulinda heshima ya mume na kuzichunga mali zake** na wanawe na mambo mengine ya nyumbani kwa kauli Yake Allah,

فَالصَّلَاةُ قُنُوتٌ حَفِظْتُمُ اللَّغَيْبِ بِمَا حَفِظَ اللَّهُ

“Basi wanawake wema ni wale wenye kutii na wanao jilinda hata katika siri kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameamrisha wajilinde...” (4:34)

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Na mwanamke ni mchungu katika nyumba ya mumewe.” (al-Qurtuby, Attabary).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Na haki yenu juu yao wanawake ni wasimruhusu yeyote mnayemchukia kukanyaga magodoro yenu wala wasimruhusu yeyote kuingia majumbani mwenu bila kupata idhini yenu.”

3) **Kubaki katika nyumba ya mumewe** asitoke isipokuwa kwa ruhusa ya mume na ridhaa yake. Kuinamisha macho yake, kuteremsha sauti yake, kuuzuiwia mkono wake usifanye maovu, ulimi wake kutoa maneno machafu na lugha mbaya. Kushirikiana na ndugu wa mume kwa wema ambao mume wake anaufanya kwao kwa sababu hatakuwa amemfanyia hisani mumewe anaye wafanyia ubaya wazazi wa mume huyo na ndugu zake.

وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَىٰ

“Na kaeni majumbani kwenu, wala msijishauwe kwa majishauwo ya kijahilia ya kizamani...” (33:33).

Na Kauli Yake:

إِنْ أَتَيْتُنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٣٤﴾

Minhajil Muslim

“...Kama mnamcha Mungu basi msiregeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema..” (33: 32).

Na kauli Yake Allah,

﴿ لَا تُحِبُّ اللَّهُ الْجَهْرَ بِالسُّوءِ مِنَ الْقَوْلِ إِلَّا مَنْ ظَلَمَ ﴾

“Mwenyezi Mungu hapendi uovu uenezwe kwa maneno ila kwa mwenye kudhulumiwa...” (4:148).

Na kauli Yake:

﴿ وَقُلْ لِلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ﴾

“Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao isipo kuwa unao dhihirika...” (24:31).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Mbora wa wake ni yule ambaye wewe mume wake ukimuangalia anakufurahisha, na ukimuamrisha anakutii, na ukiondoka anakutunzia nafsi yake (anajihifadhi) yeye na mali yako.” (al-Qurtwuby na Attabary).

Na kauli yake:

“Msiwazuwie wajakazi wa Allah kwenda kwenye misikiti ya Allah, mke wa mmoja wenu anaotaka ruhusa ya kwenda msitini msimzuie.” (Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Waruhusuni wanawake usiku kwenda misikitini.” (Muslim).

e) Adabu kwa Ndugu wa Karibu (wa damu).

Muislam kwa ndugu zake wa karibu anatakiwa awafanyie adabu kama zile anazozifanya kwa wazazi wake, wanae na ndugu zake. Kwa hiyo mama yake mdogo amfanyie kama anavyomfanyia mama yake mzazi na awafanyie adabu na haki zile zile anazozifanya kwa mwanawe na wazazi wake. Amheshimu mkubwa wao, na amhurumie mdogo wao, amzuru mgonjwa wao, amliwaze mwenye huzuni wao, ampe tanzia mfiwa wao, awapende hata kama hawamtaki. Awe mpole kwao hata kama watamfanyia ukatili na kumdhulumu. Haya yote ni kwenda pamoja na maana ya aya hizi Tukufu na Hadithi za Mtume ﷺ na Amesema Allah,

وَاتَّقُوا اللَّهَ

“Na muogopeni Allah...” (4:1).

Na Amesema,

وَأُولُوا الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ
وَالْمُهَاجِرِينَ

“...Na jamaa ni karibu wao kwa wao katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu kuliko Waumini wengine na Wahamiaji...”
(33:6).

فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِنْ تَوَلَّيْتُمْ أَنْ تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ ﴿٤٧﴾

“Basi yanayo tarajiwa kwenu mkitawala ndio mfididi katika nchi na mwatupe jamaa zenu?” (47:22).

Na Amesema Allah:

فَأْتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ لِلَّذِينَ
يُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ ۗ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٨١﴾

“Basi mpe jamaa haki yake, na masikini, na msafiri. Hayo ni kheri kwa watakapo radhi ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye kufanikiwa.” (30:38).

Na Amesema Mshindi na Mtukufu,

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَايَ ذِي الْقُرْبَىٰ ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani na kuwapa ndugu...” (16:90).

Na Amesema (Aliyetakasika):

﴿ وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۗ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ
وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ
بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ ﴾

“Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia...” (4:36).

Na kauli Yake:

وَإِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ أُولُو الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينُ فَأَرْزُقُوهُمْ مِنْهُ
وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٨﴾

“Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini, wapeni katika hayo mali ya urithi, na semeni nao maneno mema.” (4:8).

Na Mtume ﷺ amesema Allah anasema,

“Mimi ni Rahman na hii ni Rahim – yaani “undugu” – nimeutolea jina kutoka kwenye jina langu atayeunga udugu nitamuunga na atayekata udugu nitamkata” (Hadithul Qudsiy).

Aliuliza mmoja wa masahaba wa Mtume ﷺ: “Nani nimfanyie wema zaidi?” Akamjibu,

“Mama yako, kisha mama yako, kisha mama yako, kisha baba yako, kisha ndugu, kisha jamaa wa karibu.”

Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu matendo yanayomuingiza mtu peponi, na yanayomuepusha na moto. Akasema,

“Muabudu Allah na wala usimshirikishe na chochote na uunge undugu.” (Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi).

Na akasema kuhusu Mama mdogo na mama mkubwa,

“Yeye (mama mdogo) yupo katika ngazi ya Mama.” (Bukhari)

Na akasema,

“Kutoa Sadaka kwa maskini ni sadaka tu; lakini kwa ndugu ni sadaka na kuunga udugu.” (At-Tirmidhi, Ibn Majah, na Ahmad).

Na alimwambia Asmaa Binti Abubakar Swiddiqi رضى الله عنه alipomuuliza kuhusu kuendeleza udugu na mama yake aliomjia kutoka Makkah akiwa mshirikina, Mtume ﷺ akasema,

“Ndiyo endeleza udugu naye.”

1) Adabu (Heshima) kwa Jirani.

Muislamu anatambua kuwa anazo haki kwa jirani yake na adabu za kumfanyia. Kuna heshima na adabu ambazo majirani wawili kila mmoja analazimika kumfanyia mwenzake na kumpa haki zake zikiwa kamili na hayo ni kwa kauli yake Allah:

وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي
الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ

“...Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia...” (4:36).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Aliendelea Jibril kuniusia kuhusu jirani mpaka nikadhani kuwa atampa fungu katika mirathi.” (Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi).

Na kauli yake Mtume ﷺ pale aliposema:

“Anayemuamini Allah na Siku ya Mwisho basi amkirimu jirani yake.” (Muslim, Ahmad na Darimi).

1) Kutomuudhi Jirani kwa neno au kwa vitendo kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Anayemuamini Allah na Siku ya Mwisho asimuudhi jirani yake.” (Bukhari na Muslim).

Na Kauli Yake:

“Wallahi hawi Muumini kamili, wallahi hawi Muumini kamili.” Akaulizwa, “Nani huyo Ewe Mjumbe wa Allah?” Akasema, “Ambaye jirani yake hasalimiki na mabalaa yake.” (Bukhari, Imam Ahmad, Al-Hakim).

Na Kauli Yake,

“Huyo yuko motoni aliyoyasema hayo.” Kwa mwanamke aliyeambiwa kuwa mchana anafunga na usiku anaswali naanamuudhi jirani yake.” (Ahmad na Hakim.) Sanadi yake ni sahihi.

2) **Kumfanyia wema jirani**, kwa kumsaidia anapotaka msaada, kumzuru anapoumwa, kumpongeza anapofurahi, kumpa taazia anapofiwa, kumsaidia anapohitaji. Kumtolea salamu mnapokutana, na ampe maneno laini. Azungumze naye kwa upole na muelekeze kwenye kitu kilicho na maslahi kwake katika Dini yake na Dunia yake. Amuheshimu, amlinde, amsamehe makosa yake, asizipekuwe siri zake, asimbane katika kujenga au katika njia. Asimkere kwa kumuelekezea bomba au bati zinazoteremsha maji ya mvua kutoka paani au sakafuni kwake, au kwa kutupia uchafu mbele ya nyumba yake. Haya yote ni miongoni mwa hisani zilizoamrisha katika Kauli Yake Allah,

“Na jirani ndugu, na jirani asiye kuwa ndugu.”

Mtume ﷺ amesema:

“Mwenye kumuamini Allah na Siku ya Mwisho amfanyie hisani jirani yake.” (Darimyi).

3). **Kumkirimu jirani**. Kwa kumpatia misaada na kumfanyia wema. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Enyi wanawake wa Kiislamu jirani asimdharau jirani yake hata kama amepika kwato za mbuzi.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake kwa Abi Dharr:

“Éwe Abi Dhar ukipika mchuzi zidisha maji na muangalie jirani yako.” (Muslim).

Na kauli yake kwa Aisha رضي الله عنها alipomwambia, ‘Mimi nina majirani wawili yupi nimpe zawadi?’ Mtume ﷺ akamjibu,

“Yule ambaye mlango wake uko karibu nawe zaidi.” (Bukhari, Ahmad na Hakim).

4) **Kumheshimu**, asimzuie kuweka ubao wake au mti katika ukuta wake wala asiuze au kukodisha sehemu inayowaunganisha mpaka amwambie.

Mtume ﷺ amesema,

“Mmoja wenu asimzuwie jirani yake kuweka mti katika ukuta wake.” (Ahmad na Twabarani).

5) Kauli yake,

“Mwenye jirani kwenye shamba lake, mshirika asiliuze shamba hilo mpaka amtangazie.” (Hakim).

Faida Mbili:

Kwanza: Muislamu mwenyewe anatakiwa ajijue, kama atakuwa amefanya wema kwa jirani zake au amewafanyia ubaya. Kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa aliyemuuliza hilo,

“Kama ukiwasikia wanakusema kuwa umefanya wema basi jua kuwa umeufanya, na ukiwasikia wanakusema kuwa umefanya ubaya basi umeufanya.” (Ahmad kwa Sanad nzuri).

Pili: Muislamu kama atapatwa na mtihani wa kuwa na jirani mbaya basi amvumilie, subira yake, itakuwa ndio sababu ya kujikomboa. Alikuwa mtu mmoja kwa Mtume ﷺ kumshitakia kuhusu jirani yake akamwambia, “vumilia” akamwambia kwa mara ya tatu au ya nne vyombo vyako vitoe nje yaani njiani akavitoe njiani ikawa watu wanaopita hapo wanamuuliza: “Una nini?” Naye anawajibu jirani yangu ameninyanyasa. Wakawa wanamlaani jirani yake, mpaka yule jirani akamjia akasema,

“Rudisha vyombo vyako nyumbani kwako wallahi mimi sitarudia tena”. (Abu Dawud).

g) **Adabu** (Heshima) za Muslamu na Haki Zake:

Muislamu anatambua haki ya ndugu yake Muislamu na adabu zinazomlazimu amfanyie. Kwa hiyo anazitekeleza huku akiwa anaamini kuwa anachokifanya ni Ibada mbele ya Allah, na kikutubisha kinachomkurubisha kwa Allah. Kwa sababu haki hizi na adabu hizi amezilazimisha Allah juu ya Muislamu amfanyie ndugu yake Muislamu. Kwa hiyo kuzitekeleza ni Ibada –kutii – kwa Allah na bila ya shaka ni kujisogeza kwa Allah. Miongoni mwa haki na adabu hizo ni haya yafuatayo:-

1) **Amtolee Salam** kila anapokutana naye kabla hajazungumza naye aseme: “*Asa-salaam alaikum warahmatul-laai Wabarakatuhu*” Hayo ni kwa kauli Yake Allah Aliyetukuka: “***Kama mtaamkiwa kwa “salam”- jibuni kwa salaam nzuri kuliko hiyo au kama hiyo.***”

Na kauli Yake Mtume ﷺ,

“*Aliyepanda atamsalimia anayetembea kwa miguu, naye atamsalimu aliyekaa, na wachache watawasalimia wengi.*” (Bukhari, Muslim, Abu Dawud, na At-Tirmidhi).

Na kauli yake,

“*Hakika ya Malaika wanashangaa Muislamu anampita Muislamu mwenzake bila kumtolea salamu.*” (Bukhari, Muslim).

Na kauli yake:

“*Hakuna Waislamu wawili wataokutana wakapeana mikono isipokuwa watasamehewa kabla hawajaachana.*” (Daud, Ibn Majah, At-Tirmidhi).

Mtume ﷺ amesema:


“*Atakayeanza mazungumzo kabla ya salam msimjibu mpaka anze kwa kutoa salaam.*” (Attabarani).


2) **Amuombee dua akipiga chafya**, amwambie kama atasema ‘*Alhamdulillah*’ ‘*yarhamukallahu*’ mwenda chafya naye atajibu kwa kusema: ‘*Yaghfirul-laahu laahu laka*, au *Yahdykumu AI-laahu wa Yuslih Baalakum*.’

Kwa kauli yake Mtume .

“*Apigapo chafya mmoja wenu mwenzake amwambie: Yarhamukal-laahu, Nae amwambie: Yahdykumullahu wa-Yuslih Baalakum*, (Bukhari).


Abu Huraira  amesema,

“*Mtume  alikuwa anapopiga chafya anaweka mkono wake au nguo yake juu ya kinywa chake na anateremsha sauti yake.*” (Abu Dawud, Imam Ahmad, Al-Hakim).

3) **Akampe Pole anapoumwa, na amwuombee dua ya kupona kwa kauli yake** Mtume .

“*Haki za Muislamu juu ya Muislamu ni Tano, Kujibu salam, kumzuru mgonjwa, kufuata janeza, kuitika mwaliko, kumuombea dua aliyepiga chafya.*” (Bukhari, Muslim na Ahmad).


Na kwa Kauli Yake Barra-Ibni Azib .

“*Mtume  ametuamuru kuwaona wagonjwa, na kusindikiza janeza, kumuombea dua aliyepiga chafya na kumfanyia wema aliyepiga kiapo kumsaidia mdhulumiwa, kuitika mwaliko na kueneza salam:* (Bukhari).

Na Kauli Yake Mtume .

“*Mtembeleeni mgonjwa, mlisheni mwenye njaa, na mkomboeni mateka*” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake Aisha .

“*Hakika Mtume  alikuwa anawatembelea baadhi ya familia yake na anawapangusa kwa mkono wake wa kuume, na*

anasema: “Ewe Mola wangu, Bwana wa watu, ondoa ubaya na uwaponye, Wewe ndie Mponyaji hakuna uponyo isipokuwa kutoka kwako, Uponyo usio acha ugonjwa.” (Abu Dawud na Imam Ahmad).

4) Anapofariki afike katika mazishi yake kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Haki za Muislamu juu ya Muislamu ni Tano. Kujibu salaam, kutembelea wagonjwa, kufuata jeneza, kuitika mwaliko, na kumuomba dua aliyepiga chafya.”

5) Kuamini kiapo chake kama atamuapia katika kitu ikiwa hamna uharamu, akifanye alichokiapia ili asije akaivunja yamini yake, na hayo kwa Hadithi ya *Barray Ibni Aazib:*

“Mtume ﷺ ametuamuru kutembelea wagonjwa, kufuata jeneza, Kumuomba dua anayepiga chafya, kuamini kiapo, kumsaidia Anayedhulumiwa na kueneza salaam.”

6) Amnasihi anapomtaka nasaha katika kitu au jambo miongoni mwa mambo, kwa maana ya kumueleza anachokiona kinafaa, au jambo analoliona kuwa ni sahihi na hayo ni kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Mmoja wenu anapomtaka nasaha ndugu yake amnasihi.”
(Bukhari).

Na kauli yake:

“Dini ni nasaha” Akaulizwa kwa nani? Akasema, “Kwa Allah, Kitabu chake, Mtume wake na viongozi wa Waislamu, na Waislamu wote.” (Muslim na Bukhari). Bila shaka Muislamu ni miongoni mwao.

7) Ampendeleee kwa anachokipendelea katika nafsi yake kwa kauli yake Mtume ﷺ

Minhajil Muslim

“Hawi Muumini kamili mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake kwa kinachopendelewa na nafsi yake, na achukie kwa ndugu yake kile anachokichukia kwa nafsi yake.” (Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi).

Kauli yake Mtume ﷺ,

“Mfano wa waumini katika kupendana kwao, kuhurumiana kwao na upole baina yao ni sawa na mwili mmoja kinapoumwa kiungo huathirika sehemu zote za mwili zilizosalia kwa kukesha na homa.” (Muslim na Imam Ahmad).

Na kauli yake:

“Muislamu kwa Muislamu mwenzake ni kama jengo lililoshikamana, lashirikiana lenyewe kwa lenyewe.” (Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi).

8) Amnusuru na asimtelekeze popote anapohitaji msaada wake, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Msaidie Ndugu yako akiwa dhalimu au akiwa amedhulumiwa.” Akaulizwa namna ya kumsaidia dhalimu. Akajibu, “Umzuwie asifanye dhulma, huko ndiko kumsaidia kwake.” (Bukhari na Muslim).

Na Mtume ﷺ amesema:

“Muislamu ni Ndugu wa Muislamu, Hamdhulumu wala Hamtelekezi na wala Hamdharau.” (Bukhari na At-Tirmidhi).


Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakuna mtu atakayemsaidia Muislamu mwenzake mahala inapovunjwa heshima yake, na kuondolewa hadhi yake isipokuwa Allah atamnusuru mahala anapopenda atakapokuwa anauhitaji msaada Wake. Na hakuna Muislamu atayemtelekeza Muislamu

mahala anapovunjiwa heshima yake isipokuwa Allah atamtelekeza mahali ambapo anahitaji kusaidiwa.” (Ahmad).

Na kauli yake,

“Mwenye kuilinda heshima ya ndugu yake, Allah atamlinda uso wake na moto.” (At-Tirmidhi na Imam Ahmad).

9) Asimdhuru, au kumfanyia karaha, na hayo ni kwa kauli yake Mtume ,

“Kila Muislamu ni haramu juu ya Muislamu mwenzake Damu yake, Mali yake, na heshima yake.” (Muslim).

Na Kauli Yake Mtume ,

“Si halali kwa Musilamu kumtisha Muislamu mwenzake.” (Ahmad, Abu Dawud).

Na kauli yake:

“Si halali kwa Muislamu kumuelekezea ndugu yake angalio la kumuudhi” (Ahmad).

Na Kauli Yake:

“Allah anachukia kuwafanyia maudhi waumini.” (Ahmad).

Na Kauli Yake:

“Muumini kamili ni yule ambaye wanasalimika Waislamu wenzake na ulimi wake na mkono wake.” (Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi).

Na kauli yake:

“Muumini kamili ni yule ambaye Waumini wamesalimika naye katika nafsi zao na mali zao.” (Ahmad na Tirmidh).

10) Amnyenyekee wala asimfanyie kiburi na wala asimuinue kama amekaa katika nafasi yake halali ili akaye yeye, kwa kauli Yake:

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ
كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٣١﴾

“Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha.” (31:18).

Na kwa Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Hakika Allah ameniletea wahyi kuwa nyenyekeaneni mpaka mtu asijifakhiri juu ya mwengine.” (Abu Dawud, Ibnu Majah).

Na Mtume ﷺ amesema,

“Hakuna aliyenyenyekea kwa Allah isipokuwa Allah atamnyanyua.” (Ibnu Majah na Hakim)

Na kutokana na sifa yake Mtume ﷺ aliyoeleweka nayo ambayo ni unyenyekevu kwa kila Muislamu wakati yeye ni Bwana wa Mitume, alikuwa hanyanyapai, wala kuwa na kiburi katika kufuatana na mjane au maskini na wote hao alikuwa anawatekelezea mahitaji yao. Naye amesema,

“Ewe Mola wangu nihuishe nikiwa maskini, unifishe nikiwa maskini, na unifufue katika kundi la maskini.” (Ibnu Majah, Hakim).

Na Mtume ﷺ amesema,

“Asimuinue mmoja wenu mwenzake alipokaa kisha akakaa yeye hapo, lakini panueni nafasi.” (Muslim na Imam Ahmad).

11) Wasiasiane kwa zaidi ya siku tatu, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Si halali kwa Muislamu kumhama ndugu yake zaidi ya siku tatu, wanakutana huyu anampa mgongo huyu na huyu anampa mgongo huyu na mbora wao ni yule atakayeanza kumtolea salamu mwenzake.” (Bukhari, Muslim, Abu Dawud).

Na Kauli Yake:

“Na msipeane mgongo na kuweni ndugu waja wa Allah.”
(Muslim).

Na kupeana migongo ndiko kuhasiana na kumpa kila mmoja mgongo wake kwa kumpuuza.

12) Asimsengenyeye, au kumdharau au kumtia kasoro, au kumfanyia masihara au kumwita kwa jina la kejeli, jina baya, au kumpelekea usengenyi ili kumharibia, haya ni kwa kauli Yake Allah:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ ۖ وَلَا
تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَب بَّعْضُكُم بَعْضًا ۚ أَنُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ
مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ ﴿٤٩﴾

“Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anaye penda kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.” (49:12).

Na kauli Yake:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّن قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا
نِسَاءٌ مِّن نِّسَاءٍ عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۗ وَلَا تَلْمِزُوا أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَرُوا
بِالْأَلْقَابِ ۗ بِئْسَ الْإِسْمُ الْفُسُوقُ بَعْدَ الْإِيمَانِ ۚ وَمَن لَّمْ يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ
الظَّالِمُونَ ﴿٥٠﴾

“Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu.” (49:11).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Mnajua nini usengenyi?” Wakasema, “Allah na Mtume wake ndio wanaojua.” Akasema: “Kumtaja ndugu yako kwa anachochukia.” Akauliza: “Unaonaje kama ninachokisema anacho kweli huyo ndugu yangu?” Akasema: “Kama atakuwa nacho ndiyo umemsengenya, na kama hana basi umemzushia.” (Muslim).

Na kauli yake katika Hija ya kuaga (*Hijatul Wadai*),

“Hakika damu zenu, mali zenu na heshima zenu ni Haramu juu yenu.” (Muslim).

Na kauli yake,

“Kila Muislamu kwa Muislamu mwenzake ni haramu damu yake, mali yake na heshima yake.” (Muslim).

Na kauli yake,

“Yatosha kwa mtu kuitwa mbaya kwa kufanya tendo la kumdharau ndugu yake Muislamu.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake.

“Haingii Peponi mchochezi.”

13) Asimtukane bila ya haki, awe hai au amekufa, kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Mtu hamshutumu mwengine kwa tusi la ufasiki na ukafiri isipokuwa litarudi kwake tusi lile kama mshutumiwa atakuwa

hana sifa hiyo. “Watu wawili wakitukanana makosa ni kwa aliyeanza mpaka yule wa pili atapojibu kwa lugha ya matusi.” (Imam Ahmad).

Amesema,

“Kumtukana Muislamu ni ufasiki na kupigana naye ni ukafiri.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake:

“Msiwatukane waliokufa hakika hao wamekwishafika na kukutana na matendo yao.” (Bukhari, Annasaai, na al-Hakima).

Na Kauli Yake:

“Miongoni mwa madhambi makubwa ni mtu kuwatukana wazazi wake wawili.” Pakaulizwa hivi kuna mtu anayewatukana wazazi wake wawili?!”. Akasema: “Ndio, mtu anamtukana mzazi wa mwengine naye anamtukana baba yake, na anamtukana mama yake.” (Muslim).

14) Asimfanyie husda, au kumdhania vibaya, au kumbughudhi, au kumchunguza, kwa Kauli Yake Allah:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ وَلَا
تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَب بَّعْضُكُم بَعْضًا

“Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi...” (49:12).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Msifanyiane husuda, msibughudhiane, msichunguzane, na wala msipandishiane bei katika minada, na kuweni ndugu enyi waja wa Allah.” (Muslim).

Na Kauli Yake:

“Jihadharini na jiepusheni na dhana, hakika ya dhana ni maneno ya urongo mno.” (Bukhari).

15) Asimdanganye au kumhadaa, kwa Kauli Yake Allah:

وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ بَغَيْرِ مَا كَتَبْنَا لَهُمْ فَقَدِ احْتَمَلُوا
بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿٣٣﴾

“Na wale wanao waudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote, bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhaahiri.” (33:58).

Na Kauli Yake:

وَمَنْ يَكْسِبْ خَطِيئَةً أَوْ إِثْمًا ثُمَّ يَرْمِ بِهِ بَرِيئًا فَقَدِ احْتَمَلَ بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُّبِينًا

“Na atendaye kosa au dhambi kisha akamsingizia asiye na kosa, basi amejitwika dhulma na dhambi iliyo wazi..” (4:112).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Mwenye kutubebea silaha ili kutupiga, na aliyetudanganya si miongoni mwetu.” (Muslim).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Hakuna mja yeyote anayepewa na Allah jukumu la kuchunga Raia akafa siku atayokufa hali amewahadaa raia zake, isipokuwa Allah ameharamisha pepo kwake.” (Muslim na Darimi).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kumhadaa mke wa mtu au mtumwa wake si miongoni mwetu.” (AbuDaud).

16) Asimfanyie Khiana, au kumuongopea, kumcheleweshea kumlipa deni lake kwa Kauli Yake Allah:

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اَوْفُوْا بِالْعُقُوْدِ

“Enyi mlio amini! Timizeni ahadi...” (5:01).

Na Kauli Yake

وَالْمُؤْفُوْنَ بِعَهْدِهِمْ اِذَا عٰهَدُوْا

“...na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi...” (2:177).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Mambo manne kama yatapatikana kwa mtu, amekuwa munafiki hasa, na atayekuwa na moja ya hayo atakuwa na sehemu ya unafiki mpaka atakapoyaacha, anapoaminiwa anauvunja uaminifu, na anapozungumza anaongopa, na anapohidi anavunja ahadi, na anapogombana anakuwa jeuri.” (Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi).

Na Kauli Yake Allah Amesema:

“Watatu mimi ngomvi wao siku ya kiyama: Mtu ametoa kauli kwa ajili Yangu kisha akafanya khiana, na mtu amemuuzua muungwana kisha akala thamani yake, na mtu amemuajiri mtumishi naye akatimiza kazi yake kisha asimpe malipo yake.” (Ibn Majah).

Na Kauli Yake:

“Ucheleweshaji wa kulipa deni kwa mtu mwenye uwezo ni dhulma, anapohamishiwa mmoja wenu deni lake kwa mwenye uwezo basi akubali.” (Bukhari, Muslim, Abu Dawud na At-Tirmidhi).

17) Aishi naye kwa tabia nzuri, amfanyie wema asimfanye kero, akutane naye kwa uso wa furaha, aipokee hisani yake amsamehe makosa yake. Asimlazimishe kwa asichokuwa nacho, asitake Elimu kwa mtu mjinga, wala ufasaha kwa asiyeweza kusema, kwa Kauli Yake Aliyetukuka:

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿١٩٩﴾

“Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili.” (7:199).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Mche Allah popote ulipo na lifatishie ovu kwa jema litalifuta ovu, na ishi na watu kwa tabia nzuri.” (Hakim na At-Tirmidhi).

18) Kama ni mkubwa amuheshimu, na kama ni mdogo amuhurumie, kwa Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Si miongoni mwetu mdogo asiye mheshimu mkubwa, na mkubwa asiye muhurumia mdogo..” (Ahmad).

Na Kauli Yake:

“Mtangulize mkubwa.”

Na Kauli Yake:

“Katika kumtukuza Allah ni kumheshimu mwenye mvi Muislamu.” (Abu Dawud).

Na imefahamika kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alikuwa analetewa mtoto mdogo ili amuombe Baraka na kumpa jina. Mtume ﷺ anamuweka mtoto yule mapajani kwake, na mara nyingine mtoto anakojoa akiwa mapajani kwake. Imepokewa kuwa alikuwa Mtume anaporudi toka safarini watoto humkimbia. Ili kumlaki anasimama kwa ajili yao. Na anaamuru wengine wanapelekwa pale alipo basi wengine anawaweka mbele yake na wengine nyuma, na anawaamuru masahaba zake wawabebe baadhi yao. Hiyo ikiwa ni miongoni mwa huruma zake Mtume ﷺ kwa watoto.

19) Amfanyie uadilifu, na amtendee kile anachopenda kutendewa, kwa Kauli Yake Mtume ﷺ.

“Imani ya mja haikamiliki mpaka awe na mambo matatu: Kutoa pamoja na ufinyu wa pato lake, kuwa muadilifu na nafsi yake, na kutoa salam.” (Bukhari).

Na Kauli Yake:

“Anayefurahia kuepushwa na moto na akaingia peponi basi afe huku anashuhudia kuwa hakuna Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah, na Muhammad ni Mtume Wake na Mjumbe Wake, na awafanyie watu anachopenda kufanyiwa.” (Ibn Majah).

20) Ayasamehe makosa yake, amsitiri aibu yake, asitake kuyajua mambo yake ya siri, kwa Kauli Yake Allah:

فَاعْفُ عَنْهُمْ وَأَصْفَحْ إِنَّ اللَّهَ تَحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥١﴾

“...Basi wasamehe na waache. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.” (5:13).

Na Kauli Yake,

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۗ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ﴿٤٠﴾

“...Lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu...” (42:40).

Na Kauli Yake:

وَلْيَعْفُوا وَلْيَصْفَحُوا أَلَا تُحِبُّونَ أَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٢﴾

“...Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni?...” (24: 22).

Na Kauli Yake:

إِنَّ الَّذِينَ يُحِبُّونَ أَنْ تَشِيعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِينَ ءَامَنُوا لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ فِي
الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢٤﴾

“Kwa hakika wale wanao penda uenee uchafu kwa walio amini, watapata adhabu chungu katika dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui...” (24:19).

Na kwa Kauli ya Mtume ﷺ,

“Allah hamuongezei mja anayesamehe isipokuwa utukufu.”
(Muslim)

Na Kauli Yake:

“Na kumsamehe aliyekudhulumu.” (Muslim).

Na Kauli Yake:

“Mja humuhifadhi mja mwenzake Duniani isipokuwa Allah atamuhifadhi Siku ya Kiama.” (Musim).

Na kauli yake:

“Enyi mlioamini kwa ulimi na wala imani haikuingia nyoyoni mwenu msiwasengenye Waislamu na msizipekue aibu zao, na mwenye kuipekua aibu ya ndugu yake, atamfedhehesha, atamfichulia aibu yake na atamfedhehesha hata kama alikuwa ndani ya nyumba yake.” (Abu Dawud).

Na Kauli Yake:

“Mwenye kuzisikiliza habari za watu na wenyewe hawapendi itamiminwa ndani ya sikio lake risasi Siku ya Kiyama.” (Bukhari).

21) Amsaidie kama atamuomba msaada, amuombee mafanikio katika kutekeleza mahitaji yake kama ataweza, na hayo ni kwa kauli Yake Allah,

مَنْ يَشْفَعْ شَفَاعَةً حَسَنَةً يَكُنْ لَهُ نَصِيبٌ مِنْهَا

“Mwenye kuombea (wenzake) ombi zuri naye atapata hisa katika hilo.” (5:2).

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَى

“...Na saidianeni katika wema na uchamngu...” (5:2).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Mwenye kumuondolea Muislamu tatizo katika matatizo ya Duniani, Allah atamuondolea tatizo katika matatizo ya Siku ya Kiyama, na mwenye kumsaidia maskini Allah atamsaidia Duniani na Akhera, na Allah yuko kumsaidia mja kwa muda wa kuwa mja anamsaidia ndugu yake.” (Muslim).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Ombeni mtalipwa.” (Bukhari, An-Nasai na Ahmad).

Na, *“Allah anatekeleza kupitia kwa Mtume wake anachokitaka.”*
(Hakim na An-Nasai).

22) Amlinde anapomuomba ulinzi kwa ajili ya Allah, na ampe anapomuomba kwa jina la Allah, na amlipe kwa wema aliomfanyia na amuombee dua, yote hayo ni kwa Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Anayewatakeni ulinzi kwa ajili ya Allah mlindeni, na anayewaombeni kwa ajili ya Allah mpeni, na mwenye kuwaita itikeni, na anayewafanyia wema mlipeni, na msipopata cha kumlipa muombeni dua mpaka muone kuwa mmemlipa.” (Abu Dawud, Ahmad na Hakim)

h) Kumheshimu Kafiri.

Muislamu anaamini kuwa Dini zengine ni Batili na kwamba wenye dini hizo ni makafiri isipokuwa Dini ya Kiislamu. Hiyo ndio Dini ya haki, na wafuasi wa Dini hiyo hao ndio Waumini Waislamu, kwa Kauli Yake Allah,

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ^٤

“Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu....”
(3:19).

Na Kauli Yake:

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٨٥﴾

“Anayetafuta dini isiyokuwa Uislamu hatokubaliwa naye Akhera ni miongoni mwa wenye kupata khasara.” (3:85).

Na Kauli Yake:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا^٥

“...Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni uislamu uwe ndiyo Dini...” (5:3).

Kwa habari hizi za kweli zitokazo kwa Allah, Muislamu ameelewa kuwa Dini zingine zilizokuja kabla ya Uislamu zimefutwa na Uislamu. Kwamba Uislamu ndiyo Dini ya Binadamu wote. Allah hakubali dini nyingine, na wala haijui sheria isiyokuwa hiyo na kwa sababu hii Muislamu anaona kuwa yoyote atakayemuabudu Allah kwa dini isiyokuwa ya Kiislamu ni kafiri, na Muislamu anatakiwa kumfanyia kafiri adabu (heshima) zifuatazo:-

1) **Kutokumkubalia ukafiri wake**, na kutouridhia, kwani kuuridhia ukafiri ni ukafiri.

2) Kumchukia kwa vile Allah amemchukia. Kwa sababu kupenda ni kwa ajili ya Allah na kuchukia ni kwa ajili ya Allah na kwa muda wa kuwa Allah amemchukia kwa ajili ya kumkataa basi Muislamu naye anamchukia kwa kuchukiwa na Allah.

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ^ط

“Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anaye fanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu...” (3:28).

Na Kauli Yake:

لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ
اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ
عَشِيرَتَهُمْ^ع

“Hautawaona watu wanaomuamini Allah na Siku ya Mwisho wanawafanyia mapenzi wanaompinga Allah na Mtume wake, hata kama watakuwa ni Baba zao au ndugu zao au jamaa zao.” (50:22).

4) Kuwa muadilifu na kafiri, na kumfanyia wema kama hafanyi uadui, kwa Kauli Yake Allah:

لَا يَنْهَكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِنْ دِيَارِكُمْ أَنْ
تَبْرَهُمْ وَتُقَسِّطُوا إِلَيْهِمْ^ع إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٨﴾

“Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.” (60:8).

Aya hii tukufu imeruhusu kuwafanyia uadilifu makafiri, na kuwafanyia wema na haikuwavua makafikiri isipokuwa wanaowapiga vita Waislamu tu. Kwani hao wana utaratibu maalum unajulikana katika hukumu za makafiri wa kivita.

5) **Anamuhurumia (kafiri) kwa huruma za kawaida**, kama kumpa chakula akiwa ana njaa, na kumpa maji kama ana kiu, kumtibu kama ataumwa, nia kama vile kumuokoa katika halaki na matatizo, na kutomfanyia kero, kwa Kauli Yake Mtume ﷺ.

“Muhurumie aliye ardhini atakuhurumia aliye mbinguni.” (Twabarani).

Na Kauli Yake:

“Kukihurumia kila kiumbe chenye ini bichi (yaani chenye uhai) unapata malipo.” (Bukhari, Abu Dawud na Ibn Majah).

6). **Kutomnyanyasa katika mali yake au Damu yake au heshima yake** kama si kafiri wa vita kwa Kauli Yake Allah Aliyetukuka katika hadithi Qudsi,

“Enyi waja zangu mimi nimeharamisha dhulma juu ya nafsi yangu, na nimeifanya kati yenu kuwa ni haramu, basi msidhulumiane.” (At-Tirmidhi).

Na Kauli Yake:

“Mwenye kumnyanyasa dhimmiyya mimi ni ngomvi wake Siku ya Kiyama.”

7) Inaruhusiwa kumpelekea zawadi na kuipokea zawadi yake, kula chakula chake kama atakuwa Yahudi au Mkristo kwa Kauli Yake:

وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَلَالٌ لَكُمْ وَطَعَامُكُمْ حَلَالٌ لَهُمْ

“...Na chakula cha walio pewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao...” (5:5).

Na kwa habari sahihi kutoka kwa Mtume ﷺ:

“Kuwa yeye alikuwa anapelekewa mwaliko wa chakula kwa Mayahudi Madina, na anaupokea na anakula kilicho mbele yake miongoni mwa vyakula vyao.”

8) **Hafai kuoreshwa mwanamke Muislamu**, na inaruhusiwa kuwaoa wanawake wa *Ahlul Kitab* katika makafiri kwa Kauli Yake Allah Aliyetukuka alipokuwa anamzuia mwanamke Muislamu kuolewa na kafiri yeyote awavyo,

لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ

“...Wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalalikii wanawake Waumini...” (60:10).

Na Kauli Yake:

وَلَا تَنْكِحُوا الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ يُؤْمِنَ

“...Wala msiwaoze (binti zenu) wanaume washirikina mpaka waamini...” (2:221).

Na Amesema katika kuruhusu ndoa ya Muislamu kumuoa mwanamke Kitabiyyah:

وَالْحَصْنَةُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْحَصْنَةُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا

ءَاتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ مُحْصِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ وَلَا مُتَّخِذِي أَخْدَانٍ

“...Na pia wanawake wema miongoni mwa Waumini, na wanawake wema miongoni mwa walio pewa Kitabu kabla yenu, mtakapo wapa mahari yao, mkafunga nao ndoa, bila ya kufanya uasherati wala kuwaweka kinyumba...” (5:5).

9) **Kumuomba dua kama atatoa chafya** na akamshukuru Allah Aliyetukuka amwambie, *“Yarhamukumul-Laahu wa Yuslihu Balakum.”* Kwa sababu Mtume ﷺ Mayahudi walikuwa wakitoa chafya mbele yake wakitaraji atawaambia: *“Yarhamukumul-Laahu, akawa anasema, “Yahdykumu-Laahu wa Yaslihu Balakum.”*

Minhajil Muslim

10) Asianze kuwatolea salamu, na kama atamtolea salamu atamjibu kwa neno lake, “*Wa-Alaikum*”. Kwa Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Kama watawatolea saalamu Ahlu Kitabi semeni: ‘Walaikum’.
(At-Tirmidhi na Ibn Majah).

11) Anapompitia njiani asimpishe apite pembeni ya njia kwa Kauli Yake Mtume ﷺ

“Msianze kuwatolea salamu Mayahudi wala Wakisto, na kama mtakutana na mmoja wao njiani mbaneni ili alazimike kupita pembeni.” (Muslim na Abu Dawud).

12) **Kutofatiana naye na kutojifananisha naye:** katika yale yasiyokuwa ya lazima kama vile kufuga ndevu kama yeye ananyoa, na kuzitia rangi ikiwa yeye hatii, pia kutofautiana naye katika mavazi. Kama vile kirembo, kofia na mfano wake, kwa Kauli Yake Mtume ﷺ

“Anayejifaninisha na watu fulani basi naye ni miongoni mwao.”
(Abu Dawud na Ahmad).

Na Kauli Yake,

“Jitofautisheni na Mushirikina, fugeni ndevu na kateni sharubu.”
(Bukhari na Muslim).

Na Kauli Yake,

“Mayahudi na Wakristo hawatii rangi, tofautianeni nao.”
(Bukhari na Muslim)

Yaani kutia rangi ndevu au nywele za kichwa kwa rangi ya njano au nyekundu, kwa sababu kutia rangi nyeusi amekataza Mtume ﷺ kwa Hadithi aliyoipokea Muslim. Mtume ﷺ amesema,

“Badilisheni nywele hizi nyeupe na jiepusheni na rangi nyeusi.”

g) Kuwahurumia Wanyama

Muislamu anazingatia kuwa sehemu kubwa ya wanyama ni viumbe wenye kuheshimiwa, kwa hiyo anawahurumia kwa ajili ya Allah, na kwa kuzingatia haya atawafanyia wanyama yafuatayo:-

1) **Kumpa chakula na maji** kama atakuwa na njaa na kiu, kwa Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Wahurumieni walio ardhini atawahurumia aliye mbinguni.”
(Baihaqi).

Na Kauli Yake:

“Katika kukihurumia kila kilicho na roho kuna malipo.”

Na Kauli Yake:

“Asiye na huruma hahurumiwi.” (Bukhari).

2) **Kuwahurumia na kuwafanyia upole:** kwa Kauli Yake Mtume ﷺ Mtukufu alipowaona ndege wanalengwa Shabaha na,

“Wanawalenga kwa mishale yao. “Allah amemlani mwenye kukifanya Shabaha kilicho na roho.” (Bukhari na Muslim).

Na katazo lake Mtume ﷺ la kuwafungia, kwa kauli yake,

“Nani aliyempa machungu huyu ndege kwa kumchukuwa mwanawe.” Ameyasema hayo alipomuona ndege anazunguka anatafuta vifaranga vyake waliochukuliwa na Maswahaba kutoka kwenye kiota chao.” (Abu Dawud).

3) **Kuwapumzisha wakati wa kuwachinja au kuwaua,** kwa Kauli Yake Mtume ﷺ,

“Hakika Allah ameandika hisani (wema) juu ya kila kitu, hivyo mnapoua ueni vizuri, na mnapochinja chinjeni vizuri, na

ampumzishhe mmoja wenu mnyama wake anayemchinja, na akinoe kisu chake.” (Muslim)

4) **Kutomuadhibu mnyama kwa aina yoyote ya adhabu**, ama kwa kumuacha na njaa au kumpiga, au kumbebesha asichokiweza, au kwa kumkatakata au kumchoma moto, na hayo yanatokana na kauli yake Mtume ﷺ,

“Mwanamke ameingia motoni kwa sababu ya paka aliyemfunga mpaka akafa, akaingia motoni kwa sababu ya paka huyo kwani hakumpa chakula wala maji wakati alipomfunga wala hakumwachia ale vijidudu vya ardhini.” (Bukhari na Muslim).

Mtume ﷺ alipita katika kijiji chenye wadudu chungu kimechomwa moto akasema,

“Sisi hatupendi kuona mtu anaadhibiwa kwa moto isipokuwa bwana wa moto (anakusudia Allah kwani yeye Pekee ndio Mwenye haki hiyo).” (Abu Dawud).

5) **Uhalali wa kumuua mnyama mwenye madhara kwa watu** kama vile mbwa mwenye kichaa, mbwa mwitu, nyoka, nge, kunguru, panya na mfano wake na hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Wadudu wabaya watano wauliwe hata kama ni katika iliyoruhusiwa au iliyokatazwa nao ni: Nyoka, kunguru mwenye doa, panya, mbwa mwenye kichaa na mwewe.” (Muslim).

Kama ilivyothibiti kwa hadithi swahihi kuwa ni ruhusa kumuua n’nge na pia kumlaani.

6) **Ruhusa ya Kuwaweka Alama Mbuji** masikioni kwa maslahi, kwani alionekana Mtume akiwatia alama ngamia wa sadaka masikioni kwa mkono wake. Ama wasiokuwa mbuzi miongoni mwa wanyama wengine hairuhusiwi kuwaweka alama, kwa neno lake Mtume ﷺ alipomuona punda amewekwa alama usoni,

“Allah amlaani aliyemuweka alama huyu usoni mwake” (Muslim)

7) **Kuelewa haki ya Allah** katika wanyama kwa kutoa zaka ya wanyama katika wanyama wanaotolewa zaka.

8) **Kushughulikia wanyama tu** na kusahau kumuabudu Allah, kucheza nao na kuacha kumtaja Allah kwa Kauli Yake Allah:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ أَمْوَالُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ

“Enyi mlia amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu...” (63:9).

Na kwa Kauli Yake Mtume ﷺ katika farasi:

“Farasi wako wa aina tatu:- Kwa mtu ni malipo, kwa mtu ni stara, kwa mtu ni dhambi. Ama ambaye anapata malipo ni mtu amemfunga Farasi wake katika njia ya Allah akampatia malisho kwa muda mrefu, kwa hiyo alilipa katika kipindi hicho katika malisho Bustani, kwake ni wema, na kama ataufupisha muda wake akaenda mbio mara moja au mbili athari zake alipopita au choo chake, kwake ni wema, na Farasi huyo kwa huyo mtu ni malipo na thawabu. Na mtu mengine amemfunga kwa vile hana haja naye na akawa hakuisahau haki ya Allah katika shingo zao na migongo yao, wanyama hao kwake ni stara. Na mtu mwengine amewafunga kwa ajili ya fakhari na ria na akalikusudia hilo, basi wanyama hao kwake ni dhambi.” (Muslim).

Huu ndio muhtasari wa adabu anazozichunga Muislamu kwa wanyama kwa ajili ya kumtii Allah na Mtume wake, na kuyatumia yanayoamrisha na sheria ya Uislamu, sheria yenye Rahma, Sheria yenye kheri kwa kila kiumbe au mwanadamu au mnyama.



Mada ya Saba

Adabu za Udugu kwa Ajili ya Allah na Kupenda au Kuchukia kwa Ajili Yake

Muislamu kulingana na Imani yake kwa Allah anapenda kitu hakipendi isipokuwa kwa ajili ya Allah, na hachukii kitu anapokichukia isipokuwa kwa ajili ya Allah. Kwa hiyo yeye anapenda na kuchukia kwa ajili Yake. Ushahidi wa haya ni Kauli yake Mtume ﷺ.

“Anayependa kwa ajili ya Allah na akachukia kwa Ajili ya Allah, na akatoa kwa ajili ya Allah, na Akazuwia kwa ajili ya Allah basi amekamilika Imani.” (Abu-Daud).

Kwa kuzingatia haya Muislamu anawapenda waja wema wote wa Allah na anawafanya marafiki, na wote wanaoacha kutekeleza amri ya Allah na Mtume wake anawachukia hawafanyi marafiki. Isipokuwa hili halimzuwii Muislamu kuwa na marafiki na ndugu atakaowapa mapenzi ya ziada, kwa sababu Mtume ﷺ amehimiza kuwapenda na kuwafanya marafiki hawa ndugu kwa kauli yake,

“Muumini wa kweli ni yule mwenye kuzoeleka, na hakuna kheri kwa asiyezowea na kuzoweleka.” (Ahmad, Twabarani, Hakim).

Na kauli yake:

“Pembazoni mwa ardhi kuna mimbari za nuru, juu yake kuna watu, Vazi lao ni Nuru na nyuso zao ni za Nuru, si Mitume wala si mashahidi. Mitume na Mashahidi wanawaonea wivu watu hao watauliza: “Tuelezee sifa za watu hao ewe Mtume wa Allah ﷺ.” akasema, “Watu hao ni wale wenye kupendana kwa ajili ya Allah, wanaokaa pamoja kwa ajili ya Allah, na wanatembeleana kwa Ajili ya Allah.” (Muslim).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Hakika Allah Anasema: “Yamethibiti Mapenzi Yangu kwa wale ambao wanatembeleana kwa ajili Yangu, na limethibiti penzi langu kwa wale wanaosaidiana kwa ajili Yangu.” (Ahmad).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Watu wa aina saba atawafunika Allah katika kivuli chake: Siku ambayo hakutakuwa na kivuli ila kivuli chake nao ni Imamu muadilifu, kijana aliyekulia katika Ibada ya kumuabudu Allah, mtu ambaye moyo wake umetundikwa misikitini anapotoka humo mpaka anarudi tena, watu wawili waliopenda na kwa ajili ya Allah wakawa pamoja kwa hilo, na wakatengana kwa hilo, na mtu aliyemkumbuka Allah akiwa peke macho yake yakabubujika machozi, na mtu aliyetakiwa na mwanamke mrembo na mwenye cheko, akasema mimi ninamuogopa Allah, na mtu aliyetoa sadaka kwa kujificha mpaka mkono wake wa kushoto usielewe ulichokitoa mkono wake wa kulia.” (Bukhari, na Muslim).

Na Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Kuna mtu mmoja alimtembelea ndugu yake kwa ajili ya Allah, Allah akamuwekea Malaika, (njiani) yule Malaika akamuuliza, “Unaenda wapi?” Akasema, “Na kwenda kumtembelea ndugu yangu fulani”, Akamuuliza, “Una mahitaji kwake?” Naye akasema: “Hapana”, Akasema: “Kwa sababu ya udugu uliopo kati yako na yeye: Akasema, “Hapana.” Akauliza, “Kwa sababu ipi basi?” Naye akasema: “Ninampenda kwa ajili ya Allah tu.” Yule Malaika akasema: “Allah amenituma nije kwako nikueleze kuwa yeye anakupenda kwa kumpenda huyu na amethibitisha kwako pepo.” (Muslim).

Sharti la udugu huu ni lazima uwe kwa ajili ya Allah na usiwe na mchanganyiko wa Kidunia au uhusiano wa maada (maslahi mengine) na msukumo uwe umetokana na imani ya Allah Peke Yake.

Ama Adabu Zake ni kuwa Anayefanywa ndugu Awe ni:-

1) **Mwenye akili**, kwa sababu hakuna kheri katika udugu wa mjinga wala urafiki naye. Kwa sababu mjinga mpumbavu anaweza kudhuru akidhani kuwa ndiyo namna ya kuokoa.

2) **Mwenye tabia nzuri**, kwa sababu mwenye tabia mbaya hata kama atakuwa na akili timamu yawezekana nafsi yake ikamtawala hasira akamfanyia mwenzake ubaya.

3) **Awe mcha-Mungu**, kwa sababu fasiki (muovu) aliyetoka katika kumtii Mola wake haaminiki. Kwani anaweza akamfanyia maovu mwenzake, bila kujali udugu au kitu chochote. Kwa sababu asiyemuogopa Allah kwa vyovyote hamuogopi mwengine.

4) **Mwenye Kushikamana na Kitabu na Sunna za Mtume** ﷺ awe mbali na bidaa na mengine yasio sahihi. Kwa sababu mtu mwenye kufanya bidaa anaweza kumsababishia mwenzake madhara yatokanayo na bidaa zake. Pia mwenye bidaa ana ubinafsi ni vizuri kumuepuka. Kwa hiyo vipi inawezekana kumfanyia mapenzi. Mcha-Mungu mmoja ameelezea kwa ufupi adabu hizi akasema alipokuwa ana muusia mtoto wake: “Ewe mtoto wangu kama mahitaji yatakulazimisha kufanya urafiki na watu basi mfanye rafiki mtu ambaye kama ukimtumikia atakuhifadhi aibu zako, na ukiwa naye atakupamba kwa sifa nzuri, na ukikosa matumizi atakusaidia. Mfanye rafiki mtu ambaye kama utamfanyia hisani naye atakufanyia, na anapoliona kwako jema analizingatia, na akiliona ovu analizuia. Mfanye rafiki mtu ambaye kama utamuomba atakupa, na ukimnyamazia atakuanza kwa mazungumzo na, likikufika tatizo atakusaidia. Mfanye rafiki mtu ambaye kama utasema atakukubali, na mkitaka kufanya kitu au jambo atakufanya amiri wake, na mnapogombea kitu atakuachia.”

Haki za Udugu Uliungwa kwa ajili ya Allah:

Miongoni mwa haki za undugu huu ni haya yafuatayo:-

1. **Kusaidiana kwa kutoa mali:** kila moja amsaidie ndugu yake kwa kutoa mali kama atahitaji, ikiwa hela zao ziko pamoja hazina tofauti. Kama ilivyopokewa kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه alipomjia mtu mmoja akasema, “Mimi ninataka

nikufanye ndugu kwa ajili ya Allah,” Akasema, “Unajua nini haki ya udugu?” Akasema, “Nifahamishe.” Akasema: “*Usiwe na haki zaidi kwa Dinari yako kulikoni mimi.*” Akajibu: Sijafikia hatua hii bado”, Akamwambia: Niondokee.”

2) **Kila mmoja awe msaada** kwa mwingine, anamtekelezea mahitaji yake na humuweka mbele kuliko nafsi yake. Amuelewe hali zake kama anavyozielewa hali zake mwenyewe, na kuliko familia yake na watoto wake, awe anamuulizia baada ya kila siku tatu, kama anaumwa akamuone, akishughulika amsaidie akisahau amkumbushe, amkaribishe akikaribia, na ampanulie nafasi kama atakaa na amsikilize anapozungumza.

3) **Asimseme isipokuwa kwa kheri**, asizitaje kasoro zake zake awe yupo au awe hayupo. Wala asizifichue siri zake, na asijaribu kutaka kuyaelewa mambo yake ya ndani na anapomuona njiani akiyaendea mahitaji yake asitake kuelewa chanzo chake na mapato yake. Awe mpole katika kumuamuru kwa zuri au kumkataza ovu, asipende mjadala naye katika mazungumzo na asimjadili katika haki au batili, asimlaumu kwa kitu na wala asimlaumu kwa mtu mwingine.

4) **Ampe kutoka katika ulimi wake kila anachokipenda kutoka kwake** amwite kwa jina lake analolipenda, amtaje kwa wema anapokuwa hayupo na anapokuwepo. Amfikishie sifa za watu wake, huku akionesha kuwa angependa kuwa kama yeye, na aifurahie hali hiyo. Asizidishe nasaha juu yake ili asimpe wasiwasi. Asimnasihie mbele ya watu akamfedhehesha, kama alivyosema Imam Shaafii (*Mwenyezi Mungu Amwie Radhi*), “Anayemuonya ndugu yake kwa siri amemnasihie na amempamba na anayemuonya ndugu yake hadharani amemfedhehesha na kumchafua.”

5) **Amsamehe makosa yake**, azifumbie macho bahati mbaya zake. Azihifadhi kasoro zake na awe na dhana nzuri kwake. Kama atafanya maasi kwa siri au hadharani asiyakate mapenzi yake kwake. Asiwatupe ndugu zake, bali asubiri kutubu kwake, na kama ataendelea basi atakata mapenzi yake au kuendelea na udugu wake pamoja na kumpa nasaha na kuendeleza mawaidha akitaraji kuleta toba ili Allah ampokelee toba yake. Amesema Abu Dardai رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, “Ndugu yako akibadilika na akaibadili hali aliyokuwa nayo usiwache kwa sababu hiyo, kwa sababu ni kawaida ya ndugu mara kukoseana mara nyingine anafanya vizuri.”

6) **Awe muaminifu katika udugu** ili udugu uweze kudumu. Kwa sababu kuukata kunabatilisha malipo ya udugu. Kama atafariki mapenzi ya udugu yatabaki kwa watoto wake, na kwa kila anayempenda katika marafiki zake. Kuulinda udugu na kutekeleza mapenzi kwa mwenye undugu ni wajibu. Mtume ﷺ alimkirimu Bi kizee aliyemtembelea na alipoulizwa sababu ya kufanya hivyo akasema:

“Alikuwa anatumia wakati wa uhai wa Khadija, na kuheshimu yaliyopita ni katika Dini.” (Hakim).

Na katika kufanya wema asiwe rafiki wa adui wa ndugu yake. Kwani Imamu Shafii amesema رضى الله عنه, “Rafiki yako atapokuwa na utii kwa adui yako watakuwa washirika katika kukufanyia uadui.”

7) **Asimlazimishe kufanya asiloliweza:** na asimlazimishe kufanya asichokifurahia. Asijaribu kutafuta cheo kupitia kwake, au mali, au kumlazimisha kufanya kazi. Kwa sababu asili ya udugu wao ulikuwa ni kwa ajili ya Allah. Kwa hiyo usibadilishwe na kuwa kwenye maslahi ya kidunia au kuondoa madhara. Kama asivyotakiwa kumkalifisha pia asimfanye akajikalifisha mwenyewe kwa ajili yake, kwani sura mbili zote zinapingana na udugu. Zinaathiri udugu, zinapunguza thawabu za udugu zilizolengwa. Kwa hiyo, alazimike kuondoa hali na tabia ya kuwa na maoni na kulazimisha na kutetea. Kwani kwa kuwepo hayo utapatikana upweke ambao utawafanya wasizoeane. Imekuja katika athari: “Mimi na wacha-Mungu wa umma wangu hatujikalifishi.” Na wamesema baadhi ya watu wema: “Asiye na taklifa mapenzi yake yataidumu, na mwenye gharama hafifu, yanadumu mapenzi yake na alama ya kutowepo Taklifa kunakojenga mahusiano, na kuondoa upweke, ni ndugu kufanya katika nyumba ya ndugu yake mambo manne ale nyumbani mwake, aingie msalani kwake, na aswali na alale pamoja naye. Kama atafanya hayo, basi undugu wake umekamilika. Uoga umeondoka na watakuwa pamoja na hivyo kupelekea hali ya furaha.”

8) Amuombe yeye na watoto wake na kila anayehusiana naye kheri ambazo anajiombea yeye na wanawe na wapate wanaohusiana naye. Kwa sababu hakuna tofauti kati ya mmoja wao na mwenzake kwa udugu uliowakusanya, atamuombea aliye hai na aliye kufa, aliyopo na asiyekuwepo. Amesema Mtume ﷺ,

*“Mtu akimuombea ndugu yake asiyekuwepo Malaika husema:
“Nawe umepata kama hicho.”* (Abu Dawud).

Mmoja wa watu wema amesema: Yuko wapi aliyekuwa kama ndugu mwema? Ndugu wa mtu kama atakufa basi watagawana mali zake alizoziacha, na watastarehe kwa alichocha. Ndugu mwema anabaki na huzuni tu, huku akiyapa umuhimu yale aliyomfanyia ndugu yake, na hali iliyompata, anamuomba ndani ya kiza cha usiku, na anamuomba msamaha akiwa chini ya udongo wa kaburi.



Mada ya Nane

Adabu za Kukaa na za Kikao

Muislamu maisha yake yote yanafuata utaratibu wa Uislamu. Utaratibu ambao umeyachukua mambo yote ya maisha yake, mpaka kukaa na namna ya kukaa kwake na ndugu zake. Kwa msingi huo Muislamu amekuwa ni mwenye kushikamana na adabu zifuatazo katika kukaa kwake yeye mwenyewe na kwake na ndugu zake.

1) **Akitaka kukaa atawasalimia watu wa Baraza kwanza**, kisha atakaa pale mahali ambapo litamuweka Baraza, na wala asimsimamisha mtu yeyote katika kikazi kwa Kauli ya Mtume رضي الله عنه.

“Asimsimamisha mmoja wenu mtu yeyote mahala alipokaa kisha akakaa yeye, lakini toweni wasaa au toweni nafasi.” (Muslim na Imam Ahmad).

Alikuwa Ibn Umar akimpisha mtu yeyote katika kikao chake hakai hapo.

Na amesema Jabir Ibn Samurah رضي الله عنه:

“Tulikuwa tunapomwendea Mtume رضي الله عنه hukaa kila mmoja wetu mahali ambapo litamuweka baraza (palipo karibu naye).” (Abu Dawud).

Na kwa kauli ya Mtume رضي الله عنه:

“Si halali kwa mtu yeyote kutenganisha kati ya watu wawili ila kwa idhini yao.” (Ibn Majah na At-Tirmidhi.).

2) **Akisimama mtu yeyote** kutoka katika kikazi chake kisha akarudi, anakuwa na haki zaidi na kikazi hicho, kutokana na kauli ya Mtume رضي الله عنه.

“Akisimama mmoja wenu kutoka katika kikazi chake, kisha akakirudia huyo ana haki zaidi ya kikazi hicho.” (Muslim).

3) **Asikae katikati ya duara** ya watu kutokana na kauli ya Hudhaifa kwamba Mtume ﷺ,

“Alimlaani mtu mwenye kukaa katikati ya duara ya watu.” (Abu Dawud).

4) **Atakapokaa anatakiwa** kuchunga adabu zifuatazo: Akae kwa adabu na utulivu na wala sipachanisha kati ya vidole vyake, na wala asichezee ndevu zake au pete yake. Na wala asichokoe meno yake au kuingiza kidole chake puani kwake, au kukithirisha kutema mate na makohozi au kukithirisha kupiga chafya na kwenda miayo. Uwe ukaaji wake hali ya kuwa mtulivu, mchache wa harakati, na yawe maneno yake ni yenye mpangilio na yenye kupimwa. Akizungumza akusudie ukweli na wala asikithirisha maneno. Ajiepushe na mzaha na mabishano, asizungumze kwa kujiona kuhusu watu wake wa nyumbani na watoto au kazi yake au uzalishaji wake wa mali au wa fasihi miongoni mwa mashairi au tunzi. Akizungumza mtu mwingine atatega sikio kumsikiliza hali ya kutovuka mpaka katika kuvutiwa na mazungumzo ya anayemsikiliza, na asiyakatize mambo yake au asimtake kuyarudia kwani kitendo hicho humkasirisha mzungumzaji.

Muislamu wakati anaposhikamana na adabu hizi, anatakiwa ashikamane na mambo mawili:

La kwanza, asiwaudhi ndugu zake kwa tabia zake au matendo yake. Kwa sababu kumuudhi Muislamu ni haramu na *“Muislamu ni yule ambaye wamesalimika Waislamu wenzake na (madhara ya) ulimi wake na mikono yake.”*

La pili, ayavute mapenzi ya ndugu zake na azoeane nao. Kwani Mtume ﷺ ameamrisha kupenda na kuzoeana miongoni mwa Waislamu na amehimiza sana kuhusu jambo hili.

Akitaka kukaa njiani atachunga adabu zifuatazo:

a) Kuyafumba macho (kuyadhibiti); hatayafungua macho yake kuyaelekeza kwa mwenye kupita katika Waumini wanawake, au aliyesimama mlangoni kwake au aliyejitokeza kupitia korido ya juu katika nyumba yake au mwenye kuchungulia dirishani kwake kutokana na haja yake. Kama ambavyo hayaelekezi macho yake kwa kumhusudu mtu yeyote au kumdharau mtu yeyote.

b) **Asiwafanyie maudhi wapita njia.** Kwa hivyo asimuudhi mtu yeyote kwa ulimi wake kwa kumtukana au kumshutumu au kwa kumtia aibu au kumsifu kwa ubaya wa umbile au tabia. Wala asimuudhi kwa mikono yake kwa kumpiga ngumi, wala kwa kumnyang'anya mali yake kwa kumpora. Wala kwa kukingama njiani kwa kuwazuia wapita njia hali ya kuikata njia yao.

c) **Anatakiwa kujibu salamu ya kila** atakaye msalimu miongoni mwa wapita njia, kwani kuijibu salamu ni wajibu kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَإِذَا حُيِّتُمْ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِنْهَا أَوْ رُدُّوهَا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ

حَسِيبًا

“*Na mnapo amkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo.*” (4:86).

d) **Anatakiwa kuamrisha ufanywe wema ulioachwa mbele yake** na likapuuzwa jambo lake na hali ya kuwa anaona kwani yeye anahusika katika mazingira hayo ya kuamrisha huo wema. Kwani kuamrisha wema ni faradhi juu ya kila Muislamu ambaye kumelazimu juu yake (kwa kuwa hakuna mtu mwingine). Wala faradhi hiyo haiporomoki ila kwa kuisimamisha. Mfano wake ni kulinganiwa kwa Swala na wala wasiitike waliohudhuria katika watu wa baraza. Katika hali hiyo kunapasa juu yake kuwaamrisha kumwitikia mlinganiwa Swala kwani hilo ni katika wema na baada ya kuachwa kunapasa juu yake kuamrisha. Mfano mwingine ni kupita mwenye njaa au asiye kuwa na nguo pia katika hali hiyo ni juu yake kumlisha au kumvisha akiweza na kama hakuweza atawaamrisha watu wengine kumlisha au kumvisha. Kwa sababu kumlisha mwenye njaa na kumvisha asiye na nguo ni katika wema ambao kunapasa kuamrisha wakati yakiachwa.

e) **Akataze kila uovu anaouna unafanywa** mbele yake, kwani kuondosha uovu ni kama kuamrisha wema, na ni kazi ya kila Muislamu kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“*Atakaye uona miongoni mwenu uovu na auondoshe*” (Muslim, na At-Tirmidhi).

Mfano wake ni kufanya uovu mbele yake mtu yeyote dhidi ya mtu mwingine kwa kumpiga au kumnyang'anya mali yake. Kwa msingi huo kunapasa juu yake katika mazingira haya kuuondosha uovu, kusimama dhidi ya dhulma na uadui katika mipaka ya uwezo wake na nafasi yake.

f) **Anatakiwa kumuongoza aliyepotea njia** kama mtu yeyote atamtaka amuongoze katika kumwelekeza nyumba au kumuongoza njia au kumfahamisha mtu yeyote miongoni mwa watu kunapasa juu yake kumwelekeza katika nyumba hiyo, au atamuongoza njia au atamfahamisha mtu atayetaka kumjua. Zote hizi ni katika adabu za kukaa njiani kama vile (kukaa) mbele ya nyumba, maduka, sehemu za kunywa kahawa au viwanja vya halaiki na mabustani na sehemu nyinginezo. Hilo ni kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Tahadharini na kukaa njiani.” Wakasema: *“Sisi hatuna budi kwani hayo ni makazi yetu tunazungumza humo.”* Akasema: *“Iwapo mtakataa ila kuendelea kukaa basi ipeni njia haki zake.”* Wakasema: *“Ni zipi haki za njia?”* Akasema, *“Kufumba macho (kuyainamisha), kuzuia maudhi, kujibu salamu, kuamrisha wema na kukataza maovu (na katika baadhi ya pokezi za hadithi hii kuna nyongeza ya maneno haya) na kumuongoza aliyepotea.”* (Bukhari).

Katika adabu za kukaa ni kumtaka msamaha Mwenyezi Mungu wakati wa kusimama kutoka katika baraza hilo ili kuwe ni kafara ya yale ambayo huenda yatakuwa yameyatendwa katika baraza hilo. Kwani Mtume ﷺ alikuwa anapotaka kusimama anasema:

“Kutakasika na maovu ni kwako Ee Mola Wangu wa haki pamoja na sifa zako nzuri, nakiri kwa moyo na kubaini kwa ulimi kwamba hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Wewe na kuomba msamaha na ninarudi kwako.” (Ameipokea At-Tirmidhi).



Mada ya Tisa

Adabu za Kula na Kunywa

Muislamu anakitazama chakula na kinywaji kwa kuvizingatia kuwa ni nyenzo za kumfikisha kwenye mambo mengine na sio lengo lililokusudiwa kwa dhati yake. Kwa hiyo, Muislamu anakula na anakunywa kwa lengo la kuhifadhi usalama wa mwili wake ambao ataweza kwao kumuabudu Allah. Ibada ambayo itamwezesha kupata utukufu wa nyumba ya Akhera na mafanikio yake.

Hakuwa Muislamu anayekula na kunywa kwa dhati (kwa nia) ya kula na kunywa tu na matamano ya mwili, na kwa msingi huo Muislamu kama asingekuwa na njaa asingekula na kama asingekuwa na kiu asingekunywa. “*Sisi ni watu hatuli mpaka tuwe na njaa na tukila hatuli mpaka tukashiba.*” Sasa kutokana na (mafundisho) hayo Muislamu amekuwa anashikamana katika kula kwake na kunywa kwake na adabu za kisheria maalum. Katika hizo:

a) Adabu za Kabla ya Kula:

i) Akifanye kiwe kizuri chakula chake na kinywaji chake kwa kuviandaa kutokana na vyakula halali vizuri, vilivyoepukana na mchanganyiko wa haramu na shubha. Hilo ni kutokana na Kauli ya Allah (Mtukufu):

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُلُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَاشْكُرُوا لِلَّهِ إِنَّ

كُنْتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١٧٢﴾

“*Enyi mlio amini! Kuleni vizuri tulivyo kuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa kweli mnamuabudu Yeye tu.*” (2:172).

Na kilicho kizuri ni kile kilicho halali ambacho si kichafu na wala si najisi. Anuie katika kula kwake na kunywa kwake kupata nguvu katika kumwabudu Allah Mtukufu ili alipwe kwa kile alichokula au kunywa kwani jambo (*Mubah*) (jambo ambalo limeruhusiwa kisheria) linabadilika kuwa ibada kutokana na nia nzuri na hivyo Muislamu hulipwa thawabu kwa ajili hiyo.

ii) Ni kuosha mikono yake kabla ya kula ikiwa ina uchafu au hakuwa na uhakika wa usafi wake.

iii) Akiweke chakula chake katika mkeka juu ya ardhi si juu ya meza kwani kufanya hivyo kuko karibu zaidi na unyenyekevu na pia kutokana na kauli ya Anas رضي الله عنه.

“Hajawahi kula Mjumbe wa Allah juu ya meza wala katika sahani.” (Ibn Majah).

Akae kwa unyenyekevu kwa kupiga magoti yake na kukaa juu ya mgongo wa nyayo zake kwa kuusimamisha mguu wake wa kuume na kuukalia wa kushoto, kama alivyokuwa Mjumbe wa Allah akikaa na kwa msembo wake Mtume rehema na amani ziwe juu yake.

“Sili hali ya kuchegama, hakika hapana jambo jingine mimi ni (mtumwa) Na kula kama anavyokula mja na ninakaa kama anavyokaa mja”. (Bukhari).

v) Aridhike na kilichopo, miongoni mwa vyakula kikimvutia akile na kama hakikumvutia atakiacha kutoka na hadithi ya Abi Hurairah رضي الله عنه.

“Hakukitia aibu Mjumbe wa Allah chakula chochote kabisa akikipenda anakila na akikichukia anakiacha.” (Abu Dawud).

Ale pamoja na mtu mwingine miongoni mwa mgeni au mke au mtoto au mtumishi, kutokana na khabari.

“Kusanyikeni juu ya chakula chenu mtabarikiwa katika chakula hicho.” (Imam Ahmad na Ibn Majah).

b) Adabu za Wakati wa Kula:

i) Ni kuanza kula kwa kulitaja jina la Allah, kwa Kauli yake Mtume wa rehema na amani ziwe juu yake.

“Pindi akila mmoja wenu na alitaje jina la Allah Mtukufu. Iwapo atasahau kulitaja Jina la Allah Mtukufu mwanzo wa chakula na aseme: Naanza kula kwa kulitaja Jina la Allah mwanzo wake na mwisho wake.” (Abu Dawud na Imam Ahmad).

ii) **Amalizie kula kwa kumsifu Allah**, kwa kauli yake Mjumbe wa Allah ﷺ:

“Mwenye kula chakula na akasema: “Sifa njema ni za Allah ambaye amenilisha chakula hiki na ameniruzuku pasina uwezo kutoka kwangu wala nguvu, atasamehewa yaliyotangulia katika madhambi yake.” (Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah).

iii) **Ale kwa vidole vitatu vya mkono wake wa kuume**, na kulifanya dogo tonge na kutafuna vizuri na kula sehemu inayomwelekea si katikati ya sahani, kwa Kauli Yake Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake akimwambia ‘Umar Ibn Salama:

“Ewe kijana litaje jina la Allah na kula kwa mkono wako wa kuume na kula upande unaokuelekea.” (Bukhari na Muslim).

Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Baraka inashuka katikati ya chakula, kwa hiyo kuleni kwa pembezoni mwake na wala msile kutokea katikati yake.” (At-Tirmidhi)

iv) **Anatakiwa kutafuna vizuri chakula na kuramba sahani** na vidole kabla ya kuvifuta kwa lesu au kuviosha kwa maji kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Akila mmoja wenu chakula asivifute vidole vyake mpaka avirambe au amrambishe mtu mwingine.” (Bukhari na Abu Dawud).

Kutokana na Kauli ya Jabir رضي الله عنه kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

“Ameamrisha kurambwa vidole na sahani na akasema: “Hakika nyinyi hamjui ni katika sehemu gani katika chakula chenu imo baraka.” (Muslim).

v) **Kikianguka kitu chochote katika kile** anachokula ataondosha katika kitu hicho uchafu na atakila kutokana na Kauli ya Mjumbe wa Allah (Rehema na Amani ziwe juu yake):

“Ikianguka tonge ya mmoja wenu na aiokote na aiondoshe uchafu na aile na wala asiache akamwachia shetani.”(Muslim).

vi) **Asipulizie katika chakula chenye moto** na asikile mpaka kipoe na asipulize katika maji wakati wa kunywa na apumue nje ya chombo mara tatu kutokana na Hadithi ya Anas رضي الله عنه kwamba Mjumbe wa Allah ﷻ:

“Alikuwa anapumua wakati wa kunywa mara tatu.” Imam Ahmad).

Kutokana na hadithi ya Abi Saïd رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ

“Amekataza kupulizia katika kinywaji.” (At-Tirmidhi).

Kutokana na Hadithi ya Ibni Abbasi رضي الله عنه kwamba,

“Mtume ﷺ amekataza kupumulia ndani ya chombo na kupulizia ndani yake.” (At-Tirmidhi na Abu Dawud).

vii) **Ajjepushe na kushiba kwenye kuvuka mpaka**, kwa Kauli ya Mjumbe wa Allah ﷻ:

“Hakujaza mwanadamu chombo kilicho kiovu kuliko tumbo lake, zinamtosha mwanadamu tonge chache zitakazousimamisha mgongo wake. Ikiwa hakufanya hivyo basi aligawe tumbo katika theluthi tatu, thuluthi ya chakula, thuluthi ya kinywaji na thuluhi ya pumzi.” (Ibn Majah na Al-Hakim).

viii) **Aanze kwa kumpa chakula au kinywaji mkubwa wa wote kati** ya aliyokaa, kisha atakizungusha kulia, tena kulia na awe yeye ndiye mtu wa mwisho kunywa kutokana na kauli ya Mjumbe wa Allah Rehema na Amani ziwe juu yake, *“Kabbir Kabbir”* Maana yake, Muanze aliye mkubwa kati ya waliokaa.” Kwa sababu ya kutaka kwake Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake idhini kwa Ibni Abbasi katika kuwapa kinywaji watu wazima waliokuwa wamekaa kushotoni kwake. Kwa sababu Ibni Abbasi رضي الله عنه alikuwa kuliani kwake na wazee walikuwa kushotoni kwake. Kule kutaka kwake idhini kunaonyesha kuwa mwenye haki ya kupewa kinywaji ni yule aliyekaa upande wa kulia. Kwa sababu ya Kauli ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake:

*“Upande wa kulia, “Upande wa kulia.” Na msembo wake,
“Mnyweshaji wa watu ndiye wa mwisho katika kunywa.”
(Bukhari na Muslim).*

ix) **Asianze kula chakula au kunywa kinywaji** na hali ya kuwa katika kikao kile kuna mtu ambaye ni mbora kuliko yeye kwa kutangulizwa kutokana na ukubwa wa umri wake au amezidi kiubora. Kwani kufanya hivyo kuna sababisha kuvunja adabu, na kuna mpelekea mwenye tabia hiyo kusifika na uroho. Sifa ambayo ni mbaya sana. Wanasema baadhi yao:

*“Pindi ikioshwa mikono kwa ajili ya kula chakula, si kuwa mimi
mwenye haraka zaidi yao, kwani mroho wa watu ni yule
anayefanya haraka sana.”*

x) **Asimwambie** rafiki yake au mwenyeji wake: kula na kumhimiza bali ni juu yake ale kwa adabu kiasi kinachomtosha katika chakula pasina kuona haya au kujilazimisha kuonesha haya. Kwani katika kufanya hivyo pana kumtia katika matatizo rafiki yake au mwenyeji wake kama ambavyo ndani yake kuna namna ya kujionesha na kujionesha ni haramu.

xi) **Amfanyie upole rafiki yake katika kula**, asifanye mbinu ya kula zaidi kuliko rafiki yake, na hasa iwapo chakula ni kichache. Kwani yeye katika hali hiyo atakuwa anakula haki ya mwenzake.

xii) **Asiwaangalie wenzake wakati wa kula** na asiwachunguze. Bali ni juu yake kuyainamisha macho yake na kuwaangalia watu wanaokula waliyo pembezoni mwake na asiwachungulie kwani hilo litawaudhi na huenda likamsababishia chuki kwa baadhi yao. Matokeo yake atapata dhambi kwa sababu ya kitendo hicho.

xiii) **Asifanye jambo ambalo watu hulionea kinyaa mara nyingi** kwa hiyo asikung’ute mkono wake ndani ya sahani na wala asikigeuze kichwa chake kwenye sahani wakati wa kula, na kukichukua chakula kwa sababu kisije kikaanguka kutoka mdomoni mwake kitu kikaangukia katika sahani. Kama ambavyo atakapouma kwa meno yake kitu miongoni mwa mkate, asiichovye sehemu iliobaki katika sahani au bakuli. Asizungumze kwa kutumia mitambo yanayofahamisha juu ya takataka na uchafu kwa sababu huenda akapata maudhi kutokana na hilo mmoja katika wenzake, na kumuudhi Muislamu kumeharamishwa.

xiv) Iwe anapokula pamoja na mtu fakiri si kwa ajili ya kuonyesha kujipendelea, na alapo pamoja na ndugu unatakiwa ulaji huo usimame juu ya msingi wa kuwa na furaha na kufanya vitendo au maneno yenye utani ndani yake. Na alapo pamoja na watu wenye vyeo na heshima anatakiwa aonyeshe heshima na adabu.

Adabu za Baada ya Kula:

i) **Aache kula kabla ya kushiba.** Kwa kumuiga Mtume wa Allah ﷺ na ili asiingie katika kuvimbiwa kwenye kuangamiza na kujaa tumbo kwenye kuondoa fahamu (utambuzi).

ii) **Arambe mkono wake kabla hajaufuta** au hajauosha kwa maji, na kuukosha kwa maji ni bora zaidi.

iii) **Aokote kilichoanguka katika chakula** wakati wa kula kutokana na mafunzo yaliyokuja ya kupendekeza kufanya hivyo. Kwa sababu kufanya hivyo ni katika mlango wa kushukuru.

iv) **Ayachokone meno yake na asukutuwe** kwa kuuweka mdomo wake katika mazingira mema. Kwa sababu kupitia huo mdomo atamtaja Allah na atazungumza na ndugu kama ambavyo usafi wa mdomo unabakisha usalama wa meno.

v) **Amshukuru Allah Mtukufu** baada ya kula na kunywa kwake na aseme iwapo atakunywa maziwa.

“Ewe Mola wa haki tubariki katika kile ambacho umeturuzuku na tuongezee.”

Na iwapo atafungua swaumu kwa watu atasema:

أفطر عندكم الصائمون، وأكل طعامكم الأبرار، وصلت عليكم الملائكة

“Wamefungua kwenu wafungaji na wamekula chakula chenu watu wema na wamewatakia rehema malaika.”



Mada ya Kumi

Adabu za Kumkaribisha Mgeni

Muislamu anaamini wajibu wa kumkirimu mgeni na hilo analipa hadhi yake inayotakiwa. Hilo ni kutokana na Kauli ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake):

“Ambaye anamwamini Allah na Siku ya Mwisho na amkirimu mgeni wake.” (Bukhari na Muslim).

Na msembo wake:

“Mtu Ambaye anamwamini Allah na Siku ya Mwisho na amkirimu mgeni wake na hiyo ni tuzo yake.” Wakauliza: *“Ipi tuzo yake?”* Akajibu, *“Mchana wake na usiku wake na takrima ya ugeni ni siku tatu, takrima itaozidi hapo hiyo ni sakada.”* (Bukhari na Darimi).

Na kwa ajili hiyo imekuwa ni juu ya Muislamu kushikamana na adabu zifuatazo katika makaribisho ya mgeni:

(a) Adabu za kualika watu kwenye takrima:

(i) Anatakiwa kuwaalika kwenye takrima yake wacha-Mungu kinyume cha mafasiki na waovu kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Usifanye urafiki ila na Muumini (wa Kiislamu na asile chakula chako ila mcha-Mungu).” (Darimi na al-Hakim).

(ii) Asiwachague kwa takrima yake matajiri tu kinyume cha mafakiri kwa kauli yake Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake:

“Chakula kibaya ni chakula cha karamu wanaitwa kwenye karamu matajiri kinyume cha mafakiri.” (Muslim na Abu Dawud).

(iii) **Asikusudie kwa takrima yake kujifakharisha** na kujionyesha bali akusudie kufuata Sunna ya Mtume (*Rehema na Amani ziwe juu yake*). Vile vile kuwaigiza Mitume waliyokuwa kabla yake kama vile Ibrahim Amani iwe juu yake na ambaye alikuwa akiitwa Baba wa wageni. Kama ambavyo atanuia kwa hiyo takrima kuingiza furaha kwa Waumini na kueneza mapenzi na furaha katika nyoyo za ndugu zake Waislamu.

(iv) **Asimwalike kwenye takrima hiyo yule ambaye** anaelewa kuwa kutakuwa na uzito kwake kuhudhuria au kwamba yeye anapata maudhi kwa baadhi ya ndugu waliyohudhuria. Kwa kujiepusha na kumuudhi Muumini ambako kumeharamishwa.

(b) Adabu za Kuitika Mwaliko:

i) **Anatakiwa kuitika mwaliko** na wala asichelewe ila kwa udhuru kama vile kuogopea maradhi katika Dini yake au mwili wake kwa Kauli ya Mtume (*Rehema na Amani ziwe juu yake*):

“Mwenye kualikwa basi asikose kujibu.” (Abu Dawud na Imam Ahmad).

Kauli Yake:

“Lau nimealikwa kwenye miguu ya mbuzi ningeitika. Na lau ninepewa zawadi ya mkono wa mbuzi (ugoko) ningeikubali.”
(Sahih al-Bukhari)

ii) **Asibague katika kujibu mwaliko kati ya fakiri na tajiri** kwani katika kutomjibu fakiri pana kuuvunja moyo wake. Kama ambavyo ndani ya kufanya hivyo kuna namna ya kiburi kinachochukiwa. Miongoni mwa aliyopokelewa katika kuitika mwaliko wa mafakiri ni kwamba Al-Hassan Ibn Ally رضي الله عنه aliwapitia maskini na hali wametandaza vipande vya mkate juu ya ardhi na huku wanakula wakamwambia: “Njoo ule chakula Ewe mtoto wa binti wa Mtume wa Allah ﷺ akasema, ‘Ndio hakika Allah hawapendi wenye kiburi akashuka kutoka katika nyumbu wake na akala pamoja nao.’”

iii) **Asitofautishe katika kujibu mwaliko kati ya masafa ya karibu** na mbali na ikielekezwa kwake mialiko mwili ataujibu uliyotangulia na atatoa udhuru kwa ule mwingine.

iv) **Asichelewe kwenye mwaliko kwa sababu ya kufunga kwake** bali atahudhuria. Ikiwa aliyemualika atafurahishwa na kula kwake basi atafungua. Kwa sababu kuingiza furaha katika moyo wa Muumini ni katika ibada. Kama hatafungua basi atawaomba kheri kwa Allah. Kwa Kauli ya Mtume, Rehema na Amani ziwe juu yake.

“Akialikwa mmoja wenu na ajibu, akiwa amefunga na awaombee waliomwalika na akiwa hakufunga basi na ale.”
(Muslim).

Na kwa Kauli yake Mtume ﷺ:

“Ndugu yako amejikalifisha kwa sababu yako kwa kuandaa chakula kisha unasema mimi nimefunga?” (Sunan Daraqutniy na Masnad At-Twayalisi).

v) **Akusudie kwa kule kuitika mwaliko kumkirimu ndugu yake Muislamu** ili apate malipo juu ya hilo, kutokana na khabari ya Mtume ﷺ:

“Hakika hapana jambo jingine, matendo yote yanazingatiwa kwa nia na hakika hapana jambo jingine kila mtu atalipwa kutokana na kile ambacho amenuia.”

Kwa sababu kutokana na nia njema linageuka jambo (mubaha) kuwa ni ibada analipwa juu yake Muumini.

c) **Adabu za Kuhudhuria Kwenye Mwaliko.**

i) **Asiwafanye** watu waliomwalika wamsubiri kwa muda mrefu atawasababishia kero na asifanye haraka kwenda kwenye mwaliko, ikawa ghafla kabla hawajajiandaa. Kwa sababu katika kufanya hivyo pana kuwaudhi.

ii) **Atakapoingia asikae mbele ya baraza** bali atakuwa mnyenyekevu katika kikao hicho na atakapoonyeshwa pa kukaa na mwenyeji wake atakaa mahali hapo na asiondoke.

iii) **Asifanye haraka kukiondoa chakula** kabla ya kuondolewa mikono katika hicho chakula na kukamilika kumaliza watu wote katika kula.

v) **Anatakiwa amletee mgeni wake kiasi kinachotosha** katika chakula kwani kukipunguza ni upungufu katika murua. Akizidisha ni kufanya na kujionyesha na yote mawili ni mambo mabaya.

vi) Itakapokuwa mmoja wenu amekuwa mgeni kwa mtu yeyote asizidisha zaidi ya siku tatu. Ila mwenyeji wake kama atamsisitizia kukaa zaidi na wakati wa kuondoka atamtaka ruhusa ya kuondoka.

vii) **Amsindikize mgeni kwa kutoka pamoja naye mpaka nje** ya nyumba. Kwa sababu watu wema wa zamani walifanya hivyo na kwa sababu hili linaingia katika kumkirimu mgeni ambako kumeamrisha kisheria.

viii) **Aondoke mgeni hali ya kuwa nafsi yake imeridhia** hata kama yametokea kwa bahati mabaya mapungufu ambayo hayakumridhisha. Kwani kufanya hivyo ni katika uzuri wa tabia ambao humfikisha mja kwenye daraja ya mwenye kufunga na kusimama kwa kufanya ibada.

ix) **Anatakiwa Muislamu kuwa na matandiko matatu** moja lake mwenyewe, na la pili la mke na tatu la mgeni na kuongeza zaidi ya magodoro matatu kumekatazwa kutokana na kauli ya Mtume ﷺ

“Tandiko (Nafasi ya kulala ndani ya nyumba) la mwanamume na tandiko la mwanamke na tandiko la mgeni na la nne la shetani.” (Abu Dawud na Imam Ahmad).



Mada ya Kumi na Moja

Adabu za Safari

Muislamu anaona kusafiri ni katika mambo ya lazima na muhimu katika maisha yake. Mambo ambayo maisha yake hayaepukani nayo kwani kuhiji na kufanya umra na kwenda vitani na kutafuta elimu na kufanya biashara na kuwatembelea ndugu na mambo hayo yote yanagawanyika kati ya faradhi na wajibu hapana budi kusafiri na kutoka.

Na kwa msingi huo Uislamu umeipa safari hukumu zake na adabu zake na umuhimu usiokanushwa, na imekuwa ni juu ya Muislamu mwema kujifundisha hukumu na adabu hizo na afanye kila analoliweza katika kuzitekeleza na kuzifanyia kazi.

Ama Hukumu ya Safari ni:

1) Kupunguza Swala yenye rakaa nne, kwa hiyo ataswali rakaa mbili tu. Ila Swala ya Magharibi kwani hiyo ataiswali rakaa tatu. Ataanza kupunguza Swala kuanzia siku anayoondoka katika mji anaoishi mpaka ataporudi isipokuwa kama atanuia kukaa siku nne au zaidi hakika mji alikoenda katika hali hiyo, atatimiza na hatapunguza, mpaka atakapotoka kurejea mjini kwake, hapo ataanza tena kupunguza. Mpaka atakapofika mjini kwake na hilo ni kutokana na Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَإِذَا ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ إِنَّ خِفْتُمْ

أَنْ يَفْتِنَكُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ الْكَافِرِينَ كَانُوا لَكُمْ عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿١١﴾

“Na mnapo safiri katika nchi si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala, iwapo mnachelea wasije wale walio kufuru wakakuleteeni maudhi.” (4:101).

Kutokana na Kauli ya Anas:

“Tulitoka pamoja na Mtume wa Allah ﷺ Madina kuelekea Makkah alikuwa akiswali Swala yenye rakaa nne, rakaa mbili mbili, mpaka tuliporejea Madina.” (An-Nisaa na At-Tirmidhi).

(2) **Kupaka juu ya khofu mbili kwa muda wa siku tatu usiku na mchana,**

“Alijaalia kwetu Mtume ﷺ siku tatu mchana na usiku wake kwa safari na mchana mmoja na usiku wake kwa mkazi, kwa anayekusudia kupaka juu ya khofu mbili.” (Muslim).

(3) **Ruhusa** ya kutayamamu akiyakosa maji au ikiwa taabu juu yake kuyatafuta au umekuwa ghali juu yake thamani yake kwa kauli Yake Allah:

وَأِنْ كُنْتُمْ مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُم مِّنَ الْغَائِطِ أَوْ لَمَسْتُمُ
الْتِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً

“...isipo kuwa mmo safarini - mpaka mkoge. Na mkiwa wagonjwa, au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewagusa wanawake - na msipate maji...” (4: 43).

(4) **Ruhusa ya kufungua Swaumu** kwa kauli Yake Mwenyezi Mungu,

فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَّرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ

“...Na atakaye kuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimize hisabu katika siku nyengine...” (2:184).

(5) **Kufaa kuswali Swala ya sunna juu ya mnyama** kokote atakoelekea kutokana na kauli ya Ibn Umar رضي الله عنه

“Kwamba Mtume ﷺ alikuwa akiswali sunna akielekea kule ambako ameelekea ngamia wake.” (Muslim).

(6) **Kufaa kukusanya kati ya Adhuhuri na Alasiri au na kati ya Magharibi na Isha** kukusanya kwa kutanguliza kikiwa mwendo umekazana kwake kwa hiyo ataswali Adhuhuri na Alasiri katika wakati wa Adhuhuri na ataswali Magharibi na Isha katika wakati wa Magharibi au atakusanya kwa kuchelewesha Adhuhuri mpaka wakati wa Alasiri na ataziswali zote pamoja na ataichelewesha Magharibi mpaka Isha na ataziswali pamoja kutokana na kauli ya Muadh رضي الله عنه:

“Tulitoka na Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake) Katika vita vya Tabuk alikuwa akiswali Adhuhuri na Alasari pamoja, na Magharibi na Isha pamoja.” (Muslim).

Ama Adabu za Safari ni:

1-Kurudisha vitu alivyodhulumu na amana kwa wenyewe kabla ya safari, kwani safari ni pahala penye uwezekano wa kutokea kifo.

2-Atayarisha andao lake la safari kutokana na halali na aache matumizi ya wale watu ambao yanapasa juu yake matumizi yao miongoni mwa wake, watoto na wazazi.

3-Awaage watu wake wa nyumba na ndugu zake na marafiki zake na aombe kwa maombi haya kwa wale ambao anawaaga.

“Ninaweka amana kwa Mwenyezi Mungu Dini yenu na amana zenu na mwisho wa matendo yenu.” Na watamwambia wale wenye kuagwa: Akupe Allah uchaji na akughafirie madhambi yako na akuelekeze kwenye kheri kote utakakoelekea.” Kutokana na kauli ya Mtume ﷺ: “Hakika Luqman amesema, “Hakika Allah Mtukufu akiwekezwa amana ya kitu chochote anakihifadhi.” (Imam Ahmad).

Na alikuwa akimwambia mtu anayemuaga:

“Namkabidhi Allah Dini yako na amana zako na mwisho wa matendo yako.” (Imam Ahmad).

4). Atoke kwenda katika safari yake akifuatana na watu watatu au wanne baada ya kuwachagua katika wanoafaa kusafiri naye kwa sababu safari kama inavyosemwa: **“Ni nafasi ya kuwajua watu.”** Na imepewa jina la safari kwa sababu hudhahirisha tabia za watu kwa Kauli ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake)

“Msafiri mmoja ni shetani na wasafari wawili ni mashetani wawili na wasafari watatu hao ni msafara.” (Abu Dawud na Al-At-Tirmidhi).

Na kwa maneno yake:

“Lau kwamba watu wanayajua yanaotokea katika upweke yale ambayo ninayajua asingekwenda msafari usiku peke yake.”
(Bukhari).

5) Unatakiwa msafara (watu) unaosafiri kumfanya kiongozi mmoja wao atakaye watawala kwa kuwaongoza na kuwashauri kutokana na Kauli ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake).

“Wakitoka watu watatu katika safari na wamfanye kiongozi mmoja wao.”(Abu Dawud).

6) Aswali kabla ya safari yake Swala ya kutaka kheri (*Istikharah*) kwa sababu ya mapendekeo ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake) katika hilo:

“Alikuwa Mtume ﷺ akiwafundisha Swala hiyo kama alivyokuwa akiwafundisha sura katika Qur’ani Tukufu na katika mambo yote.” (Bukhari).

7) Anatakiwa kusema wakati wa kutoka nyumbani,

“Natoka kwa kulitaja jina la Allah, nimeegemea kwa Allah, hapana kukengeuka kuepukana na maasi na hapana nguvu juu ya kufanya ibada isipokuwa kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Ee Mola wa Haki nataka hifadhi kwako na kupotea au kupotezwa au kuteleza au kutelezeshwa au kumfanyia mtu uovu au kufanyiwa uovu.” (Abu Dawud).

Na akipanda atasema:

Kwa jina la Allah na kwa msaada wa Allah na Allah ni Mkubwa nimetegemea juu ya Allah, hapana kukengeuka kuepukana na maasi na hapana nguvu juu ya kufanya ibada ila kwa msaada wa Allah Aliye Mtukufu Aliye Mkubwa. Alilolitaka Allah limekuwa na ambalo hakulitaka halikuwa, Utukufu ni wa yule ambaye ametudhalilishia hiki kipandwa na hatukuwa ni wenye kuweza kukipanda lau si Allah kukidhalilisha kwetu, na hakika sisi kwa Bwana wetu ni wenye kurudi. Ee Mola wangu wa Haki hakika

mimi ninakuomba katika safari yetu hii wema na uchaji na kufanya matendo yale ambayo unayaridhia. Ee Mola wangu wa Haki ifanye nyepesi kwetu safari yetu hii na ufupishe kwetu umbali wake. Ee Mola wangu wa Haki Wewe Ndiye Rafiki safarini na Mwangalizi wa watu wangu na mali zangu baada ya kusafiri kwangu. Mola wangu wa Haki hakika mimi nataka hifadhi Kwako uniepushe na mashaka na taabu za safari na mandhari ya huzuni, na kurejea utupu, na ubaya wa mandhari katika mali, mke na watoto.” (Abu Dawud).

8) **Anatakiwa kutoka Siku ya Alhamisi mwanzoni** mwa mchana kwa kauli ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake:

“Ewe Mola wangu wa haki ubarikie umma wangu katika kutoka kwao mapema asubuhi”. (At-Tirmidhi, Abu Dawud na Ibn Majah).

Na kutokana na maelezo ya Mtume ﷺ kwamba yeye alikuwa akitoka kwenda katika safari zake siku ya Alhamisi.

9) **Anatakiwa kutoa takbira kila** anapopanda sehemu yenye mwinuko kutokana na kauli ya Abi Hurairah رضي الله عنه: “Kwamba mtu mmoja alisema: ‘Ewe Mjumbe wa Allah hakika mimi ninataka kusafiri, nakuomba uniusiye.’ Akasema

‘Jilazimisha kumcha-Mwenyezi Mungu na kutoa takbira juu ya kila mahali penye mwinuko.’ (At-Tirmidhi).

10) **Na pindi akiwaogopa watu atasema:**

“Ewe Mola wangu wa Haki hakika sisi tu na kuweka Wewe shingoni mwao na tunataka hifadhi Kwako na shari zao.”

Kwa sababu Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake amesema hivyo.

11) **Anatakiwa kumuomba Allah** katika safari yake na aombe kheri za dunia na akhera. Kwani kuomba safarini kunajibiwa kwa kauli ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake.

“Maombi matatu ni yenye kujibiwa hapana shaka yoyote. Maombi ya mwenye kudhulumiwa, maombi ya msafari na maombi ya mzazi juu ya mtoto wake.” (At-Tirmidhi).

12) Akishuka mashukio yoyote atasema:

“Ninajikinga kwa maneno ya Allah yaliyokamilika na shari ya kila alichokiumba.”

Na utapokuja usiku utasema:

“Ewe ardhi Bwana wangu na Bwana wako ni Allah hakika mimi nataka hifadhi kwa Allah na shari yako, na shari ya vilivyo ndani yako na shari ya vile ambavyo ameviumba kwako na shari ya vile ambavyo vinatambaa juu yako, na ninataka hifadhi kwa Mwenyezi Mungu na shari ya simba na kilicho cheusi na nyoka na nge, na wakazi wa mji na mzazi na alichokizaa.” (Abu Dawud, Imam Ahmad, na Al-Hakim).

13) Akiogopa upweke atasema:

“Kutakata na kila sifa mbaya ni kwa Mfalme Aliye Mtakatifu Bwana wa Malaika na Jibril, zimedhihirishwa mbingu kwa utukufu wa Allah.”

14) Atakapolala mwanzoni mwa usiku ataitandika dhira ya yake (atalalia mkono wake) na akilala wakati wa mwisho wa usiku, atasimamisha dhira ya yake na atakiweka kichwa chake katika kitanga chake ili asiune mzito usingizi wake ikampita Swala ya Asubuhi katika wakati wake.

15) Akiukaribia mji atasema:

“Ewe Mola wa haki ufanye mji huu kwetu ni mahali pa kutulizana na turuzuku ndani yake riziki ya halali, Ewe Mola wa Haki hakika mimi ninakuomba kheri ya mji huu na kheri ya vilivyo ndani yake; na ninakutaka hifadhi na shari yake na shari yavilivyo ndani yake.” Kwani Mtume ﷺ alikuwa akisema hivyo.

Minhajil Muslim

16) **Afanye haraka kurejea** kwa watu wake na mji wake atakaokuwa ametimiza mahitaji yake katika safari yake kutokana na kauli ya Mtume ﷺ

“Safari ni kipande cha adhabu inamzuilia mmoja wenu chakula chake na kinywaji chake na usingizi wake, atakapopata mmoja wenu haja yake katika safari yake na arudi haraka kwa watu wake.” (Bukhari na Muslim na Ibn Majah).

17) **Na akirudi hali ya kurejea atatoa takbir na kusema,**

أَبُون تَابُون عَابِدُون لَرَبِنَا حَامِدُون

“Sisi ni wenye kurejea, wenye kutubia, wenye kumwabudu Bwana wetu, wenye kumsifu.” (Bukhari na Muslim).

Na atayakariri maneno hayo kwa kuwa Mtume ﷺ alilifanya hilo.

18) **Asiwaendee ghafla watu** wake wakati wa usiku na awatumie mtu ambaye atawapa habari ya kurudi kwake ili asiwaendee ghafla kwa kufikiwa kwake kwani kufanya hivyo kulikuwa ni katika mwongozo wa Mtume ﷺ.

19) **Asisafiri mwanamke** safari ya mchana na usiku ila pamoja na mtu mwenye udugu naye kutokana na Kauli ya Mtume ﷺ:

“Si halali kwa mwanamke yeyote anayesafiri mwendo wa mchana na usiku ila awe pamoja na ndugu yake.” (Bukhari na Muslim).



Mada ya Kumi na Mbili

Adabu za Kuvaa

Muislamu analiona vazi kuwa limeamrisha na Allah katika Kauli yake

يَنْبِيَّ ءَادَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُؤَرِّى سَوْءَ تِكُمْ وَرِدِشًا ط وَلِبَاسُ التَّقْوَى
ذَلِكَ خَيْرٌ ذَلِكْ مِنْ ءَايَتِ اللَّهِ لَعَلَّهُمْ يَذْكُرُونَ ﴿٢٦﴾

“Enyi wanaadamu! Tumekuteremshieni nguo za kuficha tupu zenu, na nguo za pambo. Na nguo za uchamngu ndio bora. Hayo ni katika Ishara za Mwenyezi Mungu mpate kukumbuka.” (7:26).

Na ameionyesha neema hiyo katika kauli Yake:

يَنْبِيَّ ءَادَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُؤَرِّى سَوْءَ تِكُمْ وَرِدِشًا ط وَلِبَاسُ التَّقْوَى
ذَلِكَ خَيْرٌ

*“Enyi wanaadamu! Tumekuteremshieni nguo za kuficha tupu zenu, na nguo za pambo Na nguo za uchamngu ndio bora
“ (7: 26).*

Na katika Kauli Yake:

وَعَلَّمَنَّهُ صِنْعَةَ لَبُوسٍ لَكُمْ لِتُحْصِنُكُمْ مِنْ بَأْسِكُمْ فَهَلْ أَنْتُمْ شَاكِرُونَ ﴿٨٠﴾

“Na tukamfundisha kuunda mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika kupigana kwenu. Je! Mtakuwa wenye kushukuru?” (21:80)

Na kwamba Mjumbe Wake ﷺ ameliamuru hilo katika kauli yake,

“Kuleni na kunyweni na vaeni na toeni sadaka bila ya israfu wala kiburi.” (Bukhari).

Minhajil Muslim

Kama alivyoweka wazi Mtume ﷺ yanayofaa katika hayo (mavazi) na yale ambayo hayafai na yanayopendekezwa kuyavaa na yanayochukiwa. Kwa msingi huo ni juu ya Muislamu kujilazimisha katika kuvaa kwake na adabu zifuatazo:

1) **Asivae hariri kwa hali** zote hata kama ikiwa ni nguo au kilemba au visivyokuwa hivyo kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Msivae hariri kwani hakika mambo yalivyo atakayevaa duniani hatovaa huko akhera” (Muslim)

Na kauli yake hali ameikamata hariri akaiweke katika mkono wake wa kulia na dhahabu akaiweka katika mkono wake wa kushoto:

“Hakika viwili hivi ni haramu kwa mwanaume katika umati wangu.” (Abu Dawud)

Na kauli Yake:

“Kumeharamishwa kuvaa hariri kwa mwanamume katika umati wangu na kumehalalishwa kwa wanawake wao.” (At-Tirmidhi).

2) **Asirefusha nguo** yake au suruali yake au kanzu iliyounganishwa na kofia yake au shuka yake ya juu mpaka vikavuka fundo zake mbili za miguu kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Kilicho chini ya fundo mbili katika shuka hicho kitakuwa motoni.”

Na Kauli Yake:

“Kuteremsha shuka na kanzu na kilemba mwenye kuburuza hivyo hatamtazama Allah Siku ya Kiyama.” (Abu Dawud na An-Nasai).
Na Kauli Yake: *“Hata mtazama Allah mwenye, kuikokota nguo yake kwa kibri.”* (Bukhari na Muslim).

3) **Alipe kipaumbele vazi jeupe** kuliko jingine, na aone kuvaa rangi aina zote kunafaa kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Vaeni nguo nyeupe, kwani hizo ni safi na ni nzuri na wakafinini katika hizo wafu wenu.” (At-Tirmidhi).

Na kutokana na kauli ya Albraa Ibn Aazab رضي الله عنه:

“Alikuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Rehema na Amani ziwe juu yake ni kati na kati (wa umbo) na kwa hakika nilimuona katika vazi jekundu si kuona kabisa kitu kizuri sana kuliko vazi hilo.” (Bukhari).

Kutokana na yaliyothibiti kutoka kwa Mtume ﷺ miongoni mwa kuwa yeye alivaa nguo ya kijani na akifunga kilemba cheusi.

4) **Muislamu mwanamke arefusha vazi lake** mpaka lifunike nyayo zake na ateremshe mtandio wake juu ya kichwa chake mpaka afunike shingo na kifua chake kutokana na kauli ya Allah Mtukufu:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لَأَزُوجِكُمْ وَبَنَاتِكُمْ وَنِسَاءَ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلْبَابِهِنَّ

“Ewe Nabii! Waambie wake zako, na binti zako, na wake za Waumini wajiteremshie nguo zao...” (33:59).

Na kauli Yake:

وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ

ءَابَائِهِنَّ

“...Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasionyeshe uzuri wao ila kwa waume zao, au baba zao...” (24:31).

Na kutokana na kauli ya Aisha رضي الله عنها: “Awarehemu Allah wanawake waliohama (Muhajirati) wa mwanzo, alipoteremsha Allah,

“Na wateremshe mitandio yao mpaka vifuani mwao.” Walichana yaliyo mapana katika mashuka yao wakajitanda kwayo.” (Abu Dawud).

Kutokana na kauli ya Ummu Salama رضي الله عنها iliposhuka:

“Ewe Mtume waambie wake zako na mabinti zako na wake wa Waislamu wateremshe juu yao kaya zao.” Walitoka wanawake wakianswari kama kwamba pana vichwani mwao kunguru kutokana na mitandio waliyojifunika.” (Abu Dawud).

5) **Asivae pete ya dhahabu** kutokana na kauli ya Mtume Rehema na Amani ziwe yuu yake katika kuelezea dhahabu na hariri.

“Hakika viwili hivi ni haramu kwa wanamume katika umati wangu.” Kauli yake *“Kumeharamishwa kuvaa hariri na dhahabu juu ya Wanaume katika umati wangu na kumehalalishwa juu ya wanawake wao.”*

Na kauli yake na hali anaona pete ya dhahabu mkononi mwa mtu mmoja akaivaa na akaitupa akasema:

“Analikusudia mmoja wenu kaa la moto analiweka mkononi mwake?” Akaambiwa mtu yule baada ya Mtume ﷺ kuondoka ichukue pete yako unufaike nayo, akasema: *“Hapana naapa si ichukui milele na hali ya kuwa Mtume wa Allah ﷻ ameitupa.”* (Muslim).

6) **Si vibaya kwa Muislamu kuvaa pete ya fedha** au kuchapisha katika kito chake jina lake na akaifanya ni muhuri anapigia barua zake na maandishi yake na kutilia saina nyaraka zake muhimu au nyingine kwa sababu Mtume ﷺ alitengeneza pete ya fedha iliyoandikwa juu yake: **Muhammad Rasulullah** (Muhammad ni Mjumbe wa Allah) alikuwa anaivaa katika kidole chake kidogo katika mkono wake wa kushoto. Kutokana na kauli ya Anas رضي الله عنه:

“Ilikuwa pete ya Mtume ﷺ katika hiki akiashiria kwenye kidole kidogo cha mkono wa kushoto.” (Muslim).

7). Asijifunike gubigubi nako ni kujizonga kwa nguo yake juu ya mwiliwake, na asiache nafasi ya kutolea mikono yake kutokana na kukataza Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake juu ya hilo na asitembee kwa kiatu kimoja kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Asiende mmoja wenu kwa kiatu kimoja na aende bila ya viatu au na avae miguu yote miwili” (Muslim).

8) Asivae Muislamu mwanamume vazi la Muislamu mwanamke wala Muislamu mwanamke vazi la mwanamume kutokana na kuharamisha Mtume ﷺ hilo kwa kauli yake:

“Amewalaani Mwenyezi Mungu wanamume wenye kujifananisha na wanawake, na wanawake wenye kujifananisha na wanaume.” (Bukhari).

Na kauli yake:

“Amemlaani Mwenyezi Mungu mwanamume anayevaa vazi la mwanamke na mwanamke anayevaa vazi la mwanamume, kama alivyowalaani wanamume wanaojifananisha na wanawake na wanawake wanaojifananisha na wanamume.” (Abu Dawud na Imam Ahmad).

9) Wakati ukivaa viatu utaanza kuvaa mguu wa kulia na utakapovua utaanza upande wa kushoto kutokana na Kauli ya Mtume ﷺ:

“Pindi akivaa viatu mmoja wenu na aanze kwa mguu wa kulia, na pindi akivua na aanze na mguu wa kushoto, ili uwe mguu wa kulia ndiyo wa mwanzo wao kuvaa viatu na wa mwisho wao kuvuliwa.” (Muslim).

10) Aanze upande wa kulia katika kuvaa nguo zake kutokana na kauli ya Aisha رضي الله عنها:

“Alikuwa Mjumbe wa Allah anapenda kuanza upande wa kulia katika mambo yake yote, katika kuvaa kwake viatu, katika kujichana nywele kwake na kujitwahaisha kwake.” (Muslim).

11) Aseme pindi atakapovaa nguo mpya au kilemba au kivaliwa chochote:

اللَّهُمَّ! لك الحمد أنت كسوتيه، أسألك خيره، وخير ما صنع له،
وأعوذ بك من شره، وشر ما صنع له

“Allahumma lakal Hamdu anta kasawtanihi, As-aluka khayrahu, wa Khayra ma suni’a lahu, Wa-au’dhubika min sharihi, washari ma suni’a lahu”

“Ewe Mola Wangu wa Haki Sifa Njema ni Zako, Wewe ndiyo uliyenivisha ninakuomba kheri yake na kheri ya lile ambalo imetengenezwa kwa ajili yake...” (Abu Dawud na At-Tirmidhi).

Kwa sababu yamekuja hayo kutoka kwa Mtume ﷺ.

12) **Amuombee ndugu yake Muislamu** wakati akimuona amevaa nguo mpya atamwambia: *“Chakaza na uchakaze.”* (Bukhari) Kwa sababu Mtume ﷺ alimuomba hayo mama Khalidi alipovaa nguo mpya.



Mada ya Kumi na Tatu

Adabu za Mambo ya Kimaumbile

Muislamu kutokana na sifa ya kuwa yeye ni Muislamu wakati wote anashikamana na mafunzo ya kitabu cha Bwana wake na mwenendo wa Mtume wake ﷺ. Juu ya mwangaza wa viwili hivyo anaishi na kufuatana navyo amejitwika katika mambo yake yote. Na hilo ni kutokana na kauli ya Allah:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ
مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

“Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi.” (33: 36).

Na Kauli Yake:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا

“Alilowaleteeni Mtume lichukueni na lile ambalo amewakatazeni nalo komeni (kulifanya).” (59:7).

Na kutokana na Kauli ya Mtume ﷺ:

“Hatakuwa Muumini kamili mmoja wenu mpaka yawe mapenzi yake ni yenye kufuata yale ambayo nimekuja nayo.”

Na Kauli yake:

“Mwenye kufanya tendo lolote ambalo hamna ndani yake mafunzo yetu basi tendo hilo ni lenye kurudishwa.” (Bukhari na Muslim).

Kutokana na msingi huu Muislamu anajilazimisha na adabu zifuatazo katika mambo ya maumbile ambayo yamethibiti kutoka kwa Mtume ﷺ katika kauli yake:

*“Mambo matano matano ni katika mambo ya maumbile:
Kupunguza masharubu, kunyonyoa kwapa, kukata kucha,
kunyoya kinena na khitani (kutahiri)”* (At-Tirmidhi na An-Nasai).

1) **Al-Istihdad:** Ni kunyoya kinena kwa kitu kilicho kikali kama vile kisu, wembe na mfano wake na si ubaya kuziondoa nywele hizo kwa chokaa.

2) **Khitani:** Ni kukata ngozi ambayo inafunika kichwa cha dhakari na ni sunna kulifanya hilo katika siku ya saba ya kuzaliwa. Kwa sababu Mtume ﷺ aliwatahiri Hassan na Hussein watoto wa Fatima Al-Zahraa na Ally رضي الله عنه siku ya saba ya kuzaliwa. Na si vibaya kuchelewa mpaka muda uliyo kabla ya kubaleghe, kwani alijitahiri Mtume wa Allah Ibrahim katika umri wa miaka themanini na imepokewa kutoka kwake Rehema na Amani ziwe juu yake kwamba alikuwa pindi anaposilimu mtu mikononi mwake humwambia,

“Zitupe nywele za ukafari na kijahilia.”

3) **Kupunguza masharubu** kwa hiyo atakata Muislamu masharubu yake ambayo yananing'inia juu ya mdomo wake. Ama ndevu ataziacha mpaka zijae uso wake na aziendeleze kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Zikateni shurubu na ziacheni ndevu na nendeni kinyume na majusi.” (Muslim).

Na kauli yake:

“Nendeni kinyume na Mushirikina, punguzeni masharubu na ziacheni ndevu.” (Ibn Majah).

Kama ambavyo atajiepusha kuzipaka ndevu zake kwa rangi nyeusi kutokana na kauli ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake wakati alipoletewa baba wa Abubakar Al-Siddiq siku ya ufunguzi wa Makkah kana kwamba kichwa chake ni mti wenye maua au matunda meupe kwa weupe:

“Mpelekeni kwa baadhi ya wake zake wambadilishe kwa rangi yoyote lakini wamwepushe na rangi nyeusi.” (Abu Dawud).

Ama kujipaka na *katm* (mmea hupakwa kwao nywele na hutengenezwa kutokana na wino wa kuandikia inapendezeshwa kupaka hizo) na atakapozifuga Muislamu nywele za kichwa chake na asizinyoe basi na azikirimu (ataziweka vizuri) kwa kuzipaka mafuta na kuzichana kutokana na kauli ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake):

*“Ambaye mwenye nywele nyingi na azikirimu (aziweke vizuri).”
(Abu Dawud na Ibn Majah)*

4) **Kunyonyoa kwapa** kwa hiyo atanyonyoa Muislamu nywele za kwapa na kama hakuweza kuzinyonyoa atazinyoa au atazipaka chokaa na mfano wake ili ziondoke.

5) **Kukata kucha** atazikata Muislamu kucha zake, na ni Sunna kwake kuanza mkono wa kulia kisha wa kushoto kisha mguu wa kulia na kisha wa kushoto. Atayafanya Muislamu yote hayo kwa nia ya kumuigiza Mtume wa Allah ﷺ na kumfuata ili apate kwa kufanya hivyo malipo ya kumfuata Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake na kufuata mwenendo wake. Kwani matendo yanazingatia nia na kila mtu atalipwa kutokana na lile alilolinuiya.



Mada ya Kumi na Nne

Adabu za Kulala

Muislamu anaona kulala ni katika neema ambazo Allah amezineemesha kwa waja wake. Katika Kauli Yake Allah Mukufu:

وَمِنْ رَحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ

وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

“Na miongoni mwa Rehema Zake amewafanyieni usiku na mchana ili mpumzike ndani yake na ili mtafute fadhila zake na ili mpate kumshukuru.” (al-Qasas: 73).

Na katika Kauli Yake:

وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ﴿٩﴾

“Na amefanya kulala kwenu kuwa ni mapumziko ya viwiliwili vyenu.” (Annabaa: 9).

Kwa sababu kupumzika mja kwa masaa katika usiku baada ya shughuli za mchana za mfululizo ni katika mambo yanayosaidia maisha ya mwili na kubaki makuzi yake na uchangamfu wake. Ili mwili uweze kutekeleza kazi zake ambazo ameziumba Allah kwa ajili yake. Na ili kuzishukuru neema hizo kunalazimu kwa Muislamu katika kulala kwake kuchunga adabu zifuatazo:

1) **Asicheleweshe kulala kwake** baada ya Swala ya Isha ila kwa dharaura kama vile kujisomea au kuzungumza na mgeni au kumliwaza mke. Katika aliyoyapokea Abu Barzah kwamba:

“Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake alikuwa anachukia kulala kabla ya Swala ya Isha na kuzungumza baada yake (Swala ya Isha).” (Bukhari na At-Tirmidhi).

2) **Anatakiwa kujitahidi asilale ila na udhu** kutokana na kauli ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake) akimwambia Albaraa Ibn Aazib رضي الله عنه:

“Utakapoyaendea malazi yako tawadha kama unavyotawadha kwa Swala.” (Bukhari na Au Daud).

3) **Alale wakati** akianza kulala kwa ubavu wake wa kulia, na si vibaya kugeuka kwenda kwenye ubavu wake wa kushoto baada ya hapo. Kutokana na Kauli ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake) akimwambia Al-Baraa Ibn Azib رضي الله عنه.

”Utakapoyaendea malazi yako tawadha kama unavyotawadha kwa Swala. Kisha jilaze juu ya ubavu wako wa kulia.”

Na kauli yake:

“Ukishuka kwenye tandiko lako na hali ya kuwa ni mwenye tohara ufanye mto mkono wako wa kulia.” (Abu Dawud).

4) **Asilalie tumbo** lake wakati wa kulala kwake. Si usiku wala mchana kutokana na kauli iliyokuja kwamba Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake amesema:

“Hiyo ni ulalaji wa watu wa motoni.” Na amesema: *“Hakika ulalaji huo haupendi Mwenyezi Mungu Mtukufu.”* (al-Hakim).

5) Anatakiwa kuleta dhikiri zilizopokelewa na miongoni mwanzo ni:

a) **Anatakiwa aseme:**

“Kutakasika na sifa zote za upungufu ni kwa Allah na Sifa Njema ni za Allah na Allah ni Mkubwa Zaidi. Atasema hivyo mara thelathini na tatu, kisha atasema: “Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah Peke Yake hali ya kuwa hana mshirika ni Wake Yeye Mwenyewe Ufalme na ni Zake Yeye Sifa Njema na Yeye juu ya kila jambo ni Mwenye Uwezo Mkubwa sana.”

Kutokana na Kauli ya Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake) akimwambia Ali na Fatma رضي الله عنهما na huku walikuwa wameomba kwake awapatie mtumishi awasaidie nyumbani.

“Je ni wafahamisheni juu ya jambo ambalo ni bora kuliko kile ambacho mmekiomba, mkienda kwenye malazi yenu mtakaseni (Allah) mara thelathini na tatu, na msifuni mara thelatini na tatu na mtukuzeni mara thelathini na nne na kufanya hivyo ni bora kwenu kuliko mtumishi” (Bukhari).

b) **Asome Fatiha na mwanzo wa Al-Baqarah** mpaka *muflihuun* na Ayat *Al-Kursiyy* na mwisho wa “*Surat Al-Baqarah – Lillahi Mafi Ssamawat* mpaka mwisho wa sura kutokana na (maneno) yaliyokuja katika kulipendekeza hilo.

c) **Afanye maneno ya mwisho atakayoyasema ni dua** hii iliokuja kutoka kwa Mtume ﷺ:

“Kwa Jina Lako Ewe Mola wangu wa Haki nimeuweka ubavu wangu na kwa jina Lako nitaunyanyua, Ewe Mola wangu wa Haki ukikamata nafsi yangu na kuomba uighufirie na ukiiachia nakuomba uihifadhi kwa kile ambacho unawahifadhi Kwako waja Wako wema Ewe Mola wangu wa Haki hakika mimi nimeisalimisha Kwako nafsi yangu na nimeyategemeza Kwako mambo yangu, na nimeuegemeza Kwako mgongo wangu, naomba msamaha Wako na ninarejea Kwako na ninakiamini Kitabu Chako ambacho umekiteremsha na Mtume Wako ambaye Umempeleka. Nisamehe mimi kwa niliyoyatanguliza na niliyoyachelewesha na niliyoyafanya kwa siri na niliyoyafanya kwa uwazi na yale ambayo Wewe unayajua zaidi kuliko mimi. Wewe ndiye Mwenye kutanguliza na Wewe ndiye Mwenye kuchelewesha. Hapana Mola ila Wewe. Ewe Bwana wangu nikinge na adhabu Yako, siku utakapowafufua waja Wako.” (Bukhari, At-Tirmidhi, na Imamu Ahmad).

d) **Atasema atakapoamka katika kulala kwake:**

“Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah Peke Yake hana mshirika ni Wake Yeye Ufalme, na ni Zake Yeye Sifa Njema na Yeye juu ya kila jambo ni Mwenye Uwezo Mkubwa Sana. Kutakasika na sifa za upungufu ni kwa Allah na Sifa Njema ni za Allah na hapana Mola Mwenye Haki ya Kuabudiwa ila Allah na Allah ni Mkubwa Sana. Hapana

kukengeuka kuepukana na maasi na hapana nguvu juu ya kufanya ibada ila kwa msaada wa Allah.”

Na aombe chochote anachokitaka kwani yeye atakubaliwa kutokana na Kauli yake Mtume ﷺ.

“Mwenye kuvua nguo zake usiku akasema dua hiyo wakati wa kuamka (mpaka mwisho), Kisha akaomba atakubaliwa maombi yake.” (Bukhari).

Akisimama akatawadha na akaswali itakubaliwa Swala yake au aseme:

“Hapana Mola ila Wewe, kutakasika na sifa za upungufu ni Kwako, Ewe Mola wa Haki ninakutaka msamaha wa madhambi yangu na ninakuomba Rehema Yako. Ewe Mola wa Haki niongezee elimu na wala usiuponde moyo wangu baada ya kuwa umeniongoza na nipe kutoka Kwako Rehema hakika Wewe ndiyo Mpaji.”

6). Anatakiwa kuleta dhikri zifuatazo pindi akiamka asubuhi:

a) Atasema wakati akiamka na kabla hajasimama kutoka katika tandiko lake:

“Sifa njema ni za Allah ambaye ametupa uhai baada ya kutufisha na ni Kwake tu ufufuo.”

b) Anyanyue macho yake kuyaelekeza mbinguni na asome:

“Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi – aya kumi zilizo mwishoni mwa Al-Imrani pindi *“Nilipolala kwa shangazi yangu atakaposimama kwa Swala ya Tahajuud, kutokana na kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنه*.

“Nililala kwa shangazi yangu Maimuna, mke wa Mtume ﷺ, alilala Mtume (Rehema na Amani ziwe juu yake) mpaka nusu ya usiku au kabla yake kidogo au baada yake kidogo kisha akaamka akawa anaufuta usingizi usoni kwake kwa mkono wake, kisha akazisoma ayah kumi za mwisho katika Surat-Al-Imran kisha akasimama kwenda kwenye kiriba kilichotundikwa akatawadha vizuri kutoka kwenye hicho kiriba, kisha akasimama akaswali.” (Bukhari).

c) Anatakiwa kusema mara nne:

“Ewe Mola wangu wa Haki hakika mimi nimepambazukiwa pamoja na Sifa Zako ninakushuhudiza na kuwashuhudiza wachukuzi wa Arshi Yako na Malaika Wako, na viumbe Wako wote hakika Wewe Ndiye Allah ambaye hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa ila Wewe na kwamba Muhammad ni mja Wako na Mjumbe Wako.” Kutokana na Kauli yake Mtume ﷺ, *“Mwenye kuyasema maneno hayo mara moja tu ataiacha huru Mwenyezi Mungu robo yake (ya mwili wake) na moto na atakayesema haya mara mbili atamwacha nusu yake, na atakayesema mara tatu ataacha robo tatu na atakayesema mara nne Allah atamwacha huru na moto.”* (Abu Dawud).

d) **Atasema atakapoweka mguu wake** katika kuzingiti cha mlango hali ya kuwa anatoka:

“Natoka kwa Jina la Allah, nimetegemea juu ya Allah hapana kukengeuka kuepukana na maasi na hapana nguvu juu ya kufanya ibada ila kwa msaada wa Allah.” Dua hii ni kutokana na Kauli ya Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake. *“Mja atakayesema maneno hayo, huambiwa umeongozwa na umetoshelezewa.”* (At-Tirmidhi).

e) **Atakapokiacha kizingiti atasema:**

“Ewe Mola wa Haki, nataka hifadhi Kwako, dhidi ya kupotea au kupotezwa au kuteleza au kutelezesha au kudhulumu au kudhulumiwa au kufanya ujinga au kufanyiwa ujinga.” Na hilo ni kutokana na maneno ya Ummu Salama: *“Hakutoka Mtume wa Allah ﷺ nyumbani mwangu kiasi ila hunyanyua macho yake mbinguni na husema: “Ewe Mola wangu wa Haki mimi nataka hifadhi Kwako dhidi ya kupotea au kupotezwa.”* (Abu Dawud). Isome hadithi hiyo.



Mlango wa Tatu
Tabia Njema



Mada ya Kwanza

Tabia Njema na Maelezo Yake

Tabia ni hali iliyothibiti katika nafsi huchimbuka kutokana na hali hiyo matendo ya kimatakwa ya hiyari miongoni mwa matendo mema, maovu, na mazuri au mabaya. Hai hiyo huathiriwa na malezi yawe ni malezi mema au mabaya. Itakapolelewa hali hiyo na mtu kuzoweshwa kuweka mbele haki, mema na kufanya mema na kheri, hali kadhalika ikazoeshwa katika kupenda uzuri na kuuchukia ubaya na hii ndio ikawa tabia yake basi baada ya hapo yanachimbuka kutokana nayo matendo mazuri kwa urahisi, pasi na kujilazimisha husemwa kuwa: **“Mtu huyo ana tabia njema.”**

Matendo mazuri yanayofanywa na mtu huenziwa bila ya taklifu yoyote kutoka kwa mtendaji wa matendo hayo. Mfano wa sifa hizi ni kama vile; tabia ya kuona haya, busara, upole, subira, uvumilivu, ukarimu na ushujaa, uadilifu, wema na yasiyokuwa hayo katika mambo bora ya kitabia na ukamilifu wa kinafsi.

Nafsi ikipuuzwa na kuachiwa kwa kutopewa maadili mema na iwapo haikusimamiwa kwa kukuza vyanzo vya wema vilivyopo ndani ya nafsi yake au vikapewa malezi mabaya ikafikia kuwa kila baya likaona ni jema katika nafsi yake na jema likawa linachukiwa na nafsi hiyo, na yakawa mambo maovu na ya kipuuzi maneno na matendo yake maovu yanatoka katika nafsi bila ya taklifu. Mtu wa namna hii huitwa ni mtu mwenye maadili mabaya, na huitwa maneno ya matendo machafu ambayo yanatokana na hiyo nafsi kuwa ni tabia mbaya. Mfano wa tabia hizi mbaya ni kama vile; kufanya khiana, kusema uongo, na mgumu kuzoeleka kwa neno na matendo machafu.

Ni kutokana na msingi huu Uislamu umetukuza sana na kuhimiza tabia njema na umetoa wito katika kuwalea Waislamu juu ya tabia njema na kuziendeleza katika nafasi zao na umezingatia imani ya mtu kutokana na mema yake, nafsi yake, na Uislamu wake kutokana na uzuri wa tabia zake. Allah amemsifu Mtume wake kwa uzuri wa tabia yake kwa kusema:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

“Na hakika wewe uko juu ya tabia tukufu.” (al-Qalam: 4)

Aidha amemwamrisha kujipamba kwa tabia njema pale Aliposema:

أَدْفَعِ بِأَلَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ

وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿١١﴾

“Liondoe ovu kwa lile jema ghafla yule ambaye pana baina yako na baina yake uadui anakuwa kama vile ndugu yako mpenzi mwingi wa Huruma.” (Fussilat:34).

Na Amezifanya tabia njema kuwa ni sababu ya mtu kupata pepo ya juu:

وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ

لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٤﴾ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ وَالْكَبِيرِ وَالصَّغِيرِ

وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ ۗ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣٥﴾

“Na yakimbilieni maghfira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyo wekwa tayari kwa wachamngu, Ambao hutoa wanapo kuwa na wasaa na wanapo kuwa na dhiki, na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema;” (al-Imran:133-134).

Na alimpeleka Mtume wake ﷺ kwa kuikamilisha tabia njema, Mtume ﷺ amesema kuhusu hili,

“Hakika hapana jambo jengine nimepelekwa ili nitimize tabia njema.” (al-Bayhaqi).

Mtume ﷺ amebainisha sehemu zaidi ya moja kuhusu ubora wa tabia njema,

“Hakuna kitu kilicho kizito zaidi katika mizani kuliko tabia njema.” (At-Tirmidhi).

Hali kadhalika,

“Wema ni tabia njema.” (Muslim).

“Mkamilifu sawa wa waumini na wa karibu zaidi nami kwa makazi siku ya kiyama ni wazuri wenu wa tabia.” (At-Tirmidhi).

“Na aliulizwa kuhusu ni lipi katika matendo lililo bora?” Akasema: “uzuri wa tabia”

Na Amesema,

“Hakika mja hufikia kwa uzuri na tabia zake daraja kubwa za huko akhera na utukufu wa mafikio na wakati yeye ni mdhaifu wa ibada.” (At-Tirmidhi).

Maoni ya Wanazuoni wa Zamani Katika Kuweka Wazi Uzuri wa Tabia:

Al-Hassan amesema: “Uzuri wa tabia ni ukunjufu wa uso, utoaji, na kuzuia maudhi. Ama Abdullahi Ibni Al-Mubarak kuhusu hilo amesema, “Uzuri wa tabia umo katika mambo matatu: “Kujiepusha na mambo yaliyoharamishwa, kutafuta halali na kutosheleza mahitaji ya watu wa nyumbani. Na amesema mwingine: “Uzuri wa tabia ni mtu kuwa karibu na watu, lakini yu mbali katika mambo yao (ya ndani).”

Aidha wengine katika Maulamaa wa *Salaf* walisema, “Uzuri wa tabia ni kuyazuia maudhi na uvumilivu wa muumini.” “Uzuri wa tabia pasiwe na mwingine unayeshughulishwa naye asiyekuwa Allah Mtukufu (maana moyo usishughulishwe na asiyekuwa Allah).”

Hayo ni maelezo ya tabia njema kwa kuzingatia baadhi ya sehemu zake. Ama maelezo yake kwa kuzingatia dhati yake na sifa zake ni kama yalivyotangulia huko nyuma.

Wanazuoni hawa wa *Salaf* katika kuelezea alama ya mtu mwenye tabia njema wamesema, “Awe mwingi wa haya, mchache wa maudhi mwingi wa kufanya mema, mkweli wa ulimi, mchache wa maneno, mwingi wa matendo, mchache wa kuteleza katika makosa, mchache wa kufanya mambo yasiyokuwa na maana

na yasiyomuhusu, mwema, mwenye kuunga udugu, mtulivu, mvumilivu, mwingi wa kushukuru, mwenye kuridhika, mpole, mwenye kutekeleza ahadi, mwenye kujichunga na machafu, si mwenye hasadi, mwenye bashasha na ucheshi anapenda kwa ajili ya Allah na anaridhia kwa ajili ya Allah na anakasirika na kuchukia kwa ajili ya Allah.”

Hizi ni sifa zilizotajwa za mtu mwenye tabia njema. Na katika vipambanuzi na milango ifuatayo patalezwa kila sifa moja katika sifa za tabia njema peke yake. Na kwa kuikamilisha mikusanyiko ya sifa hizo zitaonekana tabia njema kwa kuzingatia mafungu yake na ni rahisi kujua na kumuona mwenye tabia njema kwa kuizingatia sifa zake.



Mada Ya Pili

Subira na Uvumilivu Juu ya Maudhi

Miongoni mwa tabia njema ambazo Muislamu anajipamba nazo ni subira, na kuvumilia maudhi kwa kutaka radhi za Allah Mtukufu.

Ama kusubiri maana yake ni kuifunga nafsi juu ya yale ambayo inayachukia, au kuvumilia mambo yenye kuchukiza kwa namna ya kuridhia na kujisalimisha. Kwa hiyo Muislamu anaifunga nafsi yake juu ya yale ambayo Allah Mtukufu anayachukia, na anailazimisha hiyo nafasi yake, na anaizuia kumuasi Allah Mtukufu, kwa hiyo haipi nafasi ya kuyakaribia, wala haipi ruhusa ya kuyafanya kadri itakavyo kuyafanya hayo kwa maumbile yake, na ikiwa na uchangamfu juu ya hilo.

Na anaidhibiti juu ya mabalaa pindi yakiishukia, haiachii ilalamike wala ichukie kwani kulalamika kama walivyosema watu wa hekima juu ya jambo ambalo limekwishapita ni kujiingiza katika janga, na kulalamika juu ya lile ambalo linatarajiwa ni upuuzi, na kuchukia juu ya yale ambayo yamekadiriwa na Allah ni kumlaumu Allah Aliye Mmoja na Mwenye Kuenza Nguvu.

Muislamu katika hali zote hizo anaomba msaada kwa kumtaja Allah Mtukufu kwa malipo mema juu ya utii, na yale ambayo yameandaliwa kwa watu wake miongoni mwa malipo mengi na thawabu kubwa. Na anakumbuka makemeo ya Allah Mtukufu kwa wenye kumbughudhi na kumuasi, miongoni mwa adhabu yenye kutia uchungu na ghadhabu kali sana.

Anakumbuka kuwa makadirio ya Allah yanakwenda, na kwamba maamuzi ya Allah Mtukufu ni uadilifu na hukumu Zake zinapita awe amevumilia na mja au amelalamika, isipokuwa iwapo atasubiri atapata malipo na akilalamika atapata madhambi.

Maadamu kutolalamika ni katika tabia ambazo zinachumwa na kupatikana kwa namna ya mazoezi na kutoa juhudi, Muislamu baada ya kuhitajia kwake Allah anampa subira. Yeye anapata subira kwa kukumbua maamrisho yaliyokuja katika kusubiri na malipo yaliyoahidiwa ya subira.

Kama inavyosema kauli Yake Allah Mtukufu:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اَصْبِرُوْا وَصَابِرُوْا وَرَابِطُوْا وَاَتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُوْنَ ﴿٢٠٠﴾

“Enyi mlio amini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa .” (3:200).

Tunajifunza katika aya hizi zifuatazo,

“Na takeni msaada kwa kusubiri na kuswali.” (Al-Baqarah:45).

وَأَصْبِرْ وَمَا صَبْرُكَ إِلَّا بِاللّٰهِ ۗ

“Na subiri haikuwa subira yako ila kwa Allah.” (16:127).

وَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا أَصَابَكَ ۖ إِنَّ ذٰلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٧﴾

“...na subiri kwa yanayo kupata. Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa...” (31:17)

Na wape habari njema wenye kusubiri ambao pindi unapowapata msiba wanasema:

إِنَّا لِلّٰهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ ﴿١٥٧﴾ أُوْلَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ
وَرَحْمَةٌ وَأُوْلَئِكَ هُمُ الْمُتَهْتَدُونَ ﴿١٥٨﴾

“Hakika sisi ni wa Allah na hakika sisi kwake ni wenye kurejea, hao wana msamaha kutoka kwa Bwana wao na Rehema na hao ndio wenye kuongoka” (2:155-157)

“Na tutawalipa wale ambao wamesubiri malipo yao mazuri zaidi kuliko yale ambayo walikuwa wanayatenda.” (16:96)

“Na tukawafanya miongoni mwao waongozi wanao ongoa watu kwa amri yetu, walipo subiri na wakawa na yakini na Ishara zetu...” (32: 24)

“Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu.” (39: 10)

Ama kauli ya Mtume ﷺ juu ya haya tunajifunza kama ifuatayo katika Hadithi zake tukufu, “Na mwenye kujichunga na maovu Allah atamzidishia uwezo wa kujichunga, na mwenye kujitosha atamtosheleza Allah, na Mwenye kusubiri atamuongezea Allah subira na hakupewa mtu yeyote kipawa kilicho bora sana na kikunjufu zaidi kuliko subira.” (Bukhari).

“Lililoshangaza hasa ni jambo la muumini hakika ya jambo lake lote ni kheri na hali kuwa hilo kwa mtu yeyote ila kwa muumini, ikimpata furaha hushukuru kukawa kushukuru ni kheri kwake na likumpata dhara husubiri kukawa kusubiri ni kheri kwake.” Muslim).

Na Kauli yake Mtume ﷺ akimwambia binti yake hali ya kuwa amempelekea ujumbe akimuomba aende kwake wakati mtoto wake huyo akiwa mahututi Mtume akamwambia mjumbe wake: **Msalimie na umwambie:**

“Hakika ni cha Allah alichokichukuwa, na ni chake alichokitoa, na kila kitu mbele yake kinakwenda kwa muda maalumu, Kwa hiyo na asubiri na amwachie Allah.” (Bukhari).

Na Kauli yake:

“Anasema Allah Mwenye uwezo na Aliyeshinda na Kutukuka Nitapomuonja mja wangu kwa wapenzi wake wawili (macho yake) akasubiri nitambadilishia kwa macho mawili hayo pepo.” (Bukhari).

Na Kauli yake:

“Yule ambaye Allah anamtakia kheri humpa mitihani.” (Bukhari).

Na Kauli yake:

“Hakika ukubwa wa malipo unakwenda sambamba na ukubwa wa majaribio. Na kwamba Allah, Akiwapenda watu huwajaribu mwenye kuyaridhia majaribio ni yake radhi na mwenye kuyachukia ni juu yake machukivu.” (Tirmidhi).

Na Kauli yake (Rehema na Amani ziwe juu yake):

“Hayatakosa majaribio kwa muumini katika nafsi yake na watoto wake na mali yake mpaka akutane na Allah hali ya kuwa hapana juu yake kosa lolote.” (At-Tirmidhi).

Ama kuvumilia maudhi huko ni kusubiri lakini pia kugumu sana. Hiyo ndio bidhaa ya watumwa kweli na alama ya watu wema na hakika yake ni kuudhiwa Muislamu katika ajili ya Allah ﷻ akasubiri na kavumilia. Kwa hiyo harudishi ovu kwa lililokuwa jema na wala haadhibu kwa sababu ya utashi wake na wala haathiriki kwa sababu yalinalogusa hadhi yake (shakhsia yake). Muda wa kuwa hilo ni katika njia ya Allah na lingepelekea kupata radhi ya Allah na kiigizo chake akitaka hilo ni Mitume na watu wema, kwa sababu ni nadra sana kupatikana ambaye hakuudhiwa katika wao kwa ajili ya Allah na pia ni nadra kupatikana ambaye hakuonjwa katika njia yake.

Amesema Abdullahi Ibni Masoud رضى الله عنه:

“Kama kwamba ninamtazama Mjumbe wa Allah ﷻ akimzungumzia Nabii katika Manabii (Rehema za Allah amani Zake ziwe juu yao), walimpiga jamaa zake na wakamtoa damu na akiwa anapungusa damu usoni kwake na huku anasema; “Ewe Mola wangu wa haki wasamehe jamaa zangu kwani wao hawaelewi ubaya wa wanachokifanya.” (Bukhari na Muslim).

Hii ni sura moja katika sura mojawapo za uvumilivu wa maudhi yaliyomtokea Mtume wa Allah ﷻ. Na sura nyingine ni pindi bedui aliposema baada ya Mtume kugawa mali, “Huu ugawaji haukusudiwa Dhati ya Allah ikamfikia habari hiyo Mtume wa Allah ﷻ vikawa vyekundu vitefute vyake viwili, kisha akasema:

“Amrehemu Alah ndugu yangu Nabii Mussa kwa hakika aliudhiwa kwa mengi kuliko haya lakini akasubiri.” (Bukhari na Muslim).

Na amesema Khabbab Ibni al-Aratt رضي الله عنه kuwa, ‘Tulishitaki kwa Mtume wa Allah ﷺ na hali yakuwa yeye amefanya mto shuka yake akiwa katika kivuli cha Al-Kaba, tukasema: Hivi hatulipizi (kwa maadui zetu) hivi hutuombei?’ Mtume ﷺ akamjibu:

”Hakika walikuwa waliyokuwa kabla yenu anachukuliwa mtu anachimbiwa shimo katika ardhi, kisha hutiwa humo kisha huletwa msumeno huwekwa kichwani kwake kisha hupasuliwa nusu mbili na anachanwa kwa chanuo za chuma katika sehemu iliyo kati ya nyama yake na mifupa yale na huko halimzuiii kufata dini ya Allah” (Bukhari).

Allah ametusimulia kuhusu Mitume na Amezungumzia kuhusu Kauli yao kuwa ni wenye kuvumilia maudhi,

وَمَا لَنَا إِلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَى اللَّهِ وَقَدْ هَدَانَا سُبُلَنَا وَلَنْصَبِرَ عَلَىٰ مَا

ءَاذَيْنَا وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿١٤﴾

“Na tuna nini hata tusimtegemee Mwenyezi Mungu, na hali Yeye ametuongoa kwenye Njia zetu. Na hapana shaka sisi tutayavumilia hayo maudhi mnayo tuudhi. Na juu ya Mwenyezi Mungu wategemee wanao tegemea.” (14:12).

Issa mwana wa Mariam aliwaambia wana wa Israel.

“Kwa hakika mmeambiwa huko nyuma kwamba jino kwa jino na pua kwa pua na mimi ninawaambia: Msipambane na shari kwa kufanya shari bali mwenye kukupiga shavu lako la kulia mgeuzie la kushoto na mwenye kuchukua kwako shuka yake ya juu mpe ya chini.” Na walikuwa baadhi ya maswahaba wa Mtume wa Allah wakisema: “Hatukuwa tunaihesabu imani ya mtu kuwa ni imani muda wa kuwa hakusubiri juu ya maudhi.. Na kutokana na mwangaza wa hizi sura zenye kuzungumziana mifano iliyo hai ya kusubiri na kuvumilia anaishi Muislamu mwenye kusubiri wala haondoi baya kwa baya lakini analiondoa baya kwa jema na anasamehe na anasubiri na anasitiri. **“Na kwa hakika mwenye kusubiri na kusamehe hakika kufanya hivyo ni katika mambo yanayokusudiwa.” (42:43).**

Mada ya Tatu

Kumtegemea Allah Kisha Kujitegemea Mwenyewe

Muislamu haoni kumtegemea Allah Mtukufu katika matendo yake yote kuwa ni wajibu wa kitabia tu bali analiona hilo kuwa ni jambo la lazima kidini, na analihesabu kuwa ni itikadi ya Kiislamu. Na hivyo ni kutokana na Allah kuliamrisha jambo hilo katika msemu Wake.

وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٢٣﴾

“Na juu ya Allah tutegemeeni mkiwa ni waumini.” (al-Maidah: 23).

Na kauli yake:

وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٢٢﴾

“Na juu ya Allah na wategeme waumini.” (al-Imran: 122).

Kwa msingi huu imekuwa kumtegemea Allah ni jambo lisilokuwa na mipaka hii ni sehemu mojawapo ya itikadi ya anayemwamini Allah Mtukufu.

Muislamu anapomuabudu Allah Mtukufu kwa kumtegemea na kujituma kikamilifu mbele Yake hafahamu katika kumtegemea Allah yale ambayo wanayafahamu wasio ufahamu Uislamu na maadui wa itikadi ya Waislamu. Maadui hufahamu hivyo kuwa hilo ni tamko tu linalotamkwa na ndimi. Na wala halizingatiwi na nyoyo? Na inatikusika kwalo midomo na wala hazilifahamu akili. Au kulitafakari fikra, au kumtegemea Allah ni kuziacha sababu, na kuacha kufanya kazi, na kutosheka na kuridhika na unyonge wa uduni chini ya nembo ya kumtegemea Allah. Na kuyaridhia yale ambayo yanaenda kwa makadirio ya Allah, Hapana!! Bali Muislamu anafahamu kumtegemea Allah ambako ni sehemu ya imani na itikadi yake kuwa ni kumtii Allah kwa kuzihudhurisha sababu zote zinazotakiwa kwa kazi yoyote ile miongoni mwa kazi ambazo anataka kuzifanya na kuziingia. Hatumaini kupata matunda pasina kutanguliza sababu zake, na wala hatarajii matokeo yoyote pasina kuweka utangulizi wake. Isipokuwa suala la kuleta matunda ya sababu hizo, na kuleta matokeo ya utangulizi huo analiegemeza kwa

Allah (s.w.t.) Kwa sababu Yeye tu ndiye muweza wa hilo. Kwa hiyo kumegemea Allah mbele ya Muislamu ni kitendo na natarajio, pamoja na utulivu wa moyo, utulivu wa nafsi na itikadi isiyoyumba. Kwamba alilolitaka Allah linakuwa na ambalo hakulitaka haliwi, na kwamba Allah hapotezi malipo ya wale wenye kufanya matendo mema.

Muislamu anapoamini taratibu za kimaumbile za Allah katika Ulimwengu huu anazitayarishia amali taratibu hizo na sababu zake zinazotakiwa kwa matendo hayo, na anatoa juhudi zote katika kuzihudhurisha na kuzikamilisha. Kamwe haamini ya kuwa sababu pekee zinatoshia kuhakikisha malengo, na kuzifanikisha. Hapana, bali anaona kwamba kuweka sababu zaidi ya moja kwenye kito kimoja ni jambo ambalo ameliamrisha Allah. Inapasa kumtii katika hilo kama mtakavyomtii katika mambo mengine ambayo ameamrisha na ambayo amekataza.

Ama kupata matokeo, na kufuzu katika matakwa yake hakika yote hayo ameyategemeza kwa Allah Mtukufu. Kwa sababu Yeye pekee ndiye anayeweza kulifanya hilo na wangapi wenye kufanya kazi na wenye kuteseka hawakula matunda ya kazi zao, na taabu zao? Ni kutokana na msingi huu umekuwa mtazamo wa Muislamu juu ya sababu. Ni kwamba kuzitegemea sababu pekee na kuzizingatia kuwa ndizo kila kitu katika kuhakikisha kuwa matakwa yake yanatekelezwa ni ukafiri na ni shirki. Anajiepusha na hayo, na kwamba kuacha sababu zinazotakiwa kwa kazi yoyote na kuzipuuza na hali ya kuwa mtu anaweza kuziandaa na kuzipitisha ni kuwa nje ya utii wa Allah. Hayo ni maasi ambayo Allah ameyaharamisha na mtu kwa hayo anatakiwa amtake *maghfira* Allah (.w.t.). Muislamu katika kuzitazama kwake sababu hizo anachukua falsafa yake kutoka katika Uislamu na mafundisho ya Mtume Muhammad ﷺ. Kwani Mtume wa Allah ﷺ katika vita vyake vingi alikuwa haingii katika vita vyovyote mpaka aviandalie maandalizi na atayarishie sababu zake. Kwa hivyo alikuwa akichagua mahali pa kuanzia vita na wakati wake. Kwani imepokewa kutoka kwake kwamba alikuwa hafanyi mashambulizi yoyote wakati wa joto mpaka anga lipoe na hali ya hewa iwe nzuri. Mwishoni mwa mchana baada ya kuwa kisha uandaa mpango wake na kisha zipanga safu zake na akimaliza maandalizi haya ya kimaada na sababu za kufanikiwa katika kanuni za kidunia kwa ajili ya kufaulu katika vita, hunyanyua mikono yake akimuomba Allah (Aliyeshinda na kutukuka) kwa kusema,

“Ewe Mola wangu wa Haki Mteremsha kitabu na mwendesha mawingu na Mwenye Kuyashinda makundi. Washinde maadui na tupe nusra juu yao.” (Bukhari, Atirmidhy na Muslim).

Hivyo ndivyo ulivyokuwa muongozo wake ﷺ katika kukusanya kati ya sababu za kimaada na za kiroho kisha hulifungamanisha jambo la kufaulu kwake juu ya Bwana wake na hutungika kufuzu kwake na matakwa ya Mola wake. Huu ni mfano wa kwanza.

Ama mfano mwingine ni kwamba Mtume ﷺ alingoja amri ya Bwana wake katika kuhamia kwenda Madina baada ya kuwa sehemu kubwa ya swahaba zake walishahama kwenda huko. Ikamjia idhini kutoka kwa Allah Mtukufu ya kuhama, sasa ni zipi taratibu ambazo alizifanya Mjumbe wa Allah Rehema na Amani ziwe juu yake, katika kuhama kwake?

Taratibu alizozifanya ni kama zifuatazo:-

- 1) Ni kumleta rafiki bora miongoni mwa rafiki zake, naye hakuwa mwingine bali ni rafiki yake mkubwa na sahibu yake, yaani Abu Bakr Sawidiq رضي الله عنه kuelekea Madina.
- 2) Kutayarisha andao la safari miongoni mwa chakula na kinywaji, Asmaa binti Abubakar alivifunga hivyo kwa mkanda wake mpaka akapewa jina maarufu la *‘Dhatu nnitwaqayni*
- 3) Kuandaa kipandwa kizuri mno! Ili kukipanda katika safari hii ndefu ngumu.
- 4) Kumleta mtaalamu wa Jiografia za jangwani, mtu anayezijua njia za eneo hilo ambazo ni ngumu ili awe ni mwelekezaji na kiongozi katika safari hii ngumu.
- 5) Alipotaka kutoka kwenye nyumba yake ambayo ilikuwa imezingirwa na maadui na ilhali yumo ndani ya nyumba hiyo na hakuwa na uwezo wa kuponyoka Mtume ﷺ alimwamrisha mtoto wa Ami yake Ali Ibn Abi Twalib رضي الله عنه kulala katika tandiko lake. Kwa kumbabaisha adui ambaye hakuacha kuwa anangojea kutoka kwake nyumbani ili amvamie. Kisha alitoka na kumuacha adui anangojea kuamka kwake kutoka katika tandiko lake ambalo lilikuwa linaonekana kupitia pasuko za mlango.

6) Mushirikina Walipokuwa wakimsaka kwa hima yeye na rafiki yake Abu Bakar Swiddik رضي الله عنه ambaye alihama pamoja naye, alishukia katika pango la mlima Thaur akaingia humo ili ajifiche na macho ya wenye kumtafuta, watu waliokuwa na usongo na mfundo juu yake.

7) Abu Bakar Alipomwambia Mtume عليه السلام maneno haya, ‘lau kwamba mmoja wao angetazama chini ya nyayo zake angetuona ewe Mjumbe wa Allah.’ Mtume عليه السلام akamwambia Abubakar,

“Nini dhana yako Ewe Abu Bakar kwa wawili ambao watatu wao ni Allah.” (Bukhari).

Ni kutokana na tukio hili ambalo unadhihiri ndani yake ukweli wa imani pamoja na kumtegemea Allah (s.w.t.) watu wanashuhudia kuwa Mtume عليه السلام alikuwa hazipingi sababu moja kwa moja na alikuwa hazitegemei vile vile moja kwa moja. Lakini baada ya kutekeleza sababu ni juu ya Muumini kumuachia Allah (s..w.t.) na kuegemeza jambo lake Kwake akiwa katika imani na utulivu.

Hakika Mtume عليه السلام alipomaliza kutafuta na kutumia njia zote katika kutafuta kuokoka hali iliyomfanya kwenda kwenye pango lenye kiza linalokaliwa na ng’e na nyoka alisema katika imani ya muumini na yakini ya mwenye kumtegemea Allah akimwambia rafiki yake wakati alipofikwa na khofu.

“Usihuzunike hakika Allah Yuko pamoja nasi, nini dhana yako Ewe Abu Bakar kwa watu wawili (ambao) watatu wao ni Allah?” (Bukhari).

Ni kutokana na muongozo huu wa Mtume عليه السلام na mafundisho yake matukufu, Muislamu anajifunza kutengeneza mtazamo wake katika kuchukua na kufuata sababu. Kwa hiyo yeye hakuwa katika hizo mwenye kuzusha au kuzidisha ambayo Mtume عليه السلام hakufundisha au kuelekeza. Katika maelekezo ambapo Muislamu anakuwa ni mfuataji wa kuigiza yale yaliyofanywa na Mtume na kuelekezwa.

Ama suala halisi la mtu kujitegemea kwa hakika Muislamu ufahamu wake ni tofauti na ufahamu waliokuwa nao wenye kuzuiliwa nafsi zao kutokana na maasi kuwa maana halisi ya kujitegemea ni kukata mawasiliano na Allah (Mtukufu), na kuwa mja ndiye anayeumba matendo yake, na mwenye kujipatia pato lake kwa

jitihada binafsi, na kwamba hapana uhusiano wowote na Allah katika hilo. Ametukuka Allah na yale ambayo wanayasawiri watu hawa.

Kwa hakika hapana jingine Muislamu anaposema kuwa ni wajibu kujitegemea katika uchumi na kufanya kazi anakusudia kwa kusema hivyo kwamba yeye hatadhihirisha uhitaji wake kwa yeyote asiyekuwa Allah. Na haoneshi uhitaji wake kwa asiyekuwa Mola wake. Anapoweza kufanya mwenyewe kazi yake hampi mwingine kumfanyia, na ikiwezekana kwake kuiondoa haja yake yeye mwenyewe haombi msaada wa mwingine. Na wala hataki msaada wa yeyote asiyekuwa Allah kwa sababu kutaka msaada kwa mtu mwingine ni kufungamana na moyo wa asiyekuwa Allah na hilo ndilo jambo ambalo Muislamu halipendi na hataki kuliridhia.

Muislamu katika kufanya hivi anafuata njia ya watu wema waliotangulia (*salaf*) na anaelekea njia za wa kweli. Kwani ilikuwa ni tabia ya mja wao kinapoanguka mti au bakora aliushika kutoka mikononi mwakie na hali ya kuwa amepanda juu ya farasi wake, kawaida ya maisha ya *Salaf* ni kuwa huteremka chini mwenyewe ili akichukue wala hamwombi mtu yeyote kumpa na hii ni katika jumla ya kuonyesha tabia ya kutokutaka makuu.

Mjumbe wa Allah ﷺ alikuwa akichukua ahadi kwa Muislamu juu ya kusimamisha Swala na kutoa zaka na hakuwa akimwomba yeyote ya kuwa Allah (Mtukufu) haja zake.

Muislamu wakati anaishi juu ya itikadi hii ya kumtegemea Allah na kujitegemea yeye mwenyewe, anaijenga itikadi yake hii na anaiendeleza tabia yake hiyo kwa kuzingatia mafundisho ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.) na hadithi tukufu za Mtume ﷺ ambazo amechukua kutoka ndani yake itikadi yake na tabia zake, na hilo ni kama anavyosema Allah katika kauli yake,

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْحَيِّ الَّذِي لَا يَمُوتُ

“Namtegemea Aliye Hai Ambaye Hafi.” (25:58).

Na kauli yake

وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

“...wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa.” (3:173).

Na kauli yake:

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ

“*Hakika Allah Anawapenda wenye kutegemea (Kwake).*” (3:159).

Na Kauli ya Mtume ﷺ

“Lau kama nyinyi mnamtegemea Allah ukweli wa kumtegemea mngeruzukiwa kama ambavyo anavyowaruzuku ndege wanatoka asubuhi na njaa na wanarudi jioni wakiwa wameshiba.” (Ahmad).

Na Kauli yake wakati anapotoka nyumbani mwake:

“Natoka kwa kulitaja jina la Allah nimemtegemea Allah na hapana kukengeuka kuepukana na maasi na hapana nguvu juu ya kufanya ibada ila kwa msaada wa Allah.”

Na kauli yake kwa wale watu sabini elfu ambao wataingia peponi pasina hisabu.

“Ni wale ambao hawaombi kufanyiwa tiba ya kusomewa wala haichomwi miili yao kwa kujitibu wala hawaoni mkosi kwa kupitiwa na ndege na juu ya Bwana wao wanategemea.” (Ahmad na Muslim).



Mada ya Nne

Kuwatanguliza Wengine na Kupenda Kheri

Miongoni mwa tabia za Muislamu ambazo amezichuma kutokana na mafunzo ya Dini yake, na mema ya Uislamu wake ni kuwatanguliza wengine kuliko nafsi yake. Kwa hiyo anaweza akawa na njaa lakini akaona bora ashibe mwingine, na akabaki na kiu lakini mwenzake kesho ondokewa nacho. Bali huenda akafa kwa ajili ya uzima wa wengine. Hili si jambo la ajabu wala geni kwa Muislamu ambaye roho yake imejaa mambo ya kheri yenye kupelekea ukamilifu wa tabia njema, na ikapambika nafsi yake na pambo la kheri na kupenda ubora na uzuri. Hayo ndiyo mapambo mazuri na kupaka uzuri wa rangi Allah alioukusudia, “*Na ni nani zaidi mwenye kupamba zaidi kuliko kupamba kwa Allah?*”

Muislamu katika kuwatanguliza kwake watu wengine na kupenda kwake kheri anaifuata njia ya watu wema waliyotangulia na anaita katika njia ya watu wa mwanzo waliofuzu ambao Allah Amesema katika kuwasifu,

وَيُؤْتِرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَن يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ

فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥٩﴾

“...wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyo pewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa..” (59:9).

Hakika tabia zote njema alizo nazo Muislamu zimechukuliwa kutoka kwenye chemchem ya hekima zake Mtume Muhammad ﷺ na yamechukuliwa kutokana na mmimiminiko wa rehema za Allah (s.w.t.). Kwa mfano kauli yake Mtume Mtukufu ambayo imepokelewa kwa pamoja na Bukhari na Muslim:

“Hawi muumini kamili mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake lile ambalo analipendelea ndani ya nafsi yake.” (Bukhari na Muslim).

Muislamu kwa kusoma hadithi hii tabia yake huzidi kuwa njema na hutukuka. Ama atakaposoma maneno matukufu ya Allah.

“Na wanawatanguliza wengine kuliko nafsi zao japokuwa wao wana dhiki, na wenye kulingwa na ubakhili wa nafsi zao basi hao ndio wenye kufuzu.”

Basi hisia ya Muislamu huzidi kwa kuipenda kheri na kuvutika nayo katika kuwatanguliza watu wengine kuliko nafsi yake, mke wake, na mtoto wake, hisia hizi kuongezeka zaidi na kustawi.

Hakika ya mja wa Kiislamu anaishi hali ya kufungamana na Allah (s.w.t.), ulimi wake hauachi kuwa mbichi kwa kumtaja Allah. Na moyo wake hauachi kuwa wenye kudumu juu ya mapenzi yake, akitembea katika ufalme wa uchaguzi anavuna na kuchukua mazingatio, na akiyapitisha mawazo yake juu ya mfano wa aya zilizo katika Suratil Al-Mazzammil na Faatir.

وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ مِنْ خَيْرٍ يَجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرًا وَأَعْظَمَ أَجْرًا

“Na chochote mnachokitanguliza kwa nafsi zenu mtakikuta mbele ya Allah kikiwa ni bora zaidi na kikubwa sana kwa malipo.” (73: 20).

وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً يَرْجُونَ تَجِرَةً لَّنْ تَبُورَ ﴿٣٥﴾

لِيُؤْفِقَهُمْ أَجُورَهُمْ وَيَزِيدَهُمْ مِنْ فَضْلِهِ إِنَّهُ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٦﴾

“...na wakatoa kwa siri na kwa dhaahiri katika tulivyo waruzuku, hao hutaraji biashara isiyo bwaga. Ili Yeye awalipe ujira wao kwa ukamilifu, na awazidishie kutokana na fadhila zake. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe Mwenye shukrani..” (35:29-30).

Muislamu huyu baada ya kuzingatia hayo yaliyopita ataidharau dunia na ataiona kuwa si chochoe si lolote na ataichagua akhera na kuitanguliza. Mtu kama huyu na hali yake ndio imeshakuwa hivi kwa nini asitoe mali yake kwa ukarimu, na

kwa nini asiipende kheri na asimtangulizie mwenzake mwenye kujua kuwa kile ambacho anakitua leo atakikuta kesho kikiwa bora zaidi na kikubwa kwa malipo. Mapenzi kwa wengine yanajidhihirisha tunaposoma historia katika visa vifuatavyo:

1. Katika jumba la mikutano (*Darun Nadwah*) liliafiki baraza la wazee wa Kiquraish kwa makubaliano ya wote juu ya mapendekezo yaliyotolewa na Abu Murah-laana ya Allah iwe juu yake—mapendekezo yanayotaka auliwe Mtume ﷺ na avamiwe ghafla nyumbani kwake. Maamuzi haya ya dhulma yalimfikia Mtume ﷺ na akawa ameruhusiwa na Mwenyezi Mungu kuhama. Akaazimia kuhama, akamtafuta yule ambaye atalala juu ya tandiko lake usiku ili awadanganye wale wanaomngojea ili wamshambulie, ili aweze kutoka nyumbani na kuwaacha wanamngoja aamke kutoka katika tandiko lake.

Mtume ﷺ akaona kuwa mtu mwenye kufaa katika jambo hili la kujitua mhangana si mwingine zaidi ya mtoto wa ami yake wakati huo ni kijana mdogo, yaani ‘Ali bn Abi Twalib رضي الله عنه. Akampa ushauri juu ya hilo naye Ali hakusita katika kuitoa nafsi yake kwa ukombozi wa Mtume wa Allah ﷺ ili alale katika tandiko ambalo hajui ni wakati gani mikono ya maadui itamnyakua kutoka hapo na kumtupa kwa watu wenye kiu ya damu maadui wa Mwenyezi Mungu. Ama wangependa wamchezee kwa panga zao kama unavyochezewa mpira kwa miguu. Ali akalala na akaona uhai wa Mjumbe wa Allah ﷺ ni bora kuliko uhai wake, pamoja na udogo wa umri wake aliweka mfano mzuri sana katika kujitua muhanga na ukombozi. Muislamu anamtanguliza mwenzake kuliko nafsi yake, na anafanya ukarimu hata kwa nafsi yake. Kwa hakika mtu kuitoa nafsi yake ni kilele na ndio ukomo wa juu wa ukarimu wa mtu kufanya.

2) Hudhaifa Al-Adawy alisema, “Niliondoka siku ya vita vya Yarmuk nikimtafuta mtoto wa Ami yangu nikiwa na maji machache na hali ya kuwa ninasemea moyoni mwangu ‘Nikimkuta ni hai bado ana roho nitamnyweshwa na nitajifuta (kwa maji haya) uso wake’, ghafla nikakutana naye, nikamwambia, ‘Nikunyweshe?’ Ghafla tukamsikia mtu mmoja anaugulia huku akitua sauti, ‘aaaha aaah’ ndugu yangu akanipa ishara nimwendee mtu yule, nikamwendea ghafla nikamkuta kuwa ni Hisham bin Al-‘Aas nikamuuliza nikunyweshe” Hapo hapo tukamsikia mwingine vile vile akiwa anaugulia kwa sauti, ‘aaah aaah’ Hisham akanitolea ishara nimfuata mtu yule, nami nikamfuata lakini bahati mbaya nilipofika akawa ameshakata roho, hivyo nikarudi kwa Hisham nikamkuta naye ameshakufa. Nikarejea kwa mtoto wa Ammi yangu naye nikamkuta amekufa (Rehema ya Allah iwe juu yao wote).”

Hivi ndivyo wanapigiwa mfano wa juu hawa mashahidi watatu katika hima ya kila mmoja kumtanguliza mwenzake na kumfanya bora kuliko nafsi yake na hii ndiyo hali ya Muumin katika maisha yake hapa duniani.

3) Imepokewa kuwa walikutana mbele ya Abi Al-Hassan Antwaky watu zaidi ya thelathini wakiwa na mikate michache, haiwatoshi lau wangetaka kushiba kwa mikate hiyo. Wakaikatakata na wakazima taa, na wakakaa kwa ajili ya kula. Mwishowe sahani iliondolewa tahamaki mikate ilikuwa iko vile vile haikupungua katika mikate hiyo kitu chochote. Kwa sababu hakuna hata mmoja aliyekula kwa mapenzi ya kuwatanguliza wengine kuliko nafsi yake. Ikafikia mpaka wote wakawa hawakula chochote.

4) Amepokea Bukhari na Muslim kwamba:

“Alishukia kwa Mtume wa Allah mgeni hakupata kwa wake zake kitu chochote cha kumpa mgeni wake yule. Akaingia kwa Mtume, Mtu mmoja katika Answare akamchukua mgeni yule nyumbani kwake kwa mke wake kisha akaweka mbele yake chakula na akamuamrisha mke wake kuzima taa, akawa anaunyoosha mkono wake kwenye chakula kana kwamba yeye anakula na hali ya kuwa hali mpaka akala mgeni na akatosheka. Alifanya hivyo kwa kumtanguliza mgeni wake kuliko nafsi yake na mke wake. Alipoamka asubuhi Mjumbe wa Allah ﷺ alimwambia bwana yule wa Ki-Answari: “Kwa hakika Amependezwa Allah na kitendo chenu usiku huu kwa mgeni wenu, na ikashuka aya hii juu yake:

وَيُؤْتِرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ

“Na wanawataguliza wenzao kuliko nafsi zao, japokuwa kwao pana dhiki.” (59:9).

5) Imepokewa kwamba: Bishri Ibn Al-Harithi alifuatwa na mtu mmoja katika ugonjwa aliofia, akamshitakia haja zake, Bishri akavua kanzu ambayo alikuwa ameivaa akampa mtu yule na akaazima kanzu nyingine ambayo alikufa akiwa ameivaa!

Hizi ni sura tano zinazounda mfano ulio hai wa tabia ya Muislamu katika kuwaweka mbele wenzake na kupenda kwake kheri. Na tumetaja mifano hii ili Muislamu ajifunze na aige mapenzi ya kheri na kuwatanguliza wengine katika kheri.



Mada ya Tano

Tabia ya Uadilifu na Unyoofu

Muislamu anaona kuwa uadilifu kwa maana yake kuu ni miongoni mwa wajibu mkubwa kuliko wajibu mwingine wowote na wenye lazima sana kwani Allah Ameliamrisha hilo katika kauli yake:

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَايَ ذِي الْقُرْبَىٰ ﴾

“Hakika ya Allah Anaamrisha kutendeka kwa Uadilifu na Wema na kuwapa ndugu.” (16:90).

Allah Anaeleza kwamba Yeye Anawapenda wenye sifa ya uadilifu. Kauli Yake:

﴿ وَأَقْسَطُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴾

“Na fanyeni uadiifu hakika Allah anawapenda wenye kufanya uadilifu.” (49:9).

Na *Iqsat*: uadilifu”. Na *Al Muqsitin* ni Waadilifu na ameamrisha Allah Mtukufu kufanya uadilifu katika maneno kama alivyoamrisha hilo katika hukumu, Amesema Allah:

﴿ وَإِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ﴾

“Na pindi mkisema fanyeni uadilifu ijapokuwa yule mnayemtolea maelezo hayo ni mwenye udugu.” (Al-An’am: 152),

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ

تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ

“Hakika Allah anawaamrisha kuzitekeleza amana kwa wenyewe, na ukihukumu kati ya watu anawaamrisheni mhukumu kwa uadilifu.” (Annisaa: 58).

Kwa msingi huu Muislamu anafanya uadilifu katika maneno yake na hukumu yake, na anakusudia uadilifu katika mambo yake yote mpaka unakuwa uadilifu ni tabia kwake, na ni sifa ambayo hufungamana nayo. Kwa hiyo zitatoka kauli zake na matendo yake yakiwa yamejaa uadilifu yakiwa mbali na uonevu na dhulma na anakuwa kwa sifa hiyo ni muadilifu hayampondowi mapenzi na wala hayamkokoti matamano ya dunia, na anathibitikiwa na mapenzi ya Allah na radhi Zake na takrima Yake na kuneemesha kwake kwa sababu Allah Ameeleza kuwa Yeye Anawapenda wenye kufanya uadilifu na kadhalika Mjumbe wa Allah (s.a.w.) amesema,

“Hakika watu waadilifu mbele ya Allah watakuwa juu ya mimbari za nuru wale ambao wanafanya uadilifu katika kuhukumu kwao na kwa watu wao na vile ambavyo wametawalishwa.” (Muslim)

Na amesema:

“Watu wa aina saba watafunikwa na Allah katika kivuli chake siku ambayo hapatakuwa na kivuli ila kivuli chake. Imamu Muadilifu na kijana aliyekulia katika ibada ya Allah na mtu ambaye umefungamanishwa moyo wake na Misikiti na watu wawili waliopendana kwa ajili ya Allah wamekutana juu ya hilo na wameachana juu ya hilo, na mtu ambaye alimwita mwanamke mwenye cheo na uzuri akasema: “Hakika mimi ninamuogopa Allah, na mtu aliyetoa sadaka akaiificha mpaka asijue mkono wake wa kushoto kile ambacho unakitoa mkono wa kulia na mtu aliyemtaja Allah hali ya kuwa faragha na akatokwa na machozi.” (Bukhari).

Uadilifu una Sura Nyingi na Miongoni Mwa Sura za Uadilifu ni:-

- 1) Kumfanyia Uadilifu Allah (Mtukufu) kwa kutomshirikisha Naye katika kuabudiwa Kwake na Sifa Zake na kitu kingine chochote na kutiwa asiasiwe na akumbukwe asisahauliwe na ashukuriwe asikufuriwe.
- 2) Uadilifu katika kutoa hukumu kati ya watu, kwa kumpa haki kila mwenye haki yake na kumpa kila anachostahiki.
- 3) Uadilifu kati ya wake na watoto asimpendelee mmoja kuliko mwingine wala hatawaweka mbele baadhi yao kuliko baadhi.
- 4) Uadilifu katika kuzungumza maneno. Kwa hiyo hapatashuhudiwa uzushi na wala hapasemwi urongo au batili.
- 5) Uadilifu katika itikadi, kwa hiyo hata kuwa na itikadi isiyokuwa ya haki na ukweli, na wala hatafikunja kifua juu ya isiyokuwa hakika na ukweli.

Mfano wa Uadilifu Katika Kuhukumu:

Wakati ‘Umar Ibn Al-Khattab amekaa, ghafla alimwendea mtu katika watu wa Misri, akasema: “Ewe Amiri Al-Muuminin!”. “Hii ni nafasi ya mtaka himaya kwako”, Umar akasema, “. . .Mtaka himaya eleza habari yako?” Akasema: “Nimefanya mashindano ya farasi na mtoto wa ‘Amr Ibn ‘Al-Asi, nikamshinda, akawa ananipiga kwa kiboko chake, na huku anasema: Mimi ni mtoto wa watu watukufu, ikamfikia habari hiyo Amiri baba yake akaogopa mimi kukujia wewe, akanifunga jela nikatoka humo jela na wakati huu nimekuja.” ‘Umari Ibn Al-Khattab akamuandikia ‘Amri Ibn ‘Asi (mtawala wa Misri): “Itapokufikia barua yangu hii hudhuria Msimu wa Hijja wewe na mtoto wako fulani”, kisha akamgeukia yule Mmisri akamwambia, ‘Baki hapa mpaka atakapokuja.”

Akaja ‘Amri bin al-‘Aas akahudhuria Msimu wa Hijja, walipomaliza hijja wakakaa pamoja na watu wakati huo ‘Amr Ibn Al-‘Asi akiwa na mwanawe ubavuni mwake. Akasimama yule Mmisri, ‘Umar akamtupia bakora kisha yule Mmisri akampiga mtoto wa ‘Amru bin Al-‘As na hakuacha kumpiga mpaka wakatamani waliohudhuria aache kutokana na wingi wa pigo lake. Huku ‘Umar akisema, “Mpige mtoto wa watukufu”; Akasema (yule Mmisri), “Ewe Amiri wa

Waumini: Nimekamilisha na nimemaliza”, Akasema: “Ewe Amiri wa Waumini nimekwisha mpiga yule aliyenipiga. ‘Umar bin Al-Khatib akasema: “Amma naapa kwa Allah lau ungefanya asingekuzuia mtu yeyote mpaka uwe wewe ndiye unayeacha.” Kisha Umar bin al-Khattab akamgeukia ‘Amru bin Al-‘As akamwambia, “Tokea lini mumewafanya watu kuwa watumwa na hali wamewazaa mama zao wakiwa huru?”

Matunda Mazuri ya Uadilifu:

Miongoni mwa matunda ya uadilifu ni kueneza utulivu katika nafsi: Imepokelewa kwamba Kaisar alimpeleka Mjumbe kwa Umar Ibnul Khattab, ili achunguze hali zake na ashuhudie matendo yake. Pindi mjumbe yule alipoingia Madina alimuulizia Umar na kuwauliza watu, ‘Yupo wapi mfalme wenu?’ Watu wakasema, ‘sisi hatuna mfalme, bali tuna Amir, naye hayupo hapa saa hizi kwani ametoka kwenda nje ya mji’, yule mjumbe akatoka katika kumtafuta Umar akamuona Umar mwenyewe akiwa amelala kwenye mchanga, na amekifanya mto kiboko chake alichokuwa na kawaida ya kutembea nacho ambacho hukitumia kuondolea munkari wakati mwingine.

Yule mjumbe wa Kaisar alipomuona Umar katika hali hii, uliingia unyenyekevu moyoni mwake na kusema, ‘Mtu ambaye Wafalme wote hawana kwao utulivu kutokana na kumuogopa kwa haiba yake, na hii ndiyo hali yake?, kwa hakika wewe Umar umefanya uadilifu na kwa hiyo umepata wasaa wa kulala kwa utulivu, na mfalme wetu anafanya dhulma, ni haki yeye kuwa ni mwenye kukesha na mwenye kuogopa.’

Ama *I'tidaal* yaani kuwa kati kwa kati, huko kuna maana pana zaidi kuliko uadilifu wenyewe (adl). Ukati na kati unaweka taratibu nzima ya maisha ya Muislamu katika maisha haya ya dunia. Kati na kati ndiyo njia ya wastani ya kufanya jambo bila ya kupunguza au kuzidisha jambo na huku kuzidisha kitu au kupunguza ni katika tabia mbili mbaya sana.

Ukati na kati katika ibada ni kujiepusha na kuvuka mipaka na kuendelea katika kupuuza na kutofanya kwa ukamilifu unaotakiwa. Hapana matumizi ya fujo na kupindukia katika jambo au kujibana. Lakini ni ukati na kati, Anasema Allah:

وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا وَكَانَ بَيْنَ ذَلِكَ قَوَامًا ﴿٦٧﴾

“Na wale ambao pindi watumiapo hawavuki mipaka na hawajidhiki, na yanakuwa matumzi yao kati ya kuvuka mpaka na kujidhiki ni ya kati na kati.” (25: 67).

Aidha katika mavazi pana mpaka kati ya kuvaa kwa ufakhari na kujionesha au kuvaa nguo zilizochanika zenye viraka, na ukati na kati katika kwenda na kujivuna na kutakabari na kati ya kwenda mwendo wa mtu aliyekuwa dhalili maskini mwenye kuogopa watu, na ukati na kati katika kila uwanja ni ukati na kati pasina kupunguza kuliko vinavyohitajika na kutozidisha kuliko kiasi kinachohitajika.

Adili ni ndugu mnyoofu wa tabia na humjengea msimamo, huu ndio ubora wa tabia ambao unamfanya sahibi yake kuchunga mipaka ya Allah katika matendo yake. Hivyo basi anakuwa havuki mipaka hiyo na humfanya kuwa ni mtendaji mzuri wa amali njema na majukumu anayotakiwa kuyafanya katika haki ya Mola wake kwa hiyo harudi nyuma katika kutekeleza majukumu yake, au haupunguzi sehemu yoyote katika sehemu na hiyo ndiyo inayomfunisha kujichunga na mambo maovu na kwa hiyo anatosheka na vile alivyo halalishiwa na kuacha vile ambavyo amekharamishiwa. Inamtosha mwenye tabia hii kuridhika na Kauli ya Allah:

وَأَلَوْ اسْتَقْنُمُوا عَلَى الطَّرِيقَةِ لَأَسْقَيْنَهُمْ مَاءً غَدَقًا ﴿١٦﴾

“...na kwamba lau wangenyooka juu ya njia tungewanyweshwa maji mengi.” (al-Jinn:16)

Na Kauli Yake:

لَخُنْ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ إِنَّهُمْ فِتْيَةٌ آمَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى ﴿١٦﴾

وَرَبَطْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا رَبُّنَا رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَنْ نَدْعُوَ

مِنْ دُونِهِ إِلَهًا لَقَدْ قُلْنَا إِذًا شَطَطًا ﴿١٧﴾

“Haikuwa wale ambao wamesema, Bwana wetu ni Allah kisha wakawa na unyofu, hapakuwa na khofu yoyote juu yao na wala wao hawatahuzunika hao ndiyo watu wa peponi hali ya kuishi humo milele yakiwa ni malipo ya yale ambayo walikuwa wakiyatenda.” (al-Ahqaf:13-14).



Mada ya Sita

Tabia ya Huruma.

Muislamu ni mwenye huruma na huruma ni tabia miongoni mwa tabia zake, hivyo hukaa mbali na shari, na hujiepusha na maovu. Yeye siku zote anakuwa katika usafi wa nafsi, uzuri wa roho na yule ambaye imekuwa hii ndiyo hali yake, hakika huruma inakuwa haiuepuki moyo wake, na kwa msingi huu Muislamu anakuwa ni mwenye huruma, hurumia wengine bali haiishii hapo analingania na wengine kuwa katika hali hiyo, ikiwa ni kuyahakikisha maneno ya Allah Mtukufu:

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ ﴿٧٧﴾ أُولَٰئِكَ

أَصْحَابُ الْيَمِينَةِ ﴿٧٨﴾

“Kisha akawa ni miongoni mwa ambao wameamini na wakausiana kufanya subira na wakausiana kufanya huruma hao ndio watu wa upande wa kuume.” (Al-Balad: 17-18).

Na kwa kufanyia kazi Kauli ya Mtume ﷺ:

“Hakika hapana jambo jingine Anawarehemu Allah wenye huruma kwa watu wengine.” (Bukhari).

Na Kauli Yake:

“Wahurumieni waliyo katika ardhi atawahurumia aliye mbinguni.” (Bayhaqi).

Na kuyafanya muongozo maneno ya Mtume (Rehema na amani ziwe juu yake:

“Asiye hurumia hahurumiwi.”

Na kutokana na Kauli yake:

“Haiondolewi huruma ila kwa mtu muovu.” (At-Tirmidhi, Abu Daud na Ahmad).

Na kuihakikisha Kauli Yake:

“Mfano wa waumini katika kupendana kwao na kuhurumiana kwao na kufanyiana upole, ni kama mwili mmoja, kikiumwa katika mwili huo kiungo chochote huita kwa ajili ya kiungo hicho mwili wote kwa (kwa uchungu) kukesha na homa.” (Muslim).

Na huruma iwapokuwa hakika yake ni ulaini wa moyo na upole wa nafsi wenye kuelekea kwenye msamaha na kufanya wema, lakini kwa hakika hiyo (huruma) haitakuwa siku zote ni hisia ya kinafsi tu ambayo haina athari yoyote nje katika matendo ya mtu, bali (huruma) ina athari za nje, na sura za hakika zinazoonekana nje katika Ulimwengu huu wenye kuchukua dalili zake katika kuonekana kwa vitu.

Miongoni mwa athari za huruma zinazoonekana nje katika matendo na amali za mja ni kama vile, kumsamehe mwenye kuteleza, kumsamehe mwenye makosa, kumuokoa aliye katika janga, kumsaidia mnyonge, kumlisha mwenye njaa, kumvisha asiye na nguo, kumtibu mgonjwa na kumliwaza mwenye huzuni, yote haya ni katika athari za huruma, na kuna nyingine nyingi sana katika athari na matendo ya wazi zenye kuwakilisha huruma ya mtu.

Miongoni mwa sura za wazi za huruma ambazo huonekana na hudhuhiri Katika hisia na machoni mwa watu ni hizi zifuatazo:

1) Amepokea Bukhari kutokakwa Anas Ibn Malik رضي الله عنه kuwa alisema:

“Tuliingia pamoja na Mjumbe wa Allah ﷺ kwa Abu Yusuf Al-Qayn (mtu huyu alikuwa ni mlezi wa Ibrahim mwanawe Mtume ﷺ. Mtume ﷺ alipofika kwake akamchukua mwanawe Ibrahim kisha akambusunakumshumu kishatkaingia kwake baadayahapo na hali Ibrahimu anatokwa roho, yakawa machozi ya Mtume ﷺ yanatoka machozi. Abdulrahman Ibni Auf رضي الله عنه akamwambia Mtume ﷺ na wewe Mjumbe wa Allah (unalia)? Mtume ﷺ akajibu, ‘Ewe mtoto wa Auf hakika hiyo ni huruma, ‘kisha akasema, “hakika jicho linatoa machozi na moyo unahuzunika na wala hatusemi ila yale yanayomridhisha Bwana wetu na hakika sisi kwa kifo chako ewe Ibrahim ni wenye huzuni kubwa.” (Bukhari).

Ziara ya Mjumbe wa Allah ﷺ kwa mtoto wake mdogo, hali yeye yuko katika nyumba ya mnyonyeshaji wake, kumkumbatia kisha na kumbusu halafu kumtembelea alipokuwa mgonjwa anaugulia na kutokwa na roho, kisha yale machozi ya huzuni aliyoyatoa yote hayo yanaonesha sura za huruma kutoka moyoni mwa mja.

2) Amepokea Bukhari kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه nae amepokea kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alisema,

“Wakati mtu mmoja anakwenda kikamzulia kiu akashuka kisimani akanywa humo kisha ghafla akatokea mbwa ametoa utlimi anatweta anakula mchanga kutokana na kiu, mtu akasema moyoni mwake, ‘hakika amefikia (mbwa) huyu ile hali ambayo ilikuwa imenifikia,’ akaijaza maji khufu yake kisha akaishika kwa mdomo wake, akapanda na kumywesha mbwa yule. Allah akamkubalia tendo lake hilo na akamsamehe, (Maswahaba) wakamuuliza Mtume ﷺ ‘Ewe Mjumbe wa Allah kwani tuna mali kwa wanyama?’ Mtume ﷺ akawajibu, “Katika kila ini bichi (yaani kukifanyia huruma kila kiumbe chenye uhai) pana malipo.” (Bukhari).

Kushuka kwa yule mtu kisimani na kuvumilia kwake taabu ya kuyatoa maji yale kisha kumnyweshwa mbwa yule mwenye kiu, yote hayo ni katika sura za huruma ya mtu yule iliyo moyoni mwake, na lau sio hivyo, asingefanya hayo aliyoyafanya. Kinyume cha kisa hiki kilichotangulia na jaza ya yake ni yale aliyoyapokea Bukhari kutokana na Abu Huraira رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba yeye alisema, “Aliadhibiwa mwanamke mmoja kwa sababu ya paka ambaye alimfunga mpaka akafa, akaingia motoni kwa sababu yake na akaamb iwa: “Hukuwa wewe umempa chakula na wala hukumnyweshwa wakati ulipomfunga na wala wewe hukumwachia akala katika wadudu wa ardhi.” (Bukhari). Hakika kitendo cha mwanamke huyu katika sura ya ugumu wa moyo na kuondolewa huruma kwake. Huruma haiondolewi ila kutoka katika moyo wa mtu muovu.

3) Bukhari amepokea kutoka kwa Abu Qatada رضي الله عنه kwamba Mjumbe wa Allah ﷺ alisema:

“Hakika mimi huwa naingia katika Swala nikiwa ninakusudia kurefusha ghafla ninasikia kilio cha mtoto mdogo ninafupisha kwa sababu ya lile ambalo ninalielewa miongoni mwa ukubwa wa huzuni ya mama yake kutokana na kilio cha mtoto yule.”

Kuacha kwake Mtume ﷺ kuirefusha sala yake ambayo alikuwa amezimbia kuirefusha na kuhuzunika mama kutokana na kulia kwa motto wake ni sura katika sura za huruma ambayo ameiweka Allah katika nyoyo za wenye huruma miongoni mwa waja wake.

4) Pamepokewa kwamba Zainul Abidin bin Ali Bin Al-Hussein رضي الله عنه alikuwa njia ni kuelekea msikitni, mtu mmoja akamtukana, vijana wa Zainu Abidin wakamkusudia kumpiga mtu yule na kumfanyia maudhi, Zainu akawakataza na akawazuia kufanya hivyo, kwa kumhurumia, kisha akamwambia mtu yule, ‘Ee huyu, mimi niko zaidi ya unavyosema na yale ambayo huyaelewi kutokana na mimi ni mengi sana kuliko unayoyaelewa ukiwa unahaja na hayo nitakutajia.’ Yule mtu akatahayari na akaona haya akamvulia Zainul Abidin kanzu yake na akaamrisha apewe Dirhamu elfu moja Kusamehe huku na wema huu havikuwa ila ni sura katika rehema ambayo imo katika moyo wa mjukuu wa Mjumbe wa Allah ﷻ.



Mada ya Saba

Tabia ya Kuwa na Staha

Muislamu ni mwenye kujichunga na maovu na ni mwenye haya, haya ni tabia yake, kwani haya ni katika imani, na Imanini itikadi ya Muislam una msimamo wa maisha yake. Mtume ﷺ amesema,

“Imani ina matawi sabini na au sitini na, bora ya yote ni Lailahailla-Allah na ya chini ya yote nikuondoa uchafu njia ninakuwa na haya ni sehemu ya imani.” (Muslim).

Na amesema:

“Haya, na imani ni mambo mawili yanayokwenda pamoja, moja likiondolewa pia litakuwa limeondolewa jingine.” (al-Hakim).

Siri ya kuwa haya ni katika imani ni kwamba kila moja ya mawili hayo linamwita mtu kwenye kheri, linamwepusha na shari na kumuweka mbali na shari. Imani inamsukuma Muumini juu ya kufanya *twa* na kuyaacha maasi na kuwa na haya kunamzuia mtu kutofanya wajibu wake, kumshukuru mwenye kuneemsha na pia kunamzuia kutofanya hima kwa mwenye haki kama ambavyo haya inamzuia mwenye haya kutenda matendo maovu au kuyasema kwa kujikinga na dhulma na lawama. Ni kutokana na msingi huo imekuwa haya ni katika mambo ya kheri na wala kaileti ila kheri kama ilivyoswihi kutokana na Mtume ﷺ katika kauli yake:

“Haya haileti ila kheri.” (Bukhari na Muslim).

Kauli yake nyingine ya Mtume ﷺ katika upokezi wa Muslim: “Kuwa na haya ni kheri yote.” Kinyume cha haya ni uchafu katika maneno na matendo, na ukavu katika kusema. Muislamu hawi muovu wala mwenye kujilazimisha kufanya uovu, wala mgumu na mkavu wa tabia, kwani hizi ni sifa za watu wa motoni na Muislamu Insha Allah ni katika watu wa peponi. Hatakiwi Muislamu kuwa na tabia hizi chafu katika kuongea kwake au kuwa mgumu wa tabia, na hoja ya haya ni Kauli Yake Mtume ﷺ:

“Haya ni katika imani na imani itakuwa peponi –na uchafu wa maneno na ugumu wa tabia vitakuwa motoni.” (Muslim na Ahmad).

Kiigizo cha Muislamu katika hizi tabia njema na utukufu ni Mtume ﷺ, Mjumbe wa Allah Bwana wa mwanzo na wa mwisho kwani alikuwa mkubwa zaidi wa haya kuliko mwali katika pazia lake. Kama alivyoyapokea haya Bukhari kutoka kwa Abu Said amesema katika kumwelezea Mtume ﷺ: “Akiliona jambo ambalo analichukia unalijua hilo usoni mwake.”

Muislamu wakati anapowaita watu kwenye kushikamana na tabia ya kuwa na hayana kuliendeleza hilo kwao hakika hapana jambo jingine analofanya isiokuwa ni kuwa anawaita watu kwenye kheri, na anawaongoza kwenye wema kwani haya ni katika imani na imani ni mkusanyiko wa mambo mema yote na ndiyo chanzo cha kheri zote.

Imepokewa katika hadithi sahihi kwamba Mjumbe wa Allah ﷻ alimpitia mtu mmoja akiwa anampa mawaidha ndugu yake akimlaumu kwa kuwa na haya Mtume ﷺ akasema,

“Mwache kwani haya ni katika imani.” (Bukhari, Abu Dawud na An-Nasai).

Ametoa wito kwa maneno hao Mtume ﷺ wa kuibakisha haya kwa Muislamu na amekataza kuiondosha, hata kama yanamzuia mwenye nayo kupata ukamilifu wa baadhi ya haki zake kwani bora kupotea baadhi ya haki kuliko kukosa haya ambayo ni sehemu katika imani, haya au staha ni kipambanuzi cha utu wa mtu na chemchem ya ubora wake. Allah amrehemu mwana mke ambaye alikuwa amepotelewa na mtoto wake mdogo akasimama mbele ya watu akiwauliza kuhusu mtoto wake, mmojawao akasema anauliza kuhusu mtoto wake na hali ya kuwa amejifunika? Mwanamke yule kayasikia maneno yale naye akasema,

“Kupatwa na msiba kwa kumkosa mtoto wangu ni bora kuliko kupata msiba wa kuikosa haya yangu ewe mtu” (Abu Dawud).

Tabia ya haya kwa Muislamu haimzuii kusema ukweli au kutafuta elimu au kuamrisha mema au kukataza maovu. Usamah Ibn Zayd kipenzi cha Mtume wa

Allah na mtoto wa kipenzi chake siku moja alimuumbea mtu mmoja mbele ya Mtume wa Allah ﷺ ili amsalimisha na adhabu, jambo hili (la kuwa ni kipenzi chake) haikumzuia Mtume wa Allah ﷺ kumwambia Usamah hali ya kuwa ameghadhibika,

“Hivi unaombea katikakuvunjwa kwa adhabu katika adhabu za Allah Ewe Usamah? Naapa kwa Allah lau angeiba (mwanamke) fulani ungekatwa mkono wake.” (Bukhari, Abu Dawud na At-Tirmidhi).

Haya haikumzuia Ummu Sulaim Al-Answariyyah kusema,

“Ewe Mjumbe wa Allah hakika ya Allah huoni haya juu ya haki je kuna wajibu wa kuoga juu ya mwanamke pindi akiota? Akamwambia Mtume ﷺ na haikumzuia haya kumuuliza swali hilo Mtume ﷺ Mtume ﷺ akamjibu, “Ndiyo atakapoon maji.” Bukhari).

Umar alitoa hotuba siku moja akazungumzia ughali wa mahari, mwanamke mmoja akamwambia, ‘Hivi Allah anatupa na unatuzulia Ewe Umar? Hivi hakusema Allah,

وَأَتَيْتُمُ إِحْدَنَّهُنَّ قِنطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ شَيْئًا أَتَأْخُذُونَهُ بِهَتَّائِنَا وَإِنَّمَا مِئِينًا ﴿٢٠﴾

“Na mkampa mmoja wao mali nyingi kwa hiyo msichukue katika hiyo mali kitu chochote.” (Nisaai:20).

Haya haikumzuia mwanamke huyo kutetea haki za wanawake wenzake, na haya haikumzuia Umar kusema na huku anatoa udhuru (juu ya maneno yake hayo), ‘Watu wote ni wajuzi zaidi kuliko wewe Ewe Umar.’

Kama ambavyo alitoa hotuba siku moja kwa Waislamu na hali amevaa nguo mbili (mpya) akaamrisha Usikizi na utiifu, mmoja katika watu waliokuwa pale akamwambia Umar, “Hapana kukusikiliza wala kukutii Ewe Umar, una nguo mbili nasi tuna nguo mojammoja, Umar akatoa ulingano kwa sauti yake ya juu, ‘Ewe Abdullah Ibn Umar akaita kwa sauti kumuita mwanae, Abdullah akaitika, Umar akamuuliza, ‘Hivi haikuwa moja ya nguo zangu (nilizovaa) ni nguo yako ambayo ulinipa? Abdullah Ibn Umar akajibu kwa kusema, ‘kwa nini, ni nguo

yangu.’ Mtume yule aliyesababisha vile akasema, ‘Ninaapa kwa Allah sasa tutakusikiliza na tutakutii Ewe Umar.’

Hebu tazama namna ambavyo haya haikumzuia ule mtu kusema, na wala Umar haikumzuia haya kukiri. Muislamu kama anavyowastahi viumbe hawafunulii tupu, na wala haachi kufanya haki ambayo wanastahiki, juu yake, na wala hakanushi wema ambao wamemtendea, wala hawasemeshi kwa ubaya wala hawakabili kwa jambo ambalo wanalichukia. Yeye anamstahi Allah, haachi kufanya wajibu wake katika kumtii Kwake wala katika kuzishukuru neema zake, na hayo ni kutokana na anayoyaona miongoni mwa uwezo wake juu yake na kumjua Kwake anayoyafanya yote, hayo kwa kufuata maneno ya Ibni Masoud:

“Muoneni haya Allah ukweli wa kumuonea haya kwa hiyo kihifadhini kichwa na vile ambavyo kimehifadhi na tumbo na vile ambavyo limekusanya na kumbukeni kufa na kuchakaa.”(al-Mundhiry).

Na Kauli ya Mtume .

“Basi Allah ana haki zaidi ya kustahiwa kuliko watu.”(Abu Dawud na At-Tirmidhi).



Mada ya Nane

Tabia ya Uhisani (kutenda wema).

Muislamu hatutazami kufanya wema kuwa ni tabia bora tu ambayo ni vizuri kujipamba nayo bali anakutazama kuwa ni sehemu ya itikadi yake na ni sehemu kubwa ya Uislamu wake kwani Dini ya Uislamu mjengo wake uko juu ya mambo matatu nayo ni Imani, Uislamu na Ihsani kama lilivyokuja hilo katika kuwekwa wazi na Mtume wa Allah ﷺ kwa Jibril عليه السلام, katika hadithi ambayo wameipokea kwa pamoja Bukhari na Muslim alipomuuliza kuhusu Imani, Uislamu na Ihsani na akasema baada ya kuondoka kwake, “*Huyu ni Jibril amewajieni kuwafundisha mambo ya Dini yenu*” akayaita mambo matatu hayo kuwa ni Dini na ameamrisha Allah Ihsani katika mahali zaidi ya pamoja katika kitabu chake Kitukufu Alisema:

وَأَحْسِنُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٩٥﴾

“*Na fanyeni wema hakika Allah anawapenda wenye kufanya wema.*”(al-Baqarah:195).

Na amesema Allah Mtukufu:

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ ﴾

“*Hakika Allah anaamrisha kufanya uadilifu na wema.*”(Annahl:90).

Na Amesema Allah,

وَقُولُوا لِلنَّاسِ حُسْنًا

“*Na waambieni watu mambo mema.*”(al-Baqarah: 83).

وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ

الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ⁴

“Na anawaamrisha kuwatendea wema wazazi wawili na ndugu na mayatima na maskini na jirani mwenye ndugu na jirani asiyekuwa na ndugu na rafiki wa ubavuni na msafiri na wale ambao imewamiliki mikono yenu ya kuume.” (Annisaa: 36).

Mjumbe wa Allah ﷻ alisema,

“Hakika Allah amewaibisha kila kitu kitendewe wema kwa hiyo pindi mkiua fanyeni vizuri katika kuua, na mkichinja fanyeni vizuri katika kuchinja na anoe mmoja wenu kisu chake na apumzishe mnyama alie mchinja.” (Muslim).

Na Ihsani katika mlango wa Ibada: Ni kutekeleza Ibada namna yoyote itakayokuwa, miongoni mwa Sala, Saumu au Hijja au zisizokuwa hizo, utekelezaji uliyo sahihi kwa kukamilisha masharti yake, nguzo zake, na kutimiza sunna na adabu zake. Na hili haliwezi kutimiza kwa mja ila atakuwa wakati wa kutekeleza kwake ibada ni mwenye kuzama katika hisa yenye nguvu kwa kumchungu Allah (Ambaye Ameshinda na Ametukuka) kwa uchache anaifanya nafsi ya kihisi kuwa Allah Mtukufu Anamshuhudia au kwa uchache anaifanyanafsi yake ihisi kuwa Allah Mtukufu Anatokezea juu yake na Anamtazama, huyo peke yake ndiye anayeweza kutengeneza Ibada yake, na kuifanya vizuri na kuitenda katika nia inayotakiwa na sura yake iliyo kamilifu, na hili ndilo aliloelekeza Mjumbe wa Allah ﷻ katika Kauli Yake:

“Ihsani ni kumwabudu Allah kana kwamba wewe unamwona, ukiwa humuoni hakika yeye anakuona.” (Bukhari).

Ama Ihsani katika mlango wa matendeano: Hiyo kwa wazazi wawili ni kuwatendea wema, ambako ni kuwatii na kuifikisha kheri kwao, kuyazuia maudhi kwao, kuwaombea kuwatakia maghfira (msamaha) kutekeleza ahadi yao na kumtukuza rafiki yao.

Ihsani kwa jamaa: Ni kuwafanyia wema, kuwahurumia, kuwafanyia upole na kufanya lile ambalo zuri, kulifanywa pamoja nao na kuliacha lile ambalo linakuwa haya kwao au kunakuwa vibaya kulisema au kulifanya pamoja nao.

Minhajil Muslim

Ihsani kwa mayatima: Ni kujihifadhi na mali zao na kuzilinda haki zao,. Na kuwafunza adabu na kuwalea na kuacha kuwaudhi au kuwatenza nguvu na kuonyesha furaha katika nyuso zao na kuvifuta vichwa vyao (kuwaondoshea machungu ya kukosa wazazi).

Kwa masikini: Nikuondoa njaa zao akusitiri tupu zao, na kuhimiza juu ya kuwalisha na kutovunjwa heshima zao na kwa hiyo hawatadharauliwa na hawatadhalilishwa na hawatapatwa kwa ubaya wowote au kuguswa, kwa uchukivu wowote.

Ihsani kwa msafiri: Ni kwa kukidhi haja yake, kuyaondoa matatizo yake na kuichunga mali yake, kuilinda heshima yake, kumuongoza akitaka kuongozwa na kumwelekeza iwapo amepotea.

Ihsani kwa mtumishi: Ni kwa kumpa malipo yake kabla yakukauka jasho lake na kutomlazimisha jambo ambalo halimlazimu au kumlazimisha jambo ambalo haliwezi kwa kulinda heshima yake na kuuheshimu utu wake, akiwa ni katika watumishi wa nyumbani ni kwa kumlisha kile ambacho kinaliwa na watu wa nyumba ile na kumvisha kile ambacho kinawaliwa na watu wa nyumba ile.

Na kufanya ihsani kwa watu wote: Ni kwa kufanya upole katika kuwaambia na kuwachukulia katika kuteteana nao na kusema nao baada ya kuwaamrisha kufanya wema, kuwakataza uovu na kwa kumuongoza mpotevu wao, na kumfundisha mjinga wao, na kuwafanyia uadilifu kutoka katika nafsi na kuzitambua haki zao na kuyazuia maudhi yao kwa kutofanya lile ambalo linawadhuru au kufanya lile ambalo linawaudhi.

Na kufanya Ihsani kwa mnyama: Ni kwa kumlisha akiwa na njaa na kumtibu akiwa mgonjwa na kutomlazimisha ambalo haliwezi na kumfanyia upole akifanya kazi, na kumpumzisha akichoka.

Na ihsani katika matendo ya mwili: Ni kwa kuifanya vizuri kazi na kufanya vizuri utengenezaji na kuyaepusha matendo mengine na udanganyifu kwa kusimama mbele ya ile Kauuli ya Mtume ﷺ iliyosema:

“Mwenye kutudanganya si katika sisi.” (Muslim).

Na Sura za Ihsani ni miongoni mwa haya yafuatayo:

1) Pindi Mushirikina walipomfanyia Mtume ﷺ walichomfanyia siku ya vita vya Uhud miongoni mwake ni kumuua Ami yake na kukatwa katwa viungo vyake, kuyavunja magego ya Mtume ﷺ na kumpasua usoni mwake, mmoja wa maswahaba alimtaka Mtume ﷺ awaapize mushirikina walio madhalimu, Mtume akasema, “Ewe Mola Wangu wa Haki wasamahe jamaa zangu hakika waohawajui chochote.”

2) Siku moja Umar Ibn Abdil-Azizi alimwambia mjakazi wake: “Nipepee mpaka nilale, akampepea mpaka akalala, ukamshika yule mjakazi usingizi naye akalala, Umar alipoamka alichukua kipepeo akampepea ya ule mjakazi, alipoamka yule mjakazi akamuona Umar anampepea akashtuka na kupiga kelele, Umar akamwambia, “Hakika si vinginevyo wewe ni mtu mfano wangu, limekupata joto mfano wa lile ambalo lilinipata mimi, nimependa nikupepea kama sulivyonipepea.”

3) Kijana mmoja alimuudhi mmoja wa watu wema walipita (*salaf*) maudhi makubwa sana. Yule bwana katika salafu akakusudia naye kumwadhibu kijana yule, Kijana kujua hilo akasema, “Na wenye kuzizuia chuki zao”, yule bwana katika salaf akasema, “Nimeizuia chuki yangu.” Yule kijana akasema, “Na wenye kuwasamehe watu”, Akasema: “Nimekusamehe” Yule kijana akasema tena, “Allah “Anawapenda wenye kufanya wema”, akamsema yule bwana wa Salaf, “Nenda wewe uko huru nami nafanya hivyo kwa kutaka radhi za Allah (s.w.t.).”



Mada ya Tisa

Tabia ya Kusema Kweli

Muislamu ni mkweli na anashikamana na ukweli kwa ndani na nje, katika maneno yake na kwa vitendo vyake. Kwani ukweli unamuongoza kwenye wema na wema unamuongoza kwenda peponi na pepo ni tukufu sana, na ni katika malengo ya Muislamu na ukomo wa matumaini yake. Na urongo nao ni kinyume cha ukweli unaongoza kwenye uonevu, nao unaongoza mtu kwenda motoni na ni miongoni mwa sharikubwa mno anayoiogopa Muislamu na kujikinga nayo.

Muislamu hautazami ukweli kama tabia bora tu ambao anapaswa kujipamba nayo bali anakwenda mbali zaidi kuliko hapo, anakwenda kwenye ukweli na kwamba ni katika vikamilishi vya imani yake na vihitimisho vya Uislamu wake, kwa kuzingatia kuwa hayo ni katika maamrisha ya Allah (s.w.t.). Mwenyezi Mungu amewasifu waumini kwa sifa hii hali kadhalika Mtume ﷺ ameliamrisha hilo na kulihimiza. Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ ﴿١١٩﴾

“Enyi ambao mmeamini mcheni Allah na kuweni pamoja na wa kweli.” (Attawba: 119).

Na amesema katika kuwasifu watu wa ukweli:

مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ

“Ni watu waliofanya kweli yake ambayo wamemwahidi Allah.” (al-Ahzaab: 23).

Na amesema:

وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ

“Na wakweli wanamume na wakweli wanawake.” (al-Ahzaab:35).

Na amesema:

وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِمْ أُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿٣٣﴾

“Na ambaye amekuja na ukweli na wakauthibitisha kwa imani na matendo hao wao ndiyo wachaji.” (Azzumar:33)

Hali kadhalika katika hili Mjumbe wake ﷺ amelisa katika kuamrisha kupenda ukweli:

“Jilazimisheni kuwa wakweli kwani ukweli unaongoza kwenye wema na hakika wema unaongoza peponi na haachi mtu kusema ukweli na anakusudia ukweli mpaka huandikwa mbele ya Allah kuwa ni mkweli.” (Muslim).

Na tahadharini na kuwa warongo, kwani urongo unaongoza kwenye uovu na hakika uovu unaongoza kwenye moto na haachi mtu kuwa anasema urongo na anakusudia urongo mpaka anaandikwa mbele ya Allah kuwa ni mrongo.” (Muslim).

Yaelewe haya: Hakika ukweli una matunda mengi mazuri wanayachuma wa kweli na zifuatazo ndizo aina zake:-

1) Mapumziko ya dhamira na utulivu wa nafasi kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Ukweli unaleta utulivu.” (At-Tirmidhy).

2) Baraka katika chumo na kuongezeka kwa kheri, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Wenye kuuziana wawili wanayo haki ya kufanya khiyari muda wa kuwa hawajatengana wakiwa wa kweli na wakaweka wazi mambo yao, watabarikiwa katika makubaliano yao na wakifichanawakasema urongo hufutwa baraka ya uuzajiwao.” (Bukhari).

3) Kufuzu kwa kupata daraja la mashahidi kutokana na kauli yake Rehema na Amani ziwe juu yake:

“Mwenye kumumba Allah ushahidi (kufa katika vita) kwa ukweli Allah atamfikisha katika daraja la mashahidi hata akifia kitandani mwake.” (Muslim).

4) Kuokoka na mambo yenye kuchukiza kwani imepokewa kwamba mtoto mmoja alikimbilia kwa mmoja wa watu wema na akamwambia nifiche na yule anayenitafuta, yule mtu akamwambia, ‘lala hapa’ akatupa juu yake kitita cha makuti walipokuja kumtafuta na wakamuulizia yule mtu mwema alisema, ‘Ehe huyu hapa chini ya haya makuti wakadhani kuwa anawafanyia utaniwakamwacha na akaokoka kwa baraka ya ukweli wa yule mtu mwema.

Yafahamu yaya: Na ukweli unaojitokeza katika aina na sura nyingi tofauti. Miongoni mwa sura hizo:

1) Ukweli Wa Mazunguzo, Muislamu akizungumza hazungumzi usiokuwa ukweli na haki na akitoa habari hatoi habari isiyokuwa yenye ukweli kwani uwongo wa mazugumzo ni katika unafiki na alama zake Mtume ﷺ amezielezea kwa kusema,

“Alama za mnaifiki ni tatu akizungumza anasema urongo, na akitoa ahadi huvunja, na akiaminiwa hufanya khiana.” (Bukhari, Muslim na Ahmad).

2) Ukweli Wa Maingiliano na watu, Muislamu akitendeanana na mtu yeyote huwa mkweli katika maingilino yake, kwa hiyo haghushi, hafanyi hadaa, wala hafanyi uzushi na wala hafanyi udanganyifu kwa hali yoyote.

3) **Ukweli Wa Maazimio**, Muislamu anapoazimia kufanya jambo ambalo kunatakikana kulitenda hasitisiti katika jambo hilo bali anakwenda moja kwa moja katika kulifanya hali ya kutoligeukia jambo lolote au kumjali mtu yeyote mpaka atekeleza kazi yake.

4) Ukweli wa ahadi, Musilamu hadhihiri katika isiyokuwa hali yake na wala hadhihirishi tofauti na yaliyo ndani yake kwa hiyo hazui mambo hajioneshi kwa

watu matendo yake na hajilazimishi kwa lile ambalo hana uwezo nalo, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Mwenye kujionesha kuwa ametosheka kwa kila ambacho hakupewa ni kama mtu aliyevaa nguo mbili za uzushi.” (Muslim).

Maana ya (maneno) haya ni kwamba mwenye kujipamba kwa kitu ambacho hakimiliki ili aonekane kwamba yeye ni ajiri anakuwa kama mtu aliyevaa nguo mbili zilizochakaa ili ajioneshe kuwa ameupa mgongo ulimwengu na hali ya kuwa hakuupa mgongo ulimwengu na wala hayumo katika hali mbaya kwa hakika.

Mifano ya Ukweli Halisi iliyo Daraja ya Juu:

Tirmidhi amepokea kutoka kwa Abdillahi Ibn Al-Hamsai amesema, “Tuliuziana na Mjumbe wa Allah ﷻ kabla hajapewa Utume na kulibaki katika haki yake kitu ni kamuahidi kumletea mahali pake nikaisahau, kisha ni kaikumbuka baada ya siku tatu nikaja nikamkuta mahala pake” Mtume ﷺ akasema, “Ewe kijana umeniweka katika taabu hapa tokea siku tatu ninakungojea.”

Na mfano wa hili ambalo lililopatikana kwa Mtume wetu (Rehama na Amani ziwe juu yake) na mfano wa lililompata babu yake wa juu Ismail Ibn Ibrahim Al-Khalil mpaka akamsifu Allah Mtukufu katika Kitabu Chake Kitukufu kwa kauli yake:

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِسْمَاعِيلَ ۖ إِنَّهُ كَانَ صَادِقَ الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُولًا نَبِيًّا ﴿٥٤﴾

“Na mtaje katika kitabu Ismail hakika yeye alikuwa mkweli wa ahadi na alikuwa Mjumbe na Nabii.”(Maryam:54).

2) Al-Hajjaji Ibn Yusuf alitoa hotuba siku moja akairefusha hotuba hiyo, mmoja wa watu waliyohudhuria akasema, ‘Asswalah’ (maana: Ipe umuhimu sala) kwani wakati haukungoji na Bwana hakupi udhuru, Hajjaj akaamrisha mtu yule afungwe, wakamjia jamaa zake wakadai kuwa yule mtu ni mwenda wazimu, Al-Hajjaji akasema, ‘Akikiri kuwa ni mwendawazimu nitamwachilia katika kifungo chake’ yule mtu akasema, ‘Hajjuzu kwangu kuikanusha neema ya Allah ambayo ameneemesha juu yangu, iweje niithibitisha nafsi yangu wendawazimu ilhali Allah ameniepusha nao’, Al-Hajjaji alipoona ukweli wake alimwachia huru..

3. Ameipokea Imam Bukhari رضي الله عنه kwamba yeye alitoka akitafuta hadithi kutoka kwa mtu mmoja, akamuona anamkimbiza farasi wake na huku anamwashiria kwa shuka yake kama kwamba ndani yake mna shairi, yule mtu akamwendea farasi na kumkamata. Bukhari akamuuliza mtu yule, “Je ulikuwa na shairi? (chakula cha farasi) yule mtu akasema, ‘Hapana lakini nilimdhamisha,’ Bukhari akasema, “Sichukui hadithi kutoka kwa anayewadanganya wanyama.” Huu ni mfano wa juu kabisa katika ukweli.



Mada ya Kumi

Tabia ya Kupenda Ukarimu

Utoaji ni tabia ya Muislamu, na ukarimu ni sifa yake, na Muislamu hawi bahili na mwenye uchoyo, kwani pupa na ubahili ni katika tabia mbili zilizo mbaya sana, na chimbuko lake ni ubaya Muislamu kwa imani yake na matendo yake mema, nafsi yake ni safi, na moyo wake unatoa nuru. Inapingana pamoja na usafi wa nafsi yake na mwanga wa moyo wake mtu kusifika na tabia ya uchoyo na ubahili Kwa hivyo basi Muislamu hatakiwi kuwa ni mwenye sifa ya uchoyo wala ubahili. Ubahili wenye kuambatana na uchoyo ijapokuwa ni maradhi katika maradhi ya moyo hasalimiki nayo mtu ilani kuwa mtu huyo awe ni Muislamu mwenye imani nzuri na matendo yake ni mema; kama kutoa zaka na kuswali. Allah Mtukufu anamkinga mtu huyu na ugonjwa huu mbaya ili amtayarishe kwa ajili, ya mafanikio ya Akhera Amesema Allah Aliyetukuka:

﴿ إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ۖ إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ۖ وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا ۗ إِلَّا الْمُصَلِّينَ ۗ الَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ۗ وَالَّذِينَ فِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُومٌ ۗ لِلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ۗ ﴾

“Hakika mwanadamu ameumbwa hali ya kulalama. Ikimpata shari anawayawaya na ikimpata kheri anazuia ila wenye kuswali ambao juu ya swala zao wanadamu na ambao katika mali zao pana haki yenye kujulikana kwa mwenye kuomba na mwenye kujizulia na kuomba.” (al-Ma’arif: 19-29).

Amesema Allah Aliyetakasika:

﴿ خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۗ ﴾

“Chukua kutoka katika mali zao sadaka utawatwaharisha na utawatakasa kwa hizo sadaka.” (Attawba:103).

Na Amesema Allah Mtukufu:

وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٩﴾

“Na mwenye kulingwa na ubakhili wa nafsi yake hao ndiyo wenye kufuzu.” (al-Hashr:9).

Taiba njema zinachumwa na kupatikana kulingana na namna ya mazoezi na malezi aliyopata mtu, Muislamu anaendeleza tabia bora na njema ambazo anataka kujipamba nazo, kwa kuyapitisha mawazo yake kwenye yale yaliokuja katika sheria yenye hekima. Hivyo basi hupendezea kwa kufanya tabia nzuri na hutishika kwa kuacha kueleza kwa kuhofia adhabu. Muislamu huvutika kufanya haya kwa kuzingatia kauli hizi zifuatazo za Allah Aliyetukuka:

وَأَنْفِقُوا مِنْ مَا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَا

أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٠﴾

“Enyi ambao mmeamini toeni baadhi ya vile ambavyo tumewaruzukuni kabla hayajamjia mmoja wenu mauti, akasema ewe Mola Wangu kwanni usingenichelewesha mpaka muda uliyo karibu nikatoa sadaka na nikawa miongoni mwa watu wema.” (al-Munafiquu:10).

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ ﴿١٠﴾ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿١١﴾ فَسَنِيَرُهُدٍ لِلْعُسْرَىٰ ﴿١٢﴾

وَأَمَّا مَنْ بَخِلَ وَاسْتَغْنَىٰ ﴿١٣﴾ وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿١٤﴾ فَسَنِيَرُهُدٍ لِلْعُسْرَىٰ ﴿١٥﴾

وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّىٰ ﴿١٦﴾

Ama yule ambaye ametoa na akamcha Mwenyezi Mungu, naakalisadikisha tamko la shahada huyo Tutamrahisishia kwa lile ambalo ni jepesi. Na ama mwenye kufanya ubakhili na akatosheka na akalikadhibisha tamko la shahada, Tutamrahisishia

kwa lile ambalo ni gumu na hayatomtosh amali yake pindi atakapoporomoka ndani ya moto.” (Allayl : 5-11).

وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ خَيْرٍ يُؤَفِّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿٥١﴾

“Na chochote mtakachokitoa miongoni mwa kheri mtalipwa na nyinyi hamtadhulumiwa.” (al-Baqarah:272).

Ama maneno ya Mtume ﷺ katika maudhui haya ni haya yafuatayo:

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkarimu na Anapenda ukarimu na Anapenda tabia bora na Anachukia tabia mbovu.” (Ibn Hajar).

“Hapana hasadi ila katika mambo mawili: Ni mtu ambaye amempa yeye Mwenyezi Mungu mali akamsaliti juu ya kuangamia mali hiyo juu ya haki na mtu ambaye amempa Mwenyezi Mungu elimu kwa hiyo yeye anahukumu kwa hiyo elimu na anawafundisha watu.” (Bukhari).

“Nani katika nyinyi mali ya mrithi wake inapendeza zaidi kwake kuliko mali yake? Wakasema, Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hapana yeyote katika sisi ila mali yake inapendeza zaidi kwake. Akasema:”Hakika mali yake ni ile ambayo ameichelewesha.” (Ibn Hajar).

“Jikingeni na moto ijapokuwa kwa kutoa kipande cha tende.” (Bukhari).

“Hapana siku yoyote ambayo anapambazukiwa waja ndani yake ila na malaika wawili wanateremka na anasema mmojawao Ee Mola wa Haki mpe mwenye kutoa badala na anasema mwengine.Ee Mola wa Haki mpe mweye kuzuiakubahili kuharibikiwa (hasana).” (Bukhari).

“Ugopeni ubahili wenye pupa, kwani ubahili wa namna hiyo umewaangamiza waliyokuwa kabla yenu, ukawapelekea juu ya kuzimwaga damu zao na wakayahalalisha mambo yaliyoharamishwa juu yao.” (Muslim).

Na kauli yake رضي الله عنه **“Amebaki mbuzi wote ila bega lake.”** Aliyasema maneno haya kumwambia Aisha رضي الله عنها wakati alipomuuliza kilichobaki katika mbuzi waliyemchinja, akasema, hakikubaki chochote katika nyama ya mbuzi wote ila bega la lake tu.

“Mwenye kutoa sadaka kwa kiasi cha tende kutokana na chumo zuri, na hakubali Mwenyezi Mungu ila kilicho kizuri, hakika Mwenyezi Mungu Ataipokea sadaka hiyo kwa Mkono Wake wa Kuume kisha Ataillea kumlelea mwenyewe kama anavyomlea mmoja wenu mtoto wafarasi wake, mpaka iwe sadaka hiyo mfano wa jabali.” (Bukhari na Ahmad).

Baadhi ya Sura za Utoaji:

- 1) Ni mtu kutoa atoacho pasina simbulizi wala maudhi.
- 2) Afurahi mtoaji kumfurahia muombaji ambaye amemuomba na afuarahi kwa kumpa
- 3) Atoe mtoaji pasina kuvuka mpaka katika kutoa, na pasina kujitia dhiki.
- 4) Atoe mwenye kingi kutokana na uwingi wake na mwenyekichache kutokana na uchache wake, katika kuridhia kwa nafsi na ukunjufu wa uso, na uzuri wa maneno.

Mifano ya utoaji wa hali ya juu ni:

- 1) Imepokewa kwa Aisha رضي الله عنها **“Kuwa alipelekewa na Muawiya mali dirham ambayo kiasi chake ni Dirham mia moja na thamanini elfu akaitisha sahani akaziweka humo akawa anazigawa kati ya watu, alipochwelewa na jua (jua lilipozama) alimwambia mjakazi wake, ‘Niletee kifungua kinywa changu,’**

akamletea mkate na mafuta na yulemjakazi akamwambia Bi Aisha, ‘Hukuweza katika Dirham ambazo umezigawa leo kutununulia nyama ukafungua kinywa kwayo?’ Aisha “akamjibu” Lau ungekuwa umenikumbusha ningefanya.’

2) Imepokewa kwamba Abdillahi Ibni Amar alinunua kutoka kwa Khalid IbnUqbah ibn Abi Muaity nyumba yake ambayo iko katika soko la Makkah kwa Dirham sabini elfu, ulipoingia usiku Abdillahi alisikia kilio cha watu wa Khalid akauliza sababu ya kilio kile akaambiwa, “Wanaisilia nyumba yao, akamwambia mtumishi wake waendee na uwaambie kuwa nyumba na vyote ni vyao.

3) Imepokewa kwamba Imamu Al-Shafi رضي الله عنه alipougua ugonjwa wake ambao aliofia ndani yake alusia aoshwe na fulani, alipokufa walimwita yule ambaye aliusiwa kumwosha alipokuja alisema, ‘Nipeni kumbukumbu yake’ wakampa ghafla ndani yake mkawa na maneno haya yafuatayo, ‘Pana juu ya Shafii deni ambalo kiasi chake ni Dirham sabini elfu yule mtu akaziandika ili azilipe kwa wenyewe, na akasema, huku ndiko kumwosha kwangu na akaenda zake.

4) Imepokewa kwamba alipojiandaa Mtume عليه السلام kavita vya Warumi, Waislamu wakati huo walikuwa katika dhiki kubwa na uzito mkubwa mpaka liliitwa jeshi la Mtume katika vita hivyo ni “*jeshi la uzito.*” Uthmani Ibn Affan رضي الله عنه alitokana sadaka ambayo kiasi chake ni Dirham elfu kumi na mia tatu pamoja na mashuka yake, matandiko yake na farasi hamsini aliweza kuandaa nusu ya matumizi ya jeshi la Mtume عليه السلام katika vita hivyo vigumu.



Mada ya Kumi na Moja
Kuhimiza Tabia ya Unyenyekevu na
Kukataza Tabia ya Kibri

Muislamu ananyenyekea pasi na kudhalilika wala kunyongea, na unyenyekevu ni katika tabia zake za kuigwa fano na sifa zake za juu, kama ambavyo kiburi si chake na wala hakitakikani kwa mtu mfano wake, kwani Muislamu ananyenyekea ili anyanyuke juu na wala hatakabari ili asije akaporomoka kwa sababu utaratibu wa Allah umepita katika kuwanyanyua wale wenye kunyenyekea Kwake na kuwaweka chini wale wenye kutakabari Amesema Mjumbe wa Allah ﷺ:

“Haikupunguza sadaka mali (ya mtoaji) na hakumuongezea Allah mja yeyote kutokana na kusamehe ila utukufu na hakunyenyekea mtu yeyote kwa Mwenyezi Mungu ila Allah humnyanyua.” (Muslim).

Mtume ﷺ alisema,

“Imethibiti juu ya Allah kuwa hakijinyanyui chochote duniani ila Allah hukishusha chini.” (Abu Dawud na An-Nasai).

Na amesema Mtume ﷺ,

“Watakusanywa wenye kutakabari (wenye kiburi) Siku ya Kiyama mfano wa sisimizi katika sura za watu, utawafunika udhalili kila mahali, watachukuliwa kupelekwa kwenye jela ndani ya moto wa Jahannam, utakuwa juu ya jela hiyo moto mkali sana, watanyweshwa kutokana na mkamuo wa watu wa motoni, ambao ni usaha wa watu wa mtoni.” (Ahmad na Al-Tirmidhy).

Muislamu wakati anaposikiza kwa masikio yake na kuzingatia moyoni mwake kwenye mfano wa habari kama hizi ambazo ni za ukweli kutokana na maneno ya Allah (s.w.t.) katika kuwasifu wanyenyekevu mara moja na kuwaponda wenye kiburi mara nyingine na mara katika kuamrisha unyenyekevu na mara nyingine katika kukataza kiburi, kwanini asinyenyekee? Na ikiwa kunyenyekea ni tabia

kwake na kwa nini asijiepushe na kiburi na asiwachukie wenye kiburi? Amesema Allah (Mtukufu) katika kumwamrisha Mtume wake ﷺ kuhusu kufanya unyenyekevu:

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ط

“Na wala usiende katika ardhi kwa kiburi.” (al-Isra: 37).

Na amesema katika kuwasifu wapenzi wake kwasifa ya unyenyekevu waliyonayo:

تُحِبُّهُمْ وَتُحِبُّونَهُمْ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ

“Anawapendana wanampenda wanyenyekevu juu ya waumini wakakamavu juu ya makafiri.” (al-Maidah: 54).

تِلْكَ الْأْدَارُ الْأَخْرَةُ نَجْعَلُهَا لِلَّذِينَ لَا يُرِيدُونَ عُلُوًّا فِي الْأَرْضِ وَلَا فَسَادًا ء

“Hiyo nyumba ya akhera tutaijifanya kuwa ni ya wale ambao hawataki ujuu katika ardhi wala ujisadi...” (al-Qaswas:83).

Mjumbe wa Allah ﷻ katika kuamrisha unyenyekevu amesema:

“Hakika Allah ameleta ufunuo kwangu kwamba nyenyekeeni mpakaasijifakhaishe yeyote wala asifanye uovu yeyote juu ya mwengine.” (Muslim).

Na amesema Mtume ﷺ katika kuwavutia watu katika kufanya unyenyekevu,

“Hukumpeleka Allah Mtume ﷺ yeyote ila Mtume huyo alichunga mbuzi wakamwambia masahaba zake na wewe? Akasema, ‘Ndiyo na mimi nilikuwa nikiwachunga kwa ujira maalumu kwa watu wa Makka.’ (Bukhari).

”Lau nikaalikwa kwenye mguu (kongolo) mwembamba wa mbuzi au kwenye mkono wake ningeliitika na kama ningeletewa zawadi kwangu ya mkono au(kongolo) ningekubali.” (Bukhari).

Mtume ﷺ amesema, katika kuwafanya watu wawe mbali na kiburi,

“Hivi si wapi habari kuhusu watu wa motoni? Ni kila mgumu wa tabia mwenye kukusanya mali na kuzuia mwenye kiburi.”
(Muslim na Ahmad).

Na amesema tena,

“Watu watatu hatawasemesha Allah Siku ya Kiyama na hatawatakasa na wala hatawaangalia na wanaadhabu yenye kutia uchungu mzinifu, na mfalme mrongo na fakiri mwenye kiburi.” (Abu Dawud).

Katika hadithi nyingine amesema tena Mtume ﷺ,

“Allah ﷻ amesema, Utukufu ni Shuka Yangu ya juu, na Ukubwa (Kiburi) ni Shuka Yangu ya chini, mwenye Kuinyang’anya Mimi kimoja katika hivyo hakika Nimekwisha Kumwadhibu.”
(Muslim).

Na amesema Mtume ﷺ:

“Wakati mtu mmoja yumo katika vazi lenye kupendeza, nafsi yake inamfanya aione, akiwa amechana nywele zake, anafanya kiburi katika kwenda kwake, ghafla Allah akimzamisha yeye ardhini kwa hiyo yeye anendelea kuzama katika ardhi mpaka Siku ya Kiyama.” (Bukhari).

Sura za Wazi Zinazoonyesha Unyenyekevu:

1) Akitangulia mtu juu ya watu mfano wake, huyo ni mwenye kiburi na akikaa nyuma yao huyo ni mnyenyekevu.

2) Akisimama kutoka katika kikao chake kwasababu ya mwenye elimu au ubora na akamkalisha hapo, na akisimama anamsawazishia viatu vyake na akitoka nyuma yake mpaka katika mlango wa nyumba kwa ajili ya kumsindikiza huyo ni mnyenyekevu.

3) Akisimama mtu wa kawaida na akakabilia naye kwa furaha na kwa ukunjufu wa usona akafanya upole pamoja naye katika kuuliza na akaitika mwaliko wake na akaenda katika haja yake na wala haoni nafsi yake bora kuliko yeye huyo ni mnyenyekevu.

4) Atakapokaa pamoja na mafakiri na masikini na wagonjwa na wenye vilema akautikia mwaliko wao na akala pamoja nao na akatembea nao katika njia yao huyo ni mnyenyekevu.

5) Atakapokula au kunywa pasina kuvuka mpaka na akavaa pasina kiburi, huyo ni mnyenyekevu.

Mifano ya Unyenyekevu:

1) Imepokewa kwamba Umar Ibn Abdul Aziz alimwendea usiku mgeni wake na alikuwa akiandika ikakaribia taa yake kuzimika, akasema yule mgeni: Nisimame mwenyewe nitengeneze taa? Umar akasema: “Si katika ukrimu kwa mtu mgeni”, ikiwa hivyo nitamuamsha mtumishi? Umar akasema, ‘Ndiyo kwanza amelala, usimwamshe: Umar akaenda mwenyewe kwenye chupa ya mafuta na akajaza taa mafuta. Mgeni akamwambia, ‘Umesimama wewe mwenyewe ewe kiongozi wa waumini?’ Umar akajibu kwa kusema, ‘Nimekwenda nikiwa Umar, na nimerudi nikiwa Umar hakikupungua kwangu kitu chochote na mbora wa watu ni yule ambaye amekuwa mnyenyekevu mbele ya Mwenyezi Mungu.’

2) Imepokewa kwamba Abu Huraira رضي الله عنه alikuja kutoka sokoni hali ya kuwa amebeba mzigo wa kuni na hali ya kuwa yeye siku hiyo ni kiongozi wa mji wa Madinah wakati wa utawala wa Marwan. Ilikuwa ni kawaida

Abu Huraira kusema, “Toeni nafasi kwa kiongozi apite kwani amebeba mzigo wa kuni.”

3) Umar Ibn Al-Khattab alionwa siku moja akiwa amechukua nyama kwa mkono wake wa kushoto na katika mkono wake wa kulia ameshika fimbo na hali ya kuwa yeye ni kiongozi wa Waislamu na ni Khalifa wao wakati huo.

4) Imepokewa kuwa wakati Fulani Ali Bin Abi Talib alinunua nyama akaweka katika mkoba wake na kubeba, akaambiwa na mtu, “Tukubebee ewe, Amirul Muuminiin?” Ali akajibu, ‘Hapana, Baba wa watoto ni mwenye haki zaidi kubeba.’

5) Amesema Anas Ibn Malik رضي الله عنه:

“Hakika alikuwa mjakazi katika wajakazi wa Madina hushika mkono wa Mtume ﷺ na anakwenda nao anakotaka.” (Bukhari).

6) Amesema Abu Salama: Nilmwambia Abu Said Al-Khudri una maoni gani katika yale ambayo wameyazusha watu miongoni mwa mavazi na vinywaji na vipandwa na chakula? Akasema, “Ewe mtoto wa ndugu yangu, kula kwa ajili ya Allah navaa kwa ajili ya Allah na kila kitu katika hivyo kilichoingiliwa na kiburi au kujifaharisha au kutaka umaarufu hilo litakuwa ni maasi na kuvuka mipaka, na fanya katika nyumba yako miongoni mwa huduma mbalimbali zile ambazo alikuwa akizifanya Mtume wa Allah ﷺ nyumbani kwake.

Abu Said akaendelea kumueleza Abu Salama, kuwa “Mtume ﷺ alikuwa akimpa majani mnyama anayehitaji, maji na chakula na anamfunga ngamia, anafagia nyumba na akikama maziwa ya mbuzi, akishona viatu, akitia viraka nguo, akila pamoja na mtumishi wake, akimsaidia mkewe kusaga anapochoka, akinunua vitu mwenyewe kutoka sokoni na wala hakimzuii hayakuning’iniza mkono wake au kukiweka katika ncha ya nguo yake. Akirudi kwa watu wake wa nyumbani, alikuwa akipeana mikono na tajiri na fakiri, mkubwa kwa mdogo na alikuwa akianza kumsalimia kila anayekutana naye miongoni mwa wa kubwa au wadogo, weusi au wekundu, waungwana au watumwa wakati wa Sala.”



Mada ya Kumi na Mbili

Aina Mbali Mbali za Tabia Mbaya

**Dhulma, Husda, Udanganyifu, Ria, Kujiona,
Uzembe na Uvivu.**

a) **Dhulma:**

Muislamu hadhulumu na wala hadhulumiwi kwa hiyo haitatokea dhulma kwake kumdhulumu mtu yeyote na wala hakubali kudhulumiwa na mtu yeyote kwa sababu dhulma kwa namna zake tatu ni haramu katika Qu'ani na Sunna kwa pamoja. Amesema Allah (Mtukufu):

لَا تَظْلِمُونَ وَلَا تُظْلَمُونَ

“Hamtadhulumu nahamtadhulumiwa.”(al-Baqarah: 279.

Na amesema Allah (s.w.t.) katika yale ambayo ameyapokea Mtume kutoka Mola wake,

“Enyi waja wangu hakika Mimi Nimeiharamisha dhulma juu ya Nafsi Yangu na Nimeifanya kuwa ni yenye kuharamishwa kati yenu kwa hiyo msidhulumiane.” (At-Tirmidhi).

Ama Mtume ﷺ amesema,

“Dhuluma ni viza Siku ya Kiyama:.” (Ahmad na al-Hakim)

Na amesema,

“Mwenye kudhulumu kiasi chasubiri ardhi atafungwa nayo shingoni mwake ardhi saba” (Bukhari na Muslim).

Na amesema tena,

“Hakika Allah anampa muda (umri mrefu) dhalimu na akimtia mikononi haponyoki”,

Kisha akasema aya katika Qur'an,

وَكَذَلِكَ أَخَذَ رَبُّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرْآنَ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخَذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿١٠٢﴾

“Ni kama hivyo mashiko ya Mola wako akivikamata vijiji na hali ya kuwa vimefanya dhulma hakika mashiko yake yanaaumizanani makali sana.” (Hud: 102).

Na Mtume ﷺ amesema,

“Na iogopeni dua ya mwenye kudhulumiwa kwani hakika hapana kati ya maombi hayo na Mwenyezi Mungu pazia lolote.” (Daraqutniy na Bayhaqi).

AinaTatu za Dhulma:

1) **Dhulma ya mja (mtu) kumfanyia Molawake** na hilo linapatikana kwa kumkufuru? Allah, Amesema Allah Mtukufu,

وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٥٤﴾

“Na makafari wao ndiyo madhalimu.” (al-Baqarah:254).

Na linakuwa hilo kwa kumshirikisha Allah Mtukufu katika kuabudiwa Kwake, kwa kutoa baadhi ya ibada yake Allah na kumuabudu asiyekuwa Yeye. Amesema Allah Mtukufu:

إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿١٣﴾

“Hakika shirki ni dhulma kubwa sana.” (Luqman:13).

2) **Dhulma ya mja kumdhulumu mtu mwingine** katika waja wa Allah na viumbe wake na hilo ni kwa kuwaudhi katika heshima zao au viwili wili vyao au mali zao pasina haki. Amesema Mtume wa Allah ﷺ:

“Mtu yeyote yule ambaye imepatikana kwake dhulma kwa ndugu yake katika heshima yake au kitu chochote basi amtake radhi leo leo kabla ya kufika siku ambayo hapata kuwepo Dinari wala Dirham, akiwa na matendo mema yatachukuliwa katika mabaya ya mwenzake ya abebeshwa juu yake.” (Al-Bayhaqi katika Sunan al-Kubra).

Na amesema,

“Mtu yeyote mwenye kuikata haki ya mtu Muislamu kwa mkono wake na kuume hakika amewajibisha Allah juu yake moto na ameharamisha juu yake pepo. Akasema mtu mmoja: ‘Ijapokuwa haki yenyewe ni kitu kidogo ewe Mjumbe wa Allah Mtume (s.a.w.) akasema: “Ijapokuwa ni kijiji chamswaki (mpilipili tawa).” (Muslim).

3) Mtu kudhulumu nafsi yake na hilo linapatikana kwa kuiingiza nafsi katika matendo maovu na kuichafua kwa aina za madhambi na uhalifu na maovu mbalimbali katika kumuasi Allah na Mtume wake, Amesema Allah Mtukufu,

﴿ وَمَا ظَلَمُونَا وَلَكِن كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴾

“Na hatukuwa dhulumu lakini walikuwa wakizidhulumu nafsi zao.” (al-A’raaf: 160).

Mwenye kutenda maovu makubwa miongoni mwa madhambi na mambo machafu huyo ni mwenye kudhulumu nafsi yake kwa sababu ameingia katika mambo ambayo yanaathiri nafsi yake na yeye mwenyewe. Miongoni mwa uovu na dhulma kwa hiyo anastahiki kulaaniwa na Allah na kuwa mbali na Allah Mtukufu.

(b) Husda

Muislamu hafanyi husda (hawi hasadi) na wala haiwi hasadi ni tabia kwake au sifa yake, muda wa kuwa anawapendelea kheri watu wote na anawaweka mbele kuliko nafsi yake katika hiyo kheri, kwa sababu husuda inapingana na zile tabia mbili bora; Kupenda kheri na kupendelea kheri.

Muislamu hapendi tabia ya husda na anaichukia kwa sababu kufanya husda ni kupinga ugawaji kwa Allah na fadhila zake kwa viumbe Wake Amesema Allah (Mtukufu)

أَمْ تَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ

“Hivi wanawahusudu watu juu ya kile ambacho amewapa wao Allah kutokana na fadhila yake?” (Annisa: 54).

Na amesema Allah Mtukufu:

أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ ۗ نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَعِيشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ
وَرَفَعْنَا بَعْضَهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِيَتَّخِذَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا سُخْرِيًّا ۗ

“Hivi wao wanaigawa rehema ya Mola wako? Sisi Tumegawa kati yao maisha yao katika uhai wa dunia na Tumegawanya baadhi yao juu ya baadhi kwa daraja ili wawafanye baadhi yao baadhi kwa wengine wenye kudhalilishwa.” (43:32).

Husda imegawanyika katika mafungu mawili:

Kwanza: Ni kutamani mtu kuondokaneema miongoni mwa mali, elimu au kumuondokea mtu mwingine ili mambo hayo yapatikane kwake.

Pili Na hili ndilo baya zaidi ni kutamani kumuondokea neema mtu mwingine hata kama neema hiyo haitahamia kwake na akaipata. Na si katika husda *Al-Ighitiba't Ghibtwa* ni kutamani kupata neema mfano wa neema ya fulani miongoni mwa elimu au mali au mambo kuwa mazuri na hali kuwa hutamani kundoka mambo hayo kwa mtu mwingine, kutokana na Kauli Yake Mtume ﷺ.

“Hapana husda (inayokubaliwa) ila katika mambo mawili. Mtu ambaye Allah amempa mali akaitumia katika haki, na mtu ambaye Allah amempa elimu kwa hiyo yeye akawa anahukumu kwa elimu hiyo na anaifundisha.” (Bukhari).

Minhajil Muslim

Mradi wa hekima hapa ni Qur’ani Tukufu na Sunna za Mtume ﷺ; Husda kwa mafungu mawili limeharamishwa uharamu wa moja kwa moja, kwa hiyo si halali kwa mtu yeyete kumuhusudu mtu yeyote. Allah Amesema;

أَمْ تَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

“Hivi wanawahusudu watu juu ya kile ambacho amewapa wao Allah ambacho ni katika fadhila Yake?” (Annisaa:54)

Na amesema tena katika sura nyingine,

حَسَدًا مِّنْ عِنْدِ أَنفُسِهِمْ

“Kwa hasadi tu lenye kutokana na nafsi zao?” (2:109).

Na amesema:

وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ

“Na shari ya mwenye husda pindi atapofanya hiyo husda?” (al-Falaq:5).

Kwa hiyo Allah (Mtukufu) anapokashifu na kuiponda tabia hii mbaya anatoa hukumu ya kuharamishwa kwake na kukatazwa.

Ama Mjumbe wa Allah ﷻ yeye amesema,

“Msibughudhiane walamshusudiaena wala msipeane migongo na wala msikatane udugu na kuweni enyi waja wa Allah ndugu si halali kwa Muislamu kumhama ndugu yake Muislamu zaidi ya siku tatu” (Bukhari, Muslim, Abu Daud).

Na amesema:

“Tahadharini na husda kwani inakula matendo mema kama moto unavyokula kuni au nyasi.” (Abu Daud).

Muislamu yakimpitia mawazo ya husda kutokana na ubinadamu wake na kutokana na kutokingwa kwake, hupambana na mawazo hayo kwa kuyasukuma na kuyatoa katika nafsi yake na anayachukia mpaka yasiwe ni makusudio yake au ni azma yake na ili asije akasema kutokana na hasadi au akatenda naakaangamia kutokana na hasadi. Ikitokea kuvutiwa na kitu chochote husema, 'Alichotaka Allah kimekuwa na hapana nguvu ila kutokana na Allah na kwa kusema hivyo hakutakuwa na athari mbaya kweke na atasalimika.

b) Kudanganya

Muislamu ananyenyekea kwa Allah Mtukufu kwa kumnasihi kila Muislamu na maisha juu yake kwa hiyo hapana njia yoyote kwake ya kumfanyia udanganyifu mtu yoyote, au kufanya utapeli au kufanya hiyana kwani kufanya udanganyifu, hiyana na utapeli ni sifa zisizotakiwa na ni mbaya kwa tuna ubaya hautakiwi kuwa tabia kwa Muislamu yoyote wala kuwa sifa kwake kwa hali yoyote ile. Kwani usafi wa nafsi yake alioupata kutokana na imani na matendo yake mema unapingana na tabia hizi mbaya na ambazo ni shari tupu hazina kheri ndani yake na Muislamu yuko karibu na kheri na yuko mbali na shari.

Tabia ya Kughushi Ambayo Ni Mbaya sana na Ukweli, ubaya huo unajionyesha katika haya Yafuatayo:

i) Ni mtu kumpambia(kumsifu) ndugu yake ubaya au shari au ufisadi. Ili atumbukie ndani yake.

ii) Ni kumuonyesha sehemu ya nje ya kitu ambayo ni nzuri na njema na kumficha sehemu yake ya ndani iliyo chafu na mbaya.

iii) Ni kumdhirishia kinyume cha yale anayodhamiria moyoni mwake na kuyaficha ili amhadae na amadanganye kwa ghushi.

iv) Ni kukusudia kukiharibu kile ambacho ni haki yake au mali yake au mkewe au mtoto wake au rafiki yake au mtumishi wake kwa kupenyeza ufisadi ndani yake na fitna.

v) Ni kutoa ahadi juu ya kulinda nafsi au mali au kuficha siri kisha akafanya hiyana na akadanganya. Muislamu katika kujiepusha kwake, kughushi,

kudanganya na kufanya hiyana. Yeye ni mwenye kumtii Allah na Mtume wake kwani mambo hayo matatu yameharamishwa katika kitabu cha Allah na Sunna za Mtume wake ﷺ.

Amesema Allah Mtukufu katika sura zifuatazo:

وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ بَغَيْرِ مَا اكْتَسَبُوا فَقَدِ
أَحْتَمَلُوا بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿٥٨﴾

“Na wale ambao wanawaudhi waumini wanamume na waumini wanawake kwa yasiyokuwa yale ambayo wameyachuma, hao wamebeba uzushi na madhambi makubwa sana.” (Al-Ahzaab:58).

فَمَنْ نَكَثَ فَإِنَّمَا يَنْكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۗ

“Na mwenye kuvunja ahadi hakika hapana jambo jingine anajivunja yeye mwenyewe.” (al-Fath: 10).

وَلَا تَحْقِيقُ الْمَكْرُ السَّيِّئُ إِلَّا بِأَهْلِهِ ۗ

“Na wala havishuki vitimbwi viovu ila kwa wenye vitimbi hivyo.” (Fatir:43).

Ama Mtume wetu Muhammad ﷺ amesema katika hadithi zake haya yafuatayo,

“Mwenye kumfisidi mke wa mtu au mtumishi wake huyo si katika sisi.” (Abu Dawud).

Na amesema:

“Mambo manne mtu ambaye yatapatikana kwake atakuwa mnafiki aliye wa hakika (hasa hasa), na ambaye litapatikana kwake jambo moja katika hayo atakuwa na sehemu ya unafiki

mpaka atakapoliacha: Akiaminiwa anakhini na akizungumza anasema urongo na akitoa ahadi anavunja na akigombana anafanya uovu.” (Bukhari na Muslim).

Na amesema Mtume ﷺ na alipopita kwenye mfuko mkubwa wenye chakula akaingiza mkono wake ndani ya mfuko ule vidole vyake vikapatwa na unyevu akasema:

“Nini hiki ulichofanya ewe mwenye chakula?” Akasema, “Kimepatwa na mvua Ewe Mjumbe wa Allah”, Akasema: “Kwanini usingeweka hii (sehemu ambayo imepatwa na mvua) juu ya chakula ili watuwaweze kuiona? Mwenye (kutughushi) kutudanganya huyo si katika sisi.” (Muslim).

c) Kujionesha (Riya).

Muislamu hafanyi matendo kwa kujionesha kwa watu, jambo hilo ni la kinafiki na shirki na Muislamu ni muumini mwenye kumpwekesha Allah (s.w.t.) kwa hakika jambo hili linapingana na imani yake na upwekesho wake kwa Mola wake. Muislamu kwa hali yoyote ile hawi mnaifiki wala mwenye kufanya matendo kwa kujionesha ili watu wamuone.

Kuna mtosha Muislamu katika kuichukia tabia hii mbaya kujiepusha nayo. Na kujua kuwa Allah na Mtume wake ﷺ wanaichukia na kuibughudhi juu yake kwani amesema Allah Mutukufu akiwakemea wenye kufanya matendo kwa kuwaonyesha watu kuwa watapata adhabu na mateso:

فَوَيْلٌ لِلْمُصَلِّينَ ۖ الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٤﴾ الَّذِينَ هُمْ
يُرَاءُونَ ﴿٥﴾ وَيَمْنَعُونَ الْمَاعُونَ ﴿٦﴾

“Adhabu kali ni kwa wale wenye kusali ambao wao sala zao wanazisahau (Katika nyakati zake), ambao wao ni wenye kuonyesha watu matendo yao na wanazuia misaada.” (al-Maun:4-7)

Minhajil Muslim

Amesema Allah katika yale ambayo ameyapokea kutoka kwake Mjumbe wake Mtume Muhammad ﷺ.

“Mwenye kufanya matendo akamshirikisha ndani ya matendo hayo (Mungu) mwingine asiyekuwa Mimi basi matendo hayo yote ni yake na Mimi Ni mwenye kujisha kabisa nasi mwenye kutegemea washirika.” (Ahmad na Muslim).

Na Mtume ﷺ amesema:

“Mwenye kufanya jambo lolote kwa kujionyesha, Allah atamfanya awe mwenye kuonwa: na mwenye kufanya ili kuakakusikika, Allah atamfanya asikike.” (Muslim).

Hali kadhalika katika hadithi nyingine,

“Hakika khofu kubwa ninayokhofioa juu yenu ni shirki ndgo Maswahaba wakauliza: ‘Ni ipi shirki ndogo Ewe Mjumbe wa Allah’ Mtume ﷺ akasema: Ni ‘Riyaa’ Akasema Allah (s.w.t.) Siku ya Kiyama wakati atakapowalipa waja kwa matendo yao. Nendeni kwa wale ambao mlikuwa mkiwaonyesha matendo yenu huko duniani, tazameni jee, mtakuta kwao malipo?’” (Ahmad). Amakwa hakika Riyani mtu kutaka kumtii Allah (s.w.t.) kwani aya kutaka kupata hadi na cheo katika mioyo ya watu.

Mambo yenye kuonekana miongoni mwa hayo ni haya yafuatayo:

- 1) Ni mja kuzidisha kufanya ibada pindi anaposifiwa au kupunguza kufanya ibada na pengine kuacha kabisa anapobainisha au anaposemwa vibaya.
- 2) Ni kuwa mchangamfu katika ibada pindi akiwa pamoja na watu na akawa mvivu na ibada hiyo pindi anapokuwa peke yake.
- 3) Ni kutoa sadaka anapoona kuna watu na kama hakungwekuwa na watu asingetoa.
- 4) Ni kusema anayoyasema miongoni mwa haki na heri au kufanyayalembayo anayafanya miongoni mwa ibada na mambo mema hali ya kuwa yeye hamkusudii

kwa matendo hayo Allah Peke Yake bali anamkusudia mwingine miongoni mwa watu moja na Allah au hamkusudii Allah kabisa bali anawakusudia watu tu.

d) Kujionana Kudanganyika:

Muislamu anajitahadhari na kuwa na sifa ya kujiona na kudanganyika na anajitahidi yasiwe hayo ni sifa kwake, katika hali yoyote kwani hayo mawili ni miongoni mwa vikwazo vikubwa sana vya kufikia kwenye ukamilifu (wa kibinadamu) na ni miongoni mwa maangamio makubwa hivi sana huko mbele.

Ni neema ngapi ambazo zimewageukia watu na kuwa ni balaa au vikwazo katika maisha yao? Ni watu wangapi na makundi au mataifa mangapi yaliyokuwa na nguvu na kujigamba lakini mwishowe zimegeuka kuwa ni dhalili?

Inatosha sifa hizo kuwa ni ugonjwa usiyokuwa na dawa na inatosha kwa sifa hizi juu ya mwenye kuwa nazo kuitwa kuwa ana balaa na kwa ajili hiyo amejitahadharisha Muislamu na anaziogopa na kwa ajili hiyo imekuja katika Qur'ani na Sunnah kuziharamisha na kuwaepusha watu nazo na kuwatahadharisha nazo, Amesema Allah Mtukufu.

﴿وَعَزَّزْتُكُمْ بِالْأَمَانِيِّ حَتَّىٰ جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ وَعَزَّزْتُكُمْ بِاللَّهِ الْغَرُورِ﴾

“Na yamewadanganyeni matumaini (mkajisahau) mpaka ikaja amri ya” Allah na akawadanganyeni kwa ‘Allah mdanganyifu (shetani).” (al-hadyd:14).

﴿يَتَأَيُّمُ الْإِنْسَانُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ﴾

“Ewe mwanadamu ni lipi lililokudanganyausimtii Molawako aliye mkarimu?” (al-Infitar:6)

﴿وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبْتَكُمْ كَثَرْتُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا﴾

“Na siku ya Hunaini wakatiuliopowapa kichwa uwingi wenu kisha asiwatoshe kitu chochote.” (Attawba:25).

Mtume ﷺ amesema katika hadithi zifuatazo,

“Mambo matatu ni yenye kuangamiza, ubakhili wenye kutiwa na matamano yenye kufuatiwa, na kupendezwa mtu na nafsi yake basi.” (al-Hithami nayo ni dhaifu).

“Utakapounauba hili wenye kutiwa na matamano yenye kufuatwa, na kupendezwa kila mtu na rai yake basi hapo shikamana na nafsi yako.” (Azzaaydy na Twabari).

“Mwervevu ni yule aliyehisabu nafsi yake na matendo yake yakamsaidia baada ya kufa. Na mpumbavu ni yule ambaye ameifuatisha nafsi yake matamano yake na akatamani kwa Allah matamano mengi.” (Imam Ahmad na al-Hakim).

Mifano ya Hilo:

1) Iblisi laana ya Allah iwe juu yake Alijiona kwa hali yake, alidanganyika kutokana nafsi yake naasili yake, akasema: **“Umeniumba mimi kutokana na moto na umemuumba yeye (Adam) kutokana na udongo.”** Allah Akamfukuza kutoka katika Rehema Yake na kutoka katika liwaziko la hadhara ya Utakatifu Wake.

1) Waliona watu wa ‘Aadi kutokana na nguvu zao, walidanganyika kutokana na uwezo wao na wakasema: Ni nani wakubwa zaidi kwa nguvu kuliko sisi? Allah akawaonjesha adhabu ya udhalili katika maisha ya dunia na huko akhera.

2) Mtume wa Allah Sulaiman عليه السلام alighafilika kwa kusema: **“Nitazunguka usiku huu kwa wanawake mia moja na atazaa kila mmoja mtoto atakayepigania Dini ya Allah.”** Alighafilika kusema Insha Allah: Akipenda Allah kwa sababu hiyo Allah akamnyima mtoto.

3) Walijiona Masahaba wa Mtume wa Allah ﷺ katika vita vya Hunaini kutokana na wingi wao na wakasema: ‘Hatutashindwa leo kutokana na uchache wetu.’ Wakapatwa na kushindwa kubaya sana mpaka ikawa finyu kwao ardhi pamoja na upana wake, wakakimia. Mpaka pale waliporejea kwa Mweyezi Mungu akawanusuru.

Sura za Wazi za Kudanganyika ni:

1) **Katika elimu:** Huenda mtu akajiona kutokana na elimu yake na akadanganyika kutokana na wingi wa mambo anayoyajua, likampelekea hilo kuacha kujiongezea elimu, na kuacha kufaidika kutoka kwa wenzake au likampelekea hilo kumdharau mtu mwengine katika wenye elimu na kumuna duni mtu mwengine, inatosha kutokana na hali hiyo kuwa ni maangamivu kwake.

2) **Katika Mali:** Huenda akiona mtu kutokana na wingi wa mali yake na akadanganyika kwa wingi wa vitu vyake, kwa hiyo anatumia vibaya na kwa kuvuka mipaka na anajikweza juu ya viumbe na anaikanyaga haki matokeo yake anaangamia.

3) **Katika Nguvu:** Huenda mtu kutokana na wingi wa nguvu zake, na kutokana na utukufu wake na uwezo wake anadanganyika kwa kuvuka mipaka na kudhulumu, na kucheza kamari na anafanya mambo ya hatari ya yakatokea katika nguvu zake maangamio na balaa kwake.

4) **Katika Utukufu:** Huenda mtu akajiona kutokana na utukufu wake na akadanganyika kutokanana uzawa wake, asili yake, akakaa na akaacha kuyatafuta mambo ya ukamilifu, kwa hiyo humweka nyuma matendo yake, kwani haumpeleki mbele ukoo wake, na asili yake, hivyo anabaki kuwa dhalili na anakuwa mtu wa chini, na anakuwa hana uzito wowote katika jamii.

5) **Katika Ibada:** Huenda mtu akajiona kutokana na matendo yake, na akadanganyika kutokana na wingi wa Ibada zake, likampelekea hilo kujidekeza juu ya Bwana wake nakujionyesha kuwa anafanya wema juu ya Allah mneemeshaji wake, kwa hiyo amali (ibada) yake inabatilika na anaangamia kutokanana kujiona kwake, na anakuwa muovu kutokana na kudanganyika kwake.

Tiba juu ya hayo:

Kuutibu ugonjwa huu, tiba yake inapatikana katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuelewa kuwa Alichompa leo miongoni mwa elimu, mali, nguvu, utukufu au ubora huenda akamnyang'anya hayo kesho akitaka. Na kwamba Ibada ya mja kwa Bwana wake vyovyote zitakavyokuwa nyingi, hazilingani sawa na baadhi ya yale ambayo ameyaneemesha Mwenyezi Mungu juu yake.

Allah Mtukufu ndiye chimbuko la fadhila zote, ni Mtoaji wa kheri zote, na kwamba Mtume ﷺ amesema,

“Hayata muokoa mtu yoyote katika nyinyi matendo yake maswahaba wakauliza, “Hata wewe Ewe Mjimbe wa Mwenyezi Mungu?” Mtume Akawajibu, “Ndio, hata mimi mpaka atakaponigubika mimi Mwenyezi Mungu kwa Rehema Yake.” (Bukhari).

e) Kushindwa na kuwa Mvivu:

Muislamu hatakiwi kushindwa wala kuwa mvivu, bali anajifunga na anakuwa mchangamfu, anafanya kazi, anakuwa na pupa katika kujishughulisha kwani kushindwa na uvivu ni tabia mbili mbaya. Mtume ﷺ aliomba kukingwa nazo kwani mara nyingi sana Mtume ﷺ alikuwa akisema,

“Ee, Mola wa haki hakika mimi na jilinda kwako na kushindwa na uvivu wa uoga, na ukongwe, na ubakhili.” (Bukhari, Muslim na An-Nasai).

Hali kadhalika Mtume ﷺ aliusia watu kufanya kazi na kuwa na pupa ya kufanya kazi pindi aliposema,

“Fanya pupa (haraka) juu ya lile ambalo linakufaa, nataka hifadhi kwa Allah na wala usishindwe, na likikupata jambo lolote, usiseme lau kama nisingefanya hivi haingekuwa hivi, lakini sema amekadiria Allah na Alilolitaka amelifanya kwani tamko la “Lau”, “Lau”, linafungua matendo ya shetani.” (Muslim).

Kwa msingi huo Muislamu haonekani kuwa ni Mwenye kushindwa na wala mvivu kama ambavyo haonwi kuwa ni muo ngo wala bahili naiweje kuwa Muislamu akae tuna kuacha kufanya kazi au akaacha kuyapupia yale anbayo yana mfaa, na hali ya kuwa yeye anaiamini nidhamu ya sababu na kanuni za taratibu za mwenendo wa Ulimwengu ulivyo? Na kwanini afanye uvivu Muislamu, na hali ya kuwa yeye anaamini wito wa Allah kwenye mashindano aliposema:

سَبِّحَ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٠٠﴾

“Shindaneni kuelekea kwenye msamaha kutoka kwa Bwana wenu. Na pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi.” (al-Hadyd:1).

Na anawaamrisha kuingia katika mashindano:

خَتَمَهُمْ مِسْكٌ وَفِي ذَلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ الْمُتَنَافِسُونَ ﴿٢٦﴾

“Na katika kuyapata hayo basi na washindane wenye kushindana.” (al-Mutwaffifin: 26).

Na kwa nini awe muoga Muislamu au ajizuie kufanya mambo na hali ana uhakika wa hukumu ya Allah na ameamini makadirio Yake, na umejua kuwa lile ambalo limempata hali kuwa lenye kumkosa na kwamba lile ambalo limemkosa halikuwa lenye kumpata kwa hali yoyote na ni kwanini akae Muislamu akaacha kufanya kazi yenye manufaa na hali yeye anausikia wito wa Qur’ani kwake.

وَمَا يَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَنْ يُكْفَرُوا ﴿١١٥﴾

“Na lolote mlifanyalo miongoni mwa kheri hamtanyimwa malipo yake.” (al-Imran:115).

وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ مِنْ خَيْرٍ نَجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرٌ وَأَعْظَمُ أَجْرًا ﴿٢٠﴾

“...Mtakuta mbele za Mwenyezi Mungu kilicho bora sana na kikubwa sana kwa malipo.” (a-Muzzammil:20).

Sura za Wazi za Kushindwa na za Uvivu:

1. Ni kusikia mtu wito wa mwadhini wa Swala na akaendelea kujishugulisha kwa kulala au kwa kuzungumza au kufanya kazi ambayo si ya lazima, na wala asijibu mwadhini, mpaka ukakaribia kutoka wakati wa Sala. Kisha anasimama akisaliki peke yake mwishoni mwa wakati wa Sala.

2. Ni kuitumia mtu saa moja au masaa mengi juu ya magenge ya kahawa, au kurandaranda barabarani na sokoni, na hali ya kuwa pana kazi nyingi zenye kumsubiri ambazo zinahitaji kutekelezwa na yeye hazitekelezi.

3. Ni kuacha mtu kazi yenye manufaa kama vile kujifundisha elimu, kulima ardhi au kujenga na kuimarisha majumba makubwa na madogo madogo na yanayofanana katika hayo katika matendo yenye manufaa duiani au akhera. Anayaacha hayo kwa madai ya kuwa yeye ni mkubwa wa umri au kwamba yeye hafanani na kazi hii au kwamba kazi hii inahitaji wakati mpana na muda mrefu kazini au masaa mengi ya kazi, hivyo anaamua kuacha kazi na siku zinapita na hafanyi kazi yoyote atakayonufaika nayo katika dunia yake au akhera yake.

4. Ni kumtokea yeye mlango katika milango ya wema na kheri kama vile fursa ya kwenda Hija, na hali ya kuwa anao uwezo wa kuhiji asihiji. Au kama kupatikana mtu aliye katika maangamivu, na hali yakuwa yeye anaweza kumuokoa asimuokoe, au kama vile fursa ya kuingia mwezi wa Ramadhani asiyatumie masiku yake kwa kusimama katika kufanya Ibada tofauti mchana na usiku. Au kama vile kupatikana wazazi wawili wazee wenye kushindwa kujisaidia au mmoja wao na hali ya kuwa yeye anaweza kuwafanyia wema na kuwaunga na kuwafanyia hisani lakini asiweze kuwafanyia, kwa kushindwa au kwa uvivu kwa ubakhili, au kwa kuwaudhi, tuna muomba Allah atukinge na Mambo hayo.

5. Ni kufanya kazi mtu katika mji ambao yeye atakuwa katika hali ya udhalili au unyonge na asifanye jitihada zozote zile za kuondokana na hali hiyo na kuhamia sehemu nyingine ambayo ataihifadhi hapo Dini yake, na utaulinda hapo utukufu wake na heshima yake.

Ewe Mola wa haki tunataka hifadhi kwako na kushindwa na uvivu, na tuntaka hifadhi kwako na uuongo, na ubahili, na tunataka hifadhi kwako na kila tabia isiyoridhisha na tendo lisilo kuwa na manufaa.

Na Amrehemu Allah Mtume wetu Muhammad ﷺ na jamaa zake na swahaba zake wote.



Mlango wa Nne
Kuhusu Mambo ya Ibada



Mada ya Kwanza

Kuhusu Tohara

Somo la kwanza:

Kuhusu Hukumu ya Tohara na Maelezo Yake:

1. Hukumu yake

Kijitoharisha ni wajibu kwa mujibu wa *Qur-aan* na *Sunna*, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا فَأَطْهَرُوا

“Na mkiwa na janaba basi ogeni.” (al:Maidah 5: 6)

Na amesema (s.w).

وَتِيَابَكَ فَطَهِّرْ

“Na nguo zako, zisafishe.” (al- Mudatthir 74: 4)

Na amesema (s.w):

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao tubu na huwapenda wanao jisafisha..” (Al-Baqarah 2: 222).

Na amesema Mtume ﷺ,

“Ufunguo wa Swala ni Kujitoharisha.” (At-Tirmidhi, Abu Dawuud na Imam Ahmad).

Na amesema tena,

“Haikubaliwi swala bila kujitoharisha.” (At-Tirmidhi).
Pia “Kujitoharisha ni nusu ya imani.” (Muslim).

2. Maelezo yake:

Kujitoharisha Kunagawanyika Katika Mafungu Mawili, fungu la kiwiliwili na fungu la nafsi au kujitoharisha kwa ndani na kwa nje.

Kujitoharisha kwa ndani, ni kuitwahaisha nafsi na athari za madhambi na maasi na hilo ni kwa toba iliyo ya kweli na pia ni kwa kuutakasa moyo na uchafu wa ushirikina na shaka, hasadi na mifundo na chuki za moyo, na kughushi na kujivuna na kujiona na kuwaonyesha watu matendo na kupenda kusifika. Na kujitoharisha huku kwa ndani pia kunapatikana kwa kumtakasia Mwenyezi Mungu matendo na kwa kuwa na yakini, kupenda kheri, upole, ukweli, na unyenyekevu, na kufanya matendo yote kwa lengo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na kujitoharisha kwa nje ni kutoharika na hadathi. Kutoharika na najisi kwa kuondoa najisi kwa maji yaliyo tohara yenye kutoharisha. Katika nguo ya mwenye kuswali na mwili wake, na mahali pa kuswali. Kutoharika na hadathi kunapatikana kwa kutawadha, kuoga na kutayammam.

Somo la Pili:

Kinachotumika katika kujitoharisha

Tohara Inapatikana Kwa Vitu Viwili:

1. **Maji yaliyo safi.** Nayo ni yale ambayo yapo katika hali yake ya asili ambayo hakikuchanganyika nayo kitu chochote ambacho kinapambanuka nayo, kikiwa ni najisi kitu hicho au ni tohara. Maji safi ni kama maji ya visima, na chemchem, mito, na barafu iliyoyayuka na bahari ya chumvi, kutoka na msemo wa Allah.

وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً طَهُورًا ﴿٤٨﴾

“...na tunayateremsha kutoka mbinguni maji safi...”(al – Furqan 25: 48)

Na msemo wa Mtume ﷺ,

“Maji ni yenye kutoharisha isipokua itakapo badilika harufu yake au ladha yake au rangi yake kwa sababu ya najisi iliyozuka ndani yake.” (Al-Bayhaqi, Muslim Abu Dawuud).

2. **Mchanga ulio tohara.** Unapatikana katika uso wa ardhi iliyo tohara miongoni mwa mchanga, au changarawe au mawe au ardhi yenye chumvi kutokana na msemu wa Mtume ﷺ.

“Imefanywa kwangu ardhi kuwa ni msikiti na ni kitu cha kujitoharishia.” (Imamu Ahmad na asili yake Imo katika Sahihi Al-Bukhari na Muslim).

Mchanga unatumika kwa kutoharisha wakati maji yanapokosekana au wakati wa kushindwa kuyatumia maji kwa sababu ya ugonjwa na mfano wake kutokana na maneno ya Allah (s.w):

فَلَمْ يَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا

“Mkayakosa maji, ukusudieni mchanga uliyo tohara.” (An-Nisaa 4: 43)

Na msemu wa Mtume ﷺ.

“Hakika mchanga ulio tohara ni kitu cha kujitoharishia kwa Muislamu hata kama hatayapata maji miaka kumi lakini atakapopata maji na ayagusishe na ngozi yake (Na ayatumie).” (At-Tirmidhi na Imam Ahmad).

Na kwa sababu Mtume ﷺ alikubali ‘Amr bin Al-‘As kutayammam (kuutumia mchanga katika kujitoharisha) kutokana na janaba katika usiku wenye baridi kali wakati alipoogopa kupata madhara iwapo angeoga maji yaliyo baridi.

Somo la Tatu:

Ufafanuzi wa Najisi

Neno *Najasat* ni uwingi wa Najisi nayo ni kitu kutoka katika tupu mbili za mwanadamu, kama vile kinyesi, mkojo, au *madhii, wadii, na manii* (*Manii* yenyewe sio *Najisi* lakini baadhi ya Wanazuoni wanasema kuwa inapendekezwa kujisafisha na kusafisha sehemu iliyoingia *manii*).

Miongoni mwa najisi ni mkojo, kinyesi na matapishi ya kila mnyama ambaye si halali kula nyama yake. Na kuwa katika hali ya kuchuruzika damu, usaha au matapishi yaliyobadilika na viungo vya mnyama vilivyokatwa kutoka katika mnyama aliye hai isipokua ngozi zitapodibaghiwa rangi, hizo zinatoharika kutokana na maneno ya Mtume ﷺ:

“Ngozi yoyote iliyotiwa rangi imetwahaarika.” (At-Tirmidhi na An-Nasai).



Mada ya Pili

Adabu za Kukidhi Haja

Somo la Kwanza:

Mambo Ya kuzingatia Kabla Ya Kwenda Haja:

1. Tafuta mahali pasipokuwa na watu hali ya kuwa mbali na macho yao kutokana na lile ambalo limepokewa kwamba Mtume ﷺ,

‘Ilikuwa anapotaka kukidhi haja huenda mbali kiasi cha kutomuona mtu yoyote.’ (Abu Dawuud).

2. Usiingie chooni na hali una pamoja nawe kitu ambacho ndani yake mna utajo wa Allah (s.w), kutokana na yaliyopokewa kwamba Mtume ﷺ,

“Alikua akivaa pete Muhammadan Rasulullah-Muhammad ni Mjumbe wa Allah – na alikuwa akiivua anapotaka kuingia chooni.” (Abu Dawuud).

3. Tanguliza mguu wako wa kushoto wakati wa kuingia chooni na useme,

بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْخُبْثِ وَالْخَبَائِثِ.

Bismillahi Allahumma Inni ‘Audhubika Minnal Khubthi wal-Khabaith

“Kwa jina la Allah, EE Mola wangu wa haki, hakika mimi ninakuomba unilinde na mashetani wanaume na mashetani wanawake.”

Kutokana na ushahidi kutoka kwa Al-Bukhari kwamba Mtume ﷺ alikuwa akisema maneno hayo anapoingia chooni.

4. Usiinyanyue nguo zako mpaka ukaribie katika ardhi kwa ajili ya kuusitiri uchi wako ambao umeamrisha kuusitiri kisheria.

5. Usielekee kibla wakati wa kukidhi haja kubwa au ukiwa katika hali ya kukipa mgongo *kibla* kutokana na maneno ya Mtume ﷺ:

“Msikielekee kibla na wala msikipe mgongo wakati wa kukidhi haja kubwa au haja ndogo.” (An-Nasai na Ad-Daraqutni).

6. Usikae katika kivuli cha watu au njia wakati wa kukidhi haja au karibu na maji yao au miti yao yenye kuzaa matunda, kutokana na msembo wa Mtume ﷺ,

“Jikingeni na laana tatu: kukidhi haja katika mapito ya maji na katikati ya njia, na katika kivuli.” (Al-Hakimu, na Abu Dawuud).

Mafundisho ya Mtume ﷺ hukataza kukidhi haja chini ya miti yenye kuzaa matunda .

7. Usizungumze wakati wa kukidhi haja kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Watakapokuwa wakikidhi haja kubwa watu wawili na ajifiche kila mmoja katika wao na mwenzake wasizungumze, kwani Allah analichukia hilo.” (Lisan al-Mizan).

Somo la Pili:

Mambo Yanayotakiwa wakati wa Kustanji Maji au Mawe?

1. Usistanji kwa kutumia mfupa au kinyesi kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Msistanji kwa kutumia kinyesi wala mifupa kwani hicho ni chakula cha ndugu zenu katika majini.” (At-Tirmidhi).

Wala usistanji kwa kutumia kitu ambacho ndani yake mna manufaa kama vile katani (mkonge) ambao unafaa kwa matumizi, na mfano wake, wala kwa kile ambacho kinaheshimiwa, kama vile chakula, kwani kuyakosha manufaa na kuyaharibu maslahi ni haramu.

a) Usijifute au kustanji kwa mkono wako wa kuume au kuishika dhakari kwa matumbo ya vidole vyako, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Asiishike mmoja wenu dhakari yake kwa mkono wake wa kuume akiwa anakojoa au anapojifuta kwa mkono wake.” (Imam Ahmad na Darimi).

b) Utumiaji wa mawe ufanywe kwa witra, kama vile kwanza kutumia mawe matatu, kama haukupatikana usafi utatumia mawe matano kwa mfano, kutokana na kauli ya Salman,

*“Alitukataza Mjumbe wa Allah (s.w.t) kuelekea **kibla** wakati wa kukidhi haja kubwa au haja ndogo, au kustanji kwa mkono wa kuume, au kustanji kwa uchache mawe matatu, au kustanji kwa kutumia kinyesi cha nyumbu na punda au kwa mfupa.” (At-Tirmidhi, Abu Dawuud na An-Nasai).*

c) Utakapokusanya maji na mawe utatambuliza mawe kwanza kisha utastanji kwa maji, na ukitosheka na kimoja inatosha, isipokuwa maji ni bora zaidi, kutokana na kauli ya Aisha رضى الله عنها.

“Waamrisheni waume zenu wastanji kwa maji, hakika mimi ninawaonea haya, kwani hakika Mjumbe wa Allah alikuwa akilifanya hilo.” (At-Tirmidhi).

Somo la Tatu:

Mambo Yanayotakiwa baada ya kukidhi Haja

1. Tanguliza mguu wako wa kiume wakati wa kutoka chooni kwa sababu Mtume ﷺ amefanya hilo.
2. Wakati wa kutoka chooni unatakiwa kusema,

Minhajil Muslim

Ghufraanak غفرانك “*Naomba msamaha wako.*” (At-Tirmidhi na Ahmad) au

الحمد لله الذي أذهب عني الأذى وعافاني

Alhamdulillah Alladhi Adh-haba ‘Annil Adha Wa-’Afani
“*Sifa njema ni za Allah ambaye ameniondolea uchafu na ameniondolea matatizo.*” au

الحمد لله الذي أحسن إليّ في أوله وآخره

Alhamdulillah Alladhi Ahsana Ilayya fiy Awwalihi Wa-Aakhiri
“*Sifa njema ni za Allah ambaye amenifanyia wema mwanzo wake na mwisho wake.*” au

الحمد لله أذاقني لذته وأبقي في قوّته، وأذهب عني أذاه

Alhamdulillah Adhaaqaniy Ladhatihi Wa-Abqa Fiyya Quwatihi,
Wa-Adh-haba ‘Anni Adhaahu

“*Sifa njema ni za Allah (s.w) ambaye amenionjesha ladha zake na akazibakisha kwangu nguvu zake, na ameniondolea uchafu wake.*”



Mada ya Tatu

Udhu

Somo la Kwanza:

Sheria ya kutawadha na Ubora Wake

1) Amri ya kutawadha:

Kutawadha kumefanywa ni sheria katika *Qur-aan* na *Sunna*, Amesema *Allah*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى
الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ^٤

“Enyi mlio amini! Mnapo simama kwa ajili ya Swala basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni.” (al Maidaah 5: 6)

Na amesema Mjumbe wa Allah (s.w.t),

“Haikubaliwi swala ya mmoja wenu bila ya kuwa na udhu mpaka atawadhe.” (Al-Bukhari).

2) Ubora wa Udhu:

Dalili ya ubora wa udhu ni kauli ya Mtume ﷺ, pale aliposema

“Hivi niwajuze juu ya kile ambacho anafuta kwacho Allah makosa na ananyanyua kwacho daraja? Wakasema masahaba. Kwa nini ewe Mjumbe wa Allah, tufahamishe” akasema *“ni kujipatia udhu bila ya kujali udhia (mfano ubaridi, hali ya hewa, kuumwa) na wingi wa hatua kwenda msikitini na kuingoja Swala baada ya Swala iliyotangulia, huo ndio ulindaji.”* [Muslim]

Na kauli yake nyingine,

“Mja Muislamu atakapotawadha akauosha uso wake, hutoka, pamoja na maji au pamoja na tone la mwisho la maji makosa yote ambayo aliyaangalia kwa macho yake. Na akikosha mikono yake huondoka dhambi zote ambazo amefanya kwa mikono yake, mwisho wake anatoka akiwa amesafika na madhambi.”
[Muslim].

Somo la Pili:

Nguzo za Udhu, Sunna Zake na Makruhu Yake

a) Nguzo Zake:

1. Kunuia, nako ni kuazimia moyoni nia ya kutawadha kwa ajili ya kutekeleza amri ya *Allah* (s.w), kutokana na msembo wa Mtume ﷺ,

“Kwa hakika hapana jambo jingine isipokua matendo yote huzingatiwa kwa nia.” (Al-Bukhari).

2. Kuosha uso, kuanzia juu ya paji la uso mpaka mwisho wa kidevu na kutokea kigingi cha sikio mpaka kigingi cha sikio jingine, kutokana na tamko la *Allah* (s.w): *“Basi osheni nyuso zenu.”*

3. Kuosha mikono miwili mpaka kwenye kongo mbili (fundo mbili) kutokana na tamko la *Allah* (s.w): *“Na mikono yenu mpaka vifundoni.”*

4. Kupaka kichwa kutoka katika paji la uso mpaka kichogoni, kutokana na tamko la *Allah* (s.w): *“Na pakeni vichwa vyenu.”*

5. Kuiosha miguu miwili mpaka kwenye fundo mbili, kutokana na tamko la *Allah* (s.w): *“Osheni miguu yenu mpaka vifundoni..”*

6. Kufuatanisha viungo vyenye kuoshwa, kwa kuosha uso kwanza kisha mikono miwili kisha utapaka kichwa kisha utaiosha miguu miwili, kwa sababu kuosha

viungo hivyo ni katika amri ya Allah hivyo uso kwanza kisha mikono miwili mpaka mwisho.

7. Ni kufululiza nako ni kutawadha katika wakati mmoja, mfululizo bila ya kukatisha kwa sababu kuikatisha ibada baada ya kuianza kumekatazwa, Anasema *Allah* Mtukufu,

وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ

“...wala msiviharibu vitendo vyenu...” (Muhammad 47: 33)

Isipokuwa kipambanuzi kidogo kinaruhusiwa, na vile vile kile ambacho kimepatikana kutokana na udhuru kama kwisha maji au kukatika au kumwagika kwa ajili hiyo, kurefusha muda kunaruhusiwa kwa sababu *Allah* haikalifishi nafsi yoyote isipokua kadri ya uwezo wake.

Ufafanuzi

Baadhi ya wanazuoni wanahesabu kusugua kuwa ni katika nguzo za kutawadha na baadhi yao wanahesabu kuwa ni katika sunna zake. Uhakika ni kwamba kusugua ni katika ukamilifu wa kuosha kiungo, na hakuja pokelewa jina au hukumu maalum.

b) Sunna za kutawadha

1. **Kusoma Bismillahi**, kwa kusema: بِسْمِ اللَّهِ, ‘Ninaanza kutawadha kwa jina la Mwenyezi Mungu’, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Hapana udhu kwa yule ambae hakulitaja jina la Mwenyezi Mungu juu yake.” [Ahmad na Abu Dawuud].

2. **Kuviosha viganja viwili kwa maji** mara tatu kabla ya kuviingiza ndani ya chombo mtu anapotoka usingizini, kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakapoamka mmoja wenu kutoka katika usingizi wake asiuzamishe mkono wake katika chombo mpaka auoshe mara tatu, kwani yeye haelewi wapi mkono wake umepitiwa na usiku.” [Muslim na Imam Ahmad].

Na ikiwa hajaamka kutoka usingizini hakuna kizuizi cha kuutia mkono wako katika chombo, na kuyanyanyua kwa huo mkono wako maji na kuviosha viganja vyako mara tatu, kama sunna ya udhu.

3. **Kupiga mswaki**, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Laiti kama sikuona kuwa nitawatia katika taabu umma wangu ningewaamrisha kupiga mswaki wakati wa kila udhu.” [Imam Maliki]

4. **Kusukutua**, nako ni kuyatikisa maji mdomoni kutoka shavu mpaka shavu jingine, kisha kuyatema kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Wakati wa kutawadha sukutua.” [Abu Dawuud]

5. **Kupandisha maji puani** “*Isitishaq*” ni kuyavuta maji kwa pua na “*Istinthar*” ni kuyatoa kwa kutumia pumzi. kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Na ataendeleza katika kuyapandisha maji puani isipokua kama amefunga.” (Abu Dawuud, At-Tirmidhi na An-Nasai).

6. **Kuzichanua ndevu**, kwa kupitisha vidole kutokana na maneno ya Ammar Ibn Yasir, watu waliposhangazwa na kitendo chake cha kuchanua ndevu zake wakati wa kutawadha,

“Ni jambo gani litakalonizua na hali kwa hakika nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anazichanua ndevu zake.” (Ahmad).

7. **Kuosha mara tatu tatu**, kwa sababu *faradhi* ni kuosha mara moja, na kuosha mara tatu ni *sunna*.

8. **Kupaka masikio mawili** mdomoni na nje kwa sababu Mtume ﷺ amelifanya hilo.

9. **Kuvichanua vidole** katika mikono miwili na miguu miwili, kauli ya Mtume ﷺ,

“Wakati ukitawadha vichanue vidole vya mikono yako na miguu yako.”

10. **Tayamun**, nayo ni kuanza upande wa kuume katika kuosha mikono miwili na miguu miwili, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ.

“Wakati mkitawadha anzeni na upande wa kuume.” [Ahmad].

Na kauli ya Bi Aisha رضي الله عنها.

“Alikuwa akipenda Mtume ﷺ kuanza upande wake wa kuume wakati akivaa viatu vyake, na kujitana kwake na katika kujitoharisha kwake, na kutenda mambo yake yote.” (Al-Bukhari na Muslim).

11. **Kurefusha** paji lako la uso katika kuosha na kurefusha mikono na miguu katika kuosha, na wakati wa kutawadha hilo ni kwa kufikia kuuosha kwenye sehemu ya shingo na katika mikono kuosha mpaka karibu na kwapa na katika miguu kuosha mpaka karibu na magoti, kutokana na msemo wa Mtume ﷺ.

“Hakika umma wangu watakuja siku ya kiyama wakiwa weupe wa nyuso na weupe wa mikono na miguu kutokana na athari za udhu, Mwenye kuweza kurefusha katika nyinyi eneo la uso wake na afanye.” [Imam Ahmad].

12. **Anza kwa** kukipaka kichwa chako **sehemu ya mbele**, kutokana na maelezo kwamba Mtume ﷺ.

“Alipaka kichwa chake kwa mikono yake akaipeleka mbele, na akairudisha nyuma alianza na sehemu ya mbele ya kichwa chake, kisha akaipeleka kichogoni kwake halafu akairudisha.” [At-Tirmidhi].

13. Baada ya kutawadha useme,

أشهد أن لا إله إلا الله، وحده لا شريك له، وأشهد أن محمدا عبده
ورسوله اللهم اجعلني من التوابين واجعلني من المتطهرين.

Ash-hadu An La Ilaha Illa Llwah, wahdahu laa sharika lahu, wa-
ash-hadu ana Muhammadan ‘Abduhu warasuuluhu, Allahumma
Ij’alni mina Tawwabiin waj’alni minal mutatawahiin.

“Nakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba, hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa hana mshirika. Na ninakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kuwa Muhammad ni Mja Wake na Mjumbe Wake, ewe Mola wa haki nifanye mimi niwe miogoni mwa wenye kutubia, na nifanye mimi niwe katika wenye kujitakasa”

Kutokana na kauli yake Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake:

“Nakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu-mpaka mwisho wake – Itafunuliwa kwako milango yote minane ya peponi utaingia katika mlango wowote utakao.” (An-Nasai na Imam Ahmad)

c) Makruhu Yake:

1. **Ni kutawadha mahali palipo na najsi** kwa kuogopa kurukiwa na najisi hiyo wakati wa kutawadha.

2. **Kuongeza kuosha zaidi ya mara tatu**, kutokana na maelezo kwamba Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake alitawadha mara tatu tatu na akasema,

“Atakayeongeza hakika atakuwa amefanya uovu na amefanya dhulma.” [Ibn-Khuzayma).

3. **Kuvuka mipaka katika kuyatumia maji**, kwani alitawadha mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa kibaba. Na kuvuka mipaka katika kila kitu kumekatazwa. (Al-Haythami)

4. **Kuacha sunna moja au sunna** nyingi katika sunna za udhu, kwani kwa kuacha sunna mtu hujikosesha malipo ambayo hakutakiwa kuyakosa.

5. **Kutawadha maji yaliyobakizwa**, na mwanamke kutokana na taarifa isemayo:

“Alikataza mjumbe wa Mwenyezi Mungu kutawadha mabaki ya maji ya kujitoharisha mwanamke.” [At-Tirmidhi na Abu Dawuud]

Somo la Tatu :

Katika Namna ya Kutawadha Nayo.

1. Kama inawezekana chombo cha maji kiwekwe kuumeni kwa mtu anayetawadha na kuanza na dua بِسْمِ اللّٰهِ, 'Naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu', na kumimina maji juu ya viganja vyake viwili, huku ukinuia kutawadha utaviosha mara tatu, kisha utasukutua mara tatu, kisha utapandisha maji puani na atayakunguta mara tatu. Kisha utauosha uso wako tokea maoteo ya nywele za kichwa chako, mpaka ukomo wa taya lako kwa urefu na kutokea kigingi cha sikio mpaka kigingi cha sikio jingine kwa upana, utauosha mara tatu. Kisha utaosha mkono wako wa kuume mpaka kwenye kiwiko mara tatu hali ya kuvichanua vidole vyako, kisha utaosha mkono wa kushoto kwa utaratibu huo. Kisha utakipaka kichwa chako mpaka mmoja, utanza sehemu ya mbele ya kichwa chake, na utaipeleka mikono yako hali ya kupaka mpaka kichogoni kwako, kisha utairudisha kule ulikoanzia kisha utapaka masikio yako nje na ndani kwa maji maji yaliyobaki mikononi mwako, au utachukua maji mapya kwa ajili ya kupaka masikio, iwapo hapatakuwa pamebaki maji maji mikononi mwako, kisha utauosha unyayo wako wa kuume mpaka kwenye nguyu mbili, kisha utauosha wa kushoto kwa utaratibu huo, kisha utaomba dua kwa kusema:

"Nakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa peke yake hana mshirika na ninakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba Muhammad ni mja wake na mjumbe wake. Ewe Mola wa haki nifanye mimi niwe miongoni mwa wenye kutubia na nifanye mimi niwe katika wenye kujitakasa."

Hayo yanatokana na yaliyopokelewa kuwa 'Ali رضي الله عنه alitawadha, akaosha viganja vyake viwili, mpaka akavisafisha kisha akasukutuwa mara tatu, na akapandisha maji puani mara tatu, na akauosha uso wake mara tatu na mikono yake mara tatu, na akapaka kichwa chake mara moja, kisha akaosha miguu yake mpaka kwenye nguyu mbili, kisha akasema,

"Nimependa kuwaonyesha jinsi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyotawadha." [At-Tirmidhi].

Somo la Nne:

Mambo Yanayobatilisha Udhu

1. **Kitokacho katika njia mbili** ikiwa ni mkojo, *madhii*, au *madii*, kinyesi au ushuzi usiyo na sauti na wenye sauti. Hali hiyo huitwa hadathi na hili ndilo lililokusudiwa na kauli ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

“Haikubaliwi swala ya mmoja wenu akipatwa na hadathi mpaka atawadhe.” [Al-Bukhari].

2. **Usingizi mzito** akiwa mwenye usingizi huo ni mwenye kujitandawaza kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Jicho ni kamba ya kusahau, atakaelala na atawadhe.” [Ibn Majah na Ad-Daraqutni].

3. **Kupoteza** na kukosa utambuzi kwa kughumiwa au kulewa au kupatwa na uwendawazimu. Kwa sababu katika hali ya kupoteza akili, mtu hawezi kuelewa kama udhu wake umebatilika au haukubatilika kwa mfano kujamba.

4. **Kushika dhakari** kwa matumbo ya vidole, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Mwenye kushika dhakari yake na atawadhe.” [At-Tirmidhi].

5. **Kuritadi (kutoka katika Uislamu)** kwa kutamka tamko la ukafiri na kukana kwani hakika udhu wa mtu hubatilika pamoja na matendo yake yote ya kiibada kutokana na tamko la Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكَ لَإِنْ أَشْرَكَتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ

وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٥﴾

“Bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu a’ mali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri.” (Az-Zumar 39: 65)

6. **Kula nyama ya ngamia** kutokana na swali la mmoja wa masahaba kwa Mtume ﷺ,

“Je, tutawadhe tukila nyama za mbuzi”. Akajibiwa, “Ukitaka”. Akauliza, “Je, tutawadhe tukila nyama za ngamia?”. Akajibiwa, “Ndio”. [Imam Ahmad].

Maelezo yaliyopo ni kwamba kundi kubwa la masahaba hawaoni haja kutawadha kwa kula nyama za ngamia kwa hoja ya kuwa Hadithi hii imefutwa, na kwa kuwa watu wengi wakiwemo makhalifa hawakuwa wakitawadha baada ya kula nyama ya ngamia.

7. **Kumgusa na kumshika mwanamke kwa matamano** Kunabatilisha udhu, kwa dalili ya kuamrisha kutawadha baada ya kuishika dhakari kwa sababu kuishika dhakari kunaamsha matamano, na kutokana na maneno yaliyo katika kitabu Muwatta kutoka kwa Ibni ‘Umar,

“Mwanamume kumbusu mkewe na kumkanda kwa mikono wake ni katika kushika. Atakayembusu mkewe au atakaye mkanda kwa mikono yake ni juu yake kutawadha.”

Mambo yanayosababisha Sunna ya Kutawadha

Moja ya mambo haya yanapotokea huwa ni suna kutawadha:

1. Kutokwa na mkojo kwa sababu ya maradhi kwa yule ambaye haukatiki katika sehemu kubwa ya wakati wake, au ushuzi wake, ni sunna kwake kutawadha kabla ya Swala kwa kufuata hukumu ya *mustahadha* (mwenye damu ya ugonjwa).

2. **Mustahadha:** Ni yule ambaye inapita juu yake damu muda wote katika zisizokuwa siku za ada yake. Ni suna kwake kutawadha kabla ya kila Swala kama yule mwenye ugonjwa wa kutokwa na mkojo kutokana na kauli yake Mtume Rehman na Amani ziwe juu yake kumwambia Fatima bint Abu Hubeish:

“Kisha tawadha kwa kila Swala.” [Abu Dawuud].

3. Baada ya kumwosha na kumbeba maiti kutokana na kauli ya Mtume ﷺ.

“Mwenye kumuosha maiti na aoge na mwenye kumbeba na atawadhe.”

Kwa vile inasemwa hadithi hii ni dhaifu wanazuoni wamependekeza watu watawadhe kama jambo la tahadhari.



Mada ya Nne
Kuoga Janaba
Somo la Kwanza:

Sheria ya Kuoga na yanayowajibisha Kuoga.

a) Amri ya kuoga:

Kuoga: Kumefanywa kuwa ni sheria kwa kufuata *Qur-aan* na *Sunna*, Amesema Mwenyeezi Mungu (s.w):

وَإِنْ كُنْتُمْ جُنُبًا

“*Na mkiwa na janaba basi ogeni.*” (Al-Maidah 5: 6)

Na Amesema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا
تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا

“*Msikaribie Sala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema, wala hali mna janaba.*” (An-Nisaa 4: 43).

Na amesema Mtume ﷺ,

“*Dhakari itakapovuka sehemu ya kukhitaniwa hakika limepasa joshu.*” [Muslim].

b) Mambo yenye kuwajibisha Kuoga

1. **Janaba** kuwa na janaba kwa kuingiza dhakari katika utupu wa mwanamke hata kama itakua bila ya kushusha *manii*. Kushusha manii nako ni kutoka *manii*

kwenye kuambatana na kitendo cha jimai, tamko la Mwenyezi Mungu (s.w): *وان كنتم جنباً فاطهروا*, “*Na mkiwa na janaba basi jitoharisheni*”.

Na kauli ya Mtume ﷺ:

(إذا التقى الختانان فقد وجب الغسل), “*Zikikutana sehemu mbili za kukhitaniwa, hakika limepasa jasho.*” (Al-Bukhari na Imam Ahmad)

2. **Kukatika kwa damu ya hedhi au ya nifasi** kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w):

فَاعْتَرِلُوا النِّسَاءَ فِي الْمَحِيضِ وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهَرْنَ فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ

“*Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi. Wala msiwaingilie mpaka wat’ahirike. Wakisha t’ahirika basi waendeeni alivyo kuamrisheni Mwenyezi Mungu...*” (al Baqara 2: 222)

Na kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“*Kaa kiasi cha ule muda ambao ilikuwa inakuzuia hedhi yako kisha oga.*” [Muslim].

3. **Kuingia katika Uislam** kafiri anaposilimu na kuwa muislam anapaswa kuoga, kwasababu Mtume ﷺ aliamrisha Thumama Al-Hanafi aoge wakati aliposilimu. [Al-Bukhari na Muslim].

4. **Kufa**, Muislam anapofariki ni wajibu kumuosha kwa sababu ya amri yake Mtume ﷺ, kwani aliamrisha kuoshwa kwa bint yake Zainab wakati alipofariki.

Matokeo yanayosuniwa

Ni sunna Kuoga Kwa Haya Mambo Yafuatayo:

1. **Ijumaa:** Kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Josho la Ijumaa ni wajibu kwa kila mwenye kubaleghe.” [Abu Dawuud, Imam Ahmad na Ibn Majah An-Nasai].

2. Kwa ajili ya **kuhirimia Hijja**, Ni sunna kwa mwenye kutaka kuhirimia umra au Hijja kuoga kama alivyofanya Mtume ﷺ na kuamrisha kwake jambo hilo lifanywe.

3. Kwa ajili ya **kuingia Makkah** na kusimama Arafa kama alivyofanya Mtume ﷺ.

4. **Baada ya kumwosha maiti**, ni sunna kwa, mwenye kumuosha maiti kuoga kwa hadathi iliyotangulia.

Somo la Pili

Nguzo za Kuoga, Sunna Zake na Makruhu Yake.

a) Nguzo Zake

1. **Kunuia** nako ni kuazimia moyo kuwa unaondosha *hadathi* kubwa kwa kuoga kutokana na kauli yake Mtume ﷺ.

“Hakika hapana jambo jingine, matendo yote huzingatiwa kwa nia, na hakika hapana jambo jingine kila mtu atalipwa kutokana na alivyonuia.” [Al-Bukhari].

2. **Kueneza** mwili wote kwa maji pamoja na kuzisugua sehemu ambazo inawezekana kuzisugua na kumimina maji juu ya sehemu ambazo kunashindikana kuzisugua mpaka maji yawe yamekuenea mwili mzima.

3. Kuvichanua vidole na nywele-nywele za kichwa na nyingine—na kuzingatia zile sehemu ambazo hazipati maji kwa urahisi kama vile kitovu na mfano wake.

b) Sunna Zake

1) Ni kusema *Bismillahi*, kwani kusema *Bismillahi* kumefanywa kuwa ni sheria katika kila tendo la hiari. 2) **Kuviosha** viganja viwili kwanza kabla ya kuviingiza katika chombo kutokana na maelezo yaliyotangulia. 3) **Kuanza** na kuondosha uchafu. 4) **Kuvitanguliza** viungo vya udhu kabla ya kuosha mwili. 5) **Kusukutuwa** na kupandisha maji puani na kuosha ndani ya tundu za masikio mawili.

c) Makruhu Yake.

1. **Kuvuka** mipaka katika kutumia maji kwa sababu alioga Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa pishi moja nayo ni vibaba vinne.

2. **Kuogea** mahali palipo na najisi kwa kuogopa kurukiwa na najisi

3. **Kuoga** kwa maji yaliyobaki baada ya mwanamke kujitoharisha kutokana na Mtume ﷺ kujitoharisha na kukataza kuoga maji yaliyobaki baada mwanamke.

4. **Kuoga** bila ya kuwepo na sitara kama vile ukuta au mfano wake, kutokana na maneno ya Maymuna رضى الله عنها ،

“*Nilimwekea Mtume ﷺ maji na nikamsitiri akaoga.*” [Al-Bukhari].

Lau kusingekuwa kuoga bila ya sitara ni makruhu asingemsitiri Rehema na Amani ziwe juu yake, Na kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“*Hakika Mwenyezi Mungu (s.w) Aliye Mtukufu ni Mwenye haya, mwingi wa kusitiri, anapenda walio na haya akienda kuoga mmoja wenu na ajisitiri.*” [An-Nasai].

5. **Kuoga** katika maji yaliyotulizana ambayo hayatiririki, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Asioge kabisa mmoja wenu katika maji yaliyotulizana wakati akiwakuwa ana janaba.” (Muslim).

Somo la Tatu:

Jinsi ya Kuoga

Jinsi ya Kuoga ni Hii:

1. **Unaanza kwa kusoma:** بِسْمِ اللَّهِ na kulitaja jina la **Allah** huku ukinuia kuondosha *hadathi* kubwa kwa kule kuoga. Kisha utaosha viganja vyako mara tatu kisha utastanji utaosha vilivyo katika tupu zako, na sehemu zilizo pambizoni mwako miongoni mwa uchafu. Kisha utatawadha, ikiwa ni tohara ndogo, ila miguu yako kwani wewe una ruhusa ya kuiosha pamoja na udhu wake, na una ruhusa ya kuichelewesha mpaka ukimaliza kuoga kwako. Kisha utavizamisha viganja vyako ndani ya maji, utachana kwavyo mashina ya nywele za kichwa chako. Inatosha kupaka kichwa chako mara tatu na kusugua wala hufungui nywele zako zilizofungwa kama ni mwanamke, kama vile alivyopokea At-Tirmidhi kutoka kwa Ummu Salama alipomuuliza ﷺ “kuwa mimi nafunga nywele zangu je nizifungue nikioga janaba? “Mtume ﷺ akajibu, hapana lakini inatosha kwako kupaka na kusugua”. Kisha utaosha kichwa chako pamoja na masikio yako mara tatu, kwa machoto matatu, kisha utamimina maji juu ya upande wako wa kulia, utauosha kwa maji hayo kutoka juu yako mpaka chini yako. Kisha upande wa kushoto, utafanya kama hivyo hali ya kufuatilia wakati wa kuoga sehemu zilizojificha, kama vile kitovu, na chini ya kwapa mbili na magoti mawili, kutokana na maelezo ya Aisha رضي الله عنها:

“Alikuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipokuwa anataka kuoga janaba alikuwa anaanza kuosha mikono yake na anatawadha kama anavyotawadha kwa ajili ya Swala kisha huzinyweshwa nywele zake maji kisha kukinyunyiza kichwa chake minyunyizo mitatu, kisha humimina maji juu ya mwili wake wote.” [At-Tirmidhi na Abu Dawud].

Somo la Nne

Mambo Yanayokatwa kwa Mtu Mwenye Janaba

Yanazuiwa Kwa Sababu ya Janaba Mambo Mengi Nayo ni Haya:

1. **Kuisoma Qur-aan**, Kwa sababu ya kutaka hifadhi na mfano wake, kutokana na kauli yake ﷺ,

“Hasomi mwenye hedhi wala mwenye janaba kitu katika Qur-aan.” [At-Tirmidhi].

Na msemo wa ‘Ali رضي الله عنه

“Alikuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akitusomesha Qur-aan katika hali zote tusipokuwa na janaba.” [An-Nasai].

2. **Kuingia misikitini**, isipokuwa kuipitia kwa mwenye dharura kunaruhusiwa, kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu:

لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا

“...Msikaribie Sala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema, wala hali mna janaba.” (An-Nisaa 4:43)

3. **Kuswali faradhi** kutokana na tamko la Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا

“Msikaribie Swala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema, wala hali mna janaba.” (An-Nisaa: 43)

4. **Kuushika au kuubeba msahafu** mtukufu, ijapokuwa kwa ujiti na mfano wake kutokana na tamko la Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَا يَمْسُهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ

“...Hapana akigusaye ila walio takaswa...” (Al-Waqia 56: 79)

Na kutokana na msemu wa Mtume Rehma na Amani iwe juu yake,

“Usiishike Qur-aan mpaka uwe na hali ya kuwa wewe ni msafi.”
[Ad-Daraqutni]



Mada ya Tano

Tayammam

Somo la Kwanza

Sheria na mwenye kuhusika

a) Amri yake:

Kutayammam kumefanywa kuwa ni sheria kwa kauli ya *Qur-aan* tukufu, na *sunna* zilizo bora. Anasema Allah Mtukufu:

يَتَأْتِيَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا
تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغْتَسِلُوا وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ أَوْ
عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا
مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ

“Enyi mlio amini! Msikaribie Swala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema, wala hali mna janaba - isipo kuwa mmo safarini - mpaka mkoge. Na mkiwa wagonjwa, au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewagusa wanawake - na msipate maji, basi ukusudieni mchanga safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu...” (An-Nisai 4:43)

Na amesema Mtume ﷺ,

“Mchanga waweza kutumika kama udhu wa muislamu hatakama atayakosa maji miaka kumi.” [An-Nasai na Ibn Hibban]

b) Nini *Kutayamam* Kisheria?

Sheria na hukumu hii inamuhusu yule ambaye ameyakosa maji baada ya kuyatafuta katika maeneo yanayomzunguka, au aliyepata maji na asiweze kuyatumia kwa sababu ya ugonjwa. Ama kwa yule ambaye ameyapata maji machache ambayo hayamtoshi kupatia udhu, huyo atatawadha kwa maji hayo katika baadhi ya viungo vyake, kisha ata *tayammam* kukamilisha sehemu iliyobaki kutokana na tamko lake Mwenyezi Mungu Mtukufu,

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ

“*Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo...*” (At-Taghabun 64: 16)

Somo la Pili

Nguzo za *Kutayamamu* na Sunna Zake

a) Nguzo Zake

Nguzo za *Kutayamam* ni Hizi:

1. **Kunuia**, kutokana na *hadathi*, “*Hakika hapana jambo lolote, matendo yote huzingatiwa kwa nia, na hakika hapana jambo jingine isipokua kila mtu atalipwa kutokana na vile alivyounuia.*”

Atanua mwenye *kutayamam* katika uhalali wa kile kilichozuiwa miongoni mwa Swala na mfano wake. Hivyo basi atanua *kutayamam* kwa kutaka kukifanya hicho alichokinua.

2. **Mchanga** uliotohara, kutokana na tamko lake Allah (s.w). “*Ukusudieni mchanga ulio tohara.*”

3. **Pigo la kwanza**, nalo ni kuweka mikono miwili juu ya mchanga kwa taratibu

4. Kupaka uso na viganja viwili, kutokana na tamko la Allah (s.w). “*Pakeni nyuso zenu na mikono yenu.*”

b) Sunna Zake.

1. al-Tasmiya: Nako ni kusema بِسْمِ اللّٰهِ, ‘*Bismillahi*’, “Naanza kwa Jina la Allah.” Kwa sababu kusoma *Bismillahi*, kunatakikana kisheria katika kila tendo la heri.

2. Pigo la Pili, pigo la kwanza ni *faradhi*, na linatosheleza, pigo la pili ni *sunna*.

3. Kupaka dhiraa mbili pamoja na viganja viwili. Kwa, hakika hapana jambo jingine isipokuwa unapaka *dhiraa* mbili kwa tahadhari na hilo ni kwa sababu kuna tofauti za wanazuoni katika maana ya mkono katika aya. Je, hiyo mikono miwili ni viganja viwili pamoja na *dhiraa* mbili mpaka kwenye kongo mbili (viwiko vya mkono)?.

Somo la Tatu

Mambo yanayoruhusiwa na yanayobatilisha Tayamam

a) Yanayoruhurusiwa baada ya kutayamam

Kila Kilichokuwa kimezuiwa kabla ya kutayamam kama vile kuswali au kutufu, au kushika msahafu au kusoma *Qur-aan* au kukaa msikitini (Itiqaf).

a) Yanayobatilisha Tayamam

Yanabatilisha Tayamam Mambo Mawili:

1) Kila kinachobatilisha udhu kwani *tayammam* ni badala ya udhu.

2) Kupatikana maji kwa yule aliyeyakosa, kabla ya kuingia katika Swala au katikati yake, ama atakapomaliza Swala, Swala yake imeswihi, na wala hatakiwi kurejesha kwake iwapo atayapata maji, kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

Mada ya Sita

“*Msiswali Swala moja mara mbili katika siku moja.*” [Abu Dawuud na Imam Ahmad na Ad-Daraqutni]

Somo la Nne:

Jinsi ya Kutayammam

Jinsi ya Kutayammam kuanza kwa: Kusema بِسْمِ اللّٰهِ, ‘*Bismillahi*’ hali ya kuleta *tayammam* kisha utapiga kwa viganja vyote viwili usoni mwa ardhi. Ikiwa ni mchanga au changarawe au mawe au ardhi ya chumvi na mfano wake, na si vibaya kukung’uta vumbi kutoka katika viganja vyako kabla ya kupaka uso wako mpako mmoja kisha utapiga ukitaka kwa viganja vyako viwili ardhi, utapaka viganja vyako, pamoja na dhiraa zake mpaka kwenye kongo mbili ukitaka na ukitosheka na viganja viwili inatosha.

Ufafanuzi

Suali: Je, unaruhusiwa kuswali Swala zaidi ya moja, kama *tayammam* ya mtu haikubatilika

Jibu: zipo kauli mbili kuhusu Swala hili, chanzo chake ni jitihada za wanazuoni kwa vile hakuna kauli ya wazi katika masuala haya, ni kuchukua tahadhari na kutayamamu kwa kila Swala.



Mada ya Sita

Kupaka Juu ya Khofu Mbili na Bandeji

Somo la Kwanza:

Kupaka Juu ya Khofu Mbili na Bandeji:

Sheria ya kupaka juu ya *khofu* mbili na vilivyo katika maana hiyo miongoni mwa soksi mbili, na khofu nzito (Inayovaliwa juu ya *khofu* nyengine nyembamba) na *Ssakh* mbili, hivyo vimethibiti kwa mujibu wa *Qur-aan* na *sunna*. Ama *Qur-aan* kwa hakika ni tamko la Allah, **وَأَرْجُلِكُمْ**, "*Waarjulikum*" kwa *tarri* (Kwa *kasiri* ya *Lam*) kwa kuingia juu ya **وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ**, "*Wamsahu Biruusikum*", kisomo hicho kinafahamisha juu ya kujuzu kwake kupaka. Ama katika *sunna* hakika amesema Mtume ﷺ:

"Akitawadha mmoja wenu huku amevaa khofu zake mbili, na apake juu yake, na aswali na wala asizivue akitaka isipokua kutokana na janaba." [Abu Dawuud].

Na yaliyokuja katika kauli hii katika kutoa muda wa kupaka kwa kutotajwa kwa wakati maalum. Hakika kuachiwa huko kumefungwa kwa hadithi inayoelezea wakati ambayo itakuja huko mbele.

Ama sheria ya kupaka juu ya bandeji kwa hakika imethibiti kauli ya Mtume ﷺ kuhusu yule mtu ambaye kilipasuliwa kichwa chake akaiosha wakati wa udhu, akafa,

"Hakika hapana jambo jingine kulikuwa kunamtosha kutayammam na kifungwa juu ya jeraha lake kwa bandeji, kisha akapaka juu yake na akaiosha sehemu nyingine ya mwili wake." [Abu Dawuud]

Somo la Pili

Masharti ya Kupaka

Masharti ya kuzingatia katika Kupaka Juu ya Khofu Mbili na Vilivyo Katika Maana ya mambo yafuatayo:

1. Ni kuzivaa khofu mbili baada ya kuwa tohara, kwa kauli yake Mtume ﷺ, alipomuambia al-Mughira Ibn Shu'uba alipotaka kuzivua khofu za Mtume ﷺ wakati akiwa na udhu wake,

“Ziache hakika mimi nimezivaa hali ya kuwa ni tohara”. [Al-Bukhari Muslim na Imam Ahmad]

2. Ikiwa khofu mbili ni zenye kufunika mahali pa fardhi.

3. Ziwe na *maki*, zisionyeshe ugozi kwa chini yake.

4. Usizidi muda wa kupaka, mchana na usiku kwa mkazi na kwa nyusiku zao msafiri muda huo usizidi siku tatu, kutokana na maelezo ya Ali رضي الله عنه

“Alizifanya Mjumbe wa Mwenyeezi Mungu siku tatu usiku na mchana kwa msafiri, na mchana na usiku kwa mkazi”. [Muslim].

5. Zisivuliwe usiku na mchana baada ya kupaka. Khofu zikivuliwa ni wajibu kuosha miguu yake, na kama haikufanyika hivyo udhu wake utabatilika .

6. Ama kupaka juu ya bandeji kunahitaji kutanguliwa na tohara, wala haukuwekwa wakati wa muda maalumu. Hakika kunasharitiwa kwa huko kupaka lisizidi juu ya mahali pa jeraha, isipokuwa sehemu ambapo hapana budi napo ni kwa ajili ya kufungia, na kutovuliwa kutoka mahali pake na kutopona jeraha, likipona jeraha kutabatilika kupaka na kutapasa kuosha.

Ufafanuzi

1. Kunajuzu kupaka juu ya kilemba kwa dharura ya baridi au safari, kutokana na upokezi wa Muslim,

Mada ya Saba

Minhajil Muslim

“*Kwamba Mtume ﷺ alitawadha katika safari yake akapaka utosini kwake na juu ya kilemba.*” (Muslim).

Lakini pamoja na kupaka kilemba pana kupaka utosi kama ilivyo katika hadithi iliyopokelewa na Muslim.

2. Hakuna tofauti kati ya mwanamume na mwanamke katika kupaka juu ya khofu mbili na bendeji na kinachovaliwa kichwani kama vile kilemba na mfano wake. Lile linalojuzu kwa mwanamume linajuzu kwa mwanamke pia kiwango kile kile.

Somo la Tatu

Jinsi ya Kupaka

Jinsi ya kupaka juu ya khofu mbili ni kwa kulowesha viganja vyako viwili, kisha uweke sehemu ya ndani ya kiganja chako cha kushoto chini ya kisigino cha khofu, na kiganja cha mkono wa kulia juu ya ncha za vidole vyako, kisha utapitisha mkono wa kulia mpaka kwenye mundu wako na wa kushoto mpaka kwenye ncha za vidole vyako. Kupaka sehemu ya juu ya khofu bila ya kupaka chini yake kungetosha kutokana na maelezo ya Ali رضي الله عنه

“*Lau ingekuwa Dini ni kwa kutumia maoni tu, ingekuwa sehemu ya chini ya khofu ni bora zaidi kwa kupakwa kuliko juu yake.*”
[Abu Dawuud].



Mada ya Saba

Hukumu ya Hedhi na Nifasi

Somo la Kwanza

Maana Yake

a) Hedhi:

Hedhi ni damu inayotoka kutoka katika mfuko wa uzazi wakati msichana anapobaleghe. Mwanamke ina kuwa ni ada kwake katika nyakati maalum, katika maandalizi ya kumlea mtoto tumboni. Uchache wake ni mchana na usiku, na wingi wake ni siku kumi na tano, na ghalibu yake ni siku sita au saba, na uchache wa masiku ya kutoharika ni siku kumi na tatu au siku kumi na tano. Uwingi wa tohara hauna mpaka na ghalibu yake ni siku ishirini na tatu au na nne. Na wanawake katika jambo la hedhi wanagawanyika katika mafungu matatu:

1) Mwenye Kuanza; 2) Aliye mzoefu; 3) Mwenye damu ya ugonjwa.

Mwenye Kuanza

Naye ni msichana ambaye anaiona damu hiyo kwa mara ya kwanza hukumu yake ni kwamba yeye atakapoiona damu ataacha kuswali na kufunga na kuingiliwa na atangojea kutoharika. Atakapoiona baada ya mchana mmoja na usiku au zaidi ya siku kumi na tano, ataoga na ataswali, na damu ikiendelea baada ya siku kumi na tano, atahesabiwa kuwa ni mwenye damu ya ugonjwa. Baada ya hapo, hukumu yake ni hukumu ya mwanamke mwenye damu ya ugonjwa, na iwapo itakatika katikati ya siku kumi na tano na akaendelea kuona baada ya siku moja au siku mbili na ikawa inakatika na kurudi yeye ataoga na ataswali kila damu itakapokatika kutoharika na atakaa kila atakapoiona tena damu.

Kwa Mzoefu

Ni Mwanamke ambaye anatambua siku zake maalum ambazo huingia hedhi kila mwezi. Hukumu yake ni kwamba yeye ataiacha Swala na Saumu na ataacha kujihusisha na mambo ya jimai siku za ada yake. Iwapo atauona umanjano au

uvumbi vumbi, baada ya ada yake hatalishughulikia hilo kutokana na maelezo ya Ummu Atiyya رضي الله عنها

“Tulikuwa hatuhisabu umanjano au uvumbi vumbi baada ya tohara kuwa ni kitu.” [Abu Dawuud).

Ama atakapoliona hilo katikati ya ada kwa kuwa uliingia kati ya siku za ada yake umanjano au uvumbivumbi, hali hiyo inahisabiwa kuwa ni katika hedhi yake hataoga kwa ajili hiyo, wala hatawali na wala hatafunga.

Mwenye Damu ya Ugonjwa

Ni yule ambaye haikatiki kwake hali ya kutoka damu. Iwapo alikuwa kabla ya kuwa na damu ya ugonjwa, yeye atakaa siku za ada yake pasina kuswali katika kila mwezi, na baada ya kukamilika siku hizo ataoga ataswali atafunga na atajihusisha na mambo ya jimai.

Na akiwa hana ada au alikuwa na ada na akasahau idadi ya siku zake hakika yeye akipambanua damu baadhi yake na baadhi, ikawa inatoka mara nyeusi, na mara nyekundu, siku ya damu nyeusi ataoga na ataswali baada ya kwisha kwake ili mradi tu haikuvuka siku kumi na tano. Na iwapo haikupambanuka damu yake si kwa weusi wala kwa rangi nyengine, yeye atakaa katika kila mwezi ghalibu ya hedhi ambayo ni siku sita au saba kisha ataoga na ataswali.

Katika siku za kuwa katika hali hiyo, kwa mwenye damu ya ugonjwa yeye atatawadha kwa kila Swala na ataziba sehemu ile na ataswali, ijapokuwa damu inatoka hatajihusisha na mambo ya jimai labda kwa dharura. Na dalili za hayo yaliyotangulia kuelezwa katika hukumu za mwenye damu ya ugonjwa, ni hadithi zifuatazo:

1. Hadithi ya Ummu Salama,

“Ni kwamba yeye alimuuliza Mjumbe wa Allah ﷺ kuhusu mwanamke anayetokwa na damu, akasema, na atazame idadi ya siku zake usiku na mchana ambazo alikuwa anaingia katika hedhi kila mwezi, kabla hajapatwa na lile ambalo limempata,

na aache kuswali kiasi cha siku hizo katika mwezi, akimaliza muda huo na aoge na kisha aswali.” [Abu Dawuud na An-Nasai]. Katika hadithi hii, pana ushahidi wa hukumu, kwa mwenye damu ya ugonjwa aliye mzoefu.

2. Hadithi ya Fatima bint Abi Hubaishi: Ni kwamba yeye alikuwa anatokwa na damu ya ugonjwa, akamuuliza Mtume ﷺ, na Mtume ﷺ akamwambia,

“Kama ni damu ya hedhi hakika damu hiyo ni nyeusi inajulikana. Itakapokuwa hivyo jizuilie na Swala na itakapokuwa nyingine tawadha baada ya kuoga na swali hakika hapana jambo jingine huo ni mshipa.” [Abu Dawuud na An-Nasai].

3. Hadithi ya Himna bint Jahshi naye amesema,

“Nilikuwa ninatokwa na hedhi nyingi sana nikamwendea Mtume ﷺ nikamuuliza, akasema hakika hapana jambo jingine huo ni msukosuko wa shetani, ingia katika hedhi siku sita au saba kisha oga, ukisafika swali siku ishirini na nne au siku ishirini na tatu na funga na swali kwani hilo litakutosha, na kama hivyo fanya kila mwezi kama wanavyoingia katika hedhi wanawake wengine.” [At-Tirmidhi].

Na katika hadithi hii pia upo ushahidi wa hukumu kwa yule ambaye hana uzoefu wala upambanuzi.

b) Nifasi:

Nifasi ni damu inayotoka katika tupu ya mwanamkebaada ya kuzaa, wala hakuna mpaka wa uchache wake, wakati wowote atakapoona mwenye nifasi imekoma, ataoga na ataswali isipokuwa hataingiliwa kwani kitendo hicho ni makruhu kwake, kabla ya siku arubaini kwa kuchelea kupatwa na adha kwa sababu hiyo.

Ama wingi wake ni siku arubaini kutokana na yaliyopokelewa kutoka kwa Ummu Salama kwamba:

“Alikuwa mwanamke mwenye nifasi akikaa siku arubaini.” na amesema nilimuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ muda gani anakaa mwanamke baada ya kuzaa? Akasema: “Siku arubaini ila isipokuwa atakapo toharika kabla ya hapo.” [At-Tirmidhi, na al-Hakim].

Kwa maelezo haya ni kwamba mwanamke mwenye nifasi akifikisha siku arubaini, ataoga na ataswali na atafunga japo kuwa hajatoharika. Kisheria atakuwa kama mwenye damu ya ugonjwa katika hukumu sawa kwa sawa.

Na imepokewa kutoka kwa baadhi ya wanazuoni kwamba, mwanamke mwenye nifasi atakaa siku hamsini au sitini, jambo hili ni kwa sababu ya tahadhari ya dini yake.

Somo la Pili:

Upambanuzi wa Tohara

Tohara hujulikana kwa moja ya mambo mawili, la kwanza ni *Al-Qasswa Al-Baydhaa*, nayo ni maji meupe yanatoka baada ya kutoharika, na la pili ni ukavu Mwanamke atafahamu hali hiyo kwa kuingiza pamba katika tupu yake kisha akaitoa ikiwa kavu, atafanya hivyo kabla ya kulala na baada yake ili aweze kuwa na uhakika wa hali yake.

Somo la Tatu:

Yanayozuiwa kwa Sababu ya *Hedhi na Nifasi*

1. Kuingiliwa kutokana na tamko la Mwenyezi Mungu (s.w)

وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهَرْنَ

“...Wala msiwaingilie mpaka wat’ahirike...” (Al-Baqarah 2:222)

2. Kuswali na kufunga, italipwa baada ya kutoharika na swala hailipwi, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Mwanamke haswali wala hafungi anapokuwa katika siku zake za hedhi.” [Al-Bukhari].

Na msembo wa Aisha رضي الله عنها:

“Wakati tukiingia katika hedhi tukiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ tulikuwa tukiamrisha kulipa swaumu na wala hatukuamrisha kulipa swala.” [An-Nasai].

3. Kuingia msikitini kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Siuhalalishi msikiti kwa mwenye hedhi wala mwenye janaba.” [Al-Bukhari].

4. Kusoma Qur-aan, kutokana na hadithi: *“Hasomi mwenye janaba wala mwenye hedhi kitu katika Qur-aan.*

5. Kuachwa mwanamke aliye na *hedhi* haachwi bali atangojewa mpaka atoharike kabla hajaingiliwa tena hapo anaweza kuachwa kutokana na maneno yaliyopokelewa,

“Kwamba Ibnī ‘Umar رضي الله عنه Alimwacha mke wake na hali ana hedhi, Mtume ﷺ akamuamrisha amrejee na akae nae mpaka atwahaarika.” [Muslim].

Yanayoruhusiwa wakati wa Hedhi na Nifasi:

1. Kufanya mengine yote katika matendo ya mapenzi isipokuwa kujamiiana kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Fanyeni kila kitu ila kuingiliana.” (Muslim, Ibn Majah na Imam Ahmad)

2. Kumtaja Mwenyeezi Mungu (s.w) kwa sababu hakuna makatazo katika kisheria kutokana na suala hili.

3. Kuhirimia na kusimama *Arafa* na matendo yote ya *Hijja* au *‘Umra* isipokuwa kutufu *Al-Ka’aba* si halali mpaka baada ya kutoharika na kuoga. Kutokana na kauli ya Mtume ﷺ aliyomwambia Bi Aisha رضي الله عنها:

“Fanya anayofanya mwenye kuhiji isipokuwa usitufu Al-Ka’aba mpaka mtoharike.” [Al-Bukhari, Muslim na Darimi].

4. Kula na kunywa na mwanamke mwenye hedhi na mwenye nifasi kutokana na maelezo ya Bi Aisha رضي الله عنها kuwa,

“Alikuwa akinywa wakati akiwa na hedhi na akimpa Mtume ﷺ kunywa pia kutoka katika chombo.” [An-Nasai na Imam Ahmad].

5. Na maelezo ya Abdillahi Ibni Masoud,

“Nilimuuliza Mtume ﷺ kuhusu kula na mwenye hedhi, akasema: kula naye.” [Ahmad na At-Tirmidhi).



Mada ya Nane

Katika Swala

Somo la Kwanza

Hukumu, Hekima na Ubora Wake

a) Hukumu ya Swala

Swala ni *faradhi* ya Mwenyeezi Mungu kwa kila Muislamu, kwani ameamrisha Allah (s.w) katika aya zaidi ya moja ndani ya kitabu Chake. Anasema:

فَأَقِمْوْا الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا ﴿١١٣﴾

“...Basi simamisheni Swala kwa hakika Swala kwa waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati maalumu.” (An-Nisaa 4:103)

Na amesema:

حَافِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَى وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴿٢٣٨﴾

“Dumuni juu ya Swala zote na Swala ya Al-asiri.” (2: 238).

Mjumbe wa Mwenyeezi Mungu ﷺ ameitaja kuwa ni nguzo ya pili katika nguzo tano za Uislamu,

“Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano. Kukiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah, na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyeezi Mungu. Na kusimamisha Swala na kutoa zaka na kuikusudia al-kaaba kwa ibada na kufunga mwezi wa Ramadhani.” [Al-Bukhari na Muslim].

Mwenye kuacha Swala katika dini ya kiislamu hukumu yake ni kuuawa na mwenye kuichezea ni fasiki.

b) Hekima Yake.

Moja ya hekima ya kufanya Swala kuwa ni lazima, ni athari nzuri inayopatikana kutokana nayo, Swala ikiswaliwa inavyostahili humsafisha mtu na makosa na inamtakasa. Pia inamfanya mja kuwa na sifa ya kunong'ona na Mwenyezi Mungu Mtukufu hapa duniani na kuwa jirani naye huko akhera. Ikiswaliwa vema Swala inamkataza mwenye kuswali mambo machafu na maovu. Amesema Allah Mtukufu:

إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ وَاللَّهُ
يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾

“...Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yatenda.” (Al-Ankabut 29: 45)

c) Ubora Wake.

Hadithi za Mtume ﷺ zifuatazo zinatoshia kuonyesha ubora na utukufu wa swala.

1. Kwa kauli yake ﷺ anasema:

“Msingi wa mambo ni Uislamu, nguzo yake ni Swala na kilele cha nundu yake ni kuipigania njia ya Allah.” [At-Tirmidhi].

Angalia maana na hadithi ya chini.

“Tofauti iliyopo kati ya muislamu na kafiri ni swala.” [Muslim,].

2. Kwa kauli yake ﷺ:

“Nimeamrisha nipigane na watu mpaka wakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba, hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na wasimamisha swala na watoe Zaka,

wakiyafanya hayo wamezilinda nami damu zao na mali zao kwa haki ya Uislamu, na hisabu yao itakuwa kwa Allah, Mwenye Kushinda, Mwenye Utukufu.” [Al-Bukhari].

3. Na kauli yake Mtume ﷺ wakati alipoulizwa ni lipi katika matendo lililo bora? Akajibu:

“Kuswali kwa wakati wake.” [Muslim].

4. Na kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa masahaba,

“Mfano wa Swala tano ni kama mfano wa mto wenye maji matamu na wenye maji mengi ulio mbele ya mlango mwa mmoja wenu, anaoga humo kila siku mara tano, jee kufanya hivyo atabaki na uchafu wake, wakajibu hapana, akasema basi Swala tano zinaondosha madhambi kama maji yanavyosafisha uchafu.” (Muslim).

5. Na kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Hakuna mtu yoyote yule Muislamu ambaye itamfikia swala iliyofaradhiwa akautengeneza udhu wake na akaswali kwa unyenyekevu wake, na rukui zake isipokuwa itakuwa ni kafara la yaliyo kabla yake miongoni mwa madhambi, ili mradi halijatendwa kosa kubwa na utaratibu huo unaendelea maisha yote.” [Ahmad na Muslim]

Somo la Pili

Katika Kuzigawa Swala Katika *Faradhi*,

Sunna na Na-fila

a) *Faradhi*:

Faradhi ni Swala tano tulizoamrishwa kuswali, kama vile Adhuhri, Alasiri, Magharibi, Isha na Swala ya Alfajiri (as-Subhi) kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Swala tano alizoandika Mwenyezi Mungu kwa waja wake atakayezisimamisha hatopoteza kitu katika Swala hizo kwa kuhofia kuacha haki zake atakuwa kwenye ahadi ya Allah ya kupata pepo yake, na kwa yule ambaye hatosimamisha Swala zake yeye hatohusika na ahadi hiyo, akipenda Allah atamuadhibu na akipenda atamsamehe.” (Imam Ahmad, Abu Dawuud na An-Nasai)

b) *Sunna*

Suna katika Swala ni: witri na raka'a mbili za alfajiri, na Iddi mbili, na swala ya kupatwa kwa jua na mwezi, na swala ya kuomba mvua na hizi ni sunna zilizotiliwa mkazo. Swala ya kuamkia msikiti, na sunna zinazofuatana na *faradhi* za kabla na baada na raka'a mbili za sunna baada ya kutawadha na Swala ya *dhuha* na tarawehe na kisimamo cha usiku na hizi ni sunna ambazo hazikutiliwa mkazo.

c) *An-Nafl*

Ni Swala za hiari ambazo hazikutiliwa mkazo na hazina wakati maalum kuswaliwa kwa kumshukuru Mungu usiku na mchana.

Somo la Tatu

Masharti ya Swala

a) Masharti kwa anayepasa kuswali

1. Uislamu. Kafiri hawezi kuswali. Kwa sababu kutanguliza shahada mbili ni sharti katika kuamrisha Swala kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Nimeamrisha nipigane na watu mpaka wakiri kwa moyo na watamke kwa ulimi kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyeezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyeezi Mungu na wasimamisha Swala na watoe zaka.”

Na kauli yake alipomwambia Muadh bin Jabal,

“Waite kwenye kushuhudia kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Mwenyeezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyeezi Mungu, wakikutii kwa hilo, waeleze kwamba Mwenyeezi Mungu amefaradhisha juu yao swala tano katika kila mchana na usiku.” [An-Nasai].

2. Kuwa na akili timamu. Haipasi Swala juu ya mwenda wazimu, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Imenyanyuliwa kalamu kwa watu watatu: aliyelala mpaka aamke, na mtoto mdogo mpaka abaleghe na mwendawazimu mpaka apate akili.” [Abu Dawuud]

3. Kubaleghe. Mtoto aliye chini ya umri hawezi kuswali mpaka abaleghe kwa kauli ya Mtume ﷺ: *“Na mtoto mdogo mpaka abaleghe.”* Isipokuwa huyo mtoto ataamrisha kwa hiyo Swala na ataiswali kwa suna kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Waamrisheni watoto wenu kuswali watakapofikisha umri wa miaka saba, na wapigeni wakiacha Swala watakapofikisha umri wa miaka kumi, na watenganisheni kati yao katika malazi.” [Abu Dawuud na Ibn Majah].

4. Kuingia wakati wake. Swala haiwezi kuswaliwa kabla ya wakati wake, kwa tamko la Mwenyezi Mungu (s.w):

فَإِذَا أَطْمَأْنَنْتُمْ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْفُورًا ﴿١٠٣﴾

“...Na mtapo tulia basi shikeni Sala kama dasturi. Kwani hakika Sala kwa Waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalumu” (An-Nisaa 4:103).

Kwa maana yenye wakati ulio na mpaka, na kwa sababu Jibril عليه السلام alishuka akamfundisha Mtume ﷺ nyakati za swala, kwani alimwambia,

“Simama uiswali, akaswali Adhuhuri wakati lilipopinduka jua, kisha akaniamrisha kuamka kuswali na nikaswali wakati wa Alasiri, wakati kilipokuwa kivuli cha kila kitu mfano wake. Kisha akamjia Magharibi akasema: Simama uiswali, akaswali Magharibi wakati lilipozama jua. Kisha akamjia Isha akasema: simama uswali, akaswali Isha wakati yalipozama mawingu mekundu, kisha akamjia Alfajiri, wakati ilipo zagaza Alfajiri, kisha akamjia kesho yake kwa ajili ya Adhuhuri, akasema: simama uswali, akaswali Adhuhuri wakati kulipokuwa kivuli cha kila kitu mfano wake, kisha akamjia Alasiri wakati kilipokuwa kivuli cha kila kitu mifano yake miwili. Kisha akamjia Magharibi hali ya kuwa wakati mmoja tu hakuondokana nao, kisha akamjia Isha wakati ilipoondoka nusu ya usiku, au alisema thuluthi ya usiku akaswali Isha, kisha alimjia wakati kulipozagaza sana akasema: simama uswali akaswali Alfajiri kisha akasema kati ya nyakati mbili hizi kuna wakati.” [Ahmad na An-Nasai].

5. Kutokuwa na damu mbili ya hedhi au ya nifasi. Haipasi Swala juu ya mwenye hedhi na wala juu ya mwenye nifasi mpaka atoharike. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Itakapo kuja hedhi yako acha swala.” [Al-Bukhari, Muslim].

b) Masharti ya Kuswihi kwa Swala

Kutoharika na *hadathi* ndogo na kwa kuwa na udhu. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“*Hakubali Mwenyezi Mungu swala yoyote bila ya tohara.*” [An-Nasai na Darimy].

1. Kusitiri tupu kwa tamko la Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿يَبْنَئِ ۙ آدَمَ خُذُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا﴾

“...*Enyi wanaadamu! Chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada...*” (7: 31).

Swala haiswihi kwa mtu aliye uchi, kwani neno *zinaa* katika aya lina maana ya nguo. Na uchi wa wanaume ni sehemu iliyo kati ya kitovu chake na goti lake na uchi wa mwanamke ndani ya Swala ni mwili mzima isipokuwa uso wake na viganja vyake kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“*Haikubali Mwenyezi Mungu Swala ya mwanamke aliyebaleghe isipokuwa kwa kujisitiri.*” [Abu Dawuud].

Na kwa kauli yake wakati alipoulizwa kuhusu Swala ya mwanamke katika kanzu ya chuma na Mtandio, pasina shuka ya chini akasema:

“*Itakapokuwa hiyo kanzu ya chuma inaenea na kufunika kuonekana nyayo zake.*” [Abu Dawuud na Ad-Daraqutni].

2. Kuelekea Kibla: Swala haiswihi kama mtu hakuelekea Kibla kwa tamko la Allah (s.w):

﴿وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا

﴿وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ۚ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ﴾

“Na popote wendako elekeza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu. Na popote mlipo elekezeni nyuso zenu upande huo ili watu wasiwe na hoja juu yenu...” (Al-Baqarah 2: 150).

Upande wa msikiti mtukufu, isipokuwa kwa mwenye kushindwa kuelekea *Kibla* kwa sababu ya khofu, ugonjwa na dharura nyingine, sharti hili litapomoka kwa sababu ya kushindwa kwake. Kama ambavyo msafiri kunajuzu kwake kuswali sunna juu ya mgongo wa mnyama wake kokote atakakoelekea kwenye *Kibla*, au kwingine, kwani alionwa Mtume ﷺ,

“Akiswali juu ya mnyama wake na hali ya kuwa yeye alitoka Maka kwenda Madina kule ambako mnyama wake alikuwa ameelekea.” [Muslim].

Somo la Nne

Nguzo za Swala, Sunna Zake, Makuruhu Yake, na Yanayoruhusiwa na yanayobatilisha Swala

a) Nguzo Zake

1. Kusimama katika Swala ya *faradhi* kwa mwenye kuweza. Kwa tamko lake Allah (s.w):

وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ

“Na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nanyi ni wenye kuqunuti (kunyenyekaa)...” (al Baqarah 2:238)

Na kauli yake Mtume ﷺ akimwambia Imrani Ibni Huswain,

“Swali hali ya kuwa umesimama, ukishindwa kusimama basi Swali umekaa, ukishindwa kuka basi swali umelala ubavu.” [Al-Bukhari na Abu Dawuud].

2. Kunuia ni kuazimia moyoni kuwa umetokeleza Swala maalumu, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika hapana jambo jingine matendo yote huzingatiwa kwa nia.”

3. Takbira ya kuhirimia, kwa tamko la الله أكبر, ‘Allahu Akbar’, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Ufunguo wa Swala ni kujitoharisha na kuifunga kwa takbira, na kuifunga ni kutoa salam.” [Abu Dawuud na At-Tirmidhi].

4. Kusoma Suratil Fatiha, kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Swala haiswihi kwa ambaye hakusoma Suratil-Fatiha.” [Al-Bukhari].

Isipokuwa hiyo Surat Fatiha inapomoka kwa maamuma iwapo imamu atadhihirisha Imamu akisoma kisomo kwa sababu maamuma ameamrisha kunyamaza kwa kisomo cha Imamu wake kwa tamko la Mwenyezi Mungu (s.w):

فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿١٠٠﴾

“Na isomwapo Qur’ani isikilizeni na mnyamaze ili mpate kurehemewa.” (Al-A’araf 7:204).

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Akitoa Takbira Imamu na nyinyi toeni Takbira, na akisoma sikilizeni.” [Imam Ahmad].

Na wakati Imamu akisoma kwa siri ataisoma maamuma kwa njia ya wajibu.

6. Kunyanyuka kutoka rukuu Kunyanyuka kutoka katika rukuu kutokana na kauli yake Mtume ﷺ kumwambia yule mtu aliye iharibu Swala yake:

“Kisha rukuu mpaka utulizane hali ya kurukuu kisha nyanyuka mpaka ulingane sawa hali ya kusimama.” [Al-Bukhari].

7. Kusujudu:

8. **Kunyanyuka** kutoka katika sijida kwa kauli yake Mtume ﷺ akimwambia yule mtu aliyeiharibu swala yake, “*Kisha sujudu utulizane na hali umesujudu, kisha nyanyuka na utulizane hali ya kuwa umekaa.*” Na tamko la Mwenyezi Mungu (s.w):

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اَرْكَعُوْا وَاَسْجُدُوْا وَاَعْبُدُوْا رَبَّكُمْ وَاَفْعَلُوْا الْخَيْرَ

لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُوْنَ ﴿٧٧﴾

“*Enyi mlio amini! Rukuuni na msujudu, na muabuduni Mola wenu Mlezi, na tendeni mema, ili mfanikiwe*” (22:77)

9. **Kutulizana** katika rukuu na sijida na kusimama na kukaa kutokana na kauli yake Mtume ﷺ kumwambia yule mtu aliyeiharibu swala yake, “*mpaka utulizane.*” Amemtajia hilo katika rukuu na sijida na kukaa, na amemtajia kulingana sawa katika kunyanyuka kutoka katika rukuu, na katika kusimama.

Hakika ya kutulizana ni kukaa mwenye kurukuu au mwenye kusujudu au mwenye kukaa au mwenye kusimama baada ya kutuliza viungo vyake muda kwa kiasi cha kutamka, “*Kutakata ni kwa Mwenyezi Mungu Aliye Mkubwa.*” (Muslim) Mara moja na kitakachozidi juu ya kiasi hicho basi hicho ni sunna.

10. Kutoa Salam:

11. **kukaa kwa ajili ya kutoa salamu**, Mtu hatatoka katika Swala bila ya kutoa salamu na hatatoa salamu isipokuwa wakati amekaa kwa kauli yake Mtume ﷺ: “*Na kufunguliwa kwake ni kutoa salamu*”.

12. **Kufuatanisha** kati ya nguzo kwa hivyo hutasoma *Fatiha* kabla ya Takbira ya kuhirimia na utasujudu kabla ya rukuu kwani muundo wa Swala umehifadhika kutoka kwa Mtume ﷺ na aliwafundisha masahaba zake, na kusema Mtume ﷺ

: “*Swalini kama mnavyoniona nikiswali.*” [Al-Bukhari].

Haijuzu kuitanguliza nguzo ya nyuma katika hiyo Swala wala kuichelewesha ilivyotangulia ukifanya hivyo Swala itabatilika.

b) Sunna Zake

Sunna za swala zipo kaika makundi mawili: zilizotiliwa mkazo ambazo ni wajibu, na zisizotiliwa mkazo ambazo ni sunna.

Sunna za Wajibu

1. Kusoma Qur-aan hata kama ni aya moja au mbili hivi baada ya kusoma *Fatiha*, katika Swala ya asubuhi, na katika raka mbili za mwanzo za Adhuhuri na Alasiri na Magharibi na Isha. Kutokana na Hadithi iliyopokelewa:

“Katika Swala ya adhuhuri Mtume ﷺ alikuwa akisoma Suratil Fatiha na sura mbili katika raka mbili za mwanzo, raka mbili za mwisho alikuwa akisoma Suratil Fatiha na alikuwa akiwasikilizisha Aya mara nyingi.” [Al-Bukhari].

2. Kusema, *سمع الله لمن حمده*, “*Samiya Llahu Liman Hamidahu*” unapotoka katika rukuu, ‘Amezisikia Yeye Mwenyezi Mungu Sifa za Anayemsifu’, *ربنا ولك الحمد*, ‘*Rabbana Walakal Hamd*’, “*Ee Bwana wetu ni zako sifa njema*” kwa Imamu na kwa mwenye kuswali peke yake. Na kusema: “*Ee Bwana wetu ni zako sifa njema*” kwa maamuma kutokana na maelezo wa Abu Huraira رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alikuwa anasema: *سمع الله لمن حمده*, “*Samiya Llahu Liman Hamidahu*.”, “*Amezisikia Allah sifa za mwenye kumsifu*,” wakati anapounyanyua mgongo wake kutoka katika rukuu kisha anasema na hali ya kuwa amesimama, *ربنا ولك الحمد*, “*Rabbana Walakal Hamdu*.”,

“*Ee Bwana wetu ni zako sifa njema.*” (Al-Bukhari na Muslim)

Na kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Akisema Imamu: Amezisikia Allah sifa za mwenye kumsifu, semeni Ewe Mola wa Haki Bwana wetu ni zako sifa njema.”
[Muslim na Al-Bukhari]

3. Kusema, سبحان ربي الأعلى, “Subhana Rabbiyal ‘ala”, “Kutakasika ni kwa Bwana wangu Aliye Mkubwa.” , katika Sijida mara tatu na kusema: سبحان ربي العظيم, “Subhana Rabbiyal Adhim”, “Kutakata na maovu yote ni kwa Bwana wangu Aliye Mtukufu.” katika Rukuu, kutokana na tamko la Mwenyezi Mungu (s.w),

فَسَبِّحْ بِأَسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٧٤﴾

“Basi litakase jina la Mola wako Mlezi aliye Mkuu”. (Al-Waqi’a 56: 74)

Tamkeni maneno hayo katika rukuu yenu na iliposhuka:

سَبِّحْ أَسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴿١﴾

“litukuze jina la Mola wako aliye Mtukufu.” (AlA’ala: 1)

Alisema Mtume ﷺ “Ifanyeni katika sijida zenu.” [Muslim na Abu Dawuud].

4. Takbira ya kuhama kutoka katika kisimamo kwenda kwenye sujudi na kutoka sijida kwenda kwenye kukaa na kutoka katika kukaa kwenda kwenye kisimamo kwa sababu limesikiwa hilo kutoka kwa Mtume ﷺ.

5. Tashahudi ya Kwanza na ya pili na Kukaa kwa Ajili Hiyo

6. Tamko la Tashahudi ni:

التحيات لله، والصلوات والطيبات، السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته، السلام علينا، وعلى عباد الله الصالحين، أشهد أن لا إله إلا الله، وحده لا شريك له، وأشهد أن محمدا عبده ورسوله.

“Utukufu wote ni wa Allah na Swala na matendo yote mema yote hayo ni kwa ajili ya Allah. Amani iwe juu yako ewe Mtume na Rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka zake. Amani iwe juu yetu na juu ya Waja wa Allah waliyo wema. Nakiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba, hapana mola apasae kuabudiwa

kwa haki ila Allah hali ya kuwa peke yake hana mshirika na ninakiri kwa moyo na kubaini kwa ulimi kwamba Muhammad ni Mja wake na Mjumbe wake.” [Al-Bukhari na Muslim].

7. Kusoma kwa sautii katika Swala ya kusoma kwa sauti, utasoma kwa sauti katika raka mbili za mwanzo za Magharibi na Isha, na katika swala ya Asubuhi na utasoma kwa siri katika zisizo kuwa sehemu hizo.

8. Kusoma kwa siri katika Swala ya kusoma kwa siri: Utaratibu huu ni katika Swala ya faradhi, ama katika Swala ya sunna, sunna katika Swala hiyo ni kusoma kwa siri ikiwa ni ya mchana, na kusoma kwa uwazi ikiwa ni ya usiku ila atakapogopa kumuudhi mtu mwengine kwa kisomo chake, katika hali hiyo, inapendekezwa kwake kusoma kwa siri.

9. Kumswalia Mtume ﷺ Tashahudi ya mwisho, baada ya kusoma Tashahudi utasema:

اللهم صلّ على محمد وعلى آل محمد، كما صليت على إبراهيم وعلى آل
إبراهيم، وبارك على محمد وعلى آل محمد، كما باركت على إبراهيم
وعلى آل إبراهيم إنك حميد مجيد

“Ee Mola wangu wa haki Mrehemu Muhammad na Jamaa za Muhammad, kama ulivyomrehemu Ibrahim na Jamaa zake Ibrahim na mbariki Muhammad kama ulivyombariki Ibrahim na Jamaa zake Ibrahim, hakika Wewe ni Mwingi wa Kusifiwa Uliye Mtukufu.” [An-Nasai, Abu Dawuud na Imam Ahmad].

Sunna Zisizotiliwa Nguvu:

1. Dua ya Ufunguzi,

((سبحانك اللهم وبحمدك وتبارك اسمك وتعالى جدك ولا إله غيرك))

“Subhanaka Allahumma Wabihamdika wa Tabaraka Ismuka wataala Jadduka Wala Illaha Ghairuka.” (At-Tirmidhi na Abu Dawuud)

2 . **Kusoma Audhubillah** katika rakaa ya kwanza na kusoma “*Bismillah*” kimya kimya” katika rakaa zote, Allah (s.w) amesema:

فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿١٠٠﴾

“*Na ukisoma Qur’ani mwombe Mwenyezi Mungu akulinde na Shetani maluuni.*” (al Nahli 16: 98)

3. **Kunyanyua mikono** miwili mpaka usawa wa mabega mawili wakati wa Takbira ya kwanza: Na wakati wa kurukuu, itidali, na wakati wa kunyanyuka toka rakaa mbili za mwanzo, kwa kauli ya Ibn Umar رضي الله عنه

“*Hakika Mtume ﷺ alikuwa anaposimama katika Swala ananyanyua mikono yake miwili mpaka usawa wa mabega yake kisha anatoa Takbrira, na anapotaka kurukuu anainyanyua mfano huo, na anaponyanyua kichwa chake toka rukuu anainyanyua pia, na anasema: Samiallah Liman Hamidah, ‘Rabban WalakaI Hamdu.’* (At-Tirmidhi, Abu Dawuud na Ibn Majah)

4. **Kusema “Amin”** baada ya kusoma *Al-fatih*a (*Al-Hamdu*) imepokewa toka kwa Mtume ﷺ kuwa aliposoma,

غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴿٢٠٠﴾

“*Ghairil-Magh’dhuwbi Alayhim Wala D-dwaallina.*” (al-Fatiha:7).

Alisema “*Amin*” kwa kurefusha tamko lake.” (Abu Dawuud)

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ kuwa, “Ataposoma Imamu,

‘*Ghayril-Magh’dhuwbi Alayhim Walad-Dhwaallin*’ (al Fatiha: 7).

Itikieni ‘*Amin*’. Kwani kauli ya mtu itakayoafikiana na ya malaika atasamehewa dhambi zake alizotanguliza.” (Al-Bukhari)

5. **Kurefusha kisomo** katika swala ya Asubuhi na kupunguza katika Swala ya Alasiri na Magharibi na kufanya kati na kati katika Swala ya Isha na Adhuhuri. Imepokewa kuwa Umar رضي الله عنه alimuandikia Abu Mussa kuwa:

“*Katika Swala ya asubuhi asome sura ndefu na katika Swala ya adhuhuri asome sura za kati na asome katika swala ya magharibi sura fupi.*” (At-Tirmidhi)

6. **Kuomba dua** kati ya sijida mbili kwa kusoma:

((رب اغفر لي وارحمني وعافني واهدني وارزقني))

“*Rabbigh Firlil War-Hamnii, Wa-Afiniy Wahdiniy War-zuqniy.*”

Kutokana na yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alikuwa anasema hivyo kati ya sijida mbili.” (An-Nasai)

7. **Dua ya Qunuti** katika raka'a ya mwisho ya Swala ya asubuhi au katika witra baada ya kisomo au kuinuka toka kwenye rukuu. Kama inavyosomwa:

((اللهم اهدني فيمن هديت، وعافني فيمن عافيت، وتولني فيمن توليت،
وبارك لي فيما أعطيت، وقني واصرف عني شرّ ما قضيت، فإنك تقضي
ولا يقضي عليك، إنه لا يذلّ من واليت، ولا يعزّ من عاديت، تباركت ربنا
وتعاليت، اللهم إني أعوذ برضاك من سخطك وبمعافاتك من عقوبتك، وبك
منك لا أحصي ثناء عليك، أنت كما أثنيت على نفسك))

“*Allahumma hdiniy Fii man Hadayta, Wa 'Afiniy Fi-Man 'Afayta,
Watawallaniy Fiy man Tawallayta Wa Baarik Liy Fi-Man
'Aatwayta, Waqiniy Waswriy Anniy Sharra ma Qadhayta,
Fainnaka Taqdhiy wala Yuqdhha Alayka Inna-Hu La Yadhillu Man
wa-layta, Wala yaizzu Man 'Aadayta, Tabaarakta Rabbana
wata'a-layta. Allahuma Inni Audhu Biridhwa-ka Min Sakhtwika
Wabimu'aa Faatika Min Uquubatika, Wabika Minka La Uh'swi
Thana'a Alayka, Anta Kamaa Ath'nayta 'Ala- Nafsika.*”

“Ewe Mola tuongoze katika uliowaongoza, na uniafu katika uliowaafu, na unitawalishe katika uliowatawalisha, na unibariki katika ulichotoa, na nikinge na uniondolee shari uliyohukumu, hakika wewe unahukumu wala huhukumiwi, hadhalili uliyomtawalia, wala hakukuki (hawi mshindi) uliomfanya adui, Umetukuka Mola wetu ulio Juu, Ewe Mola najilinda kwa radhi zako na ghadhabu zako kutokana na msamaha wako na adhabu zako, Na kwako wewe sidhibiti sifa Wewe ni kama ulivyojisifu mwenyewe.” (An-Nasai, Abu Dawuud na Imam Ahmad)

8. **Namna ya Mkao** uliopokelewa toka kwa Mtume ﷺ katika sifa ya Swala yake, nao ni kukalia mguu katika vikao vyote na kukalia tako katika kikao cha mwisho.

Iftirash: Ni kukalia tumbo la mguu wa kushoto na kuunyoosha unyayo wa mguu wa kulia.

Tawarruku: Ni kuweka tumbo la mguu wa kushoto chini ya paja la kulia na kukaa vema ardhini na kunyoosha vema mguu wa kulia na kuweka mkono wa kushoto juu ya goti la kushoto vidole vikiwa vimenyooshwa na vidole vya mkono wa kulia vyote vikiwa vimefumbwa isipokuwa kidole cha Shahada na kikitikiswa wakati wa kusoma Tashahhud Mtume ﷺ, **“Tahiyatu”**. Hayo ni kwa mapokezi kuwa:

*“Alipokaa katika **Tahiyatu** aliweka mkono wa kulia juu ya paja lake la kulia, na mkono wake wa kushoto juu ya paja lake la kushoto na aliashiria kwa kidole cha shahada, na macho yake hayakuvuka mpaka wake.”* (Muslim)

9. **Kuweka Mikono** Miwili juu ya kifua, wa kulia juu ya kushoto, kutokana na kauli ya Sahl:

“Walikuwa watu wanaamriwa kuweka mwanamume mkono wake wa kulia juu ya dhira ya kushoto katika Swala.” Na kwa kauli ya Jabir, *“Alipita Mtume ﷺ kwa mtu anayeswali na ameweka mkono wake wa kushoto juu ya mkono wa kulia, akauondosha na kuweka mkono wa kulia juu ya ule wa kushoto.”* (Imam Ahmad)

10. **Dua Katika Sijida:** Kutokana na kauli yake Mtume ﷺ :

ألا وإني نهيت أن أقرأ القرآن القرآن راععا أو ساجدا فأمر الركوع فعظمو
فيه الرب وأمر السجود فاجتهدوا في الدعاء

“Zindukeni, hakika mimi nilikatazwa kusoma Qur-aan katika rukuu na katika sijida, ama katika rukuu mtukuzeni Mola na katika sijida jitahidini kuomba dua.” (Muslim)

11. **Dua katika Tahiyatu** ya mwisho. Baada ya kumswalia Mtume ﷺ kwa kusoma:

((اللهم إني أعوذ بك من عذاب جهنم، ومن عذاب القبر، ومن فتنة
المحيا والممات، ومن فتنة المسيح الدجال))

“Allahumma Inni Audhubika Min Adha-bi Jahannamu, Wamin Adhabil-Qabri Wamin Fitnatil-Mahya- Wal-Mama-ti, Wamin Fitnatil-Masiyhi Ddajjali.”

Na hii ni kutokana na kauli yake Mtume ﷺ.

“Atapomaliza mmoja wenu tahiyatu ya mwisho na amwombe Mwenyezi Mungu amlinde kutokana na mambo manne: ,

اللهم إني أعوذ بك من عذاب جهنم.

“Allahumma inni audhubika min adhabi jahannam...” (Muslim)

12. **Salamu huanza kutolewa kwa mkono wa kulia.**

13. **Kutoa salamu** ya pili upande wa kushoto. Kutokana na yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa,

“Alikuwa anatoa salamu upande wa kulia kwanza na kisha upande wake wa kushoto.” (Abu Dawuud)

14. **Dhikri na Dua** baada ya salamu, kutokana na Hadith zifuatazo:

a) Amepokea Thauban رضي الله عنه kuwa kabla ya Mtume ﷺ kutoka ndani ya Swala alikuwa anafanya *Istighfar* (kuomba msamaha kwa Allah) “

mara tatu أستغفر الله, “Astaghfirullah”. Na kisha kuomba dua:

اللهم أنت السلام ومنك السلام، تباركت يا ذا الجلال والإكرام

“*Allahumma Anta Ssalaam Waminka Ssalam, Taba-rakta Ya Dhal Jalali Wal-Ikram.*” (Muslim)

b) Amepokea Muadh bin Jabal رضي الله عنه kuwa baada ya kila Swala ya faradhi Mtume ﷺ alimshika mkono wake siku moja kisha akasema:

“Ewe Muadh! Hakika mimi nakupenda! Ninakupa usia Ewe Muadh! Kila baada ya Swala usiache kusema:

اللهم أعني على ذكرك وشكرك وحسن عبادتك

“*Allahumma A’inniy ala- Dhikrika Washukrika Wahusni ‘Ibadatika.*” (Abu Dawuud na Al-Hakim)

c) Amepokea Mughira bin Shuuba رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alikuwa anasema baada ya kila Swala ya faradhi,

لا إله إلا الله وحده لا شريك له، له الملك، وله الحمد وهو على كل شيء قدير،
اللهم لا مانع لما أعطيت، ولا معطي لما منعت، ولا ينفع ذا الجد منك الجد

“*La ilaha Illa Llah Wah’dahu La Sharika Lahu, Lahul-Mulku, Walahul-Hamdu Wa Huwa Ala Kulli Shay’in Qadir, Allahumma La Maani’a Limaa A’atwayta, Wala Mu’utwiya Lima Mana’ata Wala Yan-Fa’u Dhal-Juddu Minkal-Jaddu.*”

d) Amepokea Abu-Umama رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

من قرأ آية الكرسي دبر كل صلاة لم يمنعه من دخول الجنة إلا أن يموت

“Atayesoma Ayatul-Kurrsiyuu baada ya kila swala hakuna kitachomzuia kuingia peponi isipokuwa kifo.” (At-Tabarani)

e) Amepokea Abu Huraira رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

“Atakayemsabihi Allah baada ya kila Swala mara thelathini na tatu, na akamuhimidi mara thelathini na tatu, na akamkabbir mara thelathini na tatu na hizo ni tisini na tisa na akasema katika kutimiza mia: La ilaha Illa Llahu Wah’dahu La- Sharika Lahu, Lahul Mulku Walahul-Hamdu Wahuwa Ala- Kulli Shayin Qadir.” Basi atasemehewa makosa yake hata kama ni mengi mfano wa povu la bahari.” (Muslim)

f) Amepokea Saad bin Abi Waqqas رضي الله عنه kuwa kila baada ya Swala Mtume ﷺ alikuwa akisema.

عن سعد بن أبي وقاص أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: كان يتعوذ
دبر كل صلاة بهذه الكلمات " اللهم إني أعوذ بك من البخل وأعوذ بك من
الجبين ، وأعوذ بك من أرد إلى أرذل العمر وأعوذ بك من فتنة الدنيا
وأعوذ بك من عذاب القبر .

“Allahumma Inni A’udhubika Minal-Bukhli, Wa A’udhubika Minal-Jubni, Wa A’udhubika Min An Uradda Ila Ardhalil-‘Umri, Wa Audhubika min Fitmatil D-dunya, Wa A’udhubika Min ‘Adhabil-Qabri.” Na Saada alikuwa akiwafundisha watoto wake.” (Al-Bukhari)

“Ewe Mola, Najilinda kwako na Ubakhili, na Najilinda kwako na Uoga, na Ninajilinda kwako na kurudishwa katika umri dhalili, na Najilinda kwako na fitina za Dunia, na Najilinda kwako na adhabu ya kaburi”

c) **Mak-ruhu za Swala**

1. **Kugeuka** kwa kutumia kichwa au macho kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Kufanya hivyo ni udokozi anaodokoa shetani katika Swala ya mja.” (Al-Bukhari)

2. **Kunyanyua macho** juu kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Wana nini wale wanaonyanyua macho yao juu wakiwa ndani ya Swala zao wakome kufanya hivyo au watapofolewa macho yao.” (Al-Bukhari)

3. **Kuweka mikono kiunoni**, kutokana na mapokezi ya Abu Huraira رضي الله عنه kuwa:

“Mtume ﷺ amekataza (mtu) kuswali huku ameweka mikono kiunoni.” (At-Tirmidhi na An-Nasai)

4. **Asiondoe mwenye** kuswali nywele zilizozidi katika paji lake la uso, na asiondoe nguo yake iliyozidi, kutokana na kauli yake Mtume ﷺ kuwa:

“Nimeamrisha kusujudu juu ya viungo saba, na nisiondoshe nywele, au nguo.” (Muslim)

5. **Kuvishikanisha vidole**, kutokana na ilivyopokewa kuwa Mtume ﷺ alimuona mtu ameshikanisha vidole akiwa ndani ya Swala, akaviachanisha na akamwambia:

“Usivishikanishe vidole vyako ukiwa ndani ya Swala.” (Ibn Majah)

6. **Kuondosha mchanga** zaidi ya mara moja toka eneo la kusujudia, kutokana na kauli yake Mtume ﷺ: *“Ataposimama mmoja wenu katika Swala hakika rehema zinamuelekea asiondoe vijiwe (mchanga)”*.

Na kauli yake nyingine:

“Ikiwa utafanya hivyo basi iwe mara moja.” (Ibn Majah na Ad-Darimi)

7. **Kucheza cheza** au kuwa mpuuzi, pamoja na kila kinachomshughulisha mja ndani ya Swala na kuondoa khushui, kama kuchezea ndevu, nguo au kutazama tazama mapambo yalio katika mabusati, kuta na kudhalika. Kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Tulieni katika Swala.” (Muslim)

8. **Kusoma katika rukuu au sujudu**, kutokana na kauli yake Mtume ﷺ,

“Nilikatazwa kusoma Qur-aan nikiwa katika rukuu, au sijida.” (Shafii)

9. **Kutenzwa na haja kubwa au ndogo.**

10. **Kuswali hali ya kuwa chakula kipo tayari.** Kutokana na kauli ya Mtume ﷺ,

“Si vema kuswali ikiwa chakula kipo tayari au mtu ameshikwa na haja.” (Muslim)

11. **Kukalia visigino viwili**, na kunyoosha dhira mbili, kutokana na maelezo Bi Aisha رضي الله عنها:

“Mtume ﷺ alikuwa anakataza mka o wa shetani wa – kukalia visigino - na alikataza kunyoosha mtu Dhira zake kama afanyavyo mbwa” (Muslim)

d) Vibatilisha Swala:

1. **Kuacha nguzo** miongoni mwa nguzo za Swala. Kama isipoletwa kabla ya kumaliza Swala au baada ya kupita kwa muda mfupi. Kwa kauli ya Mtume ﷺ kwa aliyeswali vibaya alipoacha kujituliza na itidali hali ni nguzo:

“Rudi na Swali kwani haukuswali.” (Muslim)

2. **Kula au kunywa.** Kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Ndani ya swala mna kazi.” (Al-Bukhari, Muslim na Abu Dawuud)

3. **Maneno nje ya maslahi** ya Swala ndani ya Swala, kutokana na tamko lake Allah (s.w):

وَقَوْمًا لِلَّهِ قَانِتِينَ ﴿١٧٢﴾

“...na simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu nanyi ni wenye kuqunuti (kunyenyekoa)...” (Al-Baqara 2: 238)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika ndani ya Swala haikubaliki kusemwa chochote katika maneno ya watu.” (Muslim)

Kama ikiwa maneno kwa maslahi ya Swala - mfano atapotoa salam Imamu kisha akauliza kama Swala imetimia na akajibiwa kuwa haijatimia basi atatimiza, au akikosea Imamu katika usomaji na akasomewa na Maamuma, hayo hayana ubaya. Kwani Mtume ﷺ alizungumza katika Swala yake na alizungumza - *Dhul-ya-Dayn* pia, na Swala haikubatilika, kwani *Dhul-ya Dayn* alisema kumueleza Mtume ﷺ: “Umesahau, au Swala imepunguzwa?”

Na Mtume ﷺ akajibu:

“Sikusahau wala haikupunguzwa.” (Abu Dawuud, Al-Bukhari na An-Nasai)

4. **Kucheka, kwa sauti** na sio kutabasamu. Wamekubaliana wanazuoni juu ya kubatilika Swala kwa sababu ya kucheka. Mpaka baadhi ya wanazuoni wanaona kuwa udhu hutenguka kwa kujichekesha. Na imepokewa toka kwa Mtume ﷺ kuwa: *“Haibatilishi swala tabasamu lakini inabatilishwa na kucheka kwa sauti.”*

5. **Vitendo vingi** ndani ya Swala, na sababu ni kuwa vinapingana na ibada, na kushughulisha nafsi na viungo na kisichokuwa Swala. Ama vitendo - vichache kama vile kuweka sawa kofia (kiremba) au kupiga hatua moja kwenye safu ili kuziba uwazi au kunyoosha mkono kuchukua kitu mara moja- Swala haibatiliki kwa hilo. Kwani imepokewa na Kusihhi toka kwa Mtume ﷺ,

“Alimuinua Umama na kumuweka chini hali ya kuwa yupo ndani ya Swala akiwa Imamu.” Na Umama ni mtoto wa Zainab bint Rasul. (Al-Bukhari)

6. **Kuzidisha kitu** kama rakaa kwa kusahau - kama vile kuswali Adhuhuri rakaa au Maghribi rakaa tano sita au Subhi rakaa nne kwani kusahau kwako mpaka kuzidisha Swala kwa mfano huu ni ushahidi tosha kuwa ulikuwa huna khushui ambayo ni siri ya Swala yake na roho yake na Swala ikikosa roho hubatilika.

7. **Kukumbuka Swala** ya nyuma. Mfano mtu akianza kuswali Alasiri kisha akakumbuka kuwa hakuswali Adhuhuri basi Alasiri itabilika mpaka aswali Adhuhuri. Kwa sababu utaratibu katika Swala tano ni lazima kwa kupokelewa kwake kutoka kwa Allah kwa mpangilio - faradhi baada ya faradhi, usiswali Swala kabla ya ile ya nyuma yake.

e) Yanayoruhusiwa katika Swala

1. **Harakati ndogo ndogo** (nyepesi) kama kuweka vizuri kilemba au kofia - kwani imethibiti hivyo toka kwa Mtume ﷺ.

2. **Kujikohoza kwa dharura.**

3. **Kumuweka sawa aliye** katika safu, kwa kumsogeza mbele kwa Imamu au kumrudisha nyuma au kumzungusha Maamuma kumpeleka kulia, kama alivyomtoa Mtume ﷺ Ibn ‘Abbas kushotoni kwake na kumuweka kuliani pale alipomfuata nyuma katika moja ya swala za usiku.

4. **Kupiga mwayo** na kuweka mkono kinywani.

5. **Kumkumbusha Imamu**, na kumsomea سبحان الله, ‘Sub’hanallah’ kama amesahau jambo kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Yule aliyezinduka na kitu katika Swala yake na aseme: سبحان الله, ‘Sub’hanaallah’.” (Al-Bukhari na An-Nasai)

6. **Kuwazuia wanaopita mbele yake** kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Anaposwali mmoja wenu nyuma ya kitu kinachomzuia na wapitaji, anapotaka yeyote kuvuka mbele yake na amzuie na kama akikataa, pigana naye kwani huyo ni sheitani.” (Al-Bukhari na Muslim)

7. **Kuua nyoka au n’ge** kwa kuhofia usalama wako hali ya kuwa upo ndani ya Swala, kutokana unaruhusiwa kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Uweni vyeusi viwili (nyoka na nge) hata mkiwa katika Swala.”
(Abu Dawuud na Al- Hakim)

8. **Kujikuna kwa mkono** wako kwani hilo ni miongoni mwa matendo mepesi yaliyoruhusiwa.

9. **Kuashiria kwa kiganja** cha mkono kwa aliyekusalimia, kutokana na kitendo cha Mtume ﷺ katika hilo. (At-Tirmidhi)

Somo la Tano

Katika Sijida ya Kusahau:

Yule atakayesahau katika Swala yake na akazidisha rakaa au sijida, au mfano wa hivyo, ni wajibu kwake kusujudu kufidia Swala yake - sijida mbili baada ya kumaliza Swala yake kisha atoe salamu. Na vile vile mwenye kuacha sunna iliyotiliwa mkazo miongoni mwa sunna za Swala kwa kusahau basi atasujudu sijida mbili kabla ya kutoa salamu na hiyo ni kama akiacha *Tahiyatu* ndogo na wala hakukumbuka pale pale au amekumbuka baada ya kukamilisha kisimamo chake, hapo hawezi kurudia kikao isipokuwa atasujudu kabla ya kutoa salamu. kama ataitoa salamu kabla ya kumaliza swala hiyo haraka atarudi pale alipoachia kama muda ni mfupi kisha atimize Swala yake na atasujudu baada ya salamu. Na ushahidi katika hili ni kauli yake Mtume ﷺ na vitendo vyake:

“Alitoa salamu ﷺ katika rakaa ya pili na akaelezwa, kisha akarudia na kutimiza Swala yake, na akasujudu baada ya salamu.” (Al-Bukhari na Muslim)

Wakati mwingine alisimama moja kwa moja kutoka rakaa ya pili na hakukaa *Tahiyatu*. Mwishoni alisujudu kabla ya salamu na akasema:

“Atapotia shaka mmoja wenu katika Swala yake na asijue ameswali rakaa ngapi, tatu au nne? Basi aondoe shaka na ajengee yakini (kweli) ya rakaa alizoswali. Kisha asujudu sijida mbili kabla ya kutoa salamu, sasa kama ataswali tano sijida hizo zitaifanya Swala yake kuwa shufaa si witri. Kama atakuwa ameswali timilifu nne basi sijida hizo zitakuwa ni za kumbabaisha shetani.” (Muslim)

Na ama aliyesahau kitu wakati alikuwa *Maamuma* nyuma ya Imamu basi hatasujudu isipokuwa akisahau Imamu basi atasujudu pamoja naye kwa wajibu wake kumfuata Imamu, na kwa kuwa Swala yake imefungamana na ya Imamu. Na Masahaba wa Mtume ﷺ walisujudu naye aliposahau. (At-Tirmidhi)

Somo la Sita

Jinsi ya Kuswali

Hata kabla ya kuingia wakati wa Swala Muislamu anatakiwa kujiandaa kwa kutawadha na kuvaa kwa kujisitiri vizuri kabla ya kuanza Swala mtu anatakiwa kuelekea kibla na kukimu Swala itapomaliza tamko la *Iqama*, atanyanyua mikono yake sawa na mabega yake hali ya kuwa amenuia Swala anayotaka kuiswali na kusema: الله أكبر, ‘*Allahu Akbar*’.

Na utaweka mkono wako wa kulia juu ya mkono wako wa kushoto kifuani kwako, kisha utasoma dua ya ufunguzi na usome بسم الله, ‘*Bismillah*’ ikifuatiwa na *Al-Hamdu* na ukifika mwisho wake useme, “*Amin*” kisha usome sura kutoka ndani ya *Qur-aan*, kisha unyanyue mikono yako sawa na mabega yako na urukuu hali ukisema: الله أكبر, ‘*Allahu Akbar*’. na unaweka mikono yake magotini na kunyoosha mgongo wako na usinyanyue kichwa chako wala usikiinamishe, isipokuwa ukinyooshe sawa sawa, kisha useme hali yakuwa umerukuu: سبحان ربي العظيم, ‘*Subhaana Rabiyaal-‘Adhiim*’ mara tatu au zaidi ya hapo kisha utanyanyuka kutoka rukuu na kuiweka mikono sawa na mabega

Minhajil Muslim

yako na kusema, *سمع الله لمن حمده*, ‘*Sami’ a Allahu Liman hamidah*’ mpaka ukisha simama wima katika ‘*Itidali*’ useme

ربنا لك الحمد حمدا كثيرا طيبا مباركا فيه.

“*Rabana Lakal-Hamdu Hamdan Kathiran Twayyiban Mubarakan Fih.*”

Kisha utasujudu na useme, *الله أكبر*, ‘*Allahu Akbar*’ na usujudu juu ya viungo saba navyo ni: Uso na viganja viwili vya mikono, magoti mawili na matumbo ya vidole vya miguu, tena uwe amelithibitisha paji lako la uso na pua yako ardhini huku ukisema, *سبحان ربي الأعلى*, “*Sub’hana Rabiya A’ala*” mara tatu au zaidi na kama utaomba dua ya kheri ni vizuri kisha unyanyuke toka sijida na useme, *الله أكبر*, ‘*Allahu Akbar*’ na akae juu ya mguu wake wa kushoto na akiwa amenyoosha mguu wako wa kulia huku ukisema,

رب اغفر لي وارحمني وعافني واهدني وارزقني

“*Rabbigh Firli Warhamnii Wa ‘a-finiy Wah’ dini Warzuqniy*”, kisha utasujudu kama ulivyofanya mwanzo. Kisha utainuka kwa ajili ya rakaa ya pili na ufanye kama ulivyofanya mwanzo katika rakaa ya kwanza. Kisha utakaa *Tahiyatu*.

Kama ni Swala ya rakaa mbili kama vile *al-Fajr* utamswalia Mtume ﷺ yaani utakaa *Tahiyatu* kubwa. Halafu utoe salamu kulia kisha kushoto ukisema:;

السلام عليكم ورحمة الله

‘*Assalam Alaykum Warah’matullahi*’.

Na kama sio Swala ya rakaa mbili basi ukishamaliza *Tahiyatu* ndogo utasimama hali ya kutoa *Takbira* kwa kunyoosha mikono yako usawa wa mabega yake na utimize Swala yako kwa mfano ule ule wa awali. Isipokuwa tu utasoma *Al-Hamdu* tu bila ya sura. Kisha utakaa mkaao wa kukalia tako na kunyoosha mguu wa kulia huku matumbo ya vidole vyako yakiwa ardhini. Halafu utasoma *Tahiyatu* na umswalie Mtume ﷺ na uombe dua ya kujilinda na adhabu ya jahanamu, adhabu ya moto, adhabu ya kaburi, na fitna ya uhai na umauti na fitna ya *Masihi* Dajjal kisha utoe salamu kwa sauti kulia kisha kushoto ukisema: “*Assalam Alaykum Warahmatullahi*”.

Somo la Saba

Hukumu ya Swala ya Jamaa, Uimamu, na Mtu aliyetanguliwa

a) Swala ya Jamaa

1. Hukumu Yake:

Swala ya jamaa ni Sunna iliyowajibu kwa kila muumini ambaye hakuzuiliwa kufika kwenye jamaa na udhuru wowote wa kisheria. Na hiyo ni kutokana na kauli ya Mtume ﷺ:

“Ikitokea wapo watu watatu katika kijiji au kitongoji kimoja haisimamishwi hapo Swala ya jamaa jueni kwamba wamepotezwa na shetani -basi -jilazimisheni kusimamisha jamaa hakika mbwa mwitu humla kondoo aliyejitenga.” (Abu Dawuud na An-Nasai)

Na pia kauli yake Mtume ﷺ:

“Naapa kwa Allah ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake hakika nilitaka kuamrisha ziletwe kuni na ziwashwe, kisha niamrishe Swala iadhiniwe, kisha nimuamrishe mtu awaswalishe watu. Kisha niende katika nyumba za watu ambao hawahudhuria Swala ya jamaa nikaziunguze nyumba zao.” (Al-Bukhari, Muslim, An-Nasai na Imam Malik)

Na kauli yake Mtume ﷺ kwa yule mtu kipofu aliyemueleza,

“Ewe Mtume wa Allah, mimi sina wa kuniongoza kwenda msikitini, Mtume ﷺ akamruhusu na alipoondoka akamwita tena na kumuuliza, je, unasikia adhana? Akasema; ndio, akamjibu, basi itikia wito.”

Na kauli ya Ibni Masoud رضي الله عنه:

“Na tulikuwa tunawahi Swala ya jamaa - isipokuwa mnaḥiki anayefahamika, mtu alikuwa analetwa anachechemezwa kati ya watu wawili, mpaka anasimamiswa kwenye safu.” (Muslim).

Na kauli ya Ibn Masoud رضي الله عنه.

“Wakati wetu watu walikua hawawezi kuacha Swala ya jamaa ila mtu huyo ni mnaḥiki anayejulikana unafiki wake, na ilikuwa mtu analetwa hali ya kuwa amebewa na watu wawili na anawekwa kwenye safu katika hali hiyo.” (Muslim)

2. Ubora Wake.

Ubora wa Swala ya jamaa ni mkubwa, na malipo yake ni makubwa, hakika Mtume ﷺ amesema:

“Swala ya jamaa ni bora kuliko Swala ya mtu peke yake kwa daraja ishirini na saba”. Na akasema: “Swala ya jamaa inazidi juu ya Swala ya mtu nyumbani kwake, na Swala yake sokoni kwake kwa daraja ishirini na tano. Hakika mmoja wenu akitawadha vizuri na akaja msikitini hakukusudia jingine isipokua swala, ila Allah atamnyanyua kwa kila hatua daraja na atamuondoshea kwa kila hatua kosa mpaka aingie msikitini na anapoingia Msikiti atakuwa katika swala muda wakuwa ndiyo Swala inamzuia, na malaika wanamtakia rehemu madamu yupo katika kikao chake anachoswalia. Wakisema:

“Allahuma Ghfir Lahu, Allahumma R-hamhu”, Mwenyezi Mungu msamehe na umrehemu” Madam hajatenguka udhu.” (Al-Bukhari na An-Nasai)

3. Uchache Wake

Uchache wa swala ya jamaa ni watu wawili: Imamu na mtu mwingine pamoja naye, na kila inapozidi idadi ya watu ndio inapendeza zaidi kwa Allah (s.w.t) kutokana na kauli yake Mtume ﷺ.

“Swala ya mtu pamoja na mtu ni bora kuliko Swala yake mmoja peke yake, na Swala ya mtu pamoja na watu wawili ni bora kuliko swala yake na mtu mmoja, na wanapokuwa wengi zaidi basi ndio inapendeza zaidi kwa Allah (s.w.).” (Ahmad na Baihaqi).

Ni bora Swala ya jamaa ikaswaliwa msikitini. Na Msikiti ulio mbali ni bora kuliko wa karibu kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Hakika watu wenye ujira mkubwa zaidi katika Swala ni wale wanaotembea mbali zaidi.” (Muslim).

4. Wanawake Kuhudhuria Jamaa

Wanaruhusiwa wanawake kuhudhuria jamaa Misikitini kama hakuna fitna na maudhi, kwa kauli yake Mtume ﷺ: *“Msiwazuie wajakazi wa Allah - wanawake – kwenda katika misikiti ya Allah.”*, lakini Swala ya mwanamke nyumbani kwake ni bora zaidi kwake. Kwa kauli yake Mtume ﷺ: *“Na watoke bila kujipamba.”*

Na kauli yake Mtume ﷺ: *“Mwanamke yeyote aliyejifukiza manukato asiswali nasi Swala ya Isha.”*

5. Kutoka na Kwenda Kwenye Jamaa

Ni suna kwa anayetoka nyumbani kwake kuelekea msikitini kutanguliza mguu wake wa kuume na kusema:

((بِسْمِ اللَّهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ أَنْ
أُضِلَّ أَوْ أُضَلَّ، أَوْ أَزَلَّ أَوْ أُزَلَ، أَوْ أَظْلَمَ أَوْ أُظْلَمَ، أَوْ أَجْهَلَ أَوْ يُجْهَلَ عَلَيَّ،
اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِحَقِّ السَّائِلِينَ عَلَيْكَ وَبِحَقِّ مَمْشَايَ هَذَا، فَإِنِّي لَمْ أَخْرَجْ
أَشْرًا وَلَا بَطْرًا، وَلَا رِيَاءَ وَلَا سَمْعَةَ، خَرَجْتَ اتِّقَاءَ سَخَطِكَ وَابْتِغَاءَ مَرْضَاتِكَ،
أَسْأَلُكَ أَنْ تَنْقِذَنِي مِنَ النَّارِ، وَأَنْ تَغْفِرَ لِي ذُنُوبِي جَمِيعًا، فَإِنَّهُ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ
إِلَّا أَنْتَ. اللَّهُمَّ اجْعَلْ فِي قَلْبِي نُورًا، وَفِي لِسَانِي نُورًا، وَفِي سَمْعِي نُورًا،
وَفِي بَصَرِي نُورًا، وَعَنْ يَمِينِ نُورًا، وَعَنْ شِمَالِي نُورًا، وَمَنْ فَوْقِي نُورًا،
اللَّهُمَّ أَعْظِمْ فِي نُورِ))

“Bismillahi Tawakkaltu ‘Ala Llah Wala Haula Wala Quwwata Illa Billah, Allahuma Inniy Audhubika An Adhwilla Au Udhwallu, Au Azilla au Uzallu, au Adhlima au Adhlama Au Aj Hala Au Yuj’hala ‘Alayya, Allahuma Inni As’aluka Bihaqqi Ssailina ‘Alayka Wabihaq Mamshaya Hadha, Fainni Lam Akhruji Asharan Wala Batwaran, Wala Riya’an Wala Sam’ah, Kharajtu Ittiqa-a Sakhatwika, Waibtigha-a Mardhwa-tika, As’aluka An Tunqidhaniy mina nnar, waan Taghfirliy Dhunubii Jamiy’an, Fainnahu La- Yaghfiru Dhunuwba Illa Anta. Allahumma j’al Fy Qalby Nuran. Wafi Lisaniy Nuran, Wafi Sam’iy Nuran, Wafiy Baswariy Nuran, Wa ‘An Yamiyni Nuran Wa ‘An Shima-liy Nuran, Wamin Fauqiy Nuran, Allahumma A’udhim Fiyya Nuran.”
(Al-Bukhari na Muslim)

“Kwa jina la Allah nimetawakali kwa Allah, hakuna hila wala nguvu isipokuwa kwa Allah, Ewe Mola mimi najilinda kwako kupotea au kupoteza, au kuteleza au kutelezeshwa, au kudhulumu au kudhulumiwa, au kufanya ujinga au kufanyiwa ujinga, Ewe Mola wangu Nakuomba kwa haki ya wenye kukuomba, na kwa haki ya mwendo wangu huu, mimi sikutoka kwa shari wala kwa kiburi, wala kujionesha au kusikika, Nimetoka na kuogopa hasira zako na kutaka radhi zako, Nakuomba uniokea na moto na uniondoshee madhambi yangu yote, Kwa hakika hasamehi madhambi isipokuwa wewe. Ewe Mola wangu, Ijaalie moyo wangu nuru. Nakatika masikio yangu nuru, na katika macho yangu nuru, na kuume kwangu nuru, na kushotoni kwangu nuru, na juu yangu nuru. Ewe Mola wangu itikuze nuru kwangu.”

Kisha atakwenda kwa utulivu kwa kauli yake Mtume ﷺ: *“Mtakapokuja kuswali ni wajibu kuja kwa utulivu, kile mtachodiriki swalini, na kilichokupiteni timizeni.”*

Mtu anapofika Msikitini anatakiwa kutanguliza mguu wake wa kuume wakati wakuingia na aseme:

((بِسْمِ اللَّهِ، أَعُوذُ بِاللَّهِ الْعَظِيمِ، وَبِوَجْهِهِ الْكَرِيمِ وَسُلْطَانِهِ الْقَدِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ، اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى نَبِيِّنَا مُحَمَّدٍ وَآلِهِ وَسَلَّمَ، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذُنُوبِي، وافتح لي أبواب رحمتك))

“Bismillahi, ‘Audhu Billahil-‘Adhim, Wabiwajjihil-Kariyima Wasulta-nihil Qadiym Minal Shaitwanil-Rajim, Allahumma Swalli ‘Ala Nabiyyina- Muhammadin Wa A-lihi Wasallam. Allahumma Ghfir-Liy-Dhunuwbi. Waf’tah Liy Abwaa-ba Rahma-tika.”
(Ahmad na Ibn Majah)

Na asikae mpaka baada ya kuswali *Tahiyatul-Masjid* kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakapoingia mmoja wenu msikitini asikae mpaka aswali rakaa mbili.” (Muslim)

Isipokuwa kama ni wakati wa kuchomoza jua au kuzama kwake, hapo akae na asiswali, kutokana na katazo la Mtume ﷺ kuswali katika nyakati mbili hizi.

Mtu anapotaka kutoka msikitini akatanguliza mguu wake wa kushoto, na aombe dua kama wakati alipokuwa anaingia msikitini isipokuwa atakapofika “wafilah *أبواب فضلك*, “*Waftah Liy Abwa-ba Fadhlika, badala ya وافتح لي أبواب رحمتك*, “*Waftah Liy Abwa-ba Rahmatika.*”

b) Sharti za Mtu kuwa Imamu

1. Sharti za Imamu:

Ni sharti kwa Imamu kuwa mwanamume, muadilifu, aliye mjuzi wa masuala ya ibada Mwanamke hawezi kuwa imamu wa wanamume na hauswihi Uimamu wa mtu *fasiki* (mvunja sheria) ambaye ufuska wake unafahamika. Mtu aliye na nguvu za utawala anaweza kuwa Imamu kwa kule kuhofiwa kwake na watu; Mtu mjinga hawezi kuwa Imamu labda kwa watu wanaefanana naye.

Kwa kauli ya Mtume ﷺ. “*Mwanamke au fasiki asiwe imamu kwa muumini mwanamume labda kwa kutenzwa nguvu na Sultan (utawala) au kwa kudhuriwa.*”. Isipokuwa inakubali hadithi hii kufanyiwa kazi.

Na hadithi zote zilizopokelewa kuhusu Uimamu wa mwanamke ni kuhusu kuwaswalisha watu wa nyumbani kwake, wanawake na watoto na Hadithi zilizopokelewa kuhusu Uimamu wa fasiki ni katika hali za dharura.

2. Aliye na Haki Zaidi ya Uimamu:

Mwenye haki zaidi ya kuwa imamu ni yule aliyehifadhi (anayesoma) zaidi Qur-aan, kisha ni yule mjuzi zaidi wa sheria. Kisha aliye mchamungu zaidi kisha aliye mkubwa kwa umri kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Msomaji mzuri zaidi wa Qur-aan ndio ewe Imamu wa watu na kama akiwepo mtu wanaelingana katika usomaji wao basi aliye mjuzi zaidi Imamu katika Sunna (mafundisho ya Mtume) ndio awe imamu na kama wakilingana katika Sunna basi yule aliyetangulia kuhama (Hijra) na wakilingana katika kuhama basi awe mkubwa wao katika umri.” (Abu Dawuud na At-Tirmidhi na Imam Ahmad)

Na hayo yote yanafanywa ikiwa katika watu hao hayupo kiongozi au mwenye nyumba kwa vile, huyo ndiye anayekuwa na haki zaidi kuliko mwingine katika Uimamu, hayo ni kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Mtu (mgeni) asiwe Imamu wa mtu aliye katika familia yake au utawala wake isipokuwa kwa idhini yake...” (Ameipokea Jumla hii pamoja na hadithi iliyotangulia Said Ibn Mansur رضي الله عنه)

3. Uimamu wa Mtoto Mdogo

Mtoto mdogo anaweza kuwa Imam katika Swala za Sunna sio za faradhi. Kwani haijuzu kwa anayeswali faradhi kuswali nyuma ya anayeswali sunna. Ama Swala ya mtoto ni sunna hivyo haisihi kuwa Imamu katika faradhi kutokana na kauli ya Mtume ﷺ: *“Msikhitilafiane na Uimamu wenu.”*

Na moja ya kukhitilafiana ni kuswali Swala ya faradhi nyuma ya mwenye kuswali sunna. Na Imamu Shafii ametofautiana na Jamhuri ya wanazuoni katika haya mas’ala kwani amesema:

“Unajuzu Uimamu wa mtoto katika Swala ya faradhi kwa ushahidi wa Hadithi ya ‘Amr bin Salama na imeelezwa katika hadithi hiyo kuwa Mtume ﷺ aliwaeleza jamaa zake (‘Amr) kuwa: “Awe Imamu wenu anayesoma uzuri zaidi Qur-aan akasema (‘Amr) nilikuwa nikiwaswalisha nami ni mtoto wa miaka saba.” (Abu Dawuud).

Lakini Jamhuri wamesema kuwa hadithi hii ni dhaifu na wakasema hata tukichukulia kuwa ni sahihi inawezekana kuwa Mtume ﷺ hakufahamu kuwa huyu ‘Amr bin Salama ndiye aliyekuwa Imamu wao kwani watu hao walikuwa nje ya mji mbali kidogo na Madina.

4. Uimamu wa Mwanamke

Mwanamke anaruhusiwa kuwa Imamu na kuwasilisha wanawake wenzake, na kwa kusimama katikati yao, kwani Mtume ﷺ alitoa ruhusa kwa Ummu Waraqa bin Nawfal kumuwekea muadhini nyumbani kwake ili (Ummu Waraqa) awaswalishe watu wa nyumbani kwake. (Abu Dawuud)

5. Uimamu wa Kipofu

Unasihi uimamu wa kipofu anaweza kuwa imamu wa watu, kwani Mtume ﷺ alimuweka Ibn Ummu Maktoum kuwa Khalifa Madina mara mbili na alikuwa akiwaswalisha watu hali ya kuwa ni kipofu رضي الله عنه. (Abu Dawuud)

6. Uimamu wa ‘Maf’dhuli’

Mtu aliye na hadhi ya chini anaweza kuwa Imamu wa watu hata kama aliye na hadhi ya juu yupo, kwani Mtume ﷺ alipata kuswali nyuma ya Abu Bakr رضي الله عنه pia aliwahi kuswali nyuma ya ‘Abdur-Rahman bin ‘Awf رضي الله عنه hali ya kuwa yeye Mtume ﷺ ni Mbora kuliko hao pamoja viumbe wengine wote. (Haythamy)

7. Uimamu wa Aliye Tayyammamu

Anaweza kuwa imamu. kwa aliyetawadha kwani ‘Amr bin A’as رضي الله عنه alipata kuwa Imamu wa kundi la jeshi alilokuwa nalo hali ya kuwa yeye alitayamamu aliokuwa nao wakiwa wametawadha na habari hizo zilimfika Mtume ﷺ na hakukanusha. (Abu Dawuud)

8. Uimamu wa Msafiri

Msafiri anaweza kumswalisha mtu aliye mkazi, isipokuwa ni wajibu wa huyu mkazi kutimiza swala yake baada ya msafiri kutoa salam kwani Mtume ﷺ aliwahi kuwaswalisha watu wa Makka hali ya kuwa yeye ni msafiri na akawaambia:

“Enyi watu wa Makka timiizeni Swala yenu kwani sisi ni wasafiri.”
(At-Tabarani, na Bayhaqi).

Na kama msafiri ataswali nyuma ya mkazi basi ataswali kamili kama yule mkazi. Kwani Ibn ‘Abbas رضي الله عنه aliulizwa hukumu ya kutimiliza Swala kwa msafiri aliyeswali nyuma ya mkazi akasema: *“Hiyo ndio sunna ya Abul-Qasimu (Mtume عليه السلام)”*

9. Jinsi Maamuma anavyoweza kusimama na *Imamu*:

Imamu anapokuwa mwanamume akimswalisha mwanamume mwengine basi yule maamuma atasimama karibu naye upande wa kulia, na ni hivyo hivyo kwa mwanamke kwa mwanamke mwenzie.

Na atakayewaswalisha watu wawili na zaidi basi watasimama nyuma yake. Na endapo watakusanyika wanamume na wanawake, basi watasimama wanaume nyuma ya *Imamu* na watasimama wanawake nyuma ya wale wanaume, na kama maamuma ni mwanamume na mwanamke basi huyu mwanamume hata kama ni mtoto mwenye akili timamu atasimama pembeni ya *Imamu* na yule mwanamke atasimama nyuma yao.

Na hiyo ni kwa kauli ya Mtume عليه السلام kuwa:

“Safu bora ya wanaume ni ile ya mbele na safu yenye shari ni ile ya mwisho na bora ya safu za wanawake ni ile ya mwisho na safu yenye shari ni ile ya mwanzo.” (Muslim)

Pia kwa ushahidi wa kitendo cha Mtume عليه السلام

“Alisimama mara moja katika vita akiswali. Akaja Jabir رضي الله عنه akasimama kushotoni kwake, hapo Mtume عليه السلام alimzungusha mpaka akamsimamisha kuliani kwake, kisha akaja Jabbar bin Swakhi رضي الله عنه akasimama kushotoni kwake, hapo aliwachukuwa kwa mikono yake na akawasimamisha nyuma yake.”

Pia kwa kauli ya Anas رضي الله عنه kwamba Mtume عليه السلام alimswalisha yeye na mama yake,

“Alimsimamisha kuliani kwake na akamsimamisha mama yake nyuma yao.” (Muslim) na kuna kauli ya Anas رضي الله عنه akisema: *“Nilipanga safu mimi na yatima mmoja nyuma ya Mtume ﷺ na mwanamke kikongwe alisafu nyuma yetu.”* (Al-Bukhari)

10. Sutra ya Imamu ni Kizuizi Cha Aliye Nyuma Yake.

Atakaposwali Imamu na akaweka kizuizi mbele yake hatahitaji maamuma kizuizi kingine. Kwani palikuwa panasimikwa kijimkuki kidogo (*Hirba*) kama *sutra* kwa ajili ya Mtume ﷺ na akiswali kuelekea pale na hakuamrisha yeyote aliye nyuma yake kuweka kizuizi kingine. (Al-Bukhari na Muslim)

11. Wajibu wa Kumfuata Imamu

Ni wajibu kwa maamuma kumfuata Imamu wake, na ni haramu kumtangulia, na ni karaha kwenda naye sawasawa. Endapo (maamuma) atamtangulia Imamu kwenye *Takbiratil-Ihram* (Takbira ya mwanzo) basi ni wajibu arudie. Asipofanya hivyo Swala yake ni batili, na inabatilika Swala yake pia kama atatoa salamu kabla ya Imamu na kama atamtangulia katika rukuu au sijida au katika kunyanyuka kutoka katika sehemu hizi ni wajibu arejee na arukuu au asujudu baada ya Imamu wake. Na yote hayo ni kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika amewekwa Imamu ili afuatwe, basi msikhitilafiane: na atapotoa Takbira na nyinyi toeni Takbira na ataporukuu nanyi fanyeni rukuu na ataposema: “Samia Allahu Liman Hamidah”, nanyi semeni, “Allahuma Rabbana Walakal-Hamdu.” (At-Tirmidhi, Imam Ahmad na An-Nisai).

“Na atakaposujudu nanyi sujudini, na ataposwali hali amekaa nanyi nyote swalini mkiwa mmekaa.” (Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi).

Na kauli yake Mtume ﷺ, *“Je?*

Haogopi mmoja wenu ataponyanyua kichwa chake kabla ya Imamu, kikageuzwa kichwa hicho kuwa cha punda au akaigeuza sura yake ikawa kama ya punda?” (Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi).

12. Maamuma Kushika Nafasi ya Imamu kwa Udhuru

Kama kutatokea udhuru na haja ya Imamu kutoendelea na Swala basi inajuzu kwake kumuweka badala yake mmoja wa waliokuwa nyuma yake miongoni mwa maamuma atayekamilisha Swala yao naye ataondoka.

‘Umar bin Khattab رضي الله عنه alimuachia Uimamu ‘Abdul Rahman bin ‘Awf wakati alipochomwa kisu akiwa ndani ya Swala (Al-Bukhari). Ali bin Abi Twallib رضي الله عنه alimwachia Uimamu mmoja wa maamuma kutokana kutokwa damu puani katika maradhi yaliyokuwa yamemsibu.

13. Kufupisha Swala:

Ni Suna kwa Imamu kutorefusha Swala isipokuwa katika kisomo cha rakaa ya mwanzo kwa lengo la kutoa nafasi kwa watu kuidiriki rakaa ile. Kwani Mtume ﷺ alikuwa anairefusha na hivyo ni kutokana na kauli yake Mtume ﷺ.

“Ataposwali mmoja wenu akiwa Imamu wa watu na afupishe Swala kwani katika wanaomfuata wamo dhaiifu, wagonjwa, na wazee na ataposwali peke yake na arefushe atakavyo.” (An-Nasai, na Imam Ahmad).

14. Karaha ya Imamu anayechukiwa na Watu:

Ni karaha kwa mtu kuwa Imamu wa watu hali ya kuwa watu wanamchukia hasa, ikiwa chuki yao kwake ni kwa sababu za kidini (sheria) kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Watu watatu Swala zao hazipandishwi zaidi ya vichwa vyao kiasi cha shubiri, wa kwanza ni mtu anayekuwa Imamu wa watu hali ya kuwa wanamchukia; na mwanamke aliyelala uliyempitia usiku hali ya kuwa mumewe ameghadhibika naye, na ndugu wawili wanaogombana.” (Ibni Majah)

15. Anayemfuatia Imamu, na Kugeuka Imamu Baada ya Salamu:

Ni Sunna kwa mwenye elimu kusimama wamfuata, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Wanifuata nyuma yangu wenye elimu na utambuzi.” Na imesuniwa kuwa Imamu atakapotoa salamu ageukie (Maamuma) kwa upande wa kulia, na awaelekee watu kwa uso wake. Kutokana na kitendo cha Mtume ﷺ. Amepokea Abu Dawuud na At-Tirmidhi amesema: “Alikuwa Mtume ﷺ akituswalisha na anaondoka katika pande zake zote kuliani kwake na kushotoni.”

16. Kunyoosha safu wakati wa Swala

Ni Sunna kwa Imamu na maamuma kuweka sawa safu zao na kuzinyoosha mpaka Zinyooke. Kwani Mtume ﷺ alikuwa anawaelekea watu na akawaelekeza:

“Jipangeni na kaeni sawa sawa.” (Imam Ahmad) Na akawaelekeza pia, “Wekeni sawa safu zenu kwani katika kuweka safu sawa ndio ukamilifu wa Swala.” (Al-Bukhari, Muslim na Abu Dawuud)

Na pia alikuwa anawaelekeza:

“Wallahi mtaziweka sawa safu zenu au Allah (s.w.) atatofautisha nyuso zenu.” (Ahmad). Aliwahi kusema: “Hakuna hatua yenye malipo bora zaidi kuliko hatua ya mtu aliyoundea uwazi iliopo katika safu akaziba.” (Imetajwa na Az-Zubaid na al-Munziriy katika Targhib na Tarhiib).

c) Aliyetanguliwa na Imamu

1. Mtu atakapoingia msikitini kwa nia ya kuswali na akakuta Swala inaendelea ni wajibu wake kuingia haraka na kumfuata Imamu katika hali yoyote atakayomkuta, anarukuu au anasujudu au ana mkao au ana simama. Hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Atakapofika mmoja wenu kwenye Swala na Imamu yupo katika hali aliyonayo ndani ya Swala na afanye kama anavyofanya Imamu.” (At-Tirmidhi),

(Katika *Sanad* yake kuna udhaifu, lakini Jamhuri ya wanazuoni wamekubaliana hivyo kutokana na hadithi zingine kuitia nguvu hadithi hiyo).

2. Kukamilika Rakaa kwa Kudiriki Rukuu

Rakaa inatimia kwa Maamuma pale atakapomuwahi Imamu akiwa bado yupo katika rukuu na akawa naye katika rukuu kabla ya Imamu kunyanyuka, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Mtapofika kwenye Swala nasi tukawa tumesujudu nanyi sujuduni lakini msihesabu chochote na atayediriki rukuu basi atakuwa ameipata rakaa.” (Ameitaja hadithi hii Albaani katika Irwaa al-‘Ghaliil)

3. Kukamilisha Swala baada ya Salam ya Imam:

Imam atakapotoa salamu maamuma aliyechelewa atasimama ili kutekeleza kile kilichompita katika Swala yake na atakifanya kilichompita ndio mwisho wa swala yake. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Mlichokidiriki swalini na kilichokupiteni basi timizeni.” (Imam Ahmad).

Mfano: Kama amediriki rakaa ya Maghribi atasimama na ataleta mbili ya kwanza kwa kusoma *Suratul Fatiha* na sura nyingine na rakaa ya pili atasoma *al-Fatiha* basi. Kisha atakaa *Tahiyattul* na kutoa salamu. (Imam Ahmad)

Na akitaka itajaalia kuwa kilichompita ni mwanzo wa Swala yake kwa kauli ya Mtume ﷺ katika riwaya (mapokezi mengine:

“Na kilichokupiteni tekelezeni.” (Imam Ahmad)

Na kwa msingi huo kama mtu atapitwa rakaa katika Swala ya Magharibi atasimama na ataswali rakaa kwa kusoma *al-Fatiha* na sura kwa sauti kama ilivyompita, kisha atakaa *Tahiyattu* na kutoa salamu.

Baadhi ya wanazuoni wanaohibitika hukumu kwa dalili wameona kuwa rakaa zinazompita mtu zijaaliwe kuwa ni za mwanzo wa Swala yake, rai hii ndiyo yenye nguvu.

4. Kisomo cha Maamuma Nyuma ya Imamu

Si wajibu kwa *Maamuma* kusoma kama ni katika swala ya sauti, isipokuwa ni *sunna* kwake anyamaze. Kwani kisomo cha *Imamu kinawakilisha*, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Yule anayeswalishwa basi kisomo cha Imamu ndio kisomo chake.” (Imam Ahmad na Ibn Majah)

Na kauli yake Mtume ﷺ: *“Kwanini ninagombaniwa Qur-aan?”* Hapo watu walikoma kusoma katika swala aliyokuwa akiswalisha Mtume ﷺ. Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika amejaaliwa Imamu ili afuatwe, atapotoa takbira nanyi toweni takbira na ataposoma nyamazeni (kaeni kimya).” (At-Tirmidhi na Imam Ahmad)

Isipokuwa ni *sunna* kusoma katika Swala ambazo *Imamu* hasomi kwa sauti. Ni *sunna* iliyotiliwa mkazo kusoma *Suratul Fatiha* katika vinyamazo vya *Imamu*.

5. Haijuzu Kuswali Swala ya *Sunna* baada ya kukimiwa Swala ya *Faradhi*.

Haijuzu kuanza Swala ya *sunna* pale itakaposimamishwa Swala ya *faradhi*. Endapo itakimiwa *faradhi* hali ya kuwa mtu yumo ndani ya *sunna* ataikata kama bado rakaa haijahesabika kwa kuinuka kutoka kwenye rukuu. Kama alishapata rakaa basi ataikamilisha Swala yake kwa haraka, kwa kauli yake ﷺ,

“Itaposimamishwa Swala ya faradhi hairuhusiwi kuswali isipokuwa faradhi.” (Muslim)

6. Swala ya Alasiri kabla ya Adhuhuri.

Wamekhitafiana wanazuoni katika hukumu ya mtu ambaye hajaswali Swala *adhuhuri* hali ya kuwa imeshakimiwa Swala ya Alasiri je ataingia na *Imamu* kwa nia ya kuswali *Adhuhuri*, na *Imamu* atakapotoa salamu afanyeje? atasimama na kuswali Al'asr? Au atanuia Alasiri, na atakapomaliza atasimama na kuswali *Adhuhuri* na Alasiri pamoja kwa ajili ya kuzingatia mpangilio”?

Kama si kuwepo kauli yake Mtume ﷺ: *“Msikhitalafiane na Imamu.”* Basi ingekuwa kuingia na *Imamu* kwa nia ya *Adhuhuri* ni bora. Hivyo kwa kutoa

shaka ni bora aingie na Imamu kwa nia ya Alasiri, na akishatoa salamu atasimama na kuswali Adhuhuri kisha Alasiri na ile swala yake ya alasiri na Imamu inakuwa ni sunna kwake.

7. Kusimama Nyuma ya Safu peke yako

Haijuzu kwa Maamuma kusimama nyuma ya safu peke yake. Kama atasimama nyuma peke yake kwa makusudi basi hana Swala mtu huyo. Kwa kauli yake Mtume ﷺ kumueleza mtu aliyesimama nyuma ya safu peke yake:

“Isaliti swala yako hakuna swala kwa mtu aliye pekee nyuma ya safu.” (Imam Ahmad).

Na kama atasimama kuliani kwa Imamu hakuna ubaya.

8. Safu ya Mwanzo ni Bora

Nu sunna kwa mtu kujitahidi kuwa katika safu ya mwanzo tena upande wa kulia kwa Imamu. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika Allah ni mwenye uwezo wote na malaika wake wanawatakia rehema watu wa safu ya kwanza. Wakasema masahaba “Ee Mtume wa Allah na safu ya pili je? Na mara ya tatu, akasema na ya pili.” (Imam Ahmad na Tabarani)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Safu iliyo bora kwa wanaume ni ile ya mwanzo na iliyo na shari ni ile ya mwisho, na bora ya safu ya wanawake ni ile ya mwisho na iliyo na shari kwao ni ile ya mwanzo.” (Muslim). Na kauli yake: *“Hakika ya Allah na malaika wake wanawarehemu wale wanaoswali safu za kuliani.”* (Abu Dawuud).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Tangulieni mnifuate mimi na wawafuateni walio nyuma yenu na wanaojichelewesha kwenye safu Allah atawachelewesha.” (Muslim)

Somo la Nane

Adhana na Iqama

a) *Adhana:*

1. **Maana yake:**

Ni tangazo linalojulisha kuingia kwa wakati wa Swala kwa matamshi maalum.

2. **Hukumu yake:**

Adhana ni wajibu wa *kutosheleza ulio juu* ya watu wa mji au kijiji kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Utapofika wakati wa Swala basi mmoja wenu atoe adhana, na mkubwa wenu awaswalishe .” (Al-Bukhari na Muslim)

Na ni Sunna kwa msafiri na mkazi pia, kwa kauli yake Mtume ﷺ. *“Utakapokuwa machungoni au katika kijiji chako na mkakusudia kuadhini kwa ajili ya Swala basi nyanyua sauti yako kwa mnada, kwani hawezi kusikia upeo wa sauti ya muadhini jini wala binadamu wala kitu chochote ila atakuwa shahidi siku ya kياما.” (Rabiigh bin Hubeib katika Musnad yake)*

3. **Matamshi yake:**

Matamshi ya adhana kama alivyofundisha Mtume ﷺ kumfundisha Abu Mahdhura kama ifuatavyo:

Allahu Akbar, Allahu Akbar, الله أكبر الله أكبر

Allahu Akbar, Allahu Akbar, الله أكبر الله أكبر

Ash'hadu An-La Ilaha Illa Llah , أشهد أن لا إله إلا الله

Ash'hadu An-La Ilaha Illa Llah , أشهد أن لا إله إلا الله

Minhajil Muslim

Ash'hadu Anna Muhammada Rasulallah, أشهد أن محمدًا رسول الله

Ash'hadu Anna Muhammada Rasulallah, أشهد أن محمدًا رسول الله

Hayya 'Ala Sswalaat , حيّ على الصلّاة

Hayya 'Ala Sswalaat , حيّ على الصلّاة

Hayya 'Alal-Falah , حيّ على الفلاح

Hayya 'Alal-Falah , حيّ على الفلاح

(Kama ni adhana ya Al-fajiri atasema baada ya *Hayya 'Alal-Falah* maneno yafuatayo:

Asswalatu Khairu Minan-Nnawm, الصلّاة خير من النوم

Asswalatu Khairu Minan-Nnawm, الصلّاة خير من النوم

Kisha atamalizia sehemu iliyobakia.

Allahu Akbar, Allahu Akbar, الله أكبر الله أكبر

Lailaha Illa Llahu, لا إله إلا الله

Abu Mahdhura amesema: Mtume ﷺ amenifundisha adhana, “*Allahu Akbari* mara nne (4), *Ashhadu an lailaha illa Allah* mara mbili (2). *Ashhadu anna Muhammada Rasulu Allah* mara mbili (2). Kisha anarudi anasema: *Ashhadu an lailaha illa Allah*, mara mbili (2). *Hayya 'ala Sswalaa* mara mbili(2), *Haya 'alal Falaah* mara mbili (2), ikiwa swala ya asubuhi niseme: “*Asswala-tu Khairum Mina Nnaumi* mara mbili (2), *Allahu Akbar* mara mbili (2). *La- ilaha illa Allah* mara moja.” (At-Tirmidhi)

4. Sifa za Muadhini.

Ni vizuri muadhini awe ni mtu muaminifu, mwenye sauti nzuri inayosikika, mjuzi wa nyakati za Swala. Ni vema muadhini kusoma adhana akiwa sehemu iliyoinuliwa

juu, wakati wa kuadhini awe ameingiza vidole katika masikio yake mawili na ageuke kwanza kulia na kisha kushoto anapofika “*Haya ala tusswalat na Hayya atul swalat*” Muadhini hatakiwi kuchukua ujira kutoka katika chanzo kingine cha fedha isipokuwa *Baitul-Mal* (Hazina ya Dola) au mali ya *waqfu*.

b) Kukimu Swala, (*Iqama*)

1. Hukumu yake

Iqama ni sunna iliyotiliwa mkazo katika kila Swala ya faradhi katika Swala zote tano, ni sawa na Swala katika wakati wake au katika wakati uliopita wakati wa kawaida. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Ukiona watu wanaofikia watatu katika kijiji au kitongoji halafu haisimamishwi Swala elewa kuwa wamepumbazwa na shetani. Jilazimisheni na Swala ya jamaa, kwani mbwa mwitu humla kondoo aliyejitenga.”

Na kwa kauli ya Anas رضي الله عنه:

“Aliamriwa Bilal asome adhana mara mbili mbili na asome Iqama mara moja moja.” (Muslim)

2. Tamko lake

Ni kama ilivyoelezwa katika Hadithi ya Abdillahi bin Zayd رضي الله عنه ambaye alioteshwa adhana katika ndoto ni:

Allahu Akbari, Allahu Akbari , الله أكبر الله أكبر

Ashhadu An La-ilaha Illa Llah, أشهد أن لا إله إلا الله

Ashhadu Anna Muhammada Rasulallah, أشهد أن محمدًا رسول الله

Hayya ‘Ala Sswalat, حيّ على الصلّاة

Hayya ‘Alal-Falah, حيّ على الفلاح

Qad Qa-matis-Swalat, قد قامت الصلاة

Qad Qa-matis-Swalat, قد قامت الصلاة

Allahu Akbar, Allahu Akbar , الله أكبر الله أكبر

Lailaha Illa Llah, لا إله إلا الله

Ufafanuzi:

Imamu ndiye anayemiliki *Iqama*, muadhini haruhusiwi kukimu Swala bila idhini ya Imamu na kwa habari iliyopokelewa: “*Muadhini ndiye anayemiliki zaidi adhana na Imamu ndiye anayemiliki zaidi Iqama.*” Katika sanadi kuna mtu Maj’huli (asiyejulikana) lakini wanazuoni wote wanaifanyia kazi bila hadithi hii.

Adhana inamilikiwa na muadhini kuliko imamu kwa hiyo ataadhini baada ya kuingia muda wala hawajibiki kupata idhini toka kwa Imamu au mtu mwingine yeyote.

Ni Sunna:

1. Utulivu wakati wa kuadhini ni jambo la msingi na wakati wa kukimu, *Iqama* isomwe haraka haraka. Hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ kumueleza Bilal رضي الله عنه.

“*Utakapokuwa ukisoma adhana soma kwa utulivu polepole na utakapokimu kimu haraka haraka.*” (At-Tirmidhi na al Hakim)

2. Kufuatisha *adhana* na *Iqama* kwa sauti ya chini inaposomwa, na asome yule anayesikia *adhana* kama anavyosoma muadhini au anayeqimu.

Isipokuwa katika tamko la ‘*Hayya ‘Ala-Sswalat*’ na ‘*Hayya ‘Alal Falah*’ aseme:

‘*La-haula Wala Quwwata Illa Billah.*’ لا حول ولا قوة إلا بالله”

‘*Qad Qa-mati Sswala-t*’ قد قامت الصلاة

hapo atasema, أقامها الله وأدامها, ‘*Aqa-maha Llahu Wa Ada-maha.*’

Hayo ni kwa aliyoyapokea Abu Dawuud kuwa Bila رضي الله عنه alikuwa akiqimu, na alipofika, ‘*Qad Qaamatis-Swalaat*’ Mtume عليه السلام alisema: ‘*Aqaamah Allaahu wa Adaamaha*’. Na amepokea Imamu Muslim kuwa amesema Mtume عليه السلام:

قال صلى الله عليه وسلم: (إذا سمعتم المؤذن فقولوا مثل ما يقول المؤذن ، ثم صلوا علي ، فإنه من صلى علي مرة صلى الله عليه بها عشرا ، ثم سلوا الله لي الوسيلة فإنها منزلة في الجنة لا ينبغي أن تكون إلا لعبد من عباد الله ، وأرجو أن أكون أنا هو ، فمن سأل الله لي الوسيلة حلت له شفاعتي)

“Mtakapomsikia muadhini basi someni kama anavyosoma muadhini kisha nitakieni rehema, kwani anayenitakia rehema mara moja Allah atamrehemu mara kumi, kisha nitakeni kwa Allah wasila kwani hiyo ambayo daraja katika pepo haipati isipokuwa mja mwema, na ninatarajia niwe mimi, yule atakayeniomba wasila atafikiwa na shufaa yangu.” (Muslim)

3. Dua baada ya Adhana.

Kama alivyoipokea At-Tirmidhi na akaipa daraja ya al-Hasan kuwa Mtume عليه السلام amesema: “*Dua inayoombwa kati ya Adhana na Iqama hairudi patupu.*” Na imekuja kauli wakati wa Adhana ya Magharibi,

اللهم هذا إقبال ليلك وإدبار نهارك، وأصوات دعائك فاغفر لي

“Allahuma Hadha Iqba-lu Laylika Wa Idba-ru Naha-rika, Waaswa-tu Dua-tika Fagh-Fir Liy.”

“Ewe Mola wangu huu ni ujio wa usiku wako, na kuondoka mchana wako, na sauti za walinganiaji wako, Ewe Mola wangu nisamehe.”

Somo la Tisa

Kupunguza Swala Kukusanya, ya Mgonjwa na Swala ya Khofu

a) Kupunguza “Qasr”

1. Maana yake:

“Qasr” ni kupunguza Swala yenye rakaa nne na kuswali rakaa mbili kwa kusoma *Al-Hamdu* na sura. Ama Swala ya Magharibi na ya Al-fajiri hazipunguzwi kwani Magharibi ina rakaa tatu na Al-fajiri ina rakaa mbili.

2. Hukumu yake:

Qasr imethibitishwa kisheria: Kwa kauli ya Allah Aliyetukuka.

وَإِذَا ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ

“...Na mnapo safiri katika nchi si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala...” (Nisai 4:101)

Na kauli yake Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu Swala hiyo akasema.

“Ni sadaka aliyokuleteeni Allah. Basi ipokeeni sadaka yake.”
(Muslim, Abu Dawuud, At-Tirmidhi na Ibn Majah)

Na Mtume kudumu katika swala hii kunaifanya iwe sunna iliyotiliwa mkazo. Katika safari zake zote Mtume ﷺ alipunguza Swala zake na masahaba walipunguza pia pamoja naye.

3. Umbali Ambao ni Sunna kupunguza Swala:

Mtume ﷺ hakuweka kiwango cha umbali unaosafiriwa ili mtu apunguze Swala. Lakini mkusanyiko wa masahaba na Taabiina na Maimamu waliangalia umbali ambao Mtume ﷺ alikuwa akipunguza Swala wakakuta ni karibu ya “*Burdi* nne”

na **Burdi** nne ni sawa na maili arobaini na nane (48) wakazifanya ni kiwango cha chini cha umbali wa kupunguza Swala basi atayesafiri umbali huo katika safari ambayo si ya kumuasi Allah ni sunna kwake kupunguza Swala zake. Kwa hiyo ataswali Swala za raka'a nne nne yaani: Adhuhuri, Alasiri, na Isha raka'a mbili mbili.

4. Mwanzo wa Kupunguza na Mwisho Wake:

Msafiri hupunguza Swala zake tokea anapoyaacha makazi ya mji wake, na ataendelea kupunguza Swala hata kama utarefuka muda wa safari yake mpaka atakaporudi kwake. Isipokuwa kama atanuiya kukaa mahali kwa siku nne na zaidi basi itamlazimu atimize swala zake na asizipunguze kwani kwa kutia nia ya kukaa akili yake itatulia na atafanya mambo yake kwa utulivu upo wakati Mtume ﷺ aliwahi kukaa,

“Tabuki kwa muda wa siku ishirini na alikuwa alikuwa akipunguza Swala zake.” (Abu Dawuud).

Na ikasemwa ni kwa sababu Mtume ﷺ hakutia nia ya kukaa hapo Tabuki.

5. Sunna katika Safari:

Muislamu anapokuwa safarini anaweza kuacha sunna nyingine kama zile zinazoandamana na *faradhi* na zisizokuwa hizo isipokuwa raka'a mbili za sunna ya Alfajiri na Witri, kwani si vizuri kuziacha. Ibn Umar رضي الله عنه alikuwa anasema:

“Kama ningekuwa naswali sunna basi ningetimize Swala yangu.”
(Abu Dawuud)

Pamoja na hayo msafiri anaruhusiwa kuswali za sunna bila ya karaha kadri atakavyotaka, kwani Mtume ﷺ,

“Aliswali dhuha raka'a nane akiwa safirini kama vile ambavyo aliwahi kuswali sunna akiwa juu ya mnyama wake akiwa njiani akisafiri.” (Abu Dawuud)

6. *Qasr* ni kwa Wasafiri Wote:

Hakuna tofauti katika Sunna ya kupunguza Swala kati ya msafiri aliyepanda mnyama, chombo au anayesafiri kwa mguu. Isipokuwa Baharia ambaye hashuki katika chombo muda wote na anayo familia yake humo yeye atawajibika kutimiza Swala yake.

b) *Al-Jam 'u* (Kukusanya Swala)

1. Hukumu yake:

Kukusanya Swala ni ruhusa iliyopo. kukusanya Swala ya Adhuhuri na Alasiri siku ya *Arafa* kwa aliyepo *Arafa*, na kati ya Magharibi na Isha kwa aliyepo *Muzdalifa*, ni sunna iliyolazimishwa, kama ilivyopokewa kwa Mtume ﷺ.

“Kuwa aliswali Adhuhuri na Alasiri akiwa Arafa kwa adhana moja na Iqama mbili na alipofika Muzdalifa aliswali Magharibi na Isha kwa adhana moja na Iqama mbili.” (Abu Dawuud)

2. Namna ya Kuswali:

Kukusanya ni kwa msafiri kuswali Adhuhuri na Alasiri “*Jam 'u Taqdim*”. Kukusanya kwa kuitanguliza Swala ya Alasiri na Swala ya Adhuhuri wakati wa Adhuhuri, au “*Jam 'u Taakhir*” kuikusanya swala ya Adhuhuri na Alasiri na kuziswali wakati wa Alasiri pamoja tena kwa nyakati za mwanzo za Swala hizo.

Au kukusanya Magharibi na Isha na kuziswali katika moja ya nyakati za mwanzo za Swala hizo. Na hivyo ni kwa ilivyopatikana toka kwa Mtume ﷺ:

*“Kuwa alichelewesha Swala siku moja huko **Tabuk** kisha alitoka na akaswali Adhuhuri na Alasiri kwa pamoja. Kisha akatoka wakati mwingine na akaswali magharibi na Isha pamoja wakati alipofika **Tabuk** vitani.”* (Muslim na Malik katika Muwatta)

Kama ambavyo inaruhusiwa kwa wakazi wa mji kukusanya kati Swala ya Magharibi na Isha msikitini usiku wa mvua, baridi kali au upepo mkali kama wataona taabu kurudi msikitini kwa Swala ya Isha kwani:

“Alikusanya Mtume ﷺ Magharibi na Ishai katika usiku wa mvua kali.” (Al-Bukhari na Muslim)

Kama ambavyo inaruhusiwa kwa mgonjwa kukusanya Adhuhuri na Alasiri au Magharibi na Ishai kama ataona taabu kuswali kila Swala kwa wakati wake. Kwani sababu ya kukusanya Swala zake kutolewa ruhusa hiyo ni taabu na matatizo pale yanapotokea, basi inajuzu kwa mtu katika hali hiyo. Upo wakati inaweza kutokea dharura au watu wa mji kuingiwa na hofu juu ya maisha na usalama wao, kaika hali kama hii ni halali kwake kukusanya Swala. Imesihi kwa Mtume ﷺ kwamba aliwahi kukusanya Swala akiwa mjini mara moja pasina kuwepo mvua. Amesema Ibn ‘Abbas رضي الله عنه:

“Kuwa Mtume ﷺ aliswali Madina raka saba na nane, Adhuhuri na Alasiri na Magharibi na Isha.” (Al-Bukhari na Muslim)

Na sura yake ni: kuchelewesha Adhuhuri na kuitanguliza Alasiri kwa wakati wake wa mwanzo na kuchelewesha Magharibi na kuitanguliza Ishai katika mwanzo wa wakati wa Isha na hivyo ni kuzishirikisha Swala mbili kwa wakati mmoja.

c) Swala ya Mgonjwa:

Kama itatokea kuwa mgonjwa hawezi kusimama hata kwa kuegemea kitu basi ni ruhusa kwake kuswali hali ya kuwa amekaa, na ataposhindwa kukaa ataswali akiwa amelalia ubavu wake na ataposhindwa hivyo ataswali akiwa amelala chali na ameelekeza miguu yake Kibla na ataifanya sijida yake ni ya kuinama zaidi kuliko ruku yake na kama atashindwa kabisa kurukuu au kusujudu basi ataashiria tu. Na haruhusiwi mtu kuacha kuswali kwa sababu yoyote, kwa kauli ya ‘Imran Bin Husweyn رضي الله عنه kuwa:

*“Niliugua maradhi ya **Bawasiir** (mgoro) nikamuuliza Mtume ﷺ kuhusu Swala, akasema: Swali ukiwa wima, kama hukuweza basi kwa kukaa, kama hukuweza Swali ukiwa umelalia ubavu wako kama hukuweza basi ukiwa umelala chali.” (Al-Bukhari).*

Allah haikalifishi nafsi ya mtu isipokuwa kwa kile ikiwezacho.

d) Swala ya Khofu

1. Sheria yake:

Swala ya khofu ni sheria kwa kauli ya Allah (s.w):

فَإِذَا سَجَدُوا فَلْيَكُونُوا مِنْ وَرَائِكُمْ وَلْتَأْتِ طَائِفَةٌ أُخْرَىٰ لَمْ يُصَلُّوا
فَلْيُصَلُّوا مَعَكَ وَلْيَأْخُذُوا حِذْرَهُمْ وَأَسْلِحَتَهُمْ

“Na unapo kuwa pamoja nao, ukawasalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na wachukue silaha zao. Na watakapo maliza sijida zao, basi nawende nyuma yenu, na lije kundi jingine ambalo halijasali, lisali pamoja nawe. Nao wachukue hadhari yao na silaha zao...” (An-Nisai 4:102)

2. Namna ya Kuiswali katika Safari:

Maagizo tofauti yamekuja juu ya namna ya kuswali Swala ya khofu, lakini hali zote hizo zinarudia kwenye Swala ya hofu kubwa na ndogo na aina iliyo mashuhuri ni wakati wa vita mkiwa safarini. Kiongozi wa kambi ataligawa jeshi makundi mawili, kundi moja likaelekea upande wa maadui na kundi jingine linapanga safu nyuma ya Imamu na linaswali naye rakaam moja na linabakia likiwa wima kisha litasimama na liswali rakaam nyingine na kutoa salamu, halafu kuelekea pale lilipo kundi jingine lililosimama. Na linakuja lile kundi jingine linaswali anabaki imamu akiwa amekaa, kisha linasimama kundi hili na kukamilisha rakaam ya pili kisha anatoa salamu na makundi yote.

Na ushahidi wa aina hii ya Swala ni Hadithi ya Sah’li bin Abi Hathma kuwa *“Kundi moja lilipanga safu na Mtume ﷺ na kundi jingine likielekea adui akaliswalisha kundi alilonalo rakaam moja kisha akabakia wima na kundi lile lilikamilisha rakaam ya pili lenyewe na likaelekea upande wa adui, na likaja kundi jingine akaliswalisha rakaam moja iliyobakia katika Swala yake kisha akabakia amekaa nao wakatimiza rakaam nyingine wenyewe kisha akatoa salamu na wote pamoja.”*

3. Namna Kuswali kama si Safarini:

Na kama vita inapiganwa nyumbani (mjini kwa watu) kwa vile *Qasr* haijuzu (kupunguza), basi Imamu ataswali na kundi moja rakaa mbili na likakamilisha lenyewe rakaa mbili nyingine, kisha litakuja kundi la pili na ataliswalisha rakaa mbili na atabakia amekaa kisha litakamilisha rakaa mbili nyingine kisha atatoa salamu na wote.

4. Wakati wa vita kali:

Itakapokuwa vita ni kali kutowezekana kuligawa jeshi, basi wataswali kila mmoja pekee yake wale waliopanda wanyama, chombo au wanaotembea kwa miguu wakiwa wameelekea *Kibla* au la wataashiria tu katika matendo. Kwa kauli ya Allah (s.w.):

فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَأَدْكُرُوا اللَّهَ ۚ كَمَا عَلَّمَكُم
مَا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴿٢٣٩﴾

“Ikiwa mnakhofu (Salini) na hali mnakwenda kwa miguu au mmepanda. Na mtakapo kuwa katika amani, basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama alivyo kufunzeni yale mliyo kuwa hamyajui.” (al-Baqara 2: 239)

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Wakiwa katika hali zaidi ya hiyo basi waswali wakiwa wamesimama na wamepanda.” (Al-Bayhaqi)

5. Anayefukuza Adui au Anayemkimbia Adui:

Anayemfukuza adui huku akiwa na hofu asije kumkimbia au kupotea, au anayetafutwa na adui na anahofu ya kukamatwa. ataswali katika hali yoyote atakayoweza. Akitembea au akikimbia kuelekea *Kibla* au penginepo. Na kwa yeyote anayehofia nafsi yake kwa kumwogopa mtu au mnyama basi ataswali Swala ya hofu kutokana na hali yake na ushahidi ni kauli ya Allah (s.w.):

فَإِنْ خِفْتُمْ فَرَجَالًا أَوْ زُرُبَانًا

“Ikiwa mnakhofu (Salini) na hali mnakwenda kwa miguu au mmepanda...” (Al-Baqara 2: 239).

Na alifanya hivyo ‘Abdillah bin Unaysi (r.a.) wakati alipotumwa na Mtume (s.a.w.) kumfuatilia mtu wa kabila la Hudhaliy na anasema:

“Wakati nilipohofu kuwa kitakachonichelewesha ni Swala, nilisafiri huku ninaswali ninaashiria huku nikielekea upande wake na nilipomfikia...” (Abu Dawuud)

Somo la Kumi

Swala ya Ijumaa

1. Hukumu yake:

Swala ya Ijumaa ni wajibu kwa kauli ya Allah (s.w.t):

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩﴾

“Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Swala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua...” (Al-Jumaa 62: 9)

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Wallahi wakome watu kuziacha Ijumaa ama atapiga muhuri Allah juu ya nyoyo zao kisha wawe miongoni mwa walioghafilika.” (Muslim).

Na kauli yake:

“Ijumaa ni haki iliyo wajibu juu ya kila Muislamu isipokuwa watu wanne: Mtumwa aliyemilikiwa, au mwanamke, au mtoto mdogo au mgonjwa.” (Abu Dawuud).

2. Hekima ya sheria juu ya swala ya Ijumaa:

Miongoni mwa hekima ambazo kwazo imefanywa kuwa ni Swala ya Ijumaa: Kukusanya watu baleghe wenye akili timamu “*Mukallafina*” wanaoweza kubeba majukumu katika mji huo au kijiji mwanzo mwa kila wiki katika sehemu moja ili kuelezwa na kupokea yale yaliyojitokeza katika maazimio, maamuzi anayoyotoa Imamu wa Waislamu na kiongozi wao kwa yale yanayohusiana na Dini yao na dunia yao. Pia wasikie maonyo na matumaini yatakayowafanya wawajibike vyema katika kutekeleza wajibu wao na yatakayowawezesha kusimamia kidete harakati za Kiislam za wiki nzima kwa ufanisi.

Zinabainika wazi hekima hizo kwa atakayeangalia kwa mazingatio masharti ya swala ya Ijumaa na vinavyoambatana na Swala hiyo; kwa sababu miongoni mwa sharti zake ni kuwepo mji au kijiji, na kuwepo jamaa, na kuswali katika Msikiti mmoja, na hotuba itatolewa na khalifa au mkuu wa hapo. Sharti zingine kukatazwa kuzungumza wakati wa khotuba ya Ijumaa na kuwa si wajibu kuswali Ijumaa kwa mtumwa, mtoto, mwanamke, na mgonjwa. Kwa sababu majukumu kwa watu hawa tuliowataja hayajakamilika pamoja na kuwa hawana uwezo wa kuyatekeleza yale wanayotakiwa kufanya miongoni mwa majukumu yatakayotajwa katika minbari siku ya ijumaa.

3. Uboru wa Siku ya Ijumaa:

Siku ya Ijumaa ni siku iliyo bora na tukufu. Ni bora miongoni mwa siku za duniani, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Siku bora ya zilizochozewe na jua ni siku ya Ijumaa, siku hiyo Adam عليه السلام aliumbwa, ni siku hiyo aliingizwa peponi, ni siku hiyo ndio aliyotolewa peponi na kiyama kitasimama siku ya Ijumaa.” (Muslim).

Siku ya ijumaa ni siku inayostahili kutukuzwa kama alivyoitukuza Allah (s.w.). Hivyo waislam wanahitajika kufanya mengi mema, na kujitenga na maovu.

4. Yatakiwayo siku ya Ijumaa na Adabu zake:

i). Kuoga kwa kila atakayehudhuria Swala ya ijumaa kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Kuoga siku ya Ijumaa ni wajibu imethibiti kwa kila mkubwa.”
(Al-Bukhari, Muslim na Abu Dawuud)

ii). Kuvaa nguo safi na kujipaka manukato. Hii ni kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Wajibu kwa kila Muislamu kuoga siku ya Ijumaa na kuvaa nguo safi na kama anayo manukato ajipake.” (Imam Ahmad)

iii). Kwenda Msikitini mapema kabla ya kuingia muda wake. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakayeoga siku ya Ijumaa mfano wa joshu la janaba, kisha akaenda Msikitini mapema anakuwa sawa na aliyetoa sadaka ya ng’ombe na atakayefuatia ni kama vile alitoa sadaka ya atakayekwenda saa nne ni kama vile alitoa kuku, na atakayekwenda saa ya tano ni kama vile ametoa yai, na atapotokea Imamu huhudhuria malaika wakisikiliza hotuba.”
(Imam Malik, Al-Bukhari na At-Tirmidhi)

iv). Kuswali Sunna za kutosha, baada ya kuingia msikitini rakaa nne na zaidi kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Haogi mtu siku ya Ijumaa na akajitoharisha kadri ya uwezo wake na akajitia manukato nyumbani kwake kisha akaenda Msikitini na akawa hapasuwi safu kati ya watu wawili, kisha akaswali kiasi chake, kisha akakaa kimya akamsikiliza Imamu wakati akitoa hotuba mtu huyu atasamehewa madhambi kuanzia Ijumaa ile mpaka Ijumaa nyingine kwa muda wa kuwa hajafanya dhambi kubwa.” (Al-Bukhari na Imam Ahmad)

v). Kuzungumza na kucheze wakati Imamu akitoa hotuba. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Utakapomwambia nyamaza mwenzako siku ya Ijumaa na Imamu anahutubu basi umefanya upuuzi.” (Muslim na Imam Ahmad)

vi). Utakapoingia msikitini wakati Imamu anahutubu uswali rakaa mbili nyepesi - Tahiyatu Masjid kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakapoingia mmoja wenu siku ya Ijumaa hali ya kuwa Imamu anahutubu na aswali rakaa mbili nyepesi.” (Muslim na Imam Ahmad)

vii). Ni karaha kwa Mtu aliyechelewa kuingia msikitini kuwaruka watu katika safu akijaribu kupata nafasi sehemu za mbele kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Kwa yule aliyemuona akifanya hivyo “kaa, unaudhi” (Abu Dawuud na Ibn Majah)

Na kauli yake Mtume ﷺ *“Usiwapite watu kati yao.”*

viii). Ni haramu kuuza na kununua wakati wa Swala ya Ijumaa, kwa tamko la Allah (s.w.)

إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ
ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩﴾

“...Ikiadhiniwa Swala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara.” (62: 9)

ix). Ni Suna kusoma Suratul Kahf katika usiku wa kuamkia Ijumaa au mchana wake kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakayesoma Suratul Kahf siku ya Ijumaa atang’arishiwa nuru kati ya Ijumaa mbili.” (Al-Hakim)

x). Kumswalia Mtume ﷺ kwa wingi kwa kauli yake:

“Niswalieni sana siku ya Ijumaa na atayefanya hivyo nitakuwa shahidi na muombezi wake siku ya Kiyama.” (Al-Hakim na al Bayhaqi)

xi). Kuomba dua kwa wingi siku ya Ijumaa, kwani ipo saa ya kujibiwa watu dua zao siku hiyo. Yule atayeisadifu Allah (s.w) atamjibu na atampa alichoomba. Amesema Mtume ﷺ:

“Kwa hakika ipo saa siku ya Ijumaa amabayo mja muislam akiomba dua wakati huo, Allah(s.w) atajibu na atampa anachotaka.” (Muslim na Imam Ahmad)

Kuna baadhi ya mapokezi kuwa saa hiyo ni kati ya kuingia Imamu na kumaliza Swala, na pia inasemekana ni baada ya Alasiri. (Imam Ahmad, Ibn Majah)

5. Wajibu wa Swala ya Ijumaa :

- i) Swala ya ijumaa ni wajibu kwa wanaume, na si wajibu kwa wanawake.
- ii) Kuwa huru “uungwana”, si wajibu kwa mtumwa.
- iii) Kuwa balebale, si wajibu kwa mtoto.
- iv) Uzima “afya njema”, si wajibu kwa mgonjwa asiyeweza kufika.
- v) Kuwa mkazi, si wajibu kwa msafiri.

Na haya ni kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Ijumaa ni haki na wajibu kwa kila Muislam isipokuwa; Mtumwa, mwanamke, mtoto au mgonjwa” (Abu Dawuud na al-Hakim)

Na kauli yake,

“Anayemuamini Allah na siku ya mwisho ni wajibu ahudhuri Swala ya Ijumaa, isipokuwa mgonjwa, msafiri, mwanamke, mtoto au mtumwa.” (Ad-Dar-aqutni na Baihaqi)

yeyote katika wale ambao si wajibu kwao, akihudhuria na kuswali Swala ya Ijumaa nyuma ya Imamu hatowajibika tena kuswali Swala ya Adhuhuri.

6. Sharti kukamilika Swala ya Ijumaa:

i) **Kijiji**, Swala ya Ijumaa haiswihi pahala palipo na wakazi wenyeji chini ya arobaini au ikiswaliwa watu wakiwa safrini kwani wakati wa Mtume ﷺ haikupata kuswaliwa Swala ya Ijumaa isipokuwa katika miji au vitongoji kwa masharti yaliyotajwa. Pamoja na wingi wa safari za Mtume ﷺ haikuthibiti kuwa aliswali Ijumaa akiwa safarini.

ii) **Msikiti**, haiswihi Ijumaa kuswaliwa nje ya majengo au viwanja vya Msikiti

iii) **Khutba**, Swala ya Ijumaa haiswihi bila ya kusomwa hotuba, kwani haikuwajibishwa Swala ya Ijumaa isipokuwa kwa sababu ya hotuba.

7. Asiye Mkazi wa mji:

Swala ya Ijumaa si wajibu kwa anayekaa mbali na mji unaoswaliwa Ijumaa kwa zaidi ya maili tatu, kutokana na kauli yake Mtume ﷺ :

“Ijumaa ni wajibu kwa aliyesikia adhana.” (Abu Dawuud, Ad-Daraqutni, Ahmad, Shafii na Maliki)

Kwa kawaida si rahisi kwa sauti ya muadhini kufika umbali wa zaidi ya maili tatu (kilometa nne).

8. Kuwahi (Atakayediriki) Rakaa:

Maamuma akiwahi rakaa moja katika Swala ya Ijumaa, atamalizia rakaa ya pili baada ya salamu ya Imamu. Na atakuwa amepata Swala ya Ijumaa. Kwa kauli yake Mtume ﷺ :

“Aliyeidiriki rakaa katika Swala basi ameidiriki Swala yote.”
(At-Tirmidhi, Imam Ahmad, Ibn Majah na An-Nasai).

Amma kwa aliyediriki chini ya rakaa kwa kuwahi sijida huyu atanuia Adhuhuri na atatimiza rakaa nne baada ya salamu ya Imamu.

9. Kusimamisha Ijumaa nyingi katika mji mmoja:

Kama Msikiti ni mdogo usio na uwezo wa kuchukua wakazi wote wa mji, inajuzu kusimamisha Ijumaa katika Msikiti mwingine mjini pale, au Misikiti mingine kwa kadiri ya Haja.

10. Jinsi ya kuswali Swala ya Ijumaa:

Baada ya Imamu kupanda juu ya *mimbari* atawatolea waislamu waliohudhuria msikitini Salam na kisha kukaa. Baada ya kukaa kwake muadhini atasoma adhana ya kawaida na baada ya adhana ndio khatibu atasimama na kuanza kusoma hotuba ya Ijumaa akianza kwa: Kumsifu Allah (s.w.) kisha kumsifu pamoja na kumtakia rehema Mtume wake Muhammad ﷺ kisha anatoa mawaidha kwa watu kwa sauti inayosikika, anawahamasisha kwa kutumia amri za Allah (s.w.) na Mtume wake ﷺ atawaonya waislam kuacha maovu na kuwahimiza kutenda mema na kuwapa matumaini, kisha atakaa mkao kwa muda mfupi halafu atasimama kwa kuanza hotuba ya pili kwa kumsifu na kumshukuru Allah (s.w.) na kumtakia rehema Mtume ﷺ na ataunganisha hotuba kwa mfano wa mwanzo. Na sauti iwe ni ya ukakamavu, asirefushe hotuba, kisha ateremke na *muadhini* atakimu kwa ajili ya Swala, na ataswali na *maamuma* rakaa mbili kwa sauti na katika rakaa ya kwanza atasoma *Surat A'ala*, "*Sabbihisma*" na rakaa ya pili *Suratul, "Ghashiya"* "*Hal-Ataaka Hadithul-Ghashiya.*"

Somo la Kumi na Moja

Sunna na witr, rakaa mbili za Sunna ya alfajiri, Sunna za mpango, na Sunna kwa ujumla

a) *Witr*

1. Hukumu yake na maana yake:

Witr ni sunna iliyotiliwa mkazo haifai kwa Muislamu kuiacha bila sababu za msingi. Nayo ni kuswali rakaa moja baada ya Swala ya Isha kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Swala ya usiku ni rakaa mbili mbili, akihofia mmoja wenu kuchomoza Alfajiri basi aswali rakaa moja ikiwa ni witr ya rakaa alizoswali.” (Al-Bukhari na Imam Ahmad)

2. Sunna kabla ya *Witr*:

Ni sunna kuswali rakaa mbili au zaidi mpaka 10 kabla ya rakaa moja ya *witr*, kisha uswali *witr* kwa kama alivyofanaya Mtume ﷺ.

3. Wakati Wake:

Wakati wa *witr* ni baada ya Swala ya Isha mpaka kabla ya Swala ya Alfajiri na kuswali usiku wa mwisho ni bora kuliko mwanzo wake isipokuwa kwa yule anayehofia kutoamka usiku, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Yule anayedhani kuwa hatoweza kuamka usiku wa mwisho na aswali witr mwanzo wake, anayedhani kuwa ataamka usiku wa mwisho, basi Swala ya mwisho wa usiku inatua zaidi na ni bora.” (Imam Ahmad)

4. Aliyelala bila ya Kuswali Witr:

Bila ya kuswali *witr* anaweza kuilipa kabla ya Swala ya Asubuhi kwa kauli yake Mtume ﷺ.

*“Atakapopambazukiwa mmoja wenu na Asubuhi na hakuswali
witri basi na aiswali.” (Al-Bayhaqi)*

Na kauli yake Mtume ﷺ,

*“Aliyelala bila ya kuswali witri yake au kuisahau na aiswali
atapoikumbuka.” (Abu Dawuud)*

5. Kisomo Katika Witri:

Ni sunna katika rakaa mbili za mwanzo kabla ya rakaa ya witri kusoma *Suratu A'ala* na *Al-Kafiruna*.

Na katika rakaa ya witri usome *Qul-Huwallah, Qul-Audhu Bi rabbil Falaq* na *Qul Audhu Birabbi N-nas*. Baada ya *Al-hamdu*. (Abu Dawuud na An-Nasai)

6. Karaha ya kufanya witri nyingi

Ni karaha kufanya witri nyingi katika usiku mmoja kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakuna witri mbili usiku mmoja.” (At-Tirmidhi)

Na atakayeswali witri mwanzo wa usiku kisha akaamka akataka kuswali sunna basi ataswali sunna na asiswali tena witri kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakuna witri mbili usiku mmoja.”

b) Sunna ya Al-Fajiri

1. Hukumu Yake:

Rakaa mbili kabla ya Swala ya Al-Fajiri ni sunna iliyotiliwa mkazo kama witri. Kwani hiyo Ndiyo Swala ya mwanzo ya Muislamu kwa mchana na witri ndio mwisho wa Swala yake ya usiku. Aliitilia mkazo Mtume ﷺ kwa vitendo kwani alidumu nayo na hakuiacha katu. Na amesema,

“Rakaa mbili za Alfajiri ni bora kuliko dunia na vilivyomo.” (Muslim)

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Msiziache rakaa mbili za Alfajiri hata kama mnafukuzwa na farasi.” (At-Tabarani)

2. Muda wake:

Wakati wa *sunna* ya rakaa mbili za Alfajiri ni kati ya kuchomoza alfajiri na swala ya Alfajiri. Na yule aliyelala mpaka jua likachomoza au aliyejisahau basi ataiswali pale atakapokumbuka isipokuwa jua litakapogeuka hapo tena. Hawezi kuiswali kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Yule ambaye hakiswali rakaa mbili za Alfajiri mpaka likachomoza jua na aziswali.” (Al-Bayhaqi)

Na alipata kupitiwa na usingizi Mtume ﷺ na masahaba zake رضي الله عنه،

“Mara moja katika moja ya vita na hakuamka mpaka jua limechomoza basi wakageuka kidogo toka sehemu yao waliopo kisha Mtume ﷺ akamuamrisha Bilal akaadhini na wakaswali rakaa mbili kabla ya Swala ya Alfajiri, kisha akakimu Swala wakaswali Sub’hi.” (Imam Ahmad na Al-Bayhaqi)

3. Sifa Yake

Sunna ya Alfajiri ni rakaa mbili unasoma *Suratul Kafiruna* na *Qul Huwallahu* baada ya *Al-hamdu* bila ya kutoa sauti. Na kama utasoma *Al-hamdu* bila ya sura inatosheleza kwa kauli ya Aisha رضي الله عنها،

“Mtume ﷺ alikuwa akiswali rakaa mbili kabla ya mchana na akizifanya nyepesi mpaka nilitia shaka kama anasoma *Al-Fatiha* au la.” (Imam Ahmad na Ibn Majah).

Na kauli yake ‘Aisha رضي الله عنها,

“Alikuwa Mtume ﷺ anasoma katika raka'a mbili za alfajiri: *Qul-Ya Ayyuhal Kafirun*, na *Qul-Huwallahu Ahad*.” (Al-Bukhari na Muslim) na “alikuwa anazisoma kwa sauti ya chini.”

c) Sunna za Rawatib

Rawatib: Ni sunna za kabla na baadaye zikifuatana na Swala za faradhi. Nazo ni raka'a mbili kabla ya adhuhuri na raka'a mbili baada yake, na raka'a mbili kabla ya Alasiri na raka'a mbili baada ya Magharibi, na raka'a mbili au nne baada ya Ishaa. Kwa kauli ya Ibn Umar رضي الله عنه:

“Nilihifadhi toka kwa Mtume ﷺ raka'a kumi, raka'a mbili kabla ya Adhuhuri, na raka'a mbili baada yake, raka'a mbili baada ya Magharibi, nyumbani kwake, na raka'a mbili kabla ya Asubuhi.” (Al-Bukhari na Muslim)

Na kauli ya Aisha رضي الله عنها,

“Alikuwa Mtume ﷺ haachi raka'a nne kabla ya Adhuhuri.” (Al-Bukhari)

Na kauli nyingine ya Mtume ﷺ,

“kila baada ya adhana mbili kuna Swala.” (Ad-Daraqutni).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Amehurumiwa na Allah (s.w) mtu aliyeswali raka'a nne kabla ya Alasiri.” (Abu Dawuud na At-Tirmidhi)

d) Swala za Sunna Kwa Ujumla

1. Ubora wake:

Swala za sunna ni ubora kabisa. Amesema Mtume ﷺ,

“Hakutoa idhini Allah (s.w.) kwa mja wake kwa chochote kilicho bora kuliko raka mbili anazosiswali, hakika wema humiminika kichwani kwa mja maadamu yupo katika Swala.” (At-Tirmidhi).

Na alisema Mtume ﷺ kumueleza yule aliyemuomba Mtume ﷺ, kuwa karibu naye peponi,

“Jisaidie mwenyewe kwa kuswali sana.” (Imam Ahmad)

2. Hekima Yake:

Miongoni mwa hekima za Swala za sunna ni kule kuingia kwake upungufu Utakaomtokea mja siku ya qiama katika amali zake. Atasema Allah kuwaeleza malaika - hali ya kuwa anajua,

“Angalieni Swala za mja wangu ameitimiza au ameipunguza? Kama ameitimiza aandikiwe “imetimia” na kama imepungua chochote atwauliza mja wangu ana sunna? Kama anazo Sunna atasema mtimizeni mja wangu faradhi zake kutokana na sunna zake, kisha huchukuliwa amali kutokana na hivyo.” (Al-Hakim)

3. Wakati Wake:

Usiku na mchana ni wakati wa sunna isipokuwa nyakati tano tu ndio hazina sunna. Kama ifuatavyo:

- i) Baada ya Swala ya Alfajiri, mpaka jua lichomoze.
- ii) Wakati jua likichomoza mpaka linyanyuke kiasi.
- iii) Wakati likiwa katikati yaani mchana.
- iv) Baada ya Alasiri mpaka kuwa jua la manjano.
- v) Baada ya jua kuwa la manjano mpaka lizame.

Na hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ kumueleza ‘Amr bin A’bsa رضي الله عنه wakati alipomuuliza Mtume ﷺ kuhusu swala:

“Swali Swala ya Asubuhi kisha usiswali mpaka jua lichomoze na linyanyuke, kwani wakati huo huchomoza kati ya pembe mbili

za shetani, na hapo makafiri hulisujudia, kisha baada ya muda huo swali kwani Swala hiyo hushuhudiwa (uhudhuriwa) na malaika mpaka ithibiti Adhuhuri, kisha acha kuswali kwani wakati huo huchemshwa Jahannamu, na kikigeuka kivuli swali, kwani Swala hiyo hushuhudiwa na malaika mpaka ifike Alasiri. Kisha acha kuswali mpaka lizame jua kwani wakati huo huo huzama kati ya pembe mbili za shetani hapo hulisujudia makafiri.” (Muslim).

4. Kukaa katika Sunna:

Inajuzu kuswali sunna huku umekaa ijapokuwa anayeswali Sunna huku amekaa atapata malipo nusu ya aliyeswali huku amesimama kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Swala ya mtu aliyekaa ni nusu ya aliyesimama.” (Muslim na Abu Dawuud)

5. Aina za Sunna:

i). **Tahiyyatul-Masjid**, kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Atakapoingia mmoja wenu msikitini asikae mpaka aswali raka mbili.” (Al-Bukhari na Muslim)

ii). **Swala ya Dhuha**, Nayo ni kuanzia raka nne mpaka raka nane, kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Hakika Allah (s.w.) amesema katika Hadithi Qudsy, “Ewe mwanadamu swali kwa ajili Yangu raka nne mwanzo wa mchana nitakutoshelezea mwisho wake.” (Imam At-Tirmidhi)

iii). **Tarawehe ya Ramadhani**: Kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Atakayesimama usiku wa Ramadhani kwa imani na kutaraji radhi za Allah (s.w.) basi atasamehewa dhambi alizozitanguliza.” (Al-Bukhari)

iv). Raka mbili baada ya **kutawadha**, kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Muislamu akitawadha vizuri kwa ajili ya Swala Allah (s.w) atamsamehe tangu wakati huo mpaka na Swala inayofuatia.” (Muslim)

v). Rakaa mbili unaporudi toka **safari** katika Msikiti wa mjini kwako, na hayo ni kwa kitendo cha Mtume ﷺ hivyo amesema Ka’ab bin Malik رضى الله عنه

“Ilikuwa ni kawaida ya Mtume ﷺ kuswali rakaa mbili msikitini kila anaporudi toka safarini “ (Al-Bukhari)

vi). Rakaa mbili za **Toba**, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Mtu yeyote akifanya dhambi kisha akasimama na kuchukua udhu na akaswali rakaa mbili akimtaka Allah (s.w.) msamaha atamsamehe.” (At-Tirmidhi)

vii). Rakaa mbili kabla ya **Magharibi**, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Swalini kabla ya Magharibi.” Kisha akasema kwa mara ya tatu “Kwa atakaye.” (Al-Bukhari)

viii). Rakaa mbili za **Istikhara**, kwa kauli yake Mtume ﷺ, “Anapotaka kufanya jambo mmoja wenu na aswali rakaa mbili zisizo za faradhi kisha aombe dua:

اللهم اني استخيرك بعلمك، وأستقدرك بقدرتك، وأسألك من فضلك العظيم، فانك تقدر ولا أقدر، وتعلم ولا أعلم وأنت علام الغيوب. اللهم إن كنت تعلم أن هذا الأمر خير لي في ديني ومعاشي، وعاقبة أمري، فاقدره لي ويسره لي، ثم بارك لي فيه. وإن كنت تعلم أن هذا الأمر شر لي في ديني ومعاشي وعاقبة أمري، فاصرفه عني واصرفني عنه واقدر لي الخير حيث كان ثم رضني به

“Allahuma Inniy Astakhiyruka Bi ‘Ilmika Waas aluka Min Fadhlikal-‘Adhim, Fa Innaka Taqdiru Wala Aqdiru, Wa Ta’alam Wala A’alam Wa Anta Allamul Ghuyuwbi, Allahuma In Kunta Ta’alamu Anna Hadhal-Amra Khayrul Lliy Fiy Diiniy Wa Maashiy Wa Aqibati Amrii Faqdir-Hu Liy Thumma Baarik Liy Fiihi, Wa In Kunta Talamu Anna Hadhal-Amra Sharru Liy Fiy Diinii Wa Maashiy Wa Aqibati Amrii Fasrif-hu Anniy, Waqdir Lii Al-Khayra Haythu Kana Thumma Raddhiniy Bihii.” (Al-Bukhari)

“Ewe Mola wangu nakutaka ushauri kwa elimu yako, na nakuomba kwa fadhila zako adhimu, kwani Wewe unaweza nami siwezi, na unajua nami sijui na wewe ndie mjuzi wa ghaibu. Ewe Mola wangu ukijua jambo hili ni kheri kwangu kwa dini na maisha yangu na mwisho wa mambo yangu nikadirie kwangu, kisha nibarikie. Na kama unajua kuwa jambo hili ni shari kwangu kwa dini na dunia na mwisho wa mambo yangu liondoe kwangu na unitilie kheri popote lilipo kisha uniridhie kwayo”

Na aitaje shida yake pale kwenye neno, *أَنْ هَذَا الْأَمْرُ*, ‘*Inna Hadhal Amra*’.

ix). **Swala ya Haja** nayo ni Swala inayoswaliwa na Muislamu anapokuwa na shida na anatawadha anaswali rakaa mbili kisha anamuomba Allah (s.w.) haja yake kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Mwenye kutawadha na akatimiza udhu wake kisha akaswali rakaa mbili akazitimiza basi Allah (s.w.) Atampa alichoomba mapema au baada ya muda mfupi.” (Imam Ahmad)

x). **Swala ya Tasbihi** nayo ni rakaa nne na atasema anayeswali baada ya kisomo katika kila rakaa mara kumi na tano (15):

سبحان الله، والحمد لله، ولا إله إلا الله والله أكبر

“*Sub’hana Llahi Wal hamdu Lillahi Wala Ilaha illa Llahu Wallah Akbar*”:

Katika *rukuu* Mara kumi (10), na katika *itidali* Mara kumi (10), katika *Sijida* Mara kumi (10), katika *mkao* Mara kumi (10), na katika *mkao wa tahiyatu* kati ya rakaa mbili Mara kumi (10).

Zote jumla zinakuwa *Tasbihi* katika kila rakaa ni (75) sabini na tano. Mafunzo haya ni kwa kauli yake Mtume ﷺ kumueleza Ami yake Al-Abbas:

“kuhusu Swala ya tasbihi na kumueleza, “Ukiweza kuiswali kila siku mara moja uswali, kama hukuweza hivyo basi kila siku ya Ijumaa mara moja na kama haukufanya hivyo basi kila mwaka mara moja na kama hukufanya hivyo basi katika umri wako uiswali angalau mara moja.” (Abu Dawuud na Ibn Majah)

xi). Sijida ya Kushukuru: Nayo huletwa baada ya kupata Muislamu neema kama vile kupata anachotaka au kusalimika na madhara. Inapokuwa hivyo Muislam huporomoka kwa sijida akimshukuru Allah (s.w.). Na miongoni mwa neema ambazo Mtume ﷺ alipewa na kushukuru kwa sijida ni pale Jibril alipomuambia,

“Atakaekutakia rehema mara moja Mwenyezi Mungu humtakia rehema mara kumi kwa kuambiwa hivyo Mtume ﷺ aliporomoka na kusujudu kwa kumshukuru Allah Mtukufu.” (Imam Ahmad)

“Uso wangu usujudu kwa aliyeiumba na akaitengeneza, na akapasua humo na kuweka masikio na macho yake kwa uwezo wake na nguvu zake, ametakasika Allah mbora wa waumbaji”

xii). Sijida ya kusoma Qur-aan (Tilawa): Ni sunna kuleta Sijida ya Tilawa kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Mtu anaposoma Qur-aan, na akaleta sijida pahala panapostahili katika kisomo chake shetani hujitenga na kulia huku akisema; Ee kuangamia kwangu, mtu huyu ameamrisha kusujudu na ataipata pepo. Mimi niliamrisha kusujudu nikakataa na nitaupata moto. (Muslim).

Basi Muislam atakaposoma aya ya sijida au akisikiliza kutoka kwa msomaji mwingine, ni sunna kwake kusujudu kwa kutoa takbira “Allah akbar” na katika sijida hiyo asome:

**سجد وجهي للذي خلقه وصوره، وشق سمعه وبصره بحوله
وقوته فتبارك الله أحسن الخالقين .**

*“Sajada Wajhiy Lilladhiy Khalaqahu Wasswawwarahu Washaqa
Sam’ahu Wabaswarahu Bi Haulihi Waquwwatihi, Fataba-raka
Llahu Ahsanul –Kha-liqiyn.”*

Malipo kamili yatapatikana kwa anayesujudu atapokuwa na udhu tena ameelekea *Qibla*. Na maeneo ya kusujudu ndani ya *Qur-aan* yanatambulika katika misahafu

nazo ni *Sijida* (kumi na tano). Kwa kauli ya Abdillahi Amr bin A'as رضي الله عنه:

“*Hakika Mtume ﷺ alisoma Sijida kumi na tano ndani ya Quran. Tatu kati ya hizo ni katika sura za urefu wa kati na katika Suratul Hajj kuna Sijida mbili.*” (Abu Dawuud).

Somo la Kumi na Mbili

Swala ya Iddi Mbili

a). Hukumu na Wakati wake:

Swala ya Iddi mbili *Iddil al-Fitr* na *Iddil Adh'ha* ni sunna iliyotiliwa mkazo na ni wajibu. Allah (s.w.) Aameamrisha kwa tamko lake:

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ۖ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ ۖ

“*Hakika tumekupa kheri nyingi. Basi swali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi...*” (al Kawthar 108: 1-2)

Na akahusisha na swala hiyo na mafanikio ya Muumini aliposema:

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّى ۖ وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ۖ

“*Hakika amekwisha fanikiwa aliye jitakasa. Na akakumbuka jina la Mola wake Mlezi, na akaswali.*” (Al a'ala 87:14-15)

Mtume ﷺ aliswali Swala za Idd mbili na akadumu nazo na akaamrisha watu waziswali, na akaruhusu watoke watu wote pamoja wanawake na watoto. Nazo ni alama miongoni mwa alama za Uislamu na ni *madhihari* pia katika *madhihar* zake ambapo huwekwa dhahiri dalili za Imani na Taqwa.

Na wakati wake ni tokea kunyanyuka jua mpaka kushuka jua na ni bora kuswali *al-Adh'ah* katika wakati wa mwanzo ili watu waweze kuchinja wanyama wao

baada ya Swala na icheleweshwe Swala ya *Idd al-Fitri* ili watu waweze kutoa sadaka zao. Kwani Mtume رضي الله عنه alikuwa akifanya hivyo. Amesema Jundub رضي الله عنه:

“Mtume رضي الله عنه alikuwa akituswalisha Idd al Fitri na jua limepanda kiasi cha kutosha, na Idd al Adh’ha jua likiwa limepanda.”

b). Adabu zake:

1. Kukoga na kujitia manukato na kuvaa nguo nzuri, kwa kauli ya Annas رضي الله عنه ya kwamba,

“Mtume رضي الله عنه alituamrisha tuvae nguo nzuri zaidi wakati wa swala za Iddi Mbili na tujipambe kwa manukato mazuri tuliyonayo na tuchinje wanyama wa thamani zaidi tuliyonao.” (al-Hakim)

Inahadithiwa kwamba Mtume رضي الله عنه alikuwa akivaa kishali chenye mistari katika kila *Idd*.”

2. Kula kabla ya kutoka kwenda kuswali Idd el Fitri na kula ini la mnyama wa *Udhhiya* baada ya swala ya *Iddi Adh’ha*. Kwa kauli ya Buraida رضي الله عنه

“Mtume رضي الله عنه alikuwa hatoki kwenda kuswali siku ya Idd al-Fitri mpaka amekula, na alikuwa hali siku ya Udhhiya mpaka anaporudi.”

3. Takbira huanza usiku wa kuamkia Iddi al-Fitri na usiku wa kuamkia *Idd al Adh’ha* na inaendelea katika *Idd al Adh’ha* mpaka mwisho wa siku za “*Tashriq*.” Na katika *Idd il-Fitri* mpaka atakapotokea Imamu kwa ajili ya Swala.” Na tamko lake ni:

الله أكبر الله أكبر، لا إله إلا الله، الله أكبر الله أكبر، والله الحمد.

“Allahu Akbar Allahu Akbar, La Ilaha Illa Llah, Allahu Akbar, Allahu Akbar Walillahil Hamd.”

Na inakuwa na nguvu zaidi wakati wa kwenda mahala pa kuswalia na baada ya Swala za faradhi siku tatu za *Tashriqi* kwa kauli ya Allah:

وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ﴿٢٠٣﴾

“Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazo hisabiwa...” (Al-Baqara 2: 203)

Na kauli yake Allah (s.w.),

وَأَذْكُرُوا اللَّهَ فِي أَيَّامٍ مَّعْدُودَاتٍ ﴿٢٠٣﴾

“Akakumbuka jina la Mola wake na akaswali.” (al a’la 87:15)

Na kauli yake Allah (s.w.):

لِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَانَا ﴿٣٧﴾

“...ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa alivyo kuongoeni.” (Al-Haj 22: 37)

4. **Kutoka kwenda kuswali kwa kupitia njia nyingine** tofauti na ile ya kurudia. Kwa kauli yake Mtume ﷺ Amesema Jabir رضي الله عنه:

“Wakati wa siku ya Idd Mtume ﷺ alikuwa akibadilisha njia” (Al-Bukhari)

5. **Kuswali uwanjani** isipokuwa kama kuna mvua au sababu nyingine zisizoweza kuzuilika, kutokana na Mtume ﷺ kuswalia katika viwanja kama ilivyopokewa katika hadithi sahihi.

6. **Kupongezana** kuombeana dua njema kama ilivyopokewa kuwa masahaba wa Mtume ﷺ waliombeana dua wanapokutana siku ya Idd,

“Taqabbala Llahu Minna wa Minka.” (Al-Bayhaqi)

7. Kula vizuri na kujiburudisha, unaruhusiwa kunywa na kushiriki katika michezo ya halali kwa kauli yake Mtume ﷺ katika Idd al-Adhha,

“Siku za Tash’riiq ni siku za kula na kunywa na kumkumbuka Allah (s.w.) kwa kumtaja kwa wingi.” (Imam Ahmad)

Na kauli ya Annas رضي الله عنه

“Alifika Mtume ﷺ Madina akawakuta wana siku mbili za michezo na akasema Mtume ﷺ: “Hakika amekubadilishieni Allah (s.w.) kwa siku mbili bora kuliko hizo: Siku ya Idd-il-Fitr na Idd-il-Adh’ha.” (Abu Razzak na Ibn Hajar)

Na kauli yake kumueleza Abu Bakar huku wakiimba mashairi siku ya Idd:

“Ewe Abu Bakar Hakika kila watu wana Idd yao nasi leo ndio Idd yetu.” (Al-Bukhari)

c) Namna ya Kuiswali Swala ya Idd.

Waislamu wanatakiwa kutoka kwenda sehemu ya kuswali Swala ya Idd kwa *Takbira*, mpaka litakaponyanyuka jua kiasi cha kutosha, kisha Imamu atasimama ili kuswalisha. Bila ya Adhana wala Iqama, katika rakaa mbili akitoa *takbira* Saba katika rakaa ya kwanza pamoja na *takbira* ya kuhirimia huku watu wakitoa *takbira* nyuma yake kwa kufuata *takbira* yake.

Atasoma *Suratul Fat’ha* na *Suratul A’ala* kwa sauti na atatoa *takbira* sita katika rakaa ya pili pamoja na ile aliyosimama nayo toka rakaa ya mwanzo, na atasoma *Suratul Fat’ha* na *Suratul Ghashiya* au *Wash-Shamsi Wadh-Dhuhaha*. Baada ya kutoa salamu, atasimama na atatoa hotuba kwa watu na kati yake atakaa mkaoni mwepesi atatoa mawaidha kwa kutumia hotuba hiyo na atakumbusha watu umuhimu wa kutenda mema na kuacha maovu, huku akikariri *takbira* mara kwa mara. Na ataianza hotuba kwa kumsifu na kumshukuru Allah .

Na kama ni *Idd-il-Fitri* atasisitiza *Zakatul Fitr* huku akibainisha baadhi ya hukumu na taratibu zake.

Na kama ni *Idd-il-Adh’ha* atasisitiza sunna ya kuchinja akibainisha umri wa mnyama wa kuchinja. Na atapomaliza ataondoka na watu wataondoka kwani hakuna sunna ya *Kabliya* au *Baadia* isipokuwa kama mtu amechelewa Swala

ya Idd na Imamu basi ataswali rakaa (4) nne, kwa kauli ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه kuhusiana na aliyechelewa Swala ya Idd, na aswali rakaa nne. Ama aliyeidiriki pamoja na Imamu hata kwa *Tahiyatu* tu basi atakamilisha rakaa mbili zilizobaki baada ya salamu.

Somo la Kumi na Tatu

Yahusu Swala ya Kupatwa Kwa Mwezi na Jua.

1. Wakati na Hukumu zake:

Swala ya kupatwa kwa mwezi au jua, ni sunna iliyosisitizwa kwa wanamume na wanawake. Mtume ﷺ ameamuru kuswaliwa, kwa kauli yake,

“Hakika jua na mwezi ni alama mbili miongoni mwa alama zinzoonyesha utukufu wa Allah (s.w), halipatwi jua au mwezi kwa kufa yeyote au kwa kuwa hai, kama mtaiona hali hiyo swalini.” (Al-Bukhari).

Kuiswali kwake sawa na swala ya Iddi mbili, na wakati wake, ni tokea kujitokeza kupatwa kwa moja ya vitoa nuru viwili; jua au mwezi mpaka linatanzuka, na kama itatokea kupatwa mwisho wa mchana wakati unaokatazwa kuswali katazo kali, badala ya Swala italetwa *dhikri* na *istighfari* na kunyenyekea na kuomba.

2. Sunna ya kupatwa kwa Jua au Mwezi:

Ni Sunna kusoma *Dhikiri na, Takbira, kwa wingi, kuomba toba, Dua* na kutoa, Sadaka, kumpa mtumwa uhuru wake kama unae, kufanya wema na kuungana udugu, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Hakika jua na mwezi ni alama mbili miongoni mwa alama za Allah (s.w), halipatwi jua wala mwezi kwa kufa mtu wala kwa kuwa hai, wakati ikitokea hali hiyo, muombeni Allah (s.w), na mtukuzeni na toeni sadaka na swalini.” (Al-Bukhari)

3. Namna ya Kuiswali:

Waislamu wapeane taarifa wakati ikitokea na wakusanyike watu msikitini bila ya Adhana wala Iqama, si vibaya kuitolea wito kwa tamko la: *Asswala-tu Jaamia*, Imamu *ataswalisha watu rakaa na kila rakaa itakuwa na rukuu* na visimamo viwili, imamu atarefusha kisomo, *rukuu* na *sijida*. Endapo kupatwa huko kwa jua na mwezi kutamalizika katikati ya Swala, wanaweza wakaikamilisha Swala hiyo katika muundo wa sunna za kawaida.

Hakuna sunna ya kusoma hotuba katika Swala ya kupatwa kwa jua au mwezi isipokuwa Imamu anaweza akawakumbusha watu na akawaonya akitaka, na kufanya hivyo ni vizuri. Kwa kauli ya Aysa Allah amuwie radhi:

“Lilipatwa jua wakati wa Mtume wa Allah ﷺ Akatoka Mtume wa Allah ﷺ kwenda msikitini, na akasimama akaleta takbira, na watu wakasimama nyuma yake. Mtume wa Allah akasoma kisomo kirefu, kisha akaleta takbira akarukuu rukuu ndefu iliyofupi kuliko kisomo cha kwanza, kisha akainua kichwa chake akasema: Samia Allahu liman hamidau, Rabana walakal Hamdu, kisha akasimama akasoma kisomo kirefu chini ya kisomo cha kwanza, kisha akaleta takbira akarukuu rukuu iliyo chini ya rukuu ya kwanza, kisha akasema: Samia Allahu Liman Hamidah, Rabbana Walaka Hamdu, kisha akasujudu, kisha akafanya katika rakaa nyingine kama hivyo mpaka zikakamilika rukuu nne na sijida nne, na jua likatanzuka kabla hajaondoka, kisha akasimama, akawahutubia watu, akamshukuru Allah kwa kila anachostahiki, kisha akasema: Hakika jua na mwezi ni alama mbili miongoni mwa alama za Allah (s.w.) aliyeshinda na kutukuka, havipatwi kwa kufa mtu wala kuwa hai, unapotokea hali hiyo nendeni mkaswali.” (Muslim)

4. Kupatwa kwa Mwezi:

Swala ya kupatwa kwa mwezi ni sawa na Swala ya kupatwa kwa jua, kwa kauli yake ﷺ, *“Inapotokea hali hiyo nendeni mkaswali.”* Isipokuwa baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa, Swala ya kupatwa kwa mwezi ni sawa na Swala

zingine za sunna, zinaswaliwa na mtu mmoja mmoja majumbani na misikitini, haiswaliwa kwa jamaa misikitini. Hiyo ni kwa sababu haikuthibiti kuwa Mtume ﷺ aliwakusanya watu katika Swala ya kupatwa kwa mwezi, kama alivyofanya katika Swala ya kupatwa kwa jua.

Fahamu swala hili ni pana, atakae ataiswali kwa jamaa, na atakae ataiswali peke yake, kwa sababu kinachotakiwa ni Waislamu kuswali na kuomba, wanaume kwa wanawake ili Allah (s.w.) awaondolee kilichowafika.

Somo la Kumi na Nne

Swala ya kuomba Mvua “Istisqai”

1. Hukumu yake:

Swala ya kuomba mvua ni sunna iliyotiliwa nguvu, aliiswali Mtume ﷺ na aliitangaza kwa watu na akatoka kwa ajili ya kwenda kuswali. Amesema ‘Abdullah bin Zayd رضي الله عنه:

“Alitoka Mtume ﷺ Kuswali Swala ya kuomba mvua akaelekea Kibla na akageuza nguo yake ya kujifunika kisha akaswali rakaa mbili kwa sauti.” (Abu Dawuud)

2. Maana yake:

Kuomba mvua toka kwa Allah (s.w.) kwa ajili ya nchi na watu wake kuswali na kuomba dua na kutaka maghfira wakati wa kukumbwa na ukame.

3. Wakati wake:

Ni sawa na wakati wa Swala ya *Idd*, kwa kauli ya ‘Aisha رضي الله عنها:

“Mtume ﷺ alitoka kwa ajili ya kwenda kuswali swala hiyo Wakati zilipodhihirika kinga za jua.” (Abu Dawuud na al Hakim)

Isipokuwa inajuzu kuiswali wakati wowote isipokuwa nyakati za karaha. Maamuma wakifuatisha takbira nyuma ya Imamu kwa kufuata takbira yake.

4. Yanayosuniwa kabla yake:

Ni sunna kwa Imamu kuitangaza Swala hiyo kabla ya siku yake kwa siku kadhaa, na awahimiza watu wafanye toba kutokana na maasi na waache dhuluma, wafunge saumu, watoe sadaka na waache ugomvi kati yao kwani maasi ndio sababu ya ukame kwa vile kumtii Allah (s.w.) ndio sababu za kheri na baraka.

5. Namna ya Kuswali

Imamu anatoka na watu kuelekea pahala ambapo umepangwa kuswalia Swala hiyo na kuswali na wataswali rakaa mbili huku akitoa takbira - akipenda, katika rakaa ya kwanza mara saba (7) na rakaa ya pili mara tano (5) kama vile Swala ya *Idd*, na atasoma kwa sauti katika rakaa ya kwanza *Sabbihis 'ma Rabbikal A'ala* baada ya *al-Fat'ha*, na katika rakaa ya pili atasoma *Hal-Ataaka Hadithul-Ghashiya*. Kisha atawaelekea watu na atatoa hotuba na kufanya toba kwa wingi, kisha ataomba dua na watu wakiitika Amin. Kisha anaelekea *Kibla* na ataigeuza nguo yake kulia kushoto na kushoto kulia na watu wote watafanya hivyo kisha wataomba kwa muda wa karibu na saa moja hivi halafu wataondoka. Ni kwa kauli ya Abu Huraira رضي الله عنه:

“Ametoka mjumbe wa Allah ﷺ Akaomba mvua akaswali nasi rakaa mbili bila ya Adhana wala Iqama. Kisha akatuhutubia na akamuomba Allah, tukageuza nyuso zetu kuelekeza Kibla hali ya kuinua mikono yetu, kisha akageuza nguo ya kujitanda na kuifanya kulia kushoto, na kushoto kulia.” (Abu Dawuud, Imam Ahmad na Ibn Majah na Al-Bayhaqi)

6. Baadhi ya Matamshi Katika Dua

Imepokewa kuwa Mtume ﷺ alipotaka kuomba mvua alisoma dua ifuatayo:

“Allahumma Asqina- Ghaythan Mughiythan Mariian Marii'an Ghadqan Mujalalan Twabaqan Saha- Da-iman. Allahumma Asqina- Ghaythan Wala Taj-'alna- Minal Qa-nitwiyna.

((اللَّهُمَّ اسقنا غيثًا مغيثًا مريعا غدقا مجللا عاما طبقا سحا دائما. اللَّهُمَّ اسقنا الغيث ولا تجعلنا من القانطين. اللَّهُمَّ بالعباد والبلاد والبهائم والخلق من اللأواء، والجهد والضعف ما لا نشكوه إلا إليك. اللَّهُمَّ أنبت لنا الزرع وأدر لنا الضرع، واسقنا من بركات السماء، وأنبت لنا من بركات الأرض. اللَّهُمَّ ارفع عنا الجهد والجوع والعري، واكشف عنا من البلاء ما لا يكشفه غيرك. اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْتَغْفِرُكَ، إِنَّكَ كُنْتَ غَفَّارًا، فَأَرْسِلْ السَّمَاءَ عَلَيْنَا مَدْرَارًا. اللَّهُمَّ اسق عبادك وبهائمك، وانشر رحمتك، وأحي بلدك الميت))

Allahumma Bil-'Ibadi Wal Bila-di Wal-Baha-imi Wal-Khelqi Minal-Aawai, Wal-Jahdi Wa Ddhanki Ma-lanashkuwuhu illa ilayka, Allahumma A-nbati Lana- Azzar'a wa Adirra Lana Ddhar'a Was'qina- Min Barakati Ssamai Waanabiti Lana Min Barakatil-Ardh. Allahuma Ir-fa'a 'anna Al-Juhda Wal-Ju'a Wal-'ara, Wak-Shif 'anna Minal-Balai Mala Yakshifuhu Ghayruka. Allahuma Inna Nas-taghfiruka Innaka Kunta Ghaffara-, Farsili Ssama- Alayna Mid-ra-ra. Allahuma Asqi Iba-daka Wa Baha-imaka Wanshur Rahmatoka Wa-ah-yi Baldaka Al-Mayyit." (Ibn Majah na Abu Dawuud)

"Ewe Mola tunakuomba mvua yenye kuokoa, matone manene na membamba, yenye kuendelea na tukufu, yenye kuenea na kutiririka daima, Ewe Mola tunyeshee mvua na usitufanye wenye kukata tamaa. Ewe Mola tunakuomba kwa waja na kwa wanyama na kwa nchi na kwa viumbe, na kwa tabu zetu na dhiki zetu tunakushitakia wewe tu. Ewe Mola tuoteshee mazao na tububujishie chuchu, na utunyeshee baraka za mbingu na za ardhi. Ewe Mola tuondoshee dhiki, njaa na utuondoshee balaa na hakuna awezae isipokuwa Wewe. Ewe Mola tunakuomba msamaha, wewe ni msamehevu, tuteremshie mvua yenye kuendelea mbinguni. Ewe Mola nyeshea waja wako na wanyama wako, na eneza rehema zako, na huisha nchi yako iliyokufa."



Pia imepokewa kuwa Mtume ﷺ mvua inaponyesha alikuwa akisema:

اللَّهُمَّ سَقِيَا رَحْمَةً وَلَا سَقِيَا عَذَابًا، وَلَا بَلَاءً، وَلَا هَدْمًا وَلَا غُرْقًا. اللَّهُمَّ عَلَى
الضَّرَابِ وَمَنَابِتِ الشَّجَرِ. اللَّهُمَّ حَوَالَيْنَا وَلَا عَلَيْنَا.

*“Allahumma Saqya- Rahma Wala saqya Adhabi, Wala Bala-in
Wala Hadmi Wala Gharaq, Allahumma Ala Ddhira-bi Wamana-
biti Sshajar. Allahumma Hawaaliyna Wala- ‘Alayna.”* (Al-Bukhari,
Muslim na Shafii)



Mada ya Tisa
Hukumu ya Jeneza
Somo la Kwanza

Mambo yanayotakiwa pindi Muislam
Anapougua mpaka Kufa kwake

1. Subira:

Muislamu anapopatwa na tatizo lolote lile anatakiwa kusubiri asighadhibike na wala asionyesha huzuni kwani Allah (s.w.) na Mtume ﷺ wameamrisha subira katika aya na hadithi. Ijapokuwa hakatazwi mtu anapoulizwa kuhusu hali yake akisema:

“Mimi ni mgonjwa au ninahisi uchungu, na nina maumivu, *“Al-Hamdulillah Ala Kulli Hali.”* الحمد لله على كل حال

2. Ni Sunna Kupata Matibabu.

Muislamu anapokuwa mgonjwa anawajibika kujitibu kwa dawa za halali, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika Allah (s.w.) Hakuteremsha ugonjwa isipokuwa ameteremsha na dawa yake basi jitibieni.” (Al-Hakim katika Mustadraq).

Zingatia kujitibu kwa dawa za haramu ni jambo linalokatanzwa kama vile pombe, nguruwe na mfano wake kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Allah (s.w.) Hakujaalia tiba yenu katika vitu alivyoviharamisha.”
(Al-Bayhaqi)

3. Uhalali wa “Istisqai”.

Unaruhusiwa kujitibu kwa kujisomea au kunywa au kujipaka *Qur-aan*. Inajuzu

kwa Muislamu kufanya “*Ruqya*” kwa kutumia aya za *Qur-aan* na dua alizofundisha Mtume ﷺ na maneno mazuri kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Hakuna ubaya kwa Ruq’ya kama hakuna shiriki.” (Muslim)

4. Matumizi ya Hirizi na Azima.

Ni haramu kwa Muislamu kuvaa na kutumia hirizi au azima kwa namna yeyote ile maana kufanya hivyo ni aina moja ya ushirikina kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Kwa hakika mwenye kuvaa hirizi, Hakika amefanya shiriki”.
(Imam Ahmad)

Na kwa kauli yake nyingine.

“Allah (s.w) hatimizi shida za aliyevaa hirizi na mwenye kuvaa azima, Allah hamuondolei chochote aliyevaa azima.” (Al-Hakim)

Na kauli yake Mtume ﷺ pale alipomuona kipofu mmoja anakitambaa cha njano kakifunga mkononi mwake:

“Kwanini umefanya hivi? Akasema: Hii ni kutokana na “Wahina” tatizo lililonikuta. Mtume ﷺ akasema: “Ivue kwani Allah (s.w.) Hatakuzydisha isipokuwa matatizo tu na kama utakufa umejifunga hautafanikiwa milele.” (Ibn Majah)

5. Baadhi ya Tiba za Mtume ﷺ:

Upo wakati Mtume ﷺ alikuwa akiweka mkono wake mtukufu juu ya mgonjwa na kusoma:

اللَّهُمَّ رَبَّ النَّاسِ أَذْهَبِ الْبَاسَ اشْفِ أَنْتَ الشَّافِي. لَا شِفَاءَ إِلَّا شِفَاؤُكَ شِفَاءَ لَا
يُغَادِرُ سَقَمًا.

*“Allahumma Rabba Nna-sa Adh-Hibil Ba’asa, Ash-fi, Anta Ssha-fiy.
La- Shifaan illa Shifa- uka Shifaan La- Yugha-diru Suqma.”* (Al-Bukhari)

Minhajil Muslim

“Ewe Mola wa watu ondosha mabaya, ponyesha wewe ndie mponyeshaji. Hakuna ponyo isipokuwa ponyo yako, ponyo lisiloacha ugonjwa.”

Wakati mwingine Mtume ﷺ alimueleza aliyekuwa akisikia maumivu:

“Weka mkono juu ya sehemu inayokusumbua katika mwili wako na usome: “Bismillahi kisha usome:

أعوذ بالله وقدرته من شرّ ما أجد وأحاذر.

“A’udhubillahi Wa Quدراتihi Min Sharri Ma Ajidu Wa Uhadhiru.”

Najilinda kwa Allah na kwa kudura yake katika shari ninayopata na ninayoigopa” Mara saba. (Muslim)

Imamu Muslim amepokea kuwa Mtume ﷺ aliugua na Jibril akamfanyia ruqya kwa kumsomea:

بسم الله أرقيك من كل شيء يؤذيك، من شر كل نفس، أو عين حاسد، الله يشفيك بسم الله أرقيك.

“Bismillahi Ar-Qiyka Min Kulli Shay’in Yu’udhiyka, Min Sharri Kulli Nafasi Au ‘Aynin Ha-sidin, Allah Yash-Fiyka Bismillahi Ar’qiyka.”

“Kwa jina la Allah nakutibu katika kila kitu chenye kukuudhi na kukusumbua na kwa shari ya kila pumzi au jicho lenye kuhusudu, Allah akuponye na kwa jina lake nakutibu” (At-Tirmidhi na Ibn Majah)

6. Ruhusa ya kutibiwa na Mwanamke au mtu kafiri.

Wamekubaliana wanazuoni wa Kiislamu juu ya ruhusa ya mtu kutibiwa kwa kafiri (kama ni muaminifu) pia kujitibu kwa mwanamke au mwanamke kwa mwanamume katika hali za dharura. Kwani Mtume ﷺ

“Aliwatumia baadhi ya Mushrikina katika baadhi ya mambo na wake wa masahaba walikuwa wakiwatibu majeruhi katika jihadi enzi ya Mtume ﷺ” (Al-Bukhari)

7. Ruhusa ya kuwazuia watu kwa sababu za kiafya.

Katika Uislam ni sunna kuwatenga na au kumtenga mtu aliye na ugonjwa unaoambukiza kwa urahisi kutoka mtu hadi mtu mwingine na kuzuiliwa wale walio wazima kukutana nao isipokuwa wauguzi wao tu kwa kauli yake Mtume ﷺ kuhusiana na maradhi ya **Tauni**:

“Utakapotokea ugonjwa wa Tauni katika mji nanyi mpo humo basi msitoke na kama ukitokea ugonjwa huo nanyi hampo msiingie.” (Imam Ahmad)

Ama kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakuna kuambukiza wala athari ya mkosi.” (Muslim)

“La Ad’wa Wala Twiyara.” (Muslim).

Maana hakuna kuambukiza kunakoathiri wenyewe isipokuwa ni kwa kutaka kwake Allah (s.w.) kwani hakiwezi kutokea kitu asichokitaka Allah (s.w.) katika milki yake.

Na hili halimzuii mtu kuzifuata njia za kujikinga na maradhi pamoja na kuamini kuwa hakuna anaye kinga isipokuwa Allah (s.w.). Bila shaka jambo ambalo Allah (s.w.) hajalikinga mwanadamu hawezi kuswalimika nalo. Mtume ﷺ alipatwa kuulizwa kuhusu ngamia aliyeambukizwa ugonjwa pale alipochanganyika na ngamia mgonjwa, Mtume ﷺ akauliza pia:

“Ni nani aliyemuambukiza yule ngamia wa kwanza”? (Al-Bukhari na Muslim)

Kisha akasema:

“Athari zatokana na Allah Peke Yake analotaka huwa na asilotaka haliwi.”

8. Wajibu wa Kumzuru Mgonjwa.

Ni wajibu kwa Muislamu kumtembelea nduguye Muislamu wakati akiwa mgonjwa kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mlisheni mwenye njaa na mtembeleeni mgonjwa na msameheni mwenye makosa - mateka.” (Al-Bukhari)

Na sunna kwa mtu atakae mtembelea mgonjwa kumwomba dua apona, na amuusie subira na amuambie maneno yanayofurahisha na yanayotia moyo, na ni vizuri pia asikae muda mrefu kwa mgonjwa. Wakati wote Mtume ﷺ alipokuwa anamtembelea mgonjwa alimwambia,

“Hakuna matatizo, kuwa tohara Inshaallah.” (Al-Bukhari)

Basi ni wajibu kwa Muislamu kumfariji hivyo ndugu yake.

9. Wajibu wa kuwa na dhana nzuri kwa Allah (s.w.)

Ni wajibu kwa Muislamu anapokuwa mgonjwa wakati wote awe na dhana nzuri kwa Allah (s.w.) kuwa Allah (s.w.) atamuhurumia na hatamuadhibu na atamsamehe na hatafatilia makosa yake na kuwa Allah (s.w.) ni msamehevu sana na huruma yake imeenea kwa kila kitu. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Asife mmoja wenu bila ya kuwa na dhana nzuri kwa Allah (s.w.).” (Muslim)

10. Kumlakinia Maiti.

Muislamu anapobaini *usakara* kwa nduguye aliye mgonjwa, yu katika hali ya kukata roho bora atamke لا إله إلا الله, “*La- ila-ha Illa Llah.*” Na akariri neno hilo mara kwa mara ili mgonjwa alikumbuke na alitaje, Endapo atafanikiwa kulitaja na kuwa ndio neno lake la mwisho basi litamuondolea magumu mengi na endapo mgonjwa atazungumza maneno mengine basi wewe rudia neno hilo kwa kutaraji kama litakuwa ndilo neno lake la mwisho” لا إله إلا الله, “*La- ila-ha Illa Llahu*” akifanikiwa kutamka basi ataingia peponi kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Walakinieni mauti wenu neno لا إله إلا الله , La-ila-ha illa Llah.”
(Muslim)

Na kauli yake ﷺ:

“Yule atakayetamka لا إله إلا الله , “La-ila-ha Illa Llah” likawa ndio tamko lake la mwisho basi ataingia peponi.” (Imam Ahmad na Abu Dawuud)

11. Kuelekezwa Kibla mgonjwa anayekata roho.

Ni vizuri kwa mtu aliyefikiwa na hali ya mwisho wa maisha yake akelekezwa Kibla hali ya kuwa amelalia ubavu wake wa kulia. Kama haiwezekani basi alazwe chali na miguu yake ielekezwe Kibla na hali ya *Sakaratil Maut* ikizidi sana basi asomewe *Surat Yasin*. Kwa kutaraji Allah (s.w.) atampunguzia uchungu kwa utukufu wa sura hiyo, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Wasomeeni mauti wenu *Yasin*.” (Abu Dawuud na An-Nasai).

12. Kufumba macho ya aliyefariki na kumfunika nguo.

Ni wajibu kuyafumba macho ya Muislamu aliyefariki na kumfunika vizuri kwa nguo kuanzia kichwani kwake hadi miguuni. Na mahala hapo pasisemwe neno isipokuwa la kheri,

اللهم اغفر له اللهم ارحمه

“Allahumma Gh-fir Lahu Allahumma R-hamhu.”
“Ewe Mola msamehe na umrehemu”

Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mtapokuwepo mahali alipo mgonjwa au maiti basi semeni yaliyo ya kheri kwani Malaika huitikia Amin kwa hayo mnayoyasema.”
(Abu Dawuud, At-Tirmidhi na Ibn Majah)

Abu Salama alipofariki Mtume ﷺ aliingia kwake na kukuta macho yake macho yake yako wazi alipofariki na akayafumba kisha akasema:

“Roho inapotolewa hufuatiliziwa na macho” (Muslim na Ibn Majah)

Hapo walianza kulia baadhi ya watu wa familia yake, Mtume ﷺ akawaambia,

“Msijiombee juu ya nafsi zenu isipokuwa kheri kwani malaika wanaitikia Amin kwa hayo mnayoyasema.” (Muslim).

Somo la Pili

Baada ya Muislam Kufariki Mpaka Kuzikwa kwake

1. Kutangaza Kifo Chake.

Ni sunna kutangaza kifo cha Muislamu kwa ndugu zake wa karibu, rafiki na watu wema katika mji ule ili wahudhurie mazishi yake. Hakika alitangaza Mtume ﷺ habari za kifo cha Najashi alipokufa, pia alitangaza kifo cha Zayd bin Harith, Jaafar na ‘Abdillah bin Rawaha رضى الله عنه walipokufa mashahidi. Ama matangazo yanayokatazwa ni ya kutangaza mabarabarani na katika milango ya Misikiti kwa sauti ya juu na kelele mambo ya Mfano huo ndio yanayokatazwa kisheria.

2. Kurombokeza na ruhusa ya kulia.

Ni haramu kurombokeza na kupiga kelele Muislamu anapofariki. Kwani Mtume ﷺ amesema:

“Hakika maiti anaadhibiwa kwa kilio (kurombokeza) cha aliye hai.” (Al-Bukhari na Bayhaqi)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Yule ambaye watu wamerombokeza katika kufa kwake basi naye aadhibiwa kwa kurombokezewa.” (Al-Bukhari na al Bayhaqi)

Na Mtume ﷺ alikuwa anachukua ahadi kwa wanawake wasirombokeze,

amesema Ummu Atwiyah رضى الله عنها na akasema Mtume ﷺ:

“Mimi nimejitenga mbali na anayepiga kelele na anayenyoa nywele, na anayepasua nguo kwa kufiwa” (Imam Ahmad).

Ama kulia hakukatazwi kutokana na kauli ya Mtume ﷺ pale alipofariki mtoto wake Ibrahim:

“Hakika jicho linatoa machozi na moyo unahuzunika na hatusemi ila yanayomridhisha Mola wetu, nasi kwa kufarikiana nawe Ibrahim tumehuzunika.” (Al-Bukhari)

Na alilia Mtume ﷺ alipopata habari za kifo cha Umama bint wa bint yake Zainab na akaambiwa Ee! Mtume wa Allah unalia? Je haujakatazwa kulia? Akasema,

“Kulia ni huruma ambayo Allah (s.w.) ameiweka ndani ya nyoyo za waja wake, na Allah (s.w.) anawahurumia waja wake wenye huruma.” (Imam Ahmad).

3. Mavazi baada ya kufiwa.

Ni haramu kwa mwanamke wa Kiislam kujizuia na mapambo kwa zaidi ya siku tatu baada ya kufiwa, isipokuwa kama atafiwa na mume wake kwa sababu hapo anawajibika kujizuia miezi minne na siku kumi, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwanamke asijizuie na mapambo baada ya kufiwa kwa zaidi ya siku tatu isipokuwa kwa kufiwa na mumewe hakika anatakiwa ajizuie miezi minne na siku kumi.” (Muslim, Abu Dawuud na An-Nasai)

4. Kulipa Madeni.

Inatakiwa ndugu wafanye haraka kumlipia madeni ndugu yao aliyefariki kama yapo. Kwani Mtume ﷺ alikuwa akijizuia kumswalia maiti anayedaiwa mpaka deni lake ilipwe na akasema:

“Nafsi ya muumini hutungikwa kwa deni lake mpaka lilipwe.”
(At-Tirmidhi, Ibn Majah na al-Hakim)

5. Kutamka Inna lillah na Kuomba Dua, na Subira.

Subira kwa watu waliofiwa ni jambo linalosisitizwa sana katika nyakati za msiba hasa siku za mwanzo. Mara tu baada ya kufariki mtu. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Kwa Hakika subira ni pale tu mwanzoni mwa msiba.” (Al-Bukhari)

inatakiwa muislamu azidishe dua na kauli za kurejea kwa Mola (s.w.), kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakuna mtu anayepatwa na msiba na kisha akasema Inna Lillahi Wa Inna Ilayhi Ra-jiun, Allahumma Ajirniy Fiy Muswibatii Wakh-luf Liy Khayran Minha, isipokuwa atalipwa na Allah (s.w.) katika msiba wake huo na atampatia badala iliyo bora zaidi.” (Imam Ahmad)

Na kauli yake Mtume ﷺ Amesema Allah (s.w.) katika hadithi Qudsy:

“Hakuna kwa mja wangu muumini malipo bora kutoka kwangu pale ninapomchukulia mpenzi wake duniani kisha akasubiri isipokuwa pepo.” (Ad-Darimi)

6. Wajibu wa Kumkosha.

Atakapofariki Muislamu iwe mtoto mdogo au mtu mzima ni wajibu kwa Waislamu wenzake kumuosha. Sawa sawa kiwiliwili chake kimekamilika au ni sehemu tu, na ambaye haoshwi katika maiti za Waislamu ni shahidi wa vita ambaye ameuawa na makafiri katika viwanja vya *jihad* kwa ajili ya Allah (s.w.), kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Msiwaoshe kwani kila jeraha au kila tone la damu litanukia kama miski siku ya kiama.” (Imam Ahmad)

7. Namna ya Kumuosha Maiti.

Kama maji yatamwagwa juu ya mwili wa maiti na yakaenea mwili wake wote inatosha hivyo kuwa ameoshwa. Lakini sifa iliyosuniwa ya kumuosha maiti ni:

kuwekwa juu ya kitu kilichonyanyuka na asimamie kumuosha kwake mtu muaminifu tena mwema kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Na wasimamie kuosha maiti wenu wale walio miongoni mwenu waaminifu.” (Ibn Majah)

Kisha kamua tumbo lake pole pole ili kutoa uchafu kama upo. Wakati wa kumuosha afunge kitambaa mkononi mwako na atie nia ya kumuosha. Kisha asafishe utupu wake akiondoa uchafu kisha aondoe kitambaa na umtawazishe kama udhu wa Swala, kisha ukioshe kiwiliwili chote ukianza juu kuelekea chini akiosha mara tatu tatu, akihisi bado hajasafika amuoshe mara tano tano. Na aweke katika joshu la mwisho sabuni au mfano wake.

Kama ni mwanamke afumuliwe nywele zake na zioshwe vizuri kisha zisukwe tena kwani Mtume ﷺ aliamrisha hivyo,

“Kwenye nywele za binti yake. Kisha awekwe manukato mazuri na mfano wake.” (Al-Bukhari)

8. Kama itashindikana Kuoshwa.

Ikitokea kuwa hakuna maji kwa ajili ya kumuoshea maiti au amefariki mtu kati ya wanawake au mwanamke kati ya wanamume atafanyiwa basi tayamamu kisha ativikwa sanda, ataswaliwa na kisha atazikwa.

Hiyo Tayamamu itakuwa imekua nafasi ya kuosha pale inaposhindikana kuosha. Hata mwenye janaba anaruhusiwa kutayamamu kama ameshindwa kuoga kwa udhuru na ataswali. Na hivyo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Atapofariki mwanamke akiwa kwa wanaume na hakuna mwanamke mwingine au amefariki mwanamume akiwa kwa wanawake na hakuna mwanamume mwingine basi watafanyiwa kutayamamu kisha watazikwa.” (Abu Dawuud)

Na hiyo hutumika pia panapokosekana maji.

9. Mmoja kati ya Mume au Mke Kumuosha mwenzake.

Inajuzu kwa mwanamume kumuosha mkewe aliyefariki, kwa mwanamke kumuosha mumewe aliyefariki kwa kauli ya Mtume ﷺ kwa Aisha رضي الله عنها :

“Kama ungelifariki ningalikuosha na ningekuvisha sanda.” (Ibn Majah. Imam Ahmad na An-Nasai) *Na kwa kuwa ‘Ali رضي الله عنه alimuosha Fatima رضي الله عنها.* (Al-Bayhaqi, Ad-Daraqutni na Imam Shafii)

Pia inajuzu kwa mwanamke kumuosha mtoto wa kiume mwenye umri usiozidi miaka sita, ama kwa mwanamume kumuosha mtoto wa kike asiozidi umri huo baadhi ya wanazuoni, wameona kuwa ni karaha.

10. Wajibu wa Kumvisha Sanda.

Ni wajibu kumtia maiti ndani ya sanda baada ya kuoshwa. Tena sanda inayositiri mwili wote. Alitiwa Sanda Mus’ab bin ‘Umair رضي الله عنه miongoni mwa mashahidi wa Uhud kwa shuka yake fupi, Mtume ﷺ :

“Akaamrisha wamfunike kwa sanda kichwa na mwili wake na wafunike miguu yake kwa majani ya Idh’khira. kitendo hiki ndio kimelazimisha kuwa ni wajibu kufunika mwili wote.” (Al-Bukhari)

11. Ni Sunna kutumia Sanda iliyo safi nyeupe hata kama ya zamani.

Kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Vaeni nguo zilizo nyeupe, kwani ni nguo bora na muwavishe pia maiti wenu.” (At-Tirmidhi na Abu Dawuud)

Ni Sunna pia kuifukiza sanda ubani na udi kwa kauli yake Mtume ﷺ :

“Mtapofukiza sanda ya maiti basi fukizeni mara tatu.” (Imam Ahmad)

Na ziwe shuka tatu kwa sanda ya mwanamume. Na tano kwa sanda ya mwanamke. Inasimuliwa kuwa baada ya kufariki kwake Mtume ﷺ alitiwa katika

shuka nyeupe aina ya Sahuli tena mpya na hapakuwepo kanzu wala kilemba. Isipokuwa aliyekufa hali yakuwa amehirimia Hijja mtu huyo sanda yake itakuwa ni zile nguo zake za Ihram. Shuka na nguo yake ya kujitanda basi wala hatiwi manukato wala hafunikwi kichwa chake ataachwa kama alivyokuwa na *Ihramu* zake kwa kauli ya Mtume ﷺ kuhusiana na mtu aliyeanguka toka juu ya mnyama wake siku ya Arafa na akafariki:

“Muosheni kwa maji mkunazi na fanyeni nguo zake mbili kuwa ndio sanda yake msimtie manukato na wale msifunike kichwa chake, kwani atafufuliwa hali mwenye kuitika Labayka siku ya kiama.” (Imam Ahmad)

12. Sanda ya Hariri.

Ni haramu kwa Muislamu kuzikwa nadani ya sanda ya hariri, kama ilivyo haramu kuvaliwa na Muislamu mwanamume. Ni haramu pia kuifanya sanda kwa mwanamke Muislamu pamoja ya kuwa halali kwake kuvaa hariri, wakati wa uhai wake lakini ni karaha kuzikwa ndani ya sanda ya hariri kwani ni *Israifu* (*matumizi mabaya ya mali*) na *Ghuluwwi* vilivyokatanzwa na *Sharia*. Imepokewa toka kwa Mtume ﷺ akisema,

“Sanda hata ikiwa ni ghali huisha haraka.” (Abu Dawuud).

Na amesema Abu Bakar رضي الله عنه:

“Hakika aliye hai ni bora zaidi kuvaa kitu kipya kuliko maiti, na sanda ni kwa muda tu ama saa na mfano wake vitachurizika tu kwa maiti.” (Al-Bukhari)

13. Kumswalia.

Kumswalia maiti Muislamu ni jambo la faradhi inayotosheleza wengine, kama vile kumuosha na kumtia sandani na kumzika watakapofanya hivyo baadhi ya Waislamu basi wengine wanasameheka. Kwa hakika Mtume ﷺ alikuwa anawaswalia maiti wa Kiislamu wakati hajajilazimisha kulipa madeni ya waumini. Alipofariki Muislamu na akaacha deni ambalo halijalipwa alikuwa akijizuia kumswalia na akisema: *“Mswalieni rafiki yenu.”* (Al-Bukhari)

14. Sharti za Kumswalia Maiti.

Yaliyo sharti katika Swala ya maiti ni sawa na baadhi ya masharti ya kawaida kama kuwa na tohara ya nguo na mwili na kujisitiri vilivyo sawasawa uchi na kuelekea qibla. Kwani Mtume ﷺ aliita kuwa ni Swala na akasema:

“Mswalieni rafiki yenu, kwa maana ni lazima ipewe hukumu za Swala katika sharti zake.”

15. Faradhi zake.

Kwanza ni nia ya kumswalia maiti, na kisha kusimama kwa anayeweza kwa kauli yake Mtume ﷺ: “Kwa *hakika amali huhesabiwa kutokana na nia.*” Ndani ya swala kwanza ni kusoma *Al-hamdu*, halafu kumswalia Mtume ﷺ kisha kumuomba dua na kisha kutoa salamu, swala ya maiti ni takbira nne na kutoa salamu.

16. Utekelezaji Wake.

Ni kuweka jeneza upande wa Kibla kisha Imamu atasimama na watu nyuma yake Safu tatu au zaidi. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Anayeswaliwa na safu tatu Hakika imethibiti.” (At-Tirmidhi)

Na utainua mikono yake huku akinuia Swala ya maiti au maiti wengi ukisema: *Allahu Akbar*, kisha asome *Al-Fatiha* au amsifu Allah (s.w.) kisha atoe *Takbira* kwa kunyanyua mikono yake akipenda au aiache kifuni na amswalie Mtume ﷺ swala ya *Ibrahimi* Kisha atoe takbira na aombe dua akitaka anaweza kutoa salamu au utatoa salamu baada ya *takbira* ya nne, salamu moja. Kutokana na yaliyopokelewa kuwa,

“Sunna katika swala ya jeneza ni kutoa takbira kisha kusoma Al-Fatiha baada ya takbira ya kwanza kimyakimya kisha kumswalia Mtume ﷺ na kumtakasia dua katika takbira nyingine na asisome chochote katika takbira hizo, kisha atoe salamu.” (Shafii)

17. Aliyechelewa katika Swala ya Maiti.

Aliyechelewa katika Swala ya maiti anayo hiari akitaka atalipa kilichompita katika Swala ya Imamu kwa kufuatisha *takbira* kwa mpangilio wake. Na akitaka atatoa salamu pamoja na Imamu kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa Aisha رضي الله عنها alipoeleza kuwa baadhi ya *Takbira* hazisikii, nae akamueleza: “*Ulichosikia kifuuate na kilichokupita huwajibiki kukilipa.*”

Hadithi hii ndio hoja ya rai hiyo iliyotumiwa na mtunzi wa kitabu Al-Mughni, lakini sikupata takriri ya hadithi.

18. Aliyezikwa bila ya Kuswaliwa.

Ikitokea muislamu akazikwa bila ya kuswaliwa, ataswaliwa kaburini kwake kwani Mtume ﷺ.

“Mama ambaye alikuwa akifanya usafi msikitini baada ya kuzikwa”, (Al-Bukhari)

Na wakamswalia masahaba nyuma ya Mtume ﷺ aliwahi kumswalia, si hivyo tu lakini sheria inakuruhusu pia waislamu kumswalia mtu aliyefariki mbali kwani Mtume ﷺ alimswalia Najashi hali ya kuwa amezikwa (uhabeshi) Ethiopia - Habasha, hali ya kuwa Mtume ﷺ na masahaba wake wakiwa Madina. (Ibn Abi Shayba)

19. Dua.

Mtume ﷺ amefundisha dua mbalimbali zikiwemo za kumuomba maiti, lakini muislam anaruhusiwa kuomba dua kwa namna yake ili mradi iwe ni dua inayokawidhi haja iliyo ndani ya sheria :

اللَّهُمَّ إِنَّ فُلَانًا ابْنَ فُلَانٍ فِي ذِمَّتِكَ وَحَبْلُ جَوَارِكَ فَقِهِ مِنْ فِتْنَةِ الْقَبْرِ وَعَذَابِ النَّارِ أَنْتَ أَهْلُ الْوَفَاءِ وَالْحَقِّ. اللَّهُمَّ فَاعْفِرْ لَهُ وَارْحَمْهُ فَإِنَّكَ الْعَفُورُ الرَّحِيمُ. اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِحَيَاتِنَا وَمَيِّتِنَا وَصَغِيرِنَا وَكَبِيرِنَا وَذَكَرْنَا وَأَنْثَانَا وَحَاضِرِنَا وَغَائِبِنَا . اللَّهُمَّ مِنْ أَحَبِّبْتَهُ مِنَّا فَأَحْبِبْهُ عَلَى الْإِسْلَامِ، وَمَنْ تَوَفَّيْتَهُ مِنَّا فَتَوَفَّهُ عَلَى الْإِيمَانِ. اللَّهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا أَجْرَهُ وَلَا تَضِلَّنَا بَعْدَهُ.

“Allahumma Inna Fulana Bin Fulani Fiy Dhimmika wa Habli Jiwaarika Faqih Min Fitnatil Qabri wa Adhabi Nna-ri, Wa Anta Ahlul-Wafai Wal-Haqq, Allahumma Faghfir lahu Wa R-hamhu Fainnakal-Gha-fuwru Rrahim. Allahumma Gh-fir Lihayyina Wa Mayyitina Waswaghiyrina Wakabiirina Wadhakarina Waunthana Waha-dhirina Wa Gha-ibina. Allahumma Man Ah’yaytahu Minna Fa Ahyihi Alal-Islam, Wa Man Tawaffaytahu Minna Fatawaffahu Alal-Iyman. Allahuma La Tah’rimna Aj’rahu Wala Tadhillana- Ba’adahu.”

“Ewe Mola kwa hakika fulani bin fulani yupo katika dhima yako na katika kamba ya ujirani wako, muepushe na fitna ya kaburi na adhabu ya moto, wewe ndie mtekeleza ahadi na haki, Ewe Mola mghufurie na umrehemu kwani wewe ni msamehevu mrahimu. Ewe Mola wangu waghufurie wahai wetu na maiti zetu, wadogo zetu na wakubwa zetu, wanaume miongoni mwetu na wanawake, waliokuwepo na wasiokuwepo. Ewe Mola wangu utakayemuacha miongoni mwetu mwacha katika Uislamu na utakayemfisha mfisha katika Imani. Ewe Mola Usitunyime malipo yake na usitupoteze baada yake”

Na kama maiti ni mtoto mdogo utaomba dua ifuatayo:

((اللهم اجعله لوالديه سلفا وذخرا وفرطا وثقل به موازينهم وأعظم به أجورهم، ولا تحرمنا وإياهم أجره ولا تفتنا بعده. اللهم ألحقه بصالح سلف المؤمنين في كفالة إبراهيم، وأبدله دارا خيرا من داره وأهلا خيرا من أهله، وعافه من فتنة القبر، ومن عذاب جهنم.))

“Allahumma Ij’al-hu Liwaaliday-hi Salafan wa Dhukhran wa Furutwan Wathaqqil Bihi Mawaziynahum Waa’adhim bihi Ujuurahum, Wala- Tahrinna- Wa Iyyahum Ajrahu Wala Taftinna Ba’adahu. Allahumma Al-Hiqhu Bi Swa-lihi Salafil-Mu’uminiyina Fi Kafa-lati Ibrahim Wa Abdil-hu Daran Khayran Min Daarihi wa Ahlan Khayran Min Ah’lihi Wa ‘Aafih Min Fitnatil-Qabri. Wamin ‘Adhaabi jahannam.” (Abu Dawuud, At-Tirmidhi, Ahmad, An-Nasai na Ibn Majah)

“Ewe Mola mjaalie ni kitangulizi na akiba kwa wazazi wake na zifanye nzito mizani za wazazi wake na yafanye mengi malipo yao, nna usitunyime pamoja nao malipo yake na usitufitini baada yake. Mwenyezi Mungu mkutanishe na wema na waumini, na mjaalie awe katika dhamana ya Ibrahim na umbadilishie nyumba iliyo bora kuliko nyumba yake na watu bora kuliko watu wake, na umuepushe na fitna za kaburi na adhabu ya moto”

20. Kwenda Kuzika na Ubora wake.

Ni sunna kwa Muislamu kwenda kwake pale anapokuwa Muislamu mwenzake, ni kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Mtembeleeni mgonjwa na nendeni mkazike kwani jambo hili litakukumbusheni Akhera.” (Muslim na Al-Bukhari).

Ni sunna kufanya haraka kwenda kumzika mtu aliyefariki kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Fanyeni haraka, ama ni la mtu mwema basi mharakisheni katika kheri yake, na kama sivyo hivyo basi ni shari mnayoiondoa kwenye mabega yenu.” (Al-Bukhari).

Pia imesuniwa kwenda mbele ya jeneza kwani alikuwa Mtume ﷺ na Abu Bakr na ‘Umar رضي الله عنه wakienda mbele ya Jeneza. Ama ubora wa jambo hili amelieleza Mtume ﷺ katika Hadithi yake hii:

“Atayelifuata jeneza la Muislamu kwa imani na kutaka radhi za Allah na akawa hapo mpaka likaswaliwa pia likamalizwa kuzikwa, basi atarejea na malipo sawa na Qirati mbili, na kila Qirati ni sawa na mlima wa Uhud, na atayeswalia kisha akarudi kabla ya kuzikwa basi atarudi na Qirati moja tu”. (Al-Bukhari)

21. Yaliyo Karaha Wakati wa Kusindikiza.

Ni karaha kutoka wanawake na jeneza kutokana na kauli ya Ummu ‘Atwiya:

“Tumekatazwa kufuata jeneza na haikufanywa ni Sharia kwetu sisi.” (Ibn Majah)

Pia ni karaha kunyanyua sauti kwenye jeneza kwa dhikri au kisomo au chochote, kwani walikuwa maswahaba wakichukia kunyanyua sauti katika mambo matatu:

“Wakati wa jeneza (kuzika), wakati wa kumtaja Allah, na wakati wa vita.” (Ibn al-Mundhir).

Pia ni karaha kukaa kabla ya jeneza kutuliwa chini toka mabegani. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Mtapofuata jeneza msikae mpaka liwekwe ardhini.” (Muslim)

22. Kumzika.

Kumzika maiti nako ni kuuficha mwili wake wote kwa mchanga ni *faradhi kifaya* kwa kauli ya Allah (s.w.) aliposema:

ثُمَّ أَمَاتَهُ فَأَقْبَرَهُ

“*Kisha akamfisha na akamtia kaburini.*” (Suratul Abasa: 21)

Na miongoni mwa hukumu za kuzika ni:

i). **Lifanywe kwa kina kirefu**, kinachozuia wanyama kufukua pia ndege wasifikie alipo maiti pia isiwezekane harufu kutokeza na ikaudhi. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Chimbeni na fanyeni kina na fanye Ihsani na zikeni wawili, watatu katika kaburi moja. Wakauliza ni yupi atayetangulizwa ee Mtume ﷺ wa Allah (s.w.)? Akasema, “Mtangulize aliye zaidi katika *Qur-aan*.” (Abu Dawuud, Imam Ahmad na Ibn Majah)

ii). **Iwekwe mwanandani (Lahdi)** katika kaburi kwani mwanandani ni bora pamoja na kuwa ‘*Shaq*’ inajuzu. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“*Na Allah’ di ni yetu na Al-Shaqi ni ya wasiokuwa sisi.*” (Imam Ahmad, Abu Dawuud na At-Tirmidhi)

(Katika Kiswahili tunaita mwanandani, lakini katika Kiarabu) *Allah’ di* ni kuchimba pembeni kuliani kwa kaburi. *Al-Shaqi* ni kuchimba katikati mwa kaburi.

iii). **Inasuniwa kwa aliyehudhuria maziko pale kaburini atupie mchanga** viganja vitatu kwa mkono wake upande wa kichwani kwa maiti. Kutokana na kitendo cha Mtume ﷺ kama alivyopokea Ibn Majah.

iv). **Aingizwe maiti tokea mwisho wa kaburi ikiwezekana na aelekezwe qibla** akilalia upande wake wa kulia na zifunguliwe kamba za sanda yake kichwani, kati na miguuni. Na aseme yule anayemuweka,

بِسْمِ اللَّهِ وَعَلَىٰ مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ

“*Bismillahi Wa Ala Millati Rasulillah ﷺ*”. Kwa kitendo cha Mtume ﷺ kufanya hivyo.” (Imam Ahmad)

v). **Lifunikwe kaburi la mwanamke kwa nguo wakati wa kumtia** katika mwanandani, kwani wanazuoni wa awali “*Salaf*” walikuwa wakifunika kaburi la mwanamke na wala sio la mwanamume.

Somo la Tatu

Wanayotakiwa kufanya baada ya mazishi

1. Kumtakia msamaha maiti na kumuomba dua.

Inapendeza kwa aliyehudhuria mazishi kumtakia msamaha maiti na kumwomba dua ya *taufiq* katika kuulizwa. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“*Muombeeni msamaha ndugu yenu na muombeeni tathbiit kwani yeye sasa hivi anaulizwa.*” (Al-Bukhari, Muslim na An-Nasai)

Alikuwa mtume ﷺ. Akisema hivyo baada ya kuzika na walikuwa baadhi ya *Salaf* (Waislamu wa mwanzo) wakisema:

اللهم هذا عبدك نزل لك، وأنت خير منزل به، فاغفر له ووسع مدخله

“Allahumma Hadha ‘abduka nazala bika, wa anta khayrun manzuwli bihi, Faghfir lahu wawassi’i madkhalahu.”

“Ewe Mola wangu wa haki huyu ni mja wako amefika Kwako na Wewe ndiye bora wa kufikiwa, msamehe na uyapanue maingilio yake.”

2. Kulitandaza Kaburi au Kuliweka Sawa.

Inatakiwa kuliweka sawa kaburi na ardhi kwa amri yake ﷺ kwa kuiweka sawa kaburi na ardhi isipokuwa inafaa kuliinua kaburi kiasi cha shubiri moja na wamelipenda hilo Jamhuri ya wanazuoni. Pia si vibaya kuweka alama juu ya kaburi kama vile jiwe ili ijulikane. Kwani Mtume ﷺ aliweka alama ya jiwe kaburi la ‘Uthman bin Madh’un Mungu amwie radhi na akasema: *“Ili nipate kujua kaburi ya ndugu yangu na nimzike atakae kufa katika ndugu zangu.”*

3. Uharamu wa Kupaka Rangi Kaburi na Kulijengea.

Ni haramu kulipaka rangi kaburi au kulijenga kwa alichokipokea Muslim kwamba Mtume ﷺ.

“Alikataza kupakaa rangi kaburi au kulijengea.” (Muslim na Abu Dawuud)

4. Uharamu wa Kukaa juu ya Kaburi.

Inakuwa *makruhu* kwa Muislamu kukaa juu ya kaburi la ndugu yake Muislamu au kuikanyaga kwa mguu wake. kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Laiti mtu angalikalia kaa la moto ikaunguza nguo zake na likapenya hadi kwenye ngozi yake ni bora zaidi kuliko kukaa juu ya kaburi.” (Al-Baihaqi)

5. Uharamu wa Kujenga Misikiti juu ya Makaburi.

Ni haramu kujenga misikiti juu ya kaburi na kuweka taa. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Amewalaani Allah (s.w.) Waliofanya kaburi za Manabii wao kuwa Misikiti.” (Al-Bahyaqi).

Amesema Mtume ﷺ:

“Mwenyezi Mungu amewalaani watembelea makaburi na ambao hujengea makaburi hayo misikiti.” (Al-Bukhari, Muslim na Ahmad)

“Mwenyezi Mungu amewalaani Mayahudi waliyofanya makaburi ya mitume yao misikiti.” (Al-Bukhari, Muslim na Imam Ahmad)

6. Uharamu wa Kufukua Kaburi na Kuhamisha Mifupa yake.

Ni haramu kufukua kaburi na kuhamisha mifupa ya wafu wake au kuwatoa maiti wenyewe isipokuwa kwa dharura kubwa vile kuwa amezikwa bila ya kuoshwa. Kama ambavyo ni makruhu kumhamisha maiti ambaye bado hajazikwa kumtoa kwenye mji kumpeleka kwenye mji mwingine ila itakapokuwa mji anaohamishiwa ni moja ya sehemu tukufu, Makka na Madina au *Baitil Maqdis* kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Wazikeni waliokufa katika sehemu walizofia.” (An-Nasai)

7. Sunna ya Kutoa Pole “Ta’azia”.

Inapendeza kuwapa pole wafiwa wakiwa wanamume au wanawake na hilo ni kabla ya mazishi na baada ya mazishi hadi siku tatu ila atakapokuwa mmoja wa watowa pole hayupo au yuko mbali si vibaya pole ikichelewa kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hapana muumini yeyote anayempa pole ndugu yake kwa msiba isipokuwa Allah humvalisha mtu huyo kipambo cha utukufu siku ya kiama.” (Ibn Majah)

8. Maana ya Kutoa Pole “Ta’azia”.

Ni kumtaka mtu kuvumilia na kuwafanya wafiwa wavumilie kwa kuwatajia mambo yatakayowapunguzia machungu na ukali wa huzuni. Na pole inatolewa kwa tamko lolote lile na katika yaliyopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ katika matamshi ya kutoa pole ni kauli yake Mtume ﷺ alipomwambia binti yake wakati alipomtumia habari kwamba mtoto wake amefariki. Mtume ﷺ akamtumia binti yake mjumbe kumpa salamu akamwambia:

“Hakika Allah (s.w.t.) Alichokichukua ni chake, na alichokitoo ni Chake, na kila kitu Kwake Yeye kina muda maalum basi na avumilie, na atake thawabu.” (Al-Bukhari)

Aliandika mmoja wa *Salaf* akimpa pole mwingine aliyefiwa na mwanaye akasema: “Kutoka kwa fulani kwenda kwa fulani, amani ikushukie hakika mimi namuhimidi Allah kwako, Allah ambaye hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Yeye ama baada ya hayo Allah ayafanye makubwa malipo yako na akuzindue na subira na aturuzuku kushukuru sisi na wewe kwani nafasi zetu na mali zetu ni katika vipawa vizuri vya Allah na viazimwa vyake vilivyowekwa akiba. Akustareheshe Allah katika hali nzuri na furaha na amuondoshe kwako pamoja na malipo makubwa. Tunakuombea rehema na huruma na uongofu ukitarajia kupata thawabu. Vumilia, ili malipo yako ya Kheri yasibatwilike kwa kufadhaika kwako ukaja ukajuta. Na fahamu kwamba kufadhaika hakuwezi kumrudisha mtu aliyekufa.

Na katika kutoa pole inatosha kusema:

أعظم الله أجرک، وأحسن عزاک وغفر لمیتک، آمین، أجرک الله، ولا أراک مکروها.

“A’adhimu Llahu ajraka, waahsin ‘izza-ka waghufira limayyitika, Amin, A-jaraka Llahu, Wala ara-ka makruwhan.”

“Allah ayafanye makubwa malipo yako na aifanye nzuri pole yako na amsamehe maiti wako. Atasema anayepewa Amin akukinge Allah wala asikuonyeshe jambo jingine lenye kuchukiza.”

9. Uzushi wa Matanga.

Na katika mambo yanayopasa kuwachwa na kujiepusha nayo ni mambo waliyoyazusha watu kwa sababu ya kutawaliwa na ujinga ambayo ni kukusanyika watu katika majumba kwa kisingizio cha kutoa pole na kupika vyakula na kutumia mali kwa kuonyesha ufahari.

Watu wema waliopita hawakuwa wakikusanyika katika majumba ya watu waliofiwa lakini walikuwa wakipeana pole huko makaburini na wanakutana sehemu. Si vibaya kwenda kumpa mtu pole nyumbani kwake endapo hakikuwezekana kukutana naye kaburini au pahala pengine Kwani kisichotakiwa ni mkusanyiko maalum ulioandaliwa makusudi kwa ajili hiyo.

10. Kuwatendea Wema Wafiwa.

Ni vizuri kuwatayarishia chakula wafiwa na wanaotakiwa kufanya hivyo ni watu wa karibu na wafiwa au majirani kwa ile siku ya kufiwa. Amesema Mtume ﷺ

“Watengenezeeni chakula familia ya Ja’far kwani wenzenu wamefikwa na jambo linalowashughulisha.” (Imam Ahmad, Abu Dawuud, At-Tirmidhi na Ibn Majah).

Ama ada ya wafiwa kuwatayarishia watu wengine chakula hilo ni jambo linalochukiza na lisilotakiwa. Kwa vile ni kuzidi kuwaongezea matatizo wafiwa. Na wafiwa wanapofikwa na mgeni ambaye ni lazima kumkaribisha basi ni vizuri majirani na watu wa karibu na wafiwa wafanya jambo hilo kumkaribisha mgeni badala ya kukaribishwa na wafiwa

11. Kumtolea Sadaka Maiti.

Ni vizuri kumtolea sadaka maiti kama alivyopokea Muslim kutoka kwa Abi Huraira kwamba mtu mmoja alimuuliza Mtume ﷺ:

“Ewe Mjumbe wa Allah hakika baba yangu amekufa na ameacha mali na hakuusia chochote je nikimtolea sadaka itamfutia makosa yake. Akasema Mtume, Ndiyo.”

Alipofariki mama yake Sa'ad bin Ubada - Allah awawiye radhi Sa'ad alimuuliza Mtume ﷺ akisema:

“Ewe Mtume wa Allah hakika mama yangu alifariki je nimtolee sadaka? Akasema Mtume ﷺ Ndiyo. Akauliza tena ni sadaka ipi iliyo bora zaidi”. Akasema Mtume ﷺ, “Ni kunywesha maji.”
(Imam Ahmad, An-Nasai na Ibn Majah)

12. Kumsomea Maiti Qur-aan.

Si vibaya kwa Muislamu kukaa msikitini na nyumbani kwake na akasoma *Qur-aan* na anapomaliza kusoma *Qur-aan* atamuomba Allah kumuomba maiti msamaha na kumtakia rehema kupitia kisomo hicho alichokisoma katika kitabu cha Allah Mtukufu.

Ama kukusanyika kwa ajili ya kusoma katika nyumba ile ya msiba na kuitoa thawabu hiyo ya kisomo chao kwa maiti na kulipwa kwa ajili ya hilo kutoka kwa wafiwa ni *Bid'aa* na ni jambo linalochukiza. Inabidi kuachwa na ndugu wote wa Kiislam na kukaa kando nalo, kwani waliotangulia katika Umma huu bora hawakufanya hilo. Kama halikuwa Dini kwa watu waliotangulia haliwezi kuwa Dini kwetu sisi hivi sasa kwa hali yoyote ile.

13. Hukumu ya Kuzuru Makaburi.

Kuzuru makaburi ni jambo zuri kwani jambo hilo linakumbusha akhera na linamnufaisha Maiti kwa kuombewa dua na kutakiwa msamaha. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Nilikuwa nimewakatazeni kuzuru makaburini. Kuanzia hivi sasa yazuruni hakika hayo makaburi yanawakumbusheni akhera.”
(Al-Hakim).

Amesema Mtume ﷺ:

“Mtu hasafiri kwa jambo la kufanya ziara ila safari yenyewe iwe ni kufanya ziara katika moja ya misikiti mitatu nayo ni: Msikiti wa Makka, na Msikiti wangu huu (Madina) na Msikiti wa Aqswaa.” (Al-Bukhari na Muslim)

14. Anayoyasema Anayezuru Makaburi.

Anatakiwa aseme mwenye kutembelea makaburi ya Waislamu vile alivyokuwa akisema Mjumbe wa Allah ﷻ wakati akiyatembelea makaburi ya *Baqii* nayo:

“Amani iwashukie watu wa nyumba hizi miongoni mwa waumini na Waislamu. Na sisi akitaka Allah tutakutana nanyi mmetutangulia na sisi tunawafuata. Tunamuomba Allah sisi na nyinyi msamaha. Ewe Mola wangu wa haki wasamehe. Ewe Mola wangu wa haki warehemu.” (Muslim)

15. Hukumu ya Kuzuru Makaburi kwa Wanawake.

Hawakutofautiana wanazuoni katika uharamu wa kwenda mara kwa mara kwa wanawake makaburini kwa ajili ya kuyazuru. Na hilo kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Amewalaani Allah wanawake wenye kutembelea makaburi”.

Ama kukikosekana kwenda mara kwa mara. Baadhi ya wanazuoni wamechukia kwa hali yoyote kutokana na hadithi iliyotangulia. Na baadhi nyingine wameruhusu kwa yaliyothibiti kwamba Aisha Allah awe radhi naye alitembelea kaburi la kaka yake ‘Abdul-Rahman. Ikabidi aulizwe kuhusu hilo na akasema:

“Ndiyo Mtume ﷺ alikuwa amekataza kuzuru makaburi kisha aliamrisha kuyazuru.” (Al-Hakim na Bayhaqi)

Na aliruhusu kwa wanawake kuzuru kidogo. Ameweka sharti ya kutotenda jambo baya kama vile kuomboleza makaburini au kupiga kelele au kutoka pasi na nguo za heshima au kumuita maiti na kumuomba shida zao, na mengineyo katika mambo yanayoonekana yakitendwa na wanawake wasiojua mambo ya Dini katika nyakati mbalimbali na sehemu mbalimbali.



Mada ya Kumi

Kutoa Zaka

Mada Tano: Somo la Kwanza

hukumu ya Zaka na hekima yake na hukumu ya anayezuia Kuitoa.

a) Hukumu ya Zaka.

Zaka ni fardhi ya Allah (s.w.) aliyowajibisha kwa kila Muislamu mwenye kumiliki kiwango cha mali moja. Na sharti zake amefaradhisha Allah katika kitabu chake kwa kauli yake:

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا

“Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombe rehema...” (Tauba 9:103).

Na kauli yake:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنفِقُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ

“Enyi mlioamini toweni katika vitu vizuri mlivyovichuma” (al-Baqarah 2: 267).

Na kauli yake:

وَاقْبُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ

“Dumisheni swala na toweni zaka.” (Muzammil 73: 20).

Na Mtume ﷺ amesema:

“Umejengwa Uislamu juu ya mambo matano: 1). Kukiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na Muhammad ni Mjumbe wake. 2). Na kudumisha Swala. 3). Na kutoa zaka. 4). Na kufunga mwezi wa Ramadhani. 5). Na kuhiji Al-Kaaba.” (Al-Bukhari na Muslim)

Na kauli yake:

“Nimeamrisha nipigane na watu mpaka wakubali kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na kwamba Muhammad ni mjumbe wake, na wadumisha Swala, na watoe Zaka, wakifanya hivyo watakuwa wamezikinga nami damu zao na mali zao isipokuwa kwa haki ya Uislamu na mahesabu yao yapo kwa Allah.” (Al-Bukhari, Muslim na An-Nasai)

Na kauli yake katika usia aliompa Mu’adh wakati anampeleka Yemen:

“Hakika wewe unawaenda watu ambao ni Manaswara hivyo walinganie kwenye kukubali kwamba hapana Mola apaswaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah (s.w.) na kwamba mimi ni mjumbe wa Allah (s.w.) wakikusikiliza kwa hilo wafahamisha kwamba Allah Mtukufu amewafaradhisha sadaka katika mali zao utakayochukuwa kutoka kwa matajiri wao, na kupewa mafakiri wao, na wakikusikiliza kwa hilo tahadhari na mali zao zilizo nzuri na ogopa maombi ya mwenye kudhulumiwa kwani hakuna kizuizi kati ya maombi hayo na Allah (s.w.).” (Al-Bukhari na Muslim)

b) Hekima ya Zaka

Miongoni mwa hekima zake ni kama ifuatavyo:

1. Kuisafisha nafsi ya kibinadamu na tabia chafu ya ubahili na uchoyo na kuwa na pupa na mali na kuwa na tamaa.

2. Kuwaliwaza mafakiri, na kukidhi shida za wahitaji na wenye hali mbaya na wanyonge wasionacho.
3. Kuimarisha Maslahi ya kijamii ambayo maisha ya jamii na ubora wake vinakuwepo kwa kupatikana maslahi hayo.
4. Kudhibiti ulimbikizaji wa mali kwa matajiri, na wafanyabiashara, na wenye kazi ili zisibaki mali katika tabaka maalum, au zikiwa mali katika mzunguuko wa matajiri tu.

c) Hukumu ya Mwenye Kuzuia Kutoa Zaka.

Mwenye kuzuia Zaka kwa kupinga ulazima wake anakuwa amekufuru na mwenye kuzuia kutoa Zaka kwa ubahili pamoja na kukubali ulazima wa Zaka anakuwa mtu huyo amepata dhambi. Zaka itapasa kuchukuliwa kwa nguvu, pamoja na adhabu na apigana kwa kukataa kutoa Zaka apigwe mpaka afate amri ya Allah (s.w.) na atoe Zaka. Kwa kauli yake Allah Mtukufu:

فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَإِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ ۗ

“Wakitubia na wakadumisha swala na wakatoa zaka basi hao ni ndugu zenu katika Dini.” (Surat Ttauba 9: 11)

Na kauli yake, Mtume ﷺ:

“Nimeamrisha nipigane na watu mpaka wakubali kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume wake na wadumisha Swala na watoe Zaka wakifanya hivyo watakuwa wamezikinga damu zao na mali zao ila kwa haki ya Uislamu na hesabu zao ziko juu ya Allah.” (Al-Bukhari na Muslim)

Kama alivyosema Abu Bakr Swiddiq رضي الله عنه wakati alipopigana vita na waliokataa kutoa Zaka alisema:

“Naapa kwa Allah laiti wangeninyima ngamia mdogo waliokuwa wakimtoa kwa Mtume ﷺ Ningepigana nao kwa hilo.” (Al-Bukhari)

Na maswahaba walimuafiki Abu Bakr kwa hilo na likawa ni mapatano ya pamoja ya maswahaba.

Somo la Pili

Jinsi Mali Zinazopasa Kutolewa Zaka na Nyinginezo

a) Dhahabu na fedha

Dhahabu na fedha, na kinachokuwa na vinavyothaminiwa kwavyo miongoni mwa bidhaa za biashara na vinavyotiwa katika hukumu ya hizo, miongoni mwa madini na mali zilizozikwa zamani kabla ya Uislamu na zinazoweza kuwa badala yake katika nyaraka za mali kwa kauli yake Allah:

وَالَّذِينَ يَكْتُمُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ
فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٤﴾

“...Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu...” (Suratu Tauba 9: 34).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Haipasi zaka mali iliochini ya wakia 5”. (Al-Bukhari)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Wanyama wakiuumizana jeraha la yule aliyeumizwa halina fidia na kisima hakina fidia na madini hayana fidia na rikazi inatolewa moja ya tano” (Al-Bukhari).

b) Wanyama

Wanyama ni ngamia, ng’ombe, mbuzi na kondoo. Kwa kauli yake Allah Mtukufu:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنفُقُوا مِن طَيِّبَتِ مَا كَسَبْتُمْ

“Enyi ambao mmeamrisha toweni katika vizuri mlivyovichuma.” (Suratul Baqara 2: 267)

Na kauli yake Mtume ﷺ alipomjibu mtu aliyemuuliza kuhusu Hijra:

“Acha kuuliza habari hizo kwani mambo yake ni makubwa. Je unaye ngamia unayepasa kumtolea zaka?, Yule akasema, ‘ndiyo’, akasema Mtume ﷺ, fanya hivyo nyuma ya Bahari kwani Allah haachi chochote katika matendo yako.”

Na kauli ya Mtume ﷺ :

“Naapa kwa Mola ambaye hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila yeye hakuna mtu yeyote ambaye anamiliki ngamia au ng’ombe au mbuzi na kondoo akawa hawatolei zaka isipokuwa Allah siku ya kiama atambadilisha mnyama huyo atakuwa mkubwa kuliko alivyokuwa na atamkanyaga mmiliki na atampiga mapembe na kila anapofikia wa mwisho hurudiwa yule wa kwanza wao mpaka inamalizika hukumu kati ya watu wote.” (Al-Bukhari)

c) Matunda na nafaka

Nafaka ni kila chenye kuwekwa akiba chenye kuliwa kama vile ngano, Shairi, fiwi, kunde, njegere/maharage, dengi, mtama, mahindi, shairi isiyo maganda, mchele/mpunga. Ama matunda ni kama vile tende, zaituni na zabibu kwa kauli yake Allah Mtukufu:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنفُقُوا مِن طَيِّبَتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ

“Enyi ambao mmeamini toweni katika vitu vizuri mlivyovichuma na tulivyowatoleeni kutoka ardhini” (al Baqarah 2: 267).

وَأَتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ

“Na toweni zaka yake siku ya mavuno yake.” (Al-An-‘Aam 6: 141).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Haipasi Zaka kwa mali iliyo chini ya wasaki 5.” (An-Nasai na Al-Bahyaqi).

Na kauli yake ﷺ:

“Mazao yaliyonyeshelezwa kwa mvua au maji ya chemchem au pasi na kunyeshelwa, zaka yake ni moja ya kumi na mazao yaliyonyeshelewa kwa gharama, zaka yake ni nusu ya moja ya kumi.” (Al-Bukhari)

d) Mali Zisizopasa Kutolea Zaka Nazo ni:

1. Watumwa, farasi, nyumbu, punda. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Haipasi sadaka kwa mja, mtumwa, katika farasi wake na kijana wake, na kwamba Mtume ﷺ haikuthibiti kwake kuchukua sadaka ya nyumbu na punda katu.” (Imam Ahmad)

2. Mali ambayo haikufikia kiwango. Isipokuwa mmiliki wake akipenda kujitolea, kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Haipasi zaka kwa ngamia walio chini ya watano.” (Al-Bukhari na Muslim)

3. Matunda na mboga mboga. Kwani haikuthibiti kwa Mtume ﷺ kitu chochote kutolea Zaka katika hivyo, isipokuwa inapendeza kutoa chochote katika vitu hivyo kuwapa mafakiri na majirani kwa ujumla kwa kauli isemayo:

أَنْفِقُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ

“Toweni katika vitu vizuri mliyovichuma na tulivyowatoleeni kutoka ardhini.” (al Baqara 2:276)

4. Vipambo vya wanawake ambavyo madhumini yake ni kujipamba tu. Lakini kikikusudiwa kujipambia pamoja na kuweka akiba mpaka wakati wa kuhitajika hakika kipambo hicho kitapasa kutolewa zaka kwa kufanana na vitu vingine katika uwezekano wa kuwekeka akiba.
5. Mawe ya thamani kama vile Yakut na Lulu na kadhalika ila yatakapokuwa kwa ajili ya biashara. Kwa ajili hiyo itapasa kutolewa Zaka katika kima chake kama vile bidhaa za biashara.
6. Vifaa ambavyo vipo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ambavyo si kwa ajili ya biashara kama magodoro n.k. na vile vile majumba, viwanda na magari vitu hivyo havipasi kutolewa Zaka. Kwani haikutajwa Zaka yake katika sheria.

Somo la Tatu

Viwango vya mali zinazopasa kutolewa Zaka

Sharti za viwango vya mali zinazopaswa kutolewa zaka, na kiasi kinachopasa kutolewa Zaka.

a) Dhahabu na fedha na vyenye kufanana na dhahabu na fedha

1. **Dhahabu:** Sharti za Zaka yake ni kupitiwa na mwaka na kufikia kiwango. Na kiwango chake ni Dinari 20 na kinachopasa kutolewa katika kiwango hicho ni robo ya moja ya kumi na katika kila Dinari 20 inapasa kutolewa nusu Dinari na kitakachozidi kitapigiwa hesabu yake kikiwa kichache au kikiwa kingi.
2. **Fedha:** sharti yake ni kupitiwa na mwaka na kufikia kiwango kama kile cha dhahabu na kiwango chake ni Dirham 200 ambazo ni sawa Wakia (5). Na kinachopasa kutolewa katika kiwango ni robo ya moja ya kumi kama ilicyo katika dhahabu na katika kila Dirham mia mbili (200) inapasa kutolewa Dirham (5) kitakachozidi kitapigiwa hesabu yake.

3. **Mwenye kumiliki** sehemu katika dhahabu ambayo haikufikia kiwango na kiasi kingine cha fedha ambacho pia hakikufikia kiwango italazimu kukusanywa pamoja na zikifikia kiwango zitatolewa Zaka kwa pamoja na kila moja itahesabiwa kwa hesabu zake kwa ilivyo kwa kila moja. Ilipokewa kwamba Mtume ﷺ alikusanya dhahabu akaingiza kwenye fedha na fedha akaingiza kwenye dhahabu na akazitolea Zaka kwa pamoja kama ambavyo inatosheleza kutolea Zaka moja ya dhahabu na fedha kutolea mwenzake. Kwa ambaye imepasa kutoa Dinari inajuzu kwake kutoa Dirham kumi za fedha na kinyume chake pia kinafaa, kama ambavyo nyaraka za fedha hizi leo zinatolewa zaka ya dhahabu na fedha ambayo ni robo ya moja ya kumi wakati faida ya nyaraka za fedha za serikali zinatokana na dhahabu na fedha kwa ujumla.

4. **Bidhaa za biashara** na fedha kwa ujumla huuzwa papo kwa papo na kwa bei ya wakati ule au zitakuwa ni bidhaa zinazolimbikizwa kwa kungojea kupanda kwa bei. Basi zikiwa bidhaa za kuuzwa papo kwa papo na kwa bei ya wakati wake zitathaminiwa kwa kima cha pesa za mwanzo wa kila mwaka. Na zikifikia kiwango au hazikufikia, lakini mmiliki anazo pesa zingine itampasa azitolee Zaka kwa asilimia 2 1/2 katika mia. Na zinapokuwa bidhaa zinazolimbikizwa kwa kungojea kupanda kwa bei itapasa kuzitolea ile siku ya kuziua.

5. **Madeni:** mwenye kumdai mwenziwe na akawa na uhakika wa kulipwa deni lake wakati wowote atapotaka, itampasa mtu huyu kuliingiza deni hilo katika pesa au bidhaa na azitolee Zaka wakati zitapofikiwa na mwaka. Na kama hana pesa nyingine zaidi ya deni. Na hilo deni likawa linafikia kiwango, atatolea Zaka hivyo hivyo deni hilo. Na ambaye deni lake lipo kwa mtu asiyekuwa na uwezo. Asiyeweza kulipa wakati ule mdai anapotaka kulipwa atalitolea Zaka deni hilo siku atakayolipwa. Kwa mwaka mmoja japo itapita miaka mingi.

6. **Rikazi:** nazo ni mali zilizozikwa zamani kabla ya Uislamu. Atayekuta katika ardhi yake au nyumbani kwake mali iliyozikwa katika mali za zamani, inampasa mtu huyo kuitolea Zaka mali hiyo kwa kutoa moja ya tano ya mali hiyo kuwapa mafakiri na masikini na sehemu zinazotoa huduma kwa jamii. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Zaka ya Rikaazi ni moja ya tano.” (Al-Bukhari, Muslim na Abu Dawuud)

7. **Madini:** madini ya dhahabu au fedha atakitoa kile alichokipata kama kitafikia kiwango. Ni sawa kama umefika mwaka ama haukufika mwaka kwani kinachompasa kila anapotoa kiasi atakitolea zaka kama kitafikia kiwango.

Je madini hayo yatatolewa Zaka robo ya moja ya kumi au moja ya tano, kama mali ya chini (*Rikazi*)? Wametofautiana wanachuoni katika jambo hilo: Kuna aliyesema madini yatatolewa Zaka kwa moja ya tano wakiyafanisha na *rikazi*.

Na wengine wamesema, madini yatatolewa Zaka ya dhahabu na fedha wakichukulia ujumla wa kauli yake Mtume ﷺ:

“*Haipasi Zaka kwa mali iliyochini ya wakiya tano.*”

Na kauli hiyo Mtume ﷺ ya wakiya tano inakusanya madini na vinginevyo.

Na swala hili lina wasaa (pana) *Alhamdulillah*.

Ama madini yanapokuwa ni chuma au shaba au kibiriti au vitu vingine. Kinachopendeza ni kukitolea Zaka kilichotolewa (kilichovunwa kutokana na kima chake kwa asilimia mbili na nusu katika mia (2 1/2). Kwani hapakupokewa maandishi yaliyo wazi yanayoeleza kupaswa zaka katika madini, kwani hayo si dhahabu wala fedha ili ipaswe kutolewa Zaka.

8. **Mali iliyozalishwa kwa faida:** Mali hiyo itakapokuwa ni faida ya biashara au ni zalisho la mnyama mali itatolewa Zaka pamoja na Zaka ya asili yake. Wala haitaangaliwa kwenye kufikiwa na mwaka. Ama mali itapokuwa siyo faida ya biashara au si zalisho la mnyama. Mali hiyo itangojewa ifikie kiwango na izungukiwe na mwaka kisha itatolewa Zaka.

Na mwenye kuzawadiwa mali au akawa amerithi haitapasa zaka katika mali hiyo mpaka ipitiwe na mwaka.

b) Wanyama wanaochungwa na ambao ni halali kuliwa

1. **Ngamia:** Na sharti za Zaka yake ni kupitiwa na mwaka na kufikia kiwango. Na kiwango chake ni kuanzia ngamia watano (5) na zaidi kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Haipasi zaka kwa ngamia walio chini ya watano.” (Abu Dawuud, an-Nasai na Ibn Majah).

Na kinachopasa kutolewa katika ngamia watano ni mbuzi au kondoo aliyetimiza mwaka wa pili na akaingia mwaka wa tatu wawe katika mbuzi au kondoo wa mtoa Zaka mmoja. Na katika ngamia kumi ni mbuzi wawili na katika ngamia kumi na tano mbuzi au kondoo watatu, na katika ngamia 20, mbuzi au kondoo wanne, na katika ngamia 25 ngamia jike aliyetimia mwaka mmoja na kaingia katika mwaka wa pili na akikosekana, basi ngamia dume aliyetimiza miaka miwili na akaingia katika mwaka wa tatu, na wakifika ngamia 36 ni ngamia jike aliyefikia miaka miwili na kaingia mwaka wa tatu na wakifika ngamia 46 ni ngamia jike aliyetimiza miaka mitatu na kaingia mwaka wa wanne. Wakifika ngamia 61 ni ngamia jike aliyetimia miaka minne na kaingia mwaka wa tano. Wakifika ngamia 76 ni ngamia wawili majike waliotimia miaka miwili na kuingia mwaka wa tatu. Wakifika ngamia 91 wataopasa kutolewa ni ngamia wawili wa kike waliotimia miaka mitatu na kuingia mwaka wa nne. Na wakitimia ngamia 120 katika kila ngamia 40 atapaswa kutolewa ngamia wa kume aliyetimiza miaka miwili na kuingia wa tatu na katika ngamia 50 atakayepaswa kutolewa ni ngamia jike aliyetimiza miaka mitatu na kuingia mwaka wa nne.

Ufafanuzi

Mtu ambaye imempasa kutolea Zaka rika maalumu na akawa halipo. Itampasa kulitolea Zaka rika alilionalo kama likiwa na umri wa chini kuliko rika linalotakiwa na atamuongezea mkusanyaji Zaka, mbuzi au kondoo wawili au atamuongezea Dirham 20. Na litakapokuwa rika alilotoa ni kubwa kuliko linalotakiwa mkusanyaji Zaka atamuongeza wanyama wawili au Dirham 20 kwa kukamilisha ule upungufu. Isipokuwa ngamia dume mwenye miaka miwili na kuingia mwaka wa tatu anamtosheleza ngamia jike aliyetimiza mwaka mmoja na kuingia mwaka wa pili pasi na ziada kama tulivyozungumza huko nyuma.

2. Ng’ombe:

Sharti ya Zaka ya ng’ombe ni kufikia mwaka na kufikia kiwango kama ilivyo kwa ngamia, na kiwango chake ni kuanzia ng’ombe thelathini, anayepasa kutolewa katika kiwango hicho ni ng’ombe dume aliyetimiza mwaka mmoja na wakifika 40 anayepaswa kutolewa ni ng’ombe jike aliyetimiza miaka miwili. Wakiwa zaidi

basi kila (40) anatolewa ng'ombe jike wa umri wa miaka miwili na kila (30) ng'ombe mmoja dume aliyetimiza mwaka moja. Kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Kwa kila ng'ombe 30 atapasa kutolewa ng'ombe dume aliyetimiza mwaka mmoja na kila 40 ng'ombe mmoja aliyetimiza miaka miwili.” (Abu Dawuud na At-Tirmidhi)

3. Mbuzi na kondoo

Na sharti za Zaka yao ni kufikia mwaka, na kufikia kiwango, na kiwango chao ni kufikia mbuzi au kondoo 40 anayepaswa kutolewa ni mbuzi au kondoo mmoja jike aliyetimiza mwaka mmoja na akaingia katika mwaka wa pili. Na wakifikia mbuzi au kondoo 121 anayepaswa kutolewa ni mbuzi au kondoo wawili na wakifikia mbuzi au kondoo 201 na zaidi watakopaswa kutolewa ni mbuzi au kondoo 3. Wakizidi zaidi ya 300 atatolewa mbuzi mmoja katika kila mia kwa kauli yake Mtume ﷺ :

“Wakizidi katika kila mia atatolewa mbuzi mmoja.”

Ufafanuzi

i). Jamhuri ya wanavyuoni wameweka sharti katika wanyama wawe wanachungwa. yaani wawe wanachungwa sehemu kubwa ya mwaka katika malisho yasiyokuwa miliki ya mtu. Na Imamu Maliki Allah amrehemu hakuweka sharti la kuchunga katika kuwajibika Zaka na hilo ndio tendo la watu wa Madina. Na hoja ya jamhuri ni kauli ya Mtume ﷺ :

“Na katika mbuzi au kondoo wanaochungwa wakifikia arobaini anayepasa kutolewa ni mbuzi au kondoo jike aliyetimiza mwaka mmoja hadi kufikia mbuzi au kondoo mia moja na ishirini”.

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Na katika mbuzi au kondoo wanaochungwa.”

Ndimu walimotoa wanachuoni ushahidi wa sharti la kuchunga kwa maandiko hayo na kutumia ushahidi huo huo kwa ngamia na ng'ombe kwa vile

wanavyofanana na mbuzi na kondoo. Na wamesema kwamba: ugumu ulio katika gharama za kuwapatia chakula cha kununua unalazimisha kulizingatia sharti la kuchunga.

ii). Haitapasa Zaka kiwango kilicho kati ya viwango viwili kwa Zaka za wanyama. kwa hiyo anayemiliki mbuzi au kondoo arobaini anawajibika kumtoa mbuzi au kondoo mmoja tu, hadi kufikia mbuzi au kondoo mia na ishirini, na akizidi mmoja. Wakifikia mbuzi au kondoo 121 atoa mbuzi au kondoo wawili jike. Hivyo idadi iliyo kati ya 40 na 120 ndiyo inayoitwa kuwa kilicho kati ya viwango viwili kiwango ambacho hakitolewa Zaka. Na vivyo hivyo kwa Ngamia na Ng'ombe, na hiyo ni kutokana na Mtume ﷺ pindi alipotaja faradhi za Wanyama alikuwa akisema: *Ikifikia hivyo basi na itolewe kiasi kadha.*” ikafahamika kuwa idadi iliyopo baina ya faridha mbili haitolewi Zaka

iii). Katika zaka wanakusanywa pamoja: mbuzi na kondoo kwa vile ni jinsia moja. Na vile vile nyati na ng'ombe na ngamia wanaopatikana Arabuni (Wenye nundu moja) na wale wa *Kirusi (Kharasan)*, Ngamia wenye nundu mbili) kwa vile wote wanaingia katika tamko la jinsia yao. Katika kauli yake Mtume ﷺ:

“Na katika mbuzi au kondoo wanaochungwa wakifikia arobaini atapaswa kutolewa mbuzi au kondoo jike mmoja aliyetimiza mwaka mmoja na kuingia mwaka wa pili.”

Na kauli yake:

“Katika kila thelathini katika ng'ombe”.

iv). Watu wawili waliochanganya wanyama wao wakawa kila mmoja anamiliki kiwango na mchungaji wao akawa mmoja, na wakachunga pamoja na sehemu za kupumzikia wanyama wao ni moja na sehemu za kulala wanyama wao ni moja basi Zaka zao zitachukuliwa pamoja, kisha watarejesheana sawa sawa. Kwa mfano mmoja wao anamiliki mbuzi au kondoo arobaini na mwingine anamiliki themanini, na mkusanyaji Zaka akachukuwa mnyama mmoja katika wanyama arobaini, basi mwenye wanyama themanini atamrudishia mwenye wanyama arobaini theluthi mbili ya mbuzi. Wala haifai kukusanya makundi mawili ya wanyama yaliyokuwa mbalimbali kwa kukimbia kutoa zaka. Wala kuyatenganisha makundi mawili yaliyokuwa pamoja kwa madhumuni hayohayo ya kukwepa kutoa Zaka. Kama ilivyokuja katika barua aliyoundika Abu Bakr Allah amuie radhi:

“Wala visikusanywe vilivyokuwa vimetenganishwa na wala kutenganisha vilivyo pamoja kwa kuogopa zaka, na kilicho cha wawili waliochanganya mali zao watarudishiana sawa sawa.”
(Al-Bukhari)

v). Katika Zaka hakubali mtoto wa mbuzi/kondoo wala watoto wa ng’ombe wala watoto wa ngamia lakini watazingatiwa ni ngamia kwa kauli ya Umar - Allah amuie radhi - aliyomuelezea mfanyakazi wake wa kukusanya Zaka:

“Hisabu pamoja na watoto wao lakini usiwachukue.” (Malik)

vi). Katika Zaka hawachukuliwi wanyama wazee wala wenye dosari inayoweza kupunguza thamani yake, kwa kauli ya Abu Bakr - Allah amuie radhi: *“Katika Zaka hachukuliwi mnyama mzee wala mwenye chongo wala beberu”*. Kama ambavyo hazichukuliwi mali zilizo bora zaidi kama vile mnyama mwenye mimba anayekaribia kuzaa na ng’ombe dume na mbuzi/kondoo anayenenepeshwa kwa ajili ya kuliwa na mnyama anayefugwa kwa ajili ya maziwa. Kwa kauli yake Mtume ﷺ aliyomuambia Muadhi:

“Tahadhari na kuchukuwa mali bora za watu”. (Al-Bahyaqi)

Na kwa katazo la ‘Umar - Allah amuie radhi:

“Kwa mkusanya Zaka asichukuwe mnyama anayefugwa kwa ajili ya kuliwa na anayefugwa kwa ajili ya maziwa. Na mwenye mimba anayekaribia kuzaa na dume la mbuzi/kondoo.”

c) Matunda na Nafaka

Sharti la Zaka ya nafaka na matunda ni kukomaa - nako ni kuwa na rangi ya njano au nyekundu na kuchambuliwa tumba tumba na kuwa nzuri zabibu na zaituni kwa kauli yake Allah (s.w),

وَأَتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ

“Toeni zaka yake siku ya mavuno yake.” (Al-An’am 6: 141).

Na kiwango chake ni kuanzia wasiki tano na wasiki moja ni sawa na pishi sitini na pishi moja ni vibaba vinne kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Haipasi kutolewa zaka kilicho chini ya wasiki tano.”

Na kinachopasa kutolewa - ikiwa nafaka au matunda yananyeshelwa pasi na gharama kwa kupata maji kwa uwezo wake mmea au kwa njia ya chemchem na maji ya mito - ni moja ya kumi (1/10).

Na katika kila *waski* tano ni nusu *waski*. Na yakinyeshelwa kwa gharama kama kutumia ndoo na mashine, kitakachotolewa ni nusu ya moja ya kumi. Na katika *waski* tano kinachopasa kutolewa ni robo waski na kitakachozidi kitapigiwa hesabu yake kikiwa kichache au kingi; Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Kwa vile vilivyonyeshelwa na maji ya mvua na maji ya chemchem au kupata maji kwa njia ya kawaida kitakachotolewa ni moja ya kumi. Na vilivyonyeshelwa kwa kumwagiliwa kitachotolewa ni nusu ya moja ya kumi.” (Al-Bukhari na Imam Ahmad)

Ufafanuzi:

i). Anaenyeshelwa mimea yake kwa njia tofauti kama vile kuwa mara ananyeshelwa kwa kutumia vyombo na mara nyingine pasi na vyombo, kitachompasa kutoa ni robo tatu ya moja ya kumi. Hivyo ndivyo walivyosema wanachuoni. Amesema mwanachuoni Ibnu Qudama:

“Hatujui tofauti yoyote katika masuala hayo.”

ii). Zitakusanya pamoja aina tofauti za tendele zikifikia kiwango zitatolewa Zaka kwa aina ya kati yao, haitolazimika kutoa ile nzuri wala mbaya.

iii). Itakusanywa pamoja ngano na shairi na shairi isio na maganda katika zaka mkusanyiko wote huo ukifikia kiwango itatolewa Zaka ile ilio nyingi.

iv). Zitakusanywa pamoja aina zote za mboga za jamii ya nafaka kama vile fiwi, himmas, adesi, dengi n.k. na zikifikia kiwango cha Zaka itatolewa ile ilio zaidi.

- v). Kama itakusanywa aina zote za zabibu zikifia kiwango zaituni au fijili au uta. Zitatolewa Zaka mafuta yake.
- vi). Zitakusanywa aina za zabibu kama vitauzwa kabla hazijakauka zaka yake itatolewa katika thamani yake nayo ni moja ya kumi au nusu ya moja ya kumi kulingana na umwagiliaji.
- vii). Mchele, mahindi, uwele kila moja ni aina inayojitegemea hivyo hazikusanywi pamoja, na kama haikufikia kiwango aina moja kati ya hizo haitopasa kutolewa Zaka.
- viii). Mwenye kukodisha ardhi akailima na kikafikia kiwango alichokivuna itamlazimu kukitolea Zaka.
- ix). Mwenye kumiliki matunda au nafaka kwa njia yoyote ile katika njia za kumiliki kama ni kwa kupewa au kununua au kurithi baada ya kukomaa haitolei Zaka kwani zaka yake itakuwa ni kwa yule aliyeitoa au kuiuza, na kama alimiliki kabla ya kukomaa itamlazimu zaka huyu mmiliki wa pili
- x). Mwenye kudaiwa na likawa deni limemaliza mali yake yote au limepunguza kiwango hatolazimika mdaiwa huyo kutoa Zaka.

Somo la Nne

Wanaostahili kupewa Zaka

Pande zinazopewa Zaka ni nane. Allah katika kitabu Chake Kitukufu Amesema:

﴿ إِنَّمَا الصَّدَقَتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسْكِينِ وَالْعَمِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبِهِمْ
وَفِي الرِّقَابِ وَالْغُرَمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَأَبْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِّنَ
اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴾

“Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na wasafiri. Huu ni waajibu ulio faridhiwa na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.” (At-Tawba 9: 60)

Ufafanuzi wake:

Na uwazi wa pande nane zinazopewa Zaka:

1. Mafukara:

Fakiri ni yule asiyekuwa na mali ya kuweza kumtatulia matatizo yake na wale ambao wanamtegemea katika chakula, kinywaji, kivazi na makazi hata akimiliki kiwango cha mali.

2. Masikini:

Huenda akawa afadhali au zaidi kuliko fakiri isipokuwa hukumu yao ni moja katika kila kitu. Na Mtume ﷺ amemfafanua masikini katika baadhi ya Hadithi zake na akasema:

“Masikini si yule anayezunguka kwa watu akihangaishwa na tonge moja na matonge mawili na tende moja na tende mbili. Lakini masikini ni yule ambaye hapati kitu cha kumtoshwa wala hajulikani ili apewe Zaka na wala hasimami akaomba watu.”
(Al-Bukhari na Muslim)

3. Wafanyakazi wa Zaka:

Mfanyakazi wa Zaka ni yule anayeleta au anakwenda kukusanya au anaitathmini au mwandishi wake katika daftari la Zaka huyo anastahiki kupewa Zaka ikiwa ni malipo ya kazi yake na hata kama ana uwezo, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Si halali kwa mwenye uwezo kupewa Zaka ila kwa mambo matano:- Kwa mfanyakazi wa kukusanya Zaka. Au mtu aliinunua

Zaka kwa malipo yake. Au mwenye madeni. Au mpiganaji katika Dini ya Allah. Au masikini aliyepewa Zaka na yeye akampa mwenye uwezo.” (Ibn Majah)

4. Wenye Kutiwa Nguvu Nyoyo Zao:

Naye ni mtu Muislamu ambaye bado ni dhaifu katika Uislamu na akawa na sauti katika jamii zake hivyo mtu huyo hupewa Zaka kwa kumpa nguvu na kumweka katika Uislamu kukiwa na mategemeo ya kuenea manufaa yake au kujizuia shari yake au mtu fakiri ambaye kuna matarajio katika imani yake au imani ya jamaa zake watu wa namna hiyo watapewa zaka kwa kuwapendezesha katika Uislamu.

Na huenda hisa hii akapewa kila ambae anaweza kuleta maslahi ya Waislamu na Waislamu kupitia matangazo, kama vile kuwapa Zaka waandishi wa habari na waandishi wengine.

5. Mtu Aliye katika Utumwa:

Makusudio yake ni Muislamu kuwa mtumwa hivyo akanunuliwa kutokana na Zaka na akaachwa huru katika Dini ya Allah au Muislamu mtumwa ameandikiana na Bwana wake. Mtu huyo hupewa Zaka ili analize mkataba wake hatimaye awe huru.

6. Wenye Madeni:

Mwenye madeni ni yule ambaye anabeba deni ambalo sababu zake si katika kumuasi Allah na Mtume wake, na anashindwa kulilipa basi atapewa katika Zaka kiasi kitakachomwezesha kulipa deni hilo, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Si halali kuomba ila kwa watatu: Kwa mwenye ufakiri mkubwa au mwenye deni kubwa au anayekabiliwa na faini ya kuua akawa hana uwezo wa kulipa faini hiyo.” (Ibn Khuzeima)

7. Katika Dini ya Allah.

Makusudio yake ni matendo yanayomfikisha mtu kwenye radhi ya Allah na kupata pepo yake.

Na hasa kupigana *jihadi* kwa ajili ya Allah ili kulinyanyua neno la Allah. Hivyo anapewa zaka mpiganaji katika *Dini* ya Allah hata kama ni tajiri.

Na fungu hili linakusanya maslahi mengine ya kisheria ya kijamii kama kuimarisha Misikiti na kujenga hospitali na shule na vituo vya yatima. Isipokuwa jambo ambalo linatakiwa lianzie kwenye fungu hili ni la kuandalia *jihad* tangu kuanzia kuwa na silaha za kupigania hadi maandalizi ya jeshi na mahitaji mengine ya *jihad* na ya kivita katika Dini ya Allah.

8. Msafiri (Mtoto wa Njia).

Msafiri ni yule aliyeishiwa akiwa mbali na kwao. Huyu atapewa kiasi kitachomwezesha kutatua matatizo yake katika ugeni wake, hata kama alikuwa na uwezo huko kwao, kutokana na uhitaji wake wakati wa safari yake na namna alivyoishiwa. Na fungu hilo atapewa atapomkosa mtu wa kumkopesha mkopo utaomwezesha kutatua matatizo yake na akimpata wa kumkopesha itampasa akope na wala hatopewa Zaka muda wa kuwa yeye ana uwezo huko kwao.

Ufafanuzi:

i). Muislamu kama alitoa Zaka ya mali yake kuipa pande yoyote katika zile pande nane itakuwa imetoshwa, isipokuwa anatakiwa kutanguliza pande muhimu zaidi na inayohitaji zaidi. Ikiwa mali zake ni nyingi akaigawa kwa kila pande iliyopo katika zile pande nane inakuwa vizuri zaidi.

ii). Haitotolewa Zaka kupewa ambaye mtoaji kinamlazimu chakula chake kama vile wazazi wawili na watoto wajapoenda chini (vijukuu, vitukuu). Na mke kwa kupasa chakula chao kwa mtoaji wanapohitaji chakula.

iii). Zaka haitolewi kwa familia ya Mtume Muhammad ﷺ kutokana na utukufu wao na cheo chao nao ni Bani Hashim na familia ya Ally na familia ya Jafar na familia ya 'Uqaily na familia ya 'Abbas kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Zaka haipewi familia ya Muhammad hakika si vinginevyo, hiyo zaka ni uchafu wa watu.” (Muslim).

iv). Inatosha Muislamu kutoa Zaka ya mali yake kumpa Imamu (kiongozi) wake Muislamu hata kama Imamu huyu ni muovu. Na mtoaji atakuwa ameshaepukana na dhima ya Zaka yake kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Ukishatoa Zaka kumpa mjumbe wangu unakuwa umeshaepukana nayo na unapata malipo ya Zaka yako. Na madhambi atapata mwenye kubadilisha Zaka hiyo.” (Imam Ahmad)

v). Zaka hapewi kafiri wala mtu fasiki aliyetoka katika *twa* ya Allah kama vile mwenye kuacha Swala, na anayezichezea Sheria za Uislamu kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Zaka huchukuliwa kutoka kwa matajiri wao kupelekwa kwa mafakiri wao.”

Maana matajiri wa Waislamu na mafakiri wao. Na wala hapewi tajiri wala mwenye nguvu mwenye uwezo wa kutafuta. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hana fungu tajiri katika Zaka wala mwenye nguvu mtafutaji.” (Imam Ahmad). (Mtafutaji) yaani anachuma kadri ya kumtoshesha.

vi). Haifai kuihamisha Zaka kutoka katika mji kuipeleka katika mji mwingine ulio mbali kwa masafa ya kupunguza Swala. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hupelekwa kwa mafakiri wao.”

Wameruhusu wanachuoni watapokosekana mafakiri katika mji huo au mji mwingine ulio na shida zaidi kuliko mji unaotoka Zaka. Katika hiyo itafaa kuihamisha Zaka kutoka mji kuipeleka mji mwingine kwenye wahitaji. Imamu ndiye atakayefanya hivyo au mtu mwingine.

vii). Mwenye kumdai fakiri na akataka deni lake hilo aliingize katika Zaka yake itafaa kwa mtu huyo kufanya hivyo. Laiti akilitaka deni lake kwa huyo fakiri atakuwa na uwezo wa kulipa. Ama fakiri akiwa hana uwezo wa kulipa deni, amekata tamaa kulipa deni hilo au amempa Zaka kisha amrudishie halitajuzu deni hilo kuwa Zaka.

viii). Haitofaa zaka ila kwa nia. Laiti mtu alitoa Zaka pasina nia ya Zaka ya faradhi haiwezi kufaa kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika matendo yote huzingatia nia na kila mtu atalipwa kwa alilolinuia.”

Kwa hiyo anatakiwa mwenye kutoa Zaka anuie Zaka ya faradhi inayomlazimu katika mali yake. Na akusudie radhi ya Allah Mtukufu kwani usafi wa moyo - *Ikhlās* ni sharti katika kukubaliwa kwa ibada zote au kila ibada kwa kauli yake Allah (s.w):

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

“Hawakuamrisha isipokuwa wamuabudu Allah hali ya kumtakasia Dini.”(Al-Bayyina 98: 5)

Somo la Tano

Inahusu Zakatul Fitri:

1. Hukumu yake.

Zaka ya *Fitri* ni sunna iliyothibiti kwa kila mmoja wa Waislamu kwa kauli ya mtoto wa ‘Umar Allah amuwie radhi:

“Amefaradhisha mjumbe wa Allah Zaka ya Fitri ya Ramadhani pishi moja ya tende au pishi moja ya shairi kwa mtumwa na muungwana mume na mke mdogo na mkubwa katika Waislamu.” (An-Nasai)

2. Hekima yake.

Katika hekima za Zaka ya fitri ni kwamba inaisafisha nafsi ya mfungaji na mambo ambayo yanayoweza kuganda kwenye nafsi hiyo kutokana na madhambi ya porojo na maneno machafu kama ambavyo inawaondolea mafakiri na maskini kuomba siku ya Iddi (sikukuu) amesema Ibnu ‘Abbas Allah amuwie radhi:

“Amefaradhisha Mtume ﷺ Zaka ya Fitri kuwa ni takaso la mfungaji kutokana na porojo na uchafu na ni chakula kwa masikini.” (Abu Dawuud na Ibn Majah)

Na akasema Mtume ﷺ:

“Watoshelezeni muwaepushe na omba omba kwa siku hii ya leo.”
(Bahyaqi)

3. Kiasi chake na aina ya vyakula vinavyopasa kutolewa.

Kiasi cha zaka ya *Fitri* ni pishi moja na pishi moja ni vibaba vinne na kinachotolewa ni kile kinachopendelewa katika vyakula vya watu wa mji huo. Ni sawa sawa kama ilikuwa ngano au shairi au tende au mchele au zabibu au maziwa yaliyokaushwa kwa kauli ya Abi Said - Allah amwie radhi:

“Tulikuwa wakati Mtume ﷺ Akiwa nasi tunatoa Zaka ya Fitri kumtolea kila mdogo na mkubwa, aliye huru au mtumwa pishi moja ya chakula, au pishi moja ya maziwa makavu au pishi moja ya shairi au pishi moja ya zabibu.” (Al-Bukhari)

4. Hakitolewi kisichokuwa chakula

Kinachopaswa kutolewa Zaka ya Fitri ni katika aina za vyakula. Wala haitakiwi kubadilishwa kwa kutoa fedha ila kwa dharura. Kwani haikuthibiti kwamba Mtume ﷺ alitoa pesa badala ya chakula, bali haikunakiliwa hata kutoka kwa maswahaba kuwa wametoa pesa badala ya chakula.

5. Wakati wa kupasa Zaka ya fitri na wakati wa kuitoa:

Inapasa zaka ya *Fitri* kwa kuingia usiku wa *Idd*, na wakati wa kuitoa kuna wakati wa kufaa nao ni kabla ya siku ya *Idd* kwa siku moja au siku mbili kama alivyofanya Ibn Umar.

Na kuna wakati wa kutoa ulio bora nao ni kuanzia kuchomoza kwa Alfajiri ya siku ya *Idd* hadi kabla kidogo ya swala ya *Idd*. Kwa amri ya Mtume ﷺ kwamba:

“Zaka ya Fitri itolewe kabla ya watu kutoka kwenda kwenye swala na kauli ya ibn Abbas Allah amuwie radhi: “Amefaradhisha Mjumbe wa Allah Zaka ya fitri; ni kitakaso cha mfungaji kutokana na porojo na uchafu, pia ni chakula kwa masikini, mwenye kutoa kabla ya Swala. Itakuwa kwake ni Zaka yenye kukubaliwa na mwenye kutoa baada ya Swala inakuwa ni swadaka kama swadaka nyingine.”

Na wakati wa kulipa: Nao unaanzia baada ya Swala ya Idd na kuendelea, Zaka inatolewa wakati huo na inatosheleza lakini ni karaha.

6. Anayepewa.

Sehemu inayopelekwa zaka ya *Fitri* ni sehemu zile zile zinazopelekwa Zaka nyingine isipokuwa mafukara na masikini ndiyo wanaopewa kipaumbele kuliko mafungu mengine. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Watoshelezeni ombaomba katika siku hii ya leo (Idd).”

Haitolewi kwa wasio kuwa mafukara ila wakikosekana, au wapo ila hawahitaji, au kuna wanaohitaji zaidi katika wenye mafungu.

Ufafanuzi:

i) Inafaa kwa mwanamke mwenye uwezo kumpa Zaka yake mumewe aliye fakiri, na haifai kinyume chake. Kwani matumizi ya mwanamke ni wajibu kwa mwanamume na haikuwa matumizi ya mume ni wajibu kwa mwanamke.

ii). Unaanguka ulazima wa Zaka ya *Fitri* kwa asiyemiliki chakula cha siku yake. Kwani Allah hailazimishi nafsi ila kilicho katika uwezo wake.

iii). Ambae kimezidi kiasi cha chakula chake na akakitoa hicho kitamtosheleza. Kwa kauli ya Allah Mtukufu:

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتِطَعْتُمْ وَأَسْمِعُوا وَأَطِيعُوا وَأَنْفِقُوا خَيْرًا لِّأَنْفُسِكُمْ

“Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo, na sikieni, na tiini, na toeni, itakuwa kheri kwa nafsi zenu.” (64: 16)

Minhajil Muslim

iv). Inafaa kutoa Zaka ya mtu mmoja kwa watu wengi kama inavyofaa Zaka ya watu wengi kumpa mtu mmoja. Kwani ilivyokuja sheria ni tamko la kutoa tu.

v). Inapasa Zaka ya *Fitri* kwa Muislamu katika mji anaoishi.

vi). Haifai kuihamisha Zaka ya Fitri kuitoa kwenye mji kuipeleka mji mwingine isipokuwa kwa dharura kama ilivyo katika Zaka nyingine.



Mada ya Kumi na Moja

Katika Funga

Somo la Kwanza:

Maelezo ya Swaumu na tarehe ya kufaradhishwa kwake.

1. Maelezo ya *Swaumu*.

Swaumu kilugha: Ni kujizuilia. **Kisheria:** Ni kujizuilia - na kula na kunywa Na kujiepusha kutazama wanawake kwa matamano na yenye kufunguza tangu kuchomoza kwa Alfajiri mpaka kuchwa kwa jua pamoja na nia ya kufanya ibada.

2. Tarehe ya kufaradhishwa *Swaumu*.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alifaradhisha *Swaumu* juu ya umati wa Muhammad ﷺ kama alivyofaradhisha juu ya umma zilizotangulia umati Muhammad ﷺ kwa kauli yake Allah (s.w.):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن

قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

“Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu.” (Al-Baqara 2: 183)

Na hiyo ilikuwa katika siku ya Jumatatu ya mwezi wa Shabani mwaka wa pili wa Hijra iliyobarikiwa.

Somo la Pili

Ubora wa *Swaumu* na faida zake.

a). Ubora wake

Zinashuhudia ubora wa swaumu na kuthibitisha hadithi zifuatazo: Kauli yake Mtume ﷺ:

“Funga ni kinga inayomkinga mtu na moto kama ilivyo ngao ya mmoja wenu inavyomkinga vitani.” (Imam Ahmad na An-Nasai)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kufunga siku moja tu kwa ajili ya Allah, Allah ataepusha uso wa mfungaji huyo na moto kwa siku hiyo kiasi cha umbali wa maili sabini.” (At-Tirmidhi, An-Nasai, Ibn Majah na Imam Ahmad)

Na kauli yake,

“Dua ya Mfungaji hairejeshwi pindi atakapoomba pale anapofungua” (Ibn Majah na Al-Hakim)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika peponi kuna mlango unaoitwa Rayyaan, wataingilia mlango huo siku ya kiama watu waliofunga tu. Hatoingilia mlango huo yeyote asiyekua mfungaji. Kutaulizwa wako wapi waliofunga watu watasimama hatoingilia mlango huo yeyote na wakimaliza mlango utafungwa na hatoingia katika mlango huo yeyote.” (Al-Bukhari, Muslim na An-Nasai)

b) Faida za Funga.

Funga ina faida za kiroho, kijamii na za kiafya. Miongoni mwa faida za kiroho za funga ni kwamba funga inazoesha uvumilivu na inatia nguvu. Na funga inafundisha

kuidhibiti nafsi na kuisaidia. Na katika nafsi kunapatikana uwezo wa kumcha Allah na pia inalea nafsi malezi mazuri na khasa kumcha Allah ambayo ndio sababu kubwa ya funga kama ilivyokuja katika kauli yake Allah Mtukufu:

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

“...Mmefaradhiswa funga kama walivyofaradhiswa walio kabla yenu ili mpate kumcha Mungu.” (al Baqara 2:183)

Na faida za Swaumu kijamii. Ni kwamba umma unazoeshwa hali ya nidhamu na umoja na kupenda uadilifu na usawa na funga inatengeneza hali ya huruma na kutengeneza tabia kwa waumini kama ambavyo inahifadhi jamii na shari na mambo mabaya.

Na miongoni mwa **faida za funga kiafya** ni kwamba *swaumu* inasafisha utumbo mdogo na inatengeneza utumbo wa chakula. Na inausafisha mwili kutokana na ziada ya vitu visivyotakiwa mwilini na vile vinavyogandia vilivyosababishwa na mafuta na pia hupunguza athari za unene. Na katika hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Mtume ﷺ: *صوموا تصحوا*, “*Fungeni mtapata afya*”.

Somo la Tatu

Sunna katika Swaumu na yaliyo makuruhu na yaliyo haramu.

a) Sunna za Swaumu:

i). Siku ya ‘*Arafa* kwa yule asiyekuwa *Al-Hajji*. Ile siku ya *Hijja* nayo ni siku ya tisa ya mfungo tatu kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Kufunga siku ya ‘Arafa kunafuta madhambi ya miaka miwili iliyopita na ijayo na kufunga siku ya ‘Ashuraa kunafuta madhambi ya mwaka mzima uliopita.” (Imam Ahmad).

Minhajil Muslim

ii). Siku ya ‘Ashuraa na siku ya *Tasu’a* nazo ni siku za kumi na siku ya tisa za mfunguo nne kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“...Na kufunga siku ya Ashuraa kunafuta madhambi ya mwaka uliopita.”

Kama alivyofunga Mtume ﷺ siku ya ‘Ashuraa na ameamrisha kuifunga siku hiyo na amesema:

“Utafika mwaka ujao Allah akipenda tutafunga siku ya mwezi tisa ya mfunguo nne.” (Muslim)

iii). Siku sita za mfunguo mosi kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani na akafuatiliza siku sita za mfunguo mosi anakuwa kama, aliyefunga milele.” (Muslim)

iv). Nusu ya mwanzo ya mwezi wa Shabani. Kwa kauli yake ‘Aisha Allah amuie radhi:

“Sikumuona ﷺ hata mara moja amekamilisha kufunga mwezi mzima isipokuwa Ramadhani tu. Na si kumuona katika mwezi anaofunga sana kama Shabani.” (‘Abdi Razzak).

v). Siku kumi za mwanzo za mfunguo tatu: “Mwezi wa Hija”. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakuna siku yoyote inayotendwa matendo mazuri ndani ya siku hizi - anakusudia siku kumi za mwanzo za mwezi wa Hija - wakasema maswahaba ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu wala Jihad katika dini ya Mwenyezi Mungu? Akasema wala jihadi katika Dini ya Mwenyezi Mungu isipokuwa mtu ametoka pamoja na nafsi yake na mali yake halafu asirudi na chochote.” (Ibn Majah na Imam Ahmad)

vi). Mwezi mfunguo nne (mwezi wa kwanza wa Kiislamu ambao ni *Muharram*) kwa kauli yake Mtume ﷺ alipoulizwa ni fungu gani bora baada ya Ramadhani.

Akasema Mtume ﷺ:

“Ni mwezi wa Mwenyezi Mungu mnaouita Muharram.” (Ibn Majah na Imam Ahmad)

vii). Siku nyeupe katika kila mwezi, nazo ni mwezi kumi na tatu na kumi na nne na kumi na tano, kwa kauli yake Abi Dharri Radhi za Allah zimshukie juu yake:

“Ametuamrisha Mtume wa Allah kufunga siku tatu nyeupe katika kila mwezi siku ya kumi na tatu na siku ya kumi na nne na ya kumi na tano, na amesema siku hizo ni sawa na kufunga milele.”
(An-Nasai)

viii). Siku ya Jumatatu na siku ya Alhamisi kwa yaliyopokelewa kwamba Mtume ﷺ alikuwa mara nyingi akifunga siku ya Jumatatu na Alhamisi. Akaulizwa kuhusu hilo akasema:

“Kwa hakika matendo ya waja huoneshwa kila Jumatatu na Alhamisi, basi Allah (s.w.) humsamehe kila Muislamu au Muumini, isipokuwa waliohasimiana husema (Allah) warudisheni nyuma kabisa.” (Ahmad)

ix). Kufunga siku moja na kufungua siku moja, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Funga inayopendeza zaidi kwa Allah ni funga ya Nabii Daudi na Swala inayopendeza zaidi kwa Allah ni Swala ya Nabii Daud. Alikuwa akilala nusu ya usiku na akiamka theluthi ya usiku na akilala tena sudusi (moja ya sita) na alikuwa anafunga siku moja na anakula siku moja.” (Al-Bukhari, Abu Dawuud, Imam Ahmad na An-Nasai).

x). Ni fungu kwa aliye mjane ambaye hana uwezo wa kuowa, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kuwa na uwezo wa kuoa na aowe. Kwani fungu ni kufunika macho na kudhibiti tupu, asiyekuwa na uwezo wa kuowa anapaswa kufunga kwani hiyo fungu ni kivunjio cha ukali wa matamano yake.” (Al-Bukhari)

b) Yaliyo makruhu kwa mwenye funga.

i). Kufunga siku ya ‘Arafa kwa mtu aliyesimama (aliyehudhuria) ‘Arafa. Kwa Kukataza kwake Mtume ﷺ,

“kufunga siku ya ‘Arafa kwa aliyesimama ‘Arafa. (Imam Ahmad na Al-Hakim)

ii). Kufunga siku ya Ijumaa peke yake, kwa kauli yake Mtume ﷺ :

“Hakika siku ya Ijumaa ni Iddi kwenu msifunge isipokuwa kwa kufunga kabla yake au baada yake.” (Ameitaja Al-Haytham katika Mujmai Az-Zawaid).

iii). Kufunga siku ya Jumamosi peke yake, kwa kauli ya Mtume ﷺ :

“Msifunge siku ya Jumamosi isipokuwa hiyo Jumamosi iwe miongoni mwa siku mlizofaradhishwa kufunga. Na hata mmoja wenu akipata chakula ila ganda la zabibu au kijiti cha mti na akitafunetafune”. (At-Tirmidhi, Abu Dawuud, Ibn Majah na Imam Ahmad)

iv). Kufunga siku za mwisho za Shabani, kwa kauli yake Mtume ﷺ :

“Unapogawanyika nusu mwezi wa Shabani basi msifunge”. (Abu Dawuud na Al-Bahyaqi)

Uzindushi

Umakruhu katika kufunga siku hizi ni umakruhu wa kujiepusha tu. Na zifuatazo umakruhu wake ni umakruhu wa haramu.

1. Nako ni kuunganisha kufunga kuanzia siku mbili na zaidi, pasina kufuturu (kula) kwa kauli yake Mtume ﷺ :

“Hamna msiunganishe katika kufunga”. (Al-Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Tahadharini na kuunganisha kufunga.” (Al-Bukhari, Muslim na Imam Ahmad)

2. Kufunga siku ya shaka nayo ni siku ya thalathini ya Shabani, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kufunga siku ya shaka basi huyo amemuasi Abal Qasim.” (An-Nasai)

3. Kufunga milele, nako ni kufunga mwaka mzima pasi na kufungua siku moja kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Hakufunga, mwenye kufunga milele”. (Musim na An-Nasai)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kufunga milele hakufunga wala hakufuturu.” (Imam Ahmad na An-Nasai)

4. Mwanamke kufunga (funga ya sunna) pasi na ruksa ya mumewe na hali ya kuwa mumewe yupo, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Haruhusiwi kufunga mwanamke hata siku moja hali ya kuwa mumewe yupo, ila kwa idhini yake isipokuwa Ramadhani.” (Imam Ahmad)

c) Funga iliyoharamishwa

Nayo ni Kufunga Siku Zifuatazo:

i). Kufunga **siku ya Iddi el Fitri au Iddi el Hajji**, kwa kauli yake Umar Allah amuie radhi:

“Hizi ni siku mbili alizokataza Mtume ﷺ kuzifunga, siku ya kula kwenu kutokana na funga yenu. Siku mnayokula kutokana na Ibada yenu (Ya Hijja).”

ii). **Siku za Tashriki** nazo ni siku tatu zinazofuata baada ya siku ya Iddi. Kwani alimtuma mjumbe wa Allah kwenda kutangaza akipiga kelele katika mina akisema:

“Msizifunge siku hizi kwani siku hizi ni siku za kula, kunywa na mume kuzungumza na mkewe.” (Imam Ahmad na Ad-Daraqutni).
Na katika tamko jingine na kumtaja Allah (s.w.).

iii). **Siku za hedhi na nifasi** kwani makubaliano ya pamoja ya wanachuoni ni juu ya kuharibika swaumu ya mwenye hedhi na nifasi kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hivi hakuna mwanamke anapotoka hedhi huwa haswali wala hafungi? Na huo ndio upungufu wa dini yake.” (Al-Bukhari)

iv). **Funga ya mgonjwa**. Funga ya mgonjwa ambaye anaiogopea nafsi yake kupata matatizo kwa kauli yake Allah Mtukufu:

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٩﴾

“Wala msiziuwe nafsi zenu hakika Allah (s.w.) ni Mpole.” (4: 29)

Somo la Nne

Kupaswa kwa Funga ya Mwezi wa Ramadhani na Fadhila zake.

a) Kuwajibika funga ya Ramadhani

Funga ya mwezi wa Ramadhani ni wajibu kwa mujibu wa *Qur-aan* na *Sunna* na makubaliano ya pamoja ya wanazuoni wa Kiislamu. Hakika Amesema Allah :

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ
الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ ۚ فَمَن شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۗ

“Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur’ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi. Basi ataye kuwa mjini katika mwezi huu na afunge...” (al Baqara 2:185)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Umejengwa Uislamu juu ya mambo matano. 1) Ni kukubali kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah (s.w.) na kwamba Muhammad ni mjumbe wa Allah. 2). Na kudumisha swala. 3). Na kutoa zaka. 4). Na kuhiji Al-Kaaba (Makka) 5). Na kufunga mwezi wa Ramadhani.” (Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi)

Na kauli yake Mtume ﷺ kwamba:

“... ya Uislamu na nguzo za Dini ni mambo matatu ambayo ndio misingi ya Uislamu. Mwenye kuacha moja tu katika misingi hiyo kwa kufanya hivyo anakuwa kafiri na inakuwa hataki damu yake (ni halali kuuliwa) - nayo ni kukiri kwamba hapana Mola apaswae kuabudiwa kwa haki ila Allah, na Swala za faradhi na fungu ya Mwezi wa Ramadhani.”

b). Fadhila za Mwezi wa Ramadhani

Ramadhani ina ubora mkubwa na mambo na fadhila nyingi ambazo hazipatikani katika miezi mingine isiyokuwa Ramadhani. Hadithi zifuatazo zinathibitisha suala hilo na zinatilia mkazo.

Kauli yake Mtume ﷺ:

“Swala tano, na al-Jumaa hadi al-Jumaa na Ramadhani hadi Ramadhani ni zenye kufuta madhambi yaliyo kati yake kama yakiepukwa madhambi makubwa.” (Muslim)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

Mada ya Kumi na Mbili

“Mwenye kufunga Ramadhani hali ya kuwa na imani na hali ya kutaraji kupata thawabu husamehewa mtu huyo madhambi yaliyotangulia.” (Al-Bukhari, Muslim na Abu Dawuud).

Na akasema tena Mtume ﷺ:

“Nimemuona mtu katika umati wangu akitoa ulimi kwa kiu kila akienda kunywa maji anazuliwa, ikamjia funga ya Ramadhani ndiyo ikampa maji na ikamwondoshea kiu.” (Tabarani)

Na akasema tena Mtume ﷺ:

“Inapokuwa mwanzo wa usiku katika mwezi wa Ramadhani mashetani na majini hufungwa kamba, na milango ya motoni kufungwa, na hufunguliwa milango ya peponi. Milango ya peponi haifungwi hata mmoja, na atalingania mlinganiaji; Ee! mtaka kheri njoo, na hulingania tena; Ee! mtaka shari chelewa na Allah ana watu anaowaacha huru na moto na hilo ni kila usiku.” (At-Tirmidhi na Al-Hakim)

Somo la Tano

Ubora wa Kutenda Wema na Ihsani Katika mwezi wa Ramadhani.

Kwa ajili ya ubora wa Ramadhani, yamekuwa bora kila yanayofanyika ndani ya mwezi wa Ramadhani katika matendo ya kheri na aina mbalimbali za wema na ihsani na miongoni mwa mambo hayo ni:

1. Sadaka:

Kwani Mtume ﷺ amesema:

“Bora ya sadaka ni sadaka inayotolewa ndani ya mwezi wa Ramadhani.” (At-Tirmidhi)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kumfuturisha mtu aliyefunga anapata malipo yake pasi na kupunguzwa malipo ya mfungaji hata kidogo.” (Imam Ahmad na At-Tirmidhi).

Na amesema tena Mtume ﷺ:

“Mwenye kumfuturisha aliyefunga kwa kumpa chakula au kinywaji vikiwa vya halali mtu huyo huombewa, na malaika katika masaa yote ya mwezi wa Ramadhani pia mtu huyo hutakiwa rehema na malaika Jibril usiku wa Lailatul Qadiri.” (At-Tabarani)

Na alikuwa Mtume ﷺ mkarimu zaidi katika watu kwenye mambo ya kheri na alikuwa mkarimu zaidi katika Mwezi wa Ramadhani, wakati anapokutana na Jibriil. (Al-Bukhari)

2. Kisimamo cha Usiku:

Kwani amesema Mtume ﷺ:

“Mwenye kusimama usiku kwa ibada Mwezi wa Ramadhani hali ya kuwa na imani, na hali ya kutarajia kupata thawabu mtu huyo husamehewa yaliyotangulia katika madhambi yake.” (Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi)

Na alikuwa Mtume ﷺ akihuyisha mausiku yote ya mwezi wa Ramadhani, na ilikuwa linapokuwa kumi la mwisho anaamsha watu wake wa nyumbani na kila mdogo na mkubwa anaeweza kuswali.” (Muslim)

3. Kusoma Qur’aan Tukufu.

Alikuwa Mtume ﷺ akizidisha kusoma Qur’aan katika mwezi wa Ramadhani na alikuwa Malaika Jibril akimsomesha Mtume ﷺ Qur’aan katika Ramadhani. (Al-Bukhari)

Na alikuwa Mtume ﷺ akirefusha zaidi kisomo katika kisimamo cha Ramadhani kuliko anavyorefusha katika mwezi mwingine. Hakika aliswali Mtume ﷺ pamoja na Hudhaifa usiku mmoja akasoma *Suratul Baqara* kisha akasoma *Al-Imran* kisha *Suratul Nisai*, alikuwa haipitii aya inayokhofisha ila husimama akimuomba. Hakuwali rakaa mbili akazimaliza mpaka akaja Bilal na kumpa ruhusa ya kuswali kama ilivyokuja katika sahihi.

Na amesema Mtume ﷺ:

“Funga na kisimamo ni mambo mawili yanayomuomba mja siku ya Qiyama. Inasema funga; Ewe Bwana wangu nilimzuia mja wako na chakula na kinywaji wakati wa mchana na inasema Qur-aan nilimzuia mja wako usingizi usiku basi tunamuomba kwa hiyo Qur’aan.” (Imam Ahmad)

4. Itikafu:

Nayo ni kuendeleza kukaa Msikitini kwa ajili ya ibada hali ya kujikurubisha kwa Allah Mtukufu. Hakika Mtume ﷺ alikaa itikafu na hakuacha kukaa itikafu kumi la mwisho, la Ramadhani mpaka alipomfisha Allah Mtukufu kama ilivyokuja katika sahihi. Na amesema Mtume ﷺ:

“Msikiti ni nyumba ya kila Mcha Mungu, na Allah amemdhamini kila atakayekuwa msikiti ndio nyumba yake, amemdhamini kwa malaika Jibrilu na rehema Yake; na kupita vizuri juu ya Sswira-twa (njia inayoenda kwenye radhi za Allah) mpaka peponi.” (At-Tarabani)

5. Kufanya ‘Umra:

Nako ni kuzuru nyumba ya Allah Mtukufu (*Al Kaaba*) kwa ajili ya kufanya *Tawafu* - ibada ya kuizunguka *Al Kaaba* - na kufanya *Sai* ambako ni kwenda mwendo kati ya Safa na Marwa - katika mwezi wa Ramadhani amesema Mtume ﷺ:

“Umra katika mwezi wa Ramadhani inafanana na Hijja ya mtu aliyehiji nami.” (Abu Dawuud, At-Tirmidhi, Imam Ahmad na Ibn Majah)

Na amesema tena Mtume ﷺ:

“Umra hadi ‘Umra nyingine inafuta madhambi yaliyo kati yake.”
(Al-Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi na An-Nasai)

Somo la Sita

Katika Kuthibiti Mwezi wa Ramadhani.

Kunathibiti kuingia Ramadhani kwa moja ya mambo mawili:

1. **La kwanza:** Ni kukamilika kwa mwezi uliotangulia mwezi wa Ramadhani nao ni Shaabani. Utakapotimia siku thelathini, siku thelathini na moja itakuwa siku ya kwanza ya Ramadhani kwa hali yoyote.

2. **La pili:** Ni kuonekana mwezi wake, muandamo: Utakapoonekana mwezi muandamo wa Ramadhani usiku wa thelathini wa Shaabani itakuwa umeshaingia mwezi wa Ramadhani na inapasa kufunga.

Kwa kauli yake Allah Aliyetukuka:

فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ

“Atakayeyafika miongoni mwenu hayo masiku ya mwezi basi afunge.” (Al-Baqara 2: 185)

Na kauli ya Mtume ﷺ,

“Mtakapoona mwezi fungeni na mtakapouona muandamo (wa kukamilisha Ramadhani) basi fungueni na mkizuiwa na mawingu kamilisheni hisabu ya siku thelathini.” (Muslim)

Na inatosha katika kuthibiti kuuona kwake, ushahidi wa muadilifu mmoja au waadilifu wawili. Kwani aliruhusu mjumbe wa Allah ﷻ

“Ushahidi wa mwanamume mmoja katika kuuona mwezi wa Ramadhani”, (Abu Dawuud).

“Ama kuuona mwezi muandamo wa mfunguo mosi kwa ajili ya kufuturu (kukamilisha funga) - hakuwezi kuthibiti ila kwa ushahidi wa waadilifu wawili.” (At-Tirmidhi)

Kwani hakuruhusu Mtume ﷺ ushahidi wa mtu mmoja muadilifu katika kufuturu (kumalizika).

Uzindushi

Mwenye kuuona mwezi muandamo wa Ramadhani itampasa mtu huyo kufunga hata kama ushahidi wake haukubaliki.

Na mwenye kuuona muandamo wa kufuturu na usikubaliwe ushahidi wake hatopaswa kufungua kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Fungeni ile siku mnayofunga nyote na kufungua ni ile siku mnayofungua nyote na sikukuu ya Adh-haa ni ile siku mnayochinja.” (At-Tirmidhi na Ad-Daraqutni)

Somo la Saba

Sharti na Hukumu za Funga ya Msafiri, Mgonjwa, Mzee, Mwenye Mimba, na Mwenye Kunyonyesha.

a) Sharti za Funga.

Panashurutizwa katika kupasa funga kwa Muislamu awe mwenye akili timamu na baleghe. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Imeinuliwa kalamu kwa watu watatu: Kwa mwendawazimu mpaka apate akili, na aliyelala mpaka aamke na kwa mtoto mdogo mpaka abaleghe (awe mkubwa).” (Abu Dawuud, At-Tirmidhi na Ibn Majah)

Akiwa ni Muislamu mwanamke inashartiwa katika kusihifunga yake awe msafi (mwenye kusafika na hedhi na nifasi). Kwa kauli yake Mtume ﷺ katika kuweka

wazi upungufu wa Dini ya mwanamke:

“Hivi hakuwa anapokuwa na hedhi hafungi wala haswali.” (Al-Bukhari)

b) Msafiri.

Ataposafiri Muislamu masafa ya kupunguza Swala ambayo ni maili Arobaini na nane. Sheria imeruhusu msafiri huyo kufungua na kulazimika kulipa siku aliyofungua ataporudi kwao. Kwa kauli yake Aliyetukuka:

وَمَنْ كَانَ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ

“Atakayekuwa mgonjwa kati yenu au yuko safirini (akafungua) aje alipe siku nyingine” (Al-Baqara 2: 185).

Na msafiri akiwa katika safari ambayo haitamletea matatizo na akaamua kufunga itakuwa ni vizuri zaidi. Kwa kauli yake Abii Saidi al-Khudriyyi Mungu amuwie radhi:

“Tulikuwa tunapigana vita katika mwezi wa Ramadhani tukiwa na Mtume ﷺ, katika sisi kuna waliofunga na kuna kati yetu waliokula, hakulaumu wale waliofunga na wala hakuwalaumu wale waliokula, wala waliokula kuwalaumu waliofunga kisha wakaona kwamba mwenye kupata nguvu za kufunga na akafunga atakuwa kafanya vizuri. Na wanaona kwamba mwenye kukosa nguvu za kufunga akaamua kula atakuwa kafanya vizuri.” (Muslim)

c) Mgonjwa.

Muislamu atapokuwa mgonjwa katika mwezi wa Ramadhani ataangalia akiwa anaweza kufunga pasina matatizo makubwa atafunga. Na kama hawezi atakula.

Kisha akiwa na matarajio ya kupona atasubiri mpaka apone, kisha atalipa siku alizofungua. Na akiwa hana matarajio ya kupona atakula na atatoa sadaka

Minhajil Muslim

kujitolea kila siku anayokula, sadaka ya kibaba kimoja cha chakula yaani kafi moja ya ngano kwa Kauli Yake Aliyetukuka:

وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مَسْكِينٍ

“*Na wale wasio weza, watoe fidiya kwa kumlisha masikini..*”
(Al-Baqara 2: 184)

d) Mzee

Muislamu mwanamume au Muislamu mwanamke anapofikia rika la uzee kiasi ambacho kutokana na uzee huo hawezi kufunga atafungua na atatoa sadaka kuitolea kila siku anayokula. Atatoa kibaba kimoja cha chakula kwa kauli ya Ibn ‘Abbas Mungu amuwie radhi:

“*Imeruhusiwa kwa mzee sana kutoa chakula kila siku kuwapa masikini na wala hatolipa funga.*” (Ad-Daraqutni)

e) Mwenye Mimba na Mnyonyeshaji.

Atapokuwa Muislamu mwanamke ni mwenye mimba na akaiogopea nafsi yake au kwa kilichomo katika tumbo lake, atafungua na udhuru huo utakapoondoka kutamlazimu kulipa siku alizofungua (kula). Na ikiwa ni mwenye uwezo atatoa sadaka kwa kila siku anayofunga. Sadaka ya kibaba kimoja cha ngano kufanya hivyo itakuwa ukamilifu na ni malipo makubwa zaidi.

Hii ndiyo hukumu kuhusiana na mwenye kunyonyesha akiiogopea nafsi yake au akiogopea mwanae na akiwa hakupata atayemnyonyeshea au mtoto hamkubali mtu mwingine asiyekuwa mama yake, na hukumu hii imechukuliwa kutoka kauli yake Allah Aliyetukuka:

وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مَسْكِينٍ

“*Na wale wasio weza, watoe fidiya kwa kumlisha masikini..*”
(Al- Baqara 2: 184)

Kwani maana ya kuweza; ni kuweza kwa taabu kubwa kwa hiyo wakifungua (wakila) watalipa au watalisha masikini.

Zindushi Mbili:

1. **Mwenye kupuuza** katika kulipa Ramadhani pasina udhuru mpaka ikaingia Ramadhani nyingine itampasa kulisha chakula nafasi ya kila siku anayolipa kuwapa masikini.

2. **Yeyote atayekufa** katika Waislamu na akafa ana funga atalazimika kuilipa walii wake. Kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Aliyekufa na akawa anafunga atamfungia walii wake.” (Al-Bukhari, Muslim, Abu Dawuud na An-Nasai)

Na kauli yake akimjibu yule aliyemuuliza akisema: “Hakika mama yangu alifariki na alikuwa na funga ya Ramadhani. Je, nimlipie? Akasema Mtume ﷺ ndio,

“deni la Allah lina haki zaidi ya kulipwa.” (Al-Bukhari)

Somo la Nane

Katika kuelezea Nguzo za Funga na Sunna zake na Makruhu yake.

a) Nguzo za funga ni:

1. Nia.

Nayo ni kuazimia kwa moyo kusudio la kufunga, kwa kufuata amri ya Allah aliye Mtukufu au hali ya kujikurubisha kwake kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Hakika matendo ni kwa Nia ya mja” na ikiwa funga ni ya faradhi basi nia ni wajibu kwa usiku ule kabla ya alfajiri kwa kauli yake ﷺ,
“Asiyelaza nia ya kufunga tangu usiku mtu huyo hana funga.”
(An-Nasai, Abu Dawuud na Ad-Daraqutini)

Minhajil Muslim

Kama fungua ni ya Sunna nia inaswihi hata kama itakuwa ni baada ya kuchomoza alfajiri, na kuinuka kwa mchana, na ukiwa bado hajakula kitu. Kwa kauli yake Aisha Allah awe radhi naye:

“Siku moja Mjumbe wa Allah aliingia kwangu akauliza: Je, una chochote? Tukasema, ‘hapana’, akasema basi mimi nimefunga.”
(Muslim)

2. Kujizuia.

Nako ni kujizuia na vyenye kufunguza kama vile kula, kunywa na kufanya tendo la ndoa.

3. Wakati Maalumu.

Na makusudio yake ni tangu kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuzama kwa jua. Laiti kama mtu angefungua usiku na akafuturu mchana haitoswihi fungua yake milele kwa kauli Yake Allah Alietukuka:

ثُمَّ أَتَمُّوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ

“Kisha timizeni saumu mpaka usiku”. (al Baqara: 187)

b) Sunna za fungua.:

1. **Kufanya haraka** kufuturu nako ni kufuturu baada ya kuthibiti kuzama kwa jua kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Watu huwa ndani ya kheri wanapofanya haraka kufuturu.”
(Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi)

Na kauli ya Annas Allah amuwiye radhi ni kwamba Mtume ﷺ,

“Hakuwa akiswali Magharibi mpaka kwanza afuturu ijapokuwa ni kwa kunywa maji.” (At-Tirmidhi)

2. Kufuturu kwa tende mbichi zilizokomaa au tende mbivu au maji. Na bora ya hivi vitatu ni kile cha kwanza na cha mwisho chake ni maji. Na inasuniwa kufuturia watri nayo ni vitu vitatu au vitano au saba kwa kauli ya Annas bin Maliki:

“Mtume ﷺ Alikuwa akifuturu tende zilizo komaa kabla ya kuswali zikikosekana anafuturia tende zilizo wiva zikikosekana anachukua maji kidogo.” (Abu Dawuud na Imam Ahmad).

3. Kuomba dua wakati wa kufuturu. Kwani Mtume ﷺ alikuwa akiomba wakati wa kufuturu:

((اللهم لك صمنا وعلى رزقك أفطرننا، فتقبل منا إنك أنت السميع العليم))

“Allahumma laka Swumna- wa ‘ala Rizqika aftwarni, Fataqabbal minna innaka anta Ssamiy’ul ‘Alim.”

“Ewe Mola wangu wa haki hakika mimi nimefunga kwa ajili yako na riziki yako ndiyo niliyofungulia, nikubalie, hakika Wewe Msikivu na Mjuzi.” (Abu Dawuud).

Na alikuwa Ibn ‘Umar alikuwa anasema:

((اللهم إني أسألك برحمتك التي وسعت كل شيء أن تغفر لي ذنوبي))

“Allahumma Inniy as-aluka birahmatika llatiy wasi’at kulla shayin an Taghfir Liy Dhunuwbiy”

“Ewe Mola wangu wa haki hakika mimi ninakuomba kwa rehema zako ambazo zimeenea kila kitu unisamehe makosa yangu.” (Ibn Majah)

4. Kula daku: Nako ni kula na kunywa wakati wa mwisho wa usiku kwa nia ya kufunga kwa kauli yake Mtume:

“Hakika tofauti iliyo kati ya funga yetu na funga ya Ahlul-Kitabu ni chakula cha daku”, (An-Nasai na Abu Dawuud)

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Kuleni daku kwani katika kula daku kuna baraka.” (Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi)

5. **Kucheleweshwa kula daku** mpaka karibu na wakati wa mwisho wa usiku kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Umati wangu huwa ndani ya kheri, wakati wanapofanya haraka kufuturu na wanacheleweshwa kula daku.” (Imam Ahmad)

Na wakati wa kula daku unaanza tangu nusu ya mwisho ya usiku na unaisha kabla Swala ya alfajiri kwa dakika chache kwa kauli ya Zaid bin Thabit Mungu amuie radhi:

“Tulikula daku pamoja na Mtume ﷺ kisha akasimama kuswali nikauliza: “Kulikuwa na muda gani kati ya adhana na kula daku? Akasema: kiasi cha kusoma aya khamsini.” (An-Nasai)

Ufafanuzi.

Mwenye kuwa na shaka katika kuchomoza alfajiri anaweza kuendelea kula daku mpaka awe na uhakika wa kuchomoza kwake. Kisha atajizuia na kula. Kwa kauli Yake Allah aliyetukuka:

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّى يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ
ثُمَّ أَتَمُّوا الصِّيَامَ إِلَى اللَّيْلِ

“Na kuleni na kunywa mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni Saumu mpaka usiku.” (al Baqara 2: 187)

Na ilisemwa kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنه:

“Mimi nakula daku na nikianza kutia shaka basi ninajizuia, akaambiwa kula pale unaposhuku ili usishuku.”

c) Makruhu ya Saumu.

Mambo yanayochukiza kwa mtu aliye na Saumu na yanayoweza hata kama yenyewe hayaharibu saumu kusababisha mtu kuharibu saumu yake.

1. **Kusukutua** sana na kupandisha maji puani wakati wa kutawadha. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Fanya sana katika kupandisha maji puani isipokuwa utakapokuwa umefunga.” (At-Tirmidhi, Abu Dawuud na An-Nasai)

Mtume ﷺ hakupendelea kuendeleza sana kupandisha maji puani kwa kuogopa maji yakapelekea kuharibika kwa saumu ya mtu.

2. **Kukumbatiana** ambako kunaweza kuamsha matamano yatakayosababisha kuharibu funga kwa kutokwa na madhii au kufanya tendo la ndoa jambo ambalo litabatilisha saumu na kulazimisha kafara.

3. **Kumtazama mwanamke kwa matamano.**

4. **Kufikiria** mambo yanayohusu jimai.

5. **Kumgusa** mwanamke kwa mkono au kumgusa kwa kiwiliwili bila ya kuwapo kwa dharura.

6. **Kutafuna** iliki, vitu vya gama kama vile: chingam, bigji n.k. kwa kuogopa kupenya chembechembe zake hadi kooni.

7. **Kuonja** chumvi au chakula.

8. **Kusukutua** si kwa udhu au haja yoyote inayosababisha kusukutuwa.

9. **Kupaka** wanja mwanzo wa mchana na si vibaya kupakaa mwisho wake (mchana).

10. **Kuumika** au kukata mshipa kwa kuogopa kupoteza nguvu, kutakopelekea kufungua kwa yale yaliyomo katika hilo (la kuumika).

Somo la Tisa

Matendo Yanayobatilisha Funga na Yanayoruhusiwa kwa Mwenye Saumu na Yanayosamehewa.

a) Yanayobatilisha Saumu:

1. Kuingia ndani kitu kilicho majimaji kwa kupitia puani, mdomoni au masikioni kama vile matone ya dawa, au kupitisha dawa sehemu za haja kubwa na tupu ya mbele ya mwanamke kwa kuingiza kitu.
2. Kuingiza maji ndani mpaka yakafika kooni au tumboni kwa kusukutuwa sana na kupandisha maji puani wakati wa kutawadha na mengineyo.
3. Kutokwa na manii kwa kuangalia au kufikiria sana vitendo vya jimai au kukumbatia.
4. Kujitapisha kwa makusudi. Kwa kauli yake Mtume :

“Atakayejitapisha kwa makusudi na alipe, ama kwa yule ambaye matapishi yamemjia na kumshinda akatapika bila ya kupenda, haitoharibika saumu yake.” (Abu Dawuud)
5. Kula au kwa hiyari yake kunywa au kujihusisha na vitendo vya jimai, katika hali ya kulazimishwa juu ya hilo.
6. Aliyekula au kunywa akidhani kuwa bado ni usiku baadae ikamdhihirikia kuwa tayari ni alfajiri.
7. Aliyekula au kunywa akidhani kuwa usiku unaingia kisha ikamdhihirikia kuwa kumbe bado ni mchana.
8. Aliyekula au kunywa kwa kusahau, halafu asijizuie kwa kudhani kwamba kujizuia si lazima kwa vile tayari amekwisha kula na kunywa, hivyo akaendelea kula hadi usiku.

9. Kuingiza tumboni kisichokuwa chakula, au kinywaji kupitia mdomo kama vile kumeza madini au uzi. Kwa yaliyopokewa kwamba Bin Abbas Allah amuwie radhi amesema:

“Funga ni kwa kilichoingia si kwa kilichotoka.” (Ibn Abi Shaiba)

Anakusudia Ibn ‘Abbas kwa hilo kwamba funga inaharibika kwa kilichoingia ndani si kwa kilichotoka.

10. Kutokuwepo kwa nia ya kufunga, hata kama mtu hakula au kunywa kukiwa ni kufungua basi hakutakuwa ni kibatilisho.

11. Kuritadi, kutoka katika Uislamu. Kwa kauli yake Allah (s.w) Mtukufu:

﴿مِن قَبْلِكَ لَئِنْ أَشْرَكَتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ﴾

“...Bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu a’ mali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri.” (Az-Zumar 39: 65)

Saumu inayobatilishwa kwa njia tulizotaja hulipwa bila ya kutoa kafara, saumu na kafara hutolewa pale ambapo sababu ya kubatilika kwa saumu yenyewe ni:

a) **Kujihusisha na vitendo vya jimai.** kwa makusudi pasina kulazimishwa: Kwa kauli yake Abu Huraira Allah amuwiye radhi:

“Alikuja mtu mmoja kwa Mtume ﷺ akasema nimeangamia ewe mjumbe wa Allah akamuuliza: *kimekuangamiza nini?* Akasema:

“Nilimuingilia mke wangu mchana wa Ramadhani. Mtume ﷺ akamuliza: “Je unaye mtumwa ili umuache huru? Akasema hapana. Mtume akamuliza:, “Je unaweza kufunga miezi miwili mfululizo? ‘Akasema,: ‘Hapana’. Akamuliza tena: Mtume ﷺ “Je, utapata chakula cha kuwalisha masikini sitini?” akajibu, ‘hapana’, kisha akakaa, akaja mtu kwa Mtume ﷺ a chombo chenye tende akasema: ‘chukua ukatoe sadaka’. Yule mtu akajibu

hivi kuna aliefakiri zaidi yangu. Mtume ﷺ akacheka mpaka yakaonekana meno yake chonge na akasema 'nenda ukawalishe watoto wako'." (Al-Bukhari na Muslim)

b) Kula na kunywa bila ya kuwapo na udhuru wa kisheria, kwa kauli yake Abu Hanifa na Maliki Allah awarehemu:

"Ni kwamba mtu mmoja alikula mchana wa Ramadhani Mtume ﷺ akamuamrisha mtu huyo kutoa kafara." (Muslim na Imam Ahmad)

Na hadithi ya Abu Huraira Allah amuiye radhi - alisema:

"Alikuja mtu mmoja kwa Mtume ﷺ akasema, siku moja nilifungua (mchana) wa Ramadhani kwa makusudi. Mtume ﷺ akasema, 'muache huru mtumwa au funga miezi miwili mfululizo au wape chakula masikini sitini'." (Al-Bukhari, At-Tirmidhi na Ibn Majah)

b) Yanayoruhusiwa kwa Mtu aliye ndani ya Saumu:

1. Kupiga mswaki mchana wote. Isipokuwa kwa mafunzo ya Imamu Ahmad yeye kwake ni *makruhu* kwa aliyefunga kupiga mswaki baada ya kupinduka jua.
2. Kujipoza kwa maji kutokana na joto kali kwa kujimwagia maji mwilini au kwa kuzamisha mwili wake ndani ya maji.
3. Kula na kunywa na kufanya tendo la ndoa usiku mpaka kuthibitike kuchomoza alfajiri.
4. Kusafiri kwa sababu halali hata kama ndio itakuwa sababu ya itamsababishia kufuturu.
5. Kujitibu kwa dawa yoyote iliyo halali ambayo haifiki ndani hata kidogo na miongoni mwa mambo hayo ni kutumia sindano isiyokuwa ya chakula (lishe).

6. Kumtafunia mtoto mdogo chakula kwasababu ya kukosekana kwa mtu mwingine kufafanya hivyo kukikosa kwa sharti chakula hicho ya kutofika ndani ya tumbo la mtafunaji.

7. Kujitia manukato na kujifukizia *Bukhuri*.

c) Yanayosamehewa Kwa Aliyefunga.

1. Mtu kumeza mate yake mwenyewe kwa wingi wowote

2. Kushindwa kuzuia matapishi yaliyokuja kwa nguvu na kohozi lililofika katika ncha ya ulimi wake bila ya kulirudisha hata kidogo.

3. ikitokee kumeza nzi bila ya kukusudia.

4. (Kumeza) vumbi la njiani, na viwandani na moshi wa kuni na moshi aina nyingine ambao si rahisi kujizuia nayo.

5. Kuamka na janaba hata akishinda nalo mchana wote.

6. Kuota, hailazimiki kufanya chochote kwa aliyeota akiwa amefunga. Kwa hadithi ya Mtume ﷺ:

“Kalamu imeinuliwa (isiandike habari) kwa watu watatu, mwendawazimu mpaka apate akili, aliyelala mpaka aamke, na mtoto mdogo mpaka abaleghe.”

7. Kula na kunywa kwa kusahau. Imamu Maliki anasema mtu huyo anapaswa kulipa katika funga za faradhi, ama funga za sunna hatopaswa kulipa kabisa kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kusahau hali ya kuwa amefunga akala au kunywa na akamilishe funga yake, kwani ni Allah Aliyemlisha na Ndiye Aliyemnyweshi.” (Muslim, Imam Ahmad na Addarimy)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kula mchana wa Ramadhani kwa kusahau haitompasa mtu huyo kulipa au kutoa kafara.” (Al-Bukhari na Ad-Daraqutni)

Somo la Kumi

Kafara na Hekima Yake.

a) *Kafara:*

Ni kitu kinachotolewa kama fidia kwa lengo la kufunika dhambi, kinachoandamana na kwenda kinyume na sheria. Mwenye kukhalifu sheria kumuingilia mkewe mchana wa Ramadhani au amekula au kunywa kwa makusudi itampasa mtu huyo kutoa kafara kwa kosa hili kwa kufanya moja ya haya mambo matatu: kumuacha huru mtumwa *muumini* (sio kafiri), kama anae. Kufunga miezi miwili mfululizo, au kuwapa chakula masikini sitini. Kwa kila masikini mmoja kibaba cha ngano au shairi, tende au chakula kinacholiwa sehemu hizo kwa kiasi cha uwezo wake. Na kafara huongezeka kutokana na wingi wa kuhalifu sheria. Mwenye kumuingilia mke wake kwa siku moja na siku nyingine akala au akanywa mchana. Itamlazimu mtu huyo kutoa kafara mbili ya kumuingilia mkewe kinyume na sheria na kafara ya kula mchana wa mwezi wa Ramadhani.

b) *Hekima ya Kafara.*

Kuweko kwa kafara ni kuilinda sheria isichezewe na kuvunjwa heshima yake. Kafara inasafisha nafsi ya Muislamu na athari ya kosa lililofanywa bila ya sababu. Na lazima kafara itolewe kufuatana na taratibu zile namna ile ile iliyoweka sheria kuanzia kiwango na namna yake. Ili kufaulu katika kutekeleza umuhimu wake kwa kuondosha kosa na kufuta athari zake miongoni mwa kiburi cha nafsi.

Na asili ya kafara ni kauli yake Allah (s.w.)

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١١٤﴾

“*Hakika mema yanafuta mabaya.*” (Hud 12:114)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“*Muogope Allah popote ulipo na lifuutilize jambo ovu kwa jambo jema litalifuta lile ovu na kaa na watu kwa tabia nzuri.*” (At-Tirmidhi)

Mada ya Kwanza

Kinahusu Hijja na Umra

Mada Kumi: Somo la Kwanza

Hukumu ya Hijja Umra, na hekima zake:

a) Hukumu Zake:

Hijja ni faradhi kwa kila muislamu mwanaume na mwanamke aliyejaaliwa uwezo wa kwenda kuhiji. Kwa tamko lake Allah(s.w):

وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا

“Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea...”
(Al-‘Imran 3: 97)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Umejengwa Uislamu juu ya mambo matano: Nayo ni kukiri kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah na kwamba Muhammad ni mjumbe wa Allah na kudumisha Swala na kutoa Zaka na kukusudia Al-Kaaba kwa ibada. Kwa mwenye kuweza. Na kufunga Ramadhani.” (Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi)

Hijja ni faradhi aliyofaradhisha Allah mara moja tu katika umri wa Muislam kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hijja ni mara moja tu na mwenye kuzidisha inakuwa sunna.”
(Imam Ahmad na Ad-Daraqutni)

Isipokuwa inapendeza kurudia kila baada ya miaka mitano kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa yale anayopokea kutoka kwa Mola Wake Mtukufu:

“Hakika mja ambaye mwili wake ni mzima na maisha yake ni mazuri na ikapita miaka mitano hajanikusudia kuja kuhiji mtu huyo amezuiliwa na kheri nyingi.”

Ama *Umra* ni *sunna* inayompasa mtu kwa kauli yake Allah (s.w):

وَأَتِمُّوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلَّهِ

“Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Mwenyezi Mungu...”
(Al-Baqara 2: 196).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Muhijie baba yako na mfanyie Umra.” (At-Tirmidhi, An-Nasai, Al-Hakim na Ibn Majah)

Ilikuwa ni jibu kwa aliyemueleza Hakika baba yangu ni mzee sana hawezi kuhiji wala kwenda *Umra* wala kusafiri kutoka sehemu kwenda sehemu nyingine.

b) Hekima ya Hija na Umra.

Miongoni mwa hekima za Hija na Umra: Ni kuitoharisha nafsi na athari za madhambi ili iwe ni sehemu nzuri ya takrima za Allah(s.w) siku ya hesabu na malipo akhera. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kuikusudia nyumba hii kwa ibada na hakufanya uchafu wala maovu anatoka kwenye madhambi yake na kuwa safi kama siku aliyomzaa mama yake.” (Imam Ahmad, An-Nasai, na Ibn Majah)

Somo la Pili

Sharti za Hijja na Umra.

1. **Uislamu:** Ni sharti kwa anayetaka kwenda kutekeleza ibada ya Hijja au umra kuwa muislamu kwa vile imani ni sharti la kuswihi matendo na kukubaliwa.
2. **Akili:** Kwani hakuna majukumu kwa mwendawazimu.
3. **Kuwa baleghe:** Kwani hakuna majukumu kwa mtoto aliye chini ya umri mpaka abaleghe. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Imeinuliwa kalamu kwa watu watatu: kwa mwendawazimu hadi apate akili, na aliyelala hadi aamke na mtoto mpaka abaleghe.”

4. **Kuweza:** nako ni kuwa na masurufu na usafiri kwa kauli yake Allah Mtukufu:

عَلَى النَّاسِ حُجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ

“...kwa yule awezae njia ya kwendea....” (Al-‘Imran 3: 97).

Hivyo basi fakiri ambaye hana mali itakayomuezesha kujihudumia wakati wa *Hijja* yake, na kuhudumia watoto wake akiwa na watoto wakati atapowaacha nyumbani kwake, *Hijja* na *Umra* kwa mtu huyo ni ibada zisizomuhusu. Na hukumu hiyo inamuhusu pia mtu ambaye anayo mali ya kujihudumia na kuhudumia watoto wake lakini hana kipanda na hana nguvu za kutembea au anazo nguvu lakini usalama wa njiani ni mdogo kiasi cha kumfanya aogope juu ya nafsi yake au mali yake basi kwa mtu huyo haitompasa *Hijja* wala *Umra* kwa kukosekana uwezo.

Somo la Tatu

Hukumu ya Kuiacha Hijja na Umra

Hakika sheria imezihimiza hizi ibada mbili kubwa na ikahimiza pia kuzitenda, na imelingania kwa njia mbalimbali. Kauli yake Mtume ﷺ:

“Bora ya matendo: ni kumwamini Allah na Mtume wake halafu kupigana jihadi kwa ajili ya Dini ya Allah na kufanya Hijja yenye kukubaliwa.”

Na kauli yake tena Mtume ﷺ:

“Mwenye kuhiji nyumba hii na kuacha mambo machafu na asifanye mambo yatakayomtoa katika twaa ya Allah mtu huyo atatoka kwenye madhambi yake na kuwa kama siku aliyozaliwa na mama yake”.

Na kauli yake

“Hijja yenye kukubaliwa malipo yake ni pepo.” (Al-Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi na An-Nasai)

Na kauli yake:

“Jihadi ya mtu mkubwa na mnyonge na mwanamke ni Hijja yenye kukubaliwa.” (An-Nasai)

Na kauli yake:

“Umra hadi Umra nyingine ni kifutio kwa makosa yaliyo kati yake, na Hijja yenye kukubaliwa malipo yake ni pepo.” (Al-Bukhari)

Kama ambavyo sheria inasisitiza umuhimu na ubora wa ibada hizo Mtume naye amehadharisha kuzifanyia uvivu ibada kwa kauli yake;

“Mtu ambaye hakuzuiliwa na shida za wazi na hakuzuiliwa na ugonjwa au kuzuiliwa na kiongozi muovu na mtu huyo akawa hakuhiji na achague kifo chochote, afe yahudi au afe akiwa mnaswara”. (Imam Ahmad, Al-Baihaqi)

Na amesema Ali (Mwenyezi Mungu amuwiye radhi):

“Mwenye kuwa na maandalizi ya chombo cha kusafiri kitakachoweza kumfikisha kwenye nyumba ya Allah Mtukufu na akawa hakuhiji ni juu yake mtu huyo kuchagua kifo cha Kiyahudi au kifo cha kinaswara.” (At-Tirmidhi)

Na hilo ni tamko la Allah (s.w.):

وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ ءَامِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتِطَاعَ ۗ إِلَيْهِ سَبِيلًا
وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٩٧﴾

“...Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakaye kanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu...” (Al-‘Imran 3: 97)

Na akasema Umar - Allah amuwiye radhi:

“Nilikusudia kuwapeleka watu kwenye miji hii wakakague kila mwenye uwezo ambaye hakuhiji, wakamtoze kodi maana hao si Waislamu, hao si Waislam.” (Al-Bahyaqi)

Somo la Nne

Nguzo ya Kwanza Katika Nguzo za *Hijja* na *Umra*

Hijja ina nguzo nne: kuhirimia na kuvaa Ihram na kutufu, *kusay* (kwenda matiti baina ya *safa* na *marwa*) na kuhudhuria *Arafa*. Kutotimizwa kwa nguzo moja tu kati ya nguzo hizi *Hijja* imebatilika.

'*Umra* ina nguzo tatu: Kuhirimia na kuvaa ihram na kutufu, na *kusay*, haitatimia *Umra* bila kutimizwa kwa nguzo hizi.

Nguzo ya kwanza katika nguzo za *Hijja* na '*Umra* ni *Ih-ram*, nayo ni nia ya kuingia katika ibada za *Hijja* na '*Umra*:

Ibada ya *Hijja* na '*Umra* kwa pamoja *qiran* ina wajibu, Sunna zake na yaliyokatazwa. Nayo ni:

a) Wajibu

Makusudio ya neno wajibu: Ni matendo ambayo ni lazima yafanywe kama litaachwa tendo moja kati ya hayo atawajibika kuchinja, au kufunga siku kumi kama atashindwa kuchinja.

1. Kuhirimia katika vituo maalum *müqaat*: Nayo ni sehemu iliyowekwa kwa sheria kwa ajili ya *Ihram* na haifai kuipita sehemu hiyo bila ya *Ihram* kwa anyekusudia *Hijja* au *Umra*. Amesema Ibnu Abbas Allah amuwie radhi:

“Mtume ﷺ Ameiweka *Dhul-Hulaiifa* kuwa ndio sehemu ya kuhirimia watu wa *Madina* na *Juhfa* kwa watu wa *Shamu* na *Qarnul-Manazil* kwa watu wa *Najdi* na *Yalamlam* kwa watu wa *Yemen* na sehemu hizo ni za huko na mwenye kuzipita kwa watu wasiokuwa wa sehemu hizo kwa anyekusudia *Hijja* au *Umra* na ambaye *müqaati* yake ni kutovaa nguo zilizopindwa kabla ya sehemu hizo basi *Ihram* yake itaanzia kwao na hivyo hivyo hata kwa Watu wa *Makka* watahirimia *Makka*.” (Al-Bukhari)

2. Aliyehirimia asivae nguo au shati wala kanzu wala kofia, wala asifunge kilemba wala asifunike kichwa chake kabisa, hatakiwi kuvaa khofu (aina ya viatu vyepesi au soksi nzito) wala viatu -kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Asivae aliyehirimia nguo iliyoshonwa wala kilemba wala suruali wala kofia wala khofu isipokuwa kwa yule ambaye hakupata kanda mbili ndiyo atavaa khofu mbili na atatakiwa azikate chini ya fundo mbili.” (Al-Bukhari)

Na asivae nguo iliyopakawa Zafarani au warsi, na wala mwanamke asivae nikabu wala soksi za mikono kama alivyopokea Al-Bukhari katika makatazo haya.

3. **Talbiya:** Nayo ni kutamka:

((لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنَّعْمَةَ لَكَ وَالْمَلِكُ، لَا شَرِيكَ لَكَ))

“Labbayka Allaahumma Labbayka, Labbaika la- Shariyka Laka Labbayka, Innal Hamda Wannimata Laka Wal Mulka, La Shariyka Laka.”

“Nimeitikia Mwito Wako Ewe Mola Wangu Wa Haki Nimeitikia Mwito Wako Huna mshirika Nimeitika Mwito Wako Hakika Sifa Njema Ni Zako Na Ufalme Na Huna mshirika.”

Atasema hivyo mwenye kuhirimia wakati wa kuanza *Ihram*. Wakati bado akiwa *Miiqaat* ni sunna kukariri tamko hili mara kwa mara pamoja na kuinua sauti na kuanza kuisema kila kwenye tukio kama vile kushuka au kupanda au wakati inaposimamishwa Swala au kumaliza Swala au mtu anapokutana na marafiki.

b) Sunna:

Sunna ni matendo ambayo mtu akiyaacha haitamlazimu kuchinja mnyama ijapokuwa, atakosa malipo makubwa:

1. **Kuoga** kwa ajili ya *Ihram* hata kama atakuwa ni mwanamke mwenye nifasi au hedhi kwani mke wa Abu Bakr Allah amuie radhi alijifungua na hali amenuia *Hijja* Mtume ﷺ

“Akamuamrisha aoge.” (Muslim)

2. **Kuhirimia** ukiwa umevaa shuka ya juu na ya chini nyeupe safi kama alivyofanya Mtume ﷺ.
3. **Kufanyika Ihram** bada ya swala ya Sunna au ya faradhi.
4. **Kukata** kucha na kupunguza masharubu, na kuondoa nywele za kwapa, na sehemu nyingine za mwili, hivyo ndivyo alivyofanya Mtume ﷺ.
5. **Kuirudia rudia Talbiya** na kuianza upya kila unapoanza kitendo kipya kama tukio la kupanda au kushuka au kuswali kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kuitika wito wa Allah hadi kuzama kwa jua ataingia jioni mtu huyo akiwa ni mwenye kusamehewa.”

6. **Kuomba** na kumuomba Rehema Mtume ﷺ baada ya *Talbiya*, kwani alikuwa

“Mjumbe wa Allah ﷻ anapomaliza Talbiya humuomba Bwana wake pepo na kumtaka amlinde na moto”. (Ad-Daraqutni na Shafii)

c) Matendo yaliyokatazwa:

kama mtu atatenda moja kati ya matendo yaliyokatazwa itampasa kutoa fidia ya kuchinja mnyama au kufunga au kutoa chakula:

1. **Kufunika** kichwa kwa kifuniko chochote kile
2. **Kunyoa** nywele au kuzipunguza hata kama ni kwa vichache, ziwe ni nywele za kichwani au ni za sehemu nyingine.
3. **Kukata** kucha ni sawa zilikuwa kucha za mikononi au za miguuni.
4. **Kutia** manukato.
5. **Kuvaa** nguo iliyopindwa kwa hali yeyote.

6. **Kuua** kwa kuwinda mnyama kwa kauli yake Allah Mtukufu:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَأَنْتُمْ حُرْمٌ

“Enyi mlio amini! Msiue wanyama wa kuwinda nanyi mmeharimia katika Hija...” (Al-Maida 5: 95)

7. **Michezo ya kimapenzi** kama kubusu n.k. kwa kauli yake Allah(s.w.t):

فَلَا رَفَثٌ وَلَا فُسُوقٌ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ

“...basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija...” (Al-Baqara 2: 197)

Na makusudio ya maneno machafu ni vitangulizi vya jimai na kila linalopelekea kwenye jimai.

8. **Kufunga** ndoa au kuposa. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Haowi mwenye kuhirimia wala haozeshi wala haposi”. (Muslim)

9. **Kujihusisha na Vitendo vya Jimai kwa tamko lake Allah (s.w)**

فَلَا رَفَثٌ وَلَا فُسُوقٌ وَلَا جِدَالَ فِي الْحَجِّ

“basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija.”. (Al-Baqara 2: 197)

Na maneno machafu yanajumuisha jimai na vitangulizi vyake.

Hukumu ya kutenda vilivyokatazwa:

Mwenye kutenda kimoja tu kati ya tulivyotaja hivyo mtendaji huyo itampasa kutoa fidia nayo ni kufunga siku tatu au kuwapa chakula masikini sita. Kila masikini mmoja apewe kibaba cha ngano au kuchinja mbuzi au kondoo. Kwa kauli yake Allah(s.w.),

فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَّرِيضًا أَوْ بِهِمْ أَذًى مِنْ رَأْسِهِمْ فَفِدْيَةٌ مِنْ صِيَامٍ أَوْ
صَدَقَةٍ أَوْ نُسُكٍ

“Na atakaye kuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidiya kwa kufunga au kwa kutoa sadaka au kuchinja wanyama...”(Al-Baqara 2: 196)

Na kuua mawindo fidia yake ni kutoa mfano wa mnyama uliyemuua na hilo ni kwa kauli yake Allah (s.w.):

فَجَزَاءٌ مِثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعَمِ

“...basi malipo yake yatakuwa kwa kuchinja kilicho sawa na alichu kiuwa, katika mifugo...” (Al-Maida 5: 95)

Ama kwa atakayejihusisha na vitendo vya jimai atapaswa kuchinja mnyama naye ni mbuzi au kondoo.

Jimai ni tendo linaloharibu Hijja ijapokuwa muhusika ataendelea na hijja lakini baada ya Hijja, itampasa kutoa ngamia na kama hana atafunga siku kumi. Kama ambavyo itamlazimu kuilipa *Hijja* hiyo mwaka mwingine. Kama alivyopokea Maliki katika kitabu chake *Al-Muwatta*. Kwamba ‘Umar Ibn Khattab na Ali Ibn Abi Talib na Abu Huraira waliulizwa kuhusu mtu aliyemuungilia mkewe hali ya kuwa mtu huyo ni mwenye kuhirimia *Hijja* Wakasema: wataitekeleza watakwenda wao wenyewe mpaka wamalize *Hijja* yao kisha itawalazimu *Hijja* ijayo pamoja na fidia ya kuchinja mnyama.

Ama kufunga ndoa na kuchumbia na madhambi mengine kama vile kusengenya na uchochezi na kila kinachoingia katika sifa ya *Fusuqu*, mtendaji wa hayo atapaswa kutubia na kuomba msamaha. Kwani katika sheria imekuja kuwekwa kafara kwa mambo hayo isiyokuwa kutubia na kuomba msamaha.

Somo la Tano

Nguzo ya pili ni Twawafu.

Twawafu:

Ni kuizunguuka *Al-Kaaba* mara saba, na ina sharti na sunna na adabu zake:-

a) Sharti zake:

1. **Nia** wakati wa kuanza *Twawafu*. Kwani matendo yote huzingatiwa nia na lengo la kufanya ibada kwa ajili ya kutii amri ya Allah (s.w).

2. **Kutoharika** na najisi na *hadathi*. Kwa hadithi yake Mtume ﷺ inayosema:

“Kuizunguka Al-Kaaba ni mfano wa Swala.”

3. **Kusitiri tupu**: Kwani Twawafu ni kama Swala, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Kuizunguka Al-Kaaba ni mfano wa Swala isipokuwa (katika Twawafu) mnazungumza na atakaezungumza asizungumze ila kheri.” (At-Tirmidhi)

Na atakayetufu bila ya kunuia au ametufu hali ya kuwa na hadathi au ana najisi au yuko basi uchi, Twawafu yake itakuwa imeharibika na atapaswa kuirudia.

4. Na *Twawafu* ndani ya msikiti mtakatifu hata kama ni mbali na *Al-Kaaba*.

5. *Al-Kaaba* iwe kushotoni kwa mwenye kutufu.

6. *Twawafu* iwe **mizunguko Saba** na uanze kwenye jiwe jeusi na umalizie hapohapo.

“Hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya Mtume ﷺ kama ilivyokuja katika sahihi mbili” (Al-Bukhari na Muslim).

7. Mizunguko ya *Twawafu ifuatane* isitenganishwe bila ya kuwepo na dharura kama itatenganishwa na mtu akaacha kufululiza bila ya kuwepo na dharura twawafu yake itabatilika na atapaswa kuirudia.

b) Sunna:

1. **Kwenda Matiti:** Ni sunna kwa wanaume wenye kuweza kufanya hivyo si kwa wanawake. Uhakika wa kwenda Matiti: Ni kutembea haraka haraka kwa anayefanya *Twawafu* pamoja na kuwa karibu karibu hatua zake na huko kuwa karibu karibu hatua zake ni sunna katika *Twawaful-Qudumi* (*Twawafu* ya kufika Makka) na katika ile mizunguko mitatu ya mwanzo tu.

2. **Kuliweka wazi bega** la kulia (kuvaa lubega) na hiyo ni sunna khasa katika *Twawaful-Qudumi* na ni kwa wanaume si kwa wanawake na ni wajibu katika mizunguko yote saba.

3. **Kulibusu jiwe jeusi** wakati wa kuanza *Twawafu* ikiwezekana. Isipowezekana itatosheleza kuligusa kwa mkono. Ikishindikana inatosha kuashiria, kama alivyokuwa akifanya Mtume ﷺ.

4. **Kutamka:**

بِسْمِ اللَّهِ وَاللَّهُ أَكْبَرُ، اللَّهُمَّ إِيْمَانًا بِكَ وَتَصَدِيقًا بِكِتَابِكَ وَوَفَاءً بِعَهْدِكَ وَاتِّبَاعًا
لِسُنَّةِ نَبِيِّكَ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ.

“Bismillahi Wallahu Akbaru. Allahumma Iyima-nan bika watasdiiqan bikita-bika wawafa-an bi’ahdika, Wattiba-an Lisunnati nabiiyika Muhammadin Swalla Llahu Alayhi Wasallam”

“Ewe Mola wangu wa haki nimekuwamini na nimekikubali kitabu chako na kutekeleza ahadi yako na nimefuata sunna ya Nabii wako Muhammad ﷺ.”

Utasema hivyo mara tu utakapoanza mzunguko wa kwanza.

5. **Kuomba dua** wakati wa *Twawafu* nayo haikuwekewa mipaka wala haikuainishwa bali kila Mtu ataomba kwa namna Allah alivyomuwezesha isipokuwa ni *Sunna* kila mzunguko kumalizia kwa kuomba dua hii:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

**“Rabana- A-tina Fi Dduniya Hasanata Wa Fil-Aakhirati
Hasana Waqina Adha-ba Nnaar”**

“Ewe Mola wetu tupe wema duniani na pia utupe wema akhera
na utukinge na adhabu ya moto.”

6. **Kuigusa** kwa mikono nguzo ya *Rukuni yamani*. Na kulibusu jiwe jeusi kila unapolipita wakati wa *twawafu* yake. Maana hivyo ndivyo alivyofanya Mtume ﷺ kama ilivyokuja katika sahihi.

7. **Kuomba dua** sehemu iitwayo *al-Multazim* wakati wa kumaliza *twawafu* na *Multazim* ni sehemu iliyo kati ya mlango wa *Al-Kaaba* na jiwe jeusi hivyo ndivyo alivyofanya Ibnu ‘Abbas -Allah awawiye radhi wote.

8. **Kuswali** raka mbili baada ya kumaliza *Twawafu* nyuma ya sehemu iitwayo *Makamu Ibrahimu*. Utasoma *Suratul Kafiruna* na *Suratul Ikhlas* baada ya *Fatiha* kwa tamko la Allah (s.w):

وَأَتَّخِذُوا مِنْ مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى

**“...Na alipo kuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa
kusalia...” (Al-Baqara 2: 125)**

9. **Kunywa** maji ya *zamzam* baada ya kumaliza kuswali raka mbili.

10. **Kurudia na** kuligusa jiwe jeusi kabla ya kutoka kwenda kwenye *Saayi*.

Ufafanuzi

Dalili za yote yaliyotangulia ni matendo ya Mtume ﷺ Katika Hijja ya kuaga.
c) **Adabu za Twawafu**

1. Mtu anatakiwa kutufu katika hali ya **unyenyekavu** na kuhudhurisha moyo na kutambua utukufu na ukubwa wa Allah (s.w) kuhofu adhabu zake na kutarajia neema zake.

2. **Kutozungumza** wakati wa kutufu isipokuwa kwa dharura na ukizungumza uzungumze mambo ya kheri tu kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Atakayezungumza asizungumze isipokuwa mambo ya kheri.”

3. **Usimuudhi** yeyote kwa maneno au vitendo. Kwani kumuudhi Muislamu ni jambo lililoharamishwa hasa kwenye nyumba ya Allah Aliye Mtukufu.

4. **Kuzidisha katika** kumtaja Allah (s.w) pamoja na kumuomba na kumtakia rehema Mtume ﷺ.

Somo la Sita

Katika Nguzo ya Tatu Saa'yi

Saayi ni kwenda matiti kati ya *Safa* na *Marwa* kwenda na kurudi, kwa nia ya kufanya Ibada. Nayo ni nguzo ya Hijja na Umra kwa kauli yake Allah Aliyetukuka.

✽ إِنَّ الصَّافَا وَالْمَرَوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ

“Kwa hakika Safa na Marwa ni katika alama za Dini ya Allah”
(Al-Baqara 2: 158)

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Fanyeni Saayi, kwa hakika Allah amewafaradhishia hiyo Saayi.”
(Imam Ahmad na Shafii)

Saayi ina masharti, Sunna na adabu zifuatazo:

a) Sharti za Saayi:

1). **Nia**; kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Kwa hakika kuswihi kwa amali kunategemea nia.”

Hivyo imekuwa hapana budi kutia nia ya kufanya Ibada ya *Saayi*, kwa ajili ya kumtii Allah (s.w), na kutekeleza amri Zake.

2). Kufuatisha kwa mpango kati ya (*Saayi*) na *Twawafu*, kwa kutanguliza *Twawafu* kabla ya *Saayi*.

3.) **Kufululiza** kati ya mizunguko yake, kipambanuzi kidogo kinaruhusiwa hasa kikiwa ni kwa dharura.

4). **Kukamilisha** hesabu ya mizunguko saba, kama ulipungua mzunguko mmoja au sehemu ya mzunguko basi haitatosha. Uhakika wake unasita kwa kukamilika mizunguko yake.

5). *Saayi* ifanyike baada ya *Twawafu* bila ya kujali kuwa *Twawafu* ilikuwa wajibu au ya Sunna. Isipokuwa lililo bora ni kuwa *Saayi* hutekelezwa baada *Twawafu* ya wajibu, kama ile *Twawafu Qudumi* au nguzo kama *Twawafu* ya *Ifaadha*.

b) Sunna za Saayi Nazo:

1. Kutembea haraka haraka, kwenda matiti, kati ya nguzo mbili zilizowekewa alama ya sehemu aliyoizunguka (Hajra) mama yake Ismail rehema na amani ziwashukie wote. Nayo ni Sunna kwa wanaume wenye kuweza si kwa wanyonge wala wanawake.

2. Kusimama *Safa* na *Marwa* kwa ajili ya Dua juu ya vilima hivyo viwili.

3. Kuleta dua kila unapofika *Safa* na kila unapofika *Marwa* kwa kila mzunguko katika mizunguko saba.

4. Kutamka: *Allahu akbar* mara tatu “Mwenyezi Mungu ni Mkubwa” kila unapopanda *Safa* na *Marwa* katika kila mzunguko pia kusema:

“Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah hali ya kuwa Peke Yake hana mshirika, ni Wake Ufalme na ni Zake Sifa Njema na Yeye juu ya kila kitu ni Muweza hapana mola ila Yeye Allah Amevishinda vikundi hali ya kuwa Peke Yake.”

5. Kufuatisha kati ya *Saayi* na *Twawafu* kisiingie kitu kati ya matendo haya mawili bila ya kuwepo na udhuru wowote wa kisheria.

c) Adabu za Saayi:

1. Kwenda kwenye *Saayi* kwa kutumia mlango wa *safa* hali ya kuwa unasoma kauli ya Allah (s.w.):

✽ إِنَّ الصَّافَا وَالْمَرَوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ^ط فَمَنْ حَجَّ الْبَيْتَ أَوْ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَنْ يَطُوفَ بِهِمَا ^ع وَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ اللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ ﴿١٥٨﴾

“Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anaye hiji kwenye Nyumba hiyo au akafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka. Na anaye jütendea mwenyewe kheri basi bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukrani na Mjuzi...” (Al-Baqara 2: 158)

2. Ni sharti kwa mwenye Kusaayi kuwa tohara.

3. *Saayi* ifanyike kwa kutembea kwa miguu kama itawezekana bila ya matatizo.

4. Kuzidisha dhikri na dua na kujishughulisha na hayo mawili na si mengineyo yasiyokuwa hayo.

5. Kuhifadhi macho yako na kutazama vitu au mambo ya haramu na kuzuia ulimi wako na madhambi.

6. Usimuudhi yeyote katika watu wanaofanya *Saayi* au watu wengine wanaopita kwa namna yoyote ya matamshi au ya vitendo.

7. Kuhudhurisha hisia za udhalili wako ndani ya nafsi yake na ufakiri wako na uhitaji wako kwa Allah (s.w.) katika kutafuta uongofu moyo wako na utakaso wa nafsi yako.

Somo la Saba

Nguzo ya nne nayo ni kusimama ‘*Arafa*’.

Amesema Mtume ﷺ:

(الحج عرفة)

“*Hijja ni ‘Arafa*”. (At-Tirmidhi na Abu Dawuud)

Na hakika yake ni kuhudhuria sehemu inayoitwa ‘*Arafa*’ kwa nia ya kuhudhuria, kusimama kuanzia baada ya adhuhuri ya siku ya tisa ya mwezi wa *Hijja* mpaka alfajiri ya siku ya kumi ya mwezi huo. Na ‘*Arafa*’ ina wajibu sunna na adabu zake:



a) Wajibu.

1. Kuhudhuria *Arafa* siku ya tisa ya mwezi wa *Hijja* baada ya kupinduka jua mpaka kuchwa kwake.
2. Kulala *Muzdalifa* baada ya kutoka ‘*Arafa*’ usiku wa siku ya kumi ya mwezi wa *Hijja*.
3. Kutupa vijiwe katika *Jamratul-‘Aqabat* siku ya kuchinja (siku ya Idd).
4. Kunyoa au kupunguza nywele baada ya kutupa vijiwe katika *Jamaratul-‘Aqabat* siku ya kuchinja.

5. Kulala Minna siku tatu nazo ni siku ya kumi na moja na kumi na mbili na kumi na tatu za mwezi wa *Hijja*. Au siku mbili kwa mwenye haraka nazo ni usiku wa siku ya kumi na moja na kumi na mbili.


6. Kuvitupia mawe vikuta vitatu baada ya kupinduka jua kila siku katika siku za *Tashriqi* tatu au mbili.

Ufafanuzi

Dalili na Ushahidi wa wajibu wa matendo yote haya ni matendo yake Mtume  na kauli yake Mtume .

“*Muige kutoka kwangu ibada zenu.*” (At-Tirmidhi)

Na amesema tena Mtume , “*Muhijji kama mlivyoniona nikihiji.*”

Na amesema tena Mtume .

“*Simameni katika sehemu zenu hakika nyinyi mko katika mirathi ya baba yenu Ibrahimu.*” (At-Tirmidhi)

b) Sunna za Arafa Nazo ni:

1. Kwenda Mina siku ya *Tarwiyat* - nayo ni siku ya nane ya mwezi wa *Hijja* na kulala huko usiku wa siku ya tisa na kutotoka huko mpaka baada ya kutoka jua kwa ajili ya Swala tano atakazoziswali huko.

2. Kuwepo kwako huko baada ya kupinduka jua (*Namira*) Na kuswali huko Swala ya adhuhuri na Alasir kwa kupunguza (kama swala za msafiri) na kukusanya pamoja na Imamu. (Katika msikiti wa namira)

3. Kufika sehemu ya ‘*Arafa*’ baada ya kuswali Swala ya Adhuhuri na Alasiri pamoja na Imamu na kuendelea kuwepo ‘*Arafa*’ na kumtaja kwa kumshukuru Allah (s.w) na kumuomba mpaka kuchwa kwa jua.

4. Kucheleweshwa Swala ya Magharibi hadi ufike *Muzdalifa*. Huko utaswali Magharibi na Isha kwa kukusanya pamoja kwa kuzichelewesha.

5. Kuhudhuria *Mash-aril-Haram* (Mlima Kuzahi) hali ya kuelekea *Kibla* na kumsabihii na kumdhukuru Allah (s.w)) mpaka kudhihirika kwa asubuhi.
6. Mpangilio: Unatakiwa kufanya ibada zote hizo kwa mpangilio maalum uliowekwa kati ya kutupa vijiwe *Jamratul- 'Aqabat* na siku ya Iddi kunyoa nywele na kukata na twawafu ya ziara (*Al-Ifadha*).
7. Kuifanya Twawafu ya ziara siku ya Iddi kabla ya kuzama kwa jua.

c) Adabu za Arafa.

1. Ni kutoka *Mina* asubuhi ya siku ya Tisa ya mwezi wa *Hijja* kuelekea *Namrat* Kupitia njia ya *Dhwabu*. kama alivyofanya Mtume ﷺ.
2. Kuoga baada ya kupinduka jua wakati wa mchana kwa ajili ya kuhudhuria 'Arafa na hiyo ni sheria iliyowekwa hata kwa mwenye hedhi na nifasi.
3. Kusimama sehemu aliyosimama Mtume ﷺ katika jiwe kubwa lililotandikwa lililoko chini ya *Jabal Rahmat* ambalo liko kati ya 'Arafa.
4. Kumtaja Allah (s.w.) kwa wingi na kuzidisha dua ukiwa umeelekea *Kibla* kwenye ile sehemu aliyosimama Mtume ﷺ mpaka kuzama kwa jua.
5. Kutoka 'Arafa kua ni kwa kupitia njia ya *Al-Maazamiin* si kwa kupitia njia ya *Dwabu* ambayo aliyojia. Kwani Mtume ﷺ katika miongozo yake alikuja na njia nyingine na kurudi na njia nyingine.
6. Kwenda kwa utulivu na kutofanya haraka kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Enyi watu jilazilimisheni na utulivu kwani wema si kwa kufanya haraka.” (Imam Ahmad)
7. Kuzidisha (*Talbiya*) kwa (kuitikia *Labbayka*) akiwa njiani kuelekea *Mina* na *Arafa* na *Muzdalifa* na *Mina* mpaka uanze kutupa vijiwe *Jamratul- 'Aqabat*.
8. Kuokota vijiwe Saba kutoka *Muzdalifa* kwa ajili ya kuvitupa katika *Jamratul - Aqabat*.

9. Kuondoka *Muzdalifa* baada ya kupambazuka na kabla ya kutoka jua.
10. Kwa haraka kwenda sehemu iitwayo *Muhsir* na kama itakuwa umepanda kumharakisha mnyama uliyempanda au kama ni gari uiendeshe kwa kasi kama hakutokuwa na madhara.
11. Kutupa vijawe *Jamratul-‘Aqabat* katika ule muda ulio kati ya kuchomoza kwa jua na kupinduka kwa jua.
12. Kutamka Allahu Akbar kila unapotupa kijiwe kimoja.
13. Uchinje mnyama wa kafara uombe dua wewe mwenyewe au ushuhudie wakati unapochinjiwa na kusema:

اللَّهُمَّ هَذَا مِنْكَ وَإِلَيْكَ، اللَّهُمَّ تَقَبَّلْ مِنِّي، كَمَا تَقَبَّلْتَ مِنْ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِكَ

“*Allahumma Hadha Minka Wailayka, Allahumma Taqabbal minniy, kama- Taqabalta min Ibrahiyima Khaliylika*”

“*Ewe Mola wangu kwa hakika mnyama anatoka kwako na anarudi kwako Ewe Mola wangu nikubalie kama ulivyomkubalia kipenzi chako Ibrahim.*”

Baada ya dua useme “*Ninaanza kwa jina la Allah na Allah ni Mkubwa.*”, Ni wajibu kusema maneno hayo.

14. Kula nyama ya mnyama uliyemchinja kwani Mtume ﷺ alikuwa akila ini la mnyama aliyemchinja.
15. Kwenda kwa miguu kutupa vijawe katika vikuta vitatu siku tatu za *Tashriq*.
16. Na kutamka Allah ni Mkubwa kila unaporusha jiwe na kuiomba dua:

اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ حَجًّا مَبْرُورًا، وَسَعْيًا مَشْكُورًا، وَذَنْبًا مَغْفُورًا.

“*Allahumma Ij’aluhu Hajan Mabruuran, Wasa’yan Mashkuuran, Wadhamban Maghruuran*”

“Ewe Mola wangu ijaalie Hijja yangu kuwa ni Hijja yenye kukubaliwa na ni mihangaiko yenye kushukuriwa na makosa yenye kusamehewa.”

17. Kusimama kwa ajili ya kuomba dua hali umeelekea Kibla baada ya kutupa vijiwe katika kikuta cha kwanza na cha pili isipokuwa cha tatu kwani hakuna dua yoyote inayotakiwa hapo. Mtume ﷺ alikuwa akitupa vijiwe katika kikuta cha tatu na kuondoka.

18. Tupa vijiwe katika *Jamratul-‘Aqabat* hali umeelekea kikuta hicho na *Al-Kaaba* iwe kushotoni kwako na *Mina* iwe kuumeni kwako.

19. Kwa anayetoka Makkah kusema,

“Aibuuna Taibuun, ‘Abiduuna Lirabinna Hamiduun, Swadaqa Llwahu Wa’adahu, Wanaswara ‘Abdahu, Wahazamal Ahzaab Wahdahu”

“Sisi Wenye Kurejea, Wenye Kutulia, Wenye Kuabudu, Wenye Kumsifu Mola Wetu, Amesadikisha Allah Ahadi Yake Na Amemnusuru Mja Wake Na Amevishinda Vikundi Hali Ya Kuwa Peke Yake.”

Mtume ﷺ alikuwa akisema maneno haya wakati wa kuondoka kwake Makka.

Somo la Nane

Kwa aliyeshindwa kuingia Makkah

Aliyeshindwa kuingia *Makka* au kushindwa kuhudhuria *‘Arafa* kwa sababu ya uadui au ugonjwa na mfano wake katika vizuizi vilivyo nje ya uwezo, itampasa mtu huyu kuchinja mbuzi/kondoo au ngamia au ng’ombe pale mahali alipozuiliwa au atampeleka *Makka* kama itawezekana hilo. Na atakua katika *Ihramu* yake, kwa kauli Yake Aliyetukuka:

فَإِنْ أَحْصَرْتُمْ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ط

“Na ikiwa mkizuiwa,basi (chinjeni) wanyama walio wepesi kupatikana.” (Al-Baqara 2: 196)

Somo la Tisa

“Twawaful – Wadaay” – Kutufu Twawafu ya Kuaga

Twawaful-Wadaay ni moja kati ya *Twawafu* tatu za *Hijja* nayo ni sunna iliyo wajibu na mwenye kuiacha bila ya kuwepo udhuru itamlazimu mtu huyo kuchinja mnyama wa kafara na mwenye kuiacha kwa udhuru hatolazamika kuchinja mnyama wa kafara.

Na *Twawaful-Wadaay* ataifanya mwenye kuhiji au mwenye kufanya ‘*Umra* wakati anapotaka kurudi kwao baada ya kumaliza *Hijja* yake au *Umra* yake na baada ya kumaliza muda wake wa kuwepo Makka ataifanya *Twawaful-Wadaay* saa yake ya mwisho ya kutaka kuondoka *Makka* kwa hali ambayo akimaliza kutufu tu hatoshughulika na kufanya chochote isipokuwa kuondoka *Makka* moja kwa moja. Na akiendelea kuwepo *Makka* kwa ajili ya kuuza au kununua na mengineyo bila ya dharura ya kufanya hivyo itamlazimu airudie tena *Twawaful*, kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Asiondoke mmoja wenu mpaka uwe mwisho wa muda wake ni kufika katika nyumba ya Allah Al-Kaaba.” (Muslim)

Somo la Kumi

Jinsi ya Kuhijji na Kufanya Umra

Maandalizi:

Mwenye kutaka kuhirimia moja kati ya ibada mbili hizi atalazimika kupunguza kucha zake, masharubu na anyoe nywele zake za kinena na kwapani kisha aoge na avae shuka mbili nyeupe moja ya kujifunga na moja ya kujitanda na avae kandambili na atakapofika *Miqati* Aswali Swala ya faradhi au sunna kisha atanuia ibada yake kwa kukariri: “*Nimeitika mwito Wako ewe Mola wangu wa haki,*

nimeitika mwito Wako kwa ajili ya Hijja.” Atasema hivyo kama ametaka kufanya Hijja peke yake.

Ama akitaka kutanguliza ‘*Umra* atasema (‘*Umra*) ama akitaka *Hijja* na ‘*Umra* atasema (*Hijja* na ‘*Umra*) na anayo ruhusa kujiwekea masharti kwa Bwana wake na atasema:

“Hakika mahali pangu pakufungua Ihram ni pale utakaponizuia.” (Ibn Majah)

Hakika kama mtu huyo akipatwa na kizuizi kitakachomzuia kuendelea na *Hijja* au *Umra* kama vile ugonjwa n.k. atafungua *Ihram* yake wala hatopaswa na chochote. Kisha ataendeleza *Talbiyah kwa*. (Kusema *Labbaika*). Hali ya kuinua sauti yake bila ya kujikaza sana. Ila mwanamke hatoinua sauti, si vibaya kama atainua sauti kwa kiasi cha kumsikia mwenzake aliye naye. Na inasuniwa kwake kusoma dua na kumswalia Mtume ﷺ kila anapomaliza *Talbiyah*, kama inavyosuniwa kuanza upya *Talbia* kila inapoanza upya hali yoyote ya kupanda au kushuka katika chombo cha usafiri au kuanza au kumaliza kuswali au kukutana na marafiki. Na anatakiwa kuzuia ulimi wake na kutaja chochote kisichokuwa utajo wa Allah pia kuzuia macho yake na kuangalia mambo yaliyoharamishwa.

Kama inatakiwa kwa hujaji kuzidisha wema na ihsani akiwa njiani hali ya kutaka *Hijja* yake iwe nzuri, awatendee wema wenye shida na anatakiwa kuwa mchangamfu mbele ya wenzake, mlaini wa maneno mwenye kuwapa salamu na chakula.

Na akifika *Makka* ni sunna kwake kuoga kwa ajili ya kuingia *Makka* akifika *Makka* ataingia kwa sehemu zake za juu na akifika *masjid-Haram* ataingia kwa mlango wa *Banii Shaibat*::

بِسْمِ اللَّهِ وَبِاللَّهِ وَإِلَى اللَّهِ اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ فَضْلِكَ

*“Naanza kwa jina la Allah na ni kwa Allah (s.w) marejeo yetu.
Ewe Mola wangu nifungulie milango ya fadhila Zako.”*

Na atakapoanza kuiona *Al-Kaaba* atainua mikono yake na kuomba dua:

اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ، وَمِنْكَ السَّلَامُ فَحَيِّنَا رَبَّنَا بِالسَّلَامِ. اللَّهُمَّ زِدْ هَذَا الْبَيْتَ تَشْرِيفًا
وَتَعْظِيمًا وَتَكْرِيمًا وَمَهَابَةً وَبِرًّا، وَزِدْ مِنْ شَرْفِهِ وَكِرْمِهِ مِمَّنْ حَجَّهَ أَوْ اعْتَمَرَهُ
تَشْرِيفًا وَتَعْظِيمًا وَتَكْرِيمًا وَمَهَابَةً وَبِرًّا. الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ كَثِيرًا، كَمَا هُوَ
أَهْلُهُ، وَكَمَا يَنْبَغِي لِكِرَمِ وَجْهِهِ وَعِزِّ جَلَالِهِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي بَلَّغَنِي بَيْتَهُ وَرَأَيْتُ
لِذَلِكَ أَهْلًا، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى كُلِّ حَالٍ. اللَّهُمَّ إِنَّكَ دَعَوْتَ إِلَى الْحَجِّ بَيْتِكَ الْحَرَامِ وَقَدْ
جَنَنْتُكَ لَذَلِكَ. اللَّهُمَّ تَقَبَّلْ مِنِّي وَاعْفُ عَنِّي، وَأَصْلِحْ لِي شَأْنِي كُلَّهُ. لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ.

“Allahumma antas-Salaam, waminkas-Salaam Fahhayyina Rabanna Bisallam. Allahumma Zid hadhal-Bayt tashrifan wata’adhiiman watakriiman wamhabat Wabirran. Wazid min sharafihii wakaramihii mimman hajjahu au ‘Itamarahu tashrifan wata’ghdhiiman watakriiman wamahabat wabiran. Alhamdulillah Rabil ‘Alamina Kathiiran, Kama huwa ahlahu, wakama yanbaghi likaram wajhihi wa’iz-jalalihii, Alhamdulillah lladhi balaghani baytahu waraaniy lidhalika ahlan, walhamdulillah ‘ala kuli haal. Allahumma inaka da’awta ilal Hajj baytikal Haraam waqad Ji-tuka lidhalika. Allahumma taqabbal minni wa’afu ‘anni, wa-aslih lii sha’ani kulahu. Laa ilaha illa anta..”

“Ewe Mola Wangu Ni Yako Amani Inatokana Na Wewe Amani. Tuhuishe Ewe Mola Wetu Kwa Amani. Ewe Mola Wangu Izidishe Nyumba Hii Utukufu Na Haiba Na Wema Na Uzidishe Utukufu Wake. Na Umtukuze Aliyehiji Nyumba Yako Au Aliyefanya Umra Kwa Utukufu Na Taadhima Na Ukarimu Na Heshima Na Wema. Sifa Njema Ni Za Allah Mola Wa Viumbe Vyote Kama Anavyostahiki Na Kama Inavyotakiwa Na Kwa Utukufu Wake Na Sifa Njema Ni Za Allah Aliyenifikisha Kwenye Al-Kaaba Yake Na Kuniona Kuwa Nastahiki Hilo. Na Sifa Njema Ni Za Allah Kwa Hali Yoyote. Ewe Mola Wangu Wa Haki Hakika Wewe Ndiye Uliyeniiita Kuhiji Nyumba Yako Tukufu Na Nimekujia Kwa Hilo. Ewe Mola Wangu Wa Haki Nikubalie Na Unisamehe Na Unitengenezee Mambo Yangu Yote, Hapana Mola Mwingine Ila Wewe.”

Kisha utaenda sehemu ya kutufia ukiwa msafi. utaliendea jiwe jeusi na utalibusu au utaligusa na utalitolea ishara kama hakuweza kulibusu au kuligusa kisha utaelekea jiwe na utasimama sawa sawa ukiwa mwenye kunuwia *Twawafu* yake kwa kuomba dua:

بِسْمِ اللَّهِ وَاللَّهُ أَكْبَرُ، اللَّهُمَّ إِيْمَانًا بِكَ وَتَصَدِيقًا بِكِتَابِكَ وَوَفَاءً بِعَهْدِكَ وَاتِّبَاعًا
لِسُنَّةِ نَبِيِّكَ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ.

“Bismillahi Wallahu Akbar, Allahumma Iymaanan bika watasdiiqan bikitabika wawafaa bi’ahdika watiba’an lisunna nabiiyika Muhammad Swalla Llwahu ‘alayhi wasallam”

“Naanza Kwa Jina La Allah Na Allah Ni Mkubwa. Ewe Mola Wangu Wa Haki Kwa Kukuamini Wewe Na Kwa Kukiamini Kitabu Chako Na Kutekeleza Ahadi Zako Na Kwa Kufuata Sunna Za Nabii Wako Muhammad ﷺ.”

Kisha utanza *Twawafu*, *Al-Kaaba* ikiwa kushotoni kwako hali ya kwenda mwendo wa haraka ukiwa uko katika *Twawafu-Quduumi* hali ya kuomba au kumtaja Allah au kumswalia Mtume ﷺ mpaka uelekee *Ruknul-Yamaniy* na utaigna kwa mkono wake na utamaliza mzunguko kwa kusoma dua nayo ni:

“Ewe Mola wetu tupe wema duniani na tupe wema akhera na utukinge na adhabu ya moto.”

Kisha utatufu mzunguko wa pili na wa tatu. Na utakapoanza mzunguko wa nne utaacha kwenda haraka haraka bali utaenda kwa utulivu mpaka ukamilishe mizunguko minne iliyobaki. Ukimaliza utaenda sehemu iitwayo *Multazim*, utaomba hali ya kulia na katika hali ya unyenyekevu kisha utaenda *Maqamu Ibrahim* utaswali nyuma yake raka mbili. Utasoma katika raka mbili hizo: *Suratul Faatihah* na *Suratil Kaafiruun* (raka ya kwanza) na *Suratil Faatihah* na *Suratul Swamadu* (raka iliyobaki). Baada ya kumaliza utaenda katika chenchen ya *Zamzam* utakunywa maji yake hali ya kuelekea *Al-Kaaba* mpaka kiu yako kiondoke na wakati wa kunywa utaomba dua unayoitaka akisema, *“Ewe Mola wangu hakika mimi nakuomba Elimu yenye kunufaisha na riziki kunjufu na kupona kila ugonjwa.”*

Kisha utaenda kulibusu au kuligusa jiwe jeusi huku ukisoma kauli ya Allah Aliyetukuka,

﴿ إِنَّ الصَّافَا وَالْمَرَوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللَّهِ ۖ ﴾

“*Hakika Swafaa na Marwa ni katika alama za Dini ya Allah*”.
(Al-Baqara 2: 158)

Mpaka ukifika *Swafa* utaelekea *Al-Kaaba* na utasema: “*Allah Mkubwa*” Mara tatu:

“*Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah Peke Yake asiyekuwa na mshirika Ameisadiki Ahadi Yake na Amemnusuru mja wake na Amevishinda vikundi hali ya kuwa Pekee Yake.*”

Kisha utaomba unachotaka katika kheri mbili, za duniani na akhera, kisha utashuka ukielekea *Marwa* na utaenda katika sehemu ya *Kusai* hali ya kumtaja Allah na katika hali ya kuomba mpaka ufike ndani ya bonde iliyoelekezwa ambayo sasa ina nguzo ya kijani ya pili kisha utarudia ukitembea kwa upole ukimtaja Allah (s.w.) ukiomba, ukimswalia Mtume (s.a.w.) mpaka ufike *Marwa* na hapa utasema: *لا إله إلا الله*, ‘*Lailah- illa Allah.*’ Na utaomba kama ulivyofanya ulipokuwa *swafa* kisha utashuka kwa mguu mpaka ndani ya *Wady* (Bonde). Akitoka utaenda hadi ufike *Swafa* utapanda na utasema *Allahu Akbar* na *Laila-ha Illa Allah*. Na utaomba kisha utashuka kuelekea *Marwa* utafanya kama ulivyofanya mara ya kwanza mpaka utimize mizunguko saba kwa visimamo vinane, visimamo vinne *Swafa* na vinne *Marwaa* kisha ukiwa kama mwenye kufanya ‘*Umrah* utapunguza nywele zako na utafungua *Ihramu* yako na itakuwa imetimia ‘*Umrah* yako. Vile vile ukiwa ni mwenye kufanya *Umra* pekee na baadaye ndio uende kwenye *Hijja* basi itakuwa imetimia ‘*Umrah* yako kwa kumaliza tu kutoka kwenye *Saayi* na kupunguza nywele zako na ukiwa mwenye kunuia *Hijja* pekee au *Hijja* na ‘*Umrah* pamoja itakupasa kubakia katika *ihramu* yako hadi au uhudhurie *Arafat* na utupe vijiwe katika kikuta cha *Aqaba* siku ya Iddi na wakati huo ndio utakuwa umetokana na *Ihramu* yako. Na itakapokuwa ni siku ya *Tarwiyat* ambayo ni siku ya nane ya mwezi wa *Hijja* utahirimia nia ya *Hijja* kwa namna ile ile unayohirimia ‘*Umrah* ukiwa mwenye kunuia ‘*Umrah* pekee.

Ama *Hijja* pekee au *Hijja* pamoja na ‘*Umrah* zitakuwa kama ilivyo katika Ithramu yao ya kwanza na utatoka ukisema: **لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ**, ”*Nimeitika Mwito Wako Ewe Mola Wangu Kwa Hakika Nimeitika Mwito Wako.*” Mpaka kufika Mina asubuhi na utakuwepo huko siku nzima na usiku na utaswali huko Swala tano mpaka litakapochomoza jua siku ya ‘*Arafat*. Utatoka *Mina* hali ya kusema, “**Labbaika - Talbiya** ukielekea *Namrat* kupitia njia ya *Dhhabbu* utakuwepo huko hadi kupinduka jua kisha utaoga na utaenda msikitini sehemu aliyoswali Mtume ﷺ utaswali pamoja na Imamu Adhuhuri na Alaasir kupunguza pamoja na kukusanya kwa kutanguliza na ukisha swali utaenda ‘*Arafat* kwa kuhudhuria ‘*Arafat* na utasimama sehemu yoyote ya *Arafat* unayoitaka kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“*Nilisimama hapa na Arafa pote ni mahali pa kusimama.*” (Muslim).

Ukisimama kwenye mawe chini ya *Jabal Rahmat* ni vizuri nayo ni sehemu aliyosimama Mtume ﷺ unaweza kusimama ukiwa juu ya kipando au kusimamia kwa miguu au kukaa ukimtaja Allah Mtukufu na kumuomba, mpaka kuchomoza kwa jua. Na kuingia sehemu ndogo ya usiku.

Kisha utaondoka kwa upole ukisema *Talbiyah* ukielekea *Muzdalifah* kupitia njia ya *Al-Maazimin* utashuka huko na kabla hujaweka kipando chako utaswali Magharibi na kisha ndio utaweka kipando chako na utaswali Isha. Na utalala hapo mpaka Alfajiri na utaswali Swala ya Asubuhi na utaenda *Al-Mash-’ aril-Haram* utasimama hapo utafanya *Tahlil* na *Takbira* hali ya kuomba na utasimama sehemu yoyote katika *Muzdalifah* kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“*Nilisimama hapa na pote hapa ni mahali pa kusimama.*” (Muslim)

Mpaka itakapodhihiri asubuhi na kabla ya kutoka kwa jua utaokota vijjiwe saba ili uvitupe katika kikuta cha ‘*Aqaba (Jamratul ‘Aqaba)* na halafu uondoke kwenda *Mina* huku ukisema **Labbaika** utakapofika sehemu iitwayo *Muhsira* utamtikisa mnyama wake, na kwenda haraka, kiasi kama cha kutupa jiwe, na ukifika *Mina* utaenda weye mwenyewe hadi kikuta cha ‘*Aqaba* utakitupia kikuta hicho vijjiwe saba wakati wa kutupa utainua mkono wako wa kulia huku ukisema: **الله أكبر**, “*Allah ni Mkubwa*”. Na ukizidisha maneno yafuatayo itakuwa vizuri nayo ni:

اللهم اجعله حجاً مبروراً، وسعيًا مشكوراً، وذنباً مغفوراً.

*“Allahumma ij’alhu Hajjan Mabruuran, Wasa’ayan Mashkuwran,
Wa Dhanban Maghfuwra-”*

*“Ewe Mola wa haki ijalie iwe Hijja yenye kukubaliwa na
mihangaiko yenye kushukuriwa na dhambi yenye kusamehewa.”*

Kisha ukiwa na mnyama uliyemkusudia ukamchinje au ukampe mtu atakayemchinjia kama mwenyewe ukishindwa, anachinjwa sehemu yoyote anayoitaka kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Sehemu hii na Minaa zote hizi ni sehemu za kuchinja.” (Muslim na Abu Dawud)

Kisha utanyoa au utapunguza na kunyoa ni bora zaidi na mpaka hapa utakuwa umefunguka na kifungo kidogo huwi tena ni mwenye kuhirimia isipokuwa wanawake kwa kauli yake Mtume ﷺ:

*“Atakapokitupia mawe kikuta cha Aqaba na akanyoa hakika
kimekuwa halali kwake kila kitu isipokuwa wanawake.”* (Abu Dawud)

Unaweza kufunika kichwa chako na kuvaa nguo zako kisha uende *Makka* ikiwezekana ili ukatufu *Twawaful Ifadha* ambayo ni moja ya nguzo nne za Hijja na utaingia msikitini ukiwa msafi utafanya *Twawafu* kama ulivyofanya *Twawaful-Qudumi* isipokuwa hutofungua bega lako wala hutotembea haraka katika mizunguko mitatu ya mwanzo na ukimaliza mizunguko saba utaswali raka mbili nyuma sehemu iitwayo (Makamu) na ukiwa ama huhiji au unafanya *Umra*, na umeshafanya *Saayi* pamoja na *Twawaful Qudumi* katika *Saayi* yako ni kwanza imetoshwa, na ukiwa unafanya ‘Umra peke yake utatoka kwenda sehemu ya kufanya *Saayi* na Utasay kati ya *Swafaa* na *Marwa* mizunguko saba kwa aina ile ile ya mwanzo na ukimaliza *Saayi* yako utakuwa umeshafunguka na kuliko kamili na hutokuwa ni mwenye kuanzia hapo hakitokuwa haramu tena kwa mtu huyo kitu kilichozuiliwa wakati wa ibada ya Hijja. Na utakuwa uko huru ni halali kwako kufanya yale uliyozuiliwa kuyafanya kwa sababu ya *Ihramu* kisha siku hiyo hiyo utarudi Minaa na utalala huko jua likipinduka siku ya kwanza katika siku tatu za

Tashriki (siku za Idd) utaenda kwenye vikuta utatupa mawe kwenye kikuta cha kwanza na ni ambacho kiko karibu na Msikiti Halafu ukitupie vijawe saba kimoja baada ya kingine na utasema *Allahu Akbaru* (Allah Mkubwa) kila unapotupa kijiwe kimoja ukimaliza kutupa vijawe utapumzika kidogo baadaye utaelekea Kibla na kuomba dua kisha utaenda kwenye kikuta kilicho katikati utakitupia mawe kama ulivyokitupia mara ya kwanza na utapumzika kidogo na utaelekea Kibla na utaomba kisha utaenda kikuta cha 'Aqaba nacho ndicho cha mwisho na utakitupia vizuri vijawe saba na utapiga *Takbira* kila unapotupa kijiwe kimoja. Wala hutoomba baada ya kumaliza kwani Mtume ﷺ hakuomba wakati akitupa cha mwisho. Na utaondoka likipinduka jua kwa siku ya pili utatoka kwenda kuvitupia mawe vikuta vitatu kwa namna iliyotangulia kisha ukiwa na haraka utaenda *Makka* siku hiyo hiyo kabla ya kuchwa jua.

Na kama huna haraka utalala huko huko *Minaa* na likipinduka jua siku ya pili utavitupia mawe vikuta kama ilivyotangulia kisha utasafiri kwenda *Makka* na unapoazimia kurudi kwako utafanya *Twawafu* ya kuaga mizinguuko saba na baadaye utaswali rakaa mbili nyuma ya *Maqamu Ibrahimu*. Na utaondoka kurudi kwao ukiwa unasema:

لا إله إلا الله وحده لا شريك له، له الملك وله الحمد وهو على كل شيء
قدير. آتوبون تائبون، عابدون لربنا حامدون، لا إله إلا الله وحده، صدق وعده،
ونصر عبده، وهزم الأحزاب وحده.

“*Hapana Mola Apasaye Kuabudiwa Kwa Haki Ila Allah Hali ya Kuwa Peke Yake Hana Mshirika. Ni Wake Uflame Na Ni Zake Sifa Njema Na Yeye Juu Ya Kila Kitu Ni Muweza. Ni Wenye Kurejea, Ni Wenye Kutubia, Ni Wenye Kuabudu Ni Wenye Kusujudia Ni Wenye Kumsifu Mola Wetu. Hapana Mola Apasaye Kuabudiwa Kwa Haki Ila Yeye Allah Hali Ya Kuwa Peke Yake, Ameisadikisha Ahadi Yake Na Amemnusuru Mja Wake Na Amevishinda Vikundi Hali Ya Kuwa Peke Yake.*”



Mada ya Kumi na Tatu

Ziara katika Msikiti wa Mtume ﷺ na Kumtolea Salam Kwenye Kaburi lake Tukufu

Somo la Kwanza

Ubora wa Mji wa Madina Msikiti wa Mtume ﷺ, na Watu wake.

a). Ubora wa Mji wa Madina:

Madinatul Munawarah ni mji Mtukufu wa Mtume ﷺ na ndiyo mji aliohamia, na ni mji ulipokuwa ukishukia Wahyi. Utukufu wa mji huu aliutangaza Mtume Muhammad ﷺ kama Nabii Ibrahim alivyotangaza utukufu wa mji wa Makka pale aliposema:

“Ewe Mola hakika Nabii Ibrahim aliitangaza Makka kuwa ni Tukufu na mimi nalitangaza eneo lililoko kati ya Labataiha (vilima vivili viko Mashariki na Magharibi mwa mji huo).” (Al-Bukhari na Muslim)

Kisha Mtume ﷺ akasema:

“Madina ni Mji mtakatifu kuanzia Airi mpaka Thauri. Atakayefanya uzushi wowote katika eneo lake, au akamlinda mwenye kufanya uzushi katika eneo hilo, basi itakuwa juu yake laana ya Allah na Malaika na watu wote, na haitopokelewa (toba yake) kwa kutoa mali wala kwa kufanya fidia. Si ruhusa kwa mtu kukata majani yake, wala kuwinda wanyama wake, wala kuokota mali ya mtu iliyopotea isipokuwa kwa kuihifadhi wala haifai kwa mtu kubeba silaha kwa ajili ya vita humo. Wala si ruhusa kukata mti katika eneo hilo isipokuwa kwa nia ya kuwapa malisho ngamia wake.” (Imam Ahmad).

Na amesema Adiy bin Zaid رضي الله عنه:

“Ameupa himaya Mtume ﷺ mji wa Madina katika pande zake zote. Haikatwi miti yake, wala haingolewi ila kwa kiasi cha kuwalisha Ngamia.” (Abu Dawuud).

Na Mtume ﷺ amesema:

“Hakika imani inapata nguvu kwa watu wa Madina kama anavyopata nguvu nyoka anapokuwa katika shimo lake. Hafanyi subira mtu yeyote kwa matatizo yanayompata akiwa katika mji wa Madina ila nitakuwa muombezi wake au shahidi yake siku ya Qiyama.” (Al-Bukhari, Muslim na Ibn Majah).

Mtume ﷺ amesema:

“Mwenye kuweza miongoni mwenu kufia Madina basi afanye hivyo, kwa hakika mimi namtolea ushahidi yule anayefia hapo.” (Ibn Majah na Imam Ahmad).

Mtume ﷺ amesema:

“Hakika mji wa Madina ni kama fukuto (kichochea moto cha fundi chuma) kinawakataa (wachuja) watu wabaya na kuwanasih (waongoza) watu wazuri.” (Muslim).

Na amesema Mtume ﷺ:

“Madina ni mji bora kwao laiti wangelikuwa wanajua. Hauachi mtu yoyote kwa kuuchukia ila Allah ataleta badala yake mtu wa kheri kuliko yeye, na wala havumilii yoyote juu ya matatizo na tabu za mji huo, ila mimi nitakuwa muombezi au shahidi yake siku ya qiyama.” (Muslim).

b). Ubora wa Watu wa Madina:

Watu wa Madina ni jirani za Mtume ﷺ na waimarishaji wa Msikiti wake na wakazi wa mji wake, na wenye mshikamano katika eneo lake takatifu na wenye kuihami mipaka yake. Watu hao wakiongoka na wakawa wema, watakuwa juu ya watu wengine kwa cheo na utukufu na itawajibika kuwaheshimu na italazimika kuwapenda na kuwafanya viongozi.

Mtume ﷺ alitahadharisha kuwa wasifanyiwe maudhi kwa kusema:

“Yeyote anayewafanyia vitimbi watu wa Madina huyayuka kama chumvi inavyoyayuka katika maji.” (Al-Bukhari).

Kisha akasema Mtume ﷺ:

“Hakuna mtu anayewatakia ubaya watu wa Madina ila Allah atamyayusha katika moto kama inavyoyeyuka risasi au inavyoyayuka chumvi katika maji.” (Muslim).

Na akawaombea Dua watu wa Madina waongezewe riziki zao kwa mapenzi yake na kuwakirimu aliposema

“Allahumma wabarikie katikia vipimo vyao na vibaba vyao.”
(Al-Bukhari na Muslim)

Na Mtume aliwausia umati wake kuwafanyia kheri watu wa Madina aliposema:

“Madina ni mahamio yangu na hapo ni malazi yangu na hapo ndipo nitakapofufuliwa, ni haki juu ya umati wangu kuwalinda jirani zangu kwa muda ambao watakuwa hawatendi madhambi makubwa (kabair) na atakayewalinda (kuwahifadhi) nitakuwa muombezi wake au shahidi yake siku ya Kiyama.” (Ibn ‘Adii na Tabarani).

c). Ubora wa Msikiti Mtukufu wa Mtume ﷺ:

Msikiti wa Mtume ﷺ ni moja ya Misikiti mitatu ambayo Qur-aan imeitaja, pale Allah Anaposema:

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى
الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا الَّذِي بَرَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ

“SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.” (al-Israa 17:1).

Katika neno (Msikiti wa mbali zaidi) mna ishara ya wazi inayotaja kuwepo kwa Msikiti wa Mtume, kwani neno ‘Āqswa’ lina maana ya mbali zaidi na hiyo ni ishara ya kuwepo Msikiti wa mbali, lakini siyo mbali zaidi. Na kwa aliyoko Makkah Msikiti wa mbali ni ule wa Madina na msitikiti wa mbali zaidi ni ule wa Baitul Muqaddas- Palestina. Hivyo kuutaja Msikiti wa Madina kwa ishara wakati wa kutaja Misikiti miwili, hiyo ni kwa kuwa kipindi ilipoteremka Aya hii ilikuwa Msikiti wa Madina bado haujajengwa. Na Mtume ﷺ amesema katika kubainisha utukufu wa Msikiti huo:

“Kuswali Swala moja katika Msikiti wangu huu ni bora kuliko kuswali Swala elfu moja katika Msikiti usiyokuwa huu, isipokuwa Msikiti Mtakatifu wa Makkah. Na Swala moja katika Msikiti wa Makkah ni bora kuliko kuswali swala laki moja katika Misikiti mingine.” (Muslim).

Na ameufanya (Msikiti huu) kuwa wa pili wa Misikiti mitatu sehemu pekee zinazoruhusiwa kwa Muislamu kuzifungia safari za Ibada. Amesema Mtume ﷺ:

“Haifungwi safari ila kwenda kwenye Misikiti mitatu: Msikiti wa Makkah na Msikiti wangu huu na Msikiti wa Baitul Muqaddas.”

Na (Allah) amehusisha Msikiti huu sifa bora na (mambo mengine) ambayo hayapatikani katika Misikiti mingine mambo kama vile;

1. **Raudhah Tukufu** ambayo Mtume ﷺ ameitaja kwa kusema:

“Eneo lililopo kati ya nyumba yangu na mimbari yangu ni kiwanja miongoni mwa viwanja vya peponi.” (Al-Bukhari, Muslim na At-Tirmidhi).

2. Na imepokewa kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

“Mwenye kuswali katika Msikiti wangu Swala Arobaini (mfululizo) bila kupitwa na Swala yoyote ataachwa huru kutokana na moto, huru kutokana na adhabu na huru kutokana na unafiki.” (Imamu Ahmad, Tabarani na At-Tirmidhi).

Kutokana na msisitizo wa hadithi hii, ndiyo maana ziara katika Msikiti huu kwa ajili ya kuswali ndani yake, ni moja ya ibada ambazo Muislamu hujikurubisha kwazo mbele ya Mola wake katika kumuomba akidhi haja zake na kufuzu kwa kupata radhi zake ﷻ.

Somo la Pili

Ziara katika Msikiti wa Mtume ﷺ na Kumtolea Salamu Mtume na Maswahaba Zake Wawili

Kuzuru msikiti wa Mtume ﷺ ni ibada na kwa hiyo inatakiwa kuweka nia kama zilivyo ibada zingine, kwani amali huzingatiwa kwa nia, basi Muislamu anapofanya ziara katika Msikiti wa Mtume ﷺ, anatakiwa kwa ziara yake hiyo anuwie kuswali ndani yake kwa nia ya kujikurubisha kwa Allah (s.w) na kuonyesha mapenzi kwa Mtume wake. Utakapofika Msikitini huku ukiwa tayari umejitoharisha utatambuliza mguu wako wa kulia kama ilivyo sunna kwa mwenye kuingia Msikitini, na utasema:

بِسْمِ اللَّهِ ، اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى نَبِيِّنَا مُحَمَّدٍ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذُنُوبِي ، وافتح لي أبواب رحمتك

“Kwa Jina La Allah (s.w) Na Rehma Na Amani Ziwe Juu Ya Mjumbe Wa Allah, Ewe Mwenyeezi Mungu Nisamehe Dhambi Zangu Na Unifungulie Milango Ya Rehema Zako”.

Kisha uende katika sehemu ya *Raudha* kama utakuta bado pana nafasi, kama hapana nafasi utasimama eneo lolote ndani ya Msikiti na utaswali rakaa mbili, au utaswali kwa kadiri utakavyojaaliwa. Kisha utakwenda kwenye chumba kitukufu (alikoziwa Mtume ﷺ) utamtolea salamu Mtume ﷺ, utasimama ukiwa umelielekea kaburi lake, utamtolea salamu kwa kusema:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نَبِيَّ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا خَيْرَةَ خَلْقِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّكَ عَبْدٌ وَرَسُولُهُ، قَدْ بَلَغْتَ الرِّسَالَةَ وَأَدَيْتَ الْأَمَانَةَ، وَنَصَحْتَ الْأُمَّةَ، وَجَاهَدْتَ فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْكَ وَعَلَى آلِكَ وَأَزْوَاجِكَ وَذُرِّيَّاتِكَ، وَسَلَّمَ تَسْلِيمًا كَثِيرًا.

“Assalamu ‘alayka Ya Rasula Llah! Assalamu ‘alyka Ya Khira Khalqi Llah! Assalamu ‘alayka Ayuha Nabiyy Warahmatullah Wabarakatuh, Ash-hadu an La ilaha Ila Llah, wa-ash-hadu anaka ‘abdu Warasuuluhu, Qad Ballaghta Rrisala Wa-adaytal Amana, Wanasahat Umma, Wajahadta fiy Llahi Haqa Jihaadihi, Swalla la Llwahu ‘alayka wa’ala Aalika wa-azwajika wadhuriyatika, wassalim Tasliiman Kathiiran”.

“Amani Ziwe Juu Yako Ewe Mjumbe Wa Allah, Amani Ziwe Juu Yako Ewe Mbora Wa Viumbe Wa Allah, Amani Ziwe Juu Yako Ewe Nabii Na Rehema Za Allah Na Baraka Zake. Nashuhudia Kuwa Hapana Mola Apasaye Kuabudiwa Ila Mwenyeezi Mungu Na Nina Shuhudia Kuwa Wewe Ni Mja Wa Allah Na Ni Mjumbe Wake. Hakika Ulifikisha Ujumbe, Na Ulitekeleza Amana Na Uliupa Nasaha Umma Na Ulijitolea Kwa Ajili Ya Allah Kwa Kufanya Jihadi Ya Kweli. Allah Ateremshe Amani Juu Yako Na Juu Ya Aali Zako Na Sahaba Zako, Wake Zako Na Kizazi Chako Ewe Mola mteremshie Amani Nyingi.”

Minhajil Muslim

Kisha utasogea kando kidogo upande wa kulia, utamtolea salamu Abu Bakr Siddiq رضي الله عنه kwa kusema:

“Amani ziwe juu yako ewe Abu Bakr Siddiq uliye msafi kwa Mjumbe wa Allah na mwenzake katika pango, Allah akulipe kheri kutokana na umma wa Mjumbe wa Allah”.

Kisha utasogea kidogo upande wa kulia na utamtolea salamu ‘Umar bin Khatab رضي الله عنه kwa kusema:

“Amani ziwe juu yako ewe Umar ul- Faruq na rehma za Allah na baraka zake, ukulipe Allah kutokana na ummati wa Muhammad kila kheri.

Kisha utaondoka. Iwapo utataka kufanya *tawasul* kwa Allah kwa ziara yako hiyo, utasogea mbali kidogo na eneo hilo lenye makaburi kisha utaelekea *qibla* na utamuomba Allah kwa dua yoyote uitakayo na utamuomba kutokana na fadhila zake akupe kila ukitakacho. Na hapo itakuwa ziara ya kuzuru Msikiti wa Mtume imekamilika. Ukitaka utasafiri na ukitaka unaweza kuendelea kukaa (Madina), isipokuwa vyema ukiendelea kukaa Madina, Swala zote uswalie katika Msikiti wa Mtume ﷺ na hasa kwa kuwa imepokewa hadithi ya Mtume inayowataka Waislamu waswali huko Swala arubaini.

Somo la Tatu

Ziara ya Sehemu Takatifu Katika Mji wa Madinah

Ni vizuri Muislamu anapojaaliwa na Allah (s.w) kwenda Madina kufanya ziara ya Msikiti wa Mtume ﷺ na kuzuru kaburi lake ﷺ Baada ya hapo atembelee *Twayiba* (Madina) na kufika Msikiti wa *Quba* kwa ajili ya kuswali ndani yake kwani Mtume ﷺ alikuwa akizuru na kuswali ndani yake na hivyo hivyo walifanya masahaba zake baada yake na alisema Mtume ﷺ:

“Mwenye kujitoharisha nyumbani kwake, na akifanya vizuri tohara yake, kisha akaja Masjid Quba kwa ajili ya kuswali katika Msikiti huo, atapata malipo ya mtu aliyefanya ‘Umrah.’” (Ibnu Majah).

“Mtume ﷺ akienda Masjid Quba akiwa amepanda mnyama au kwa miguu, akishafika anaswali humo raka mbili.” (Muslim).

“Pia akizuru makaburi ya mashahidi yaliyoko Uhudi. Mtume ﷺ alikuwa akienda kuyazuru makaburi yao na kuwatolea salamu.”

Na kwa ziara hii ya mashahidi wa Uhudi itakuwa ni nafasi nzuri kwa mtu huyo kuushuhudia mlima wa Uhudi, mlima ambao Mtume ﷺ ameutaja kwa kusema:

“Uhudi ni mlima unaotupenda na sisi tunaupenda.” (Al-Bukhari)

“Uhudi ni Mlima miongoni mwa milima ya peponi.” (Tabarani).

Siku moja mlima wa Uhudi ulitikisika chini ya miguu ya Mtume, alipokuwa amesimama juu ya mlima huo akiwa pamoja na Abu Bakr, ‘Umar na Uthman, Mtume ﷺ aliuambia:

“Tulia Uhudi na akaupiga (akaukanyaga) kwa mguu wake hakuna aliyejuu yako ila ni Nabii na Siddiq na mashahidi wawili.” (Al-Bukhari).

Mtu akipata nafasi pia azuru makaburi ya Baqii, kwani Mtume ﷺ alikuwa akizuru watu wa makaburi hayo na kuwatolea salamu. Kama ilivyopokewa katika hadithi sahihi, kuwa Baqii imekusanya maelfu ya masahaba na tabiina na wengine miongoni mwa waja wema wa Allah. Tembelea Baqii na utawatolea salamu masahaba waliozikwa katika makaburi ya hapo:

((السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُسْلِمِينَ أَنْتُمْ سَابِقُونَ، وَإِنَّا إِن شَاءَ اللَّهُ بِكُمْ لَاحِقُونَ، يَرْحَمُ اللَّهُ الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنَّا وَمُنْكُمْ وَالْمُسْتَأْخِرِينَ. نَسْأَلُ اللَّهَ لَنَا وَلِكُمُ الْعَافِيَةَ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ. اللَّهُمَّ اغْفِرْ لَنَا وَلَهُمْ، وَارْحَمْنَا وَإِيَّاهُمْ، اللَّهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا أَجْرَهُمْ، وَلَا تَفْتِنَّا بَعْدَهُمْ))

Minhajil Muslim

“Assalamu Alaykum ahla Ddiyaari minal-muuminiin wal-muslimiin, antum saabiquun Wainna InshaAllah Bikum Laahiquun. YarhamuLlahul-Mustaqdimiina Minna Waminkum wal-Musta-akhirina. Nas-alu Llahu lanaa Walakumul-’Afiya fy Dunya wal-Akhira. Allahumma ghfir Lana Walahu, Warhamna Waiyaahum. Allahumma La Tahrimna Ajrahum, Wala Taftinna Ba’dahum.”

“Amani ziwe juu yenu watu wa nyumba hizi miongoni mwa waumini na Waislamu, nyingi ni wenye kutangulia nasi Allah akipenda ni wenye kuja. Awarehemu Allah wenye kutangulia katika sisi na nyinyi na wenye kuchelewa. Tunamuomba Allah afya kwetu na kwenu duniani na akhera. Ewe Allah tusamehe sisi na wao, na uturehemu sisi na wao. Ewe Mola usitunyime malipo yao na wala usitufitini baada yao.” (Muslim)



Mada ya Kumi na Nne
Udhhiya na ‘Aqiqa
Mada Mbili: Somo la kwanza
Udhhiyah

1. Maana ya Udhhiyah:

Udhhiya ni mnyama anayechinjwa siku ya Iddi (ya mfungo tatu) kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allah (s.w).

2. Hukumu Yake:

Kuchinja ni sunna ambayo ni wajibu kwa kila watu wa nyumba ya Muislamu ambaye amejaliwa kuwa na uwezo nayo. Ushahidi wa sunna hii ni kauli yake Mtume ﷺ:

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَأَنْحَرْ

“Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili yake).”
(al Kauthar 108:2).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Aliyekuwa amechinja kabla ya Swala basi achinje tena.” [Al-Bukhari, Muslim na An-Nasai].

Na kauli ya Abi Ayub ul-Answari:

“Alikuwa mtu katika enzi ya Mtume ﷺ anachinja mbuzi (wa Udhuhiya) kwa ajili yake na watu wa nyumbani kwake.” (At-Tirmidhi).

3. Ubora Wa Udhiya

Mtume ﷺ anashuhudia ubora wa *Udh-hiya*:

“Hakuwahi kufanya amali njema mwanadamu siku ya Iddi ya kuchinja anayoipenda sana Allah (s.w) kama kuchinja mnyama wa kafara, na kwa hakika mnyama wa udhiya atakuja siku ya Qiyama akiwa na pembe zake na kucha zake na manyoa yake, na kwa hakika damu yake ina thamani kubwa mbele ya Allah kabla ya mnyama huyo kuchinjwa, hivyo zifurahisheni nafsi zenu kwa kuchinja udhiya.” (Ibn Majah na At-Tirmidhi).

Na kauli yake Mtume ﷺ watu walipomuuliza: Nini hizi *udhiya*? Naye akajibu:

“Ni sunnah ya baba yenu Ibrahim.” Wakasema, ‘na sisi tutapata nini?’ akasema Mtume ﷺ kuwaambia: “Kwa kila unywele ni jema.”, wakasema na je, ‘sufi?’ Akasema Mtume ﷺ “Na kila unywele wa sufi ni jema moja.” (Ibn Majah, Imam Ahmad)

4. Hekima yake:

a) **Kujikurubisha kwa Allah (s.w)** kwa kuchinja mnyama, kwani Allah (s,w) Anasema:

“Hakika swali kwa ajili ya Mola wako, na chinja kwa ajili ya Mola wako”.

Kisha anasema:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ ۗ

“Sema hakika Swala yangu na ibada zangu na uzima wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hana Mshirika...” (Al-An-A’am 6: 162-163).

Na neno *nusuki* katika aya hii maana yake ni kuchinja kwa nia ya kujikurubisha kwa Allah (s.w).

b) **Kuhuisha sunna** ya Imamu (kiongozi) wa watu wa *Tauhidi* Nabii Ibrahim, amani ziwe juu yake Allah alipompelekea *Wahyi* (amri) wa kumuamrisha amchinje mwanawe Ismail, kisha akamfidia kwa kondoo. Akachinja kondoo badala ya mwanawe. Allah Amesema:

وَقَدَيْنَهُ بِذَبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١٧٠﴾

“*Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa Mtukufu.*”
(As- Swafat 37:107).

c). **Kuifanyia wasaa familia** siku ya *Iddi* na kueneza furaha ya sikuku kwa mafakiri na masikini na kuhurumiana miongoni mwa jamii.

d). **Kumshukuru Allah** (s.w.) kwa kuwalisha wanyama hao kwetu kama anavyosema ndani ya Qur-aan:

فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطِعُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ كَذَلِكَ سَخَّرْنَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

﴿١٧١﴾ لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَائُهَا وَلَكِنْ يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنْكُمْ كَذَلِكَ

سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْنَاكُمْ وَبَشِّرِ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٧٢﴾

“...kuleni katika hao na walisheni walio kinai na wanao lazimika kuomba. Ndio kama hivi tumewafanya hawa wanyama dhalili kwenu ili mpate kushukuru. Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamngu wenu. Namna hivi tumewadhalilisha kwenu ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa alivyo kuongoeni. Na wabashirie wafanyao mema.” (al-Hajj 22: 36-37).

5. Hukumu za *Udhhiya*:

a). **Umri wake:** katika *udhhiya* haifai kuchinja kondoo ambaye hajawa *Jadha* na *jadha* ni ambaye ana umri wa mwaka au amekaribia kufikisha mwaka. Ama kwa mbuzi, ngamia na ngómbe, haifai kuchinja aliye na umri chini ya *Thaniyu*. Na *Thaniyu* katika mbuzi ni mwenye umri wa mwaka mmoja na ameingia mwaka wa pili. Na katika ngamia ni mwenye umri wa miaka minne na ameingia katika mwaka wa tano. Na katika ngómbe ni aliyekamilisha umri wa miaka miwili na ameingia mwaka wa tatu. Kwa ushahidi wa kauli yake Mtume ﷺ:

*“Wala msichinje ila musinna isipokuwa kama itakuwa tabu juu yenu kumpata basi mtachinja **Jadhia** katika kondoo. Na **Musinna** katika wanyama ndiyo **Thaniya**”.* (Muslim).

b). **Ukamilifu wake:**

Hafai kutolewa *udhhiya* ila mnyama aliyesalimika na kila dosari na upungufu katika umbo lake, hafai mwenye chongo, wala mbovu wa miguu, wala aliyevunjika pembe katika mwanzo wake, (isiyo ncha yake), wala aliyekatwa sikio katika mwanzo wake, wala mgonjwa, wala mnyama aliyekonda – asiye na nyama. Na ushahidi wa yote hayo ni kauli yake Mtume ﷺ:

*“Wanyama wa aina nne hawafai kutolewa *udhhiya* nao ni: mwenye chongo ya wazi, mwenye ugonjwa ulio wazi, mbovu wa miguu na ambaye hana nyama.”* (Abu Dawuud na Imam Ahmad).

c). **Mnyama Aliye Bora Kuliko Wengine:**

Bora katika *udhhiya* ni kuchinja kondoo mwenye mapembe, dume, mwenye rangi nyeupe iliyochanganyika na nyeusi pembeni mwa macho yake na miguuni mwake. Kwani hizi ndizo sifa alizozipendelea Mtume ﷺ na ndiyo wanyama aliowachinja. Bi Aisha amesema:

*“Hakika Mtume ﷺ lichinja *udhhiya*, kondoo dume mwenye mapembe aliyekuwa na rangi nyeusi mguuni na sehemu zake za machoni.”* (At-Tirmidhi).

d). Wakati wa Kuchinja:

Wakati wa kuchinja *udhhiya* ni siku ya Iddi, asubuhi baada ya Swala yaani Swala ya Iddi, na haifai kuchinja kabla yake, kutokana na kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kuchinja kabla ya swala atakuwa amechinja kwa mahitaji yake binafsi, na atakayechinja baada ya Swala itakuwa ametimiza ibada yake na amepata sunna ya Waislam.” (Al-Bukhari).

Ama (kuchinja) baada ya siku ya Iddi inajuzu kuakhirisha mpaka siku ya pili, na ya tatu, baada ya Iddi kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume ﷺ:

“Siku zote tatu za tashriqi ni siku za kuchinja.” (Imam Ahmad).

e). Mambo yaliyo Sunna wakati wa kuchinja:

Ni sunna kumuelekeza mnyama kibla na kusema:

“Wajjahtu Wajhiya Lilladhi Fatwara Samawaati wal-Ardha Haniifan (Musliman) wama Ana Minal Mushrikina, Inna Swalati, Wanusukii, Wamahyaya, Wamamati Lillahi Rabil ‘Alamiina, Laa Sharika lahu Wabidhalika Umirtu wa-ana Awwalul Muslimiin.”

“Hakika Mimi Nauelekeza Uso Wangu Kwa Muumba Wa Mbingu Na Ardhi Hali Ya Kuwa Ni Mwenye Kujitakasa, Nami Si Miongoni Mwa Washirikina. Kwa Hakika Swala Zangu Na Ibada Zangu Na Yote Ninayofanya Katika Uhai Wangu Na Nitakayoacha Baada Ya Kufa Kwangu Yote Nayafanya Kwa Ajili Ya Allah, Mola Wa Wote, Hana Mshirika Wake Na Hayo Nimeamrisha Nami Ni Wa Kwanza Kuwa Muislamu.”

Na atakapoanza kuchinja atasema:

“Ninachinja kwa jina la Allah na Allah ni Mkubwa, Allahumma mnyama huyu ametoka kwako na ni wako.”

f). Kusihi uwakala katika kuchinja:

Inasuniwa mtu kuchinja *udhhiya* mwenyewe na ikiwa atamuweka mtu mwingine wa kumchinjia inajuzu na hilo ni jambo linalokubaliwa na wanazuoni.

g). Ugawaji Uliopendekezwa:

Inasuniwa kugawanywa udhhiya katika mafungu matatu:

- (a) Theluthi ya kwanza watakula watu wa nyumbani kwako.
- (b) Theluthi ya pili itatolewa sadaka (Kwa mafakiri na masikini).
- (c) Theluthi ya tatu itatolewa zawadi kwa marafiki, jamaa na ndugu.

Hayo ni kwa kauli yake ﷺ:

“Kuleni nyama ya udhhiya na wekeni akiba na toeni sadaka”.
(Abu Dawuud na An-Nasai).

Na inajuzu kuitoa sadaka yote, kama ambavyo inajuzu kutoitoa zawadi kabisa.

h). Malipo ya Mchinjaji Kutoka Kwingine:

Mchinjaji wa *udhhiya* hapewi ujira (wa kazi aliyoifanya) ya kuchinja. Kutoka kwenye *Udhhiya*. Kwa kauli ya ‘Ali bin Abu Twalib:

“Aliniamuru Mtume ﷺ nisimamie kuchinja ngamia wake wa udhhiya na kuwa nitoe sadaka nyama yake, ngozi yake, mifupa yake na nisimpe chochote mchinjaji kinachotokana na ngamia huyo, na akasema: “Sisi tutampa kutoka kwetu.” (Muslim na Abu Dawuud, Ibn Majah na Imam Ahmad).

i). Je, Anatosheleza Mbuzi Mmoja Kuwa *Udh-hiya* Kwa Watu wa familia nzima? (Watu wa nyumba moja)

Anatosheleza mbuzi mmoja *udhhiya* kwa familia nzima hata kama ni watu wengi kwa kauli ya Abu Ayubu (Amesema):

“Ilikuwa wakati wa Mtume ﷺ mtu anachinja udhhiya mbuzi mmoja kwa ajili yake na watu wote wa nyumbani kwake.” (Al-Bukhari na Muslim).

j). Mambo Anayojiepusha Nayo Alieazimia Kuchinja Udhiya:

Ni karaha mno kwa mwenye nia ya kuchinja *udhiya* kupunguza chochote katika nywele zake au kucha zake, hasa baada ya kuandama mfungo tatu (*Dhulhija*) mpaka baada ya kuchinja. Kwa kauli ya Mtum ﷺ:

“Mtakapouona mwezi wa Dhulhija, na akataka mmoja wenu kuchinja udh-hiya, basi ajizuwie kukata nywele zake na kucha zake mpaka achinje.” (Muslim).

k). Uchinjaji wa Mtume ﷺ Kwa Ajili ya Umati Wake Wote:

Atakayeshindwa kuchinja *udhiya* miongoni mwa Waislamu, atapata malipo (thawabu) kutoka kwa waliochinja, na hiyo ni kwamba Mtume ﷺ alipochinja mmoja wa kondoo wawili alisema:

“Ewe Mola, kondoo huyo nimemchinja kwa ajili yangu, na kwa ajili ya wale wote ambao hawakuchinja katika umati wangu.” (al Hakim).

Somo la Pili

‘Aqiqah

1. Maana ya ‘Aqiqah: ‘Aqiqah ni mbuzi anayechinjwa kwa ajili ya mtoto aliyefikisha umri wa siku saba tokea kuzaliwa kwake.

2. Hukumu ya ‘Aqiqah: ‘Aqiqah ni sunna iliyotiliwa mkazo na kuisisitizwa kwa wazazi wa mtoto walio na uwezo kwa (ushahidi) wa kauli ya Mtume ﷺ:

“Kila mtoto amefungika na aqiqah yake, itachinjwa kwa ajili yake siku yake ya saba na atapewa jina, na atanyolewa kichwa chake.” (Imam Ahmad na An-Nasai).

3. Hekima ya ‘Aqiqah: Miongoni mwa hekima katika ‘Aqiqah ni :

- (1) Kumshukuru Allah kwa neema ya kupata mtoto,
- (2) Wasila (njia) ya kumuomba Allah (s.w) amuhifadhi mtoto na kumchungu na majanga ya kuvunjika mifupa na mengineyo.

4. Hukumu Zake:

a) Kusalimika kwake na umri wake:

Mnyama anayefaa kuchinja ‘Aqiqah ni yule aliyekamilika asiye na kasoro yoyote na umri unaofaa ni kama anayefaa kuchinja katika *udhhiya* kwa kuzingatia kusalimika kwake na mapungufu na umri wake. Na mnyama asiyejaa kuchinja katika *udhhiya* pia hafai kuchinja katika ‘Aqiqah.

b) Kuliwa na kutolewa kwake sadaka:

Ni sunna kugawiwa (nyama ya ‘Aqiqah) kama inavyogawiwa nyama ya *udhhiya*, baadhi (ya nyama) watakula watu wa nyumbani na nyingine sadaka na nyingine itatolewa zawadi.

c) Mambo ya Sunna Kufanywa Siku ya ‘Aqiqah:

Ni sunna kwa ‘Aqiqah ya mtoto wa kiume kuchinjiwa mbuzi wawili

“kwani Mtume alichinja mbuzi wawili alipozaliwa Hassan.” (At-Tirmidhi).

Pia ni sunna kwa mtoto aliyezaliwa kupewa jina siku ya saba na achaguliwe jina ambalo ni zuri, na kichwa chake kinyolewe na nywele zake zilinganishwe na uzito wa dhahabu au fedha, au kinachochukuwa sifa ya vitu hivyo viwili katika pesa, na kitolewe sadaka, kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume ﷺ:

“Kila mtu amefungamanishwa na aqiqa yake, huchinjwa kwa ajili yake siku ya saba na hupewa jina na hunyolewa kichwa chake.” (Abu Dawuud).

d) Kuadhiniwa na kukimu katika masikio ya mtoto:

Wamesema Ulamaa kuwa ni sunna anapozaliwa mtoto itolewe adhana katika sikio lake la kulia na akimiwe katika sikio lake la kushoto, kwa nia ya kumuomba Mwenyeezi Mungu amuhifadhi na subiani ambaye ni miongoni mwa majini. Kwa ushahidi wa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mwenye kupata mtoto akaadhiniwa katika sikio lake la kulia na akakimiwa katika sikio lake la kushoto hatapatwa na madhara ya subiani”. (Ibn Sunniy na Imam Nawawi katika al adhkaar).

e) Kama siku ya saba bila ya kuchinja:

Ni sahihi kuwa atachinjiwa siku ya kumi na nne, au siku ya ishirini na moja. Na iwapo mtoto aliyezaliwa atafariki kabla ya siku ya saba hatachinjiwa *‘Aqiqa*.



Mlango wa Tano
Katika Muamalaat



Katika ‘Jihadi’

Mada ya Kwanza

Hukumu ya Jihadi, aina Zake na hekima iliyomo Ndani Yake.

Hukumu ya Jihadi:

Hukumu maalum ya *jihadi* ambayo ni kupambana na makafiri na wanaopiga vita Uislamu nayo ni *faradhi kifaya*, yaani si lazima kwa watu wote kwa muda mmoja, watakapoisimamia baadhi yao itatosha kwa wengine waliobaki. Haya ni kwa ushahidi wa *Qur-aan* Allah amesema:

﴿ وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنْفِرُوا كَافَّةً فَلَوْلَا نَفَرَ مِنْ كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴾

“Wala haiwafalii Waumini kutoka wote. Lakini kwa nini hawatoki baadhi katika kila kundi miongoni mwao, wakajifunze vyema Dini, na kisha waje kuwaonya wenzao watakapo warejea, ili wapate kujihadharisha?” (9:122).

Isipokuwa jihadi inakuwa *faradhi ‘aynin* (yaani nguzo ya lazima kwa kila mtu aliyechaguliwa na Imamu). Kwa mtu huyo ni faradhi kwake kushiriki bila kukosa kwa ushahidi wa Hadithi ya Mtume ﷺ

“Na mtakapotakiwa kutoka kwenda kwenye jihadi basi tokeni.”
(Wamepokea Bukhari, Muslim, Ahmad na Ibn Majah).

Pia adui atakapovamia mji wa Waislamu ni wajibu kwa watu wote wa mji ule wanaume na wanawake kupigana jihadi kwa ajili ya kujitetea.

2) Aina za Jihadi:

a) Jihadi dhidi ya makafiri

Jihadi dhidi ya makafiri na wapiganaji wengine wasiokuwa makafiri. Jihadi hii hufanywa kwa kutumia mkono, mali, ulimi na moyo (maneno), haya ni kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume ﷺ

“Wapigeni Jihadi washirikina kwa mali zenu, nafsi zenu na ndimi zenu.” (Imepokewa na Abu Dawud, Ahmad na An-Nasai).

b) Jihadi dhidi ya mafasiki

Jihadi hii hufanywa kwa kutumia mkono na ulimi (maneno) na moyo. Kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume ﷺ

“Atakayeona maovu miongoni mwenu basi auondoe kwa mkono wake, na Kama hakuweza basi kwa ulimi wake na kama hakuweza basi kwa moyo wake, (yaani ayachukie) nao (kuchukia) ni udhaifu zaidi wa Imani.” (Muslim).

c) Jihadi’ Dhidi ya Shetani:

Jihadi hii hufanywa kwa kuondoa yote yanayosababishwa na shetani katika mambo yenye utata (*shubha*) (yasiyokuwa wazi) na kuyaacha yote anayowapambia watu katika matamano ya nafsi. Kwa ushahidi wa maneno ya Allah (s.w.)

“Na asikupotezeni mkakosa kumuamini Mwenyezi Mungu mpotezaji (yaani shetani)”

Na kauli Yake Mwenyezi Mungu:

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا

“... Hakika Shet’ani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui....” (35:5-6).

d) Jihadi' Dhidi ya Nafsi:

Jihadi hii hufanywa kwa kuilazimisha nafsi kupenda kujifunza mambo ya dini, na kuyatumia na kufundisha (wengine) na kuiondoa katika matamania na kuinyoosha udhaifu wake. Jihadi ya nafsi ni miongoni mwa jihadi kubwa, ndiyo maana ikaitwa jihadi kubwa (*Jihadul-Akbar*)

3) Hekima ya Jihadi'.

Hekima za jihadi kwa aina zake zote ni kuabudiwa Mwenyezi Mungu peke yake, pamoja na yanayoambatana na hilo kama kuondoa uadui, maovu na kuhifadhi (kuilinda) nafsi na mali. Pia kuchunga haki na kuhifadhi uadilifu na kueneza kheri na fadhila, Allah (s.w.) anasema:

وَقَالَتْ أُولَئِكَمُ لِأَخْرَجَهُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ فَذُوقُوا

الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٣٩﴾

“Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayo yatenda.” (8:39).



Mada ya Pili

Fadhila ya Jihadi

Katika kueleza fadhila ya *jihadi*, na kufa shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu, zimepokuja Aya na Hadithi nyingi sahihi zinazoifanya *jihadi* iwe ni kiburudisho kikubwa na ni ibada bora zaidi. Miongoni mwa Aya zilizoshuka katika kuelezea ubora wa *jihadi* Mwenyezi Mungu Amesema:

✽ إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنْ لَّهُمُ
الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدًّا عَلَيْهِ حَقًّا
فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ
فَأَسْتَبْشِرُوا بَبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١١﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanauwa na wanauwawa. Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur’ani. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyo fanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.” (9:111).

Katika aya nyingine anasema,

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الَّذِينَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِهِ صَفًّا كَانَهُمْ بَيْنَ
مَرَّضُونَ ﴿٤﴾

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao pigana katika Njia yake kwa safu kama jengo lililokamatana.” (61:4)

Katika aya nyingine anasema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا هَلْ أَذُلُّكُمْ عَلَىٰ تَجْرَةِ تُجَيِّكُمْ مِّنْ عَذَابِ ٱلْإِيمِ ﴿١٠﴾
 تُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِ وُتُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ
 ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١١﴾ يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ
 جَنَّاتٍ تَجْرَىٰ مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَارُ وَمَسْكِنٍ طَيِّبَةٍ فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ ذَٰلِكَ
 ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ ﴿١٢﴾

“Enyi mlio amini! Nikuonyesheni biashara itakayo kuokoeni na adhabu iliyo chungu? Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na piganeni Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yenu na nafsi zenu. Haya ni bora kwenu, ikiwa nyinyi mnajua. Atakusameheni dhambi zenu, na atakutieni katika Mabustani yapitiwayo na mito kati yake, na maskani nzuri nzuri katika Bustani za milele. Huko ndio kufuzu kukubwa.” (61:10 – 12).

Kisha Allah anatumfahamisha ubora wa wanaopigana jihadi na wanaokufa mashahidi:

وَلَا تَحْسَبَنَّ ٱلَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ أَمْوَاتًا ۚ بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرَزَقُونَ ﴿١٣﴾ فَرِحِينَ بِمَا ءَاتَاهُمُ ٱللَّهُ مِن فَضْلِهِ وَاَسْتَبْشِرُونَ بِٱلَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِم مِّنْ خَلْفِهِمْ ۖ أَلَّا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٤﴾

“Wala kabisa usiwadhania walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahi, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi. Wanafurahia aliyo wapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila yake, na wanawashangilia wale

ambao bado hawajajiunga nao, walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.” (3:169 – 170).

Na kauli ya Mtume ﷺ alipoulizwa ni mtu gani bora kuliko wengine? Alisema:

“Muumini anayepigana jihadi kwa nafsi yake na mali yake katika njia ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.), kisha muumini anayeishi katika mtaa miongoni mwa mitaa anamuabudu Mwenyezi Mungu na hana mabaya anayowafanyia watu.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Mfano wa mtu mwenye kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu (Na Allah peke Yake Ndiye Anayemfahamu Mujahidi wa kweli) ni kama mfano wa Mtu anayefunga mchana na kusimama kuswali usiku. Na Mwenyezi Mungu ni wakala wa Mujahidi katika njia yake, kama atamfisha (yaani akifariki) atamuingiza peponi au amrejeshe salama pamoja na malipo na ngawira (ghanima).” (Imepokewa na Bukhari, Muslim na An-Nasai).

Na kauli yake Mtume ﷺ alipoulizwa na mtu kuwa:

“Nijulishe amali inayolingana na jihadi, Mtume ﷺ akasema: “Sioni amali hiyo, kisha akasema, je, unaweza akitoka Mujahid ukaingia msikitini mwako ukasimama wala hupumziki, na ukafunga na usifuturu? Akasema ni nani anayeweza hilo?” (Bukhari na An-Nasai).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Naapa kwa ambaye (nafsi) yangu iko mikononi mwake, haumizwi (hajeruhiwi) mtu katika njia ya Mwenyezi Mungu (Naye Ndiye Mjuzi zaidi wa wale wanaomia katika njia yake) ila mtu huyo atakuja siku ya Qiyama hali ya kuwa rangi yake ni rangi ya damu na harufu hii harufu ya misk.” (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ anasema:

“Mwenye kufa na hakupigana jihad na hakuiambia nafsi yake kuhusu jihadi basi mtu huyo amekufa na fungu la unafiki”.
(Imepokewa na Abu Dawud, An-Nasai na Imamu Ahmad).

Na kauli yake Mtume ﷺ amesema:

“Naapa kwa ambaye nafsi yangu (roho) iko mkononi mwake, kama siyo watu miongoni mwa waumini ambao nafsi zao hazipendi kwenda kinyume na mafunzo yangu na ambao (wakati wa kwenda kwenye jihadi) sipati cha kuwabebea wao, kama siyo watu hao ningeshiriki katika vita vyote (nilivyotuma) na ni naapa kwa ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, natamani Kuuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu, kisha nikawa hai, kisha nikauawa kisha nikawa hai kisha nikauawa”. (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ amesema:

“Hakuna unyayo wa mja uliopata vumbi katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha ukaingia motoni.” (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ amesema:

“Hakuna yoyote atakayeingia peponi kisha akatamani arudi Duniani...ila shahidi (wa jihadi) atatamani arudi Duniani ili auawe, mara kumi (mara kadhaa) kwa sababu ya yale anayoyaona ya utukufu.” (Bukhari).



Mada ya Tatu

Ribati (Ulinzi)

Hukumu yake na ubora wake

1) Maana ya *Ribati*:

Ribati ni jeshi la Kiislamu linaloweka kambi likiwa na silaha zake na zana zote za kivita, mpakani mwa adui au mahala popote pa hatari ambapo kuna uwezekano kwa adui kupita hapo na kuingia hapo kuwashambulia Waislamu na miji yao kutokea sehemu hiyo.

2) Hukumu ya *Ribati*:

Ribati hukumu yake ni wajibu “*Faradhi Kifaya*’, yaani ni wajibu wa kutoshelezana kama vile jihadi, baadhi ya waumini wakiisimamia hupomoka kwa waliobakia, na Mwenyezi Mungu Ameamrisha kutekelezwa *Ribati* katika *Qur-aan* kwa kusema:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَصْبِرُوا وَصَابِرُوا وَرَابِطُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾

“*Enyi mlio amini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa.*” (3:200)

3) Fadhila yake:

Ribati ni miongoni mwa amali kubwa na ibada adhimu za kumuweka mja karibu na Mola wake. Mtume ﷺ amesema kuhusu *Ribati* kuwa:

“*Kulinda siku moja katika njia ya Mwenyezi Mungu ni bora kuliko Dunia na vilivyo juu yake.*” (Wamepokea Bukhari, Tirmidhi na Imam Ahmad).

Mtume ﷺ amesema tena:

“Kila maiti amali yake huhitimishwa juu ya amali yake, ila aliyelinda amali yake inakuwa mpaka Siku ya Kiama, atasalimika na fitina za kaburini.” (Abu Dawud, Tirmidhi).

Fitina za kaburi maana yake hapa ni Malaika Munkari na Nakiri. Na amesema tena:

“Kulinda usiku mmoja katika njia ya Mwenyezi Mungu ni Kheri kuliko usiku elfu zinazosimamiwa (Usiku kwa Ibada) na kufungwa mchana wake.” (Imepokewa na Tabarani, Ibn Majah na Hakim). Na

“Umeharamishwa moto juu ya jicho lililokesha usiku kulinda katika Njia ya Mwenyezi Mungu.” (Imam Ahmad na Darimiy).

Kauli yake ﷺ kuwa,

“Atakaekesha nyuma ya Waislamu akiwa amejitolea, jicho lake halitoona moto, isipokuwa kwa kufungua kiapo.” (Imam Ahmad).

Mtume ﷺ alimwambia Anas bin Abi Mirthad baada ya kumuamrisha kulinda kikosi cha jeshi usiku mmoja, ilipofika asubuhi Mtume ﷺ alimjia akamwambia:

“Je ulishuka usiku? (Ulipumzika kulinda?)” Anas alisema hapana isipokuwa kwa ajili ya swala au kwenda haja, Mtume ﷺ akasema: Umefanya kazi ya wajibu ya kukuingiza peponi, hata kama hutafanya kazi nyingine baada yake.” (Abu Dawud na Hakim).




Mada ya Nne

Wajibu wa Kujiandaa kwa Ajili ya Jihadi

Kujiandaa kwa ajili ya *Jihadi* ni kutayarisha mazingira na kuandaa nyenzo na zana za kivita kwa aina zake zote. Kazi hii ni wajibu sawa na wajibu wa *jihadi* yenyewe. Allah Anasema:

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ
اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَآخَرِينَ مِنْ دُونِهِمْ لَا تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ

“Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, na wengineo ambao hamwajui, lakini Mwenyezi Mungu anawajua...” (8:60)

Amesema ‘Uqba bin Aamin 

“Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akiwa juu ya mimbari akisema: “Basi waandalieni nguvu za silaha mnazoweza; fahamuni hakika maana ya nguvu ni kurusha mishale, fahamu hakika nguvu ni kurusha mishale, fahamuni hakika nguvu ni kurusha mishale.” (Abu Dawud).

Amesema Mtume 

“Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu atawaingiza peponi watu wa aina tatu kwa sababu ya mshale mmoja: aliyeutengeneza kwa nia ya kutaka kheri na malipo kwa Mwenyezi Mungu na mwenye kuutupa kwa mafunzo ya shabaha na mwenye kuutumia katika jihadi; na jifunzeni kulenga shabaha na kupanda vipando (farasi, ngamia, vifaru, ndege za kivita n.k.) na kujifunza shabaha kunapendeza kwangu zaidi kuliko kupanda.”

Katika hadithi nyingine,

“Anasa haiwi isipokuwa katika matatu nayo ni (1) Mtu kumfunza farasi wake. (2) Mtu kuchezeana na mkewe . (3) Na kutupa upinde (mshale)” (An-Nasai, Ahmad, na Hakim).

Kwa kujenga hoja kutokana na Aya na hadithi hizi, ni wajibu kwa Waislamu wa nchi moja au mbali mbali watayarisha silaha na zana zingine za kivita, na wawaandae watu wazijue elimu na fani za kivita na mapambano ili wawe na uwezo wa si tu kujibu mashambulizi ya adui bali pia kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa kutangaza neno la Allah na kueneza haki, amani na utulivu katika ardhi. Kama ilivyo wajibu pia kwa Waislamu kulifanya suala la mafunzo ya kijeshi kuwa la kulazimishana baina yao. Asibaki kijana mwenye umri wa miaka kumi na nane bila ya kulazimishwa kulitumikia jeshi kwa muda wa mwaka mmoja na nusu ili kwa muda huo aweze kuelewa vizuri fani mbali mbali za vita na mapambano na baada ya hapo lisajiliwe jina lake katika daftari la majina ya wanajeshi wote. Hapo tayari atakuwa amejiandaa wakati wowote atakapohitajika na kiongozi wa jihad atamwita kupitia kwenye daftari hilo na kutokana na uzuri wa nia yake anaweza kuhesabiwa kuwa yeye atakuwa tayari katika kipindi chote ambacho jina lake limo katika daftari la majina ya wanajeshi wote. Kama ambavyo ni wajibu kwa Waislamu kujenga viwanda vya kutengeneza zana za kivita zinazotengeneza aina zote za silaha zinazopatikana hapa Ulimwenguni. Hata kama kwa matayarisho hayo watalazimika kujinyima na kuacha matumizi yasiyokuwa ya lazima katika vyakula, mavazi vinywaji na makazi jambo ambalo linawafanya waweze kutekeleza wajibu wa jihadi na watekeleze nguvu yake kwa njia nyepesi na kwa ukamilifu. Na kama Waislamu hawatofanya hivyo watadhalilishwa na watakuwa walengwa wa maadui wa Uislamu na Waislamu na kisha watapata madhila makubwa hapa duniani; na baadaye akhera wataulizwa kwa nini walizembea kusimamisha majukumu hayo.



Mada ya Tano

Nguzo za Jihadi:

Jihadi inayokubalika kisheria, na ambayo hupatikana kwayo moja ya mazuri mawili:-Ama kuishi katika hali ya kuheshimiwa au kufariki dunia ukiwa shahidi, ina nguzo nne:

1. Nia njema, kwani kila amali inalipwa kutokana na nia, na nia katika *jihadi* ni kuwa na lengo la kutangaza neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu na si vinginevyo. Aliulizwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuhusu mtu anayepigana *jihadi* kwa ajili ya hamasa na kwa ajili ya ria (kujionesha), je mtu huyo yuko katika njia ya Mwenyezi Mungu? Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

“Yeyote mwenye kupigana ili neno la Allah liwe juu, huyo atakuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu.” (Bukhari, Muslim)

2. Jihadi hiyo iwe chini ya kiongozi (Imamu) Muislamu, na chini ya bendera yake na kwa idhini yake. Kama isivyofaa kwa Waislamu hata kama idadi yao itakuwa ndogo kuishi bila kiongozi (Imamu) pia haifai kwao kupigana bila kiongozi, Mwenyezi Mungu Anasema:-

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ

“Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mt’iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi....”(4:59).

Kwa kujengea hoja juu ya aya hii, kwa hakika ni wajibu kwa kundi la aina yoyote miongoni mwa Waislamu linalotaka kupigana jihadi na kupigana vita katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu au linataka kujikomboa na kuwa huru, kutoka mikononi mwa makafiri, kundi hilo kabla ya lolote litoe ahadi ya Utii (bay’a) kwa mmoja miongoni mwao ambaye ametimiza masharti muhimu ya uongozi (Uimamu) ambayo ni pamoja na elimu, Uchamungu na afya. Baada ya kuwa na kiongozi, kundi lipange safu zake na likusanye mambo yake na lipigane jihadi kwa kutumia ndimi zake (maneno) na mali zake na mikono yake mpaka pale Mwenyezi Mungu atakapowapa ushindi.

3. Kufanya matayarisho na kutayarisha yote yanayohitajika katika *Jihadi* kama vile silaha, vipando na wanajeshi kwa kadri iwezekanavyo pamoja na kutoa michango (ya mali) kikamilifu kila mtu kwa uwezo wake wote. Na kujiweka tayari kwa ajili ya *Jihadi* kama Anavyosema Allah (s w):

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهَبُونَ بِهِ

“Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo...” (8:60).

4. Ruhusa ya wazazi wawili. Idhini ya wazazi (kwa ajili ya jihadi) ni kwa yule ambaye bado ana wazazi wawili au mmoja wao. Haya ni kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume ﷺ mtu mmoja alimuomba idhini aende katika jihadi akasema:

“Je, wazazi wako, bado wapo hai? Akasema ndiyo, Mtume ﷺ akasema: “Katika wao ifanye jihadi.” Isipokuwa adui anapovamia kijiji au mji au kiongozi anapomchagua mtu kushiriki katika jihadi hapo haisubiriwi idhini ya wazazi.”
(Bukhari)

5. Kumtii kiongozi (Yoyote atakayepigana huku akiwa amemuasi kiongozi na akafariki katika jihadi, basi atakuwa amekufa kifo cha kijahilia kwa kauli yake Mtume ﷺ amesema:

“Mtu atakayeona karaha kwa amiri wake basi na afanye subira juu yake (amvumilie) kwani hakuna mtu yeyote atakayeasi amri ya kiongozi kwa umbali wa shubiri moja na akafa katika hali hiyo atakuwa amekufa kifo cha kijahilia.” (Bukhari na Muslim).



Mada ya Sita

Mambo yanayolazimu wakati wa kuingia vitani

Hanabudi kila mwenye kupigana wakati wa mapigano ya vita atimize yafuatayo:

1.Kuazimia, kutorudi nyuma) na kupigana kufa na kupona katika vita, kwani Allah (s.w) ameharamisha kukimbia mbele ya adui wakati wa mapigano. Anasema:-

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيْتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا زَحْفًا فَلَا تُوَلُّوهُمُ الْآدْبَارَ ﴿١٥﴾

“Enyi Mlio amini! Mkikutana na walio kufuru vitani msiwageuzie mgongo.”(8:15)

Hukumu hii inatumika iwapo idadi ya maadui itakuwa si zaidi ya mara mbili ya Waislamu. Iwapo itazidi ikawa Muislamu mmoja anapigana na makafiri watatu, au zaidi, wakati huo kukimbia siyo haramu (ni ruhusa).

Pia mwenye kukimbia kwa ujanja wa kuwachanganya maadui ili wajisahau, na aweze kuwashambulia vizuri, au akimbie ili ajiunge na kundi la wenzake baada ya kubaki peke yake, huyu haitwi kuwa amekimbia wala hana makosa, kwa ushahidi wa Aya Allah Anasema:-

وَمَنْ يُؤَلِّهِمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ أَوْ مُتَحَرِّزًا إِلَىٰ فِتْنَةٍ فَقَدْ بَاءَ بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٦﴾

“Na atakaye wageuzia mgongo wake siku hiyo - isipo kuwa kwa mbinu za vita au kuungana na kikosi - basi atakuwa amestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na pahala pake ni Jahannamu, na huo ni mwisho muovu..” (8:16).

2. Kumtaja Mwenyezi Mungu kimoyomoyo, na kwa ulimi (maneno) kwa nia ya kuomba msaada wa nguvu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa kutaja ahadi zake za kuwanusuru waja Wake, na kuwaangamiza makafiri, na utawala wao, na nusra yake kwa wale wanaotawalia mambo ya Waislamu; kwa hayo moyo unazidi ujasiri na kuendelea kuthibiti na kutorudi nyuma.”

3. Kuntii Mwenyezi Mungu na Mtume wake ﷺ kwa kutokwenda kinyume na amri zao na kutotenda makatazo yao.

4. Kuacha ugomvi na khitilafu ili waingie vitani wakiwa katika safu moja isiyo na pengo wala upenyu wa adui, nyoyo zimeshikamana na miili imefungana kama jengo imara pande zake zimeungana.

5. Subira, na usubirifu, na kupigana kufa na kupona katika mapigano mpaka adui akimbie na safu zake zipanguke. Mwenyezi Mungu Anasema:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اِذَا لَقِيْتُمْ فِئَةً فَاَنْبِئُوْا وَاذْكُرُوْا اللّٰهَ كَثِيْرًا لَّعَلَّكُمْ
تُفْلِحُوْنَ ﴿٤٥﴾ وَاَطِيعُوْا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهُ وَلَا تَنَزَعُوْا فِتْفَسَلُوْا وَتَذَهَبَ رِيْحُكُمْ
وَاَصْبِرُوْا اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿٤٦﴾

“Enyi mlio amini! Mkikutana na jeshi, basi kueni imara, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu sana ili mpate kufanikiwa. Na mt’iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri..” (8:45-46).



Mada ya Saba

Adabu ya Jihadi

Jihadi ina adabu ambazo inabidi zichungwe kwani hizo ni nyenzo za nusura katika, nazo ni:

1) Kutotowa siri za jeshi na mbinu zake za kivita. Hakika ilikuwa Mtume ﷺ alipotaka kwenda kwenye vita huficha kwa kutaja vita nyingine ili adui akiona maandalizi ajue kuwa anaenda huko kulikotajwa.

2) Kutumia ishara, na alama kati ya wanajeshi. Ishara hizo zitawafanya watambuane watapochanganyika na adui, au watapokuwa wamekaribia eneo la adui. Mtume ﷺ anasema,

“Mkilala katika mapambano na adui isomeni (Hamim la Yun Swaruun)”

na neno la siri lililotumika katika moja ya vita alizoziongoza Abubakari ni Amit Amit.” (Tirmidhi).

3) Kuwa kimya wakati wa mapigano ya vita kwani kusema sema na kupiga kelele husababisha kushindwa na kugawanyika nguvu, na mawazo. Kwa hadithi iliyopokelewa na Abu Dawud kuwa maswahaba wa Mtume ﷺ walikuwa wakichukia kutoa sauti wakati wa mapigano.

4) Kuchagua sehemu nzuri zinazofaa kwa mapigano na kuwapanga wapiganaji na kuchagua muda mzuri wa kuanza mashambulizi kwa adui. Kwani alikuwa Mtume ﷺ katika muongozo wake vitani akichagua mahala na wakati mzuri wa kuanza mapigano ya vita.

5) Kuwalingania (kuwapa *da'awa*) makafiri kabla ya kuwatangazia vita au kabla ya kuwashambulia, na kuwaita kwenye Uislamu, au kuacha mapignao, kwa kutoa kodi (*Jizya*), wakikataa hapo ndipo inabidi kupigana nao. Kwani Mtume ﷺ alikuwa alipomtuma amiri kuongoza kikosi cha jeshi kwenda kwenye mapambano humuusia uchamungu, na kuwatakia kheri wale walio pamoja naye katika Waislamu. Akasema Mtume ﷺ

“Utakapokutana na adui yeyote katika washirikina walinganie katika moja ya mambo matatu, watakalolikubali kati ya hayo basi wakubalie, na waache, wakikataa waambie wakubali kutoa jizya (kodi) kama watakubali” (Muslim).

6) Kuacha Kuiba, na kutopiga wanawake na watoto, vikongwe, watawa kama watakuwa hawakushiriki katika vita, ama kama watashiriki katika kupigana basi nao watapigwa, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume ﷺ Kwa Maamiri wake:

“Nendeni kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Na kwa mila ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na msiue wazee, wala watoto wadogo, wala wanawake, wala msivuke kiwago mkazidisha mauaji, na kusanyeni ngawira zenu, na fanyeni suluhu na fanyeni hisani, kwani Allah anawapenda wanaofanya hisani.” (Abu Dawud).

7. Kutomuua mtu aliyepewa himaya na Muislamu, na kusalimisha maisha yake. Kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume ﷺ, anasema,

“Basi msimuue aliyejisalimisha na kuomba himaya.” (Muslim)

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Hakika wanaowaua waliojisalimisha kwa kuomba himaya, siku ya qiyama kutasimamishwa bendera na wataambiwa: Hii ni khiyana ya fulani bin fulani.” (Bukhari na Muslim).

8. Kutomchoma adui kwa moto. Kwa ushahidi wa kauli ya Mtume ﷺ

“Mkimkuta fulani muueni lakini msimchome kwa moto kwani haadhibu adhabu ya kuchoma moto ila Mola aliyumba moto.” (Bukhari).

9. Kutowasulubu waliouawa, kwa hadithi ya Imran bin Haswain, “Mtume ﷺ

Minhajil Muslim

Alikuwa akitusisitiza kutoa sadaka, na akitukataza kuwatesa na kuwasulubu waliokufa.” (Abu Dawud)

Na Kauli ya Mtume ﷺ anasema:

“Wasamehevu wa maiti ni watu wenye Imani.” (Abu Dawud).

10) Kuomba dua ya nusra dhidi ya maadui, kwani Mtume ﷺ alikuwa akisema baada ya kutayarisha jeshi lilipokwenda vitani.

“Ewe Mola Uliyeteremsha kitabu, na mwenye kuyatembeza mawingu, na mwenye kutimua adui, watimue na utunusuru juu yao.” (Wamepokea Bukhari, Muslim na Abu Dawud).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Dua za namna mbili hazirudi patupu au mara chache kurudi patupu bila majibu, ya kwanza ni dua ya wakati wa adhana, na ya pili ni dua ya kuomba wakati wa vita na pande mbili zimeumana na kushambuliana.” (Abu Dawud).



Mada ya Nane

‘Aqdu-Ddhimma’

Mikataba ya dhima na hukumu zake

1) ‘Aqdu dhima

Maana yake ni kupewa amani (wasiokuwa Waislamu) waliokubali kuishi chini ya himaya ya dola ya Kiislamu na hivyo kutoa kodi (jizya) na wakakubali kujilazimisha kuchunga sheria za Kiislamu kwa kulinda mipaka yake kwa kuacha kuua, kuiba na kulinda heshima na vyeo vya watu.

2) Msimamizi wa mkataba wa ‘Aqd Dhima.

Msimamizi Mkuu wa mkataba huu ni Imamu, kiongozi wa Waislamu au Naibu wake katika maamiri wa kijeshi peke yake. Ama wasiokuwa hao hawana ruhusa, wala haki ya kusimamia mkataba huo. Hii ni tofuati na hukumu ya kumpa hifadhi kafiri au kumpa amani kafiri mwenye wasiwasi na usalama wake. Haya yanafanywa na Muislamu yeyote, mume au mke, kwani Ummu-Hani binti Abi Taalib alimpamtu mushrikina siku ya Fathi ya Makka akamwendea Mtume ﷺ akamwambia kisa alichokifanya, akasema Mtume ﷺ

“Tumekubali kumpa hifadhi huyo uliyemuhifadhi na tumempa huyo uliyempa amani ewe Ummu Hanii.”

3) Kuwatenganisha watu wa Dhima na waislamu:

Inalazimika kuweka mambo yanayowatofautisha watu wa dhima na Waislamu katika mavazi, na mfano wa mavazi, ili wafahamike kwa alama hiyo. Pia haifai kuwazika katika makaburi ya Waislamu. Pia haifai kuwasimamia kwa heshima wala kuwatolea salamu wala kukaa safu ya mbele katika vikao. Kwa kauli ya Mtume ﷺ amesema:

“Msiwaanze Mayahudi na Manasara kuwasalimia, mkikutana na mmoja wao njiani mbaneni asipate nafasi pana ya kupita”
(Muslim)

4) Mambo Yanayokatazwa kwa Ahlu Dhima

Ahlu Dhima hawaruhusiwi kufanya yafuatayo:

a) Kujenga makanisa, kuuza na kujenga upya majengo yaliyobomoka katika makanisa, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Halijengwi kanisa katika nchi ya Kiislamu, wala hakijengwi upya, kilicho bomoka katika makanisa hayo.” (al Mughni ya Ibnu Qudaman. Naylul-Awtaar ya Shawkaani).

b) Haruhusiwi kurefusha nyumba yake zaidi ya nyumba za Waislamu. Kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Uislamu uko juu na hakuna kinachokuwa juu yake.” (Baihaq).

c) Kujidhihirisha (Kujiweka wazi) mbele ya Waislamu kwa ulevi, na kula nguruwe, au kula na kunywa katika mchana wa Ramadhani. Bali ni juu yao wafanye kwa uficho yale yote ambayo ni haramu kwa Waislamu ili kuepusha isiwe fitina kwa Waislamu.

5) Yanayovunja mkataba wa Ahlu Dhima

Mkataba wa *Ahlu Dhima* unavunjika kwa yafuatayo:

a) Kukataa kutoa kodi (Jizya). (b) Kuvunja sheria na hukumu za Kiislamu ambazo ni kaitika masharti ya kufikiwa mkataba. (c) Kuwafanyia uadui Waislamu kwa kuua au ujambazi, au kufanya ujasusi au kutoa nafasi kwa jasusi au adui au kuzini na mwanamke wa Kiislamu. (d) Kumtaja Mwenyezi Mungu na Mtume wake ﷺ au kitabu chake kwa uovu.

6) Haki wanazotakiwa kufanyiwa Ahlu Dhima:

Haki za *Ahlu Dhima* juu ya Waislamu ni kuhifadhi roho zao, na mali zao, heshima zao, kuacha kuwaudhi kwa muda wote watakaojilazimisha kuchunga mkataba na kutoutengua. Kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mtu Mwenye kumfanyia maudhi Dhimmi mimi nitakuwa khasimu wake (mgomvi wake) siku ya Qiyama.” (Ibn Masud).

Kama watatengua mkataba na wakaenda kinyume kwa kufanya mambo yanayovunja mkataba, basi itakuwa halali damu yao, na mali zao, ila wanawake wao na watoto wao. Kwani haadhibiwi mtu kwa dhambi iliyofanywa na mwingine. Huu ndio msimamo wa Uislamu.



Mada ya Tisa

Mkataba wa *Hudnah*’ na *Suluhu*’

1) Mkataba wa *‘Hudnah*’

Ni mkataba unaofikiwa kati ya Waislamu na makafiri wa kusimamisha vita baina yao. Mkataba huu unafaa kufanyika kama utakuwa na maslahi ya wazi kwa Waislamu. Mtume ﷺ alifanya mikataba mingi ya *‘Hudnah*’ katika vita zake na makafiri, miongoni mwa mikataba hiyo ni mkataba wake na Mayahudi wa Madina, baada ya kuhama Madina. Mkataba huo uliendelea mpaka Mayahudi walipouvunja na Mtume ﷺ akalazimika kuwapiga vita na kuwafukuza kutoka Madina.

2) *Mu’ahadah* (Mkataba wa kutoa ahadi)

Mkataba wa *Mu’ahadah* ni mkataba unaofanyika kati ya pande mbili kwa kutaka kila upande kuacha kufanyia uadui upande wa pili, na kujenga ujirani mwema kati ya Waislamu na adui zao iwapo kwa mkataba huo kutapatikana maslahi kwa upande wa Waislamu. Mtume ﷺ Alifanya mikataba mingi ya aina ya *‘Mu’ahadah*’ na alikuwa akisema:

“Tutatekeleza mkataba wao na tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe ushindi juu yao.” (Muslim)

Mwenyezi Mungu Amesema:

إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ فَمَا اسْتَقْنُمُوا لَكُمْ فَاسْتَقِيمُوا
هَمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧﴾

“...ila wale mlio ahidiana nao kwenye Msikiti Mtakatifu? Basi maadamu wanakwenda nanyi sawa, nanyi pia nendeni sawa nao. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wachamngu.” (9:7)

Mtume ﷺ aliharamisha kumuua mwenye mkataba wa aina hii (*muahidi*) pale aliposema:

“Mwenye kumuua Mu’ahid aliyefanya mkataba wa ahadi (Mu’ahada) hatonusa harufu ya pepo.” (Bukhari)

Na Amesema Mtume ﷺ

“Mimi sitengui ahadi, wala simfungi mjumbe aliyetumwa.” (Abu Dawud, An-Nasai)

3) Mkataba wa ‘Suluhu’:

Inafaa kwa Waislamu kufanya suluhu na yeyote anayetaka suluhu katika adui zao iwapo wataomba kufanya hivyo na ikiwa suluhu hiyo ina faida ambazo hazipatikani ila kwa njia ya suluhu. Mtume ﷺ alifanya suluhu na watu wa Makkah katika mkataba wa suluhu ya Hdaybiyyah. Kama alivyofanya suluhu na watu na Najrani kwa Masharti ya wao kutoa mali. Na alifanya suluhu na watu wa Bahrain kuwa watatoa kodi (*jiyya*) iliyoainishwa. Na kwa Ukaidiru alifanya suluhu na alihifadhi damu yake kwa ahadi kuwa atatoa *jiyya* (kodi).



Mada ya Kumi

Kugawa *Ghanimah*, *Fay-u*, *Kharraji*, *Jizya* na *Nafli*

1) Ugawaji wa *Ghanimah* (Ngawira):

Ghanimah ni mali inayotekwa na Waislamu kutoka kwa makafiri katika mapigano ya vita ya *jihadi* baada ya makafiri kukimbia mapigano.

Hukumu ya *Ghanima*, (ngawira) itagawiwa mafungu matano. Fungu moja litachukuliwa na kiongozi mkuu, (Imamu) yeye ataangalia namna ya matumizi yake kwa kuchunga maslahi ya Waislamu. Mafungu manne yaliyobakia yatagawiwa kwa wanajeshi walioshiriki kwenda vitani bila kuangalia kuwa walipigana au hawakushiriki katika kupigana. Kwa ushahidi wa kauli ya Amirul Muuminina Umar رضي الله عنه.

“*Ghanimah* ni mali ya kila aliyeshiriki katika vita’ Waliopigana wakiwa wamepanda farasi, watapewa mafungu matatu na waliokuwa hawana vipando watapewa fungu moja Allah Anasema:

• وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ

وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَأَبِ السَّبِيلِ إِنْ كُنْتُمْ ءَامَنْتُمْ بِاللَّهِ وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَىٰ

عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ التَّقَىٰ أَتَقَى الْجَمْعَانَ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤١﴾

“NA JUENI ya kwamba ngawira mnayo ipata, basi khums (sehemu moja katika tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume ﷺ, na jamaa, na mayatima, na masikini, na wasafiri, ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyo yateremsha kwa mja wetu siku ya kipambanuo, siku yalipo kutana majeshi mawili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu..” (8:41).

Tanbihi:

Jeshi linashiriki katika kugawana ngawira zilizopatikana kwa njia ya jeshi dogo (sariya) liliotumika kwa dharura kisha likapata ushindi na likarudi na *Ghanima* yaani ngawira. Basi ngawira hizo hazitakuwa kwa wale tu aliotumwa bali ni kwa kikosi kizima.

4) Ugawaji wa *Fay-u*:

Fay-u ni mali zilizoachwa na makafiri na waliokimbia na kuziacha kabla ya mapigano kuanza.

Hukumu yake Imamu ataangalia namna ya kuigawa kwa kuchunga maslahi ya Waislamu wote na wale wenye matatizo maalumu, sawa sawa na anavyogawa moja ya tano ya *Ghanima*. Allah (s.w.) Anasema:

مَا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ
وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَىٰ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ

“Mali aliyo leta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa hivi vijiji ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na msafiri, ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu....”(59:7).

5) Ugawaji wa *Kharaj*

Kharaj ni mali (mapato) inayopatikana kutoka katika ardhi iliyotekwa na Waislamu toka kwa makafiri kwa kutumia (nguvu za kijeshi) Imamu ana hiari baada ya kuiteka ardhi hiyo ama aigawe kwa wapiganaji wake (jeshi), alifanye wakfu kwa Waislamu. Na yeyote atakayetumia ardhi hiyo awe Muislamu, au *dhimii*, atatoa kodi ya mapato (*Kharaj*) mapato hayo yataendelea kutolewa kila mwaka. Baada ya kukusanya mapato yote kwa mwaka, Imamu atayagawa na kuyatumia katika mambo atakayoona yana maslahi kwa Waislamu wote. Kama alivyofanya Umar رضي الله عنه katika maeneo aliyoyafungia katika ardhi ya Shamu, Iraqi na Misri.

Tanhibi:

Iwapo Imamu atafanya suluhu na makafiri wakakubali kutoa *Kharaj* kutoka katika ardhi yao kisha watu wa eneo lile wakasilimu basi kodi ile itakuwa ndiyo mwisho kwao baada ya wao kusilimu. Hii ni tofauti na ardhi iliyopatikana kwa nguvu yaani kwa vita na mapigano, badala ya suluhu hata kama watu wa ardhi hiyo watasilimu baadaye itaendelea kuwa chini ya sheria ya kulipiwa kodi ya mapato.

6) Ugawaji wa *Jizyah*:

Jizya: ni kodi ya mali inayotokana na *Ahlu Dhima* (yaani makafiri wanaoishi katika utawala wa Kiislamu) kodi yao inaitwa *Jizya*. (Ama kodi ya Waislamu inaitwa *zakah*). Kodi hii inatolewa kila mwisho wa mwaka na kiasi chake kwa wale ambao mji wao ulikombolewa kwa nguvu, yaani kwa mapigano ni Dinari nne za dhahabu, au Dirham arobaini za fedha. Zinakusanywa toka kwa watu wazima na si watoto na wanawake. Ama masikini asiyejiweza na asiyeweza kufanya kazi ama kwa ugonjwa, uzee na ulemavu hawa hawatoi hiyo *jizyah*. Ama waliofanya suluhu. *jizya* itachukuliwa kutoka kwao kulingana na mkataba wa suluhu, ama wakisilimu basi *Jizyah* kwao itafutika kabisa Hukumu ya *jizyah* ni kutumika katika kutatua na kutengeneza mambo yenye maslahi kwa jamii ya watu wote. Na asili ya *jizyah* inapatikana katika maneno ya Mwenyezi Mungu:

قَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ
وَرَسُولُهُ وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّى يُعْطُوا
الْجِزْيَةَ عَنْ يَدٍ وَهُمْ صَاغِرُونَ ﴿٩٩﴾

“Piganeni na wasio muamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, wala hawaharimishi alivyo harimisha Mwenyezi Mungu na Mtume, wala hawashiki Dini ya Haki, miongoni mwa walio pewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa khiari yao, hali wametii.” (9:29).

7) Ugawaji wa Nafali:

Nafali ni fungu analolitoa Imamu maalum kwa watu aliowatuma kufanya kazi muhimu ya kivita (kama kuwatuma kufanya ujasusi) atawapa ziada baada ya mgao wao wa ngawira (*Ghanima*) ambayo Imamu anaruhusiwa kuigawa kwa kuangalia maslahi ya Waislamu. Na inatakiwa *Nafali* hii isiwe zaidi ya robo ikiwa watu hao wametumwa kazi hiyo wakati wa kuingia katika ardhi ya adui na isiwe zaidi ya theluthi, ikiwa watatu wa baada ya kurudi kwao kutoka katika ardhi hiyo kwa ushahidi wa hadithi ya Habibi bin Maslama:

“Nilishuhudia mjumbe wa Mwenyezi Mungu akigawa robo ya nafali mwanzo, na theluthi wakati wa kurejea.” (Ahmad, Abu Dawud).



Mada ya Kumi na Moja

‘Mateka wa Kivita’

Ulamaa wa Kiislamu wametofautina katika hukumu ya mateka wa kivita baina ya Waislamu na makafiri. Je, hukumu yao ni kuuawa, au wafidiwe, au waachiwe bila masharti, au wafanywe watumwa? Sababu ya tofauti hiyo inatokana na Aya zinazoelezea mateka wa kivita hazikufafanua hukumu yao. Aya mojawapo ni ya nne ya Suratu Muhammad:

فَإِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَخْنَتُمْهُمْ فَشُدُّوا الْوَتَانَ
فَأَمَّا مَن بَعْدَ وَإِنَّمَا فِدَاءً حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا ۗ ذَٰلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ
لَآتَتْصَرَّ مِنْهُمْ وَلَٰكِن لِّيَبْتَلُوا بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ ۗ وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَن
يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٤٧﴾

“Basi mnapo wakuta walio kufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe. Ndio hivyo. Na lau angeli taka Mwenyezi Mungu angeli washinda mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu akutieni mitihani nyinyi kwa nyinyi. Na walio uliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu hatazipoteza a’ mali zao.” (47:4).

Aya hii tukufu inampa hiari Imamu kati ya kuwaacha huru mateka bila fidia, au waachiwe kwa kulipa fidia ya mali, au silaha, au kubadilishana mateka. Na kauli ya Allah (*Subhaanahu wa Taala*):

“Na piganeni na washirikina popote mtakapowakuta.”

Aya hii inatoa hukumu ya kuwapiga na kuwaua washirikina na si kuwateka nyara kisha kuwaacha kwa kuchukua fidia au kuwaacha bila fidia. Ulamaa wengi anakubaliana kuwa Imamu ana hiari kati ya kutoa hukumu ya kuwaua au kupokea

fidia au kuwafanya watumwa au kuwaacha bila masharti. Atatoa hukumu kwa kuzingatia maslahi ya Waislamu. Imethibiti katika Hadithi sahihi kuwa Mtume alitoa hukumu ya kuwa baadhi ya mateka na wengine kulipa fidia na wengine aliwaacha huru. Hukumu hizo zilitolewa kwa kuangalia maslahi ya Waislamu. Ewe Mola teremsha Sala na Salamu juu ya Mtume wako Muhammad ﷺ.



**‘Mashindano’ ya ‘Kulenga Shabaha’,
‘Riadha’ ya ‘mwili’ na ‘Akili’**

Mada ya Kwanza

Katika kuhamasisha michezo yote ambayo katika kipindi cha awali cha Uislamu ilifahamika kwa jina la *Furusia* (yaani kujifunza ushujaa), na pia ni kutafuta katika michezo hiyo nguvu za kujilinda na kutetea haki na kuinusuru. Lengo lake toka awali halikuwa kupata mali na kuikusanya wala kupata umashuhuri na kupenda kutangazwa, wala yanayoambatana na hayo ya kupanda na ukubwa katika ardhi, wala kufanya ufisadi, kama inavyofahamika kwa wana michezo walio wengi leo hii. Hakika kinachokusudiwa kwa kufanya mazoezi na michezo ya aina zake zote ni kujenga uwezo, nguvu, na afya ya mwili ili kukuwezesha kufanya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa sura hiyo ndiyo tunavyotakiwa tuifahamu michezo ama atakayefahamu kinyume na hiyo atakuwa ameitoa michezo kwenye lengo lililokusudiwa na ukweli wake sahihi na kuipeleka kwenye lengo na nia mbaya ya kipuuzi isiyofaa na kuifanya kuwa kamari iliyo haramishwa. (chanzo cha asili ya uhalali wa michezo na mazoezi katika Uislamu ni Maneno ya Mwenyezi Mungu:

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ

“Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo.” (8:60).

Na katika maneno (hadithi) ya Mtume ﷺ anasema:

“Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendeza sana kwa Mwenyezi Mungu kuliko Muumini dhaiifu.” (Imepokewa na Muslim, Ibn Majah na Imam Ahmad).

Mada ya Pili

Michezo Inayofaa kuweka zawadi, au rehani (kitu cha kushindania) na michezo isiyofaa kuweka rehani.

Inafaa kuweka *rehani* (zawadi) katika mashindano na kutolewa rehani hiyo (kwa mshindi) bila khitilafu yoyote kati ya Ulamaa (wataalamu) wa Kiislamu katika mashindano ya farasi, ngamia na kulenga shabaha kwa ushahidi wa Hadithi ya Mtume ﷺ inayosema:

“Hakuna kuweka rehani ya kushindania katika mashindano isipokuwa katika mashindano ya farasi ngamia, au kulenga shabaha.” (Abu Dawud na Tirmidhi).

Kinachokusudiwa katika mashindano ni kile kinachowekeka rehani na anakichukua mshindi katika mashindano hayo.

Ama mashindano yasiyokuwa ya aina hizi tatu, kama vile mieleka, kuogelea, kukimbia, baiskeli, au gari au kunyanyua vitu vizito, au maboti ya baharini, au kujibu maswali ya kielimu, au kuyahifadhi na kuyadhihirisha (yaani kuyasoma bila kuangalia) kwa hakika haya yote pamoja na kuwa ni michezo inayoruhusiwa kisheria lakini haifai kufanywa kwa kushindania kitu, wala haifai kwa mshindi kuichukua hii kuwa ndio kauli sahihi. Wala haichukuliwi kuwa ni hoja ya kuruhusu hayo kisa cha Mtume ﷺ alivyoshindana na Rukana bin Zaid katika mieleka na kumshinda na kuchukua mbuzi ambaye Rukana alimuweka rehani kwa atakayeshinda. Pia haichukuliwi kuwa ni hoja pale Abubakar Siddiq alivyowekeana rehani na Makureish katika suala la ushindi wa Warumi na aliposhinda alichukua kilichowekeka rehani, kwani kipindi kile ilikuwa ni mwanzo wa Uislamu kabla ya kuweka rehani katika michezo ya aina tatu kama iliyotajwa katika Hadithi, na kuruhusiwa mshindi kuchukua rehani hiyo. Michezo hii mitatu ina faida kubwa (katika matayarisho ya *jihadi*, ama aina zilizobaki hazina athari yoyote katika *jihadi*).

Jihadi inategemea sana uwezo wa mtu katika kupanda farasi, ngamia, na kulenga shabaha kwa kutupa mishale. Kama vifaru na ndege za kivita kwa wakati huu vitalinganishwa na ngamia na farasi katika kusihhi kufanyika mashindano, na kuweka

rehani, na kuichukua inafaa, kwani vitu hivyo vina athari kubwa katika jihadi na ambavyo ndiyo lengo kuu la kufanya michezo (si michezo mingine inayoishia kuvimbisha mwili tu). Kwa upande mwingine ni kuwa kama sheria ya Kiislamu ingeruhusu kuwekwa rehani katika mchezo isiyokuwa mitatu iliyotajwa katika Hadithi, baadhi ya watu wangepanya michezo hiyo kuwa ndiyo shughuli yao ya kuendeshea maisha na kupatia riziki. Hiyo ingesababisha kusahaulika lengo muhimu la kuruhusiwa michezo katika mapambano ya jihadi. Katika kutetea haki itawale na kupiga vita na kuondoa ubaya na maovu katika ardhi kwa kuabudiwa Mwenyezi Mungu Peke Yake na kufuatwa sheria yake mpaka watu wote waishi katika furaha katika Dunia hii kisha katika akhera yaona wala wasiishi katika mashaka na matatizo.



Mada ya Tatu

Namna ya kuweka rehani (zawadi) katika mashindano ya mbio na kulenga shabaha

Njia bora na nzuri katika kuweka *rehani* katika mashindano ya michezo ya shabaha ni kuwekwa na serikali, au taasisi binafsi, au wahisani binafsi. Hii itaondoa *shub'ha* (yaani sura inayofanana na Kamari) katika rehani, na ibebe sura sahihi ya kuhamasisha michezo ambayo haikusudiwi ila kuwavuta watu wapende kujiandaa kwa *jihadi*. Pamoja na yote hayo hakuna ubaya iwapo upande mmoja katika wanaoshindana utajitolea kuweka kitu cha kushindania mmoja wa wanaoshindana anaweza kumwambia mwenzake: Ukinishinda nitakupa dinari kumi au mia (au mfano wa hizo). Jamhuri ya Ulamaa wanaona kuwa inafaa (ni ruhusa) kwa pande mbili zinazoshindana kila upande utoe kitu cha kushindania (*rehani*) lakini kwa sharti kuwa washirikishe mtu wa tatu ambaye yeye hatatoa chochote. Mtazamo huu ni wa Saidi bin Musayyib; ama Imamu Maliki hakubaliani nao. Lakini kuna Ulamaa wengine wanaunga mkono rai ya bin Musayyib.



Mada ya Nne

Namna ya kupanga mashindano

Katika kupanga mashindano ni lazima yawepo maandalizi yafuatayo:

1. Kutaja aina ya chombo cha kufanyia mashindano kama farasi, ngamia, kifaru au ndege.
2. Wanaoshindana wote watumie vifaa au vyombo vya aina moja isiwe wengine wanatumia farasi na wengine ngamia.
3. Kutaja umbali wa mashindano na yasiwe mafupi sana wala marefu sana.
4. Kutaja zawadi (*rehani*) zilioandaliwa kama ni shindano lenye zawadi.

Kisha farasi wanaoshindaniwa wanapangwa kwenye safu moja, miguu yao iwe imeelekeana, kisha refa au kamisaa wa mashindano anatoa amri ya kila anayeshiriki kujitayarisha na kujiandaa, na kisha anatoa *tabkira* tatu, *tabkira* ya mwisho ndiyo inayowaruhusu wote kuanza kuondoka kwa upande wa pili yanakomalizikia mashindano wanakuwepo marefa wawili kila mmoja anasimama kwenye ncha ya mstari uliowekwa kuwa ndiyo alama ya mwisho ya mashindano. Wanaangalia ambaye atakuwa wa kwanza kuufikia katika wanaoshindana na huyo ndiye atakayekuwa mshindi. Iwapo washindi watakuwa wengi watakaopata zawadi ni kuanzia namba moja mpaka kumi tu. Ama mashindano ya kulenga shabaha kwa mishale au bunduki (risasi) na kadhalika, hii ni bora kuliko mashindano ya farasi na mengineyo kwa hadithi ya Mtume ﷺ

“Jifunzeni shabaha na kupanda farasi, na iwapo mtajifunza shabaha basi Hiyo inapendeza kwangu kuliko kupanda farasi.”

Hii ni kwa kuwa faida ya kujifunza kurusha mishale na mikuki katika jihadi ni kubwa kuliko kupanda farasi na hiyo inafahamika. Katika mashindano ya shabaha yatazingatia mambo yafuatayo:

Inatakiwa Katika Mashindano Kuzingatia Yafuatayo:

- a) Mashindano yawahusisha walenga shabaha wazuri.

b) Kujua idadi ya alama alizopata kila mtu, na hilo ni kwa kuainisha alama ya kila mmoja anazotakiwa awe amepata.

c) Kujua kuwa mshindi ni yule atakayekuwa amefanya vizuri mwanzo, au ni yule atakayefanya vizuri kwa wingi kuliko mwingine. Kwa mfano itangazwe kuwa, atakayewahi kupata pointi tano za mwanzo katika pointi ishirini basi huyo ni mshindi, au itangazwe kuwa yeyote kati yetu atakayemzidi mwenzake zaidi ya pointi tano katika pointi ishirini atakuwa mshindi.

d) Kuainisha ukomo na mpaka wake (na mashindano) na kuwa katika masafa yanayokubalika kiakili kwa ukaribu wake na umbali wake. Wakishakubaliana, mmoja wao atanza kutupa. Na iwapo watabishana zawadi ya shindano hilo. Wajiepushe katika shindano hilo na aina yoyote ya dhulma mpaka mwisho wake. Mshindi atachukua zawadi (*rehani*).

Tanbihi:

Makubaliano ya mashindano ya michezo na kulenga shabaha ni jambo linaloruhusiwa na si wajibu, kwani mmoja katika pande zinazoshindana anaruhusiwa kuvunja makubaliano muda wowote. Na mtu akisema: ‘Yeyote atakayenishinda nitampa zawadi fulani.’ Kauli hii itachukuliwa kama ahadi, na iwapo atatokea mtu akamshinda hatalazimishwa kutekeleza ahadi yake, bali ataitekeleza kwa kulinda ucha-Mungu na ukarimu wake, kwani kuvunja ahadi kwa Muislamu ni haramu. Mtu akisema: ‘Yeyote nitakayemshinda katika ninyi atanipa zawadi fulani, au nitamdai kitu fulani’, hii haifai kwani tayari imeshatoka nje ya kanuni za mashindano na imegeuka kuwa njia ya kuchuma mali kwa njia isiyokuwa ya haki.



Mada ya Tano

Michezo isiyoruhusiwa iwe kwa kushindania zawadi au bila zawadi.

Haifai kufanya mashindano katika michezo ya drafti, karata, bao, dhumna na mpira wa meza, na mpira wa vinyoya, na mfano wa michezo hiyo. Yafaa mashindano ya mpira wa miguu kwa masharti. Kwanza: Lengo na nia yake iwe ni kujenga vizuri uwezo na maandalizi ya kufanya vizuri katika *jihadi*. Pili: washiriki wasicheze wakiwa mapaja wazi (wako uchi). Tatu: Wasichelewe kusali Sala kwa wakati wake uliopangwa kisheria. Nne: Uwe mbali na matendo maovu kama uongo, kutukanana na mfano wa hayo.

Tanbihi:

Inaruhusiwa mfadhili yeyote kutangaza kuwa: ‘Atakayehifadhi juzuu za Qur-aan au Hadithi kadhaa za Mtume ﷺ au atakaye jibu maswali kadhaa ya mirathi, au ya hisabati, atapata zawadi ya vitu kadhaa au fedha. Lengo ni kuhamasisha wahifadhi kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur-aan) na Hadithi za Mtume ﷺ na masuala ya kitaaluma ambayo ni muhimu kwa umma wa Kiislamu. Atakayeshinda anaruhusiwa kuchukua zawadi akitaka au kuziacha, na mtayarishaji wa mashindano anatakiwa akabidhi zawadi kwa mshindi.



Katika Kuuza na Kununua

Mada ya Kwanza

Hukumu ya kuuza, hekima na nguzo zake

1) Hukumu ya kuuza:

Kuuza kumeruhusiwa kwa aya ya *Qur-aan*. Allah (*Subhanahu wa Taala*) Anasema:

وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا

“...*Na Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na ameharimisha riba....*” (2:275).

Pia katika sunna ya kimaneno na kivitendo zote kwa pamoja zimeruhusu kwani Mtume ﷺ aliuza na pia alinunua na akasema:

“*Mtu wa mjini asiuze kwa niaba ya mtu wa mashambani.*”
(Imepokewa na Abu Dawud, Tirmidhi na Ibn Majah).

Akasema pia?

“*Wanaouziana wana hiyari (ya kukubaliana au kukataa) katika kipindi ambacho bado hawajafunga makubaliano na kuachana.*”
(Bukhari, Muslim).

1.Hekima yake:

Hekima inayopatikana katika sheria hii inayoruhusu kuuza na kununua ni kumuwezesha kila mtu kupata mahitaji yake kutoka kwa mwenzake bila madhara wala maudhi.

2.Nguzo za Kuuza:

Nguzo za kuuza ni tano nazo ni:

Minhajil Muslim

a) Muuzaji: Nilazima muuzaji awe ndiye mmiliki wa kinachouzwa au awe ameruhusiwa na muhusika awe na akili kamili na siyo mjinga.

b) Mnunuzi; na awe ni mtu anayeruhusiwa kisheria kutumia mali yake, yaani asiwe mjinga, wala mtoto mdogo ambaye bado hajaruhusiwa kutumia mali yake anavyotaka.

c) Mali inayouzwa; ni lazima mali hiyo iwe ni mali ya halali, iwe *twahir* (isiwe najisi), iwezekane kuikabidhi, iwe yenye kufahamika kwa mnunuzi.

d) Tamko la mauziano, nalo ni tamko la makubaliano, mfano: Niuzie mali yako fulani'. Na Muuzaji anajibu, 'Ninakuuzia mali yangu kadhaa. 'Na inaweza kuwa kwa kitendo pasi na maneno kwa mfano anaweza kusema, 'Niuzie nguo fulani', na Muuzaji bila kujibu anachukua nguo ile na kumpa.

e) Maridhiano; mauziano hayawezi kuwa sahihi na halali bila makubaliano yapande mbili kwa Hadithi ya Mtume ﷺ anasema:

“Kwa hakika kuuza kunatokana na maridhiano.” (Ibn Majah)



Mada ya Pili

Masharti yanayosihi na yasiyosihi Kutumika katika kuuziana.

1) Masharti yanayokubalika.

Inasihi kutaja sharti (sifa) na wasifu wa kinachouzwa wakati wa kuuziana (kama kinachouzwa kiko mbali), iwapo sifa hiyo itapatikana mauziano yatakuwa sahihi na kama sifa hiyo haitakuwepo mauziano yatakuwa batili. Kwa mfano mnunuzi wa kitabu atoe sharti kuwa karatasi za kitabu hicho ziwe za rangi ya njano, au mnunuzi wa nyumba aseme kuwa mlango wa nyumba hiyo uwe wa chuma. Pia inasihi kuweka masharti kwa manufaa binafsi, kwa mfano, mtu anauza farasi lakini akaweka masharti kuwa ataendelea kumpanda mpaka amfikishe mahali kadhaa. Au mtu ameuza nyumba anayoishi kwa sharti kuwa ataendelea kukaa ndani yake mwezi mmoja, au mnunuzi wa nguo aseme kuwa ni sharti ishonwe, au mnunuzi wa kuni aseme kuwa sharti zivunjwe kwani sahaba wa Mtume ﷺ Jabir aliweka sharti kwa ngamia wake aliyemuuzia Mtume ﷺ ambebe baada ya kumuuzia.

2) Masharti yasiyokubalika:

a) Haifai kuweka masharti mawili katika kitu kimoja kilichouzwa. Kwa mfano kuweka sharti katika kuni zilizounuliwa kuwa azivunje na kuzibeba, Haifai kwa hadithi ya Mtume ﷺ.

“Haifai kukopesha na kuuza hapo hapo, wala masharti mawili katika uzo moja.” (Abu Dawud na Tirmidhi).

b) Si kuweka sharti linaloingilia mambo ya msingi katika kuuziana. Kwa mfano muuzaji kuweka sharti kuwa mnyama huyu ukimnunua huruhusiwi kumuuzia au usimuze kwa Zaid au usimtoe kumpa Umar au kuwa akimnunua basi akubali kumpa mkopo au naye amuuzie kitu fulani. Kwa hadithi ya Mtume anasema;

“Haifai kukopesha na kuuza hapo hapo, wala masharti mawili katika uzo moja wala kuuza asichokimiliki.” (Bukhari na An-Nasai).

c) Haifai kuweka sharti batili ambalo kunasihi pamoja nalo na linabatilika, kama vile asipate hasara atakapouza mnunuzi, au muuzaji kuweka sharti mtumwa kuwa uongozi utakuwa wake, sharti katika mfano wa mambo haya mawili ni batili lakini mauzo ni halali kwa neno lake Mtume ﷺ.

“Atakayeweka sharti ambalo halipo katika kitabu cha Mwenyezi Mungu sharti hilo ni batlli, na hata ikiwa ni masharti mia moja.”
(Abu Dawud na Hakim).



Mada ya Tatu

Hukumu ya khiyari katika kuuziana.

Imewekwa sheria ya mtu kukhiyari katika kuuziana katika masuala mbali mbali nayo ni:

1) Katika muda ambao muuzaji na mnunuzi bado wako katika kikao kabla hawajaachana, hapo kila upande una fursa ya kukubali au kukataa (*khiyar*) katika kupitisha mauziano au kuyavunja kwa Hadithi ya Mtume ﷺ;

“Wanaouziana wako kwenye khiyari maadam hawajaachana; iwapo watakuwa wa kweli na wakibainisha wazi watabarikiwa katika mauziano yao, na wakificha wakadanganya itaondolewa baraka ya mauziano yao.” (Bukhari na Muslim)

2) Iwapo mmoja wao ataweka sharti la kuwoko muda maalumu wa mwisho kuhusu makubaliano na wote wakakubaliana, basi wote wana *khiyari* mpaka muda wote utakapoisha, na hapo ndipo mauziano yatakapoanza kwa hadithi ya Mtume ﷺ

“Na Waislamu wako juu ya masharti yao (waliojiwekea).” (Abu Dawud).

3) Mmoja wao akibainika kuwa amepunja (amemdhulumu) mwenzake waziwazi ikifikia theluthi au zaidi, kwa mfano kitu shilingi kumi anamuuzia kwa kumi na tano au ishirini, mnunuzi akigundua hilo anahiyari kuvunja makubaliano, au kuchukua kitu kile kwa bei inayokubalika. Kwa hadithi ya Mtume ﷺ alipokuwa akimwambia mtu aliyekuwa akipunjwa wakati wa kununua kutokana na udhaifu wa akili yake.

“Utakayeuziana naye mwambie tusifanyiane udanganyifu.” (Muslim na Ahmad)

Hiyo ni kwa kuwa ikibainika kuwa amepunjwa itasaidia kurudishiwa ile ziada au kuvunja makubaliano.

4) Muuzaji atakapo *ghushi* katika mali anayouza, ama kwa kuweka juu mali nzuri na kuficha mali mbaya, au kuweka juu mali nzuri na mali mbovu akaificha, au akakusanya maziwa katika chuchu za mbuzi ili aonekane ana maziwa mengi, hapo mnunuzi atakapogundua ana *khiyari* kuvunja makubaliano au kuendelea nayo kwa Hadithi ya Mtume ﷺ inasema:

“Msilimbikize maziwa katika chuchu za ngamia au kondoo na mbuzi, na atakayemnunua atakhiyarishwa kati ya mambo mawili baada ya kumkamua maziwa yake akitaka abaki naye, na akitaka amrudishe, na kama ni kumrudisha basi iwe ni pamoja na pishi ya tende.” (Wamepokea Bukhari, Muslim, Abu Dawud na An-Nasai).

5) Mnunuzi ana hiyari ya kuvunja mapatano au kuendelea nayo iwapo mali iliyouzwa ikikutwa na kasoro inayosababisha kupungua thamani yake na mnunuzi hakuifahamu na kuridhika nayo wakati wa mapatano. Kwa hadithi ya Mtume ﷺ inayosema:

“Si halali Muislamu kumuuzia ndugu yake kitu chenye aibu isipokuwa atapombainishia aibu hiyo.” (Imepokewa na al-Hakim na al-Baihaq).

Na katika hadithi sahihi Mtume ﷺ anasema:

“Anayetu ghushi si katika sisi.” (Muslim na Imam Ahmad).

6) Watakapotofautiana wanaouziana katika kiasi cha thamani walichokubaliana au wasifu wa bidhaa iliyouzwa, kila mmoja ataapa kiapo kwa mwenzake kisha wote wawili watahiyari katika kuendelea na makubaliano au kuyavunja. Kwa Hadithi iliyopokewa:

“Watakapotofautiana wawili wenye kuuziana na biashara bado ingalipo na hakuna ushahidi basi kila mmoja ataapa kwa mwenzake.” (Ashabu Sunan).



Mada ya Nne

Aina za Mauziano yaliyokatazwa

Mtume ﷺ amekataza aina kadhaa za kuuziana, kutokana na udanganyifu uliomo na unaopelekea watu kula mali za wenzao kwa njia ya *haram*, na kughushi kunakosababisha watu kuwekeana mifundo, ugomvi, na kutoelewana. Miongoni mwa aina hizo ni:

1) ‘Kuuza biashara kabla ya kukabidhiwa’.

Haifai kwa Muislamu kununua biashara kisha kabla hajakabidhiwa toka kwa aliyenunua kwake akauza bidhaa ile kwa mtu mwingine, kwa ushahidi wa Hadithi ya Mtume ﷺ

“Unaponunua kitu usikiuze mpaka baada ya kukabidhiwa.”
(Ahmad na Addaraqutni)

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Mtu mwenye kununua chakula asikiuze mpaka akimiliki.” (Bukhari)

Amesema Ibn Abbasi رضي الله عنه, ‘Sina shaka kuwa kila kitu kipo katika hukumu hii. Yaani hukumu ya vitu vingine ni sawa na iliyotajwa katika Hadithi hiyo.

2) Kuingilia Mauzo ya Muislamu Mwezake.

Haifai Muislamu kununua bidhaa kwa nduguye Muislamu kwa shilingi tano (kwa mfano) kisha akasema, “Mrudishieni mwenyewe bidhaa yake, mimi nitakuuzia kwa bei nafuu ya shilingi nne”. Hiyo ni kwa ushahidi wa Hadithi ya Mtume ﷺ

“Na wasiuze baadhi yenu kwa mauzo ya watu wengine.”
(Imepokewa na Tirmidhi, Ibn Majah, Imam Ahmad na An-Nasai)

3) ‘Kuuza Kwa “Najash”

Najash katika lugha ya Kiarabu, ni kugutusha windo kutoka mahala pake ili kipate kuwindwa. Na katika sheria, ni kuzidisha thamani katika bidhaa bila ya kukusudia kuinunua, bali tu wapate kuingia wanunuzi na kununua.

Haifai kwa Muislamu kuingiza chochote katika thamani ya bidhaa hali ya kuwa hataki kuinunua, ila tu kutaka wanunuzi wamfuata, na waghurike naye kama ambavyo haifai kumwambia mnunuzi. Bidhaa hii imenunuliwa kwa kiasi kadha wa kadha, hali ya kuwa ni uwongo mtupu, ili tu amdanganye mnunuzi. Hii ni sawasawa alikubaliana na mwenye bidhaa au laa. Kwa mujibu wa kauli ya Ibn Umar رضي الله عنه:

“Mtume ﷺ amekataza “Najash.”

Na kauli yake Mtume ﷺ

“*Wala msifanyiane Najash*” (Imepokewa na Abu Dawud, Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Majah)

4) ‘Kuuza kilicho Haramu na Najisi’:

Haijuzu kwa Muislamu kuuza kitu kilichoharamishwa wala kilicho najisi, wala nguruwe, wala picha, wala mzoga, wala sanamu, wala zabibu kwa anayezitengezea pombe. Kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ

“*Hakika Allah ameharamisha kuuza pombe, mzoga, nguruwe, na masanamu.*” (Abu Dawud)

Na akasema vile vile Mtume ﷺ

“*Mtu mwenye kulimbikiza zabibu siku za mavuno ili aje kuziuzua kwa myahudi au mnasara (mkristo) au kwa anayezitengeza pombe, basi amejitosa Motoni hali ya kuwa anaona.*”

5) ‘Kuuza kwa Udanganyifu’

Haifai Muislamu kuuza kitu ambacho ndani yake kuna udanganyifu. Samaki hawauzwi wakiwa kwenye maji, wala sufi zilizo mgongoni mwa kondoo, wala mtoto wa (mnyama tumboni), wala maziwa (ya mnyama) yaliyo ndani ya matiti, wala matunda kabla ya kupevuka, wala punje (za nafaka) kabla hazijakomaa, wala bidhaa bila ya kuiangalia au kuigeuza geuza na kuichunguza kama iko pale pale, au bila ya hata kutolewa maelezo na kujua aina yake, na uwingu wake, kama bidhaa hiyo haiko pale, na hayo ni kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ

“Msinunue samaki wakiwa ndani ya maji, hakika kufanya hivyo ni Udanganyifu” (Wamepokea al Baihaqi, Tabarani, Ahmad).

Na kauli ya Ibn Umar رضي الله عنه:

“Mtume ﷺ amekataza kuziua tendi mpaka ziwe na ladha, au sufi juu ya mgongo (wa kondoo) au maziwa kwenye matiti, au samli kwenye maziwa.” (Daraqutniy).

Na kauli yake,

“Mtume ﷺ amekataza kuuza matunda mpaka yaanze kuiva. Alipoulizwa Mtume ﷺ maana ya kuanza kuiva. Akasema, ‘Yafanye wekundu’, na akasema (katika kufafanua sababu ya kukatazwa kuuza matunda kabla ya kuanza kuiva) Allah atakapozuia matunda itakuhalalikia vipi mali ya nduguyo?”. (Imepokewa na Imam Ahmad na Ibn Majah).

Na kauli ya Abu Said al-Khudry kuwa,

“Mtume ﷺ amekataza kuuza kwa kugusa na kurusha.” (Imepokewa na Bukhari, An-Nasai na Ibn Majah)

Kugusa, ni mtu kugusa nguo ya mtu mwingine kwa mkono wake, wakati wa usiku au mchana wala haigeuzi geuzi. Kurusha: Mtu kumtupia nguo yake mtu mwingine na yule mtu kumtupia nguo yake mtu mwingine ikawa hayo ndio mauziano kati yao bila ya kuiangalia wala kuipekuapekua wala kuigeuzageuza.

6) ‘Kuuza Mauzo Mawili Katika Uzo Moja:

Haifai Muislamu kufanya mauzo mawili ndani ya uzo moja, bali kila patano la uzo moja lifanyike peke yake, kutokana na ubabaishaji uliomo katika hilo unaopelekea kumuudhi Muislamu au pia kula mali yake bila haki yoyote. Kuuza mauzo mawili ndani ya uzo moja kuna sura nyingi, miongoni mwa hizo ni kumwambia mnunuzi; - Nimekuuzia kitu hiki kwa (shilingi) kumi fedha taslimu, au kwa (shilingi) kumi na tano kwa mkopo na mauzo yakapita bila ya kumbainishia ni ipi kati ya aina mbili hizo ameipitisha? Na miongoni mwa (Sura zake) ni kumwambia mnunuzi kwa mfano: Nimekuuzia nyumba hii kwa (shilingi) kadhaa kwa sharti uniuzie mimi kitu Fulani kwa thamani fulani. Miongoni mwa sura zake kwa mfano: Kumuuzia kitu tofauti kwa dinari na mapatano yakapita bila ya kujua yule mnunuzi ni kipi kati ya vile vitu viwili amenunua. Ni kutokana na yaliyopokewa kutoka kwake ﷺ

“Kwamba yeye amekataza kuuza mauzo mawili katika uzo moja.” (Ahmad na Tirmidhi)

7) ‘Kuuza kwa “Urbuun”

Haifai Muislamu kuuza kwa mauzo ya ‘Urbuun’ au kuchukua kwa hali yoyote, ni kutokana na yaliyopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ

“Kwamba yeye amekataza kuuza kwa ‘Urbuun.’” (Imam Malik)

Imam Malik amesema kakika ufafanuzi wake, ‘Urbuun’ ni kununua kitu au kukodi mnyama kisha akasema ‘nimekupa dinari moja ili kama mimi nitaiacha hii bidhaa au kukodi basi hiyo niliyokupa ni yako.

8) Kuuza asichokuwa nacho

Haifai Muislamu kuuza bidhaa asiyokuwa nayo au kuuza kitu kabla hajakimiliki. Ni kutokana na yale yanayoweza kuletwa na hali hiyo kama vile kumuudhi muuzaji na mnunuzi katika hali ya kupatikana hiyo bidhaa iliyouzwa. Na kwa sababu hiyo amesema Mtume ﷺ

“Usiuze kitu usichokuwa nacho” (Wamepokea Abu Dawud, Tirmidhi, An-Nasai, na Ibn Majah)

“Na amekataza kuuza kitu kabla ya kukipokea.” (Bukhari).

9) Kuuza deni kwa deni

Haifai kwa Muislamu kuuza deni kwa deni kwani hiyo iko katika hukumu ya kuuza kitu kisichokuwepo kwa kitu kisichokuwepo na Uislamu haukubaliani na hilo. Na mfano wa kuuza deni kwa deni ni kuwa na *qintwara* mbili kwa mtu deni la muda ukamuuzia mtu mwingine deni hilo kwa shilingi elfu ishirini kwa mkopo. Mfano mwingine ni wewe kuwa unamdai mtu mbuzi mmoja kwa muda maalum na unapofika muda wa kulipa yule mdaiwa anashindwa kulipa, na anakwambia: Niuzie (hili deni) kwa Shilingi Elfu kumi kwa muda maalum mwingine, basi utakuwa umemuuzia. Deni kwa deni amekataza Mtume ﷺ kuuza deni kwa deni. (Daraqutni).

10) Kuuza kwa ‘Al-lyna

Haifai Muislamu kuuza kitu kwa mkopo kisha akakinunua kutoka kwa yule aliyemuuzia tena kwa thamani ndogo kuliko ile aliyomuuzia. Kwa sababu atakapomuuzia kwa kumi kisha akakinunua kwa tano anakuwa kama vile mtu aliyempa mtu tano kwa mkopo kwa (kulipa) kumi, na hii ndio riba hasa ya kucheleweshwa iliyoharamishwa kwa mujibu wa kitabu (Qur-aan) na Sunnah, na pia kwa Ij-maai (makubaliano ya wanazuoni wote). Hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Watu watakapofanyia ubakhili dinari na dirham na wakauziana kwa ‘Al-lyn’ Na wakai fuata mikia ya ng’ombe (wakashughulika sana na kuchunga mifugo Yao), na wakaacha jihadi katika njia ya Allah, Allah atawateremshia balaa na Kamwe hatawaondolea mpaka warejee katika dini yao.” (Imam Ahmad).

Mwanamke mmoja alisema kumwambia Aisha - Radhi za Allah zimshukie:

‘Mimi ni kijana (Mtumwa) kwa Zaid bin Arqam kwa dirham mia nane kwa mkopo wa muda maalum, nami tena nikamnunua kutoka kwake kwa Dirham mia taslim. Aisha –Radhi za Alla zimshukie – akasema: “Ni ubaya mno ulichokinunua na ni kibaya mno ulichokuza,. Kwa hakika jihadi yake (asiyeshiriki vitani) pamoja na Mtume ﷺ imekwishabatilika isipokuwa akitubu’. (Daraqutniy).

11) ‘Mtu wa mjini kuuza bidhaa za mtu wa shamba’.

Mtu wa shamba au mgeni katika mji ule atapoleta bidhaa ambayo anataka kuiuza sokoni kwa bei ya siku ile basi haifai mtu wa mjini kumwambia (yule wa shamba) bidhaa hii iache kwangu nakuuzia baada ya siku moja au zaidi kwa thamani kubwa zaidi kuliko hii ya leo na hali ya kuwa watu wanaihitaji bidhaa hiyo. Ni kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ.

“Mtu wa mjini asimuuzie wa shamba, watu waacheni wapane riziki wao kwa Wao.” (Wamepokea Bukhari, Muslim na Imam Ahmad)

12) ‘Kunuuu kutoka kwa wasafiri’

Haifai Muislamu kusikia kuwa kuna bidhaa inawasili nchini/mjini basi akatoka ili akaipokee kutoka kwa wasafiri waletao bidhaa nje ya mji akanunua kutoka huko huko nje, halafu yeye akaingia (Mjini) na kuuza atakavyo. (Haijuzu) kutokana na hilo la kuwadanganya wenye bidhaa na kuwaletea madhara watu wa mji ule, miongoni wa wafanyabiashara na watu wengine, na kwa sababu hiyo ndipo Mtume ﷺ akasema:

“Msiende kupokea misafara ya biashara, wala mtu wa mjini asimuuzie bidhaa Zake (Mtu) wa shamba.” (Bukhari na Muslim)

13. ‘Kununua mnyama aliyelimbikizwa maziwa’

Haifai Muislamu kumuacha mbuzi au ng’ombe au ngamia bila ya kumkama maziwa kwa maana ya kuyakusanya maziwa yake kwenye chuchu kwa siku kadhaa ili aonekane kama kwamba anatoa maziwa kwa wingi mno ili watu wapende kumnunua apate kumuuzia. Kwa vile ndani yake kuna kughushi (kuficha kasoro iliyomo ndani ya bidhaa) na hadaa. Amesema Mtume ﷺ

“Msiache ngamia na mbuzi bila ya kuwakama, basi atakayewanunua baada ya Hapo (yaani baada ya kuachwa kukamwa) ana khiari ya kuangalia moja ya mambo mawili, baada ya kumkama, akimridhia basi atabaki naye na kama

hakumridhia basi atamrudisha (Kwa mwenyewe) pamoja na pishi moja ya Tende” . (Bukhari na Muslim).

14) ‘Kuuza wakati wa adhana ya mwisho (ya pili) ya ijumaa’

Haifai Muislamu kuuza kitu chochote au kununua hali ya kuwa pameshaadhiniwa kwa ajili ya swala ya Ijumaa adhana ya mwisho, adhana ambayo pamoja nayo Imam huwa juu ya mimbari, kwa kauli yake (Allah) Mtukufu:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ
وَذَرُوا الْبَيْعَ ۗ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩﴾

“Enyi mlio amini! Ikiadhiniwa Sala siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu, lau kama mnajua.” (62:9)

15) ‘Kuuza kwa muzaabana au muhaaqala’

(Ni kuuza zabibu mbichi zilizo kwenye mti kwa kuzikisia na zabibu mbivu katika kipimo cha ujazo).

Haifai kwa Muislamu kuuza zabibu mbichi zilizo kwenye mti kwa kuzikadiria na zabibu mbivu kavu kwa kipimo cha ujazo, wala mimea iliyo katika shuke lake kwa (kuyakadiria) na punje za nafaka kwa kipimo cha ujazo, wala tende mbichi zilizo katika mitende kwa tende mbivu kwa kipimo cha ujazo. Isipokuwa kuuza kwa “Al-araayaa” ameruhusu Mtume ﷺ. “Al-‘Araayaa” ni Muislamu kumpa nduguye Muislamu mtende (kwa njia ya hiba) au mitende ambayo matunda yake hayazidi wasqi tano (ni kama kg. 715) halafu akaona ni madhara/taabu kwenda kila anapotaka kuchuma zile tende zake mbivu, basi akazinunua kwa kuzikadiria na tende kavu. Na dalili ya lile la kwanza ni kauli yake Ibn Umar رضي الله عنه zimshukie

“Mtume ﷺ amekataza ‘Muzaabana’ kuuza matunda yaliyo bustanini mwake ikiwa ni miende basi kwa tende zilizoima kwa ujazo, na ikiwa ni mizabibu basi ni kwa zabibu kavu zilizopima kwa ujazo na ikiwa ni mimea mingine basi ni kwa chakula

Minhajil Muslim

kilichopimwa kwa ujazo, amekataza yote hayo.” (An-Nasai na Ibn Majah).

Na dalili ya hili la pili ni kauli ya Zaid Bin Thabiti رضي الله عنه zimshukie:

“Kwamba Mtume ﷺ ameruhusu kwa mwenye “Aria” kuiuza kwa kuikadiria.” (Bukhari).

16) ‘Kuuza kwa ‘Thunayya (kuvua kitu)’

Haifai Muislamu kuuza kitu kisha akavua baadhi ya kitu hicho, isipokua kama kitajulikana hicho kilichovuliwa. Kwa mfano atakapouza shamba, haisihi kuuvua mtende au mti wowote usiojulikana. Kutokana na udanganyifu ulioharamishwa ndani yake. Kwa kauli ya Jabir رضي الله عنه zimshukie

“Mjumbe wa Allah ﷻ amekataza muhaaqala, muzaabana, na thunayya, isipokuwa kikijulikana (hicho kilichovuliwa).” (Bukhari).



Mada ya Tano

Kuuza Mashina ya Matunda

Muislamu atakapouza mtende au mti wowote, kama ule mtende tayari umekwishapandishwa mbegu za dume, na tayari ule mti matunda yake yameshadhihiri, basi yale matunda ni (Haki) ya muuzaji isipokuwa kama huyo mnunuzi atashurutisha (kuwa hayo mazao yawe yake yeye na wakakubaliana, basi yatakuwa ni yake) na kama si hivyo basi ni ya muuzaji, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mtu atakayeza mtende ambao tayari umeshapandishwa, basi matunda yake ni ya muuzaji isipokuwa akishurutisha mnunuzi.”
(Bukhari).



Mada ya Sita

'Riba' na'Swarfu'

1) Riba

(a) Maana yake ni:

Ziada maalumu katika vitu vya mali. Nayo iko aina mbili:- Riba ya Kuzidisha, na Riba ya Kucheleweshwa '**Riba ya Kuzidisha**' ni kuuza jinsi moja ya kitu miongoni wa zile jinsi zinazoingia Riba kwa jinsi nyingine kwa kuzidisha. Hilo ni kama vile kuuza *Qintwara* moja ya ngano kwa *Qintwara* moja na robo ya ngano, au kuuza pishi moja ya tende kwa pishi moja na nusu ya tende, au kuuza wakia moja ya fedha kwa wakia moja na dirham moja ya fedha.

Riba ya kuchelewesha iko sehemu mbili: Riba ya kijahiliya nayo ndiyo ile aliyoisema Allah katika kuiharamisha kwake:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا لَا تَاْكُلُوْا الرِّبَاۤ اَضْعَافًا مُّضَاعَفَةً وَّاتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ

تُفْلِحُوْنَ

“Enyi mlio amini! Msile riba mkizidisha juu kwa juu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.” (3:130)

Uhakika wake ni kwamba, Mtu anakuwa na deni kwa mtu mwingine kwa muda maalum unapofikia muda wake, (mdai) anamwambia (mdaiwa) ima ulipe deni au nikuzidishie (thamani ya deni) kama hakulipa humzidishia asilimia fulani ya fedha na humngojea muda mwingie, basi huwa hivi hivi mpaka huongezeka (lile deni) katika kipindi fulani likawa zaidi na zaidi. Miongoni mwa 'Riba za kijaahiliya, ni kumpa mtu dinari kumi kwa kumkopeshana alilipe kwa dinari kumi na tano kwa muda wa karibu.

'Riba ya kuchelewesha' ni kuuza kitu kinachoingia *Riba* kama vile moja ya mali mbili (dhahabu na fedha) au ngano, au shairi, au tende kwa nyingine ambayo nayo imeingiwa *Riba* ya kuchelewesha na hiyo ni kama vile mtu kuuza lundo la

tende kwa lundo la ngano kwa mkopo na kwa muda maalum, au kuuza dinari kumi za dhahabu kwa mfano, kwa dirham mia kwa ishirini za fedha kwa mkopo na muda maalum.

(b) Hukumu yake:

Riba imeharamishwa kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا الرِّبَا أَضْعَافًا مُّضَاعَفَةً

“Enyi mlio amini! Msile riba mkizidisha juu kwa juu...”

Na kwa kauli ya Mjumbe ﷺ

“Allah amemlaani mla Riba na mwakilishi wake na mashahidi wake Wawili na katibu wake.” (Imepokewa na Ahmad, Abu Dawud, Tirmidhi na Ibn Majah)

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Dirhamu moja ya Riba anayoila mtu hali ya kuwa anajua ni dhambi kubwa mno kwake kuliko zinaa thalathini na sita.” (Imam Ahmad).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Riba ina milango sabini na tatu, mwepesi wake ni mtu kumwingilia mama yake, na kwamba Riba kubwa mno ni (kumvunjia heshima) kwa cheo cha mtu Muislamu.” (Hakam).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Jiepusheni na madhambi saba yenye kuangamiza akaulizwa: Ewe mjumbe Allah ni yepi hayo? Akasema ni kumshirikisha Allah, Uchawi, na kuiua nafsi ambao Allah ameiharamishaisipokuwa kwa haki, na kula Riba, na kula mali ya Yatima na kugeuka (Kukimbia) siku ya vita (dhidi ya maadui wa Uislam) na Kusingizia

Minhajil Muslim

(machafu) wanawake waumini wenye kuhifadhika walioghafilika nayo (wasiofanya uchafu huo).” (Imepokewa na Bukhari, Muslim na Abu Dawud)

(c) Hekima ya kuharamishwa kwake: Miongoni mwa hekima za dhahiri katika kuharamishwa *Riba* zaidi ya zile hekima za ujumla zilizo katika aina zote za majukumu ya kisheria nayo ni kuitathmini imani ya mja katika utii na kutenda na kuacha, na zingine ni:

i) Kuhifadhi mali ya Muislamu ili isiliwe kwa njia za batili.

ii) Kumuelekeza Muislamu katika kuzalisha mali yake katika njia ya chumo halali na tukufu isiyokuwa na hila wala hadaa, kama vile, Kilimo, viwanda na biashara safi. Na kumuelekeza katika kilichokuwa mbali kabisa na kila linaloweza kuleta migongano kati ya Waislamu na kuchukiana.

iii) Kuziba njia zinazompelekea Muislamu kwenye uadui na nduguye Muislamu na kugongana naye. Na hivyo kumsababishia ghadhabu na chuki.

iv) Kumuepusha Muislamu na yanayopelekea kuangamia kwake, kwani mla Riba ni ‘asi na ni dhalimu na mwisho wa uasi na udhalimu ni mbaya sana, Allah Mtukufu ‘Amesema:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنَّمَا بَغْيِكُمْ عَلَىٰ أَنْفُسِكُمْ

“Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe...” (10: 23)

Na amesema Mjumbe wa Allah ﷻ

Ogopeni dhuluma, kwani dhulma ni kiza siku ya Qiama, na ogopeni Ubakhili kwani huo umewaangamiza waliokuwa kabla yenu, uliwapelekea Kumwaga damu zao, na wakahalalisha walivyoharamishiwa.” (Imam Muslim)

v) Kufungua milango ya wema mbele ya Muislamu ili apate kuandaa masurufu kwa ajili ya akhera yake, atamkopesha ndugu yake muislamu bila ya faida na

atam dai na kumngojelea muda wake wa nafasi (ya kulipa) na atamuhurumia kwa ajili ya kutaka radhi za Allah, na katika hili kuna hali inayoeneza upendo kati ya Waislamu na kuleta roho ya udugu na kusafiana kati yao.

(d) Sheria zake:

i) Misingi ya vitu vya Riba ni sita nayo ni:

Dhahabu, fedha, ngano, shairi, tende na chumvi kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Dhahabu kwa dhahabu, na fedha kwa fedha, ngano kwa ngano, shairi kwa shairi tende kwa tende, na chumvi kwa chumvi zilingane sawa kwa sawa, mkono kwa mkono zitakapo tofautiana jinsi hizo aina basi uzianeni kama mpendavyo itakapokua mkono kwa mkono.” (Muslim).

Wanavyuoni Masahaba na Taabiina na Maimamu Allah awarehemu wote (wao) wamekiambatanisha katika hukumu hii kila kinachoafikiana na hivi sita katika maana na sababu za uharamu. Wamekiambatanisha kila kipimwacho kwa ujazo au kipimwacho kwa mizani (uzito) au kinacholiwa na kinchohifadhiwa mwaka mzima, na hii kwa mfano punje za nafaka, mafuta ya kula, asali na nyama. Amesema Abu Saïd رضي الله عنه.

“Hapana Riba isipokuwa katika kitu ambaho kimepimwa kwa ujazo au uzito (Mizani) miongoni mwa vyakula na vinywaji.”

ii) ‘Riba katika aina zote za Vitu

Vitu vinavyopitia Riba inakua katika njia ya aina tatu:

Kwanza: kuuza kitu jinsi moja kwa jinsi mwenzake kama dhahabu kwa dhahabu, ngano kwa ngano, tende kwa tende kwa kuzidisha. Kwa mujibu wa waliyoyapokea Bukhari na Muslim,

“Kwamba Bilali alileta tende kwa Mtume ﷺ, aina ya Burniy, Mtume ﷺ akamuuliza, “Umezipata wapi hizi ewe Bilali? Akasema: Tulikuwa na tende mbaya nikauza pishi mbili kwa pishi

Minhajil Muslim

moja ili nimlishe Mtume ﷺ, akasema Mtume ﷺ, “Ooh”...Ndio hasa Riba usifaye tena, lakini ukitaka kunuuua (hizo nzuri) basi ziuze zile tende kwa wengine kisha nunua hizo (Nzuri kwa pesa).”

Pili: Ni kuuza jinsi mbili tofuati kama vile dhahabu na fedha, au ngano kwa tende baadhi yake kwa nyingine kimojawapo kipo na kingine cha pili hakipo na hayo ni kwa kauli yake ﷺ.

“Msiuze katika hizo kisichokuwapo kwa kilichopo.”

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Uzeni dhahabu kwa fedha, mkono kwa mkono.”

Pia kauli yake Mtume ﷺ

“Dhahabu kwa fedha inakuwa riba, isipokuwa papo kwa papo.”
(Bukhari na Muslim)

Tatu: Kuuza jinsi moja ya kitu kwa jinsi moja hiyo hiyo kwa sawa sawa lakini kimojawapo hakipo ni mkopo kama vile kuuza dhahabu kwa dhahabu au tende kwa tende, kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Ngano kwa ngano kuna Riba ndani yake isipokuwa mkono kwa mkono (na maana ya haawahahh: ni mkono kwa mkono, yaani kwa mkato)

iii) Hakuna Riba pamoja na kuishana pale pale na kutofautiana jinsi za vitu.

Haiingii Riba katika bei ambayo thamani na kilicholipiwa thamani vimetofautiana, isipokuwa kama itakuwa kimojawapo kitacheleweshwa nacho si dhahabu na fedha. Hivyo inafaa kuuza dhahabu kwa fedha kwa kuzidiana na kuuza ngano kwa tende au chumvi kwa shayiri kwa kuzidiana itakapokuwa mkono kwa mkono, yaani kimojawapo hakikucheleweshwa, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Vitakapotofautiana vitu hivi basi uzeni vyovyote mtakavyo, itakapokuwa mkono kwa mkono.”

Kama ambavo hakuna *Riba* katika vitu vilivyouzwa miongoni mwa vitu vinavyoingia *Riba* kwa fedha taslim zilizopo au zisizokuwepo, ni sawa kisichokuwepo ni thamani au bidhaa, kwani Mtume ﷺ alinunua Ngamia wa Jabir bin Abdillahi رضي الله عنه akiwa safarini na hakumpa thamani yake, isipokuwa kule Madina, kama ambavyo Mtume ﷺ amejujiza ‘*Bay’ Salam*’ kwa kauli yake,

“Atakayeza kwa mkopo kitu chochote basi na auze kwa mkopo kwa kipimo cha ujazo kinachojulikana, uzito unaojulikana na muda unaojulikana.” (Bukhari na Muslim)

Na ‘*Salam*’ hutangulizwa thamani, fedha taslim na kitu kilichothamaniwa huchelewa mpaka muda wa mbali.

iv) Ufafanuzi wa jinsi ya vitu vinavyoingia Riba

Vitu vinavyoingia Riba viko jinsi nyingi na msimamo walionao watu wengi miongoni mwa Masahaba na Maimamu (Mabingwa) wengine wanaoongoza michango yao katika kufahamisha Dini kwamba, Dhahabu ni jinsi na fedha ni jinsi, na ngano ni jinsi na shairi ni jinsi, na aina mbali mbali za tendeleo zote ni jinsi, na pamba ni jinsi tofauti, maharage ni jinsi na njegere ni jinsi. *Hirmas* ni jinsi na mpunga/mchele ni jinsi na mahindi ni jinsi, na aina zote za mafuta ya kula ni jinsi, na asali ni jinsi, na nyama ni jinsi tofauti, nyama ya Ngamia ni jinsi, nyama ya ng’ombe ni jinsi nyama ya mbuzi/kondoo ni jinsi na nyama za ndege ni jinsi nyama ya samaki mbalimbali ni jinsi nyingine.

v) Ambavyo havipimwi Riba miongoni mwa vyakula

Havipimwi *Riba* katika vitu mfano matunda na mboga mboga kwa sababu vitu hivyo haviwekwi akiba kwa muda mrefu kwa upande mmoja. Na kwa upande mwingine, vitu hivyo katika zama za kwanza havikuwa vikipimwa kwa ujazo au kwa mizani (uzito). Kingine, vitu hivyo si miongoni mwa vyakula vya msingi kama zilivyo punje za nafaka na matunda na nyama, ambayo vina maelezo ya wazi kutoka kwa Mtume ﷺ yaliyokuja kuvielezea.

Zinduzi Mbili:

Kwanza: Mabenki:

Mabenki yaliyopo hivi sasa katika miji mbali mbali ya Ulimwengu wa Kiislamu, sehemu yake kubwa yanaendesha shughuli zake kwa *Riba*. Bali hazikuwekwa isipokuwa kwa misingi halisi ya *Riba*, hivyo basi haifai kushughulika nazo isipokuwa katika hali ya dharura kama vile kufanya *hawala* kutoka nchi moja kwenda nyingine na kwa misingi hii imewajibika kwa ndugu wema miongoni mwa Waislamu kujianzishia mabenki ya Kiislamu yasio na *Riba* na yaliyoepukana na shughuli zake nyinginezo za *Riba*.

Hii ifuatayo ni sura ya Benki ya Kiislamu ya ukaribu iliyopendekezwa kuanzishwa. Watakusanyika ndugu Waislamu watu wa nchi fulani, na wataafikiana juu ya kuanzishwa nyumba watakayoita (Hazina ya Jamaa) wataichagulia mtu miongoni mwao atakayekuwa Gavana wao, atasimamia Idara zake na kuendesha shughuli zake. Jukumu la hazina hii linaishia tu katika mambo yafuatayo:

a) Kupokea na kuhifadhi amana za wale ndugu bila gharama yoyote.

b) Kukopesha ndugu Waislamu mikopo ambayo inalingana na mapato yao, au chumo lao, bila faida (*Riba*).

c) Kushiriki katika Nyanja za kilimo, biashara, ujenzi na viwanda. Hazina itachangia katika kila uwanja ambao itaona kuwa inaleta kipato au faida kwenye hazina.

d) Kusaidia uhamishaji wa fedha za ndugu hao kutoka nchi moja hadi nyingine, itapokuwa Hazina ina tawi katika nchi hiyo inayotakiwa kuhamishwa fedha.

e) Mwisho wa kila mwaka mahesabu ya hazina yatawekwa sawa (yatakaguliwa na kurekebisha) na faida zitagawiwa kwa wenye hisa kulingana na hisa zao.

Pili: Bima:

Hakuna ubaya kwa watu wa mji fulani au nchi miongoni mwa Waislamu wema kuunda mfuko maalum watakaouchangia kulingana na mapato yao ya kila mwezi,

kulingana na watavyokubaliana, katika kuchangia kila mmoja fungu maalumu watakuwa sawa sawa.

Kwa sharti mfuko huo uwe “*Waqfu*’ maalumu kwa ndugu washiriki basi yule atakayepatwa na tukio zito la kidunia kama vile moto au upotevu wa mali na kupatwa na tatizo mwilini basi atapewa kutoka mfuko huo kitu cha kumpunguzia janga au tatizo lake isipokuwa tu, inapasa kuzingatia yafuatayo:

- a. Mchangiaji anuwie mchango wake (huo mfuko) kupata radhi za Allah ili apate thawabu juu yake.
- b. Kutajwe kiasi maalumu atakachopewa mtu atakayepatwa na janga kama ambavyo pameainishwa viwango vya wanaochangia kwa namna ambayo itasimama katika usawa kamili kamili.
- c. Haikatazwi kuzalisha mali ya mfuko kwa kufanya *mudhaarabaati* wa kibiashara na ukandarasi na shughuli za viwanda zilizoruhusiwa kisheria.

1-Swarfu, Biashara ya kubadilishana Fedha

a) Maana ya ‘Swarf’:

Swarfu ni kuuza dhahabu au fedha zenyewe kwa zenyewe kama vile kuuza dinari za dhahabu kwa dirham za fedha.

b) Hukumu yake:

Swarfu inafaa kwani ni aina mojawapo ya kuuza, na kuuza inafaa kwa mujibu wa Kitabu na Sunna, Allah Mtukufu Amesema:

وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا

“...Lakini Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na ameharimisha riba...” (2:275).

Mtume ﷺ amesema:

“Uzeni dhahabu kwa fedha vyovyote mpendavyo mkono kwa mkono.”

c) Hekima yake:

Hekima ya kufaa kisheria hiyo *sarfu* ni kumfanyia wepesi Muislamu katika kuwakilisha pesa zake kwenda kwenye pesa za aina nyingine ambayo yeye anaihitajia.

d) Masharti yake:

Inashurutishwa ili kuswihi kufaa *swarfu* kukabidhiana papo hapo mkono kwa mkono. Kwa kauli yake رضي الله عنه,

“Uzeni dhahabu kwa fedha vyovyote mpendavyo, mkono kwa mkono”

Na kauli ya Umar رضي الله عنه,

“Hapana, naapa kwa jina la Allah usiachane naye mpaka nawe uchukue kutoka kwake.”

Mtume ﷺ, amesema,

“Dhahabu kwa fedha kuna Riba isipokuwa haa na haa (mkono kwa mkono).”

Haya aliyasema Umar رضي الله عنه kumwambia Twalha Bin Ubaydillah alipombadilishia fedha Malik bin Awsī akazichukua dinari na akamwambia,

“Mpaka aje muweka hazina wangu kutoka huko shambani.”
(Bukhari).

Yaani baada ya hapo ndipo atampa zile Dirham zake.

e) Hukumu Zake:

Swarfu ina hukumu (nyingi) nazo ni:

a. Inajuzu kubadilishana dhahabu kwa dhahabu, na fedha kwa fedha iwapo zitakuwa na uzito mmoja (sawa) kwa namna ambayo hakitazidi kimoja juu ya kingine, kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Msiuze dhahabu kwa dhahabu, isipokuwa sawa kwa sawa wala msizidisha baadhi juu ya nyigine, wala msiuze fedha kwa fedha isipokuwa sawa kwa sawa, wala msizidisha baadhi juu ya nyingine, wala msiuze katika hizo zilizopo kwa zisizokuwepo.”
(Imepokewa na Bukhari, Muslim, Tirmidhi, na An-Nasai).

Hayo yafanyike katika majlis (Kikao) kwa kauli yake

“Dhahabu kwa dhahabu (ni vitu vya) riba isipokuwa mkono kwa mkono na fedha kwa fedha ni Riba isipokuwa mkono kwa mkono” (Imepokewa na Bukhari, Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Majah) (haa na haa yaani mkono kwa mkono).

b. Inafaa kuzidisha pamoja na kutofautiana jinsi kama vile dhahabu kwa fedha, ikiwa ni pale pale katika kikao cha Mapatano, kwa kauli yake 

“Vitakapotofuatiana vitu hivi basi viuzeni mpendavyo itapokuwa mkono kwa mkono.”

c. Watakapoachana wawili wabadilishanao fedha kabla kukabidhiana uzo la 'Swarfu imebatilika, kwa kauli yake 

“Isipokuwa mkono kwa mkono.”

Na kauli yake,

“Itakapokuwa mkono kwa mkono.”



Mada ya Saba

‘Ssalam’

1. Maana yake:

As-Salam au *As-Salf*, ni kuuza kitu kilichotolewa wasifu kilicho katika dhima ya mtu, na mfano wa hivyo ni kama mtu kununua bidhaa iliyodhibitiwa kwa wasifu, kama vile chakula au mnyama au visivyokuwa viwili hivyo kwa muda ulioainishwa, thamani hutolewa na hungojea muda uliowekwa maalum ili kupokea bidhaa, muda utakapofika muuzaji anamuwasilishia mnunuzi ile bidhaa.

2. Hukumu yake:

Hukumu ya *As-salam*, ni inafaa kwani hiyo ni katika jumla ya kuuza na kuuza kunajuzu, na kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Mwenye kuuza kwa mkopo katika kitu chochote basi na auze kwa mkopo katika kipimo cha ujazo maalum, na kipimo cha uzito maalum na kwa muda Maalum.” (Muslim)

Kauli ya Ibn Abasi رضي الله عنه

“Mtume ﷺ aliwasili Madina hali ya kuwa wao (Watu wa Madina walikuwa) wanauziana kwa deni katika matunda mwaka mmoja, miwili na mitatu.” (Bukhari na Muslim).

3. Sharti zake:

Ili *As-salam* iswihi kuna masharti yafuatayo:

a. Thamani iwe ni fedha taslimu dhahabu au fedha, au kinachokaa nafasi za hivyo miongoni mwa sarafu ili isije ikawa kimeuzwa kitu kiingiacho riba kwa mwenzake kwa kuchelewesha.

b. Kilichouzwa kidhibitike kwa wasifu kamili unaoweza kuonwa na mtu, na hilo ni kwa kutaja jinsi yake, aina yake, na kiasi chake, ili pasije pakatokea tafauti

kati ya Muislamu na nduguye Muislam. Tafauti itakayosababisha uhasama na uadui.

c. Muda wake uwe unajulikana uwe umewekewa mipaka, na wa mbali kama vile nusu mwezi au zaidi.

d. Thamani ikabidhiwe pale pale katika kikao ili isije ikageuka kuwa ni namna ya kuuza deni kwa deni kuliko haramishwa. Asili/dalili ya masharti haya ni kauli yake

“Mwenye kuuza kwa mkopo katika kitu chochote basi na auze kwa mkopo katika kipimo cha ujazo maalum, na uzani maalum na kwa muda maalum.”

4. Sheria zake:

a. Muda uwe ni katika ambao soko hubadilika ndani yake, na huo ni kama mwezi na mfano wake, kwa sababu kuuza kwa deni (*As-salam*) katika muda mfupi hukumu yake ni hukumu ya kuuza kwa kawaida, na kuuza kwa kawaida kunashurutiswa ndani yake kuona kitu kinachouzwa na kukikagua.

b. Uwe muda ambao mara nyingi hupatikana kile kilichouzwa kwa deni, haitaswihi kuuza kwa deni tendeleo mbivu wakati wa masika (*Rabii*), au zabibu mbivu wakati wa kipupwe kwa mfano kwa sababu hiyo inapelekea magomvi kati ya Waislamu.

c. Katika makubaliano iwapo hapakutajwa mahali pa kukabidhi bidhaa, ni wajibu kuikabidhi pale mahali yalipofanyika makubaliano, na iwapo pametajwa na kuainishwa mahali mahususi basi ni kama palivyoainishwa katika makubaliano, na popote pale watapoafikiana kuhusu mahali pa kukabidhi (bidhaa) ni wajibu kukabidhi hapo hapo, kwani waislamu wanapaswa kuzingatia masharti yao.

Mfano wa maandishi (hati) ya Kuuza

Baada ya Bismillah Tukufu atasema: “amenunua fulani wa fulani yeye mwenyewe kutoka kwa fulani wa Fulani kwa ajili yake mwenyewe, nao wawili hao wakiwa katika hali ya uzima wao, na akili zao timamu, na ruhusa yao weyewe amenunua kutoka kwake bila ya kulazimishwa, tena kwa khiari. Amenunua nyumba yote

iliyopo mahali... katika mji au kijiji... ardhi na jengo juu yake na chini yake, na ambao sifa yake ni kama vile uonaji ulivyojulisha na pande mbili waliyouziana. Wamehakikisha kuwa nyumba hiyo inajumuisha vitu... (vitatajwa wasifu kamili) na ambayo inapakana nayo upande wa mashariki nyumba... ambayo inajulikana kuwa ni ya... na upande wa magharibi ni ya... kaskazini na kusini... na...

Pamoja na manufaa yake yote na viambatanisho vyake vyote njia zake, (sehemu zake za) juu na chini yake, mawe yake, mbao zake, milango yake, madirisha yake, njia zote za maji, manufaa yake yote yaliyo ndani yake na nje yake, (amenunua) ununuzi wa kisheria ulioepukana na kuvua kitu (rejea aina ya kumi na sita ya kuuza kulikokatazwa katika kitabu hiki). Imeepukana na kila sharti baya katika kuuza linaloiharibu, na hiyo ni kwa thamani ya... Mnunuzi aliyetajwa hapo juu ametoa thamani yote iliyotajwa hapo juu kwa muuzaji aliyetajwa hapo juu, akakabidhi kisheria vyote vilivyotajwa wasifu wake na vilivyotajwa mipaka yake hapo juu na mnunuzi akavipokea kutoka kwake upokeaji wa kisheria kama unavyopasa upokeaji wa vitu kama hivyo.

Kila mmoja kati yao amechagua mwenzie kwa ridhaa na wakachagua kupitisha mauzo na kuithibitisha na wakitengana juu ya hilo baada ya kuwashuhudilisha (watu kutoa ushahidi) juu yao watu wanaowajua ambao ni... (jina) na... (jina). hayo yamekamilika mnamo tarehe.....

Hati ya Maandiko ya mauzo ya mkopo *As-Salam*

Baada ya kumuhimidi Allah Mtukufu, "... (jina) amekiri kwamba yeye amepokea na kukabidhiwa kutoka kwa... (jina)... (kitu) ni... malipo ya mauzo ya *salam*, katika kuuza kitu... (cha ngano kwa mfano, ataitaja aina yake). Na hiyo ni kwa kipimo cha ujazo cha nchi.....

Atapewa kitu hicho baada ya kupita miezi miwili kamili kutoka tarehe yake (hii) hali ya kuwa atabebewa hadi mahali fulani. Na amekiri ule ujazo na kiasi juu ya hayo, na alipokea rasilimali ya mauzo ya '*Salam*' ya kisheria katika kikao cha mapatano nayo ni kiasi... (cha fedha). Na hayo yalikamilika tarehe...



Mada ya Nane

‘Shufaa’ na hukumu zake’

1) Maana yake:

Ni mshirika kuchukua hisa ya mshirika mwenzake ambayo ameiuzua, kwa thamani yake aliyoiuzia huyo mshiriki.

2) Hukumu zake ni:

a) Kuthibitika kwake kisheria; *Shufaa* imethibitika kwa hukumu ya Mtume ﷺ kupitia hiyo *shufaa*, Imepokewa katika sahihi kutoka kwa Jaabir bin Abdillah رضي الله عنه kuwa,

“Mtume ﷺ amehukumu kwa *shufaa* kwa kila kinachogawika ikawekwa mipaka, na kuwekwa njia za kupita basi hapana tena *shufaa*.” (Bukhari na Muslim)

b) *Shufaa* haithibitiki ila kwa kitu ambacho kinaweza kugawika, ikiwa hakiwezi kugawika kama vile vijibafu, vijikorido, vijumba vyembamba, hapana *Shufaa* kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Katika kitu kinachokubali kugawika.”

c) Haithibiti *Shufaa* katika kitu kilichokwishagawiwa ambacho kishawekwa mipaka yake na zishawekwa nia zake, kwa kauli yake ﷺ,

“Ikishawekwa mipaka na kuwekwa nia basi hakuna *Shufaa*.”

Kwamba baada ya kugawiwa mshirika anageuka kuwa ni jirani na hakuna *Shufaa* kwa jirani kwa mujibu wa maelezo sahihi.

d) Hakuna *Shufaa* katika vitu vinavyohamishika kama vile nguo, na mnyama. *Shufaa* ni katika vitu vinavyomilikiwa kwa pamoja katika ardhi, navinavyohusiana nayo kama vile jengo, miche, na mimea. Kwani hakuna madhara yanayodhaniwa

Minhajil Muslim

kuwepo kwa kitu kisichokuwa ardhi na kinachoandamana na ardhi ndipo *Shufaa* ikaondolewa kwa vitu vingine.

e) Haki ya mtaka *Shufaa* huanguka (hawi na haki tena) kwa kuhudhuria makubaliano ya kuuza au kujua kwake (kwamba mshirika mwenzake) ameuzwa (hisa yake) naye asitake *Shufaa* mpaka ukapita muda (mrefu) kwa mujibu wa Hadithi,

“*Shufaa ni kwa anayeharakisha kudai.*”

Hadithi nyingine,

“*Shufaa ni kama vile kufunguakamba*” (Ibn Majah),

Isipokuwa asiyekuwepo kwa hakika bado atakuwa na haki ya kudai *Shufaa* japokuwa baada ya miaka mingi.

f) Huanguka *Shufaa* iwapo mnunuzi ataweka *waqfu* au kumpa mtu hiba au sadaka. Kwani kuthibiti *Shufaa* maana yake (ni) kubatilisha hizo ibada za kujikurubisha kwa Allah. Kusahihisha matendo ya kujikurubisha, kwa Allah ni bora zaidi kuliko kuthibitisha haki ya *Shufaa* ambayo haikusudiwi isipokuwa kuondoa madhara yanayodhaniwa kuwepo.

g) Mnunuzi ana haki ya pato na faida inayopambanuka, hivyo basi, kama atajenga au kupanda miche. Basi mdai *Shufaa* anaweza kumiliki hicho kwa thamani yake au kung’oa pamoja na kutoa gharama (ya alichoking’oa) kwani hakuna kujidhulumu wala kumdhulumu mwingine.

h) Jukumu la mtaka *Shufaa* iko juu ya mnunuzi na jukumu la mnunuzi (atamdai) atamrejea muuzaji katika kila linalohusiana na linalowajibishwa na *Shufaa*.

i) Haki ya *Shufaa* haiuzwi wala haitolewi hiba, hivyo yule iliyomuwajibikia *Shufaa* hanaruhusa kuiuza haki yake katika *Shufaa* au kuitoa *hiba* kwa mtu mwingine, kwani kuiuza au kuitoa *hiba* kunapingana na lengo ambalo *Shufaa* imewekwa kisheria nalo ni kuondoa madhara kwa mshirika.



Mada ya Tisa

'Iqala'

'Kuvunja bei'

1) Maana yake:

'*al-Iqaa'* ni kuvunja mauziano na kuiacha na kurudisha thamani kwa mwenyewe na kurudisha bidhaa kwa muuzaji wake iwapo atajuta mmoja wa wauziano wawili au wote wawili.

2) Hukumu yake:

Ni jambo lililopendekezwa kisheria kuvunja bei pindi atapotaka mmoja wa wauziano wawili, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

"Mtu atakayemkubalia Mwenye kujuta kuvunja uzo lake basi Allah atamuondolea dhambi zake." (Abu Dawud na Ibn Majah). Na

"Mtu mwenye kumkubalia kuvunja bei aliyejuta. Allah atamfutia na kumuondolea dhambi zake Siku ya Kiama." (Al Baihaqi)

3) Hukumu Zake Mbalimbali:

Hukumu za Iqala ni:

(a) Wametofautiana wanavyuoni je *al-Iqaala* ni kuvunja bei ile ya kwanza au hiyo ni bei mpya? Imam Ahmad ameenda na (kauli) ya kwanza na maimamu Shaafii Abu Hanifa na Maliki رضى الله عنه wameenda na kauli ya pili.

(b) Inafaa kuvunja mauzo kwa sehemu iliyobaki kitapoangamia baadhi ya kilichouzwa.

(c) Katika *al-Iqaala* haifai kupungua thamani au kuzidi la sivyo, hapana *al-Iqaala*. Na hapo zitajiri bei mpya kwenye hiyo hukumu ya bei kwa ukamilifu wake katika kustahiki *Shufaa* na kushurutisha kukabidhi katika (kuzuza) vyakula na yaliyo kama hayo kama vile matamko ya kuuziana na mengineyo.

Mikataba na Aina Zake

Mada ya Kwanza

‘Ushirika’:

1) Sheria yake:

Ushirika umethibiti kwa neno la Allah aliyetukuka

فَهُمْ شُرَكَاءُ فِي الثُّلُثِ

“Bei hao ni washirika katika thuluthi.” (4: 12) Na

وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْخَالِطَاءِ لَيَبْغِي بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا

الصَّالِحَاتِ

“Na hakika washirika wengi hudhulumiana wao kwa wao, isipo kuwa walio amini na wakatenda mema.” (38: 24)

Anasema Mtume ﷺ kuwa amesema Allah (Subhaanahu wa Taala):

“Mimi ni wa tatu kati wa washirika wawili madamu mmoja hajamkhini mwenzie.”

(Daraqutni na Abu Dawud)

Na anasema,

“Mkono wa Allah uko juu ya washirika wawili madamu hawajafanyiana khiyana.” (Daraqutni)

2) Maana yake:

Ushirika ni kushirikiana wawili au zaidi katika mali waliostahiki kwa kurithi na mfano wake, au wameichangia kati yao ili waiendeleze kwa biashara au ufundi au kilimo na ushirika uko wa aina nyingi.

Aina ya Kwanza:

Ushirika wa ‘Inaan: Ushirika wa ‘Inaan ni ushirikiano kati ya watu wawili na zaidi wanaoruhusiwa kisheria matumizi yao katika kukusanya kiwango maalum cha mali kilichogawanywa kati yao mafungu maalum au hisa maalum iliyotamkwa, ili kwa pamoja waiendeleze, na faida itayopatikana ni yao kulingana na hisa zao katika rasilimali au katika msingi. Pia hasara itakua kulingana na hisa, na kila mmoja wao ana haki ya utendaji katika ushirika katika hisa yake akiwa mwenye mali na hisa ya mwenzake kwa niaba ya kumwakilisha mwenzake. Kwa hiyo basi atauza na kununua hali kadhalika kuipokea na kuitoa, atadai deni na kufungua madai, na atarejesha kama kuna kasoro, kwa kifupi ni kuwa: Atafanya kila kilichokuwa na maslahi kwa ushirika huo.

Ili ushirika huu ukubalike kuna masharti yafuatayo:

a) **Ushirika uwe kati ya Waislamu,** kwa sababu upo uwezekano kwa asiye kuwa Muislamu kuingiza *Riba* katika ushirika au akaingiza mali ya haramu. Isipokuwa pale ambapo kuuza na kununua kutakapokuwa mkononi mwa Muislamu, kwa sura hiyo hakuna pingamizi, kwa vile hakuna hofu ya kuingiza mali ya haramu katika ushirika.

b) **Rasilimali iwe kwa msingi unaoeleweka,** na hisa ya kila mmoja kati ya wana ushirika ijulikane kwa sababu faida na hasara zinategemea kueleweka kwa msingi na hisa katika ushirika. Kutojulikana msingi au hisa za washirika kunawafikisha watu kula mali za wegine kwa batili na kufanya hivyo ni haramu kwa neno lake Allah Aliyetukuka:

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ وَتُدْخُلُوا بِهَا إِلَى الْحُكَّامِ لِيَأْكُلُوا
فَرِيقًا مِّنْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٨٨﴾

“Wala msiliane mali zenu kwa baat’ili na kuzipeleka kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu kwa dhambi, na hali mnajua.” (2: 188)

c) **Faida ienee igawanywe kulingana na hisa na si sahihi kusema:** Faida tulioipata katika kondoo ni ya fulani, na tulioipata –kwa mfano katika katani ni ya fulani kwa sababu ya kutojulikana hayo na kufanya hivyo ni haramu.

d) **Rasilimali ni lazima iwe sarafu,** na aliyekuwa na bidhaa naye akataka kujiunga na ushirika atatakiwa aithamini bidhaa kwa thamani ya siku hiyo na ataingia katika ushirika, kwa sababu bidhaa zisizojulikana thamani yake na ushirika usiojulikana hauruhusiwi kisheria, kwa sababu ya hilo linalopelekea kupoteza haki au kula mali za watu kwa batili.

e) **Na utendaji uwe kulingana na hisa kama faida na khasara,** kwa hiyo aliye na hisa katika ushirika robo kwa mfano atalazimika katika siku nne afanye kazi siku moja n.k. . . Na kama watamuajiri mfanyakazi, mshahara wake utatoka kwenye rasilimali kulingana na hisa za washirika.

f) Endapo mmoja wa washirika wawili atafariki basi na ushirika utakuwa umekoma, pia kama kwa mfano atapatwa na ugonjwa wa akili, warithi wa marehemu au ndugu wa mwendawazimu wana haki ya kuufumua ushirika au kuziendeleza. Kwa mkataba wake wa kwanza.

Aina ya Pili:

‘Ushirika wa Viwiliwili’: Nayo ni kushiriki watu wawili na zaidi katika kile wanachokipata kwa kutumia nguvu za miili yao, kama vile wameshirikiana na kutengeneza kitu fulani, au kushona au kuosha nguo na mfano huo, na wanachokipata kwa kazi hiyo wagawane kati yao nusu kwa nusu au kulingana na wanavyokubaliana.

Hoja ya kuruhusiwa aina hii ya ushirika ni Hadithi aliyopokea Abu Dawud kuwa Abdallah, Sa’ad na Ammar siku ya Badri walishirikiana katika mali za kushirikiana, Abdallah na ‘Ammar hawakupata kitu Saad akapata mateka wawili, Mtume ﷺ akawashirikisha pamoja katika mateka wale, na hayo yalikuwa kabla ya sheria ya kugawa ngawira.

Hukumu za Ushirika huu ni:

- a) Kila mmoja wao anaruhusiwa kuchukua malipo kutoka kwa aliyewaajiri.
- b) Mmoja wao kama ataumwa, au hakufika kazini kwa udhuru atakachokipata mmoja wao watashirikiana.
- c) Kama kitarefuka kipidi cha kutokuhudhuria kwa mmoja wao au muda wa kuumwa kwake umerefuka yule mzima anaruhusiwa kumuweka mtu mwingine katika nafasi ya mgonjwa na malipo yake ni yale ya yule mgonjwa au asiyekuwepo.
- d) Ikishindikana kufika kabisa yule mmojawao, yule mwingine anaruhusiwa kuufuta ushirika.

Aina ya Tatu:

Wa Hadhi': Ushirika wa hadhi ni kushirikiana wawili au zaidi katika kununua bidhaa kwa hadhi zao na wanaiuza, na faida wapatayo wagawane kati yao, na kama kutatokea hasara itawalazimu wote kuichukua sawasawa kama faida.

Ainaya Nne:

'Ushirika wa Mufawadhwa: Na ushirika huu ni mpana kuliko *inaan* au *miili* na *hadhi* kwa sababu hizo aina nyingine zinaingia humo. Na unaigia pia ushirika wa *Mudhwarab*, nao ni kila mshirika anamuegemezea mwenzake utendaji wa kifedha na kimwili katika aina za ushirika, kwa hiyo anauza, ananunua, anafanya *Mudhwaraba*, anawakilisha, anafungua madai, na anaweka rehani, na anasafiri na mali, na faida watagawana kulingana na walivyokubaliana, na hasara itakuwa kulingana na hisa ya kifedha ya kila mmoja.



Mada ya Pili

‘Mudhwaraba’:

1) Maana yake:

‘Mudharaba’ au *Qiradh* ni mtu mmoja kumpa mwingine mali maalum afanyie biashara, na wagawane faida kama watakavyokubaliana, na hasara kama itatokea itakuwa kwenye msingi tu. Kwa sababu mfanyakazi kwake, nguvu zake na juhudi zake ndiyo hasara yake tosha hakulazimishwa hasara nyingine tena. Kwanini alazimishwe hasara nyingine?

2) Sheria yake:

‘Mudhwaraba’ upo kisheria kwa makubaliano ya Masahaba na Maimamu, na imefanyika wakati wa Mtume ﷺ naye akaikubali.

3) Hukumu Zake:

Hukumu za ‘Mudhwaraba’ ni:

- a) Iwe kati ya Waislamu wanaoruhusiwa kisheria matumizi ya mali, na si vibaya kuwa kati ya muislamu na kafiri kama msingi au hiyo rasilimali itakuwa ni ya huyo kafiri, na utendaji kwa Muislamu kwa sababu Muislamu hahofiwi *Riba*, wala mali ya haramu.
- b) Msingi ujulikane.
- c) Fungu la mfanyakazi na faida yake iainishwe na kama halijaainishwa basi atapewa ujira wa kazi yake tu, na faida yote itakuwa ya mwenye msingi ama kama walisema faida tugawe basi watagawana faida mafungu mawili kila mmoja fungu moja (nusu) ya faida.
- d) Na kama watatofautiana katika fungu ulilokubaliana lilikuwa robo au nusu kwa mfano, itakubaliwa kauli ya mwenye mali pamoja na kuapa.

e) Haruhusiwi mfanyakazi kufanya *Mudhwaraba* katika mali ya mtu mwingine kama utasababisha madhara kwa mtu wa kwanza, isipokuwa kama ataruhusu yule wa kwanza, kwa ajili ya kuharamishwa madhara baina ya Waislamu.

f) Wakati mkataba wa ushirika unaendelea faida haigawanywi, isipokuwa kwa ridhaa ya pande mbili na wakakubaliana.

g) Rasilimali siku zote litazibwa kwa faida, mfanyakazi hana haki yoyote kwenye faida isipokuwa baada ya kuliziba pengo lililo kwenye msingi na hii ni ikiwa faida bado haijagawanywa. Kamawalifanya biashara ya mbuzi, na kila mmoja akachukua hisa yake katika faida, halafu wakafanya biashara ya nafaka kwa mfano au katani wakapata hasara katika msingi, basi hasara hiyo itakuwa katika msingi wala halazimiki mfanyakazi kuziba pengo hilo kutoka kwenye faida yake aliyoipata hapo mwanzo.

h) Endapo ushirika utakufa na kuna baadhi ya mali imesalia ikiwa ni bidhaa au deni liko kwa mtu fulani na mwenye mali akataka hiyo bidhaa iuzwe ili ziwe fedha taslimu au ametaka hilo deni lirejeshwe basi mfanyakazi ana lazimika kufanya hivyo.

i) Itakubaliwa kauli ya mfanyakazi katika dai lake la kuteketea mali au kupata hasara kwa muda wa kuwa hakuna ushahidi unaothibitisha kinyume na madai yake. Kama atadai kuteketea mali na akatoa ushahidi unaothibitisha madai yake atatakiwa aape na madai yake yatakubaliwa.



Mada ya Tatu

Kumwagilia na Kulimisha

‘Kumwagilia’

1) Maana yake:

Kumwagilia ni kumpa mtu mtende au mti au mtende na mti aumwagilie maji na huduma nyingine zinazohitajika katika kustawisha kwa kupata yule mhudumu fungu maalumu kutoka kwenye matunda yake, kutoka katika jumla ya yote.

2) Hukumu yake:

Kumwagilia kunaruhusiwa kisheria na hoja ya kuruhusiwa kwake ni tendo lake Mtume ﷺ na tendo la makhalifa wake waongofu baada yake. Amepokea Bukhari kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ alishirikiana na watu wa *Khaibar*) kwa nusu ya mavuno (Kutoka katika ardhi ya *Khaibar*) katika nafaka na matunda, kama walivyoundeleza Ushirika huu baada yake: Abubakar, Umar, na ‘Uthman, pia Ally, Radhi za Allah ziwashukie.

3) Hukumu zake

Sheria za umwagiliaji ni:

a) Mtende, au mti ueleweke wakati wa mkataba. Mkataba wa kumwagilia mti usioeleweka hautambuliwi; hii ni kuhofia udanganyifu ambao ni haramu.

b) Mgao wa mfanyakazi ueleweke kwa mfano: Robo, au Khumsi ya mavuno, na liene katika mitende, au miti yote, kwa sababu kama litakuwa kwenye mitende tu au miti tu, inaweza izea na ndani yake kuna udanganyifu unaoharamishwa marufuku na Uislamu.

c) Mfanyakazi analazimika kulifanya kila lenye maslahi kwa mtende au mti ambao ni kawaida kulifanya katika kumwagilia.

- d) Kama ardhi inayotumiwa kumwagilia inalipiwa, basi malipo hayo atayatoa muajiri si mfanyakazi, kwasababu malipo ya ardhi ni sehemu ya msingi, kwa sababu malipo ya ardhi yanatolewa hata kabla ya kupandikiza miche au kupanda mbegu. Ama Zaka, inamlazimu mwenye gawio lililofikia kiwango katika matunda, awe mfanyakazi au mwajiri, kwa sababu Zaka inahusiana na matunda yenyewe.
- e) Inakubalika kumwagilia mashina tu, kwa mfano, Mtu kampa mtu mwingine ardhi ili apandikize mitende, au miti, aimwagilie na kuihudumia mpaka itakapotoa matunda, na gawio lake liwe, kwa mfano, robo ya mavuno, au theluthi kwa sharti muda ukomee msimu wa matunda yake, na mfanyakazi achukue gawio lake katika ardhi na miti.
- f) Kama Mfanyakazi mwenyewe atashindwa kazi, anatakiwa amlete mwingine badala yake, na atapata matunda yaliyokubaliwa katika mkataba.
- g) Kama mfanyakazi atakimbia kabla mazao hayajapevuka, mwajiri ana haki ya kubatilisha mkataba na kama amekimbia baada ya kupevuka, mwajiri atamuweka atayekamilisha kazi kwa malipo kutoka kwenye gawio la mfanyakazi aliyekimbia.
- h) Kama mfanyakazi atafariki warithi, wanatakiwa walete mtu atayekuwa badala ya marehemu, na kama pande mbili zitakubaliana kubatilisha Mkataba basi utabatilishwa.



‘Kulimisha’:

1) Maana yake:

Kulimisha ni mtu kumtoa ardhi kumpa mwingine ailime kwa gawio maalumu lenye kuenea katika pato lote.

2) Hukumu yake:

Jamhuri ya Masahaba, Taabiina na Maimamu wamekubali kulimisha na wengine wamezuia. Hoja ya wenye kuridhia ni tendo la Mtume ﷺ kuchukua kutoka kwa watu wa *Khaibar* nusu ya mavuno kutoka kwenye nafaka na matunda.

Ampokea Bukhari kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ aliwapa watu wa *Khaibar* nusu ya mavuno kutoka kwenye nafaka na matunda akawa anawapa washirika wake *wasqi* mia moja (tende *wasqi* thamanini na *wasqi* ishirini za shairi). Katazo lililokuja katika kulimisha wamelichukulia ima lilikuwa kwa kitu kisichofahamika, na hoja yao ni Hadithi ya Raafii Ibn Khadij رضي الله عنه aliposema:

“Tulikuwa wakubwa wa Answare kwa kilimo tukawa tunakodisha ardhi kwa Sharti gawio letu liwe hili na lao hili, na huenda mara nyingine likitoe mazao hili na lile lisitoe katukataza hayo,” (Bukhari na Muslim).

Au wameichukulia kuwa ni makruhu ya tahadhari kwa hoja kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنه: Mtume ﷺ hakukataza hilo, lakini amesema,

“Kumpa mtu ndugu yake akalima bure ni bora kuliko kuchukua mapato Maalumu.” (Bukhari)

3) Hukumu zake:

Sheria za kulimisha ni:

a) Muda ujulikane na uwe na ukomo kwa mfano mwaka mmoja.

b) Na fungu la walilokubaliana lieleweke kiwango chake kama vile nusu au thuluthi, au robo na ienee katika mapato yote yatokayo katika ardhi hiyo, kama ilisemwa: “Wewe utapata kitachoota mahala kadhaa”, haitosihii.

c) Mbegu itoke kwa mwenye shamba, na kama itatoka kwa mfanyakazi basi huo utaitwa *Mukhaabara*, na tofauti yake katika kukubalika kwake ni kubwa sana kati ya wanazuoni ukilinganisha tofauti zilizopo katika *muzara'h* (kulimisha), kwa neno la Jabir رضي الله عنه.

“Mtume ﷺ amekataza *Mukhaabara*” (Ahmad)

d) Kama mmiliki wa ardhi ataweka sharti kuwa kwanza achukue mbegu yake kutoka kwenye mavuno yatakayopatikana kitachobakia ndicho watakachogawana yeye na mfanyakazi kulingana na walivyokubaliana basi kulimisha huko si sahihi.

e) Kukodisha ardhi kwa fedha taslimu ni bora kuliko kulimisha, kwa neno la Raafi Ibni Khadij رضي الله عنه.

“...Ama kwa dhahabu au fedha hakutukataza.”

f) Ni suna kwa mwenye ardhi ya ziada katika mahitaji yake ampe ndugu yake Muislamu bila malipo, kwa neno lake Mtume ﷺ.

“Mwenye kuwa na ardhi ailime au ampe ndugu yake bure.”
(Bukhari na Muslim)

Na neno lake Mtume ﷺ.

“Kumpa ndugu yake bure ni bora kwake kuliko kuchukua malipo maalumu.”

g) Jamhuri wamezuia kukodisha ardhi kwa malipo ya chakula, kwani kufanya hivyo kuna maana ya kuuza chakula kwa chakula kwa muda na ziada na kufanya hivyo kumezuiliwa. Ama kilichopokewa kutoka kwa Ahmad kuwa inaruhusiwa kulimisha si kukodisha ardhi kwa chakula.



Mada ya Nne

'Kukodisha'

1) Maana yake:

Kukodisha ni Mkataba wa lazima juu ya manufaa kwa muda maalumu kwa thamani maalumu.

2) Hukumu yake:

Kukodisha kunakubalika, kwa neno lake Allah Aliyetukuka,

قَالَ لَوْ شِئْتَ لَتَّخَذْتَ عَلَيْهِ أَجْرًا ﴿٧٧﴾

“...Ungeli taka ungesi chukua ujira kwa haya.” (18:77).

Na

إِنَّ خَيْرَ مَنْ آسْتَجَرْتَ الْقَوِيُّ الْأَمِينُ ﴿٢٦﴾

“...Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu.” (28: 26)

Na

عَلَىٰ أَنْ تَأْجُرَنِي ثَمَنِي حِجَجٍ ۗ

“...kwa kunitumikia miaka minane...” (28: 27)

Katika neno la Mtume ﷺ

“Allah Aliyeshinda na Kutukuka Amesema: “Watatu mimi ni hasimu wao siku ya Kiyama, mtu aliyetoa kwa ajili yangu kisha asitimize, na mtu aliemuza muungwana akala thamani yake,

na mtu aliyemuajiri mfanyakazi na akaifanya kwa ukamilifu kisha hakumkamilisha malipo yake.” (Bukhari)

Mtume ﷺ na Abubakar walimkodi mtu, siku waliyohama, muongozaji njia hodari katika Bani Dayl awaongoze njia ya kwenda Madina.

3) Masharti yake:

- a) Kujua manufaa yake kama vile kuishi katika nyumba, au kwa mfano kushona nguo, kwani haya ni kama biashara, na biashara lazima kinachouzwa kieleweke.
- b) Uhalali wa matumizi. Asikodishwe mjakazi kwa ajili ya kuingiliwa au mwanamke kwa kuimba, au kulia katika msiba mathalani, au isikodishwe ardhi ili lijengwe kanisa au kiwanda cha pombe au baa.

Kueleweka malipo kwa neno la Abu Saidi,

“Mtume ﷺ amekataza kumkodisha mfanyakazi mpaka aelezwe malipo yake.” (Ahmad).

4) Hukumu zake:

- a) Inaruhusiwa kumkodisha mwalimu kufundisha elimu au ufundi, kwa Mtume ﷺ kukubali fidia ya baadhi ya mateka wa Badri kufundisha idadi fulani ya watoto wa Madina kuandika.
- b) Inaruhusiwa kumkodisha mtu kwa malipo ya kula na kuvaa, kwa kauli yake Mtume ﷺ alipoisoma sura Twaa Siin Miim mpaka alipofikia kisa cha Musa.

“Musa amejajiri mwenyewe miaka minane au kumi kwa malipo ya kuihifadhi tupu yake na chakula cha tumbo lake.” (Ahmad).

- c) Ni sahihi kukodi nyumba maalumu inayodhaniwa kuwa itaishi mpaka muda wa kukodi.

d) Kama atamkodisha kitu uliozuiwa kukitumia kwa muda, na malipo yatapomoka kulingana na muda huo uliozuiwa. Kama mwenye kukodi ameacha kutumia yeye mwenyewe tu atalazimika kutoa malipo yote kamili.

e) Kukodisha kutakoma kwa kuharibika kilichokodiwa kama vile kuanguka nyumba au kufa mnyama, na mwenye kukodi analazimika kulipa muda ambao ametumia hicho kilichokodiwa.

f) Aliyekodi kitu akakuta kina kasoro ana haki ya kuvunja Mkataba, iwapo kabla ya kukodi hakuelewa kuwa hicho kina kasoro hiyo na akairidhia. Kama alikitumia alichokikodi kwa muda atalipia muda alioutumia.

g) Mkodiwa wa ushirika kama vile fundi cherehani na mhunzi atalipa chombo alichokiharibu kwa tendo lake, si kilichopotea kiwandani kwake, kwani hicho kinakuwa kama amana anayoitunza, na amana hazilipwi madamu muhusika hakuzembea. Muajiriwa binafsi, kama vile aliyemwajiri mtu fulani amtumikie yeye tu, alichokiharibu hakilipi madamu haukuthibitika uzembe wake katika hilo au kuruka mpaka.

h) Malipo yatathibitika kwa kukamilika Mkataba, na itakuwa lazima kuyatoa baada ya matumizi au kukamilika kazi, isipokuwa kama kuna sharti la kutoa malipo katika mkataba kwa hadithi ya Mtume ﷺ

“Lakini muajiriwa atapewa malipo yake anapomaliza kazi yake.” (Ahmad)

i) Mfanyakazi ana haki ya kuzuia kitu mpaka apate malipo yake kamili kwa kazi yake. Kama ina athari katika macho yake kama vile fundi cherehani, au kama ina taathira kwa aliekodiwa kubebea bidhaa kuipeleka mahala fulani hana haki ya kuzuia bidhaa hiyo bali ataifikisha alipotakiwa kisha atadai malipo yake.

j) Atakayemtibu mgonjwa kwa malipo na akawa hajui kutibu akaharibu kitu au kiungo analazimika kulipa au kutolea dhamana kwa neno lake Mtume ﷺ

“Mwenye kutibu na tiba kwake haifahamiki hakufahamu tiba basi tabibu atalipa.” (Imepokewa na Abu Dawud, Hakim, Daaqutni)



Mada ya Tano

‘Zawadi’:

1) Maana yake:

Zawadi ni kitu anachopewa mtu kwa jambo alilolifanya, na katika sheria mtu anaruhusiwa kutumia kiasi maalum cha mali ya mtu aliyemfanyia kazi maalumu inayojulikana, kwa mfano anasema: “Atakayenijengea ukuta huu, atapata Kiasi kadhaa cha mali”, hivyo basi akitokea mtu akamjengea ukuta huo atastahiki zawadi aliyoiweka iwe chache au nyingi.

2) Hukumu yake:

Zawadi inakubaliwa kwa neno lake Allah (s.w) aliyetukuka,

وَلَمَنْ جَاءَ بِهِ جَمَلٌ بَعِيرٌ وَأَنَا بِهِ زَعِيمٌ ﴿٧٢﴾

“...Na ataye lileta atapewa shehena nzima ya ngamia. Nami ni dhaamini wa hayo.” (12: 72).

Neno lake Mtume ﷺ kwa wale walioweka zawadi kwa atakayemtibu aliyeng’ atwa na ng’e katika kundi la mbuzi.

“Chukueni na mnipe katika hisa hiyo.” (Bukhari).

3) Hukumu zake: Sheria za zawadi ni:

a) Zawadi ni Mkataba unaokubalika, na kila mmoja kati ya pande mbili ana haki ya kusitisha Mkataba, na kama kusitisha litakuwa kablaya kazi hakuna malipo kwa mfanyakazi, na kama ni katikati ya kazi mfanyakazi atapewa zawadi kulingana na kazi aliyofanya.

b) Si lazima katika Mkataba huu kujulika na muda wa kazi, na mtu akisema, ‘Atakayenirejeshea mnyama wangu aliyepotea au aliyekimbia atapata Dinari’, atastahiki Dinari atakayemrejesha hata kama baada ya mwezi au mwaka.

c) Kama kazi itatekelezwa na kundi la watu, watastahiki zawadi kwa pamoja na watagawana sawa sawa.

d) Haitakubaliwa zawadi katika kazi ya haramu. Kwa hiyo haikubaliwi mtu kusema, “Atakayeenimbia au kunipigia zumari au atakayempiga fulani au kumtukana atapata kitu kadhaa.”

e) Atakayerejesha kilichookotwa au kupotea au akafanya kazi kabla hajajua kama kuna zawadi hana haki ya zawadi hiyo. Kwa sababu tokea mwanzo kazi yake ilikuwa ya kujitolea, kwa hiyo hana haki katika zawadi isipokuwa katika kumrejsha mtumwa aliyekimbia ‘asi, au kumuokoa anayezama maji, huyo atapewa kwa ajili ya motisha kwa kazi yake.

f) Kama atasema, ‘Atakayekula kitu kadhaa au kunywa cha halali atapata zawadi kadhaa’, zawadi hiyo itakuwa sahihi. Isipokuwa kama atakayesema, ‘Atakayekula kitu kadhaa na atakayebakisha kwenye kitu hicho kitu kadhaa atapata kitu kadhaa’, haitakubaliwa.

g) Kama watatofautiana mmiliki na mfanyakazi katika kiwango cha zawadi, itayokubaliwa ni kauli ya mmiliki pamoja na kiapo chake. Na watakapotofuatiana katika asili ya zawadi, itakayokubaliwa ni kauli ya mfanyakazi pamoja na kula yamini.



Mada ya Sita

'Hawala'

1) Maana yake:

'Hawala' ni kuhamisha na kuhawilisha deni kutoka kwenye dhamana ya mtu na kuipeleka kwenye dhamana ya mwingine. Kama vile mtu fulani anadaiwa, naye anamdai mtu mwingine deni sawa na analodaiwa, na mwenye deni lake anamdai, nae akamwambia nimekuhawilisha, yaani kukuhamisha uende kuchukua deni lako kwa fulani, kwani yeye namdai deni kama lako kachukue huko. Mhamishiwa kama ataridhika tokea hapo mhamishaji hana deni tena.

2) Hukumu yake:

'Hawala' inakubaliwa, isipokuwa mhamishwaji kama atahamishiwa kwa mwenye uwezo anatakiwa akubali kwa neno lake  tume

“Kucheleweshwa kulipa deni kwa mwenye uwezo ni dhulma na anapohamishiwa mmoja wenu kwa mwenye uwezo akubali kuhamishwa.” (Bukhari na Muslim)

Na

“Tajiri kucheleweshwa kulipa deni ni dhuluma, na Ukihamishiwa kwa mwenye uwezo kubali.” (As-habu Ssunan)

3) Masharti yake:

Mashati ya 'Hawala' ni:

a) Deni la anayehamishiwa liwe tayari limethibitika katika dhamana ya anayehamishiwa.

b) Wote wawili mhamishaji na mhamishwaji waridhike, kwa sababu mhamishaji ingawa anadaiwa lakini halazimiki deni hilo kulilipa kwa njia ya hawala bali ana

hiyari namna ya kulipa deni hili. Na anayehamishwa ingawa Muweka sheria amemtaka akubali kuhamishwa lakini halazimishwi bali ni hisani tu, kwa sababu hawala si Mkataba wa lazima, bali ni Mkataba uliokusudiwa huruma kati ya Waislamu.

4) Hukumu zake:

a) Anayehamishiwa awe na uwezo wa kulipa kwa neno la Mtume ﷺ,

“Kama atahamishiwa mmoja wenu kwa mwenye uwezo.”

b) Kama atahamishiwa kwa mtu akaja akagundua kuwa amefilisika, amefariki, au ameondoka mbali, atarudi kudai deni lake kwa muhamishaji.

Kama mtu atahamisha anayemdai kwa mwingine, unakubalika uhamisho huo kwa sababu hakuna madhara katika kukaririka uhamisho, madamu masharti yamekamilika.



Mada ya Saba

'Dhamana', 'Kafala', 'Rahani',

'Akala', na 'Suluhu

Dhamana:

1) Maana yake:

Dhamana ni kubebesha haki juu ya anayetakiwa kama vile mtu fulani anadaiwa mwenye deni akamtaka, mtu mwingine akasema anayeruhusiwa kutumia mali: Haki hiyo iko juu yangu nami ninaichukua dhamana hiyo, kwa kusema hivyo tayari amekuwa mdhamini, na mwenye deni anayo haki ya kumdai mdeni wake, na asipolipa atamdai mdhamini.

2) Hukumu yake:

Dhamana inakubalia kwa Neno la Allah aliyetukuka,

وَأَنَا بِرِزْعِي

“...Nami ni dhaamini wa hayo.”(12: 72)

Na neno la Mtume ﷺ

“Mdhamini atalipia.” (Abu Dawud na Tirmidhi).

Na

“Isipokuwa kama atasimama mmoja wenu akamdhamini.”
(Bukhari)

Malezo hayo yalikuwa yanamhusu mtu aliyefariki akiwa na deni na hakuacha cha kulipia. Mtume ﷺ akakataa kumswalia.

3) Hukumu zake:

Sheria za dhamana ni:

-Katika *dhamana* inazingatiwa ridhaa ya mdhamini, ama ridhaa ya mdhaminiwa haizingatiwi.

-Mdhaminiwa hatoepuka dhima mpaka pale dhimma ya mdhaminiwa itaposafika, na endapo dhimma ya mdhaminiwa itakuwa huru basi na mdhamini naye atakuwa huru.

-Si lazima katika dhamana kumjua mdhaminiwa, kwani inafaa mtu kumdamini asiyemjua kabisa, kwa sababu dhamana ni kujitolea na hisani.

-Hakuna dhamana isipokuwa katika haki tayari ilihibitika katika dhima au kitu ambacho hatimaye kitathibitika kama vile zawadi.

-Si vibaya wadhamini kuwa wengi pia si vibaya mdhamini naye akadhaminiwa na mwingine.

Namna ya kuandika *Dhamana*:

Baaada ya *Bismillahi* , na *Alhamdulillah*:

Jina la mdhamini, mdhaminiwa na mashahidi:

Amefika kwa mashahidi wake siku ya tarehe kadhaa...na akawathibitisha mashahidi wake kuwa yeye amedhamini dhimma ya fulani...kiwango chake ni kadhaa...taslimu au kwa awamu, au mpaka tarehe kadha... dhamana ya kisheria katika dhimma yake na mali yake, na amekubali kuwa ana uwezo wakutekeleza hayo, na maana ya dhamana anaijua, na kinacholazimika kisheria, na mdhaminiwa amekubali dhamana yake, na hayo ni tarehe kadha...



‘Kafala’

1) Maana yake:

‘Kafala’ ni kujilazimisha anayeruhusiwa kutumia mali kulipa haki iliyothibiti juu ya mtu fulani au kujilazimisha kumleta mbele ya mahakama.

2) Hukumu yake:

‘Kafala’ inakubaliwa kwa kauli yake Allah (*Subhanahu wa Taala*) Aliyetukuka:

قَالَ لَنْ أَرْسِلَهُ مَعَكُمْ حَتَّى تُؤْتُونِ مَوْثِقًا مِنْ اللَّهِ لَتَأْتُنِي بِهِ إِلَّا
أَنْ يُحَاطَ بِكُمْ

“Akasema: Sitampeleka nanyi mpaka mnipe ahadi kwa Mwenyezi Mungu kwamba lazima mtamrejeza kwangu, ila ikiwa mmezungukwa...” (12:66)

Na neno lake Mtume ﷺ

“Hakuna dhamana katika adhabu (*Haddi*).” (*al Baihaqi*).

Na neno lake Mtume ﷺ

“Mdamini atalipia.”

3) Hukumu zake: Hukumu za *Kafala* ni:

-Inashurutishwa kufahamika yule anayedhaminiwa ajulikane, na hasa zaidi dhamana ya kumleta (anapohitajika kisheria).

-Katika *kafala* aridhike mdhaminiwa.

-Kama mtu atamdhamini dhamana ya mali akafa mdhaminiwa atadhamini mali, na kama atadhamini dhamana ya hadhi na kuleta akafa mdhaminiwa hadaiwi.

-Mdhamini anapomleta mdhamaniwa mbele ya mahakama hana tena dhimma.

-Dhamana hairuhusiwi isipokuwa katika haki ambayo inakubali niaba miongoni mwa yanayohusiana na dhimma kama vile mali. Ama yasiyokubali niaba kama vile adhabu, na kisasi hakuna dhamana, kwa neno la Mtume ﷺ

“*Hakuna dhamana katika adhabu.*” (al Baihaqi).

‘Rahani’:

1) Maana yake:

Ni uthibitisho wa deni kwa kitu kinachoweza kulipa deni hilo, au thamani yake, kama vile mtu amekopa na akatakiwa aweke kitu kama vile mnyama, au shamba au visivyo hivyo ili iwe dhamana ya deni lake. Tarehe ya kulipa deni inapofika na ikawa haikulipwa, atalipa kwa kile kilicho dhamana, Mdeni anaitwa *Murtahin* (mwekewa Rahani) na mdaiwa anaitwa *Raahin* (mweka Rahani). Na kilichowekwa rahani kinaitwa Rahani.

2) Hukumu yake:

Rahani inakubaliwa kwa neno lake Aliyetukuka,

﴿ وَإِنْ كُنْتُمْ عَلَىٰ سَفَرٍ وَلَمْ تَجِدُوا كَاتِبًا فَرِهْنَ مَقْبُوضَةً ۗ ﴾

“*Na mkiwa safarini na hamkupata mwandishi, yatosha kukabidhiwa rahani...*” (2:283)

Na kwa neno lake Mtume ﷺ

“*Haifungwi rahani kwa mwenyewe ambaye amemuwekea rahani kilicho chake Ni mapato yake na jukumu lake ni gharama yake.*” (Shaafii na Daraqutni).

Na neno la Anas رضي الله عنه

“Mtume ﷺ ameweka rahani deraya (mavazi ya kivita) kwa Yahudi ndani ya Madina na akachukua kutoka kwa Yahudi huyo shairi kwa ajili ya watoto wake.” (Bukhari).

3) Hukumu zake:

Hukumu za *Rahani* ni:

- i) ‘*Rahani*’ itathibitika kwa *Murtahin* kukabidhi rahani na si muwekewa rahani (*Rahiin*). Muweka rahani kama atataka kukirejesha hicho alichokiweka rahani atakuwa hana haki. Ama muwekewa rahani anayo haki ya kukirejesha.
- ii) Kitu kisichofaa kuuzwa miongoni mwa vitu hakifai kuwekwa rahani, isipokuwa mimea na matunda kabla hayajapevuka, akiyaweke rahani ni haramu kuyauza, hata kama yataharibika matunda au mazao.
- iii) Na muda wa rahani unapofika, muwekewa rahani ana haki ya kutaka kulipwa deni lake kama muweka rahani atalipa deni basi muwekewa rahani atarejesha *rahani*, na asipolipa atachukuwa deni lake kutoka kwenye rahani aliyonayo kutoka kwenye pato la rahani kama lipo, na kama hakuna atauza rahani na atachukua haki yake. Na kitachozidi atamrejeshea mwenyewe, na kama rahani imeshindwa kulipa deni lote basi kilichosalia kitakuwa katika dhimma ya mdaiwa muweka rahani.
- iv) *Rahani* ni amana mikononi mwa muwekewa rahani kama itaharibika kwa uzembe wake au kwa maksudi atalipa, la si hivyo halipi na deni lake litabakia kwa muweka *Rahani*.
- v) *Rahani* Inafaa kuwekwa katika mikono ya mtu muaminifu asiye muwekewa *Rahani*, (mtu wa tatu kati yao) kwa sababu kinachozingatiwa udhamini huo utapatikana kwa mtu muaminifu.
- vi) Kama muweka rahani ataweka sharti ya kutouza rahani tarehe inapofika hiyo rahani ni batili. Pia muwekewa rahani kama ataweka sharti tarehe zikifika akawa hakulipwa rahani isiuzwe bali achukuwe yeye itakuwa rahani hiyo ni batili kwa neno lake Mtume ﷺ

“Rahani haifungwi, rahani ni ya muweka rahani, Pato ni lake yeye, ni juu yake gharama yake.” (Bukhari).

vii) Wanapotofautiana muweka na muwekewa rahani katika kima cha deni itatangulizwa kauli ya muweka rahani pamoja na kuapa, isipokuwa kama muwekewa rahani ataleta ushahidi, na kama watakhitalafiana katika rahani muweka rahani akasema, “Nimekuwekea rahani mnyama na mwanawe”, na muwekewa rahani akasema, “Bali ni mnyama tu”, itatangulizwa kauli ya muweka rahani isipokua kama muweka rahani ataleta ushahidi unaothibitisha dai lake kwa neno lake Mtume ﷺ

“Ushahidi uko juu ya mlalamikaji na yamini ni juu ya anayepinga.”
(al Baihaqi)

vii) Iwapo Muwekewa rahani atadai amerejesha rahani na muweka rahani akakataa itatangulizwa kauli ya muweka rahani pamoja na yamini, isipokuwa kama muwekewa rahani ataleta ushahidi unaothibitisha hilo.

ix) Anaruhusiwa muwekewa *rahani* kupanda rahani. Au kukamua maziwa kwa kadri ya matumizi anayoyatoa katika rahani hiyo, lakini analazimika kuwa muadilifu. Asije akatumia zaidi ya anavyogharimu kwa neno lake Mtume ﷺ

“Mnyama anapandwa kwa matumizi yake kama amewekwa rahani, na maziwa yatanywewa kwa matumizi yake kama amewekwa rahani, na anayepanda na kukama atoe matumizi.”
(Abu Dawud na Ibn Majah).

x) Matunda ya *rahani* kama kodi, watoto na mfano wake ni miliki ya muweka rahani, na yeye ndiye anayelazimika kumwagilia, na yote yanayohitajika ili kilichowekwa rahani kiendeleo kuishi, kwa neno lake Mtume ﷺ

“Rahani ni ya mwenye kuiweka, yeye ndiye mwenye mapato yake, na yeye ndiye anayelazimika kugharimia.”

xi) Muwekewa Rahani kama atatoa gharama juu ya mnyama wa rahani bila ya ruhusa ya muweka rahani hana haki ya kumtaka muweka rahani amrejeshee gharama zake, na kama itashindikana kumtaka ruhusa labda kama yupo mbali,

anaweza kumtaka kama atatoa alichotoa kwa nia ya kurejeshewa, kwa sababu aliyejitolea harejeshewi.

xii) Kama rahani itaharibika, kwa mfano ilikuwa nyumba kisha muwekewa rahani kaifanyia matengenezo bila ya ruhusa ya muweka rahani hana haki ya kumtaka muweka rahani amlipe, isipokua chombo kama vile mti au jiwe kwa sababu ni vigumu kuitoa, hivyo anaweza kumtaka muweka rahani amlipe.

xiii) Kama atakufa muweka rahani au kufilisika, basi muwekewa rahani ndiye mwenye haki zaidi kwa kile kilichowekwa rahani kuliko wadeni wengine, tarehe ikifikika atakiuza na atachukua deni lake, na kilichozidi atakirejea, na kisipolipa deni lote basi atakuwa pamoja na wadai wengine katika hicho kilichosalia.

4) Sura ya mkataba wa *Rahani*

Baada ya *Bismillaahi na Alhamdulillah*:

Fulani amekubali... Kuwa anadaiwa deni Kiasi kadha... na fulani, na muda wa deni hili ni mwezi au mwaka kadha... Na ili kupata uthibitisho ameweka rahani mtajwa aliyekiri chini ya mwenye kudai aliyetajwa, ili kupata utibitisho wa deni lililotajwa hapo juu. Kilichotajwa kuwa ni chake na kwa mkono wake na miliki yake mpaka hapo tarehe inapofika. Rahani yenyewe ni nyumba yote ya fulani, au kitu fulani chote... Rahani sahihi ya kisheria imekabidhiwa na imepokewa iko mikononi mwa muwekewa rahani na muwekewa rahani amekubali rahani iliyotajwa kisheria. Toka tarehe kadha.

‘Uwakala’:

1) Maana yake:

‘Uwakala’ ni kumpa unaibu mtu atakayekuwa badala yake katika jambo miongoni mwa mambo yanayokubali ndani yake kufanywa kwa niaba, kama vile kuuza na kununua na kudaiana na mfano wake. (Haifai kumpa *uwakala* kafiri katika mambo ya kuuza na kununua kwa kuhofia kuchukua/kufanya yaliyoharamishwa).

2) Masharti yake:

Inashurutishwa kwa kila mmoja ya wakili na muwakilishwa kuruhusiwa kutumia. Yaani awe balebale na mwenye akili timamu.

3) Hukumu yake:

‘Uwakala’ ni kitu kinachofaa kwa mujibu wa Qur-aan na Sunna. Allah Mtukufu Amesema,

وَالْعَمَلِينَ عَلَيْهَا

“...na wanao zitumikia...” (9:60)

Yaani hao ni wale mawakala wa Imamu katika kukusanya Zakka. Allah Mtukufu Amesema:

فَأَبَعْتُمْ وَأَوْكَذَلِكَ أَحَدَكُمْ بَوْرَقِكُمْ هَذِهِ إِلَى الْمَدِينَةِ فَلْيَنْظُرْ أَيُّهَا أَزْكَىٰ

طَعَامًا فَلْيَأْتِكُمْ بِرِزْقٍ مِّنْهُ وَلْيَتَلَطَّفْ وَلَا يُشْعِرَنَّ بِكُمْ أَحَدًا ﴿١٩﴾

“...Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi fedha zenu ende mjini, akatazame chakula chake kipi kilicho bora kabisa akuleteeni cha kukila. Naye afanye mambo hayo kwa busara, wala asikutajeni kabisa kwa yeyote...” (18: 19).

Wamemuwakilisha mmoja wao katika kuwanunulia chakula. Na Mtume ﷺ amesema kumwambia Sahaba jina lake – Unays.

“Rauka mapema asubuhi ewe Unays kwa mke wa huyu, akikiri kuwa anazini Basi mpigeni mawe.” (Bukhari).

Mtume ﷺ amepa uwakala Sahaba “Unays” katika kuhakiki madai ya zinaa kisha katika kusimamisha na kutekeleza adhabu. Na amesema Abu Hurayra رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ amenipa uwakala katika kutunza Zaka ya Ramadhanani (Zakatul Fitr). Na Mtume ﷺ alisema kumwambia Jabir رضي الله عنه zimshukie.

“Utakapomwendea wakili wangu, chukua wasaki kumi na tano kutoka kwake, na Akitaka aya - alama kutoka kwako basi weka mkono wako katika mtulinga wako.” (Abu Dawud na Daraqutni).

Mtume ﷺ alimtuma baba Raafii Mtumwa wake na mtu mwingine katika Answaar wakamuoza Maimuna bint Al-Haarith رضى الله عنه zimshukie –na ilhali yeye yuko Madina, akawapa uwakala wa kufungisha ndoa. (Muwatta cha Imam Malik).

4) Hukumu zake mbalimbali:

Hukumu za Uwakala ni:

-Uwakala unathibiti kwa kauli inayojulisha kutoka idhini. Hapashurutishwi tamko maalumu.

-Uwakala unaswihi katika kila haki ya kibinadamu, miongoni mwa mikataba ya mapatano kama vile kuuza, kununua, kuoa, kumrejea mke, na kuvunja ndoa au mauzo, kama vile talaka, na khuluu. Pia uwakala katika haki za Allah Mtukufu ambazo katika haki hizo unaibu unafaa, kama vile kugawa Zaka, Hija na Umra kwa niaba ya mtu aliyekufa au aliyeshindwa kufanya hivyo.

-Uwakala unaswihi katika kuthibitisha adhabu, na katika kuzitekeleza, kwa kauli yake Mtume ﷺ akasema “Unays”.

“Rauka mapema asubuhi kwa mke wa huyu, akikiri basi mpige mawe hadi kufa.”

-Uwakala hauswihi katika aina zote za kujikurubisha (kwa Allah) ambazo katika hizo unaibu. Haifai kama vile: kuswali, kufunga, kama ambavyo katika kila lililoharamishwa, kwani jambo lisilofaa kufanya pia uwakala haufai katika (jambo) hilo.

-Uwakala hubatilika kwa kuvunja moja ya ncha mbili (uwakal na mwakilishwa). Au kwa kufa mmoja wao au kupata wazimu, au kwa muweka wakili kuuzulu uwakili.

Minhajil Muslim

-Atakayewekewa uwakala katika kuuza au kununua basi hatauzau au kununua kwa nafsi yake, wala kwa mtoto wake, wala kwa mkewe au mtu yoyote miongoni mwa (wale) ambao ushahidi wake haukubaliki kwao, kwa sababu yeye anatumia kuwapendelea kwa sababu ya ukaribu wa kindugu. Na mfano wa wakili katika haya ni wasii wa mudharaba, na mshirika, na hakimumu na muangalizi wa Waqfu.

-Wakili halipishwi kitu kilichopotea, au kilichoharibika ikiwa hakuzembea. Au kuchupa mpaka katika kile alichopewa uwakala ndani yake. Kama atazembea au kuvuka mipaka itamuwajibikia kulipishwa kilichopotea au kuharibika.

-Uwakala unaswihi wa hivi hivi (*Mutlaqa*) kwa hiyo inafaa kuwakilisha katika haki nyingine za kibinaadamu, hivyo basi wakili atatumia katika haki zilizobai za aliyeweka wakili isipokuwa katika mambo kama talaka, kwani hapana budi ndani yake (talaka) utashi wa muachaji na azma yake juu yake.

-Mtu anapomtaka muakilishi wake kununua kitu fulani, haitajuzu kwake kununua kitu kingine. Kwa wakati wowote ataponunua kitu kisichokuwa kile alichoinishiwa aliyempa uwakala atakuwa na hiari katika kukikubali au kukirudisha (kukikataa), na hivyo hivyo ikiwa atamnunulia kitu chenye dosari au alimnunulia kwa kupunjwa kwa dhahiri, kwani mtoa uwakala ana hiari kati ya kuchuku au kuacha.

-Uwakala unaswihi kwa ujira (Malipo), na inashurutishwa kutaja kiasi maalumu cha malipo, na kubainisha kazi inayowakilisha (kazi ya kutendwa na wakili)

Mfano wa Kuandika Uwakala:

Baada ya kumhimidi na Kumshukuru Allah Mtukufu, fulani amemuweka wakili fulani kuwa wakala na wawili hao...wakiwa katika uzima wao na akili zao timamu, na mambo yao yanafaa: kusimamia (kwa niaba) jambo kadhaa.. na ameukubali huyo wakili aliyetajwa uwakala na ameukiri baada ya kumshuhudisha fulani na fulani...juu ya uwakala huo, na hayo ni katika tarehe kadha...

‘Suluhu’:

1) Ufafanuzi wake:

Suluhu ni mapatano/makubaliano yanayofikiwa kati ya watu wawili wenye mzozo baina yao na kuleta ufumbuzi wa tofauti zao; hiyo ni kama vile mtu kudai haki juu ya mtu mwingine, anaitakidi kwamba yeye ndiye mwenyewe halafu mdaiwa anakiri kwa kutojua kwake kisha anafanya nae suluhu kwa sehemu ya haki hiyo ili kuepuka ugomvi, na kiapo kitakacholazimu wakati atakapokanusha.

2) Hukumu yake:

Suluhu ni kitu kinachojuzu kwa kauli yake (Allah) Mtukufu,

فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يُصْلِحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا وَالصُّلْحُ خَيْرٌ

“...*basi si vibaya kwao wakisikizana kwa suluhu. Na suluhu ni bora...*” (4:128)

Na kauli yake Mtume ﷺ

“*Suluhu inafaa kati ya Waislamu. Isipokuwa suluhu ambayo itaharamisha halali au itahalalisha haramu.*” (Abu Dawud na Tirmidhi).

3) Vigawanyo vyake:

Suluhu katika mali imegawanyika katika mafungu matatu nayo ni:

a) *Suluhu* Juu ya kukiri:

Ni kudai mtu haki juu ya mtu mwingine, akamkubalia na mdai akampa kitu kwa kusuluhisha pale ambapo hakumkatalia haki yake. Kama vile kumuondolea (kumpunguzia) baadhi ya deni ambalo amelikiri, au kumpa hiba baadhi ya vitu alivyokiri kuwa ni vyake au atafanya nae suluhu katika kitu alichokiri kisichokua katika jinsi ya alivyokiri, kama vile kumkiria nyumba kua ni yake, yeye akampa Dirhamu au kumkiria mnyama yeye akampa kwa nguo mfano.

b) Suluhu juu ya kukanusha:

Nayo, ni mtu kudai haki juu ya mwingine naye akaikana yule mdaiwa kisha akafanya nae suluhu kwa kumpa kitu ili aache madai yake na ampumzishe na magomvi na kiapo ambacho kitamlazimu pindi atapokanusha.

c) Suluhu juu ya kunyamaza:

Ni mtu kudai haki juu ya mwingine, na mdaiwa akanyamaza wala asikiri wala kukanusha. Mdaiwa akafanya suluhu na mdai kwa kumpa kitu ili aondoe madai yake na aache kuzozana naye.

4) Hukumu zake mbalimbali:

Sheria za Suluhu Ni:

a) *Suluhu* juu ya kitu kinachodaiwa bila ya kukichukua ni sawa na kuuza na kununua (*Bay-u*) katika yale yanayofaa na yanayokatazwa, katika hukumu zake mbalimbali za mauzo katika kurudisha kitu kwa kasoro, kuwa na hiari ya kupunja, na "*Shuf-a*" katika kitu kisichogawika lau mtu akidai nyumba kwa mtu mwingine, akafanya nae suluhu kwa kumpa nguo na akamshurutisha kua, nguo hiyo asimpe mtu fulani kuivaa, suluhu haitaswihi kwa sababu (sharia hiyo) inakuwa ni kama bei itakaposhurutishwa ndani yake shuruti inayoathiri mkataba wa bei. Mtu akimdai mtu mwingine kwa mfano dinari za wakati huohuo na yeye akafanya suluhu kwa dirham za baadae suluhu haitaswihi kwa sababu *sarfu* (kubadilisha fedha) inashurutishwa kukabidhiana kikaoni. Lau alidai kwa mtu mwingine bustani akafanya naye suluhu kwa nusu ya nyumba, hakika yule mshirika ana haki ya kudai "*Shufaa*" katika ile nusu iliyotolewa katika saluhu. Na lau alifanya nae suluhu kwa (Kumpa) mnyama juu ya madai fulani akamkuta yule mnyama ana dosari basi atakuwa na hiari ya kumshurutisha au kumchukua; na ndivyo hivi hivi ila suluhu itakayokuwa si katika jinsi ya kile kinchofanyiwa suluhu basi hiyo ni kama bei katika hukumu zake zilizobaki.

b) Itakapokuwa mmoja wa wanaofanya suluhu anajua uwongo wa nafsi yake, basi suluhu ni batili kwake yeye, na alivyovichukua kwa nia ya suluhu hivyo ni haramu juu yake.

c) Mtu atakayekiri haki fulani, na akajizua kuitekeleza isipokuwa kwa kupewa yeye kitu, hilo halitakuwa halali kwake. Kama mtu aliyekiri kuwa anadaiwa dinari alfu; na akajizua kuzilipa isipokua apunguziwe katika hizo mia tano, ama asiposhuritisha hilo la kupunguziwa kitu, ila tu yule mwenye kukiriwa deni akajitolea yeye mwenyewe au kwa uombezi wa mtu mwingine aliye pale, ndipo akampunguzia kitu basi hapo itafaa kwa aliyekiri kukichukua. Hayo ni kutokana na habari iliyoswihi kwamba Mtume ﷺ,

“Aliongea na wadai wa Jabiri wamuondolee sehemu ya deni lake – wanalomdai.” (Bukhari).

Kama ambavyo “*Ibnu Abihadrad*” alidaiana na Ka’ab Bin Malik deni lake msikitini. Sauti zao zikapaa mpaka akazisikia Mtume ﷺ chumbani kwake, akawatokea kisha akamwita:

“Ewe Kaab, Kaab akasema: Labaika ewe Mjumbe wa Allah ﷻ akampa ishara amuondolee sehemu ya deni lake, akasema tayari nimeshafanya hivyo ewe Mjumbe wa Allah ﷻ, akasema:” haya simama umpe.” (Bukhari).

d) Ikiwa watawekeana suluhu na mwenzake, katika ugomvi wa ukuta, kwa sharti la kufungua dirisha au mlango, kwa kubadilishana na kitu kingine, basi suluhu imekubalika kwa sababu imethibiti ridhaa ya mbadilishano.

Mfano wa Kuandika Suluhu:

Baada ya Bismillahi tukufu na kumuhimidi Allah Mtukufu, na Swala na Salaam kwa Mtume wake ﷺ...

Fulani amefanya suluhu na fulani kutokana na yale aliyokuwa akidai ya kwamba yeye anamiliki na anastahiki nyumba fulani (Ataelezea na kutaja mipaka yake).

Nyumba ambayo iko mkononi kwa mdaiwa fulani baada ya kuzozana kwao katika dhati ya madai, na amekiri mfanya suluhu wa kwanza baada ya hao kwa aliyoyadai huyo wa pili. Amemthibitishia uthibitisho wa kisheria, kwa kitu ambacho kiasi chake ni kadha...katika dirham au kwa chenye thamani kadha...miongoni

Minhajil Muslim

mwa vitu usuluhishi wa kisheria. Wameitana kuridhia na kuafikiana juu ya suluhu hiyo. Anatoa mwanasuluhu wa kwanza kumpa huyu wa pili yote waliyofanyia suluhu, na amemkabidhi ukabidhi wa kisheria. Amekiri mwana suluhu wa pili aliyetajwa kwamba yeye hastahiki pamoja na mwana suluhu wa kwanza, katika nyumba hii iliyofanyiwa suluhu haki wala hastahiki madai, wala malalamiko yoyote, wala miliki wala shubha (utata) wala manufaa yoyote, kwa kitu chochote, kichache au kingi. Na wamethibitishiana kisheria juu ya yote hayo kisheria, yote hayo yametimia kwa njia kadha...



Mada ya Nane

‘Kuendeleza Maeneo Yaliyokufa, Nyongeza ya Maji Vipande vya Ardhi na mipaka (Ardhi Iliyohifadhiwa na Dola) Kuendeleza Maeneo Yaliyokufa

1) Maana yake:

Kuendeleza maeneo yaliyokufa: ni Muislamu kukusudia ardhi ambayo si miliki ya mtu yoyote akaiimrisha kwa kupanda miti humo, au kujenga au kuchimba kisima akahusika nacho na kuwa mmiliki wake.

2) Hukumu yake:

Kuendeleza ardhi iliyokufa –hukumu yake –inafaa na ni halali, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mtu atakayeendeleza ardhi iliyokufa, basi ni yake.” (Ahmad na Tirmidhi)

3) Hukumu zake:

a) Huthibitika umiliki wa ardhi iliyohuishwa (iliyoendelezwa) kwa aliyeendeleza kwa sharti mbili:

Ya kwanza: Ni kuimarisha kwa uhakika kwa kupanda miti au kujenga nyumba au kuchimba visima vyenye maji. Haitoshi kupanda mmea mdogo, au kuweka alama, au kuizuia kwa kizuizi kama vile miba na mfano wake. Na aliyeihusha ardhi atakuwa na haki zaidi kuliko mtu mwingine.

Ya pili: Isiwe imehusika na mtu yeyote miongoni mwa watu, na hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mtu mwenye kuimarisha ardhi si ya mtu yeyote basi yeye ana haki zaidi kuliko mwingine”. (Bukhari)

b) Ikiwa ardhi iko karibu na mji au iko ndani yake basi, haitaendelezwa isipokuwa kwa idhini ya kiongozi (serikali). Kwani huenda ikawa ni katika maeneno yaliyoambatanishwa na mji kwa manufaa ya Waislamu wote. Kama imeachwa kwa maslahi ya wote watapata adha kwa yeye kupamiliki na kupaimarisha.

c) Madini hayamilikiwi kwa kuendeleza ardhi tu ni sawa iwe chumvi au mafuta au visivyokuwa hivyo miongoni mwa madini, kutokana na kuhusiana (hayo madini) na maslahi ya Waislamu kwa jumla, Mtume ﷺ

“Aliwakataza watu eneo la madini chumvi akarejewa katika hilo, akamtaka yule aliyempa alirejeshe.” (Abu Dawud na Tirmidhi).

d) Mtu ambae katika ardhi aliyoihuishayatamdhihirikia maji yanayotiririka, basi yeye ana haki zaidi kuliko mwingine, atakuwa ni mwenye kutumia maji yale kiasi cha mahitaji yake, na yatakayozidi na kubakia basi hayo ni ya Waislamu wote. Kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Watu wanashirikiana katika vitu vitatu: katika maji, malisho, na moto.” (Ahmad na Abu Dawud)

Tanbihi:

-Eneo la kuzunguka (la hifadhi ya) kisima iwapo ni cha zamani isipokuwa, mchimbaji kakichimba upya, ni dhiraa khamisini. Na kama amechimba kipya basi eneo lake la hifadhi katika ardhi inayokizunguka ni dhiraa ishirini na tano, Basi eneo hili atalimiki mwenye kisima hicho (eneo la pembeni mwa Kisima).

Kwani wamefanya hivyo baadhi ya wanazuoni waliotangulia (Salafu Swalih) na kwa yaliyopokewa kutoka kwa Mtume ﷺ

“Eneo la hifadhi la kisima ni urefu wa kamba yake.” (Ibn Majah).

-Eneo la hifadhi ya mti au mtende ni kiasi cha urefu wa matawi yake au makalala yake, basi atakaye miliki mti katika ardhi isiyondelezwa ana haki ya kumiliki eneo lililozunguka ule mtu kwa kiasi cha urefu wa matawi yake na makalala yake, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Eneo la hifadhi la mtende ni urefu wa makalala yake.” (Ibn Majah)

-Eneo la hifadhi ya nyumba ni lile linalotosha pembezoni mwake kutupia takataka au kumuegesha ngamia, au kuegesha gari, basi mtu atakayejenga nyumba kwenye ardhi iliyokufa anakuwa na haki ya kumiliki eneo linalozunguka nyumba hiyo inayoitwa kwa faida viambata.

‘Ziada ya Maji’

1) Maana yake:

Yaliyokusudiwa kwa neno ... ‘Maji ya Ziada’ ni kuwa Muislamu ana maji ya kisima, au mto yanayozidi kiasi cha mahitaji yake katika kunywa kwake na kumwagilia kwake mimea yake, au miti yake.

2) Hukumu yake:

Hukumu ya ziada ya iliyozidi haja yake ni kwamba ayatoe kwa wanaoyahitaji miongoni mwa Waislamu bila malipo, na hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Ziada ya maji haiuzwi, yakapata kuuzwa malisho ya wanyama.”
(Bukhari na Muslim)

Na Kauli yake Mtume ﷺ

“Ziada ya maji isizuiwe ikazuiwa malisho ya wanyama.”
(Bukhari na Muslim)

3) Hukumu zake:

Sheria za maji ni hizi:

-Hailazimiki kugawa maji ziada isipokuwa baada ya kujitosheleza nayo.

-Ni kuwa, huyo anayegawiwa ni muhitaji wa hayo maji

-Isiambatane dhara yoyote kwa mwenye maji kwa sababu ya kugawa kwake.

Al-Iqtwaai, Vipande vya Ardhi

1) Maana yake:

Al-Iqwaai, ni hakimu kuikata sehemu ya ardhi ya wote ambayo kwa sasa si miliki ya yeyote, (kukata) kipande kitakachotumika kwa manufaa, katika kupanda mimea, au (Kupanda) miche ya miti au kujenga, kwa ajili tu ya kutumia nafasi au kumilikisha.

2) Hukumu yake:

Al-Iqwaai, Kukata ardhi kunafaa kwa kiongozi mkuu wa Waislamu si mwingine yeyote. Mtume ﷺ alimega ardhi, na Abubakari alimega pia na baada yake Umar na wengine radhi za Allah ziwashukie:

3) Sheria zake:

-Asikate (ardhi) asiyekuwa Imamu, kwani hana ruhusa kuitumia milki ya wote isipokuwa yeye tu.

-Asimege zaidi ya kiasi atakachoweza kukihuisha/ kukiendeleza na kukiamirisha.

-Atakayekatiwa ardhi kisha akashindwa kuimarisha, Imamu atamtaka airudishe, kwa ajili ya kulinda maslahi ya watu wote.

-Imamu ana haki ya kuikata ardhi kukata viambata (vipande vipande) kwa amtakaye miongoni mwa raia, iwe maeneo ya kuuzia katika Masoko na viwanja vya pamoja (vya wazi), barabara pana, kama hayakupatikana madhara kwa hilo kwa watu wengi na atakayekatiwa (katika kifungu hiki) hamiliki lile eneo isipokuwa tu anakuwa na haki zaidi kuliko mtu mwingine. Kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Atakayekatiwa kitu ambacho hajakatiwa Muislamu mwingine basi yeye ana Haki zaidi na hicho.” (Abu Dawud)

-Hana ruhusa mtu aliyekatiwa (eneo) na Imam kufanya mahala pa kukaa, au amepawahi bila ya kumegewa na Imam kumdhuru mtu kwa kumzibia Mwanga au kumuwekea kizuizi kwa wanunuzi, kwa kutoweza kuiona bidhaa yake inayooneshwa kwa ajili ya kuuza. Kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Hapana kujidhuru wala kuwasababishia madhara wengine.” (Ibn Majah na Ahmad)

Tanbihi:

(Maji ya Bonde) yatakapotiririka, watanufaika nayo Waislamu wa juu zaidi kisha wanaofuata, mpaka yataishia kwenye mashamba yaliyotakiwa kumwagiliwa, kufuatana na ukubwa wa shamba au udogo wake. Na ikiwa watazozana basi kura itapigwa kati yao, na hayo ni kutokana na aliyopokea Ibn Majah kutoka kwa ‘Ubaada bin Swamit, kwamba Mtume ﷺ.

‘Alihukumu katika kumwagilia mitende kwenye kurumo za maji kuwa wa juu ataanza kabla ya yule wa chini na atayaacha maji mpaka yafikie vifungo viwili vya miguu, kisha atayaacha maji yaende kwa anayefuatia, na ndiyo hivi hivi mpaka yaishe mashamba au yaishe maji.’

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mwagilia ewe Zubair kisha au yaache maji (yaende) kwa jirani yako.” (Bukhari)



Al-Himaa, Hifadhi:

1) Maana yake:

Alhimaa: Ni ardhi isiyoendelezwa, imehifadhiwa, kwa kuchungia mifugo humo, ili majani yapate kuwa mengi waje kula wanyama maalum.

2) Hukumu yake:

Haifai kwa mtu yeyote kuhifadhi ardhi ya pamoja kwa Waislamu dhira moja na zaidi isipokuwa Imam (peke yake) iwapo hilo ni kwa maslahi ya Waislamu. Hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Hapana kuhifadhi isipokuwa kwa ajili ya Allah na Mtume wake ﷺ.” (Bukhari)

Hadithi hii imejulisha kwamba: Hana ruhusa yeyote kuhifadhi ardhi isipokuwa Allah na Mtume wake ﷺ au Khalifa wao naye ni kiongozi kama ambavyo inajulisha kuwa Imam hahifadhi ardhi pasi na maslahi ya jumla (wote). Kwa sababu kinachokua kwa ajili ya Allah, na Mtume wake ﷺ hutumiwa daima katika maslahi ya wote. Kama moja ya tano ya ghanima (Ngawira) wanayoiacha maadui baada ya kukimbia, na moja ya tano ya rikaz (mali inayogunduliwa chini ya ardhi ikiwa imezikwa katika mazingira ya kijaahiliyya) na mfano wake. Mtume ﷺ

“Alihifadhi ardhi ya “Naqiya” kwa ajili ya ngamia na farasi wa Jihadi.” (Bukhari).

Kama ambavyo Umar رضي الله عنه alihifadhi ardhi, na pakasemwa maneno juu ya hilo, naye akasema:

“Mali ni ya Allah, na hawa waja ni wake Allah, na naapa kwa Allah na naapa kwa Allah: lau kama si jukumu nililobebeshwa katika Jihad nisingehifadhi ardhi, walau shubiri moja kwa shubiri” . (Bukhari)

3) Hukumu zake:

-Hatengi hifadhi ya ardhi isipokuwa kiongozi (khalifa) wa Waislamu na Imamu wao, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Hapana kutenga hifadhi ya ardhi isipokuwa kwa Allah na Mtume wake ﷺ.”

-Haitengwi hifadhi isipokuwa ardhi ambayo haijaendelezwa ambayo si miliki ya mtu yoyote.

-Khalifa hatengi ardhi hifadhi kwa nafsi yake hasa, bali kwa maslahi ya Waislamu wote kwa jumla.

-Yanaambatanishwa kwa kukisiwa maeneo yanayohifadhiwa na dola kama baadhi ya milima kwa ajili ya kustawisha miti katika mapori, itaangaliwa katika hilo, iwapo kweli linaleta maslahi ya wazi (ya thamani) kwa Waislamu, serikali itakubaliwa juu ya hilo, na itapobainika hilo linaleta madhara kwa Waislamu, na halikuweza kuwa nguvu haitakubaliwa kwani hakuna na kuihifadhi isipokuwa kwa Allah na kwa Mtume wake ﷺ.



Katika Kutaja Jumla ya Hukumu

Mada ya kwanza

‘Kukopesha’

1) Maana yake:

Kilugha: Kukopa maana yake ni kukata.

Kisheria: Ni kutoa mali kumpa itakayemsaidia kisha arudishe badala yake. Hali hiyo kama kusema mwenye shida kumwambia mmiliki wa mali hiyo ambaye kunafaa kutoa kwake, “Nikopeshe kitu fulani katika mali yako au chombo au mnyama kwa muda fulani kisha nitakurudishia.” Na akafanya hivyo mmiliki wa mali au kitu hicho.

2) Hukumu yake:

Kukopesha ni sunnah (Jambo zuri) kwa mkopeshaji na hilo linathibitishwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضِعْفَهُ لَهُ وَلَهُ أَجْرٌ كَرِيمٌ ﴿٥٧﴾

“Ni nani atakaye mkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili amrudishie mardufu, na apate malipo ya ukarimu.” (57: 11).

Na kauli yake Mtume ﷺ amesema,

“Mwenye kumwondoshea ndugu yake tatizo moja katika matatizo ya dunia na Mwenyezi Mungu atamuondoshea mtu huyo tatizo moja katika matatizo ya Siku ya Kiyama.” (Tirmidhi na Abu Dawud).

Ama kuhusiana na anayetaka kukopa ni jambo linalofaa nani halali kwake na hakuna ubaya wowote katika jambo hilo. Kwani Mtume ﷺ alinikopesha Ngamia mdogo na akamrejeshea ngamia mkubwa akasema,

“Hakika mbora wa watu ni yule mzuri wao anapokopa na kulipa.” (Bukhari)

3) Masharti yake:

- a) Kiasi kinachotakiwa kifahamike kukopeshwa ikiwa kinapimika kwa kilo au idadi yake.
- b) Kijulikane sifa yake na umri wake kama mkopo ni mnyama.
- c) Mkopeshaji anatakiwa awe na uwezo wa kutoa kisheria. Hivyo haitofaa kuazima vitu kwa asiyekimiliki kitu kinachotakiwa kuazimwa wala kwa ambaye hana uwezo wa kutoa maamuzi kutokana na udogo wa umri wake.

1. Hukumu zake:

- a) Mkopeshaji awe na uwezo wa kumiliki au kudhibiti kinachokopwa. Kwa hali hiyo wakati wowote mkopaji atakapokea anachokopa atakuwa ameshakimiliki na kimeshakuwa katika dhamana yake.
- b) Ni vizuri kuweka muda wa kukopesha, na kutoweka muda ni vizuri zaidi kwa ajili ya kumpunguzia uzito mkopaji.
- c) Kikibakia kitu kilichoazimwa (kopwa) kama kilivyokuwa siku kilipoazimwa (kopa) kitarudishwa hivyo hivyo na ikiwa kimebadilika kwa kupungua au kwa kuzidi kitarudishwa kilicho mfano wake, kikiwepo, na kama kikikosekana basi itarudishwa thamani yake.
- d) Ikiwa kitu kinachokopwa hakina gharama za uchukuzi inafaa kukilipa sehemu yoyote anayotaka mkopeshaji na kitakapokuwa kina gharama za uchukuzi itamlazimu mkopaji kurudisha kitu hicho mahali pale pale alipokichukua.
- e) Ni haramu kwa mkopeshaji kunufaika kwa manufaa yoyote yatokanayo na kitu alichokikopesha. Ni sawa manufaa hayo yawe kwa kuzidisha katika kukodisha au kwa kukifanya vizuri kitu hicho kilichokodishwa au kwa manufaa mengine yoyote yaliyo nje ya kukopesha itakapokuwa wamewekeana sharti na kuhurumiana kati yao mkopeshaji na mkopaji. Ama itakapokuwa manufaa hayo

Minhajil Muslim

anayonufaika nayo mkopaji ni hisani tu ya mkopeshwaji itakuwa si vibaya. Kwani Mtume ﷺ alitoa ngamia mkubwa kwa ngamia mdogo na akasema:

“Hakika mbora wa watu ni mzuri wao zaidi wa kulipa” (Bukhari).



Mada ya Pili

‘Amana’:

1) Maana yake:

Kuweka amana ni kitu kinachowekwa – kuachwa – ikiwa mali au kitu kingine kwa atakayekihifadhi na kuweza kukirudisha kwa mwenyewe wakati wowote anapokihitaji.

2) Hukumu yake:

Kuweka amana ni jambo linaloruhusiwa kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo. Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema:

فَإِنْ أَمِنَ بَعْضُكُم بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ الَّذِي أُؤْتِمِنَ أَمْنَتَهُ وَلْيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُ

“...Na mmoja wenu akimwekea amana mwenziwe basi aliye aminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi...” (2:283)

Amesema tena.

✽ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا

“*Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe...*” (4:58).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“*Itoe amana uliyoaminiwa kumrudishia aliyekupa wala usimfanyie khiana aliyekufanyia khiana.*” (Abu Dawud na Tirmidhi).

Kwa hivyo kuwekeza ni miongoni mwa aina za amana na hukumu ya kuwekeza inatofautiana kulingana na hali na mazingira yanavyotofautiana.

Inaweza kuwa kukubali kuweka amana ni wajibu kwa Muislamu. Na hali hiyo ni pale atakapolazimika Muislamu kuhifadhi mali yake na asimpe mtu mwingine wa kuhifadhi mali hiyo zaidi yake.

Pia inaweza kuwa ni Sunnah. Hiyo itajitokeza pale mtu atakapotakiwa kuhifadhi kitu cha mwenzake na huyo mwenye kitu akawa ana uwezo wa kuhifadhi kitu chake hicho. Kwani jambo hii la kuwekeana ni katika mlango wa kusaidiana kwa wema ulioamrisha na Mwenyezi Mungu katika Qur-aan.

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ

“...Na saidianeni katika wema na uchamngu...” (5:2).

Na kunaweza kuwa karaha jambo linalo chukiza kukubali kuwekeza na hali hiyo ni atakapokuwa aliyepewa hifadhi hana amana hiyo au hawezi kuihifadhi.

3) Hukumu za amana:

a) Anatakiwa mweka amana na mwenye kuwekewa wawe na akili timamu kisheria. Kwa sababu hairuhusiwi kuweka amana kwa mtoto mdogo au mwenda wazimu.

b) Halipishwi aliyewekewa amana na kikiharibika kitu kilichowekwa bila kukusudia kukiharibu au kupetuka mpaka katika matumizi. Na hilo ni kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Hapana kulipishwa mwenye kuaminiwa.” (Daraqutni)

Na kauli yake

“Mwenye kuwekewa amana hana dhamana.” (Ibn Majah).

Mlolongo (Isnadi) wa hadithi hii ni dhaifu kulingana na maelekezo ya wataalamu wa Elimu ya hadithi.

c) Anapaswa kila mmoja kati ya aliyewekewa amana na aliyewekewa kurudisha kilichowekwa wakati wowote atakapotaka.

d) Haifai kwa mwenye kuwekewa amana kunufaika na kilichowekwa kwake kwa namna yoyote katika aina za kunufaika ila itakapokuwa kwa idhini ya mwenyewe.

e) Watakapobishana katika kukirudisha kilichowekwa kauli itakayosikilizwa ni kauli ya aliyeweka (aliyekihifadhi kwake) kitu hicho pamoja na kiapo ila muwekewaji atakapoleta ushahidi unaoweka wazi kwamba aliyewekezwa kitu hicho hajakirudisha.

Namna ya kuandika mikataba ya kuwekeza:

1) Sura ya kuandika kuweka amana:

Amekiri fulani. . .kwamba amekabidhiwa na amepokea kutoka kwa fulani. . .kiasi kadhaa cha fedha kwa njia ya kuweka amana kisheria hali ya kulazimika kuhifadhi kitu na kukichunga katika hifadhi ya mfano wake na katika sehemu aliyoamrisha muwekezaji kuwekwa kitu chake katika sehemu hiyo. Na alihudhuria muwekaji aliyetajwa na amethibitisha juu ya hilo kisheria.

2) Maandishi ya kukiri kuweka amana:

Amekiri fulani kwamba amepokea kutoka kwa fulani. . .kitu ambacho kiasi chake ni kadhaa. Kupokea kwa kisheria na kitu hicho kimeshakuwa kwake na katika dhamana yake na hiari yake na hicho kiasi ndicho alichokiweka kwa aliyemuweka kabla yake na hakumcheleweshea katika kitu hicho, aliyetajwa juu ya hilo kusadikisha kisheria. Na hilo ilikuwa ni tarehe. . .



Mada ya Tatu

‘Kuazima’

1) Maelezo yake

Kuazima ni kitu anachopewa mtu atakayefaidika nacho kwa muda maalumu na kukirudisha. Kama vile Muislamu kuazima kalamu kwa Muislamu mwenzake aandikie au nguo ili avae kisha airudishe.

2) Hukumu yake:

Kuazima ni jambo linalokubalika kisheria kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu,

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ

“...Na saidianeni katika wema na uchamngu...” (5:2).

Na kauli yake nyingine

وَيَمْتَعُونَ الْمَاعُونَ

“Nao huku wanazuia msaada.” (107:7)

Kauli ya Mtume ﷺ

“Kitu chenye kuazimwa ni chenye kudhaminiwa.”

Mtume ﷺ alisema hilo kumwambia Swafwan Bin Umayyat wakati alipomwazima nguo ya vita.

3) Hukumu zake: Hukumu za kuazima ni hizi:

a) Hakiazimwi ila kitu kilicho halali wala haazimwi mwanamke mtumwa kwa ajili ya ngono. Wala Muislamu kwa kumtumikia kafiri. Wala mafuta mazuri au nguo kwa kufanyia mambo ya haramu, kwani kusaidiana kwa mambo mabaya ni haramu kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu,

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ

“...Na saidianeni katika wema na uchamngu...” (5:2).

b) Mwenye kitu kinachoazimwa akiweka masharti ya kulipa atalazimika muazimaji kulipa atakapokiharibu. Na hilo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Waislamu wako juu ya sharti zao walizowekeana.” (Abu Dawud, Hakim)

Na kama mwenye mali hakuweka sharti na ikaharibika kwa bahati mbaya pasi na kufanya uadui. Kwa hali hiyo haitompasa kulipa lakini ni vizuri kulipa. Na hilo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mkono ni dhamana ya ulichokichukua mpaka ukitoe.” (Abu Dawud, Tirmidhi na Hakim).

c) Muazimishaji analazimika kutoa gharama za kurudisha alichokiazima kitakapokuwa hakirudi ila kwa mbebaji au kwa malipo ya usafiri na hili ni kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Mkono utakuwa ni dhamana ya ulichokichukua mpaka ukitoe.”

d) Haifai kwa aliyeazima kitu cha watu naye kukodisha, ana kuazimisha si vibaya kama ridhaa aliyeazimwa itathibitika na kama hakuna makubaliano haifai.

e) Akiazima ukuta kwa kuwekea mbao haitojuzu kurudisha kwa mwenyewe mpaka uanguke na ndivyo hivyo hivyo kwa mwenye kuazima ardhi kwa ajili ya kulima hatoirudisha ardhi hiyo mpaka avune kwani kinyume cha hivyo ni kumdhulumu ndugu yake Muislamu jambo ambalo ni haramu.

f) Mwenye kuazima kitu chochote kwa muda maalumu inakuwa vizuri kwa mmiliki wake kutotaka kurudishiwa kitu hicho hadi baada ya kuisha muda.

4) Namna ya kuandika makubaliano ya kuazima:

Fulani amemuazima fulani... kitu kilichotajwa na kwamba ni kitu chake na kiko katika dhamana yake na chini ya matumizi yake. Na hiyo ni nyumba yote iliyoko

Minhajil Muslim

sehemu fulani au mmea fulani au nguo kadhaa ili akae au apande au avae huyu aliyetajwa mpaka muda kadhaa. au masafa kadhaa. . . . ni kuazima kuliko sahihi kunakofaa.

Fulani amemkabidhi anayeazimisha fulani anayeazima mnyama aliyetajwa. Ametoa kutoa kwa kisheria na kuanzia hivi sasa ameshakuwa katika dhamana yake juu ya hukumu iliyowekwa wazi hapo juu na amekubali hilo kila mmojawao kutoka kwa mwenzake kukubali kisheria na hilo ni kuanzia tarehe kadhaa.



Mada ya Nne

‘Kunyang’anya’:

1. Maelezo yake:

Kunyang’anya ni kupokonya mali ya mtu mwingine kwa kutumia nguvu pasi na haki. Hali hiyo ni kama mtu kutawala nyumba ya mwenzake ili akae au mnyama wa mtu mwingine ili ampande.

2. Hukumu yake:

Kunyang’anya (au kupokonya) ni tendo lililoharamishwa kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu,

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ

“Wala msiliane mali zenu kwa batili....” (2:188).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Zindukeni hakika damu zenu na mali zenu ni haramu.” (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Mwenye kuchukua ardhi ya mwenzake shubiri moja kwa dhuluma atazungushiwa Siku ya Qiyama mzunguko wa ardhi saba.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Ahmad).

Na pia kasema Mtume ﷺ,

“Si halali mali ya mtu Muislam ila kwa ridhaa ya nafsi yake.” (Daraqutni)

3. Hukumu zake:

a) Kumuadhibu mnyang' anyaji kwa haki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu adhabu yake ni kufungwa jela au kupigwa lengo la kumkemea yeye na waliyo mfano wake.

b) Inamlazimu mnyang' anyi kurudisha alichokinyang' anya na kikiharibika mkononi mwake atalipa mfano wake na kama hakina mfano atalipa thamani yake.

c) Mwenye kunyang' anya kitu akalikuta na dosari inayomuondoshea mwenyewe thamani yake. Itamlazimu mnyang' anyi kulipa mbadala wake naye achukue alichokinyang' anya pamoja na sehemu aliyoitia dosari na ikishindikana atarudisha kitu cheneyewe pamoja na thamani ya uharibifu aliousababisha.

d) Zalisho la kitu kilichonyang' anywa litarudishwa pamoja na kitu chake kamili kama kitu hicho ni zalisho la mnyama au zalisho la mti au ni kodi ya mnyama anayepandwa.

e) Ikiwa kilichonyang' anywa ni ardhi na mnyang' anyi atajenga nyumba juu yake au kulima itamlazimu mnyang' anyi kubomoa jengo lake na kung' oa miti yake na kusawazisha ardhi aliyoiharibu kwa kujenga au kupanda na akitaka ataacha alichokipanda au alichokijenga na atachukuwa thamani yake kwa thamani ya kifusi na hilo kama ataridhia mwenye ardhi. Kwa kauli ya

“Halina haki jasho la dhalimu.” (Imepokewa na Abu Dawud, Tirmidhi na Daraqutni).

f) Mnyang' anyaji akifanya biashara na akapata faida atarudisha alichokinyang' anya pamoja na faida.

g) Wakitofautiana kati ya mnyang' anyi na mwenye mali katika thamani ya kitu kilichonyang' anywa au sifa zake, itazingatiwa kauli ya mnyang' anyi pamoja na kiapo chake kama mwenye kitu hana ushahidi.

h) Mwenye kuharibu mali ya mwenzake pasi na idhini yake mwenyewe itamlazimu kulipa na hilo ni kama kuchoma au kuchana au kufungua mlango uliofungwa au tundu au kufungua kizuizi chochote kikatoka kilichokua ndani ya nyumba au tundu.

i) Iwapo Mbwa mkali hakufungwa vizuri na mbwa huyo akang'ata mtu itampasa mwenye mbwa kulipa fidia au kumpa gharama za matibabu aliyeng'atwa.

j) Mnyama anayeachwa usiku na akaharibu mimea. Mwenyewe atalazimika kulipa. Na hilo ni kwa kauli yake Mtume 

“Wenye mali wanatakiwa kuhifadhi mali zao mchana na ilichoharibu usiku wenye mali watalipishwa.” (Tabarani).

k) Mnyama asiyekuwa na mwenyewe akiharibu kitu hatolipishwa. Kwa kazi yake

“Mguu wa mnyama ukiharibu kitu halipishwi.” (Ahmad)

Ama anachokiharibu kwa mdomo wake au kwa mikono yake atalipishwa akiwa amepandwa.



Mada ya Tano

Mali ya Kuokota au Mtoto Akiokota Kitu

1. Mali ya Kuokota:

Ni kukuta kitu kilichoachwa katika sehemu isiyokuwa na mmiliki na hali hiyo ni kama kukuta pesa njiani au nguo na akaogopea kupotea kitu hicho itabidi akiokote.

2. Hukumu yake:

Inafaa kuokota kitu kwa kauli yake pale Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu hilo na akasema: kuokotwa kinachookotwa kwa kauli yake wakati alipoulizwa kuhusu kiokotwa,

“Taja mfuko wake na kifuniko chake halafu ukitangaze mwaka mzima akija–mwenyewe atakichukuwa na kama hakutokea kitakuwa chako.” (Imepokewa na Bukhari na Muslim).

Aliulizwa Mtume ﷺ ikiwa kitu kilichookotwa ni mbuzi/kondoo akasema,

“Mchukue kwani huyo ni wako au ndugu yako au ni wa mbwa mwitu.” (Imepokewa na Bukhari, Tirmidhi na Ibn Majah).

Ni sunnah kuokota mwenye uhakika wa uaminifu wa nafsi yake na kunakuwa vibaya kuokota yule asiyejamini katika uaminifu wake.

3) Hukumu zake:

a) Ikiwa kitu kinachookotwa ni kitu duni ambacho hakina umuhimu wowote kwa watu kama vile kokwa moja ya tende au ya zabibu au kitambaa kilichochakaa, au bakora au fimbo inakuwa si vibaya kukiokota na muokotaji atafaidika na kitu hicho wakati ule ule anapokiokota wala halazimiki kukitangaza na kukihifadhi. Hayo ni kwa kauli ya Jabir رضي الله عنه.

“Mtume ﷺ alituruhusu katika fimbo, bakora, kamba na mfano wa vitu hivyo mtu akiviokota afaidike navyo.” (Abu Dawud).

b) Ikiwa kitu kilichookotwa ni chenye thamani katika jamii itampasa aliyekiokota kukitangaza mwaka mzima akikitangaza kweye milango ya msikiti na katika sehemu za mikusanyiko ya watu au kupitia kwenye magazeti na kwenye matangazo ya Radio au vyombo vingine vya habari. Akija mwenyewe akataja chombo kilichobebea kitu hicho au idadi yake au sifa yake itabidi apewe na kama hakuja baada ya mwaka kamili atakitumia muokotaji au atakitoa Sadaka akitaka lakini kwa nia ya kulipa pindi mwenyewe akija kukitafuta.

c) Cha kuokota cha Makkah haifai ila kukiokota kitakapohofiwa kupotea. Na mwenye kukiokota itampasa akitangaze muda wa kuwa bado yuko Makkah na akitoka Makka atapeleka kwa kiongozi na wala si haki yake kukimiliki. Kwa kauli yake ﷺ

“Hakika (mji wa Makkah) ni haramu (Mtukufu) hakiokotwi kitu chake”.

d) Kiokotwa aina ya mnyama kinaitwa myama aiyepotea (mbuzi/kondoo) akiwa porini inafaa kumuokota na kunufaika naye kuanzia wakati huo kwa kauli yake

“Huyo ni wako au wa ndugu yako au wa mbwa mwitu.”

Na akiwa ni ngamia haifai kumuokota pale pale kwa kauli yake ﷺ,

“Unamtakia nini na mwenyewe ana kwato zake na maji yake anakwenda kwenye maji na anakula miti mpaka afike mmiliki wake na amchukue.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim).

Na mfano wa ngamia aliyepotea ni punda, nyumbu na farasi waliopotea na wanaitwa ‘wanaopuuzwa’ kwani hairuhusiwi kuwaokota.

4) Namna ya kuandika hati ya kitu kilichookotwa:

Amekiri fulani...kwamba katika siku...ya mwezi...aliokota kitu katika sehemu kadha. Mfuko uliokuwa na pesa kadha...na kwamba aliutangaza wakati huo huo na saa hiyohiyo na aliutangaza katika sehemu yake na katika masoko, njiani na msikitini siku mfululizo na katika makundi tofauti na miezi mfululizo inayozidi mwaka kamili. Hakufika yeyote kutafuta na akakiopea kifo. Walimshuhudia mashahidi wake kwamba yeye alikikata akauokota na kwamba kiokotwa hicho

kiko katika mkono wake na dhamana yake. Akifika anaye dai na akatoa wasifu wake na akathibitisha umilikaji wake atakichukua na yeye muokotaji ataepukana wake muokoaji aliyetajwa na utakuwa umeacha mkono wake kitu hicho kwa kukisalimisha kwa mmilikaji wake halali kwa njia ya kisheria na hilo lilitokea tarehe...

‘Mtoto wa Kuokota’:

1) Maana yake:

Nacho ni mtoto aliyetelekezwa sehemu akiwa hajulikani ukoo wake wala hakuna yeyote anayedai kuwa ni wake.

2) Hukumu yake:

Inafaa kwa faradhi kifaya (kutoshana) mmoja kumchukua na kumlea kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu,

“Saidianeni juu ya wema na kumcha Mwenyezi Mungu.”

Na kwamba huyo mtoto ni nafsi yenye kuheshimiwa ambayo anapasa kuheshimiwa.

3) Hukumu za mtoto aliyeokotwa:

a) Inatakiwa mwenye kumuokota mtoto kumshuhudisha pamoja na alichomkuta nacho kikiwa chombo au mali.

b) Mtoto akiokotwa katika mji wa Kiislamu naye atakuwa Muislamu hata kama yupo na watu wasio Waislamu.

c) Cha kuokota kikikutwa pamoja na mali kitahudumiwa kutokana na mali hiyo na kama hakikutwa na mali kitahudumiwa kutoka mfuko wa Waislamu na kama hakuna mfuko wa Waislamu kitatunzwa na Waislamu.

d) Mirathi ya mtoto aliyeokotwa akifa na fidia yake akiuawa itapelekwa katika mfuko wa Waislamu (*Baytul-maal*) na imamu ndiye mtawala wake katika kulipiza kisasi na kupokea fidia. Akitaka atamlipizia kisasi na akitaka atamchukulia fidia kuipeleka kwenye mfuko wa Waislamu (*Baytul-maal*).

e) Mtu akija kukiri kwamba mtoto aliyeokotwa ni wake atakutanishwa naye (atapewa) ikiwa inawezekana kuwa mtoto wake na vile vile akimkiri mwanamke mtoto huyo atapewa.

4) Namna ya kuandika hati ya kuokota:

Fulani amemshuhudia kwamba katika wakati fulani aliingia sehemu fulani akamkuta mtoto ametupwa ardhini na sifa yake ni kadha...na kwamba yeye ni mtoto aliyeokotwa hakukuwa na mmiliki yoyote wala kinachofanana na miliki wala hakuwa na haki yoyote katika haki zinazomfikisha kwenye miliki yake. na kwamba ni mwenye kuendelea kuwa katika mikono yake kwa hukumu ya kumuokoa juu ya hukumu iliyoelezwa hapo juu. Alijua haki juu ya hilo na akaikubali na ukweli na akaufuata kwa kuwajibika kwake kisheria. Na alishuhudia hilo tarehe kadhaa.....



Mada ya Sita

‘Kumzuia’:

1) Maana yake:

Ni Kumzuia mtu kutumia mali yake kwa ajili ya utoto au wenda wazimu, uzuzu au utaahira au kufilisika.

2) Hukumu yake:

Kuzuiwa kutumia mali ni jambo la kisheria kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَمًا وَارْزُقُوهُمْ فِيهَا
وَاصْوَهُمْ

“Wala msiwape wasio na akili mali yenu ambayo Mwenyezi Mungu ameyajaalia yawe ni kiamu yenu. Walisheni katika hayo na muwavike, na msem nao maneno mazuri...” (4: 5)

Na kwa alivyofanya Mtume ﷺ,

“Kwani alimzuia Muadhi kutumia mali yake wakati alipozidiwa na madeni na Mtume ﷺ akauza mali zake na akamlipia madeni mpaka Muadhi hakubaki na chochote” (al-Hakam)

3) Sheria za Wanaozuiwa Kutumia Mali Zao’

a) ‘Mtoto mdogo’

Ni yule ambaye hajafikia balebhe hukumu yake ni kwamba matumizi yake ya fedha hayafai isipokuwa kwa ridhaa ya wazazi wake wawili au aliyeteuliwa kuwa msimamizi wa mambo yake akiwa ni yatima. Na kuzuiwa kutumia mali zake kutaendelea hadi atakapobaleghe. Madam hajadhihirika kuwa punguani na

hakuathirika nao kutaendelea kuzuiwa hadi atakapokuwa makini na akiwa aliyeusiwa ni yatima kuzuiwa kwake kutabaki hadi atakapokuwa na akili kamili baada ya kubaleghe kwake. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَأَبْتَلُوا الْيَتَامَىٰ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ فَإِنْ ءَادَسْتُمْ مِنْهُمْ رُشْدًا فَادْفَعُوا إِلَيْهِمْ
أَمْوَالَهُمْ

“Na wajaribuni mayatima mpaka wafike umri wa kuo. Mkiwaona ni wekevu, basi wapeni mali yao. Wala msiyale kwa fujo na pupa kwa kuwa watakuja kuwa watu wazima...” (4:6)

b) ‘Mbadhirifu’:

Ni mtu anayetumia ovyo mali zake kwa kuzitoa katika matamania yake au kwa matumizi mabaya kutokana na uchache wa maarifa yake kuhusu maslahi yake, atazuiwa kwa ombi kutoka kwa warithi wake au ndugu zake wa karibu na atazuiwa kutumia mali yake kwa kutoa bure au kuuza au kununua mpaka awe na akili. Na akitumia baada ya kuzuiwa matumizi yake hayo yatakuwa ni batili na hayatazingatiwa hata kidogo na matumizi aliyotumia kabla hajazuiwa yatakuwa sahihi na hakitorudishwa kitu chochote.

c) ‘Mwenda Wazimu’:

Ni yule ambaye zimeharibika akili zake na kudhoofu, kuelewa kwake kwa hiyo atazuiwa na matumizi ya mali yake hadi hapo atakapopona au ukamilifu wa akili yake utakaporudi kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Imeinuliwa kalamu kwa watu watatu (isiandike kitu (dhambi) katika hali tatu mwenda wazimu Aliyeshindwa na akili yake hadi aponena kwa aliyelala mpaka aamke na mtoto Mdogo hadi baleghe.” (Abu Dawud na Tirmidhi)

b) ‘Mgonjwa’:

Ni mtu aliyegua maradhi na inahofiwa kifo chake, warithi wake watataka azuliwe ili asitumie mali yake zaidi ya haja yake katika kula, kunywa, mavazi, makazi na dawa hadi apone au atakapofariki.

‘Kufilisiwa’:

1) Maana yake:

Kufilisiwa ni deni la mtu kumaliza chote anachomiliki mtu, hawi na mali ya kutosha kulipa deni lake.

2) Hukumu yake:

a) Mdaiwa atazuiwa kutumia mali zake pindi wadai watakapotaka kulipa madeni yao.

b) Kuuza mali zake zote anazozimiliki isipokuwa nguo zake na vitu ambavyo lazima awe navyo kama chakula na kinywaji chake kisha itagawanywa mali yake hiyo kwa wadai wake kulingana na madeni yao.

c) Atakayekuta katika wadai kitu chake kikawa khasa ndicho na kikawa hakikubadilika atakichukua mwenyewe si wale wadai wengine. Kwa kauli yake

“Mwenye kupata kitu chake kikawa ndicho chenyewe kipo kwa yule mtu aliyefilisiwa basi yule mwenyewe atakuwa na haki zaidi ya kukichukua.” (Bukhari na Muslim)

Hali hii pia imewekewa sharti ikiwa hakuchukuwa kitu chochote katika thamani yake, ni kama kachukua itakuwa ni haki ya mdai.

d) Ambaye umedhibiti uzito wake wa kutokuwa na uwezo mbele ya hakimu kwa maana hakuwa na chochote kitakachouzwa na kulipwa deni lake kwa mtu huyu haitafaa kumtaka alipe hata kumlazimisha. Kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَإِنْ كَانَتْ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ ۗ وَأَنْ تَصَدَّقُوا خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ

تَعْلَمُونَ ﴿٢٨٠﴾

“Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike. Na mkiifanya deni kuwa ni sadaka, basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua.” (2:280)

Kauli yake Mtume ﷺ kwa mmoja wenye kudai katika maswahaba zake.

“Chukueni mtakachokipata na msichukue zaidi ya hicho.” (Muslim).

e) Itakapogawiwa mali na akatokea mdai ambaye hakujua kuzuiwa mdaiwa kutumia amali zake, na kuuzwa mali za huyo aliyezuiwa mdai huyo aliyejitokeza atawarudia wadai wenzake katika haki yao ya mali waliyoigawa.

f) Aliyejua kuzuiwa kwa mali ya mdaiwa kisha yeye akawa na muamala naye hawatomgawia wale wadai wengine waliomzuia, mdaiwa kutumia mali zake. Na deni lake litabaki katika dhima ya aliyefilisiwa hadi awe na uwezo.

Namna ya kuandika hati ya kuzuiwa kwa aliyefilisiwa:

Baada ya *Bismillahi* na kumuhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu... Haya ndiyo aliyoshuhudia juu yake yeye mwenyewe kadhi wa mahakama bwana fulani kwamba amemzuia fulani kuzuia kuliko sahihi na kwa kisheria na amemzuia katika kutumia mali zake zilizoko katika mkono wake siku hiyo. Na atakayekuweko baadaye kuzuia kuliko sahihi na kisheria. Na yaliyo wajibu katika dhima yake kwa wenyewe. Madeni yaliyozidi Kiasi cha mali yake na Kiasi anachodaiwa cha fedha ni kadhaa... na uwazi wa hilo ni mali ya fulani kadhaa... kwa mujibu wa kielelezo cha tarehe yake kadhaa... na fulani kadha na amethibitisha katika deni lake kila mmoja katika wadai mbele ya mahakama kwa mujibu wa vielelezo sahihi vyenye kuzingatiwa kisheria.

Na ameapa kiapo kila mmoja kati yao na hilo limethibitika mbele ya mahakama kwa ushahidi wa kisheria kwamba mdaiwa aliyetajwa hana uwezo wa kulipa madeni yanayomkabili na kwamba alichochacho hakiwezi kulipa thamani yake

kutokana na madeni aliyonayo isipokuwa kwa njia ya kugawana na hii imethibitika kisheria. Na imehukumiwa kufilisiwa mtajwa na kusihhi kuzuiliwa na kuwekewa pingamizi kutumia mali zake hali ya kuwajibika katika hukumu hiyo. Na amempangia katika kutumia mali yake, chakula chake na anayemlazimu chakula chake akiwa ni mkewe na watoto wake nao ni fulani na fulani. . . .katika kula na kunywa na vitu vya lazima ya kila siku ambavyo ni kadha. . .hadi atakapomaliza kuuza vitu vyake na anavyovimiliki na kugawa kitachopatikana kwa wadeni kwa kadiri madeni yao kwa njia ya kisheria na hilo ni tarehe kadha. . .

Namna ya Kuandika hati kumzuia asiyekuwa na akili na mtumiaji ovyo mali yake

Baada ya *Bismillahi* na Kumuhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu. Alimshuhudisha kadhi wa mahakama kwamba yeye amemzuia fulani kuzuia sahihi na kwa kisheria na amemzuia kutumia mali yake aliyonayo kuanzia siku hiyo na atakazokuwa nazo baadaye kuzuia kwa kisheria na kunakozingatiwa baada ya kuthibitika mbele yake pamoja na ushahidi wa kisheria kwamba fulani aliyetajwa hana akili na anaharibu bure mali yake na anaitumia ovyo na anavuka mpaka katika kuitoa, katika kuiuza na katika kuinunua hivyo anastahiki kuwekewa pingamizi la kumzuia kutumia mali yake hadi itakapo kuwa hali yake ni nzuri na kuthibitika akili yake na kudhihiri kufaa kwake na kwamba maslahi yapo katika kumwekea pingamizi na kubatilisha matumizi yake na hakimu ndiye aliyehukumu hivyo na ndiye aliyemwekea kizuizi aliyetajwa na amemzuia kutumia mali yake hadi itakapokuwa nzuri hali yake na kuthibiti akili yake na kudhihiri kufaa kwake na kwamba maslahi yapo katika kumwekea kizuizi na kubatilisha matumizi yake, na hakimu ndiye aliyehukumu hivyo na ndiye aliyemwekea kizuizi mtajwa na amemzuia kutumia mali yake na amemhukumu kutokana na ujinga wake hukumu ya kisheria na amemkataza matumizi yoyote. Na amebatilisha tendo lake lolote katika matumizi yake kisheria Na ameweka fungu maalumu katika mali yake kwa ajili ya chakula chake na chakula cha ambaye inamlazimu yeye chakula chake akiwemo mkewe fulani. . . .na watoto wake wadogo nao ni. . .na mambo mengine ambayo hayana budi yapatikane kila siku kisheria kuanzia tarehe kadhaa. Na amewajibisha hilo katika mali yake kisheria baada ya kuthibiti mbele yake pamoja na ushahidi wa kisheria kwamba Kiasi hicho kinamtosha pamoja na walio naye na kwamba hakuna ziada ya kutosha kwake. Imethibitika kudhibitika kisheria imeandikwa tarehe kadhaa. . .

Mada ya Saba

‘Usia’

1) Maana yake:

Usia ni kutoa ahadi ya kusimamia kitu au kujitolea ahadi baada ya kifo na kwa maelezo haya Usia umegawika katika sehemu mbili. Aina ya kwanza ni kumuusia mtu atakayelipa deni au kutoa haki yoyote au kusimamia watoto wadogo hadi watakapokuwa wakubwa. Aina ya pili ni kuusia kitu kitakachotolewa kwa mwenye kuusiwa kwa kitu hicho.

2) Hukumu yake:

Usia ni jambo la kisheria kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:-

يَتَأْتِيَا الَّذِينَ ءَامَنُوا شَهَادَةً بَيْنِكُمْ إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ حِينَ الْوَصِيَّةِ
أَتْنَانِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ

“Enyi mlio amini! Yanapo mfikia mauti mmoja wenu na akataka kutoa wasia, basi wawepo mashahidi wawili miongoni mwenu ambao ni waadilifu.” (5:106)

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu,

مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِي بِهَا أَوْ دِينٍ^{*}

“...Haya ni baada ya kutolewa alichu usia au kulipa deni...” (4:11)

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Si haki kwa Muislamu mwenye kuusia kulala kwa muda wa siku mbili bila usia wake kuandikwa.” (Bukhari na Muslim).

Na Usia ni wajibu kwa mwenye deni au mwenye kitu kilichowekwa au mwenye haki ambaye anahofiwa kufariki na kupotea mali za watu zao akaulizwa siku ya kiyama. Kama ambavyo Usia unasuniwakwa mwenye mali nyingi na warithi wake wana uwezo wa kuusia sehemu kidogo ya mali yake ikiwa ni thuluthi au chini yake kwa ajili ya ndugu zake wasiokuwa warithi au sehemu yoyote katika sehemu za kheri. Kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume رضي الله عنه kwamba amesema:

“Anasema Mwenyezi Mungu: “Ewe mwanaadamu mambo mawili moja si lako. Nimekufanyia kuwa ni sehemu katika mali yako wakati nitakapokutoa roho ili nikutwaharishe na nikutakase na dua za waja wangu kwako baada ya kumalizika muda wako wa kuishi.” (Musnad Ibn Humayd).

Na kauli yake Mtume رضي الله عنه alipomwambia Sa’ad bin Abi Waqqas wakati alipomuuliza kuhusu Usia akasema Mtume رضي الله عنه.

“Theluthi na Theluthi ni nyingi, Hakika ewe kuwaacha warithi wako kuwa na uwezo ni bora kuliko kuwaacha maskini wanaombaombwa watu.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Tirmidhi na Abu Dawud).

3) Sharti za Usia:

Ni hizi zifuatazo:

- a) Inashurutishwa kwa muusiwa kusimamia kitu awe ni Muislamu mwenye akili timamu. Kwani kwa asiyekuwa Muislam mwenye akili hawezi kusalimika kupotea aliyopewa kusimamia katika kutekeleza haki au kuwalea watoto wadogo.
- b) Kama mtoa usia atakuwa mgonjwa basi lazima aweze kufahamu anachokusia na mwenye kuvimiliki anachokusia.
- c) Kinachotolewa usia lazima kiwe kitu cha halali; Usia hautekelezwi katika haramu kama vile kumuusia mtu atake muombolezea siku ya kifo chake au kuusia mali ipelekwe kanisani au kwenye jambo la bid-aa yenye kuchukiza au kwenye kumbi za starehe au kwenye maasi.

d) Ni sunnah kwa aliyeachiwa Usia wa kusimamia kitu au mali kukubali kama akiukataa utakuwa usia huo umebatilika na hatakuwa na haki yoyote kwa muusiwa baada ya kuukataa usia huo.

4) Sheria za Usia:

a) Inafaa kwa aliyeusia kitu baada ya kifo chake kurudi katika usia wake na kuubadilisha kama anavyotaka kutokana na kauli ya 'Umar رضي الله عنه.

“Anaruhusiwa mtu kubadili Usia wake anachokitaka.”

b) Haifai kwa mwenye warithi kuusia zaidi ya theluthi ya mali yake. Kutoka na na kauli yake Mtume ﷺ kumwambia Sa'ad Ibn waqqas alipomuuliza Je, nitoe sadaka theluthi mbili ya mali yangu? Akasema Mtume ﷺ

“Hapana, akasema je, niweke sadaka theluthi mbili ya mali yangu? Akasema Mtume hapana. Akasema Saad je, theluthi? Akasema Mtume ﷺ theluthi na theluthi ni nyingi; kuwaacha warithi wako wana uwezo ni bora kuliko kuwaacha maskini wanaombaomba tu.” (Bukhari, Muslim).

c) Haufai Usia kwa wanaorithi hata kama ni Usia mdogo mpaka upitishwe na warithi wote baada ya kufa aliyeusia. Na hilo ni kauli ya Mtume ﷺ

“Hakika Mwenyezi Mungu amempa kila mwenye haki haki yake hapana Usia kwa anayerithi ila watakapokubali wanaorithi.”
(Tirmidh)

d) Kama haikutosheleza theluthi ya kinachousiwa kitagawiwa hicho hicho kilichousiwa sawa kwa sawa kama wanavyogawiwa wadeni.

e) Hauptishwi Usia ila baada ya kulipa madeni yote kwa kauli ya Ali رضي الله عنه:

“Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alilipa deni kabla ya Usia.” (Tirmidh).

Na hiyo ni kwamba deni ni wajibu kulipa na Usia ni kujitolea na wajibu unatangulizwa kuliko sunnah.


f) Unasihi Usia kwa kitu kisichojulikana au kisichokuwepo kwani Usia ni kujitolea na hisani akipatikana sawa na kama haikupatikana inakuwa si vibaya. Na hali hiyo ni kama mtu kuusia atolewe mbuzi atakayezaliwa au mavuno ya mazao yake.

g) Inasihi kukubali Usia katika uhai wa anayeusia na baada ya kifo chake. Kama ambavyo inafaa kwa mwenye kuusia kila pale atakapokua anaogopea kupotea kitu alichokitolea Usia katika mali au hakina haki za mayatima.

h) Mwenye kuusia katika kitu maalumu itakuwa haiwezekani kutumia katika kitu kingine kwa kukosekana ruhusa kwani haisihi kisheria kutumia haki ya watu pasi na ruhusa yao.

i) Likijitokeza deni kwa maiti baada ya kutoa fungu la Usia aliyepewa Usia atakuwa hana dhamana ya deni hilo kwa sababu hakuwa akijua na hakufanya makusudi wala hakuzidisha matumizi kwa aliyoahidi.

j) Akiusia mtu juu ya kitu maalumu kisha kitu hicho kikaharibiwa hapo Usia utakuwa umebatilika wala hatolazimika mtoa (Usia kutoa kitu kingine katika mali yake).

k) Mtu atakapowausia wanaomrithi kisha baadhi ya wanaomrithi wakaacha kupitisha Usia huo na baadhi yao wakaupitisha. Kwa hali hiyo Usia utapitishwa kwa wale watakaoupitisha katika fungu la wale walioupitisha tu. Kwa kauli yake Mtume .

“Ila watakapotaka wanaorithi.”

l) Atakayesema katika Usia wake,

“Nimewausia watoto fulani kitu kadhaa na kadhaa,” itabidi kwa waliousiwa kugaiwa sawa kwa sawa waume na wake kwani tamko linajumuisha waume na wanawake kwa kauli yake

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثَيَيْنِ

“Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili.” (4:11)

Kama vile mwenye kusema, “Nimeusia kwa watoto wa kiume kadhaa... itakua kwa watoto wa kiume tu na atasema nimeusia watoto wa kike fulani kadhaa”, itakuwa kwa wanawake tu.

m) Mwenye kuandika Usia na asiushuhudishe kwa mashahidi unafaa madam kuwa yeye amerudi dhidi ya Usia wake, kwa hiyo (kama amerejea) utabatilika hautopitishwa.

Namna ya kuandika Usia:

Baada ya *Bismillahi* na Kumuhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Huu ndio Usia aliousia fulani Bin fulani... na mashahidi wake kwa aliyowausia ni wenye kujua uzima wa akili yake na uthabiti wa fahamu. Naye anakubali kwamba hapana mola ila Allah peke yake hana mshirika na kwamba Muhammad ni Mjumbe wake na kwamba pepo ni kweli na moto ni kweli vipo na Qiama kitakuja tu hakina shaka na kwamba Mwenyezi Mungu atawafufua walio katika makaburi. Amemuusia mtoto wake na mkewe na ndugu zake kumcha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumtii na kushikamana na sheria zake na kuhuisha dini yake na kufa juu ya Uislamu kama alivyousia Allah amsamehe na amuhurumie kwamba yeye atakapofikwa na mauti, maandiko ya Mwenyezi Mungu juu ya viumbe wake, vikusanywe vitu vyake vyote alivyoviacha na kitakachoanza kutokana na mali hiyo iliyoachwa ni gharama za kumuandaa maiti na kumtia sandani na kumzika kisha alipiwe madeni ya kisheria yaliyo katika dhima yake na ambayo aliyakubali mbele ya mashahidi wake nayo ni kiasi kadhaa na itolewe theluthi ya mali yake ambayo ni kadhaa apewe fulani kisha kilichobakia atakigawa kwa wanaorithi ambao ni fulani na fulani juu ya mafungu aliyoyagawa Mwenyezi Mungu Mtukufu na ameusia kuangaliwa watoto wake wadogo nao ni fulani na fulani na awahifadhie vinavyowahusu watoto hao katika mali yao alizorithi mpaka watakapofikia baleghe na kuwa na akili yote timamu hayo amemuusia yeye na matunzo katika yaliyotajwa

Minhajil Muslim

baada ya Mwenyezi Mungu ni juu yake kwa ufahamu wake wa dini yake na uaminifu wake na uadilifu wake na uwezo wake yote hayo ndiyo yalio mfanya amuegemezee anayemtaka na awausie watoto wake kwa aliyempenda na amekubali usia uliotajwa katika Baraza la Wasia na mbele ya mashahidi kukubali kisheria na amewashuhudisha hilo na kusainiwa Usia huu kumefanyika baada ya kumalizwa kuandikwa na kuusoma tarehe kadhaa...



Mada ya Nane

‘Waqfu’:

1) Maana yake:

Waqfu: Ni kuzuia kitu cha asili kikawa hakirithiwi wala hakiuzwi wala hakitolewi; na hutolewa kitu hicho matunda (na tija) yake kuwapa wale waliowekewa waqfu.

2) Hukumu yake:

Waqfu ni sunna na limetiliwa mkazo na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu.

إِلَّا أَنْ تَفْعَلُوا إِلَىٰ أَوْلِيَآئِكُمْ مَعْرُوفًا كَانَ ذَٰلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا ﴿٦﴾

“Ila muwe mnawafanyia wema marafiki zenu. Haya yamekwisha andikwa Kitabuni...” (33: 6).

Na kauli yake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ

“Mtu anapokufa matendo yake yote yanakatika ila mambo matatu sadaka ya kuendelea au ilimu yenye kunufaisha au mtoto mwema atakae muombea dua.” (Muslim).

Na katika sadaka yenye kuendelea ni kuweka waqfu majumba na ardhi na misikiti na vitu vingine.

3) Sharti za Waqfu:

a) Mtoaji waqfu awe na haki ya kumiliki anachokiwekea wakfu na akili yake iwe kamili.

b) Mwenye kuwekwa Waqfu –kiwe ni chenye kujulikana na –ni ambacho kunasihi kumiliki kwake hawekewi wakfu mtoto ambaye hajazaliwa bado yuko tumboni wala Mtumwa aliyemilikiwa. Na waqfu unawekewa pande isiyojulikana

itashurutiwa iwe pande inayowekewa waqfu iwe katika mambo ambayo inafaa kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu hivyo haitosishi kuweka waqfu juu ya vitu vya anasa au kanisa au vitu vya haramu.

c) Kuweka waqfu kuwe ni kwa maneno yaliyo wazi kama vile kutumia maneno waqfu au habsi au kutoa sadaqa.

4) Hukumu zake: Hukumu za Wakfu ni hizi

a) Inasihi Waqfu Kuwekea watoto. Atakaposema nimewawekea waqfu watoto wangu neno hilo linakusanya watoto wa kiume na wa kike. Kama ambavyo linakusanya watoto wa kiume tu. Na akisema: Nimewawekea waqfu watoto wangu na walio baada yao neno hili linakusanya watoto wa kiume na wa kike. Akisema nimewawekea wakfu watoto wa kiume itakuwa ni watoto wa kiume tu. Kama ambavyo angesema watoto wangu wa kike. Ingekuwa kwa wanawake tu. Yote haya ni pale itakapofahamika matumizi ya maneno haya na kama hayafahamiki yatakuwa hayana maana.

b) Maneno hayo yakubaliane na sharti aliyotoa muweka wakfu, katika sifa au kutanguliza au kuchelewesha. Laiti angesema nimeweka kadha kwa mwanachuoni wa hadithi au wa fiqhi, tamko hilo halitambusu isipokuwa mwanachuoni mwenye sifa husika awe wa *nahwu au 'arudhi* (Elimu ya mashairi-Mfasiri) au nyenginezo. Kama angesema nimeweka waqfu kadha kwa watoto wangu kisha watoto wao na watoto wao kisha akasema watoto tabaka la juu linazuia tabaka la chini itakuwa kama alivyosema tabaka la chini halitokuwa na haki yoyote katika waqfu mpaka liishe tabaka la juu. Laiti aliweka waqfu kitu chochote kuwawekea ndugu watatu na akafa mmoja wao nae akawaacha, watoto wake hao hawatopata fungu la baba yao bali fungu la marehemu litarudi kwa ndugu zake wawili waliobakia muda wa kuwa muweka waqfu ameweka sharti ya tabaka la juu lilizuie tabaka la chini.

c) Waqfu hautafaa baada ya hapo kuubadilisha wala kuuzwa wala kuutoa bure

d) Yakiharibika manufaa ya waqfu kwa kubomoka baadhi ya wanachuoni wamejuzisha kuuza waqfu huo. Na kuipeleka thamani yake katika kitu kinachofanana nacho na kikizidi kitu chochote kitatolewa msikitini au kitatolewa Sadaka kupewa mafukara na masikini.

5) Namna ya kuandika Waqfu

Baada ya *Bismililahi* na kumuhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Fulani amemshuhudia kwamba aliweka *waqfu* na amefunga na ameiweka mkononi mali itakayotajwa, inaendelea baada ya hayo katika mkono wake na miliki yake na matumizi yake na hiyaza yake na ndiye muhusika mpaka muda ulipotoka waqfu huu na kilichothibitika ni kwamba hiyo mali ni yake kwa ushahidi wa namba yake kadha...na ni ya kwake kwa kurithi kutoka kwa baba yake na umezuiwa kuzuiwa kwa wazi kwenye sheria, hauuzwi, hautolewi bure, haurithiwi, hauwekwi rehani, haumilikiwi wala haubadilishwi ila kwa mfano wake yatakapokosekana manufaa yake kwa uhalali wake katika jambo hili radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na hali ya kufuata sheria za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Haubadilishwi kwa kurefuka kwa zama wala hauinyongeshi kutofautiana kwa zama bali kila inapofika na zama uzidi kuudhihirisha na kuuthibitisha.

Fulani mtoa waqfu ameanzisha azipitisha kheri Mwenyezi Mungu juu ya mikono yake Waqfu wake huu juu ya kadha Kwa msimamizi katika waqfu huu na anayeutawalia ataanzia ardhi ya wakfu pamoja na jengo lake na kulikarabati na kulitengeneza ile asili yake libaki na ili lipatikane kusudio la mtoa wakfu na kuzidi mavuno yake na kinachozidi baada ya kutekeleza maagizo ya waqfu –kitatolewa kwa sehemu zilizotajwa hapo juu nazo ni kadha. Itabakia hivyo mbele na milele mpaka atarithi Mwenyezi Mungu ardhi na vilivyo juu yake naye ndiye Mbora wa wenye kurithi. Na mwisho wa waqfu huu wakati wa kukatika njia zake zote na kuwa kuzito kuwafikia mafakiri na masikini katika umma wa nabii wetu Muhammadi ﷺ.

Sharti la kuweka waqfu aliyetajwa ni kuangalia waqfu wake huu na kusimamia yeye mwenyewe muda wa uhai wake peke yake hashirikiani na yeyote wala hana mpinzani anayeweza kuusia na kuuweka kwa yeyote anayemtaka kisha baada ya kufa kwake uhamie kwa mtoto wake fulani...au mwenye akili zaidi katika watoto wake navizazi vyake na walio baada yake katika vizazi vyake na walio baada yake katika watu wa waqfu waliotajwa. Na wakiisha wote na ikawa hakubaki hata mmoja usimamizi utakuwa kwa fulani...sharti ya muweka wakfu aliyetajwa ni kwamba usikodishwe wakfu wake huu wala kitu chochote katika

Minhajil Muslim

waqfu huo kwa zaidi ya mwaka na asiingie aliyekodi bei juu ya bei nyingine mpaka umalizike muda wa bei ya mwanzo na kurudi kilichokodiwa kwa msimamizi wake na amri yake.

Muweka waqfu ametoa kutoka katika miliki yake na amekata kutoka sehemu ya mali yake. Na ameufanya ni sadaqa moja kwa moja na milele yenye kupita katika waqfu uliotajwa juu ya hukumu ya kisheria iliyosimamishwa hapo juu kihali na mali kwa kutowezekana na kuwezekana na ameondosha umiliki wake, na ameweka mkono wa mwangalizi na utawala wake.

Hakika umetimia waqfu huu, umelazimu na umepita hukumu yake na yamepitishwa mapatano yake na umekuwa ni waqfu katika waqfu za Waislamu. Si halali kwa yeyote kuutengua waqfu huu au kuubadilisha au kuuharibu au kusimamisha kwa jambo lolote lile wala kwa fat-wa wala kwa ushauriano wala kwa hila yoyote na hali ya kuwa yeye anamtaka msaada Mwenyezi Mungu Mtukufu juu ya mwenye kukusudia waqfu wake huu kuuharibu au kuufanyia uadui na umuhukumu na agombane naye siku ya ufakiri wake, umasikini wake, udhalili wake siku ambayo hautowanufaisha watu wabaya udhuru wao na wana laana na wana makazi mabaya. Amekubali muweka waqfu aliyeashiriwa mali yake kisheria na ameishuhudisha nafsi yake kwa hilo na yeye yuko katika hali nzuri ya kifya na salama na kwa ruhusu yake na hiyari yake na kufaa jambo lake kisheria.

Limeandikwa tarehe...



Mada ya Tisa

‘Hiba’, ‘Umra’, ‘Ruqba’

‘Hiba’

1) Maelezo yake:

Hiba ni kujitolea kwa mtu mwenye akili kitu anachokimiliki iwe mali na vitu vilivyoko halali kama vile Muislamu kumpa Muislamu mwenzake ikiwa nyumba au nguo au chakula au ampe pesa.

2) Hukumu yake:

Hiba ni kama zawadi nayo ni mambo mazuri kwani hizo ni katika kheri inayosisitizwa kufanya na wanatakiwa watu washindane katika haya kwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ^ع

“*Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda...*” (3: 92).

Na

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَى

“*Saidianeni juu ya wema na kumcha Mwenyezi Mungu.*” (5:2)

Na

وَأَتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَابْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ

“*...na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao....*” (2: 177).

Kauli yake Mtume ﷺ

“Peaneni (zawadi) mtapendana na peaneni mikono zitawaondokeen chuki.” (Malik na al-Baihaqi)

Kauli yake Mtume ﷺ

“Mwenye kukirudia kitu chake alichokitoa ni sawa na mtu aliyerudia matapishi yake.” (Imepokewa na Bukhari, Abu Dawud na Nasai).

Na kauli ya mama Aisha رضي الله عنها

“Alikuwa Mtume ﷺ anapokea zawadi na alikuwa anakilipa.” (Bukhari).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Ambaye inamfurahisha kukunjuliwa riziki yake na kuongezewa umri wake na aunge udugu wake.” (Bukhari).

3) Sharti za Hiba

a) Ni tamko la kutoa litokalo kwa mtoaji kumpa aliyemuomba kitu na kumpa kwa ridhaa ya nafsi.


b) Tamko la kukubali nako ni kukubali yule aliyepewa hiyo hiba kwa kusema nimekubali ulichonipa au akawa anampa kwa mkono wake na mpewa akapokea. Kwani lau kwamba Muislamu ametoa kitu au ametoa bure kitu hicho kumpa yeyote na akawa hakukipokea mpewaji mpaka amekufa mtoaji hakika kitu hicho kitabaki kuwa katika haki ya warithi si haki ya yule aliyepewa hiba hiyo kwa kukosekana sharti yake ambayo ni kukubali kwani lau angekikubali angekipokea.

4) Hukumu za Hiba: Hukumu za hiba ni hizi:

a) Ikiwa kilichotolewa ni cha mmoja wa watoto itakuwa vizuri kuwapa watoto wengine mfano wa kitu hicho kwa kauli yake Mtume ﷺ *“Mcheni Allah na fanyeni uadilifu kwa watoto wenu”*

b) Niharamu kurudia hiba kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mwenye kurudia katika hiba yake ni kama mwenye kurudia matapishi yake.” (Imepokewa Bukhari, Abu Dawud na Nasai).


Ila itakapokuwa hiba inatokana na mzazi kwa mtoto wake. Kwani mtoto na mali yake ni mali ya mzazi wake kwa kauli yake Mtume .

“Si halali kwa mtu kutoa kitu halafu akakirudia isipokuwa mzazi kwa anachompa mtoto wake.” (Ibn Majah na al Hakam).

c) Ni makuruhi hiba ya thawabu (ziada), nayo ni Muislamu kumpa mwenzake kitu ili baadae amlipe zaidi ya alichompa. Kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَا آتَيْتُمْ مِّن رَّبًّا لَّيْرُبُوا فِي أَمْوَالِ النَّاسِ فَلَا يَرْبُوا عِنْدَ اللَّهِ وَمَا
آتَيْتُمْ مِّن زَكَاةٍ تُرِيدُونَ وَجْهَ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُضْعِفُونَ ﴿٣٩﴾

“Na mnacho kitoa kwa riba ili kiongezeka katika mali ya watu, basi hakiongezeki mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini mnacho kitoa kwa Zaka kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi hao ndio watao zidishiwa.” (30: 39).

Anayepewa ana khiari kukubali na kuikataa na akikubali yampasa kumlipa alichompa kama aliyompa au amlipe zaidi. Kwa kauli yake Aisha .

“Alikuwa anakubali zawadi na analipa.” (Bukhari).

Kauli yake Mtume .

“Mwenye kutendewa wema na akimwambia aliyemtendea wema, Mungu akulipe kheri atakuwa amefanya vizuri zaidi katika kusifu.” (Nasai).

Namna ya kuandika Hiba:

Baada ya *Bismillahi* na kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu. Fulani ametoa hiba ambaye ni balebhe mwenye akili katika hali ya uzima wake na kufaa matumizi

yake. Hiba hiyo kampa fulani sehemu yote iliyowekewa mipaka ambayo ni kadha. . . wanajua wote wawili kujua kwa kisheria kutoa kwa kisheria pasi nabadili wala hiba nayo imekusanya makubaliano kwa matamshi (ijabu-tamko la kutoa-na *kabuli*-tamko la kukubali) na mtoaji ameacha kati ya Usia na aliyepewa hiba kuacha kwa kisheria na imepaswa kwa hilo kuukabidhi na kuwa hiba iliyotajwa ni miliki katika miliki zake na ni haki katika haki zake na hio ilikuwa ni tarehe kadha. . .

Tanbihi:

Itakapokuwa hiba inatoka kwa mzazi kwenda kwa mtoto itasemwa katika hiba hiyo. Amekubali hilo mtoa hiba aliyetajwa kwa nafsi yake kumpa mtoto wake aliyetajwa kumpa kisheria na imekuwa ni hiba iliyotajwa juu yake. Na imeshakuwa miliki katika miliki za moto wake mdogo aliyetajwa na ni haki katika haki zake na imefika kwa hilo katika mkono wa mzazi aliyetajwa na umiliki wake ni kwa mtoto wake fulani. Hilo lilitimia tarehe. . .

‘Al-Umri’

1) Maelezo yake:

‘Umri ni kusema Muislamu kumwambia ndugu yake Muislamu nimekupa nyumba yangu muda wa umri wako au bustani yangu au nimekupa hiba bure kukaa nyumba yangu au mavuno ya bustani yangu muda wa umri wako au uhai wako wote.

2) Hukumu yake:

‘Umri inafaa kwa kauli yake Jaabir رضي الله عنه.

“Hakika umri alioruhusu Mtume ﷺ ni mtu kusema: “Mali hii ni yako na walio baada yako ama akisema mali hii ni yako utakavyoishi hakika mali hiyo itarudi kwa mwenyewe.”

3) Sheria zake:

a) Tamko lake likiwa la moja kwa moja kwa kusema: nimekupa nyumba hii muda wa umri wako. Nyumba hiyo itakuwa kwa huyo aliyepewa na walio baada yake kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Umri ni kwa yule aliyepewa.” (Imepokewa Muslim, Abu Dawud na Nasai).

Vile vile akilihusisha neno lake kwa tamko: ‘Hiyo ni yako na watoto wako baada yako’, itakuwa ni ya kwake na ya watoto wake baada yake wala hatorudisha *umra* huo kwa aliyeutoa kwa hali yoyote. Kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Mtu yeyote aliyetoa umra kumpa mtu na watoto wake ‘umri huo utakuwa ni wa yule aliyepewa hatorudi kwa yule aliyetoa kwa sababu Ameshatoa kitu ambacho mambo ya mirathi yameishaingia.” (Imepokewa na Abu Dawud, An-Nisai, Tirmidhi).

b) Ukihusishwa *umra* kwa kutumia tamko: “Ni wa kwako muda wa uhai wako na ukifa utarudi kwangu au kwa watoto wangu walio baada yangu.’ Hakika *umra* huo utarudi kwa mtoaji baada ya kufa aliyepewa *umra* kwa kauli ya Jaabir رضي الله عنه ,

“Hakika umra alioruhusu Mtume ﷺ ni kusema huo ni wa kwako na walio baada yako ama akisema: huo ni wa kwako katika maisha yako katika ‘umri huo utarudi kwa mwenyewe.”

‘Ruqba’:

1) Maelezo yake:

‘*Ruqba*’ ni Muislamu kumwambia Muislamu mwenzake nikifa kabla yako hii nyumba yangu ni ya kwako au bustani yangu, kwa mfano na ukifa wewe kabla yangu nyumba yako itakuwa yangu au sehemu hii ni ya kwako katika umri wako ukifa kabla yangu na nikifa mimi kabla yako itakuwa ya kwako yakawa mauti kwa mmoja wao.

2) Hukumu yake:

Ruqba ni makruhu kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Msiweke masharti ya kufa katika kupeana vitu. Mwenye kutoa kitu kwa kuweka sharti la kifo kitu hicho ni njia ya mirathi”
(Imepokewa na Ahmad, Abu Dawud, Ibn-Majah na An-Nasai).

Pia kufanya hivyo ni kungojea mauti ya yule mwenye kitu. Huenda ikampelekea yule mwenye kuwekewa kile kitu kutamani kumuua yule ndugu yake aliyeweka kitu. Bali huenda akajitahidi kusababisha kifo chake na Mwenyezi Mungu atukinge dhidi ya hili na kwa ajili hiyo wamechukia wanachuoni hiyo *ruqba*.

3) Sheria za Ruqba

Muislamu atakapofanya jambo hilo la makuruhu hakika *ruqba* itapita juu ya hukumu za *umra*. Akitaja kwa tamko pana itakuwa ni ya yule aliyemwekea *ruqba* na watoto wake baadaye na akihusisha itakuwa kwa waliohusishwa. Na akiweka masharti ya kurudi utarudishwa baada ya kufa aliyemuhusisha na kama hakuweka masharti hautorudishwa.

4) Namna ya Kuandika ‘Umri au Ruqba:

Baada ya *Bismillahi* na kumuhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumtakia Rehma na Amani Mtume Wake ﷺ.

Hakika fulani ameweka umri au ruqba kumwekea fulani nyumba yake au bustani iliyotajwa iliyoko kadha... Kuweka umra au ruqba kisheria na sahihi kwa kumuambia: Nimekuwekea muda wa umri wako au nimekuwekea kwa sharti la kifo kitu kadha... ukifa kitu hicho kitarudi kwangu na akitaja walio baada yake baada ya kufa kwake na akampa mtoaji kumpa aliyemuwekea itakuwa ni yake nyumba yote iliyotajwa na aliyewekewa akaipokea kisheria na ikawa katika mkono wa aliyepewa aliyetajwa akaitumia kwa kukaa au kukalisha watu wengine na kunufaika muda wote wa uhai wake, ushahidi umepita na saina juu ya hilo tarehe kadha...



**Kuhusu Ndoa, Talaka, Rejea, Khulu, Liaani,
Al-Iyilaau, Dhihaar, ‘Eda’ ‘Matumizi ya
Mke na Malezi’**

Mada ya kwanza:

‘Ndoa’

1) Maana yake:

Nikah au *Ziwaji* ni makubaliano yanayomuhallalishia kila mmoja wa wanandoa wawili kustarehe na mwenziwe.

2) Hukumu yake:

Ndoa ni kitu kilichosisitizwa sana kisheria kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu.

وَأِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ
مَثْقَىٰ وَتَلْتَّ وَرَبَعٌ ۗ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةٌ أَوْ مَا مَلَكَتْ
أَيْمَانُكُمْ ۚ ذَلِكَ أَدْنَىٰ ۗ أَلَّا تَعْلَمُوا ﴿٤٣﴾

“Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia mayatima uadilifu, basi oeni mnao wapenda katika wanawake, wawili au watatu au wane. na mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki. Kufanya hivi ndiko kutapelekea msikithirishe wana.” (4:3).

Kauli yake Mwenyezi Mungu:

وَأَنْكِحُوا الْأَيْمَىٰ مِنْكُمْ

“Na waozeni wajane miongoni mwenu (Waislamu)” (24:32).

Minhajil Muslim

Isipokuwa inawajibika ndoa kwa mtu anayeweza gharama zake, na akahofia nafsi yake kuingia katika jambo lililoharamishwa. Ni sunnah kwa mtu anayeweza (gharama za kuoa) na akahofia zinaa, kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ,

“Enyi makundi ya vijana mwenye kuweza gharama za kuoa miongoni mwenu, basi na aoe, kwani kuoa kunafumbisha jicho na kunahifadhi tupu.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, An-Nasai).

Kisha Mtume ﷺ akasisiiza tena,

“Waoeni wenye upendo, wanaozaa, kwa hakika mimi nitajifaharisha kwa wingi wenu siku ya Qiama.” (Ahmad).

3) Hekima yake:

Miongoni mwa hekima za ndoa:

- a) Kubakisha/kuendeleza aina ya binadamu, kwa kuzaaana kunakotokana na ndoa sahihi na halali.
- b) Ni haja ya kila mmoja wa wanandoa wawili kwa mwenziwe, ili kulinda tupu yake kwa kukidhi matamano ya kimaumbile.
- c) Kila mmoja wa wanandoa wawili kusaidiana juu ya kulea kizazi na kulinda afya yake.
- d) Kujenga mahusio mazuri kati ya mwanaume na mwanamke, juu ya msingi wa kubadilishana haki na kusaidiana kunakozaa matunda, katika mzunguko wa mapenzi, heshima, kuthaminiana na kuhurumiana.

1. Nguzo za ndoa:

Ili ndoa isihii lazima zikamilike nguzo nne ambazo ni:

- a) ‘Walii’: Awepo baba wa mke muolewaji, wakili (muwakilishi), ndugu wa karibu zaidi, na anayefuatia ukaribu katika aswaba zake, au wenye rai/busara njema katika jamaa zake, au mtawala/sultani, kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ

“Hapana ndoa bila ya walii.” (Imepokewa na Abu Dawud, Tirmidhi na Hakim).

Na kauli ya Umar رضي الله عنه:

“Mwanamke haolewi isipokuwa kwa idhini ya walii wake, au mwenye rai njema katika jamaa zake, au sultani.” (Muwatta Imam Maliki).

Hukumu zinazomuhusu ‘Walii’:

Walii anatakiwa kutimiza mambo muhimu yafuatayo:

i) Awe na sifa za utawala, awe mwanamume, baleghe, mwenye akili timamu, muungwana, aliyeongoka (mwenye busara).

ii) Kumtaka idhini yule binti anayemtawalia kuhusu yule anayetaka kumuoza, kama mtawaliwa ni bikra, na walii akawa baba mzazi, atamtaka amri yake, yaani atataka amri yake kama ni mke mkubwa (asiyebikira), au alikuwa bikra na walii akawa si baba mzazi. Kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ:

“Mke mkubwa ana haki zaidi ya nafsi yake kuliko walii wake na bikra hutakiwa amri na amri yake ni kunyamaza kwake.”
(Ameipokea Malik katika Muwatta)

iii) Uwalii wa karibu hautasihi pamoja na kuwepo wa karibu zaidi yake na wala hausihii uwalii wa kaka wa baba mmoja, pamoja na kuwepo wa baba mmoja; na mama mmoja. Wala hausihii uwalii wa mtoto wa ndugu pamoja na kuwepo ndugu.

iv) Mwanamke atakapotoa idhini kwa watu wawili miongoni mwa nduguze ili kumuozesha, na kila mmoja akamuozesha kwa mtu, basi yeye ni wa yule wa kwanza. Na ikitokea kufungisha ndoa katika wakati mmoja, basi ndoa yake imebatilika kabisa kwa wote wawili pamoja.

b) ‘Mashahidi Wawili’:

Makusudio ya mashahidi: kuwepo watu wawili au zaidi katika fungisho la ndoa, miongoni wa wanaume waadilifu.

وَأَشْهِدُوا ذَوَىٰ عَدْلٍ مِّنكُمْ

“Na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu.” (65: 2)

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Hapana ndoa isipouwa kwa walii na mashahidi wawili waadilifu.” (wameipokea Daruqutni na Baihaqi).

Hukumu ya Mashahidi wawili, na miongoni mwa hukumu za nguzo hiii ni:

i) Ni kuwa wawili au zaidi.

ii) Ni kuwa waadilifu wawili, uadilifu unaopatikana kwa kujiepusha na madhambi makubwa, na kuacha aghlabu ya dhambi ndogo ndogo. Hivyo basi mtu *fa-siki* (‘asi) kwa zinaa au pombe, au kula riba hauswahi ushahidi wake, kwa kauli yake Mtukufu,

“Wenye uadilifu miongoni mwenu.”

Na kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Na mashahidi wawili waadilifu.” (Baihaqi).

iii) Inakuwa vizuri kufanya wingi wa mashahidi kwa sababu ya uchache wa uadilifu katika zama zetu hizi.

c) **‘Swiygah’, tamko la kufungisha ndoa:**

Tamko la kufungisha ndoa ni kauli ya mume au wakili wake katika kufunga ndoa, “Niozeshe Binti yako, au Muusiwa wako fulani . . .na kauli ya walii.” “Nimekuoza au nimekuozesha Binti yangu fulani . . .”, na kauli ya Mume, “Nimekubali ndoa yake kwa nafsi yangu.”

Hukumu Zake:

Nguzo hii ina hukumu zifuatazo:

i) Kuwepo uwiano wa mume na mke, kwamba awe muungwana, mwenye tabia njema, Dini, na Uaminifu, kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ,

“Atakapokujieni ambaye mnamridhia tabia yake na dini yake, basi muozeni, na msipofanya hivyo basi itakuwa fitna na ufisadi mkubwa katika ardhi.” (Tirmidhi).

ii) Uwakala unasihi katika kufunga ndoa, mume anaruhusiwa kumpa uwakala mtu amtakaye. Ama mke, walii wake ndiye ambaye atakayetawalia kufungisha ndoa yake.

d) ‘Mahari’:

Mahari au “*Swadaaq*” ni kile anachopewa mwanamke ili kuhalalika kustarehe naye. Mahari ni wajibu kwa kauli ya Allah Mtukufu.

وَأَتُوا النِّسَاءَ صَدُقَاتِهِنَّ نِحْلَةً فَإِنْ طِبْنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ

هَنِيئًا مَّرِيئًا ﴿٤﴾

“Na wapeni wanawake mahari yao hali ya kuwa ni kipawa. Lakini wakikutunukieni kitu katika mahari, kwa radhi yao, basi kileni kiwashuke kwa raha.” (4: 4).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Tafuta japokuwa pete ya chuma.” (Bukhari na Muslim).

Hukumu zake:

i) Inapendeza mahari kuwa kidogo, kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ,

*“Wanawake wenye baraka kubwa ni wale wenye mahari nyepesi/
kidogo kati yao.” (Ahmad na Hakim).*

Mahari ya Binti zake Mtume ﷺ ilikuwa Dirham mia nne au mia tano, na hivyo hivyo ndivyo ilivyokuwa mahari ya wakeze Mtume ﷺ.

ii) Inasuniwa kutaja mahari wakati wa kufungisha ndoa.

iii) Inasihhi kuwa mahari kila kitu kitachokuwa mali, cha halali, thamani yake inazidi robo Dinari, kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ.

“Tafuta japakuwa ni pete ya chuma”.

iv) Inasihhi kuyaharakisha sambamba na kufunga ndoa.

Inasihhi pia kuyachelewesha, au baadhi yake kuichelewesha, na baadhi yake kulipia papo hapo, kauli yake Allah Mtukufu,

وَإِنْ طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَنِصْفُ
مَا فَرَضْتُمْ

*“Na mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha
wawekea hayo mahari makhsusi, basi wapeni nusu ya mahari
mlio agana.” (2:237).*

Isipokuwa inasuniwa kumpa kitangulizi kabla ya kumuingilia kimwili, kutokana na aliyoyapokea Abu Dawud na An-Nasai –Allah awarehemu kwamba Mtume ﷺ alimuamuru Ali رضي الله عنه kumpa Fatma kitangulizi kabla ya kumuingilia kimwili, akasema,

*“Sina kitu, akasema: Iko wapi diraya yako? ile (Nguo yako ya
vita?) Basi akampa nguo yake ya vita.”*

v) Mahari inafungamana kwenye dhima (shingo) muda wa kufunga ndoa, na huwajibika kwa kumuigilia kimwili yule mwanamke. Iwapo mume atamuacha

mke kabla ya kumingilia kimwili basi nusu ya mahari itaondoka na itabakia nusu yake, kwa mujibu wa kauli yake Allah Mtukufu.:-

وَإِنْ طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَنِصْفُ مَا فَرَضْتُمْ

“Na mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea hayo mahari makhsusi, basi wapeni nusu ya mahari mlio agana.” (2: 237).

vi) Akifa mume kabla ya kumingilia huyo mke na baada ya kufunga ndoa, (huyo mke) itamthibitikia mirathi na mahari kamili, kutokana na Mtume ﷺ kuhukumu hivyo, ikiwa aliwahi kumtajaia (Kiasi cha) mahari. Na kama hakuwahi kumtajaia basi atastahiki mahari ya mfano wake na itawajibika juu yake kukaa eda ya kufiwa.

5). ‘Adabu za ndoa na sunna zake:

a) ‘Khutbah’:

Nayo ni kusema:

“Kila sifa njema anastahiki Allah tunamuoba msaada yeye, na tunamuomba msamaha Na tunajilinda kwa Allah, kutokana na shari za nafsi zetu na kutokana na matendo yetu maovu, mwenye kumuongoa Allah hapana wakumpotoa, na anaemwacha kupotea hapana wa kumuongoa, na nakiri kwa moyo nakutamka kwa ulimi kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na nakiri kwa moyo na natamka kwa ulimi kwamba Muhammad ni Mtumwa Wake na Mjumbe Wake.”

Kisha atasema,

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اتَّقُوا اللّٰهَ حَقَّ تُقَاتِهٖۙ وَلَا تَمُوْنُوْا اِلَّا وَاَنْتُمْ مُّسْلِمُوْنَ ﴿١٠٢﴾

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu...” (3: 102).

Na

يَتَأْتِيَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمْ

“Enyi watu mcheni Mola wenu...” (4: 1)

Na

يَتَأْتِيَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ

وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya sawasawa. Apate kukutengenezeeni vitendo vyenu na akusameheni madhambi yenu. Na anaye mt’ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.” (33: 70-71).

Kutokana na yaliyopokewa kuwa Mtume ﷺ amesema,

“Anapotaka mmoja wenu kuhutubu kwa ajili ya haja kama ni ndoa au jambo jingine basi na aseme: “Kila sifa njema anastahiki Allah...” (As-haab As-Sunan).

b) ‘Walima-Karamu’:

Walima ni chakula cha harusi. Kwa kauli ya Mtume ﷺ, kumwambia ‘Abdur Rahman bin ‘Awf رضي الله عنه alipooa.

“Fanya walima japo kuwa mbuzi.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim na Tirmidhi).

Walima ni chakula cha harusi na ni wajibu kwa aliyealikwa kuhudhuria, kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Mwenye kualikwa katika (chakula cha harusi) au mfano wake, basi aitikie wito.” (Muslim).

Inaruhusiwa kutokuhudhiria *Walima* kama ikiwa kuna vitu vya kipuuzi au vitu batili. Mtu akialikwa na wawili basi na aitikie ule wito wa mwanzo, na hualikwa katika chakula hicho masikini kwa matajiri; kwa neno lake Mtume ﷺ:

“Ubaya wa chakula ni walima hukatazwa wanaokuja, na hualikwa wasioitikia.” (Muslim).

Atakayealikwa na hakuitikia mwaliko atakuwa amemuasi Allah Mtukufu na Mtume ﷺ wake, na atakayealikwa na hali ya kuwa amefunga basi ataitika wito na akitaka atakula kama hiyo funga yake ni ya sunna na anaweza kuwaombea dua tu kisha kuondoka. Kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Atakapoitwa mmoja wenu katika chakula cha walima) basi na ajibu. Kama akiwa amefunga basi aombe dua, na kama hakufunga, basi ale.” (Muslim).

c) ‘Kuitangaza ndoa kwa Dufu’ na nyimbo halali:

Kwa mujibu wa kauli yake Mtume ﷺ,

“Utenganisho uliopo kati ya halali na haramu ni dufu na sauti.”
(Wameipokea wanazuoni wa vitabu ya Sunnah).

d) ‘Dua kwa wanandoa wawili:

Kwa kauli ya Abu Hurayra رضي الله عنه,

“Kuwa Mtume ﷺ alikuwa akioa mmoja wa watu akiwaombea dua hii: “Baaraka Allahu laka wabaaraka alayka, wajama-a bainakuma - fil-khayri.” (Tirmidhi)

(Mwenyezi Mungu abariki kwa ajili yako (mke huyo, na abariki, juu yako, awaunganisheni katika kheri)

e) Kumuingilia katika Mwezi wa mfungo Mosi:

Kwa kauli ya Aisha رضي الله عنها,

“Mtume ﷺ alinioa katika mwezi wa shawwal (Mfungo Mosi) na akaniingilia katika mwezi (huo huo) wa Mfungo Mosi. Ni mwanamke gani alipata bahati kuliko mimi? Na alikuwa akihimiza kuingilia wakeze katika mwezi wa Shawwal.” (Muslim).

f) Akiingia kwa mkewe amshike utosini

Na kusema kulingana na mafundisho ya Mtume ﷺ

“Ewe Mola hakika na kuomba miongoni mwa kheri zake, na kheri za tabia aliyoubiwa, na najilinda na shari zake na shari za tabia aliyoubiwa.” (Ibn Majah na Tirmidhi).

g) Atasema wakati anapotaka kumuingilia “Kwa jina la Allah, ewe Mola niepushe na shetani, na kiepushe na shetani ulichoturuzuku”, kutokana na yaliyopokewa kwake Mtume ﷺ kwamba yeye amesema:

“Mwenye kusema...hadi mwisho Ikiwa patakadiriwa kati yao mtoto, basi huyo mtoto hatodhuriwa na shetani kamwe.” (Muslim).

h) Ni haramu kwa wana ndoa wawili kueneza siri zao.

Ni haramu kueneza kwa watu yale yaliyojiri kati yao miongoni mwa matukio ya kuingiliana. Kutokana na kauli ya Mtume ﷺ

“Kwa hakika miongoni mwa watu waovu sana kwa hadhi mbele ya Allah Siku ya Qiyama ni mwanaume anaemuingilia mwanamke, nae mwanamke anaingiliana na mwanaume, kisha wanaeneza siri zao.” (Muslim).

6) Masharti ya Ndoa

Huenda pengine mke akaweka masharti au vikwazo juu ya huyo anayetaka kumposa, masharti maalumu ndipo amuo mtu huyu. Ikiwa hayo anayo yalazimisha ni miongoni mwa mambo yanayoimarisha ndoa na kuipa nguvu, nayo ni kama vile kulazimisha kumpa chakula, na kumuingilia au kumgawia zamu kama huyo

mchumba tayari ana mke mwingine, basi sharti hili linapita kwa ajili ya kufunga ndoa wala hapana haja nalo.

Na kama sharti hilo ni miongoni mwa masharti yanayoharibu ndoa kama vile alilazimisha asifanye naye starehe au asimuandalie chakula chake au kinywaji chake katika namna ambayo imejiri kwayo ada, kufanya mke kwa mumewe, basi sharti hili ni batili halipaswi kutekelezwa kwa sababu linakwenda kinyume na lengo la kuoa. Na kama sharti hilo liko nje kabisa ya mzunguko wa hayo yote, kama vile lazima kuwazuru nduguze wa karibu au asimtoe katika nchi/mji yake/wake; kwa maana kuweka sharti ambalo halikuhalaisha haramu na haikuharamisha halali, kwa hakika (sharti) hilo linawajibika litekelezwe na kama lisipotekelezwa basi atakuwa na haki ya kuvunja ndoa yake akitaka, nahayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Sharti yenye haki zaidi kutekelezwa ni ile mnayohalalisha tupu.”
(Tabarani).

Kama ilivyokuwa haramu juu ya mwanamke kuweka sharti kwa mwanaume kumwacha mkewe (wa kwanza), kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Si halali kuolewa mwanamke kwa kuachwa mwingine.” (Ahmad).

Ni kwa aliyoyapokea Imamu Bukhari na Muslim kwamba yeye Mtume ﷺ amekataza mwanamke kulazimisha kuachwa mwenzake.

7) Hiari katika Ndoa:

Hiari inathibitika kwa kila mmoja wa wanandoa wawili ya kubaki katika himaya ya ndoa au kuivunja kutokana na kuwepo sababu moja wapo miongoni mwa sababu zifuatazo:

Kasoro za Kimaumbile au maradhi:

Kama vile wendawazimu, au ukoma au mabalanga, au ugonjwa wa kwenye utupu unaokosesha ladha ya kustarehe; kama vile mume kuwa amekatwa makende, au mwenda wazimu au hana nguvu za kuweza kumwendea mwanamke

na kumingilia. Katika hali ya kutaka kuvunja ndoa, pataangaliwa, ikiwa uvunjaji ni kabla ya kuingilia, basi mume ana haki ya kurudi kwa mke kwa (kutaka amrudishie) kile alichompa katika mahari. Kama ni baada ya kuingilia basi hana haki ya kurudi kwa mwanamke kutaka ampe chochote, kwani mahari yake yamemthibitika kwa kile kiasi (ambacho mume) amempata mke. Inasemekana pia anaweza kumrudia kwa hilo yule aliyemdanganya miongoni mwa ndugu, jamaa zake (huyo mwanamke) kama ikiwa yule ndugu aliyemdanganya anajua kasoro ile.

Dalili ya maswala haya ni kauli ya ‘Umar رضي الله عنه katika (Kitabu kiitwacho) Al Muwatwa,

“Mwanamke yoyote, mwenye wazimu au ukoma, au mbalanga amedanganywa nayo mtu (akamuoa akamuingilia) basi anastahiki mahari yake kutokana na Kiasi alichompa; na mahari ya yule mwanamume (aliyoyatoa kwa mwanamke) yako juu ya yule mtu aliyemdanganya.”

b) Udanganyifu:

Ni kama vile mtu kumuoa hali ya kujua ni Muislamu kisha ikadhihirika kuwa ni katika *Ahlul Kitabu*, au (kumuoa hali yakuwa) ni mzima kiafya ikajadhihiri kuwa ni mgonjwa, kwa kuwa na chongo, au anachechemea kiguu. Kwa kauli ya Umar رضي الله عنه, Mwanamke yoyote, mwenye wazimu au ukoma au mbalanga, mtu akadanganywa kwayo (mtu akamuoa na akamuingilia) basi atastahiki mahari yake, kutokana na kile kiasi alichompa, na mahari ya yule mwanaume (aliyoyatoa kwa mwanamke) yako kwa yule mtu aliyemdanganya.

c) Kuwa na hali ngumu ya kutoa mahari ya papo hapo.

Basi atakayekuwa na hali ngumu ya kutoa mahari ya mkewe hapo hapo si ile ya baadae, kwa hakika mkewe ana haki ya kuvunja ndoa klabla ya kumingilia ama ikiwa ni baada ya kumingilia hatakuwa na haki ya kuvunja ndoa, bali kifungo cha makubaliano kitapita moja kwa moja, na mahari itathibitika katika dhima (shingo) yake (yaani itakuwa deni). Pia hatakuwa na haki ya kujizuilia nafsi yake kwa mumewe kamwe.

d) Hali Ngumu ya maisha

Mtu atakayekuwa na hali ngumu ya matumizi ya chakula cha mkewe, mke atamngojea kiasi awezacho cha muda, kisha atakuwa na haki ya kuivunja ndoa yake na mume huyo kupitia usimamizi wa kisheria wa kadhi. Haya wameyasema masahaba kama vile Abu Huraira رضي الله عنه, Umar رضي الله عنه na Umar bin ‘Abdil-Aziz, Rabiyy-a na Malik –Rehma za Allah ziwashukie wote.

e) Atapokosekana mume, na haikujulikana Mahala alikopotelea

Ikiwa hakumwachia mkewe matumizi, na hakumpa mtu yoyote maagizo ya kutoa matumizi kwake mke, na hakusimama mtu mwingine kwa matumizi yake, na hakuwa na cha kujifanyia matumizi ya chakula ili baadaye aje mume amlipe, mke atakuwa na haki ya kuvunja ndoa yake kupitia Kadhi wa Kisheria. Shauri lake atalipeleka kwa Kadhi, atampa mawaidha na kumuusia kusubiri na kuvumilia. Akikataa basi kadhi ataandika muhtasari wa maelezo kupitia mashahidi wanaomjua huyo mwanamke, na wanaomjua huyo mwanamme ambao watashuhudia kutokuwepo kwake na ugumu wa hali yake. Baadaye utapita uvunjaji wa ndoa kati ya wana ndoa hao wawili. Na uvunjaji huu wa ndoa unazingatiwa kuwa ni talaka moja rejea, iwapo mume atarudi katika muda wa eda, basi mke atarudi kwake mume.

Namna ya kuandika ule muhtasari wa maelezo:

Baada ya *Bismillahi* na kumuhimidi Allah Mtukufu, na Sala na salama kwa Mjumbe wa Allah ﷺ, “Wamehudhuria mbele yetu mashahidi wawili fulani...na fulani...ambao ni miongoni mwa watu ambao ushahidi wao unafaa kutokana na uadilifu wao na kukamilika busara na uoni wao. Wameshuhudia kwa hiari yao ushahidi ambao hawataki isipokuwa radhi za Allah, wameshuhudia kwamba wao wanamjua kila mmoja kuanzia fulani na fulani (fulani mwanamke). Kuwa ni mke na mume wameoana kwa ndoa ya kisheria iliyo sahihi, imetimia pamoja na ndoa hiyo kukaa faragha na kuingiliana. Kisha (huyo mume) amekosekana (ameghibu) kwa mkewe muda unaozidi kiasi na amemwacha mkewe bila ya fedha za matumizi, wala mavazi. Wala hakumwachia matumizi katika hali ya kutokuwepo kwake, wala mtu wa kujitolea matumizi kwa mwanamke huyo katika kipindi cha kutokuwepo kwake. Wala hakumtumia kitu chochote kitakachomfikia, wala hana

mali ya kutumia yeye mwenyewe, na kujarudishiwa mume, nae bado amedumu katika kumtii yeye (mume) pale pale mahala alipomwacha. Na anataka kuepuka madhara hayo kwa kuvunja ndoa yake naye. Hali ya kuwa wanajua hilo (Hao mashahidi wawili) hio, na wanashuhudia hali ya kuwa wataulizwa hilo kesho mbele ya Allah Mtukufu.

Kisha mke aliyekwishatajwa (Fulani), alifika (mbele ya kadhi) akaapa kwa jina la Allah Mtukufu ambaye hapana Mola ila Allah Mtukufu ambaye hapana Mola mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye, kiapo cha kisheria kwamba mumewe aliyetajwa fulani, amempotea kwa muda kadhaa, na amemwacha bila ya matumizi (*nafaqa*) wala mavazi... Na hakumwachia cha kutafutia matumizi yeye mwenyewe wakati akiwa hayupo, wala hakuna mtu aliyejitolea kumpa matumizi, wala hakumtumia chochote kikamfikia, wala yeye mwenyewe (mke) hana mali ya kujipatia matumizi, apate kumdai huyo (mume atakaporudi). Na kwamba aliyeshuhudia hivyo ni mkweli katika ushahidi wake, na kwamba huyo (mke) bado anadumu katika kumtii yeye (mumewe). Na akataka kujiondolea madhara kwa kuivunja ndoa yake na mumewe.

Kutokana na yote hayo tumemjibu ombi lake kwa kuivunja ndoa yake. Kutokana na ushahidi uliothibitika na (kutokana) na kupita kiapo kilichobainishwa hapo juu, ametamka kwa tamko la wazi: “Nimeivunja ndoa yangu kutoka kifungo cha ndoa ya mume wangu Fulani. Kwa hiyo ndoa ya mume wangu fulani, hivyo imekuwa iko katika nafasi ya talaka mojarajea, kwa hiyo ndoa yake mume aliyetajwa (hapo juu) ndio imevunjika, na hayo ni katika tarehe kadhaa”

f) Kuwa huru baada ya utumwa:

Kama mke ni mjakazi (mtumwa mwanamke) yuko chini ya ameolewa na mtumwa (mume) Mtumwa kisha (yule mke) akawa huru. Basi ana hiari ya kuivunja hiyo ndoa yake na mume wake mtumwa (au kuivunja) kwa sharti, baada ya kujua kwake kuwa yeye ni mtu huru (muungwana) asimkubalie tendo la ndoa, iwapo atamkubalia tendo la ndoa baada ya kujua (kuwa yeye ni mtu huru) basi hatakuwa na haki ya kuvunja ndoa.

Kwa kauli ya Aisha رضي الله عنها katika mapokezi ya Muslim,

“Kwa hakika, Barira aliachwa huru, na mumewe alikuwa bado mtumwa, basi Mtume ﷺ alimpa khiari (kati ya kubaki na mume Mtumwa au kuivunja ndoa) na lau alikuwa muungwana asingampa khiari.”

8) Haki za Kindoa katika Uislamu

(Haki hizi ni muhimu sana kwa wanandoa kuzijua na kuzitumia, zina umuhimu wa kipekee katika maisha ya kila siku ya wanandoa.)

a) Haki za Mke juu ya Mume:

Mke ana haki nyingi zinawajibika juu ya mume. Zimemthibitikia, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْعُرُوفِ وَاللرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٨﴾

“...Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.” (2:228).

Na anasema Mtume ﷺ

“Kwa hakika nyinyi mna haki kutoka kwa wake zenu, na wake zenu wanazo haki juu yenu.” (Ibn Majah).

Na miongoni mwa haki hizi ni:

i) Matumizi yake:

Kama vile chakula, kinywaji, kivazi, na makazi kwa wema, kwa kali yake Mtume ﷺ kwa aliyemuuliza kuhusu haki za mke juu ya mume,

“Utampa chakula unachokula, na utampa kivazi unapovaa, wala usimpige usoni, wala usimtakie mabaya (kama kumwambia Allah au fanye mbaya uso wako). Wala usimuhame isipokuwa humo nyumbani yaani usimuhamishie kwenye nyumba nyingine (ambayo hautakuwepo).” (Ahmad).

ii) Kustarehe nae:

Inawajibika juu ya mume kumingilia japo mara moja katika kila miezi minne iwapo atashindwa kiasi cha kumtoshia, kwa kauli ya (Allah) Mtukufu:

لِّلَّذِينَ يُؤْتُونَ مِن نِّسَائِهِمْ تَرَئُصَ أَرْبَعَةِ أَشْهُرٍ فَإِن فَاءُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٢٦﴾

“Kwa wanao apa kuwa watajitenga na wake zao, wangojee miezi mine. Wakirejea basi Mwenyezi Mungu hakika ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu” (2: 226).

iii) Kulala kwake:

Katika kila siku nne usiku mmoja kwani ilihukumiwa hivyo katika zama za Umar رضي الله عنه.

iv) Kungawia zamu kwa Uadilifu

Kama mume ana wake wengine kwa kauli yake,

“Mtu mwenye wake wawili, akawa anahimili kwa mmoja wao dhidi ya mwingine, basi Siku ya Qiama atakuja il-hali moja ya mbavu zake mbili imeanguka (inaburuzika).” (Ahmad).

v) Kukaa kwake, siku ya kumuoa kwake

Kama mke akiwa ni bikra ni siku saba, au siku tatu kama mke akiwa si bikra (Thayyiba), kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Mwanamke bikra ana siku saba na thayyiba ana siku tatu, kisha atarudi kwa wakeze.” (Daraqutni).

vi) **Kumpa idhini ya kuuguza**

Kumpa idhini ya kuuguza mmoja wa maharimu zake, na kuhudhuria mazishi yake atapokufa, na kuwatembelea ndugu zake wa karibu kuwatembelea ambako hakudhuru (na kuathiri) maslahi ya mume.

b) **Haki za Mume:**

Na mume ana haki juu ya mkewe, haki nyingi zimethibitika, kwa kauli ya Allah Mtukufu.

وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْنَ بِالْعُرُوفِ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْنَ دَرَجَةٌ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٢٨﴾

“Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao. Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.” (2:228).

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Kwa hakika nyinyi mnazo haki juu ya wake zenu.” (Imepokewa na Tirmidhi, Abu Dawud, Ahmad na Hakim).

Haki hizi ni:

i) **Kutiwa katika mambo mema**

Mke atamtii mumewe si katika maasi ya Allah asimtii katika jambo asiloliweza au linalotaabisha juu yake. Kwa kauli yake (Allah) Mtukufu:

فَإِنْ أَطَعْنَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِنَّ سَبِيلًا

“...Wakikutini basi msiwatafutie njia...” (4: 34).

Minhajil Muslim

Na kauli ya Mtume ﷺ,

“Lau ningalikuwa naamrisha mtu kumsujudia mtu mwingine, basi ningalimwamrisha mwanamke kumsujudia mumewe.”

ii) Kuhifadhi mali ya Mume

Na kuhifahi heshima yake, na kwamba asitoke katika nyumba) yake isipokuwa kwa idhini yake; na hayo ni kwa kauli yake Allah Mtukufu,

فَالصَّلِيحَةُ قَنْبَتُهُ حَفِظْتُ لِّلْغَيْبِ بِمَا حَفِظَ اللهُ

“...Basi wanawake wema ni wale wenye kutii na wanao jilinda hata katika siri kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameamrisha wajilinde...”(4: 34).

Na kauli ya Mtume ﷺ,

“Bora ya wanawake ni ambaye unapomuangalia anakufurahisha, na unapomuamrisha hukutii na usipokuwepo, hukulindia nafsi yake na mali yako” (Abu Dawud).

iii) Kusafiri naye, akitaka hilo (Mume)

Na ikawa hakulazimisha hilo wakati wa ndoa yake la kutosafiri naye, kwani safari yake pamoja naye ni utiifu wa wajibu juu yake.

iv) Kujisalimisha nafsi yake kwake

Wakati wowote atakapomtaka kwa starehe, ni miogoni wa haki zake mume kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Mume atakapomwita mkewe kwenye godoro lake (kwenye tendo la ndoa) nae akakataa, kuja, na (mume) akalala usiku hali ya kuwa amemkasirikia, basi malaika humlaani mwanamke yule mpaka kupambazuke.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim na Abu Dawud).

v) Kumuomba Ruhusa ya kufunga

Kama akiwa mume yupo, si msafiri, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Si halali mwanamke kufunga (suna) na hali ya kuwa mumewe yupo, isipokuwa kwa idhini yake.” (Bukhari).

9) ‘Uasi wa Mke’:

Mke atakapomuasi mume, yaani atakapomkiuka mumewe na akamkalia juu yake, na akakataa kutekeleza haki zake, atamuonya, akimtii (Basi ndiyo ndivyo) na kama si hivyo atamuhama katika kulala muda autakao, na pia katika kuongea naye muda wa siku tatu si vinginevyo, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Si halali kwa Muumini kumuhama nduguye zaidi ya siku tatu.” (Abu Dawud).

Akimtii, (ndiyo Ndivyo) na kama sio hivyo atampiga pasipokuwa usoni, pigo ambalo si la kujeruhi akamtii. Na kama si hivyo kutapelekwa muamuzi wa upande wa mume na muamuzi upande wa jamaa zake mke, watawasiliana kila mmoja peke yake ikiwa ni jitihada za usuluhishi na kuwapatanisha kati yao, ikishindikana hilo watatenganishwa talaka isiyo rejea na hayo ni kwa kauli yake Allah Mtukufu:

وَأَلَّتِي تَخَافُونَ نُشُوزَهُمْ فَعِظُوهُمْ ۖ وَاهْجُرُوهُمْ فِي الْمَضَاجِعِ وَأَضْرِبُوهُمْ
فَإِنْ أَطَعْتَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِمْ سَبِيلًا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا كَبِيرًا ﴿٦٠﴾
وَأِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوا حَكَمًا مِّنْ أَهْلِهِمْ وَحَكَمًا مِّنْ أَهْلِهَا ۖ إِنْ
يُرِيدَا إِصْلَاحًا يُوَفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٦١﴾

“...Na ambao mnachelea kutoka katika ut’ifu wanasihini, muwahame katika malazi na wapigeni. Wakikut’iini msiwatafutie njia ya kuwaudhi bure. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliye juu na Mkuu. Na mkichelea kutakuwapo mfarakano baina ya mke na mume basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa za mume, na muamuzi kutokana na jamaa za mke. Wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye khabari.” (4:34-35).

10) Adabu za Kuingiliana

Kuna adabu za kuingiliana ambazo inapasa kuzizingatia:

- a) Kumchezea-mke na kumtaniatania hali ambayo huchochea mvuto wa kujamiiana.
- b) Asiangalie tupu yake, kwani hiyo inamsababishia yeye kumchukia na ni miongoni mwa mambo yanayopasa kujihadhari nayo.
- c) Aseme, “Kwa jina la Allah ewe Mola tuepushie shetani, na kiepushie shetani kile utakachoturuzuku’, Kutokana na Mtume ﷺ kuvutia katika hilo kwa hadithi aliyoipokea Bukhari na Muslim kwa tamko,

“La ingalikuwa mmoja wenu anapotaka kumwendea mkewe akasema ewe Mola tuepushie shetani, na kiepushie shetani kile utakachoturuzuku kwa hakika ikiwa patakadiriwa kati yao mtoto katika (tendo lao) hilo shetani kamwe hatamduru.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Abu Dawud Na Tirmidhi).

- d) Ni kutomuingilia katika hali ya hedhi au damu ya uzazi (nifasi); na kabla ya kuoga kutokana na damu mbili hizo. Baada ya kutwahaika, kwa kauli yake Allah Mtukufu:

فَاعْتَرِلُوا الْبَسَاءَ فِي الْمَحِيضِ وَلَا تَقْرُبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ

“Waepukeni wanawake katika hedhi wala msiwakurubie mpaka Watwahaika.” (2:222).

e) Ni haramu mkeo kumingilia kusikokuwa tupu ya mbele. Kutokana na yaliyokuja ya kushadidia (adhabu) hilo, kama kauli ya Mtume ﷺ

“Mtu mwenye kumingilia mwanamke kwenye utupu wake wa nyuma, Allah hatamuangalia kwa Huruma Siku ya Qiyama.” (Darimy).

f) Asiitowe kabla ya (mke) kumaliza matamano yake, kwa vile katika hilo ni kumuudhi mke na kumuudhi Muislamu ni haramu.

g) Asimwage-nje-mbegu zake kwa kuhofia mimba isipokuwa kwa idhini yake (mke) na asimwage nje isipokuwa kwa dharura kubwa mno, kwa kauli yake Mtume ﷺ kuhusu tendo la kumwaga mbegu nje,

“Ni uuaji wa watoto uliojificha.” (Imepokewa na Ibn Majah, Ahmad na Hakim).

h) Inapendeza kwake anapotaka kurudia tena tendo la ndoa kutawadha udhu wa (hadathi) ndogo, na pia (imesuniwa hilo) anayetaka kulala au kula kabla hajaoga.

i) Inafaa kwake kukumbatiana naye ilhali ana hedhi au damu ya uzazi katika sehemu isiyokuwa kati ya kitovu na magoti, kwa kauli yake Mtume ﷺ

“Wafanyeni kila kitu isipokuwa kuwaingilia.” (Muslim).

Ndoa mbovu ambazo Mtume amezikataza ni hizi:

11) ‘Ndoa ya **‘Mut-a’**’:

Nayo ni kuoa kwa muda maalum, uwe wa mbali au wa karibu, kama vile mwanaume kumuoa mwanamke kwa muda maalumu kama mwezi mmoja au kwa mfano – mwaka, na hayo ni kutokana na hadithi iliyoafikiwa na Bukhari na Muslim kutoka kwa Ally رضي الله عنه. *“Kwamba Mtume ﷺ ametakataza ndoa ya Mut-a, na nyama ya punda wa mijini zama za Khaybar”*

Hukumu ya ndoa hii ni batili, inawajibika kuivunja rasmi wakati wowote itokeapo, na huthibitika kwayo mahari ikiwa kama amewahi kumingilia yule mwanamke, na kama si hivyo basi hapana.

b) ‘Ndoa ya Shighar’

Nayo ni walii kumuozesha (mwanamke) anayemsimamia wake miongoni mwa wanaume kwa sharti yeye (muoaji) amuozeshe yeye huyo anayemsimamia, ni sawa waitaja mahari au hawakuitaja, na hayo ni kwa kauli ya Mtume رضي الله عنه.

“Hakuna Shighari katika Uislamu,” (Muslim na Tirmidhi).

Kauli ya Abu Hurayra رضي الله عنه.

“Mtume ﷺ amekataza shighar, na shighar ni mtu kumwambia mwingine: Niozeshe binti yako, nami nitakuoza binti yangu, au niozeshe dada yako, nami nitakuoza dada yangu.” (Imepokewa na Tirmidhi, Nasai, Abu Dawud na Ibn Majah).

Na kauli ya Ibn Umar رضي الله عنه.

“Mtume ﷺ amekata za shighar nayo ni mtu kumuozesha mtoto wake na kumtaka aliyeoa nae amuozeshe binti yake na hakuna mahari baina yao.” (Bukhari na Muslim).

Hukumu ya ndoa hii batili ni kuvunja kabla ya kumuingilia, na kama ilivunjwa baada ya kumuingilia, itavunjwa itakavyokuwa ila ya mahari, na ile ambayo kila upande una mahari hiyo haivunjwi.

c) ‘Ndoa ya Muhalalishaji’

Nayo ni mwanamke kuachwa talaka tatu, akawa haramu kwa mumewe kwa sababu ya hizo talaka. Kwa kauli yake Allah Mtukufu,

فَإِنْ طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِنْ بَعْدُ حَتَّىٰ تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ

“Na kama amempa talaka (ya tatu) basi si halali kwake baada ya hayo mpaka aolewe na mume mwingine...” (2:230).

Akamuoja mume mwingine kwa kusudi la kumuhalalishia kwa le mume wake wa kwanza. Basi hii ndoa ni batili, kwa kauli ya Ibnu Masoud رضي الله عنه.

“Mjumbe wa Allah amemlaani mhalalishaji na muhalalishiwa.”
(Imepokewa na Tirmidhi, Abu Dawud, Ibn Majah na Ahmad).

Na hukumu ya ndoa hii ni kuvunjwa tu wala mke halaliki kwa mume aliyemwacha talaka tatu, na mahari yatathibitika kwa mke ikiwa amewahi kuingiliwa, kisha watatenganishwa.

d) ‘Ndoa ya mtu aliyehirimia Hija Au Umra’:

Ni mtu kuo na lhali ni mwenye kuhirimia Hija au Umra kabla ya kufungua Ihram ya Ibada mbili hizo. Na hukumu ya ndoa hii ni batili, pia, anapotaka kumuoa atafunga ndoa upya baada ya kumaliza Hija yake au Uma yake, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Aliehirimia haowi wala haozeshi.” (Muslim).

e) Ndoa katika Eda:

Ni mtu kumuoa mwanamke aliye katika eda ya kuachwa au ya kufiwa, basi ndoa hii ni batili. Hukumu yake, “Kutenganishwa kati ya mke na mume. ’Kutokana na kubatilika kifungu cha ndoa, na inathibitika mahari kwa mwanamke ikiwa mume amewahi kukaa naye faragha. Ni haramu kwa Mume huyo kumuoa mwanamke yule baada ya kumalizika eda yake, ni adhabu kwake, na hayo ni kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

وَلَا تَعْرَمُوا عُقْدَةَ النِّكَاحِ حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ

“Wala msiazimie kufunga ndoa mpaka kitabu kifikie muda wake.” (2:235).

f) Ndoa bila ya Walii:

Hayo, ni mtu kumuoa mwanamke bila idhini ya walii wake, basi ndoa hii ni batili. Kutokana na kupungua nguzo miongoni mwa nguzo zake, nayo ni walii kwa kauli yake ﷺ, *“Hapana ndoa isipokuwa kwa walii.”* Basi hukumu yake ni kutenganishwa kati yao, na yanamthibitikia mahari ikiwa alimuingilia, na baada ya kujitakasa ana ruhusa kuuoa kwa kifungu cha ndoa (mpya ikiwa walii wake ataridhia hilo).

Minhajil Muslim

g) Ndoa ya kafiri mwanamke, asiye kitaabiya:

Kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

وَلَا تَنْكِحُوا الْمُشْرِكَةَ حَتَّىٰ تُؤْمِنَ

“Wala msiwaoe wanawake washirikina, mpaka waamini.” (2: 221).

Basi ni haramu juu ya Muislamu kumuoa mwanamke kafiri mmajusi au alikuwa mkomonisti au muabudu masanamu. Kama ambavyo si halali kwa mwanamke Muislamu kuolewa na kafiri kwa hali yoyote, awe ni yule wa Kitabu au asiye wa Kitabu kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ وَءَاتُوهُنَّ مِمَّا أَنْفَقُوا وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ
أَنْ تَنْكِحُوهُنَّ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ

“...Wanawake hao si halali kwa hao makafiri, wala hao makafiri hawahalalikii wanawake Waumini...” (60:10).

Na miongoni mwa hukumu za kadhia hii ni mambo yafuatayo:

i) Atakaposilimu mmoja wa wanandoa wawili, mke au mume makafiri wawili, basi imebatilika ndoa yao. Akisilimu yule wa pili kabla ya kwisha eda, basi wawili hao wako katika ndoa yao ya kwanza. Na ikiwa alisilimu baada ya kwisha eda, hapana budi kufunga ndoa mpya, kwa mujibu wa madhehebu ya wanazuoni wengi.

ii) Atakaposilimu mke kabla ya kuingiliwa, basi hana chochote katika mahari, kwa sababu utengano umekuwa kutoka kwake yeye. Na akisilimu mume, basi ana nusu ya mahari na ataposilimu mke baada ya kuingiliwa basi ana mahari kamili. Na hukumu ya kuritadi mmoja wa mke na mume, ni kama hukumu ya kusilimu mmoja wao. Sawa sawa tu.

iii) Mtu atakayesilimu na chini yake ana wake zaidi ya wanne ambao wamesilimu pamoja nae au walikuwa watu wa kitabu japokuwa hawakusilimu, basi achague

kati yao wanne na waliobaki ataachana nao kwa kauli yake Mtume ﷺ kumwambia mtu aliyesilimu aliyekuwa na wake kumi,

“Chagua wane miongoni mwao.” (Imepokewa na Ahmad, Abu Daud na Ibn Majah).

Mtu mwenye kusilimu na chini yake ana madada wawili, atatengana na amtakea kati yao, kwani si halali kukusanya kati ya madada wawili, kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ

“Na kukusanya kati ya madada wawili.” (4:23).

Kauli ya Mtume ﷺ kwa mtu aliyesilimu na chini yake ana wakeze walio madada,

“Muache yeyote umtakea.” (Imepokewa na Ahmad, Abu Daud na Ibn Majah).

h) Ndoa zilizoharamishwa:

i) ‘Zilizoharamishwa Uharamu wa Milele’.

‘Walioharamishwa kwa Nasaba’ ni:

Mama na bibi kwa ujumla. Wa upande wa mama au wa upande wa baba na kuendelea hata wakienda juu namna gani. Binti na binti yake, na wakiendelea chini. Binti wa mtoto wa kiume na binti yake vyovyote watakavyoshuka, na dada kwa ujumla mabinti zake, na mabinti wa mtoto wake wa kiume, vyovyote watavyoshuka, na shangazi kwa ujumla na kuendelea juu. Na ndugu wa kike wa mama (mama mdogo/mama mkubwa) yeyote na hata akaenda namna gani, na binti wa ndugu wa kiume yeyote na binti wa mtoto wake na kiume, na binti wa mtoto wake wa kike, na kuendelea chini. Hayo ni kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الْأَخِ وَبَنَاتُ الْأَخْتِ وَأُمَّهَاتُكُمْ

“Mmeharamishiwa kuwaoa mama zenu, na mabinti zenu, na madada zenu, na shangazi zenu, na ndugu wa mama zenu na mabinti wa ndugu zenu na mabinti wa dada zenu.” (4: 23).

Walioharamishwa kwa kuoleana ni:

Mke wa baba na mke wa babu, hata na kwenda juu, kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

وَلَا تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ

“Wala msiwaoe wake walio waoa baba zenu, ila yaliyo kwisha pita...” (4: 22).

Mama wa mke, na bibi yake na kwenda juu, na binti wa mke ikiwa ameshawahi kumuingilia mama yake na pia binti wa binti yake mke, au binti wa mtoto wake wa kiume. Kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

وَأُمَّهَاتُ نِسَائِكُمْ وَرَبِّبَاتِكُمُ اللَّيْثِي فِي حُجُورِكُمْ مِّنْ نِّسَائِكُمُ اللَّيْثِي
دَخَلْتُم بِهِنَّ فَإِنْ لَّمْ تَكُونُوا دَخَلْتُم بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ

“...Na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu walio zaliwa na wake zenu mlio waingilia. Ikiwa hamkuwaingilia basi hapana lawama juu yenu...” (4: 23).

Walioharamishwa kuoa sababu ya kunyonya ziwa pamoja nao ni:

Wanawake wote, walioharamishwa kwa sababu ya nasaba, kama vile mama, mabinti, madada, mashangazi, ndugu zake mama na mabinti wa ndugu wa kike, na mabinti wa ndugu wa kiume, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Inaharamika kwa kunyonya kama inavyoharimika kwa nasaba.” (Imepokewa na Nasai, Ibn Majah na Ahmad).

Kunyonya kunakoharamishwa ni kule kunakokuwa chini ya miaka miwili (ya umri wa mtoto) na ikathibitika pamoja naye, kufika maziwa mpaka tumboni mwa mtoto anayenyonyeshwa katika namna inayozingatiwa kuwa hiyo ni kunyonya. Kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hauharamishi mfyonzo mmoja tu au mifyonzo miwili.” (Muslim),

Kwa sababu mfyonzo mmoja ni kitu kisichokuwa na na maana au thamani yoyote huenda pengine maziwa yasifike tumboni mwa mtoto kwa sababu ya uchache wake.

Tanbihi:

-Mume wa mama mnyonyeshaji atazingatiwa kuwa ni baba kwa mtoto mnyonyeshwaji kwa hiyo watoto wake wasiotokana na mama mnyonyeshaji ni nduguze, na ni haramu juu yake mama wa baba yake, dada zake, na shangazi zake, na wadogo wote wa mama zake, kama ambavyo mama mnyonyeshaji watoto wote wake kutoka kwa mume yeyote wao ni nduguze wa kunyonya. Hayo ni kwa kauli yake Mtume ﷺ kumwambia Aisha رضي الله عنها ,

“Mpe idhini Allah ndugu wa baba Quays kwani huyo ni ndugu wa kiume wa baba yako (Ammi), na mkewe alikuwa amemnyonyesha Aisha رضي الله عنها .” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Nasai na Ahmad).

Hadithi imethibitisha “Ubaba” wa kunyonya hivyo basi yote yaliyotajwa yatafuata.

-Ndugu wa kiume na wa kike wa mnyonyeshwaji hakiharamiki juu yao chochote miongoni mwa walioharamika kwa mnyonyeshwa ni kwa sababu hawakunyonya

kama yeye, hivyo basi ni halali kwa ndugu (wa mnyonyeshwa) kumuoa mwanamke aliyemnyoyesha ndugu yake. Au mama yake, au binti yake, kama ambavyo inahalalika kwa dada kuolewa na yule mwenye maziwa ambaye kayanyonya nduguye wa kiume au nduguye wa kike, au babake, au mtoto wake wa kiume – kwa mfano.

Al-Mulaana: Kulaaniana.

Ni haramu milele juu ya mwanaume kumuoa mwanamke/mkewe ambaye amemlaani kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Waliyolaaniana wakifarikiana kamwe hawawi pamoja.” (Daraqutni)

Na Maliki amesema katika ‘Muwattaa’. Suna kwetu sisi ni kwamba waliolaaniana kamwe hawataoana.

ii) Walioharamishwa uharamu wa muda:

a) Dada wa mke, ni mpaka kuachwa dada yake na kumalizika eda yake, au kufa. Kwa kauli Yake Allah Mtukufu katika mlolongo wa kubainisha wanawake walioharamishwa:

وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ

“Na kukusanya madada wawili.”(4: 23).

b) Shangazi wa mke au mama yake mkubwa au mdogo, haolewi mpaka aachwe au binti wa kaka yake au binti wa dada yake, na imalizike eda yake au afe, kwa kauli ya Abu Hurayra رضى الله عنه Mtume ﷺ,

“Amekataza kuolewa mwanamke pamoja na shangazi yake au ndugu wa mama yake.” (Imepokewa na Tirmidhi, Nasai na Ahmad).

c) Mwanamke aliyehifadhika (aliyeolewa). Mpaka aachwe au awe mjane na eda yake imalizike kwa kauli Yake Allah katika milolongo wa kutaja wanawake walioharamishwa kuwaoa:

✽ وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ

“NA WANAWAKE wenye waume...” (4:24).

d) Mwanamke aliye katika eda, ya kuachwa au kufiwa, mpaka eda yake imalizike na ni haramu pia kumposa, na hapakatazwi kumfumbia. Kama vile kauli yake Mtume kwa mfano, “*Mimi na kupenda wewe.*” hayo ni kwa kauli ya Allah Aliyetakasika:

لَا تُوَاعِدُوهُنَّ سِرًّا إِلَّا أَنْ تَقُولُوا قَوْلًا مَعْرُوفًا ۖ وَلَا تَعْزَمُوا عُقْدَةَ النِّكَاحِ
حَتَّىٰ يَبْلُغَ الْكِتَابُ أَجَلَهُ ۗ

“...*Lakini msiwaahidi kwa siri, ila mnene maneno mema. Wala msiazimie kufunga ndoa mpaka eda ifike mwisho wake...*”(2:235).

e) Aliyeachwa Talaka tatu mpaka aolewe na mume mwingine na aachane nae kwa talaka au kifo na eda yake imalizike, kwa kauli Yake Allah Mutukufu:

فَإِنْ طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِنْ بَعْدُ حَتَّىٰ تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ ۗ

“*Na kama amempa talaka (ya tatu) basi si halali kwake baada ya haya mpaka aolewe na mume mwingine...*”(2: 230).

f) Mzinzi mwanamke mpaka atubu katika zinaa na ijulikane kwa yaqini kuwa ametubu, na eda yake imalizike, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

الزَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ مُشْرِكٌ
وَحَرِّمَ ذَلِكَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٧﴾

Minhajil Muslim

“Mwanamume mzinifu hamwai ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Na hayo yameharimishwa kwa Waumini” (24:3).

Na kauli ya Mtume 

“Mzinifu aliyepigwa mijeledi hamuowi isipokuwa mtu kama yeye.” (Ahmad).



Mada ya Pili

‘Talaka’

1) Maelezo yake:

Ni kufungua fungo la ndoa kwa tamko bayana, kama vile, ‘Wewe umeachwa.’ Au la fumbo pamoja na nia ya talaka, kama vile mtu kumwambia mkewe, ‘Nenda kwa ndugu zako.’

2) Hukumu yake:

Talaka ni halali kwa ajili ya kuondoa madhara kwa mmoja wa wanandoa. Kwa kauli Yake Mwenyezi Mungu:

الطَّلُقُ مَرَّتَانِ ط فِيمَا سَاكَ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٍ بِإِحْسَانٍ ٤

“Taalaka ni mara mbili. Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri...” (2:229)

Na kauli yake Allah Aliyetakasika:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَاءَ فَطَلِّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ وَأَحْصُوا الْعِدَّةَ ط

“Ewe Nabii! Mtakapo wapa talaka wanawake, basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao...” (65:1)

Talaka inaweza kuwa wajibu ikiwa madhara yanayomfika mmoja wa wanandoa hayataondoka ila kwa talaka. Pia inaweza kuwa haramu ikiwa talaka hiyo itamfikisha mmoja wa wanandoa katika madhara na ikawa talaka haikuleta manufaa au maslahi zaidi kuliko yale mahara au yanalingana. Na anautolea ushahidi wa lile la kwanza kwa kauli ya Mtume ﷺ kwa yule aliyemshitakia uchafu wa mke wake kwake na Mtume ﷺ akamwambia, “Mwache.” Na ushahidi wa lile la pili kauli yake Mtume ﷺ

“Mwanamke yeyote aliyemtaka mumewe talaka bila ya ovu lolote ni haramu kwake kupata harufu ya pepo” (Imepokewa na Ahmad, Ibn Majah na Darimi).

3) Nguzo Zake

Talaka ina nguzo tatu nazo ni:

a) Mume balebeghe mwenye akili timamu, asiyekuwa mume hatoi talaka kwa kauli yake Mtume ﷺ:

“Hakika talaka ni ya mwenye kushika mguu” (Imepokewa na Ibn Majah na Daraqutni).

Pia mume kama hana akili timamu si balebeghe si kwa khiari yake na kulazimishwa haipatikani kwake talaka. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Imenyanyuliwa kalamu kwa watatu. Kwa aliyelala mpaka aamke, na mtoto mpaka abalebeghe na wenda wazimu mpaka azinduke akili.” (Abu Dawud).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Kumeondolewa kwa uma wangu kukosea na kusahau na walicholazimishwa.” (Tabarani).

b) Mke ambaye anaunganishwa na mume aliyemuacha kifungo cha ndoa hasa. Kama vile yuko katika himaya ya mume hakutoka kwa mume huyo kwa kufumua (faskh) ndoa au talaka. Au (yuko katika himaya yake) kwa hukumu kama aliye ndani ya eda ya rejea, au eda ya rejea ambayo muda wake umekwisha talaka haipatikani kwa asiye kuwa mke wa mwenye kutoa talaka hiyo, wala kwa mke aliyeachwa talaka tatu au kufumuliwa ndoa au kwa kuachwa kabla ya kumuingilia, kwani talaka isiposadifu mahali pake (ndoa) hiyo ni upuuzi kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Hakuna nadhiri kwa mwanadamu katika kitu asichokilimiki wala hakuna kuacha huru (mtumwa) kwa asiyommiliki wala talaka asiyoimiliki.” (Tirmidhi).

c) Tamko lenye kujulisha talaka liwe la wazi (*bayana*) au si la fumbo (*kinaya*) nia peke yake bila ya tamko la talaka haitoshi na wala haachiki mke kwa hilo tu kwa kauli yake Mtume ﷺ

“*Hakika Allah ameacha kwa umma wangu yale yaliyoelezwa na nafsi zao ikiwa hawakuyatamka au kufanya.*” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Tirmidhi na Ibn Majah).

4) Aina za Talaka:

Talaka Ina vigawanyo vingi:

a) **Talaka ya Sunna:** Hiyo ni Mume kumuacha mke katika utwahara hakumuin gilia ndani yake. Muislamu anapotakapomuacha mkewe kwa sababu ya madhara yamfikayo mmoja wa wanandoa, na ikiwa haliondoki, isipokuwa kwa talaka, amsubiri mpaka apate hedhi na atwaharike, akishatwaharika asikutane nae kimwili, na hayo ni kwa ajili ya kauli yake Allah Aliyetukuka:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِذَا طَلَقْتُمُ النِّسَاءَ فَطَلِّقُوهُنَّ لِعَدَّتِهِنَّ وَأَحْصُوا الْعِدَّةَ

“*Ewe Nabii! Mtakapo wapa talaka wanawake, basi wapeni talaka katika wakati wa eda zao...*” (65: 1).

b) ‘**Talaka Bidaa**’: ni mume kumwacha mkewe akiwa katika hedhi au yuko katika damu ya uzazi au katika utahara ambao amemuingilia ndani yake au anamuacha talaka tatu kwa tamko moja wakati mmoja kama vile akisema: Yeye ameachika kisha ameachika kisha ameachika.

Hayo ni kutoka na amri ya Mtume ﷺ kwa Ibni ‘Umar رضي الله عنه alipomuacha mkewe hali ya kuwa na hedhi akamuamuru amrejee kisha amsubiri mpaka atwaharike kisha apate hedhi kisha atwaharike. Kisha akitaka ataendelea kuishi naye au akitaka atamwacha kabla hakumuingilia. Kisha Mtume ﷺ akasema, “*Hicho*

ndicho kipidi cha eda ambacho Allah ameamuru waachwe wanawake ndani yake.” (Muslim).

Na kwa kauli yake Mtume ﷺ baada yakuelezwa kuwa mtu fulani amemuacha mke wake talaka tatu katika tamko moja,

“Kinachezewa kitabu cha Allah nami bado niko baina yenu.” (Nasai).

Na ikajitokeza kwa Mtume ﷺ nasira kali. Na Talaka Bidaa, ni kama talaka ya Sunna kwa jamhuri ya wanazuoni katika kutuka kwake na kufunguka kifungo cha ndoa.

c) **Talaka Baain:** (ya kutengana moja kwa moja) ni yule atakaeacha bila kuwa na haki ya kumrejea mke huyo, na talaka hiyo muachaji anakuwa kama waposaji wengine na mtalikiwa mwenye kuachwa ana khiari akitaka atamkubali kwa ndoa nyingine na mahari mengine, na akitaka atamkataa. Na talaka inakuwa Baain katika sura tano nazo ni:

i) Ikiwa atamwacha talaka rejea kisha amwache asimrejee mpaka muda wake unamalizika, kwa kwisha eda tu tayari utengano umepatikana.

ii) Ikiwa atamwacha kwa makubaliano ya kupewa mume mali (*khului*).

iii) Ikiwa ataachwa na mahakimu wawili (mmoja kutoka kwa mume na mwingine upande wa mke). Endapo wataona Talaka ni maslahi zaidi kuliko kubakia katika ndoa.

iv) Ikiwa atamuacha kabla ya kumingilia kwa sababu mtalikiwa wa sura hii hana eda kwa hiyo utengano utapatikana kwa kumuacha tu.

v) Ikiwa atamuacha talaka tatu iwe tamko moja au mbalimbali, katika kikao kimoja au talaka ya tatu aache baada ya talaka mbili kabla yake, atakuwa ametengana naye utengano mkubwa, (mke huyo) hawi halali kwa mume huyo mpaka aolewe na mume mwingine.

d) **Talaka Rejea:** Rejea ni ambayo mume anamiliki haki ya kumrejea mtalikiwa wake. Hata kama mtalikiwa hakuridhika, kwa kauli yake Mwenyezi Mungu (*Subhanahu wa Taala*).

وَيُعَوِّلُهُنَّ أَحَقُّ بِرَدِّهِنَّ فِي ذَلِكَ إِنْ أَرَادُوا إِصْلَاحًا

“...Na waume wao wana haki ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka kufanya sulhu...”(2: 228).

Kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنه baada ya kumwacha mkewe: *“Mrejee...”*

Talaka rejea ni ile iliyo chini ya talaka tatu kwa mke aliyeingiliwa na mume kimwili ndani ya (ndoa hiyo) amemuacha bila ya kutoa badala. Na mtalikiwa talaka rejea hukumu yake (kipindi cha eda) ni kama mke, ana haki zote za mke kama vile matumizi, makazi na mengine mpaka eda imalizike. Eda yake ikimalizika ameachika kwa mume huyo, mume anapotaka kumrejea yatosha kumwambia “Nimekurejea”, yasuniwa kuweka ushahidi juu ya rejea yake kwa mashahidi wawili waadilifu.

e) **‘Talaka Bayana’**: Na Talaka bayana ni talaka ambayo mwenye kuacha haihitaji nia ya talaka bali yatosha tamko bayana la talaka kama vile kusema “Wewe umeachwa” au (nimekuacha) au linalofanana na hayo.

f) **‘Talaka ya fumbo (Kinaya)’**: “Hiyo ni talaka ambayo inahitajika ndani ya nia talaka lazima akusudie talaka, kwa sababu tamko lake si bayana- katika maana ya talaka, kama vile kusema, “Nenda kwa ndugu zako” au (toka humu ndani) au “Uiseme na mimi” na yanayofanana na hayo ambayo hayana uwazi wa talaka wala maana ya talaka, matamko kama hayo hayawi talaka isipokuwa ya ambatanishwe na nia ya talaka na Mtume ﷺ

“Amewahi kumuacha mmoja wa zake bila tamko ‘Nenda kwa ndugu zako.’ (Imepokewa na Al-Hakam, Ibn Majah, Daraqutni).

Bila shaka alinuia talaka vinginevyo tamko hili amelitumia Kaab Ibn Maliki alipoambiwa: kuwa Mtume ﷺ anakuamuru ujitenge na mkeo. Akauliza: “Nimwache au nifanyeje? Akaambiwa na Mtume ﷺ: *“Jitenge nae na wala usimsogelee”*. Akamwambia mkewe: *‘Nenda kwa ndugu zako’* Akaondoka na tamko hili halikuzingatiwa kuwa talaka.

Haya yanahusu talaka ya kinaya kilichojificha mno lakini kama kiko wazi kama vile “Wewe uko huru, au huko nami, uko huru na kinaya cha namna hii hakihitaji nia, bali itakuwa ni talaka kwa kuyatamka tu”

g) Talaka ya hapo kwa hapo na talaka ya kutungikwa:

‘Talaka ya hapo kwa hapo’ ni ile ambayo inapotolewa mke huachika hapo hapo bila kuchelewa. Na talaka hiyo mfano wake ni mume kumuambia mke wake. “Wewe umeachika” basi yule tayari baada ya mume kutamka maneno hayo atakuwa ameachika.

h) Ama ‘Talaka ya kutungika’.

Ni talaka ambayo mume ameitungika juu ya kufanyika jambo kuwa kitu hicho akikifanya au akiacha kukifanya mke atakuwa ameachika, talaka hii itabaki bila kufanya kazi mpaka yatokee yale aliyoitungika talaka juu yake. Kwa mfano, mume akimwambia mke wake” ‘Ukitoka hapa nyubani kwenda kutembea utakuwa umeachika’, au amwambie:: ‘Ukijifungua mtoto wa kike utakuwa umeachika (ndiyo talaka yako) basi huyu mke hatakuwa ameachika mpaka pale atakapotoka nyumbani, au pale atakapojifungua mtoto wa kike.

i) Talaka khiyari na kumilikisha’: Nayo ni mume kumwambia mkewe: Chagua nimekupa khiyari kutengana nami au kubaki nami, kama atachagua utengano atakuwa ameachika. Na Mtume ﷺ aliwakhayarisha wakeze wakachagua kubaki naye, kwa hiyo hawakuachika. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ قُلُوبًا لِأَزْوَاجِكَ إِنْ كُنْتُمْ تُرَدُّونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا

فَتَعَالَى رَبُّكُمْ وَأَسْرَحُكُمْ سَرَّاحًا جَمِيلًا ﴿٧٤﴾

“Ewe Nabii! Waambie wake zako: Ikiwa mnataka maisha ya dunia na pambo lake, basi njooni, nitakupeni kitoka nyumba, na kukuacheni mwachano mzuri.” (33:28).

Ama kumilikisha mtu kusema: Nimekumilikisha jambo lako au jambo lako liko mikononi mwako. Akimwambia hivyo na mke akasema: Kama hivyo ndiyo basi mimi nimeachika. Basi atakuwa ameachika talaka moja, Talaka rejea.

j) ‘Talaka kwa uwakala au maandishi’: Mtu akimuwakilisha mtu mwingine kumuacha mkewe au akamuandikia mke wake talaka akimuarifu katika maandishi hayo kuwa amemuacha, kisha akaidhinisha kwake atakuwa ameachika. Hakuna upinzani baina ya wanazuoni katika hili, kwa sababu uwakala katika haki unakubalika na maandishi yanakuwa badala ya tamko inaposhindikana kupata tamko kwa umbali au ububu mathalani.

K) ‘Talaka kwa kuharamisha’: na talaka ya kuharamisha ni mtu kusema kumwambia mkewe: Wewe ni haramu kwangu, au unakua haramu au kwa haramu, kama atakusudia kwa tamko hilo talaka itakuwa talaka, na kama atakusudia dhahari itakuwa dhahari itawajibika kwa tamko hilo kafara la Dhahari na akiwa hakukusudia talaka wala dhahari au amekusudia kiapo, kama vile angesema: Kama utafanya kadha, jambo Fulani utakuwa haramu na akafanya basi atawajibika katika hili kutoa kafara la yamini – kiapo tu.

Ibn Abbas رضي الله عنه amesema: Mume atakapomharamisha mkewe hiyo yamini aifanyie kafara, kisha akasema: Hakika kwenu kuna kiigizo kizuri kwa Mjumbe wa Allah ﷻ.

f) ‘Talaka haramu’: Na talaka haramu ni mume kumuacha mkewe talaka tatu kwa tamko moja, au matamko matatu katika kikao kimoja. Kama vile kusema: Wewe umachika talaka tatu. Au akasema: Wewe umeachika, umachika, umachika, talaka hii ni haramu kwa makubaliano ya wanazuoni wote. Kwa kauli yake Mtume ﷺ baada ya kuambiwa kuwa kuna mtu amemuacha mkewe talaka tatu kwa pamoja. Mtume ﷺ akasimama akiwa amekasirika na akasema,

“Hivi kinachezewa kitabu cha Allah nami niko baina yenu?”

Kiasi cha kusimama mtu mmoja na akasema, Ewe Mjumbe wa Allah kwanini hauniruhusu nikamuua?”

Hukumu ya talaka hii kwa Jamhuriyanawazuoni, Maimamu wanne na wengine inakubalika kuwa ni talaka tatu, na kwamba aliyeachwa kwa hii hawi halali kwa mume huyo mpaka aolewe na mume mwingine. Ama wasiokuwa jamhuri miongoni mwa wanazuoni wanaona hiyo ni talaka moja baina tu au rejea kulingana na tofauti zao. Na rai za wanazuoni (hapa) zimetofautiana. Kutokana na tofauti za dalili zilizokuja (katika suala) hili na kutokana na tofauti za kidalili jinsi kila kikundi kilivyoifahamu.

Kutokana na tofauti za wanazuoni katika suala hili Allah ndiye mjuzi zaidi. Na ni vizuri katika hili kuangalia hali ya muachaji, kama akiwa hakusudii kwa tamko lake yaani kusema, “Wewe umeachika; talaka tatu.” Isipokuwa kumtisha tu mke au amekusudia kumua pia au amemkusudia hivyo akifanya jambo fulani yaani akisema, “Wewe umeachika talaka tatu kama utafanya jambo fulani”, na akalifanya au alikuwa katika hasira kali mno, au amesema hivyo bila ya kupendelea talaka kabisa, basi itathibitika juu yake talaka moja baina, na ikiwa anakusudia kutengana nae hasa na asirudi tena kwake kwa hali yoyote basi itathibitika juu yake talaka tatu, na mke huyo hatakuwa halali kwa mume huyo mpaka aolewe na mume mwingine. Na hivi ndio kutumia dalili zote zilizokuja katika maudhui haya na ni huruma kwa ummah.

Tanbihi

Wanazuoni wamekubaliana kuwa mke aliyeachwa talaka tatu akiolewa na mume mwingine ndoa sahihi na mume huyo akamungilia, basi mke huyo kama atarudi kwa mume wa kwanza talaka za kwanza zimevunjika na mbele yake kutakuwa na talaka tatu zingine na wametofuatiana kuhusu mke aliyeachwa talaka moja au mbili, kisha akaolewa na mume mwingine kisha akarudi kwa mume wa kwanza, je ndoa hii itavunja talaka yakwanza? Au bado itahesabiwa? Imamu Maliki amesema ndoa ya mume mwingine haivunji isipokuwa talaka tatu basi

uwezekano wa kuvunja chini ya talaka tatu ni mkubwa zaidi na hiyo ndiyo kauli ya Ibnu Abbas na Ibnu ‘Umar رضي الله عنه na Allah ndiye anaye jua zaidi.

Jamhuri ya Maswahaba na Taabiina na Maimamu wanasema: Mtumwa hamiliki kwa mkewe isipokuwa talaka mbili. Kwa hiyo kama atamwacha talaka ya pili atakuwa ametengana naye (baina) na si halali kwake mpaka aolewe na mume mwingine.



Mada ya Tatu

'Khului'

1) Maana yake:

Khului ni mke kujifidia kwa mumewe aliyemchukia kwa kumpa mali ili aepukane nae.

2) Hukumu yake:

Khului inafaa ikiwa itakamilisha masharti yake kufuatia kauli ya Mtume ﷺ kwa mke wa Thabiti Ibn Qais alipomjia na kusema kuhusu mumewe:

“Ewe Mjumbe wa Allah ﷺ, simlaumu katika tabia wala dini, lakini mimi nachukia Ukafiri baada ya Uislamu. Mtume ﷺ akamuuliza, “Utarudisha bustani yake? Akajibu: Ndiyo”. Mtume ﷺ akamwambia mume yule kubali bustani na umwache Talaka moja.” (Bukhari).

3) Masharti yake:

Sharti za khului ni:

a) Chuki itoke kwa mke, endapo mume ndiye aliyemchukia mume hana haki ya kuchukua fidia kutoka kwa mke huyo, bali inamlazimu amvumilie au kama anahofia dhara amwache.

b) Mke asitake kujifidia kwa mume mpaka ifikie katika kiwango cha kuhofia madhara anahofia pamoja na hayo hatoweza kutekeleza sheria za Mwenyezi Mungu katika nafsi yake au haki za mumewe.

c) Mume asifanye makusudi kumnyanyasa mke ili apate kujifidia kama mume atafanya hivyo haitakuwa halali kwa mume huyo kuchukua chochote kutoka kwake kabisa, na kwa kufanya hivyo atakuwa amefanya maasi na Khului inathibitisha talaka isiyo na rejea. Na kama atataka kumrejea hatoruhusiwa isipokuwa kwa kufunga ndoa nyingine.

4) Hukumu zake:

Hukumu za *Khului ni*:

- a) Ni sunna kwa mume kutochukua zaidi ya mahari aliyompa kwa sababu Qais alitosheka kufidiwa bustani ambayo alimpa kuwa mahari yake na hilo ni kwa amri ya Mtume wa Allah ﷺ
- b) Endapo Khului itakuwa kwa tamko la *Khului* basi mke atakaa eda hedhi moja, kama anayejitakasa, kwa Mtume ﷺ alimuamuru mke wa ‘Thabit kukaa eda kwa hedhi moja na ikiwa kwa tamko la Talaka Jamhuri wanasema atakaa kurui tatu (ni hedhi tatu au tohara tatu).
- c) Mwenye kuacha kwa *Khului* hamiliki rejea katika eda ya mke huyo kwa sababu Khului imemtenganisha.
- e) Baba wa mke mtoto mdogo atatoa fidia kwa niaba ya binti yake anapopata madhara kwa vile mwenyewe mke ni mtoto hana uongofu.



Mada ya Nne

‘Al’Iylaa-Kiapo’

1) Maana yake:

Iylaa ni mume kuapa kwa Allah kuwa hatomuingilia mkewe kipindi kinachozidi miezi minne.

2) Hukumu yake:

Iylaa inakubalika kwa lengo la kumfundisha mke adabu kama kitakuwa chini ya miezi minne. Kwa kauli Yake Allah (*Subhanahu wa Taala*).

لِّلَّذِينَ يُؤَلُّونَ مِن نِّسَائِهِمْ تَرَبُّصُ أَرْبَعَةِ أَشْهُرٍ ۖ فَإِن فَاءُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ

رَّحِيمٌ

“Kwa wanao apa kuwa watajitenga na wake zao, wangojee miezi mine. Wakirejea basi Mwenyezi Mungu hakika ni Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.” (2:226).

Mtume ﷺ aliwaapia wakeze kwa muda wa mwezi mmoja kamili. Kiapo kitakuwa haramu ikiwa lengo lake ni madhara tu kwa mke si kwa lengo la kumfundisha. Kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Hakuna madhara wala kudhurisha.” (Ahmad na Ibnu Majah).

3. Hukumu zake:

Hukumu za Iylaa ni:

a) Muda wa Iylaa (kiapo) ukishapitia yaani miezi minne—na akawa hakumuingilia na mkewe akamtaka hilo mbele ya hakimumu imara au amwache, kwa kauli yake Allah:

وَإِنْ عَزَمُوا الطَّلَاقَ فَإِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٢٧﴾

“Na wakiazimia kuwapa talaka basi, Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mjuzi.” (2: 227).

Na kwa kauli ya Ibn ‘Umar 


“Inapomalizika miezi minne atasimamishwa mpaka amwache.”
(Bukhari).

b) Anaposimamishwa muapaji na akawa hakumwacha basi hakimumu atamuachisha ili kuondoa madhara yampatayo mke.

c) Endapo muapaji atamwacha mke baada yakusimamishwa basi talaka itakuwa kulingana na atakavyoacha, kama moja basi itakuwa talaka rejea na kama atamwacha kabisa basi hana rejea ila kwa kufunga upya ndoa .

d) Mwanamke aliyeachwa kwa kiapo atakaa eda ya talaka wala hakumtoshi kujitakasa kwa hedhi moja, kwa sababu eda si kwa usafi wa mfuko wa uzazi tu.

e) Mume kama ataacha kumuingilia mkewe kipindi cha kiapo bila kiapo naye atasimamishwa kama mwenye kuapa ima amuingilie au amwache endapo mke atadai hilo.

f) Endapo muapaji atarejea katika kiapo kabla ya muda ambao ameapa kutomuingilia kipindi hicho, itamlazimu kafara la yamini yake kwa kauli yake Mtume .

“Unapoapa na ukaona vinginevyo– ni bora kuliko yamini basi fanya ambalo ni bora kisha toa kafara ya yamini yako”
(Imepokewa na Bukhari, Muslim Abu Daud, Nasai na Tirmidh).



Mada ya Tano

Inahusu *Dhihari*

1) Maana yake:

Dhihari ni tamko la mume kumwambia mkewe, ‘Wewe kwangu ni kama mgongo wa mama yangu.’

2) Hukumu yake:

Dhihari ni haramu kwa vile Allah ameita ‘*Munkar*’ na ‘*Zuur*’ na yote hayo ni haramu. Amesema Allah Mtukufu kuhusu wafanyao *dhihar*.

وَأَيْمٌ لِّيقُولُونَ مُكْرَماً مِّنَ الْقَوْلِ وَزُوراً

“...Na hakika hao wanasema neno linalo chusha, na la uwongo...” (58:2).

3) Sheria Zake:

a) Jamhuri ya wanazuoni inasema *Dhihari* si lazima kwa tamko la mtu bali inapatikana kwa kumfananisha mke na maharim yake. Uharamu wa kudumu kama vile Binti yake, bibi yake, dada yake, shangazi yake na mama yake mkubwa au mdogo. Kwa sababu wote wako katika hukumu ya mama katika uharamu wa kudumu.

b) Itawajibika kafara juu ya mume aliyetamka *dhihari* kama ataazimia kurudi kwa mkewe aliyemtamkia *dhihari*, kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

وَالَّذِينَ يُظَاهِرُونَ مِن نِّسَابِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُوا فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِّن قَبْلِ
أَنْ يَتَمَآسَا ذَٰلِكُمْ تُوَعِّظُونَ بِهِ ؕ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٥٨﴾

“Na wale wanao jitenga na wake zao, kisha wakarudia katika yale waliyo yasema, basi wamkomboe mtumwa kabla hawajagusana. Mnapewa maonyo kwa hayo. Na Mwenyezi Mungu anayajua yote mnayo yatenda.” (58: 3).

c) Itawajibika kutoa kafara kabla ya kumingilia mke huyo au utangulizi wake kwa aya iliyotangulia.

d) Kama alimwingilia kabla ya kafara, amepata dhambi kwa hiyo atubie kwa Allah Mtukufu kwa kujuta na kuomba msamaha na atoe kafara na hakuna kitu kilichomlazimu kwa kauli yake Mtume ﷺ kwa aliyemwambia,

“Mimi nimemwambia mke wangu wewe ni kama mgongo wa mama yangu nikamuingilia kabla sijafanya kafara.” Akasema, “Nini kilichokuchukua ufanye hivyo Allah Akurehemu usimuingilie mpaka ufanye alichokuamuru Allah.” (Tirmidhi) hivyo hakumlazimu kafara.

e) Kafara ni kufanya moja ya mambo matatu, asifanye la pili isipokuwa kwa kushindwa kufanya la kwanza, nayo ni kuacha huru mtumwa Muislamu au kufunga miezi miwili mfululizo au kulisha masikini sitini, kwa kauli yake Allah Mtukufu:

فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَتَمَاسًا ۖ فَمَنْ لَمْ
يَسْتَطِعْ فَاِطْعَامُ سِتِّينَ مَسْكِينًا ۚ ذَلِكَ لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۗ وَتِلْكَ
حُدُودُ اللَّهِ ۗ وَلِلْكَافِرِينَ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥٨﴾

“Na asiye pata mtumwa kumkomboa, basi na afunge miezi miwili mfululizo kabla hawajagusana. Na asiye weza hayo basi awalishe masikini sitini. Hayo ni hivyo ili mumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na kwa makafiri iko adhabu chungu.” (58:4).

Minhajil Muslim

f) Yalazimika kufululiza funga ni sawa awe amefunga miezi miwili ya kuandamana au siku sitini kwa kuhesabu. Na akiitenganisha funga bila ya udhuru wa ugonjwa funga hiyo ni batili na itawajibika kuirudia, kwa kauli Yake Allah Mtukufu:

“Basi ni kufunga miezi miwili mfululizo.”

g) Kilicho wajibu katika kulisha ni kibaba kimoja cha ngano au vibaba viwili vya tende au shairi kwa kila masikini, na kama akitoa wajibu chini ya masikini sitini haitatosheleza.



Mada ya Sita

‘Liaan’, Laana.

1) Maana yake:

Laana maana yake mume kumshutumu mkewe uzinzi kwa kusema: Nimemuona anazini au akakataa mimba yake, kesi ikafikishwa kwa hakimu, mume atatakiwa ushahidi nao ni kuleta mashahidi wanne wanaoshuhudia kuona zinaa (inatendeka). Asipoleta ushahidi hakimu atataka mume na mke kila mmoja ajilaani mwenyewe, kwa hiyo mume atashahadia shahada nne kwa kusema: **‘Nashuhudia kwa Allah nimemuona anazini au mimba hii si yangu na atasema laana ya Allah iwe juu yake kama atakuwa miongoni mwa warongo.’** Kisha ikiwa mke atakiri kuwa amezini atapewa adhabu ya kuwa amezini na asipokiri nae atashahadia mara nne kwa kusema, **“Nashuhudia kwa Allah kuwa hakuniona ninazini au mimba hii ni yake”,** na atasema: **“Hasira za Allah ziwe juu yake kama mume atakuwa miongoni mwa wa kweli.”** Kisha hakimu atawatenganisha baina yao hawatakuwa pamoja maisha.

2) Sheria yake:

Laana ni sheria kwa kauli Yake Allah Aliyetukuka,

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ
 ثَمَانِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٤١﴾
 إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٤٢﴾
 وَالَّذِينَ يَرْمُونَ أَزْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ شُهَدَاءُ إِلَّا أَنْفُسُهُمْ فَشَهَدَةُ
 أَحَدِهِمْ أَرْبَعُ شَهَدَاتٍ بِاللَّهِ إِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٤٣﴾

“Na wale wanao wasingizia wake zao na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushuhudilia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba hakika yeye ni katika wasema kweli. Na mara ya tano kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa waongo. Na mke itamwondokea adhabu kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba huyu mume ni miongoni mwa waongo. Na mara ya tano ya kwamba ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama mumewe yu miongoni mwa wanao sema kweli.” (24: 6-9).

Laana aliyoitekeleza Mtume ﷺ kati ya Uwaimir Al-Ajlani na mkewe, na kati ya Hilal Ibn Umayyah na mkewe katika Swahili. Kwa kauli yake Mtume ﷺ,

“Wanaolaaniana wanapotengena hawakutani tena daima.”

3) Hekima yake:

Miongoni mwa hekima za sheria hii ya laana ni hizi zifuatazo:

- a) Kulinda heshima ya mume na mke, na kutunza hadhi ya Muislamu.
- b) Kumuondolea mume adhabu ya shutuma na adhabu ya zinaa kwa mke.
- c) Uwezekano wa kumkataa mtoto ambaye yawezekana asiwe wa mwenyewe.

4) Hukumu Zake:

Hukumu za Laana ni:

- a) Mume na mke wawe baleghe na akili timamu, kwa vile hakuna majukumu kwa kichaa na mtoto mdogo kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Imenyakuliwa kalamu kwa watatu...”

- b) Ni Mume kudai kumuona mke akizini, na katika kuikataa mimba akatae kuwa hakupata kuingilia kabisa, au kwa muda wa kuhusishwa na mimba kama vile

aseme amezaa chini ya miezi sita tokea wakutane. Kinyume cha hivyo hakuna laana kwani hakuna sheria ya laana kwa tuhuma tu, au dhana. Kwa kauli yake Allah Mtukufu:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ

“Ee ninyi mlioamini jiepusheni uwingi wa dhana hakika ya baadhi ya Dhana ni dhambi...” (49:12).

Na kauli ya Mtume ﷺ,

“Mjihadhari na dhana.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Tirmidhi na Malik).

Kilicho bora kuliko kumlaani katika hali ya kumtuhumu ni kumuacha tu na kwa kufanya hivyo atapumzisha nafsi yake na usumbufu wa mawazo na maumivu ya kulaumu nafsi.

c) Hakim aitekeleze laana mbele ya kundi la waumini, na iwe kwa muundo wa maneno yaliyokuja katika *Qur-aan* Tukufu.

d) Hakim ampe nasaha mume kama vile kauli ya Mtume ﷺ.

“Mume yeyote atakayemkataa mtoto wake huku akimuangalia basi mtu huyu hatomuona Allah, nae atamfedhehesha mbele ya wa mwanzo na wa mwisho.” (Nisai na Darimi).

Amnasihi mke kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Mwanamke yeyote aliyemuingiza katika familia asiyekuwa miongoni mwao, hana kitu kwa Allah na hatomuingiza peponi.” (Darimi).

e) Watenganishwe baina yao na wasijumuike baada ya hapo tena, kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Wenye kulaaniana wakishatengana hawajumuiki tena maisha.”

Minhajil Muslim

f) Mtoto atakanushika kwa mume aliyelaaniana hawatarithiana, wala hampi matumizi isipokuwa ataishi nae kama mtoto kwa tahadhari, kwa hiyo hatampa zaka (yake) na atakuwa maharimu wa watoto zake, na hakuna kisicho kati ya mume na mtoto huyo na hautakubaliwa ushahidi wa mmoja kwa mwingine. Na mtoto atakuwa wa mama tu na watarithiana, kufuatia hukumu ya Mtume ﷺ kuhusu mtoto wa waliofanya mula'ana kuwa mtoto atamrithi mama na mama atamrithi mtoto.

g) Endapo mume atasema niliongopa hapo baadaye, mtoto atakuwa wake.



Mada ya Saba

‘Eda’

1) Maana yake:

Eda ni ambayo mwanamke aliyetengana na mumewe anasubiri ndani ya siku hizo, haolewi na wala hajitokezi kwa kuolewa.

2) Hukumu yake:

Eda ni wajibu juu ya kila mke aliyetengana na mumewe iwe kwa uhai au kifo kwa kauli ya Allah Mtukufu.

وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ^ج

“Na wanawake walio achwa wangoje peke yao mpaka twahara (au hedhi) tatu zipite...” (2:228).

Na kauli Yake Aliyetukuka,

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَعَشْرًا^ط

“Na wale miongoni mwenu wanao kufa na wakaacha wake, hawa wake wangoje peke yao miezi mine na siku kumi...” (2:234).

Isipokuwa mwanamke aliyeachwa kabla ya kuingiliwa na mume huyo hana eda kama asivyokuwa na mahari isipokuwa mutaa.

Kwa kauli yake Allah.

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ طَلَقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ^ب

فَمَا لَكُمْ عَلَيْهِنَّ مِنْ عِدَّةٍ تَعْتَدُونَهَا^ط فَمَتَّعُوهُنَّ وَسَرَخُوهُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا ﴿٢٣٤﴾

“Enyi mlio amini! Mkiwaoa wanawake, Waumini, kisha mkawapa t’alaka kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayo ihisabu. Basi wapeni cha kuwaliwaza, na muwawache kwa kuwachana kwa wema.” (33: 49)

3) Hekima yake:

Miongoni mwa hekima ya sheria ya eda ni hizi zifuatazo:

- a) Kumpa mume uwezekano wa kurudi kwa mtalikiwa wake bila ya gharama ikiwa talaka rejea.
- b) Kuelewa kuwa mfuko wa uzazi una kitu au la, ili kulinda kizazi kuchanganyika.
- c) Kupata kushiriki mke katika kuliwaza ndugu wa mume na kudhihirisha mke utu wake kwa mume ikiwa eda ni ya kufiwa.

4) Aina za Eda:

Eda ina aina nyingi nazo ni:

- a) Eda ya mke aliyeachwa ambaye anapata hedhi, basi eda yake ni kurui tatu kwa kauli Yake Allah:

وَالْمُطَلَّقَاتُ يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ ثَلَاثَةَ قُرُوءٍ

“Na wanawake walio achwa wangoje peke yao mpaka t’ahara (au hedhi) tatu zipite...” (2:228).

Mwanamke kama akiachwa katika twahara kisha akapata hedhi, kisha akatwaha kisha akapata hedhi, kisha akatwaha kisha akapata hedhi kama atatwaha kisha eda yake itakuwa imekwisha, na kama tutasema madhumuni ya kurui hapa ni twahara kama ilivyo rai ya Jamhuri basi yeye eda yake itamalizika kwa kuingia kwake katika hedhi ya tatu. Pamoja na kuzingatia kuwa kama ataachwa katika hedhi, kwake haitazingatiwa kuwa hedhi ya eda. Haya ni kwa

kwa mke muungwana, ama mjakazi eda yake ni kurui mbili tu. Kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Talaka ya kijakazi ni talaka mbili na eda yake ni hedhi mbili.”
(Daraqutni) na jamhuri wamesema ni dhaifu.

b) Eda ya mtalikiwa asiye na hedhi aidha kwa ukubwa wa umri wake au udogo wake’ ni miezi mitatu, kwa kauli Yake Aliyetukuka:

وَالَّتِي يَبْسَنَ مِنَ الْمَحِيضِ مِنْ نِسَائِكُمْ إِنْ آرْتَبْتُمْ فَعِدَّتُهُنَّ ثَلَاثَةُ أَشْهُرٍ
وَالَّتِي لَمْ يَحْضَنْ

“Na wale walio sita hedhi miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, pamoja na ambao hawapati hedhi... (65: 4).”

Hii ni kwa yule muungwana mjakazi ni miezi miwili na si zaidi ya hapo.

c) Eda ya mtalikiwa mjamzito nayo ni kuzaa mimba yake yote awe muungwana au mjakazi kwa kauli Yake aliyetukuka

وَأُولَاتُ الْأَحْمَالِ أَجَلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ

“Na wenye mimba eda yao mpaka watakapo zaa.” (65: 4).

d) Eda ya mtalikiwa anayepata hedhi na hedhi yake ikakatika kwa sababu inayoeleweka au haeleweki, kama itaeleweka sababu, kama vile kunyonyesha au ugonjwa, basi huyu atasubiri kurudi kwa hedhi hata kama muda utarefuka. Na hata ikiwa kama sababu za kukatika kwake haziko wazi basi atakaa eda mwaka mmoja: Miezi tisa ni muda wa mimba na mitatu iliyobakia ni ya eda. Mjakazi atakaa eda miezi kumi na mmoja kufuatia hukumu ya ‘Umar Ibnil al-Khattwab kwa tukio hili baina ya Ansaar na Muhajirin na hakuna aliyempinga.

e) ‘Eda ya aliyefiwa na mumewe naye ni muungwana’ ni miezi minne na siku kumi na kwa mjakazi ni miezi miwili na siku tano kwa kauli Yake Aliyetukuka:

وَالَّذِينَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُونَ أَزْوَاجًا يَتَرَبَّصْنَ بِأَنْفُسِهِنَّ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ
وَعَشْرًا ۖ فَإِذَا بَلَغْنَ أَجَلَهُنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِي مَا فَعَلْنَ فِي أَنْفُسِهِنَّ
بِالْمَعْرُوفِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٢٣٤﴾

“Na wale miongoni mwenu wanao kufa na wakaacha wake, hawa wake wangoje peke yao miezi mine na siku kumi. Na wanapo timiza eda yao basi hapana ubaya kwao kwa wanao jifanyia kwa mujibu wa ada. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayo yatenda.” (2: 234).

f) Eda ya mwenye damu ya ugonjwa (*Al-Mustahaadha*): na ni ambaye damu yake haikatiki, iwapo damu yake (Hedhi) itatofautiana na damu, au ana mazoea ambayo anayafahamu basi eda yake itakuwa ya kurui. Na ikiwa damu yake haipambanuliwi wala haina ada inayomtoka mwenye kuanza, basi eda yake itakuwa ni kwa miezi nayo ni: miezi mitatu na iwapo ni kama ya mwanamke mdogo, na hukumu hii ni kipimo kwa hukumu yake katika swala.

g) Eda ya mke aliyepoteza mume wake na wala haijulikani maisha yake au amekufa atasubiri miaka minne na itaanzia ile siku ya mwisho ya kukatika habari zake (mume), kisha baada ya muda huo atakaa eda ya kufiwa ya miezi minne na siku kumi.

5) Maingiliano ya Eda:

Eda zinaweza kuingiliana, kama ifuatavyo:

a) Mtalikiwa talaka rejea aliyekufa mtalaka wake alipokuwa kwenye eda huyu atahama katika eda ya talaka na kuhamia eda ya kufiwa na hivyo basi ataka eda ya miezi minne na siku kumi kuanzia siku aliyofariki mtalaka wake. Kwani talaka rejea ina hukumu ya mke tofauti na ile baina ambayo hahami eda yake. Na rejea anarithi, na bain harithi.

b) Mtalikiwa anayekaa eda kwa hedhi akapata hedhi moja au mbili kisha akakata tamaa ya kupata hedhi tena basi huyo atahamia kwenye eda ya miezi, na atakaa eda ya miezi mitatu.

c) Mtalikiwa mdogo bado ambaye hajapata hedhi au mkubwa alie kata tamaa na hedhi akakaa eda ya mwezi mmoja au miezi miwili ya eda yake akaona damu hedhi basi huyo atahama kwenye eda ya hedhi hii kama haijakamilika eda yake kwa miezi ama kama imekamilika eda kisha ikamjia hedhi haitazingatiwa kwani eda yake imemalizika.

d) Mtalikiwa aliyeanza kukaa eda kwa miezi au kurui kabla haijamalizika ikabainika kwake mimba basi atahamia kwenye eda ya mimba kwa kauli Yake Aliyeukuka:

وَأُولَئِكَ الْأَحْمَالُ أَجْلُهُنَّ أَنْ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ

“Na wenye mimba eda yao mpaka watakapo zaa...” (65:4).

Tanbihi:

1. **Kusafishika:** inapasa kwa yule mwenye kumiliki mjakazi amwingilie kwa njia yoyote ambayo mmiliki anaweza lakini haimpasi mpaka atakaposafika ikiwa ni hedhi basi ni kwa hedhi moja, na ikiwa ana mimba ni mpaka atakapozaa. Na ikiwa hana hedhi kwa udogo wa umri au kwa ukubwa atakaa ule muda ambao unahakikishwa kuwa hana mimba; kwa neno lake Mtume ﷺ.

“Haingiliwi mwenye mimba hadi azae, na yule asiye na mimba mwenye hedhi hadi itakapotoka hedhi moja.” (Abu Daud).

Kama inavyopasa kwa aliyemwingilia muungwana kwa shubha au kubaka au kuzini nikujisafisha kwa kurui tatu ikiwa ana hedhi, au miezi mitatu ikiwa hazai, na anazaa ikiwa ana mimba kwa neno lake Mtume ﷺ.

“Anayemuamini Allah na siku ya mwisho na asiitupe mbegu yake kwa kisicho chake.” (Tirmidhi).

Na neno lake lingine,

“Usimwage maji yako katika shamba la mwenzako.” (al Hakim)

2. Kukaa Matanga msibani: *Al-Ihdaad* ni hali ya mwenye eda kujizuia kinachopelekea kuingiliwa, au anachofanya ambacho kitamvutia mwanamme kumuangalia kama vile kujipamba na kujitia manukato na kujipendezesha. Hivyo ni wajibu kwa aliyefiwa na mume wafanye *hidaada* kwa muda wote atakaokaa eda, nayo ni kutokuvaa nguo nzuri za kuvutia, na asijipake hinna au wanja na kujitia manukato na kuvaa mapambo kwa neno lake Mtume ﷺ.

“Si halali anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho kukaa matanga siku tatu ila kwa mume ni miezi minne na siku kumi.”
(Imepokewa na Bukhari, Muslim, Abu Daud na Nasai).

Na kwa kauli ya Ummi ‘Atwiya رضي الله عنها

“Tulikuwa tunakatazwa kukaa matanga msibani kwa maiti zaidi ya siku tatu isipokuwa kwa mume miezi mine na siku kumi, tusitie wanja na tusivae nguo za rangi isipokuwa nguo ya msiba ni aina ya nguo zenye mistari (zilizotengenezwa Yemen)”

Pia yalazimika juu ya mke aliye katika eda asitoke nyumbani kwake na endapo atatoka kwa haja, basi asilale isipokuwa nyumbani mwake alimokuwa wakati mmewe anafariki. Kwa kauli ya Mtume ﷺ kwa aliyemuomba amruhusu aende kwa ndugu zake baada ya kufariki mumewe:

“Kaa nyumbani kwako ambapo humo taarifa ya kufa kwa mumeo imekufikia mpaka eda imalizike” akasema: Nikakaa eda humo miezi minne na siku kumi.”



Mada ya Nane:

‘Matumizi’:

1) Maana yake:

Matumizi ni kitu kinachotolewa kama vile chakula, mavazi na mkazi kwa mwenye haki ya kupewa.

2) Nani anawajibika kupewa na wajibu huo uko juu ya nani?

Yawajibika kupewa matumizi aina sita ya watu nao ni:

a) Mke yawajibika juu ya mume ni sawa awe mke hasa kama yule anaeishi naye maisha ya ndoa au kwa hukumu kama mtalaka talaka rejea kabla eda haijamalizika kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Elewa kuwa haki zao juu yenu muwafanyie hisani katika vazi lao na chakula chao.” (Tirmidhi).

b) Aliyeachwa talaka isiyo na rejea kama ana mimba yamlazimu mtaliki katika kipindi cha eda ampe matumizi kwa kauli yake Allah Mtukufu:

وَإِنْ كُنَّ أُولَاتٍ حَمَلٍ فَأَنْفِقُوا عَلَيْهِنَّ حَتَّىٰ يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ

“...Na wakiwa wana mimba, wagherimieni mpaka wajifungue...” (65: 6)

c) Watoto wanawajibika kwa Baba na mama yao, kwa kauli ya Allah Mtukufu,

وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَذَى الْقُرْبَىٰ

“...na muwafanyie wema wazazi na jamaa...” (2:83).

Na kwa kauli ya Mtume ﷺ alipoulizwa nani mwenye haki zaidi ya kufanyiwa hisani. Akasema:

“Mama yako – mara tatu –kisha baba yako.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim Abu Daud na Nasai).

d) Watoto wadogo, wazazi wanawajibika juu yao, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَأَرْزُقُوهُمْ فِيهَا وَاكْسُوهُمْ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا

“Wapeni matumizi ndani ya mali na wavisheni na waambieni lugha nzuri.” (4:5).

Na kauli ya Mtume ﷺ

“Na mtoto anasema. Nilishe unaniachia nani?” (Ahmad na Daraqutni).

e) Mfanyakazi juu ya Mwajiri wake au Mtumwa juu ya Bwana wake analazimika Bwana wake ampe matumizi kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Jua kuwa haki zao juu yenu muwafanyie hisani katika vazi lao na chakula chao na asilazimishwe kazi asiyooweza.” (Bukhari, Muslim na Ibn Majah).

f) Wanyama matumizi yao ni juu ya wamiliki kuwapa, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Mwanamke ameingia motoni kwa sababu ya paka aliyemfunga mpaka akafa kwa njaa hakumpa chakua wala hakumwachia akaokota kujilia vijidudu vya ardhini.” (Bukhari na Muslim).

3) Kiwango cha matumzi yaliowajibika:

Matumizi kuwa ni kitu cha lazima katika kuhifadhi maisha kwa kupata kama vile chakula kinachofaa na kinywaji kizuri na vazi linalokinga joto na baridi na nyumba ya kupumzikia na kutulia hii hali na tofauti, bali tofauti iko katika kiwango, wingi na uchache, uzuri na ubaya, kwa sababu haya yanaenda kulingana na uwezo wa muhusika. Pia hali ya anayepewa na mahala alipo ni mjini au kijijini kwa hiyo ni vizuri jamb hili waachiwe viongozi Waislamu. Wao ndio hufaradhisha na kukadiria hali tofauti za Waislamu na mazingira, na desturi zao.

4) Wakati Gani Wajibu wa Matumizi Unaanguka? (Unaondoka) wajibu Unaanguka katika hali zifuatazo:

- a) Unaanguka wajibu wa mume kumpa matumizi mke anapokuwa anamuasi mume wake au hampi unyumba mumewe, kwa sababu matumizi ni kwa kumtumikia na kuwa nao katika harakati za unyumba, yanapokosekana hayo na matumizi hayapo.
- b) Kwa mwanamke mtalikiwa talaka rejea kwa kwisha eda yake, kwani kwa kwisha eda uhusiano unakoma.
- c) Kwa mtalikiwa mjamzito utakoma wajibu wa matumizi kwa kuzaa mimba yake isipokuwa kama mtoto huyo atanyonyeshwa na mama huyo upo wajibu wa kupewa malipo ya unyonyeshaji kwa kauli ya Allah Mtukufu.

أَسْكِنُوهُنَّ مِمَّنْ حَيْثُ سَكَنْتُمْ مِّنْ وَّجَدِكُمْ وَلَا تَضَارُّوهُنَّ لِيُتَضَيَّقُوا عَلَيْهِنَّ

**“Kama watawanyonyeshea (watoto zenu) wapeni malipo yao.
Na mshauriane kati yenu kwa uzuri.” (Twalaq:6).**

- d) Utaondoka wajibu (wa kuwapatia) baba na mama kwa kutajirika wazazi hao au kukosa huyo mtoto uwezo wa kuwapa matumizi hayo, kiasi cha kukosa chakula cha ziada cha siku yake, kwa sababu Allah hakalifishi nafsi ila kwa ilichoipa nafsi hiyo.
- e) Wajibu wa baba kuwapa watoto matumizi utasita pindi anapobaleghe mtoto mwanauume au kuolewa mwanamke. Itavuliwa katika hali hiyo endapo atabaleghe mtoto mwanamume hali ana ugonjwa usiotibika au kichaa, kwa hali hiyo wajibu wa kumpa matumizi utaendelea kwa baba.

Tanbihi:

Ni wajibu kwa Muislamu kudumisha uhusiano mzuri na ndugu zake. Na ni ndugu zake wa upande wa baba yake na mama yake, kwa hiyo aliye na haja ya chakula

Minhajil Muslim

au mavazi au makazi basi ampe chakula au amvishe au ampatie makazi kama ana ziada katika mali zake na aanzie na aliyekaribu zaidi kisha anayefuata na kadhalika, kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Mkono wa mtoaaji uko juu, anaza na aliye katika familia: mama yako, baba yako, dada yako, na ndugu, kisha aliye karibu zaidi na wewe na anayefuatia.” (Imepokewa na Nasai, Ahmad na al Hakim).

Endapo mwenye mnyama amegoma kumpa mnyama wake chakula basi dola itamuza au kumchinja mnyama huyo ili asiadhibiwe kwa njaa, na kumuadhibu mnyama ni haramu kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Mwanamke ameingia motoni kwa sababu ya paka amemfunga akafa hakumpa chakula, wala hakumwacha akapata kula vijidudu vya ardhini.”



Mada ya Tisa

Malezi:

1) Maana yake:

Malezi ni kumtunza mtoto mdogo na kumlea mpaka umri wa kubaleghe.

2) Hukumu yake:

Malezi ni wajibu wa kuwalea watoto wadogo kwa kutunza miili yao akili zao na dini zao.

3) Nani analazimika kutekeleza wajibu huo?

Wajibu huo uko juu ya baba na mama, wanapokosekana basi ndugu wa karibu na wanaofuatia miongoni mwa ndugu zao kama ndugu hakuna basi ni serikali au Waislamu.

4) Nani mwenye haki zaidi ya kulea mtoto?

Unapotokea utengano kati ya wazazi wa mtoto kwa talaka au kifo basi mwenye haki zaidi ya kumtunza ni mama yake kwa muda wa kuwa mama huyo hajaolewa na mume mwingine, kwa kauli ya Mtume ﷺ kwa mama aliyemlalamikia kunyang'anywa mtoto wake.

“Wewe ndiye mwenye haki zaidi madamu hajaolewa.” (Ahmad na Abu Daudi)

Kama mama hayupo basi mama wa mama (bibi) kama bibi hayupo basi mama wa mama (bibi) kama bibi hayupo basi ni mama mkubwa au mdogo kwa sababu ni mama mkubwa au mdogo ni sawa na mama kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Mama mkubwa au mdogo ni sawa na mama.” (Imepokewa na Bukhari, Abu Daud na Tirmidhi).

Kama hayupo basi mama yake baba (bibi) kama hayupo basi dada, kama hayupo shangazi, kama hayupo binti wa ndugu, kama hao waliotajwa hawakupatikana

basi malezi yatahama kwa baba yake mtoto kisha baba yake, kisha kaka yake, kisha ami yake kisha wa karibu zaidi, kisha anayefuatia miongoni mwa ‘aswaba. Na wa baba mmoja mama mmoja anatangulizwa juu ya wa baba mmoja tu, pia kwa wanawake.

5) Wakati gani haki ya ulezi Inakoma?

Kwa kuwa madhumuni ya ulezi ni kutunza maisha ya mtoto na kumlea kimwili, kiakili na kiroho basi haki hiyo itakoma pale lengo na madhumuni ya malengo yanapokosekana, kwa hiyo haki ya mama itaanguka pale tu kama ataolewa na mume asiyekuwa ndugu wa mtoto anayelelewa, kwa kauli ya Mtume ﷺ: “...*Madamu haujaolewa.*” Kwa sababu kuolewa kwake na mume asiye ndugu wa mtoto kutakuwa na ugumu kumtunza mtoto na kumlea.

Pia itakoma haki ya ulezi kwa mlezi kama (mama):

- a) Atakuwa kichaa au punguani.
 - b) Atakuwa mgonjwa ugonjwa wa kuambukiza kama ukoma, na kadhalika.
 - c) Atakuwa mdogo hajibaleghe na hana uwezo wa kutunza mali.
- Atakuwa hawezi kutunza mtoto na kutunza mwili wake, akili yake na dini yake.
- d) Atakuwa kafiri, ili kuhofia dini yake na itikadi yake.

6) Kipindi cha malezi:

Kipindi cha malezi kinaanzia kuanza kumlea mpaka ana baleghe mvulana, na kuolewa msichana na kukutana na mwanaume, isipokuwa katika hali ya utengano katika mume na mke na mama akawa ndiye mlezi au mtu mwingine basi kipindi cha malezi ya msichana kinaishia miaka saba tu. Baada ya hapo malezi yanahamia kwa baba, kwani yeye ndiye mwenye haki zaidi kuliko walezi wengine, katika umri huo pia mvulana akifikia umri wa miaka saba atapewa khiyari kuishi na mama au baba yeyote atakayemteua na wazazi wakimgombea basi itapigwa kura kati yao.

7) Matumizi ya mtoto na malipo ya mlezi:

Baba wa mtoto anayelelewa ndiye mwenye wajibu wa kumpa matumizi huyo mtoto, pia malipo ya mlezi kulingana na hali yake, kwa sababu mlezi ni kama mnyonyeshaji, anayenyonyesha anapewa malipo kwa kauli ya Allah Mtukufu

فَإِنْ أَرْضَعْنَ لَكُمْ فَآتُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ^ط

“Kama watawanyonyesha wapeni malipo yao.” (Twalaq: 6)

Isipokuwa kama mlezi amejitolea tu basi hakutakuwa na malipo, na makadirio ya matumizi ya mtoto na malipo ya mlezi yatakuwa kulingana na uwezo wa baba mwenye mtoto kwa kauli ya Allah:

لِيُنْفِقَ ذُو سَعَةٍ مِّن سَعَتِهِ^ط وَمَن قُدِرَ عَلَيْهِ رِزْقُهُ فَلْيُنْفِقْ مِمَّا آتَاهُ اللَّهُ^ع
لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا مَاءً آتَاهَا^ع

“Na atoe mwenye uwezo kulingana na uwezo wake na asiyekuwa nauwezo atoe alichompa Allah, Allah hailazimishi nafsi ila kile alichoiipa.” (Twalaq:7)

8) Mtoto anaelelewa kutembelea baba na mama yake:

Mtoto akifikia umri wa miaka saba na akapewa hiyari kati ya baba na mama yake kama atamteua mama basi atakuwa kwa mama usiku na mchana atakuwa kwa baba, na kama atamteua baba basi atakuwa kwa baba usiku na mchana ndiyo bora zaidi kwa malezi yake, kwa vile baba ndiye anayemfundisha na kumuonesha mara nyingi wakati mambo hayo mama hayafanyi.

Pia ikiwa kamteua baba basi mtoto asizuiliwe wakati wowote kwenda kwa mama yake inapowezekana kwa sababu kuunga na kuimarisha udugu ni wajibu na kukata udugu ni haramu.

9) Kusafiri na mtoto:

Mmoja wa wazazi wawili anapotaka kusafiri safari ya kurudi baada ya hapo mjini kwake mtoto atabaki kwa aliye nyumbani, na ikiwa anayetaka kusafiri harudi nyumbani, yataangaliwa maslahi ya mtoto, Je, yatakuwa kwa asiyesafiri awe baba au mama, au yatakuwa pamoja na anayeondoka kwenda kuishi nchi nyingine, basi pale maslahi ya mtoto yaliyo ndipo atakapokuwa mtoto kwa sababu maslahi ya mtoto ndio madhumuni ya sheria katika malezi yake.

10) Mtoto anaelewa ni Amana:

Mlezi (mama) anawajibika aelewe kuwa mtoto anaelewa ni amana hivyo basi analazimika kumchunga na kumtunza kwa ukamilifu; kama atahisi kuwa yeye hawezi malezi kamili, analazimika aweke jukumu hili kwenye mkono wa wenye uwezo wa kutekeleza hayo. Lisiwe lengo lake la msingi kupata mshahara utokao kwa mwenye mtoto, kwa hiyo atang' ang' ania kulea hali anajua uwezo huo hana ili mradi tu apate mshahara. Kutokana na haya analazimika mlezi wa mtoto, pia viongozi wa nchi wakati wote wachunge katika mlango wa malezi maslahi ya mtoto tu, nayo ni kulea mwili wake, akili yake na roho yake, bila kuangalia lolote katika yasiyokuwa hayo kwa sababu kutunza mtoto ndio madhumuni ya msingi katika malezi kwa muweka sheria.



Mirathi na Hukumu Zake

Mada ya Kwanza

Hukumu ya kurithiana:

Kurithiana kati ya Waislamu ni wajibu uliothibitika kwa Kitabu na Sunnah. Amesema Allah Mtukufu:

لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ
الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ أَوْ كَثُرَ ۗ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٧﴾

“Wanaume wana sehemu katika wanayo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Na wanawake wanayo sehemu katika waliyo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Ikiwa kidogo au kingi. Hizi ni sehemu zilizo faridhiwa.” (4:7)

Na Akasema:

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثَيَيْنِ ۗ

“Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili...” (4: 11).

Na amesema Mtume ﷺ,

“Wapeni mafungu wenye mafungu yao, kitakachosalia ni aliye karibu zaidi mwanamume.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Tirmidhi na Ahmad).

Na amesema:

“Hakika Allah amempa kila mwenye haki haki yake, hakuna wasia kwa mrithi.” (Imepokewa na Nasai, Ibn Majah, Abu Dawud na Tirmidhi).

Mada ya Pili

Sababu za Kurithi

Pingamizi na Sharti zake:

1) Sababu za kurithi:

Mtu hapati kumrithi mwingine isipokuwa kwa kuwepo moja ya sababu tatu, nazo ni:

a) Nasaba, yaani udugu, kama vile kuwa anayerithi ni baba wa anayerithiwa, au ni miogoni mwa watoto zake au jamaa zake kama vile ndugu na watoto wa ndugu, maami na watoto zao, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَلِكُلِّ جَعَلْنَا مَوْلَىٰ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ^ع

“Na kila mmoja tumemwekea warithi katika waliyo yaacha wazazi wawili na jamaa...” (4: 33).

b) Ndoa, mkataba–makubaliano sahihi juu ya mke, hata kama hakingiliwa wala kukaa faragha kati ya mume na mke, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَلَكُمْ نِصْفُ مَا تَرَكَ أَزْوَاجُكُمْ إِنْ لَمْ يَكُن لَّهُنَّ وَلَدٌ^ع

“Na fungu lenu ni nusu walicho acha wake zenu ikiwa hawana mtoto...” (4:12).

Na wanarithiana mume na mke, kama mke yuko katika kipindi cha eda rejea, na asiyekuwa na talaka rejea akiwa amemwacha katika ugonjwa aliofia huyo mume.

c) *Al-Walaau*: *Walaau* maana yake mtu kama atampa uhuru mtumwa wake, kwa tendo hili atamiliki utawala unaoitwa *Walaau*. Kama atakufa aliyeacha huru na akawa hana wakurithi basi huyu aliyekuwa bwana atamrithi kwa kauli ya Mtume ﷺ.

‘Walaau ni wa aliyempa uhuru mtumwa.’ (Bukhari na Muslim)

2) Pingamizi za kurithi:

Inaweza ikapatikana sababu ya kurithi lakini ikatokea pingamizi akashindwa mtu kurithi kwa pingamizi hizo ambazo ni:

a) **Ukafiri:** Ndugu Muislamu hawezi kumrithi ndugu yake kafiri, wala kafiri hawezi kumrithi ndugu yake Muislamu kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Kafiri hamrithi Muislamu na Muislamu hamrithi kafiri”
(Imepokewa na Ahmad, Darqutni na Hakim)

b) **Kuuwa:** Aliyeua hapati mirathi ya aliyeuawa, ikiwa ni adhabu kwake kwa jinai yake, ikiwa uuaji ni wa makusudi, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Muuaji hana kitu katika mali ya muuliwa.” (Abdu Daar na Baihaqi).

c) **Utumwa:** Mtumwa hapati mirathi na wala harithiwi sawa awe mtumwa kamili au pungufu kama yule aliyekuwa sehemu mtumwa na sehemu muungwana na mukaatab (muandikiwa) na mjakazi aliyezaa na Bwana wake (mama mtoto) kwani wote bado wako katika hukumu ya utumwa. Baadhi ya wanazuoni wakasema: Atapata kurithi na atarithiwa kwa kadiri ya uhuru alionao, kwa hadithi aliyopokea Ibnu ‘Abbas رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema:

“Aliyeachwa huru sehemu na akabaki mtumwa sehemu nyingine atarithi na atarithiwa kwa kadiri ya uhuru alionao.” (Angalia Mughni ya Ibnu Qudama).

d) **Zinaa:** Mtoto aliyezaliwa kwa zinaa hamrithi baba yake, wala baba yake hamrithi mtoto, isipokuwa atamrithi mama yake na mama atamrithi mwanawe. Kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Mtoto ni wa kitanda na kwa mzinifu ni jiwe”. (Imepokewa na Bukhari, Abu Dawud, Ibn Majah na Tirmidhi)

e) **Laana (Kulaaniana):** Mtoto wa waliyelaaniana hawezi kumrithi baba yake aliyemkataa na baba yake pia hawezi kumrithi mwanae huyo, kwa kigezo cha

mtoto kuwa wa zinaa.

f) Kutokutoa sauti wakati wa kuzaliwa. Mtoto atakayezaliwa hali ya kuwa amekufa na kutoa sauti wakati wa kuzaliwa harithi na wala harithiwi kwa kukosa uhai unaofuatiwa na kifo ambao kurithi kunapatikana.

3) Shatri za kurithi:

Ili Kurithi kuwe sahihi yapatikane masharti yafuatayo:

- a) Kusiwepo pingamizi miongoni mwa pingamizi zilizotangulia kutajwa hapo juu.
- b) Kufa kwa mrithi japo kwa hukumu kama vile kadhi akahukumu kuwa aliyepotea amefariki kwa mfano. Kwa sababu aliye hai harithiwi kwa makubaliano ya wanazuoni wote.
- c) Uhai wa anayerithi wakati wa kufa anayerithiwa. Kama kulikuwa na mwanamke ambaye mmoja wa watoto wake amekufa, na huyo mama tumboni mwake mna mimba, basi mimba hii ina haki ya kumrithi ndugu yake, ikiwa wakati wa kuzaliwa atatoa sauti, sauti yake itatuthibitishia uhai wake siku aliyofariki ndugu yake, lakini kama ujauzito huo mama kaupata baada ya kufa huyo ndugu, mtoto atakayezaliwa hana haki ya kupata mirathi ya ndugu yake huyo aliyefariki. Kwani wakati huo anakuwa bado hajaumbwa.



Mada ya Tatu

Ufafanuzi wa anayerithi miongoni mwa Wanaume na Wanawake

1) Wanarithi katika wanaume, nao wanagawika sehemu tatu:

a) Mume anamrithi mkewe akifariki, hata kama mtalikiwa yuko katika eda, kwa muda wakuwa eda bado inaendelea, ikimalizika eda mume hana mirathi kwa mke huyo.

b) Muacha huru au aswaba zake wanaume anapokosekana.

c) Ndugu, nao ni mashina, matawi na hawashi (pambizo), mashina: Ni baba na babu hata kama wa juu, na matawi ni: Mtoto na mtoto wa mtoto na kwenda chini, na hawashi wa karibu nao ni ndugu na watoto zao na kwenda chini, na ndugu wa mama mmoja. Na hawashi wa mbali nao ni: Ami, mtoto wa Ami na kwenda chini, wa baba mmoja mama mmoja au baba mmoja tu. Hawa ndio wanaume wanaorithi na haipatikani taswira ya kuwepo wote hao hali yakuwa ni warihi wakati mmoja kwa mrithiwa mmoja, kwani wengine kuwepo kwao kunamnyima Ami kurithi na kadhalika, kwa hiyo kama walikusanyika wote kwa marehemu mmoja wakati mmoja basi hakuna atakayerithi miongoni mwao isipokuwa watatu tu. Mume, mtoto na baba tu.

2. Wanawake wanaorithi:

Wanawake wanaorithi wanagawika sehemu tatu: Nazo ni:

a) Mke (b) Muacha huru mtumwa c) Ndugu: nao wanagawika sehemu tatu: Mashina nao ni: Mama na bibi mzaa mama, na matawi, nayo ni Binti na Binti wa mtoto wa kiume na kuelekea chini hawashi wa karibu nae ni dada yeyote.

Tanbihi:

Shangazi, mama mkubwa na mdogo, binti wa mtoto mwanamke, binti wa ndugu na binti wa Ami hawarithi.

Mada ya Nne

Kubainisha Mafungu Kadiriwa:

Mafungu yaliyowekewa viwango ndani ya kitabu cha Allah Aliyetukuka katika *Surat Nisai* Sura ya tatu, ni sita na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

1) Nusu na inarithiwa na watu watano nao ni:

a) Mume, kama mke aliyefariki hakuacha mtoto mwanamume au mwanamke wala hakuacha mtoto wa mtoto wake mwanamume ni sawa awe mwanamume au mwanamke.

b) Binti, anapokuwa peke yake hana kaka au dada au ndugu mmoja au zaidi kwani binti harithi nusu isipokuwa anapokuwa peke yake.

c) Binti wa mtoto mwanamume kama atakuwa peke yake wala hakuwa pamoja na mtoto wa mtoto mwanamume mwingine kama yeye.

e) Dada wa baba mmoja anapokuwa peke yake, hana kaka, wala baba, wala mtoto wa mtoto mwanamume.

2) Robo (Moja ya nne) ni fungu la watu wawili tu, nao ni:-

a) Mume kama mke amecha mtoto au mtoto wa mtoto mwanamume ni sawa awe mwanamume au mwanamke.

b) Mke ikiwa mume hakuacha mtoto au mtoto wa mtoto mwanamume ni sawa awe mwanamume au mwanamke.

3) Thumni (Moja ya nane) nalo ni fungu la mmoja tu naye ni:

Mke, hata kama wakiwa zaidi ya mmoja watagawa wote sawa sawa kati yao, na hii ikiwa mume amecha mtoto, au mtoto wa mtoto wa mwanamume awe mwanamume au mwanamke.

4) Thuluthi mbili (mbili ya tatu): ni fungu la watu wanne, nao ni:

- a) Mabinti wawili na zaidi, wanapokuwa mabinti watupu, yaani hawana kaka yao.
- b) Mabinti wawili wa mtoto mwanamume wawili na zaidi, ikiwa hakuna mtoto awe mwanamume au mwanamke, na asiwepo baina yao yaani mtoto mwanamume aliyekuwa mtoto wa mtoto mwanamume kama walivyo wao.
- c) Dada wa baba mmoja mama mmoja wawili na zaidi wakiwa bila ya baba, na mtoto wa marehemu awe mwanamume au mwanamke, na asiwepo kaka na baba mmoja mama mmoja.
- d) Dada wa baba mmoja wawili na zaidi, kama hawatakuwa pamoja na waliotajwa kwa dada wa baba mmoja na mama mmoja, asiwepo kaka wa baba mmoja.

5) Thuluthi (moja ya tatu): hili ni fungu la watu watatu, nao ni:

- a) Mama ikiwa marehemu hakuacha mtoto wala mtoto wa mtoto mwanamume, awe mwanamume au mwanamke, wala hakuna idadi ya ndugu wawili na zaidi wawe wanaume au wanawake.
- b) Ndugu wa mama mmoja wakiwa zaidi ya mmoja kama vile wawili na zaidi ikiwa marehemu hakuacha baba, wala babu, wala mtoto wala mtoto wa mtoto mwanamume, ni sawa awe mwanamume au mwanamke.
- c) Babu, akiwa anarithi pamoja na ndugu na ikawa thuluthi kwake ndio bora, na hiyo ni inapokuwa idadi ya ndugu wanaume zaidi ya wawili na wanawake zaidi ya wanne.

Tanbihi: Thuluthi iliyosalia:

1. Kama mwanamke amekufa akaacha mume, mama na baba yake tu bali kigawio chake kitakuwa ni sita mume nusu yake nayo ni tatu, na mama thuluthi ya nusu iliyosalia nayo ni moja na baba mbili zilizosalia kwa taaswibi.

2. Na akifa mume akaacha mkewe, mama yake na baba yake tu, basi kigawio kitakuwa nne: Robo yake nayo ni moja itakuwa ni kwa mke, na mama thuluthi ya kilichobakia anayo ni moja na baba anapata kilichosalia nacho ni mbili kwa taaswibi. Kwa hiyo mama katika Mas-ala haya ni mbili hakupata thuluthi ya mali yote, bali amepata thuluthi ya kilichosalia katika mali ya marehemu mwanawe. Na hukumu hii ndio aliyoitoa ‘Umar رضي الله عنه na kwa sababu hiyo Mas-ala mbili hizi zinajulikana kuwa ni mas-ala mbili za ‘Umar رضي الله عنه.

6) Sudusi, (moja ya sita) ni fungu la watu saba, nao ni:

a) Mama, ikiwa marehemu ameacha mtoto au mtoto wa mtoto mwanamume, au alikuwa na kundi la ndugu kuanzia wawili kuendelea mbele wawe wanaume au wanawake, wawe baba mmoja mama mmoja, au baba mmoja au mama mmoja ni sawa wawe wanapata mirathi au wamepingwa.

b) Bibi, ikiwa aliyekufa hana mama atarithi yeye tu kama atakuwa peke yake na akiwepo bibi mwingine katika ngazi yake watagawana sawa sawa.

Tanbihi:

Bibi halisi katika kurithi ni bibi mzaa mama ama bibi mzaa baba hakika yeye anabebwa na Bibi mzaa mama tu.

c) Babu, anapata sudusi nae ana mrithi katika hali zote sawa marehemu awe ana mtoto au hana.

d) Babu atapata sudusi kama baba hayupo tu kwani babu anakaa nafasi ya baba.

e) Ndugu wa mama mmoja awe mwanamume au mwanamke, anapata sudusi kama marehemu hakuacha baba wala babu, wala mtoto wala mtoto wa mtoto mwanamume, awe mwanamume au mwanamke, kwa sharti awe peke yake asiwepo kaka wa mama mmoja na dada, mkubwa au mdogo.

f) Mtoto mwanamke wa mtoto mwanamme, atapata sudusi kama kuna binti wa marehemu mmoja na huyu mjukuu akiwa hana kaka, wala mtoto wa Ami yake aliye katika ngazi yake hakuna tofauti kati ya mjukuu mmoja au zaidi katika kurithi sudusi kwa binti wa mtoto wa kiume au wengi.

g) Dada wa baba mmoja kama atakuwa na dada mmoja wa baba mmoja mama mmoja, na akawa hana kaka wa baba mmoja wala wa mama mmoja, wala wa babu wala wa mtoto wala wa mtoto wa mtoto mwanamume.



Mada ya Tano

Inahusu Taaswibi:

1) Maana ya 'Aaswib':

Aaswib katika Istilahi: Ni yule anayekusanya mali zote anapokuwa peke yake au (kama kuna mafungu basi anachukua yote) kilichobakishwa na mafungu na atakosa endapo mafungu yamemaliza mali yote, na hayo ni kwa kauli ya Mtume ﷺ katika Hadithi sahihi:

“Wapeni mafungu wenye mafungu yao na kilicho salia mpeni mwanamume wa karibu”.

2) 'Vigao vya Aaswib':

'Aswaba wana sehemu tatu:

a) **Aaswib binafsi:** Kila mwanamume ndugu ambaye uhusiano wake na marehemu haukuwa kwa mtu mwanamke tu, naye ni baba na babu na kushuka wajukuu na mtoto na mtoto wa mtoto mwanamume na kushuka, kaka wa baba mmoja mama mmoja, au baba mmoja, na mtoto wa kaka baba mmoja mama mmoja au baba mmoja, na kushuka, Ami wa baba mmoja mama mmoja au baba mmoja mtoto wa Ami baba mmoja mama mmoja au baba mmoja, hata kama atashuka, na muacha huru mtumwa awe mwanamume, au mwanamke na Aswaba wa muacha huru mtumwa waliokuwa ni aswaba binafsi na Baitul Maal (Hazina).

b) *Aaswib kwa Mwingine:* Nao ni kila mwanamke aliyerithi pamoja na mwanamume kwa kupata mwanamume mara mbili ya mwanamke. Nao ni dada wa baba mmoja mama mmoja anaporithi na kaka yake wa baba mmoja mama mmoja, na dada wa baba mmoja anaporithi na kaka yake wa baba mmoja, na binti wa mtoto mwanamume anaporithina kaka yake au anarithi na Mtoto wa mtoto mwanamume, kama huyu binti wa mtoto wa kiume Ibni hana fungu, kama atakuwa na fungu basi harithi kwa taaswibi pamoja na mtoto wa mtoto mwanamume aliye katika ngazi ya chini kuiko yeye. Kwa mfano mtu anafariki akaacha mtoto mwanamke (binti) na mtoto (binti) wa mtoto mwanamume na mtoto wa mtoto wa mtoto mwanamume hapa huyu mtoto atapata nusu na yule

binti wa mtoto mwanamume atapata sudusi kamilisho la thuluthi mbili, na yule mtoto wa mtoto wa mtoto wa mtoto mwanamume anachukua kilichosalia kwa Taaswibi. Maelezo haya yote yanamuhusu binti wa mtoto mwanamume aliye ngazi moja na mtoto wa mtoto mwanamume, au binti wa mtoto ambaye ngazi yake ni ya juu kuliko binti wa mtoto, na kama ngazi yake ni ya chini kwa ngazi moja au zaidi, hapa huyu aliye juu atamzuia aliye chini, kwa hiyo binti hapa atazuiliwa kabisa.

c) Aaswib pamoja na mwingine. Nayo ni kila mwanamke anayekuwa aswaba kwa kuwa pamoja na mwanamke mwingine, na huyo ni dada wa baba mmoja mama mmoja na zaidi, anaporithi pamoja na binti mmoja au mabinti au pamoja na Binti wa Ibn au binti na binti zake, na dada wa baba mmoja sawa na dada wa baba mmoja mama mmoja katika haya yote (kama yeye hayupo) na kitakachosalia baada ya kuchukua binti mmoja au mabinti au binti wa mtoto mwanamume mabinti zake fungu lao atachukua dada kama yuko peke yake, au pamoja na wenzake kama ni zaidi ya mmoja na watagawana sawa. Pamoja na kuzingatia kuwa hapa dada wa baba mmoja na mama mmoja ana nguvu za kaka wa baba mmoja mama mmoja, kwa hiyo atamzuia dada wa baba mmoja na dada wa baba mmoja ambaye ana nguvu za kaka yake, kwa hiyo atamzuia mtoto wa kaka yoyote.

Tanbihi: Mas-ala ya Ushirika:

Ikiwa mwanamume amefariki akaacha; mume, mama, ndugu wa mama mmoja, na kaka wa baba mmoja, mama mmoja au zaidi, kigawo hapa ni sita: Mume anapata nusu, nayo ni tatu, na mama sudusi nayo ni moja na ndugu wa mama mmoja thuluthi nayo ni mbili, hakuna kilichosalia kwa ndugu wa baba mmoja mama mmoja, kwa sababu yeye ni aswaba na aswaba anakosa endapo mafungu yatamaliza hisa zote kama ilivyo hapa, hivi ndivyo anavyotakiwa katika mas-ala hii. Isipokuwa ‘Umar رضي الله عنه amehukumu kumshirikisha ndugu wa baba mmoja, mama mmoja sawa na wa mama mmoja, mwanaume sawa na mwanamke, kwa sababu hii iliitwa ushirika, au mas-ala ya jiwe, kwa sababu ndugu wa baba mmoja mama mmoja walimwambia ‘Umar رضي الله عنه pale mwanzo alipowanyima: Kadiria kuwa baba yetu alikuwa jiwe hivi mama yetu si mmoja?! Vipi tunanyimwa wanapewa ndugu zetu!? ‘Umar رضي الله عنه akatosheka na hoja zao na akahukumu washiriki katika thuluthi pamoja na ndugu zao wa mama mmoja.

Mada ya Sita

'Hajbu':

1) Maana yake:

'Hajbu': Ni kuzuia kupata mirathi yote au sehemu yake

2) Vigawanyo viwili vya Hajbu

a) Kuzuia kwa upungufu:

Na kinachokusudiwa katika tamko hili: ni kumuhamisha anayerithi kutoka kwenye fungu kubwa kwenda kwenye fungu dogo, au kutoka kwenye fungu kwenda kurithi kwa taaswibi, au kinyume chake, yaani kutoka kwenye taaswibi kwenda kwenye fungu.

Wanaozuia kwa upungufu ni watu sita, nao ni:

-Mtoto mwanamume, na mtoto wa mtoto mwanamume, na kuelekea chini wanamzuia mume kutoka kwenye nusu kwenda kwenye robo, na mke kutoka kwenye robo kwenda kwenye thumni na wanamzuia baba na babu kwa kuwahamisha kutoka kwenye taaswibi kwenda kwenye sudusi kwa fungu.

-Binti, anamzuia binti wa mtoto mwanamume kwa kumuhamisha kutoka kwenye nusu, kwenda kwenye sudusi, na kuwahamisha binti wawili na zaidi wa mtoto mwanamume kwa kuwahamisha kutoka kwenye thuluthi mbili kwenda kwenye sudusi, na kumzuia dada wa baba mmoja mama mmoja au baba mmoja, kutoka kwenye nusu kuja kwenye taaswibi na dada wawili au zaidi wa baba mmoja mama mmoja au baba mmoja kutoka kwenye thuluthi mbili kwenda kwenye taaswibi, na anamzuia mume kwa kumuhamisha kutoka kwenye nusu kwenda kwenye robo, na mama kutoka kwenye thuluthi kwenda kwenye Sudusi, na baba na babu kwa kuwahamisha kutoka kwenye taaswibi kwenda fungu la Sudusi, na watachukua kilichosalia ikiwa kipo kwa Taaswibi.

-Binti wa mtoto mwanamume, anamzuia aliye chini yake miongoni mwa mabinti wa watoto wakiwa hawana kaka wa kuwapatia taaswibi au mtoto wa Ami yao

aliye katika ngazi yao, kwa kumuhamisha akiwa mmoja kwenye nusu kwenda kwenye Sudusi, na anamuhamisha dada wa baba mmoja mama mmoja kutoka kwenye nusu kwenda kwenye taaswiba, pia wa baba mmoja na anawazuia dada wawili na zaidi wa baba mmoja mama mmoja, au baba mmoja mama mmoja kwa kuwatoa kwenye thuluthi mbili kwenda kwenye taaswibi pia anamzuia mume mke, mama, baba na babu kama alivyowazuia binti.

-Ndugu wawili na zaidi yeyote yule anamzuia mama, kwa kumuhamisha kutoka kwenye thuluthi kwenda kwenye Sudusi.

-Dada wa baba mmoja mama mmoja, anamzuia dada wa baba mmoja kwa kumuhamisha kutoka kwenye nusu kwenda kwenye Sudusi, kama hakuna kaka yake yaani wa baba mmoja atakayerithi nae kwa Taaswibi, na dada wawili wa baba mmoja na zaidi kwa kuwahamisha kutoka kwenye thuluthi mbili kwenda kwenye sudusi kama hawana kaka wa baba mmoja watakayerithi naye kwa taaswibi.

b) 'Hajbu' ya kuangusha:

Madhumuni ya...*Hajbu'* ya kuangusha ni kumnyima anayerithi fungu lote ambalo lilikuwa haki yake kulipata kama si huyu aliyemzuia, na wanaozuia kwa kuangusha ni watu kumi na tisa nao ni:

i) Mtoto mwanaume, mtoto wa mtoto hapati mirathi pamoja na mtoto mwanamume, pia binti wa mtoto mwanamume, wala ndugu mwanamume au mwanamke wa baba mmoja mama mmoja au baba mmoja au mama mmoja, pia Ami hapati mirathi mbele ya mtoto mwanamume ni sawa awe ami baba mmoja, mama mmoja au baba mmoja tu.

ii) Mtoto mwanamume wa mtoto mwanamume, aliye chini yake hapati mirathi mbele yake kama vile mtoto wa mtoto wa mtoto mwanamume, pia anamzuia yule aliyezuiliwa na mtoto mwanamume bila tofauti sawa kwa sawa.

iii) Binti, harithi pamoja na ndugu wa kiume wa mama mmoja.

iv) Binti wa mtoto mwanamume, harithi pamoja na ndugu wa kiume wa mama mmoja.

v) Binti wawili na zaidi, ndugu wa mama mmoja hapati mirathi pamoja nao wala binti wa mtoto mwanamume awe mmoja au zaidi ikiwa hawana kaka au mtoto mwanamume wa ami yao atakayerithi pamoja nao kwa taaswibi aliye katika ngazi yao.

vi) Binti wawili na zaidi wa mtoto mwanamume, ndugu wa kiume wa mama mmoja hapati nao mirathi, na wala binti au mabinti wa mtoto wa mtoto mwanamume isipokuwa kawe pamoja nae kuna atakayerithi nae kwa taaswibi, kama vile kaka au mtoto wa ami anayelingana nae katika daraja.

vii) Kaka wa baba mmoja mama mmoja, anamzuia kaka wa baba mmoja, na ami awe wa baba mmoja mama mmoja au baba mmoja.

viii) Mtoto wa kaka wa baba mmoja mama mmoja, anamzuia ami, mtoto wa kaka wa baba mmoja na aliye chini yake miongoni mwa watoto wa kaka.

ix) Kaka wa baba mmoja, anamzuia ami, pia mtoto wa kaka baba mmoja mama mmoja au baba wa mmoja.

x) Mtoto wa kaka wa baba mmoja anamzuia ami, na aliye chini yake miongoni mwa watoto wa watoto wa kaka.

xi) Ami wa baba mmoja mama mmoja, anamzuia ami wa baba mmoja, na walio chini yake miongoni mwa watoto wa Ami.

xii) Mtoto wa Ami wa baba mmoja, mama mmoja, anamzuia mtoto wa Ami baba mmoja, na walio chini yake miongoni mwa watoto wa mtoto wa Ami.

xiii) Ami wa baba mmoja anamzuia mtoto wa ami awe baba mmoja mama mmoja au baba mmoja.

xiv) Dada wa baba mmoja mama mmoja anapokuwa na binti anamzuia kaka wa baba mmoja, kwa sababu dada wa baba mmoja mama mmoja anakuwa sawa na kaka baba mmoja mama moja, na kaka wa baba mmoja mama mmoja, na kaka wa baba mmoja mama mmoja anamzuia kaka wa baba mmoja.

xv) Dada wa baba mmoja mama mmoja anapokuwa pamoja na binti wa mtoto mwanamume anamzuia kaka wa baba mmoja.

xvi) Dada wawili na zaidi wa baba mmoja mama mmoja, wanamzuia dada wa baba mmoja, isipokuwa kama atakuwa na kaka yake atayerithi pamoja nae kwa taaswibi, kwa hiyo dada wa baba mmoja hapa sawa na binti wa mtoto mwanamume anapokuwa na binti wawili, kwani nae anakosa mirathi kama hakuwa na kaka yake au mtoto wa ami yake aliye katika ngazi yake atakayerithi kwa taaswibi.

xvii) Baba, anamzuia babu, bibi mzaa baba, na ami na ndugu pia.

xviii) Babu, anamzuia baba yake, ndugu wa mama mmoja ami na watoto wa ndugu pia.

xix) Mama, anamzuia bibi mzaa mama na mzaa baba.



Mada ya Saba

‘Hali za Babu’

1) **Babu na watoto wa mtoto mwanamume**, na Ami, na watoto wa ami, pia watoto wa ndugu, ingawa haikuja aya iliyo wazi katika kuwarithisha katika Qur-aan lakini neno la Mtume ﷺ katika kurithi kwao:

“Wapeni mafungu wenye mafungu.”

Linathibitisha kurithi kwao. Kama linavyowaunganisha watoto wa mtoto mwanamume, na binti yake neno *Waladun*—katika kauli ya Allah:

“*Anawaamuru Allah kuhusu watoto wenu.*”

Kwa sababu hiyo maimamu wote wamekubaliana kupata mirathi waliotajwa isipokuwa babu alipoingia katika kauli Yake Allah:

وَلِأَبْوَيْهِ لِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا أَلْسُدُسُ

“*Na wazazi wake wawili kila mmoja anapata sudusi.*” (4:11)

Kwa hiyo babu akawa kama baba katika kupata sudusi anapokuwepo mtoto au mtoto wa mtoto mwanamume na anachukua mali zote kama anakuwa peke yake, na anachukua kilichobakishwa na mafungu kama kipo, babu hatofautiani na baba isipokuwa katika maswala ya ndugu, baba anawaangusha wote wakati babu anarithi nao, kwa vile analingana nao katika ukaribu na marehemu. Kwa sababu ndugu wamefika kwa marehemu kwa kupitia kwa baba yao, na babu amefika kwa marehemu kwa kupitia kwa baba ambaye ni mtoto wake huyo babu.

Kutokana na maelezo haya Babu ana hali tano, nazo ni:

a) Kuwa hakuna kabisa pamoja naye anayerithi na hapa babu anakusanya mali zote kwa *Taaswibi*.

- b) Pamoja na babu kuwapo na wenye mafungu tu, babu apate sudusi pamoja na hao wenye mafungu na kama kitasalia kitu atakichukua babu kwa *Taaswibi*.
- c) Kama pamoja na babu kuna mtoto na mtoto wa mtoto hapa babu atapata sudusi tu.
- d) Kama pamoja na babu kuna ndugu tu, basi babu atapewa fungu kubwa kati ya hali mbili thuluthi ya mali yote au kugawana nao. Na kugawana nao kutampa fungu kubwa kuliko thuluthi. Kama idadi yao haikuzidi wawili au wanaolingana nao kama vile dada wanne.
- e) Kama pamoja na babu kuna ndugu na wenye mafungu basi hapa atapewa kilicho bora (kati ya matatu) sudusi ya mali yote au thuduthi ya kilichosalia baada ya kutoa mafungu au kugawana sawa na ndugu na endapo mafungu yatamaliza hisa zoe katika mali basi ndugu wataanguka, ama babu haanguki bali atapatiwa sudusi, hata kama italazimika kuingilia katika mas-ala kwa ajili yake.

Tanbihi:

Kwanza: Inahusu kumbana Babu:

Wanapojumuika babu na ndugu wa baba mmoja mama mmoja na wa baba mmoja, ndugu wa baba mmoja mama mmoja wanamuhesabu babu kuwa ndugu wa baba mmoja miongoni mwao, na watagawana nae kwa idadi iliyojumlishwa na ndugu wa baba mmoja, wakishagawana na babu ndugu wa baba mmoja mama mmoja wanakuja kuwazuia wale ndugu wa baba mmoja na kuchukua fungu lao bila ya babu (kwa sababu ndugu wa baba mmoja anazuiliwa na ndugu wa baba mmoja mama mmoja).

Mfano wake: amefariki akaacha babu na ndugu wa baba mmoja mama mmoja, ndugu wa baba mmoja, kigawio cha ushirika ni tatu kulingana na idadi, babu anapata moja, na kaka wa baba mmoja mama mmoja anapata moja na kaka wa baba mmoja anapata moja, isipokuwa kaka wa baba mmoja mama mmoja baada ya kumuhesabia babu, ndugu wa baba mmoja anakuja na kuchukua hili fungu la kaka kwa baba mmoja, kwa sababu kaka kwa baba mmoja anazuiliwa na kaka kwa baba mmoja mama mmoja kama tulivyosema hapo nyuma.

Ya pili: Inahusu ‘Akdariyyah’

Anapofariki mwanamke akaacha mume, mama yake na dada yake kwa baba mmoja na mama mmoja au baba mmoja na babu yake, kigawo hapa ni sita (kwa vile katika mas-ala kuna sudusi) nusu ya mume nayo ni tatu, na thuluthi ya mama nayo ni mbili, na nusu ni ya dada, nayo ni tatu na sudusi ya babu nayo ni moja. Na mas-ala itazidi na idadi ya hisa kuwa tisa, kisha babu anawataka dada agawane nao, kwa hiyo, atakusanya moja yake pamoja na mafungu yao matatu jumla inakuwa ni nne watagawana fungu la mwanamume mmoja sawa na wanawake wawili, maudhui haya nimeyatenga peke yake kwa sababu ilivyo dada wanalazimika kutopewa fungu pamoja na babu kwa sababu yeye pamoja na wao ni Aswaba kama alivyo kaka yao, lakini hapa anapewa nusu kisha babu anarudi na kuchanganya hisa yake na ya dada na wanagawanya fungu la mwanamume sawa na wanawake wawili, kwa hiyo dada anajikuta amepata sudusi na babu thuluthi takriban kinyume na kile alichopewa hapa. Maudhui haya yameitwa *Akdariyyah* kwa sababu imemvurugia dada kwani alipata kingi (nusu) akajikuta anapokea kidogo (Sudusi) ni (kuliko kilichotajwa).



Mada ya Nane

Kusahihisha Mafungu

1) Vigawio vya Mafungu, Navyo ni:

Saba, Mbili, Tatu, Nne, Sita, Nane, Kumi na Mbili na Ishirini Na nne:

Nusu kigawio chake ni mbili, na thuluthi kigawio chake ni tatu. Robo kigawio chake ni nne, sudusi kigawio chake ni sita, thumni kigawio chake ni nane, na zinapokutana robo na sudusi basi kigawio chake ni kumi na mbili na zinapokutana thumuni na sudusi au na thuluthi basi kigawio chake kinakuwa ishirini na nne.

Mfano:

a) Mume na ndugu kiwagio ni mbili. Mume nusu, na ndugu nusu.

b) Mama na baba, kigawio ni tatu. Mama thuluthi moja na kilichosalia ni cha baba taaswibi.

c) Mke na ndugu, kigawio ni nne. Mke robo, moja na kilichosalia ni cha ndugu kwa taaswib.

d) Mama, baba na mtoto mwanamume kigawio ni sita, mama sudusi moja, baba sudusi moja, na kilichosalia anachukua mtoto kwa taaswib.

(e) Mke na mtoto mwanamume, kigawio ni nane, Mke thumni, moja na kilichosalia anachukua mtoto kwa taaswib.

f) Mke, mama na ami, kigawio ni 12 kwa sababu zimekutana robo na thuluthi, robo yake ni ya mke tatu na thuluthi yake ni ya mama nne, na kilichosalia anachukua Ami kwa taaswibi.

g) Mke, mama na mtoto mwanamume, kigawio ni ishirini na nne, kwa vile zimekutana thumni na sudusi, mke thumni nayo ni tatu, mama sudusi nayo ni nne, na kilichosalia ni cha mtoto kwa taaswib.

2) 'Aul'.

a) Maana yake:

Aul Katika Istilahi: Ni nyongeza katika hisa, na upungufu katika kiwango.

b) Hukumu yake:

Wamekubaliana Masahaba رضي الله عنه isipokuwa Ibnu Abbas, kutumia na hivyo ndivyo inavyofanyika na Waislamu wote.

c) Mafungu yanayoingia 'Aul:

'Aul inaingia katika vigawio vitatu tu:- Navyo ni: sita, kumi na mbili na ishirini na nne. Sita inazidi na kufikia kumi na saba kwa witra na mume, na kumi na mbili inazidi kumi na saba kwa witra tu. Na ishirini na nne inazidi mara moja tu na kufikia ishirini na saba kwa witra.

Mfano:

1. Mfano wa kuzidi sita kuwa saba: Mume, dada kwa baba mmoja mama na mama mmoja na bibi. Kigawio ni sita, mume nusu nayo ni tatu na dada nusu tatu na bibi sudusi moja, kwa hivyo imezidi kufikia saba witra.

2. Kuzidi sita na kufikia nane: Mume ana dada wawili wa baba mmoja mama mmoja na mama, kigawio ni sita, mume nusu tatu dada wawili baba mmoja mama mmoja theluthi mbili nne na mama sudusi moja, imezidi na kufikia nane kwa Shufa.

3. Kuzidi kumi na mbili kufikia kumi na tatu. Mke, mama na dada wawili na baba mmoja kigawio ni kumi na mbili kwa vile sudusi imekutana na robo, mke robo tatu, mama sudusi mbili, na dada wawili thuluthi mbili nane. Imezidi kufikia kumi na tatu.

4. Kuzidi, ishirini na nne kufikia ishirini na saba, mfano: Mke, babu, mama na bibi wawili thuluthi mbili kumi na sita, kwa hivyo imezidi kufikia ishirini na nne kwa kiwepo thumni na sudusi. Thumni tatu kwa mke, na sudusi nne kwa baba, na

sudusi nne vile vile kwa mama, na theluthi kumi na sita kwa mabinti wawili, ikazidi ishirini na saba.

2) Kutafuta Kigawio:

Hali za warithi:

Warithi ima watakuwa wanaume tu aswaba, au mchanganyiko wanaume na wanawake. Na ima watakuwa aswaba pamoja nao wenye mafungu au wenye mafungu tu. Basi kutokana na tofauti hizo kama watakuwa aswaba tu, kigawio kitawekwa kulingana na idadi yao kwa mfano: watoto watatu, basi kigawio chao ni tatu, ambayo ndio idadi yao, kila mmoja anapata hisa moja na wakiwa aswaba wanaume na wanawake vile vile, isipokuwa fungu la mwanamume na binti wawili kigawio kitakuwa nne ndio idadi yao, mtoto mwanamume mbili na kila binti moja.

Na kama pamoja nao kuna mwenye fungu, basi, kigawio chao ni namba iliyo chini ya mstari (unaogawa sehemu katika fungu hilo) kwa mfano: Mume, mtoto mwaamume na mwanamke Basi kigawio ni nne ambayo ndiyo iliyo chini ya mstari $\frac{1}{4}$ moja ya mume na mtoto mwanamume mbili, na moja binti, fungu la mwanamume sawa na wanawake wawili.

	4
Mume	1
Mtoto mwanaume	2
Binti	1

4) Mifanano Minne:

Na kama katika mas-ala yumo mwenye fungu, mmoja na zaidi basi italazimika kuangalia namba zilizo chini kwa mifanano miwili au minne ambayo ni tamathuli, tadakhul, tawafuq na takhalufu, ili kupata kigawio na kuepukana na visehemu.

Minhajil Muslim

Katika Tamathuli

Ni kama vile nusu mbili, au sudusi mbili basi hapo itachukuliwa moja ya namba mbili hizo nakufanywa ndicho kigawio cha mas-ala hayo, na mgao utafanywa.

Mfano:

Mume, dada wa baba mmoja mmoja, mume anapata nusu, dada nusu kwa hiyo itatumika moja tu kati ya namba hizo mbili za chini, kwa sababu zinafanana. Na hiyo inayochukuliwa ndio itakayokuwa kigawio kama unavyoona kwenye jedwali:-

	2
Mume	1
Dada	1

Katika Tadakhuli

Ni mfano wa sita na tatu katika hali hii itatumika kubwa kati ya namba mbili. Kwa sababu ile ndogo inaingia ndani ya namba kubwa. Kwa hiyo namba kubwa ndiyo kigawio. Mfano: Mama, ndugu wawili wa mama mmoja na ami na kugawa kutakuwa kama hivi:

	6
Mtoto mwanamme	1
Ndugu	2
Binti	3

Kwa hiyo, kigawio hapa ni sita. Mama sudusi moja, ndugu wawili thuluthi mbili, na ya mama mbili na iliyobaki tatu ni aswaba anachukua kilichosailia. Utaona hapa imechukuliwa sita na kuwa kigawio kwa vile tatu inaingia katika sita.

Katika *Tawafuq*:

Inaangaliwa namba ndogo zaidi kati ya namba mbili zinakubali kugawa kwa namba hiyo, namba utakayoigawa kwa hiyo jibu lake utalizidisha mara ile namba nyingine jibu ndilo litakuwa kigawio. Mfano: Mume, mama, watoto wanaume watatu na binti. Mume robo, na namba yake ya chini nne, mama ni sudusi na namba yake ya chini ni sita.

	12
Mama	3
Ndugu za Mama	2
Ami	2
Mume	2
Mama	2
Mtoto wa Kiume	1

Na uhusiano ulio katika namba mbili hizi (robo na sudusi) zinaafikiana kukubaliana kugawa kwa nusu kwa vile kila moja ya namba mbili hizi ukigawa jibu lake linakuwa nusu ya namba iliyogawanywa. Kwa hiyo nusu moja ya hizi namba mbili itazidishwa katika ile isiyogawanywa jibu lake ni kumi na mbili ndio kigawio cha mas-ala yenyewe.

Katika Takhalufu:

Kutoafikiana namba katika mnasaba wowote ule, kama namba nne na tatu, hapa namba moja inazidishwa mara namba ya pili jibu lake litakuwa ndicho kigawio, mfano: Mume, mama na kaka wa baba mmoja mama mmoja, mume anapata nusu ya namba yake ya chini mbili, na mama thuluthi, namba yake ya chini ni tatu. Na uhusiano kati ya namba mbili ni kutofautiana ikizidishwa mbili mara tatu jibu lake ni sita, kwa hiyo sita ikafanywa kigawio na mgao ukafanywa.

	6
Mume	3
Mama	2
Kaka	1

5) Namba Kutokubali Kugawika (Al-Inkisaar)

Kutokubali kugawika namba ni kuwa hisa fulani haikubali kugawika kwa warithi wake, kwa hiyo uangaliwe uhusiano kati ya hisa na idadi ya warithi wa hisa hiyo, kama zitaafikiana basi utachukuliwa huo muafaka wa idadi ya warithi na itawekwa juu ya kigawio cha fungu na kuzidishwa muwafaka mara kigawio jibu itakuwa ndicho kigawio na kigawio chini ya jumla iliyosahihishwa kama ina vyoonekana katika jedwali katika mfano wa mume na watoto wawili wanaume na binti wawili.

	2	
	4	8
Mume	1	2
Mtoto	3	2
Mtoto		2
Binti		1
Binti		1

Na kama zitatofautiana idadi ya warithi (ambao idadi yao ni tofauti na hisa yao) itawekwa juu ya fungu na itazidishwa mara fungu jibu hilo ndilo kigawio, itawekwa katika jumla nyingine na kuzidishwa hisa ya kila mmoja mara namba iliyo juu ya fungu na jibu litawekwa mbele yake chini ya jumla kuu sahihi.

Mfano: mke, mtoto, binti, kigawio ni nane, mke thumni moja, inabaki saba wanakuwa na saba nayo haigawiki juu yao kwa sababu idadi yao ni watatu kwa sababu fungu la mwanamume mmoja ni sawa na wanawake wawili. Itaangaliwa hisa na idadi ya wanahisa, na uhusiano wao, na kupatikana kutofuatiana kwa hiyo idadi ya warithi itawekwa juu ya fungu nayo ni tatu itazidishwa mara fungu jibu ishirini na nne na hiyo inakuwa kigawio na kazi itaenda kama ilivyotangulia.

	3	
	8	24
Mke	1	3
Mtoto	7	14
Binti	7	

Minhajil Muslim

Tulichokieleza hapo juu ikiwa kitakataa kugawika kwa kundi moja la warithi, kama itakataa kugawika kwa zaidi ya kundi moja, kitakachofanywa ni kuangalia uhusiano kati ya kila kundi na hisa yake ambayo imekataa kugawika kwa sura mbili *takhaluf*, na kitachopatikana kwa mtazamo huo kitawekwa nyuma ya kundi hilo, kisha namba hizo zilizowekwa nyuma ya kila kundi zitaangaliwa tena kwa sura nne, kama itakuwa *tamathul* itachukuliwa moja na ikiwa *tadakhul* itachukuliwa namba kubwa, kwa sababu ndogo imeingia chini ya kubwa, na ikiwa *tawafuq*, itachukuliwa namba ya muafaka na kuzidishwa na namba ya pili na kuchukuliwa jibu lake na kama uhusiano ni kutofautiana basi itazidishwa namba moja mara namba nyingine na jibu lake ndio litakalochukuliwa na hicho kilichopatikana kitawekwa juu ya fungu, kisha kitazidishwa mara kigawio jibu litakuwa ndio jumla, na kazi itaenda kama ilivyotangulia.

Mfano wa kutogawika makundi mawili, wake wawili na kaka wawili wa baba mmoja mama mmoja, kigawio hapa ni nne, kwa wake wawili ni moja haikubali kugawika juu yao na kilichobakia ni tatu kwa ndugu wawili wanaume kwa taasib pia nayo haikubali kugawika kwa mbili, inaangaliwa hisa ya wake na idadi yao, na hapo uhusiano ni tofauti, kwa hiyo namba yao itawekwa nyuma yao pia kisha utaangaliwa uhusiano kati ya idadi ya wake na kaka wawili, hapa ni mfanano (*tamathul*) kwa hiyo itachukuliwa namba moja tu. Itawekwa juu ya fungu itazidishwa mara fungu na jibu litawekwa kuwa jumla kubwa na itaendelea kama tulivyoeleza hapo nyuma na huu hapa ni mfano wake. Na huu ni mfano wa kufanana idadi ya wahusika:

	2	
	4	8
Mke	1	1
Mke	1	
Kaka	3	3
Kaka	3	

Na mfano wa namba zilizoingiliana na zikazotofautiana, wake wanne, na binti watatu na dada wawili wa baba mmoja mama mmoja itakuwa kama unavyoona hapa chini

	12	
	24	288
Mke	3	9
Mke		9
Mke		9
Mke		9
Binti	16	64
Binti		64
Binti		64
Dada	5	30
Dada		30

Cha kuangalia ni kwamba namba zilizokataa kugawika ni za makundi matatu, kwamba kila kundi linatofuatiana na hisa yake, hivyo basi namba ya idadi yao ikawekwa nyuma ya kila kundi husika, kisha ikaangaliwa idadi ya kila kundi ikaonekana mbili na nne zinaingiliana ikachukuliwa namba kubwa nayo ni nne kisha ikaangaliwa nne na tatu ikabainika kuwa zinatofuatiana ikazidishwa moja-nne mara nyingine tatu au kinyume chake, jibu ni kumi na mbili ikawekwa juu ya fungu- kigawio-na ikazidishwa kumi na mbili mara kigawio ishirini na nne sawa sawa na mia mbili na themanini na nane (288) ikawa ndio jumla kuu na itafanywa kama tulivyosema hapo nyuma.

Mada ya Tisa

Kugawa Mali Zilizoachwa na Marehemu

Kugawa mali zilizoachwa na marehemu, ndio matunda yanayotarajiwa kwa kusoma na kujifunza somo hili la mirathi, na matokeo yaliyokusudiwa ya somo hili.

Na kugawa mali zilizoachwa na marehemu kuna njia nyingi, lakini tutachukuwa mbili tu:

Ya kwanza ikiwa mali zilizopo ni vitu (si fedha taslimu), na **ya pili** ni fedha taslimu, njia ya kwanza inajulikana kwa jina la “*Takrit*” yaani mali zote zinagawanywa katika mafungu ishirini na nne, kila fungu linaitwa *Kirati*. Na namna ya kuitumia njia hii unatakiwa uweke ishirini na nne katika jumla kubwa baada ya jumla iliyosahihishwa kisha unaangalia uhusiano uliopo kati ya *Kirati* na kigawio kama zinafanana mambo yanakuwa mepesi, kwani unachotakiwa kufanya ni kuchukua hisa ya kila mmoja na kuiweka mbele yake au chini ya namba kuu ya *kirati*, na hilo ndilo fungu la hisa ya mhusika katika *kirati*.

Mfano, mtoto mwanamume, mke na mama, Kama hivi:

	24	24
Mke	3	3
Mama	4	4
Mtoto	17	17

Na kama hazikufanana na zikawa zinaafikiana katika uhusiano fulani, basi utachukuwa muafaka wa *kirati* utaweka juu ya jumla ya kigawio na utachukua muafaka wa kigawio utaweka katika *kirati* nyuma ya jumla ya *kirati*, kisha zidisha muafaka wa *kareti* mara hisa ya kila mmoja iliyowekwa juu ya kigawio, jibu iliyo nyuma ya jumla ya *kareti*, na jibu utakalolipata kama itakuwa namba kamili sehemu

ile kamili itawekwa chini ya jumla ya kareti na ile sehemu itawekwa chini ya jumla ya mwisho ambayo ni muwafaka wa kigawio, na hapo ile sehemu inakuwa ni sehemu ya kilicho juu yake. Na unapotaka kusahihisha kazi ili ujuwe ni sahihi au umekosea kwanza jumlisha namba kamili kisha jumlisha sehemu,

Namba kamili itapatikanautajumlisha na zile namba kamili kama jibu litakuwa ishirini na nne kulingana na idai ya kareti basi kazi ni sahihi, kama jibu halitakuwa hlo basi si sahihi.

Mfano wake: mume, mama, mtoto mwanamume na binti:

	3	2		
	12	36	24	3
Mume	3	9	6	0
Mama	2	6	4	
Mtoto	7	14	9	1
Binti		07	4	2

Hapa utaona: Kigawio ni kumi na mbili, kisha kitasahihishwa na kuwa thelathini na sita kutokana na kukataa kugawika hisa ya mtoto na binti. Na hapa kazi imefanyika kulingana na kanuni tulizozieleza.

Mfano mwingine: Ameacha mke, mama na kaka wa baba mmoja mama mmoja: inakuwa kama hivi:

	2		
	12	24	1
Mke	03	06	0
Mama	04	08	0
Kaka	05	10	0

Kinachoonekana hapa ni kwamba muafaka umepatikana kwa nusu ya sudusi kwahiyo ikawekwa nusu ya sudusi ya kirati nayo ni mbili ikawekwa juu ya kigawio na ikawekwa muafaka kigawio nayo ni moja, nusu ya sudusi ya kumi na mbili na kazi ikaendelea kama tulivyoeleza nyuma, isipokuwa namba ukigawa kwa moja inatoka namba hiyo hiyo bila ya kuzidisha au kupunguza na hii haidhuru, litawekwa jibu mbele yake kama ilivyotangulia.

Na ikiwa zimetofautiana basi utachukua kirati yote 24 utaiweka juu ya kigawio na uchukue kigawio utakiweka katika jumla kubwa nyuma ya jumla ya kirati, kisha unazidisha hisa ya kila mmoja mara namba iliyokuwa juu ya kigawio 24, na jibu utaligawa kwa kigawio kilichowekwa katika jumla ya mwisho nje ya mgao, kama itakuwa ni namba kamili tu basi utaiweka mbele ya mhusika wake chini ya jumla ya kirati na ikiwa na sehemu ile namba kamili utaweka chini ya jumla ya mwisho na itakuwa ni sehemu ya namba hiyo. Kama utazijumlisha hizo sehemu utapata kitu kamili utajumlisha na ile namba kamili na itakamilika namba ya kirati ishirini na nne.

Mfano wake, (amekufa na kuacha) Mke, mama na dada wawili na baba mmoja itakuwa kama hivi:

		24		
	12	13	24	13
Mke	3	3	5	7
Mama	2	2	3	9
Dada	4	4	7	5
Dada	4	4	7	5

Kinachoonekana hapa:

1. Kati ya kigawio na karati kuna tofauti kwa sababu 13 na 24 ni tofauti na hazikubaliani kwa uhusiano wowote, kwa sababu hiyo tumeiweka kareti yote juu ya kigawio. Na tukaweka kigawio chote katika jumla nyuma jumla ya kirati.

2. Sehemu ambazo ziko chini ya jumla ya mwisho baada ya kuijumlisha imetengeneza namba kamili ya kareti. Nayo ni mbili na hio mbili tukaziweka chini ya jumla kuu ya kirati, na namba ya kirati imekamilika 24 na tumeelewa kuwa kazi iliyofanywa ni sahihi.

Njia ya pili kama mali ya marehemu ni fedha taslimu: Dirham au Dinari, kazi ya hapa haitofautiani na ile ya kwanza ya kareti, isipokuwa hapa unaweka idadi kamili ya Dirham au Dinari yote katika jumla kubwa nafasi ambayo kwa njia ya kwanza ulikuwa unaweka kirati, kisha utafanya kama tulivyokwishaeleza hapa mwanzo.

Mfano: Mume na mtoto mwanamume na marehemu ameacha mali kiasi cha Riali arubaini, utafanya kama tulivyoeleza:

	10		
	4	40	1
Mume	1	10	0
Mtoto	30	3	0

Utaona tumeangalia uhusiano kati ya kigawio na idadi ya mali tunakuta uhusiano wao ni muafaka kwa robo, tukachukua muafaka wa mali tukauweka katika jumla kubwa ya mwisho ili igawanywe kwa hiyo na tukachukua muafaka na mali nao ni 10 ili tuzidisha mara kigawio, hivyo tukauweka juu ya kigawio kisha tukaizidisha mara hisa ya mume nayo ni moja tukaizidisha mara namba iliyo juu ya kigawio 10 jibu tukaigawa kwa muafaka wa kigawio nayo ni moja mara kumi ni kumi tukaiweka mbele ya mwenye hisa yake, na hivi hivi ndivyo tulivyofanya kwa mtoto, kwa hiyo mume akapata kumi kutoka kwenye arubaini (40) na hiyo ndio robo, na thalathini (30) akapata mtoto na hiyo ni robo tatu ya arobaini.

Mfano mwingine: mume, mama, na kaka na baba mmoja mama mmoja na mali ni Dirham sitini.

	10		
	6	60	1
Mume	3	30	0
Mama	2	20	0
Kaka	1	10	0

Inaonekana kuwa muafaka ulikuwa kwa sudusi.

Mfano mwingine: ambao kigawio kimetofautiana na mali kwa idadi, mke, mama na baba na mali ni Dirham 235 kama hivi:

	235		
	12	235	12
Mke	3	58	9
Mama	4	78	4
Baba	5	97	11

Hapa haukupatikana uhusiano wowote kati ya kigawio na mali, kama inavyoonekana ni kwamba hakuna tofauti ya utendaji kati ya njia hii na ya kirati isipokuwa kule kuweka idadi ya mali badala ya kirati, ama utendaji hauna tofauti kabisa, mke kachukua robo yake nayo ni tatu, iliyozidishwa mara mali 235 ikigawanywa kwa kigawio 12 jibu Dirham 58 ikawekwa mbele yake chini ya namba kubwa ya mali, na ikabaki iliokataa kugawika nayo ni 9 ikawekwa chini ya jumla kubwa ya kigawio, na uhusiano wake utakuwa kama hivi $\frac{9}{12}$ nayo sawa na robo tatu ya namba kamili na hisa ya mama ikazidishwa mara namba iliyo juu ya kigawio na jibu likagawanywa kwa 12 jibu likawa 58 na sehemu nayo ni 9 ya kumi na mbili, na baba hisa yake ikazidishwa na ikagawanywa jibu likawa 97 na sehemu, nayo ni 11 ya kumi na mbili zikajumlishwa sehemu zikawa 24 yaani namba mbili kamili, ikawekwa chini ya namba chini ya jedwali ikajumlishwa pamoja nayo ikawa jumla ya namba chini ya jedwali, ikajumlishwa pamoja nayo ikawa jumla ya muafaka inalingana na mali, kwa hiyo tukaelewa kuwa kazi iliyofanywa ni sahihi, na hicho ndicho kinachotakiwa.



Mada ya Kumi

‘Munasakha’

Kinachokusudiwa katika *‘Munasakha’*, ni tendo litakalofikisha warithi wa marehemu kuelewa kutoka kwa warithi wa marehemu wa kwanza kabla ya kugawa mali na njia ya kufikia hayo ni kusahihishwa kigawio cha marehemu wa kwanza, na utaiweka (T) (Tuwufiya- Yaani amekufa) hii ni alama ya kujulisha kuwa aliyewekewa mbele yake herufi hiyo amefariki kisha wanaorithi miongoni mwa warithi wa marehemu wa kwanza utawaweka kwa anuani zao mpya za kurithi, kwa hiyo yule aliyekuwa mke wa marehemu wa kwanza kwenda kwa marehemu wa pili, kama mama kwa mfano, utawaweka mbele ya hisa zao kwa marehemu wa kwanza na kama atatokea mrithi mpya na zaidi utamuweka katika jedwali chini ya jedwali la kwanza, kisha kitapatikana kigawio cha mas-ala yao. Na utaangalia uhusiano kati ya kigawio na hisa ya marehemu, kama hisa zitakubali kugawika kwa kigawio cha mas-ala ya pili, basi mas-ala hayo mawili kigawio chake ni kile cha mas-ala ya kwanza.

Mfano wake: amefariki akaacha mume, mama, mtoto na binti, na mume akafariki akaacha mtoto na binti, wale waliotajwa kwa marehemu wa kwanza, basi mas-ala ya kwanza kigawio chake ni 12 kusahihishwa kuwa 36, kwa sababu ya kutokubali kugawika hisa ya mtoto na binti, na mas-ala ya pili kigawio chake ni tatu, na hisa ya marehemu ni tisa inakubali kugawika kwa kigawio cha mas-ala ya pili nacho ni tatu. Kwa hiyo kigawio cha mas-ala mbii ni 36. Na kigawio hicho kitakuwa ndio jumla kuu ya Munasakha, na namba ambayo ingegawanywa kwa kigawio cha mas-ala ya kwanza zitahamishiwa kwenye kigawio cha mwisho ambacho (36), na zitahamishiwa hapo hisa na kuwekwa chini yake, kwa hiyo yule ambaye alikuwa hana hisa katika mas-ala ya pili hisa yake katika mas-ala ya kwanza itawekwa kama ilivyo chini ya jumla kuu ya Munasakha, mbele ya wenye hisa na yule mwenye hisa katika mas-ala ya pili utaizidisha mara namba iliyo juu ya kigawio na jibu lake litajumlishwa pamoja na hisa yake kwa marehemu wa kwanza kama anayo na utaiweka mbele yake chini ya jumla ya munasakha. Kama hivi:

	3	3			
	12	36	3		36
Mke	3	9	T		
Mama	2	6			6
Mtoto	7	14	Mtoto	2	20
Binti		07	Binti	1	10

Ikiwa hisa ya marehemu wa pili haikubali kugawika kwa kigawio cha mas-ala yake ya pili basi utaangalia uhusiano kati ya namba mbili hizo kwa sura mbili muafaka na kukosana, kama zitaafikiana basi chukua muafaka wa hisa na weka juu ya jumla iliyokuwa kigawio, na chukua muafaka wa kigawio weka juu ya kigawio cha mas-ala ya kwanza na utazidisha mara kigawio cha mas-ala ya kwanza, jibu litakuwa ndio jumla kuu ya munasakha, kama anayo hisa katika mas-ala ya pili utazidisha mara namba iliyo juu ya kigawio cha pili (mas-ala ya pili) na jibu utakalopata lijumlishe pamoja na hisa yake katika mas-ala ya kwanza, na uziweke mbele yake chini ya jumla kubwa ya munasakha, na hilo ndio fungu lake kama hivi:

Mfano: mke, binti na dada wa baba mmoja mama mmoja, kisha akafa binti akamuacha: mama ambaye ndiye mke katika mas-ala ya kwanza na mume na mtoto mwanamume. Kigawio hapa ni nane na mas-ala ya pili kigawio ni 12 na kati ya hisa ya marehemu wa pili nayo ni nne, na kigawio cha mas-ala ya pili nayo ni 12 ni muafaka na robo, kwa hiyo muafaka wa hisa (1) utawekwa juu ya kigawio cha pili, na muafaka wa kigawio cha mas-ala ya pili (3) utawekwa juu ya kigawio cha mas-ala ya kwanza, na yataendelea yote tuliyoyaeleza nyuma na huu ni mfano wake:

Minhajil Muslim

	3		1	
	8		12	24
Mke	1	Mama	2	05
Binti	4	T		0
Dada	3			09
		Mume	3	03
		Mtoto	7	07

Hisa kama zitatofautiana pamoja na kigawio cha mas-ala ya pili, chukua hisa yote iweke juu ya kigawio cha mas-ala ya pili, na chukua kigawio cha mas-ala ya pili utakiweka juu ya kigawio cha kwanza na utazidisha mara kigawio cha kwanza, na jibu lake utaliweka katika jumla kuu ya kigawio cha pili na itaendelea kama ilivyotangulia.

Mfano wake: Mke, watoto wanaume watatu na binti, kisha mke akafariki na kuacha wale watoto watatu na binti.

	7		1	
	8		7	56
Mke	1	T		
Mtoto	2	Mtoto	2	16
Mtoto	2	Mtoto	2	16
Mtoto	2	Mtoto	2	16
Binti	1	Binti	1	08

Hapa utaona:

1. Marehemu hakuacha mrithi mpya akawekwa katika jedwali chini ya mas-ala ya kwanza.
2. Kazi imelingana na ile ya kwanza.



Mada ya Kumi na Moja

‘Khuntha Mushkel’

Kilichokusudiwa kwa Khuntha Mushkel ni mtu ambaye anazaliwa na hali ya jinsia yake; ni mwanamume au mwanamke, kwa hivyo, atasubiriwa mpaka anapofikia baleghe ili hali yake ieleweke. Inapotakiwa kugawanywa basi njia inayotumiwa na baadhi ya wanazuoni ni kwamba atapewa mtu wa namna hii nusu ya fungu la mwanamume na nusu ya fungu la mwanamke.

Njia ya kufanya ni kumuwekea kwanza kigawio akiwa kama mwanamume halafu kigawio kama mwanamke, hii ni kama Khuntha ni mmoja, lakini kama watakuwa wawili basi vigawio itakue vine na baada ya kupata vigawio tunaangalia kati ya vigawio katika hali nne, ili vyote viwe kigawio kimoja tu, kisha matokeo ya kuangalia utayazidisha mara hali ya Khuntha (hali ya kumkadiria mwanamume na mwanamke) jibu litalopatikana litakuwa ndicho kigawio, baada ya kigawio cha kwanza, kisha jibu utaligawa kwa vigawio vyote (akiwa mwanamume na akiwa mwanamke) na jibu utakalopata utaliweka juu ya kigawio hicho, kisha utazidisha hisa ya kila mrithi mara namba (uliyoweka) juu yake.

Yaani kigawio cha kila kadirio mwanamume na mwanamke juu ya kigawio chake jibu utakalopata utalijumlisha na matokeo ya kuzidisha na jibu utaligawa kwa namba ya hali ya Khuntha) na jibu utakalopata liweke mbele ya mhusika chini ya jumla kuu, kisha jumlisha hisa ya kila mmoja, kama jawabu la kujumlisha litakuwa sawa na jumla kuu. Elewa hizo kazi ni sahihi laa sivyo basi hiyo kazi si sahihi.

Mfano: Marehemu ameacha mwanamume na Khuntha kama hivi:

	6	4	
	2	3	12
Mtoto	1	2	07
Khuntha	1	1	05

Kilichoonekana katika mas-ala:

- a) Tumeweka vigawio viwili, kwanza kwa kuzingatia ni mwanamume na cha pili kwa kuzingatia ni mwanamke.
- b) Tumeweka vigawio viwili tukavikuta vinatofautiana, tukazidisha mara hali ya Khuntha, nazo ni mbili, tukazifanya jumla kuu sahihi.
- c) Tukavigawa kwa jumla kuu nayo ni kumi na mbili kama vile vigawio viwili, kigawio cha kwanza jibu likawa sita, tukaliweka juu ya kigawio hicho na kigawio cha pili mne, tukakiweka juu yake pia.
- d) Tukazidisha hisa ya kila mmoja katika vigawio vile viwili mara namba iliyo juu ya kigawio chake, kwa hiyo Khuntha akapata kumi, kumi tukaigawa kwa namba ya hali za Khuntha, yaani mbili, jibu likawa tano tukaliweka mbele yake chini ya jumla sahihi 12 na hiyo ndiyo hisa yake na kwa yule mtoto kumi na nne, tukaigawa kwa hali za Khuntha 2 jibu likawa saba, tukaliweka mbele yake chini ya jumla sahihi, na hivyo ndivyo hisa yake inavyotafutwa.

Mfano mwingine: Marehemu ameacha watoto wanaume wawili na khuntha mmoja kama hivi:

	10	6	
	3	5	30
Mtoto	1	2	11
Mtoto	1	2	11
Khuntha	1	1	08

Minhajil Muslim

Cha kuangalia hapa ni kwamba kazi haitofautiani na ile iliyotangulia. Wanazuoni wengine wana njia nyingine nayo ni kila mmoja katika warithi atapewa namba ndogo kabisa ambayo angapata katika tofauti ya makadirio na kilichosalia kitawekwa mpaka hapo utata wa hali yake utakapotatuka au watakapokubali na uamuzi wa kugawa.

Njia ya kufanya ni kumkadiria Khuntha kuwa ni mwanamke ili apate namba ndogo zaidi katika miradhi kulingana na mabadiliko yake, atakadiriwa kuwa mwanamme ili apate namba ndogo zaidi kwa mwingine kwa vile yeye (Khuntha) ni mwanamume, na kilichosalia kitawekwa, kwa hiyo katika mas-ala ambayo marehemu ameacha mtoto mmoja mwanamme, kigawio ni mbili, kisha atakadiriwa mwanamke, na mara hii kigawio ni tatu halafu utaangaliwa uwiano kati ya vigawio viwili na hapo itabainika tofauti kati ya namba mbili hizi kwa hiyo zitazidishwa kigawio mara kigawio jibu ni sita, na sita itakuwa ndio jumla kuu sahihi, itajumlishwa hisa iliyopatikana katika kila kigawio na jumla yake itawekwa mbele ya kila mhusika chini ya jumla kuu sahihi. Fungu la mtoto mwanaume ni tatu na khuntha ni mbili inabaki moja, itawekwa mpaka hapo utata wa hali yake unapotatuka, kama itabainika kuwa ni mwanamume atapewa ile moja na kama mwanamke basi kile kilichowekwa atapewa yule mwanamume, na kama utata utaendelea basi watakubaliana litakalowaridisha wote juu ya kugawa.

Mfano wake:

	2	3	6
Mtoto	1	2	3
Khuntha	1	1	2

Cha kuangalia hapa ni kwamba kilichosalia hapa ni moja kwa dalili kuwa jumla kuu sahihi ni sita. Jumla ya namba zilizo chini ya jumla hiyo ni tano tu, na hii moja iliyosalia ndio itakayowekwa mpaka hapo hali inapobainika



Mada ya Kumi na Mbili

Kurithi kwa Mimba aliyepotea, Aliyezama na anayefana na hali zao

1-Mimba:

Suala la mimba, warithi wakitaka wanaweza kuacha kugawa, mpaka mimba izaliwe na hapo mgawo utapita, na wakitaka wataharakisha kugawa, isipokuwa kama wataamua kugawa kabla mimba haijazaliwa itawalazimu wafuate utaratibu ule wa Khuntha aina tuliyozungumzia hapa mwisho. Kwa maana wapewe urithi wao watakaowarithi kwa kuwepo mimba hiyo na kwa makadirio kuwa mwanamume au mwanamke kile kiwango cha chini mpaka hapo mimba itakapozaliwa ikiwa hai.

Mfano wake: Marehemu ameacha mke mjamzito, mke atarithi kama mtoto atazaliwa akiwa hai, thumni, na ikiwa hakuna mtoto atarithi robo, kwa hiyo thumni ndicho atakachopewa kwani hiyo ndio namba ya chini kwake, na kilichosalia kitawekwa mpaka izaliwe mimba ikiwa hai, kama mtoto atazaliwa hai mke hapewi kitu, na akizaliwa amekufa atapewa mke kile kilichowekwa kukamilisha robo kwani hakuna mtoto.

2-Aliyepotea:

Ama mtu aliyepotea kama atakufa mmoja wa ndugu zake, na waliopo wakataka igawanywe mali ya marehemu ndugu yao kabla hawajapata uhakika wa ndugu yao aliyepotea kuwa yuko hai au laa, au kabla hakimumu hajatoa hukumu ya kufa kwake, basi warithi hawa watafanyiwa kama ilivyofaywa katika mirathi ya mama mjamzito, watapewa kichache kinachojulikana kwa uhai wake na kufa kwake, na kilichosalia kitawekwa mpaka hapo uhakika wa hali yake utapopatikana, au hakimumu atakapo hukumu kufa kwake.

Mfano mwingine: Marehemu ameacha watoto wawili, mmoja hayupo, kwa aliyepotea hakumuathiri kitu, ama mama atapewa sudusi, kwa sababu hicho ndicho kima cha chini kwa mama hapa, ama yule ndugu atapewa nusu ya kilichosali baada ya hisa ya mke na mama kwani hicho ndicho kima cha chini kwake hapa,

Minhajil Muslim

na kilichosalia kitawekwa, kama itabainika kuwa yu hai basi atapewa kilichowekwa kwani ni fungu lake, na ikibainika amekufa basi mama atakamilishiwa thuluthi yake na kilichosalia atachukua ndugu. Kigawio kitakuwa kumi na mbili na itasahihishwa kwa ishirini na nne, na sura yake ni kama ifatavyo:

		1	2	
	12	24	12	24
Mke	3	6	3	6
Mama	2	4	4	4
Ndugu	7	7	5	7
Ndugu		7	0	0

Kinachoonekana hapa:

a) Tumeweka vigawio viwili, cha kwanza kwa kuzingatia aliyepotea kuwa yuko hai, na kigawio chake ni ishirini na nne kwa vile hisa ya ndugu haikubali kugawika. Na cha pili katika kuzingatia amekufa na kigawio chake ni kumi na mbili.

b) Tumeangalia asili mbili tukazona zinaafikiana kwa nusu ya sudusi, muafaka wa kigawio cha kwanza, tukaweka juu yakigawio cha pili nacho ni mbili na muafaka wa kigawio cha pili ni moja, tukaiweka juu ya kigawio cha kwanza na tukazidisha moja mara ishirini na nne jibu ni ishirini na nne na hilo jibu tukaliweka katika jumla kuu ya mwisho na ikawa ndio jumla sahihi.

c) Kwa kuzingatia kila anayeathirika kwa uhai wa aliyepotea tunampa namba ndogo, tukazidisha hisa ya mke nayo ni sita mara namba iliyo juu ya kigawio cha kwanza (nayo ni moja) jibu likawa sita tukaliweka jibu hilo mbele ya mke chini ya jumla kuu sahihi na tukazidisha hisa ya mama ambayo ni nne mara moja ambayo kwanza tulizidisha hisa ya mke jibu likawa nne kuwa hisa ya mama ni nne,

tukaiweka mbele yake chini ya jumla kuu sahihi na tukazidisha hisa ya ndugu aliyepo nayo ni saba mara moja jibu ni sababu tukaiweka mbele yake chini ya jumla kuu sahihi.

d) Jumla ya hisa chini ya jumla kuu ni kumina saba (17) kutoka katika ishirini na nne, kwa hiyo kilichosalia ni saba itawekwa mpaka itapotolewa hukumu kuhusu uhai wake au kifo chake aliyepotea, kama itahukumiwa kuwa yuko hai atachukua kilichowekwa kwani ni fungu lake, la, kama amekufa litakamilishwa fungu la mama thuluthi na itakuwa nane, na kilichosalia kitaongezwa kwa ndugu, kwa hiyo fungu lake litakuwa kumi na hiki ndicho kinachotakiwa.

3) Waliozama Majini:

Ama waliozama majini wakafa na waliokufa kwa sura inayofanana na hiyo kama vile waliofunikwa na kifusi na waliuongua moto, hukumu ya watu hawa kwa wanazuoni hakuna atakaye mrithi mwingine, bali kila mmoja atarithiwa na warithi wake nje ya hao walio kufa katika tukio hilo. Mfano wake: Ndugu wawili wamefariki katika tukio na haikueleweka nani aliyetangulia kufa kabla ya mwingine, na mmoja wao ameacha mke, binti, na ami na wa pili ameacha binti wawili na ami yule aliyetajwa mwanzo, kwa hiyo hukumu ya hawa kila mmoja atarithiwa na warithi wake tu. Hivyo, basi yule wa mwanzo atarithiwa na mkewe thumni, na binti yake nusu. Na kilichosalia atachukua ami. Na yule wa pili watarithi binti zake wawili thuluthi mbili na kilichosalia nacho ni thuluthi moja atachukua ami.



Mada ya Kumi na Tatu

Namna ya kuwarithisha *Dhawil –Arham:*

Dhawil Arham ni watu gani?

Dhawil Arham ni ndugu wa marehemu ambao hawamo katika orodha ya watu waliotajwa wala kubainishwa viwango vyao vya kurithi kwa maana hiyo wao hawana mafungu maalumu yaliyotajwa wala hawamo katika aswaba. Watu hao ni mfano wa mjomba, mama mdogo (mdogo au mkubwa wa mama mzazi), shangazi, binti ya baba mdogo (ami), mtoto wa kiume wa dada, mtoto wa kike wa dada, watoto (wajukuu) wanaozaliwa na watoto wa kike, na kila ndugu ambaye hayumo miongoni mwa warithi, kwani hakutajwa kuwa atapata fungu gani katika orodha ya wenye mafungu ya kurithi wala hakutajwa katika orodha ya aswaba (*Aswaba* ni wale wanaorithi kinachosalia baada ya kugawa mafungu ya wale wanaorithi kwa mafungu yaliyotajwa).

Hukumu ya kuwarithisha *Dhawil Arham:*

Maoni ya ulamaa yametafutiana kuhusu uhalali wa kuwarithisha *Dhawil Arham:*

Baadhi yao wakiwemo maswahaba, Tabiina, na Maimam. ambao hawaoni uhalali wa kuwarithisha *Dhawil Arham* hoja yao kwa msimamo huo ni kuwa: suala la kurithisha amelifanya yeye Mwenyewe Allah (*Subhanuhu wa Taala*) katika kitabu Chake Kitukufu Katika kutaja mafungu ya warithi na aswaba Allah (*Subhanuhu wa Taala*) hakutaja *Dhawil-Arhami* kuwa wamo, na kutowataja hakuna maana kuwa Allah alisahau ili sisi tumkumbushe.

Imam Maliki na Imam Shafii (Allah awarehemu) Ni miongoni mwa maimamu wenye rai hii. Kuna ulamaa wengine wanaona kuwa ni halali kuwarithisha *Dhawil-Arhami*. Na miongoni mwao ni Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad (Allah awarehemu).

Hoja yao kwa msimamo wao huo ni kuwa: Imepokewa kuwa Mtume ﷺ aliwapa mirathi *Dhawil Arham* pale walipokosekana warithi, miongoni mwa warithi ambao wametajwa na Allah katika kitabu Chake Kitukufu pale aliposema:

“*Mjomba ni mrithi wa mtu aliyekufa bila kuacha mtu wa kumrithi*”.
(Imepokewa na Tirmidhi na Abu Dawud na Sanadi yake ina udhaifu).

Rai yenye nguvu baina ya Rai hizi Mbili:

Rai yenye nguvu kati ya rai hizi mbili ni rai yenye kukubali uhalali wa kuwapa mirathi *Dhawil-Arhami*, kwa hoja kuwa *Dhawil Arhami* ni katika ndugu na udugu ni muhimu kuendelezwa, na kwa kuwa kinachowaunganisha watu hawa ni udugu (*Qaraaba*) Uislamu. Na hiyo ni tofauti na *Baitul Mali*, kwani hakuna uhusiano wa marehemu na *Baitul Mal* ila kwa njia moja ya Uislamu tu. Zaidi ya hoja hiyo ni kuwa ili mali ya marehemu ipelekwe *Baitul Mali* inalazimika yakamilike masharti yafuatayo:

Kwanza: *Baitul Mali* iwe na mpangilio mzuri.

Pili: Viongozi wake wawe waadilifu.

Tatu: Wasimamizi wake wawe waaminifu.

Nne: Mali yake itumike kwa ajili ya maslahi ya Waislamu wote ka ujumla.

Lakini wakati mwingine masharti haya huwa hayakamiliki katika uongozi wa *Baitul Mali* na hili linazidi kutufanya tuone umuhimu wa kuwapa mirathi *Dhawil Arhami* badala ya *Baitul Maali*.

Namna ya kurithisha *Dhawil Arhami*.

Dhawil Arhami wanarithi kwa kufananishwa na warithi ambao ndio wanaowaunganisha na marehemu kwa hiyo wanachukua nafasi yao na wanapata mafungu sawa na mafungu ambayo wangepata kama wangukewepo. Hivyo mmoja wao anapewa mgao (fungu) ambalo angapewa yule aliyesababisha uhusiano baina ya *Dhawil Arhami* huyo na marehemu na ambaye *Dhawil Arhami* amechukuwa nafasi yake.

Kwa Mfano: Mtu amekufa na amemuacha binti amezaliwa na mtoto wake wa kike (mjukuu anayezaliwa na mwanae wa kike). Pia akamuacha mtoto wa kiume wa dada, hawa watagawana nusu kwa nusu. Binti wa binti anapata nusu kwani

Minhajil Muslim

ndio fungu la mama yake kama angelikuwepo. Akifa mtu akamuacha binti yake na dada yake hapa mali itagawiwa baina yao nusu kwa nusu, sawa kwa sawa, kwani fungu la binti katika mas-ala haya anapata nusu, pia fungu la dada, nayeye anapata nusu.

Na tukijaalia kuwa dada huyu ni dada kwa baba na mama (*shaqiqat*) na pamoja naye yuko binti wa kaka wanaochangia baba tu, huyo binti wa kaka anayechangia baba hapati kitu kwa sababu mtu aliyemuunganisha na marehemu na ambaye ni kaka wa baba tu hapati chochote anapokuwa na kaka wa kwa baba na mama. Hivyo mali iliyoachwa hapa inagawiwa kati ya binti wa mtoto wa kike na mtoto wa kiume wa dada nusu mbili kama ifuatavyo:

Angalia katika jedwali hili namba (1)

	2
Binti wa binti	1
Binti wa dada kwa baba na mama	1
Binti wa kaka kwa baba tu	-

Mas-ala Mengine

Amekufa mtu kaacha binti wa dada yake kwa mama na baba, na binti wa dada yake kwa baba tu, na mtoto wa kiume wa dada anayechangia mama tu, na binti wa baba mdogo (ami) wanachangia baba na mama. Katika hali hii binti wa dada kwa baba na mama anachukua nusu kwani ndio fungu la mama yake naye amechukua nafasi ya mama yake, na binti wa dada kwa baba tu anapata sudusi (1/6) ili kukamilisha theluthi mbili, na hilo ndio fungu la mama yake ambaye kachukua nafasi yake, na mtoto wa kiume wa dada kwa mama atapata sudusi (1/6) kwani ndio fungu la mama yake ambaye amechuka nafasi yake. Kilichobaki kitachukuliwa na binti wa baba mdogo (ami) na kwa baba na mama ambalo ndilo fungu la baba yake kwani yeye katika mas-ala ni aswaba.

Angalia jedwali namba 2:

	6
Binti wa dada kwa baba na mama	3
Binti wa dada kwa baba tu	1
Mtoto wa kiume wa dada kwa mama tu	1
Binti wa ami kwa baba na mama	1

Mas-ala haya inafanyika kwa sita (6) kwa sababu kuna waliopata sudusi (1/6) na nusu ya sita ni tatu (3) ambayo tumempa binti wa dada kwa mama na baba (*shaqiqa*) na sudusi yake ni moja ambayo tumempa binti wa dada kwa upande wa baba tu ili kukamilisha theluthi mbili, na sudusi yake moja nyingine tumempa mtoto wa kiume wa dada kwa upande wa mama tu na kilichobaki (moja) ambacho ni sudusi (1/6) anakichukua binti wa mdogo (ami) wa upande wa baba na mama.

Mas-ala Mengine:

Amekufa mtu hakuacha mtu wa kumrithi ila *Dhawil Arhami* hao ni: Binti wa Binti yake, na mtoto wa kiume wa dada kwa baba na mama (*shaqiqat*) na mtoto wa kiume wa dada wanayechangia mama tu, na binti wa kaka wanayechangia baba tu.

Katika hali kama hii binti au binti yake atapata nusu ya mali yote kwani ndilo fungu ambalo angepata mama yake kama angekuwepo na kwa kuwa yeye amepitia kwa mama yake basi anagawiwa kama mama yake. Mtoto wa kiume wa dada na mama atachukuwa nusu iliyobaki kwani ndio fungu ambalo angelipata mama yake kama angekuwepo na kuwa yeye kapitia upande wa mama basi anapewa fungu ambalo lingekuwa ni la mama yake. Ama mtoto wa kiume wa dada wanayechangia mama tu huyo hapati kitu kwani mama yake ambae yeye kapitia upande wake katika hali kama hii hapati urithi kwa sababu ya kulingwa na mtoto wa kike anayezaliwa na binti yake. Vile vile binti wa kaka wanachangia

Minhajil Muslim

baba tu katika hali kama hii hapati urithi kwani njia aliyopitia ambayo ni kaka kwa upande wa baba tu hapa amekingwa kwa kuwepo dada wa baba na mama *shaqiqat* na hii ndiyo sura ya mas-ala haya:

Jedwali namba 3

	2
Binti ya binti	1
Mtoto wa kiume wa dada <i>shaqiqat</i>	1
Mtoto wa kiume wa dada kwa mama tu	-
Binti wa kaka wa kwa baba tu	-

Mas-ala haya yanafanywa kwa namba mbili kuwa namba hiyo ina nusu mbili ambazo ni moja aliyopewa binti ya binti kwani ndiyo mirathi ya mama yake, na nusu ya pili ambayo ni moja aliyopewa mtoto wa kiume wa dada *shaqiqat*, kwa vile ndiyo fungu la mirathi ya mama yake ambaye ni dada *shaqiqa*.

Ama mtoto wa kiume wa dada wanayechangia mama yeye harithi kwani mama yake amekingwa na binti wa binti. Pia binti ya kaka wanayechangia baba naye harithi, kwani baba yake ambaye ndiye sababu ya yeye kurithi amekingwa kwa kuwepo dada *shaqiqat* kama ilivyoonyeshwa.

Mas-ala mengine:

Amekufa mtu ameacha mama mdogo na shangazi. Mama mdogo hapa atapata theluthi (1/3) kwani ndio fungu ambalo angepata mama ambaye yeye kapitia upande wake kwa hiyo amechukua nafasi yake. Na shangazi anachukua theluthi mbili zilizobaki kwani ndio fungu ambalo lingechukuliwa na baba ambaye yeye amepitia kwake, kuwa baba ni katika *Aswaba* anarithi kilichobaki baada ya kugawa mafungu yote.

Angalia mfano katika wa Jedwali namba mne:

	3
Mama mdogo	1
Shangazi	2

Mas-ala hapa inagawika kwa tatu, kwani ndani yake kuna theluthi mbili (2/6) theluthi moja ambayo ni moja (1) ndiyo fungu la mama mdogo kwani cheo chake ni sawa na mama ambaye yeye amepitia kwake, hivyo amechukua nafasi ya mama. Ama theluthi mbili zilizobaki ambazo ni mbili (2) hizo ni fungu la shangazi kwani shangazi amepitia kwa baba na amerithi sawa na baba kama angekuwepo, na fungu lake ni kuchukua kitachobaki baada ya kugawiwa mafungu yote.

Mambo ya kuzingatia:

a) *Dhawil Arhami* hawarithi iwapo atakuwepo yeyote miongoni mwa warithi ambao mafungu yao tayari yametajwa katika mirathi au wale wanaorithi kwa kuchukua kinachobakia (maswaba) kwani kinapobaki kitu baada ya kugawa mafungu yote hunadishwa tena wakapewa walewale warithi mpaka mali yote imalizike, isipokuwa kama mrithi pekee atakuwa ni mume au mke hapo *dhawil-Arhami* anapata nafasi ya kurithi:

Kwa mfano: Amekufa mtu kaacha kaka yake, wamechangia mama au kaka wanayechangia baba pia akaacha shangazi.

Hukumu ya mas-ala haya:

Kaka yake anayechangia mama au kaka wanayechangia baba atachukua mali yote na shagazi hapati cha kurithi kwani shangazi ni katika *Dhawil-Arhami* na hakuna kilichobaki ambacho kitakuwa fungu lake.

Pia akifa mtu akaacha mama mzazi na mama mdogo, mali yote ni ya mama, atarithi fungu lake kisha kinachobaki atapewa na mama mdogo hapati urithi kwani mama ni katika warithi waliotajwa na kutajwa fungu lake, na mama mdogo miongoni mwa *Dhawil-Arhami*. Hivyo mama anamkinga mama mdogo.

Pia kama atakufa mtu akaacha mke na binti ya kaka. Hapa mke atachukua robo kwani ndilo fungu lake na kitachobaki kitachukuliwa na binti wa kaka kwani yeye anachukua nafasi ya baba yake na aswaba ambaye hurithi kwa kuchukua kilichobaki baada ya kugawa mafungu yote.

b) *Dhawil Arhami* wanapokusanyika na kujumuika wote huangaliwa wanavyoangaliwa warithi wa asili wanaofahamika katika mafungu na asaba. Hivyo yule wa karibu na marehemu miogoni mwao atamzuia wa mbali katika kurithi na kaka *shaqiqi* anamkinga kaka wa baba.

Wanapolingana katika daraja na ukaribu, wao kwa marehemu watalingana katika kurithi hatazidi yoyote kwa mtoto wa kiume atachukua mara mbili ya mtoto wa kike (dada yake).

Mfano wa hilo ni: Amekufa mtu ameacha binti ya binti na binti ya binti ya binti ya binti, au mtoto wa kiume wa binti ya binti. Mali yote itachukuliwa na binti ya binti, peke yake, na waliobaki hawapati chochote kwani huyu binti wa binti daraja lake na ukaribu wake kwa marehemu ni mkubwa sana, na kila anayekuwa karibu anamkinga wa mbali.

Mfano mwingine:

Amekufa mtu ameacha binti ya kaka yake kwa baba na mama, pia binti ya kaka yake kwa baba tu, mali yote ni ya binti ya kaka yake kwa baba na mama (*shaqiqi*) na binti ya kaka yake kwa baba hatapata urithi kwani kaka kwa baba na mama anamkinga kaka wanayechangia baba tu.

Hivyo anayechukua nafasi ya kaka *shaqiqi* atafanana naye katika kurithi au kukosa urithi. *Dhawil Arhami* watakaopitia upande wa anayerithi basi nao watarithi fungu ambalo lingekuwa lake, na watakaopitia upande wa asiyepata chochote basi nao watakosa.

Kwa mfano:

Amekufa mtu akaacha binti wa binti wa mtoto wa kiume, na mtoto wa kiume wa mtoto wa kiume wa binti mali hapa ni ya binti ya binti ya mtoto wa kiume hivyo mwenzake hapati chochote.

Kwani hata kama wanalingana katika daraja kwa sababu kila mmoja wao amefika kwa marehemu kwa daraja mbili lakini binti ya binti ya mtoto wa kiume amepitia kwa anayerithi, hivyo naye ndiyo maana anarithi, naye mtoto wa kiume wa mtoto wa kiume wa binti amepitia njia ya mtu asiyerithi ndiyo maana hakurithi. Kwani mtoto wa kiume wa mtoto wa kiume ni katika warithi na mtoto wa kiume wa mtoto wa kike si miongoni mwa warithi.



Kinahusu Yamini na Nadhiri

Mada ya Kwanza

‘Yamini’

1-Maana yake:

‘Yamini’ ni kuapa kwa majina ya Allah Mtukuka, au Sifa zake Mfano. Wallah nitafanya kitu kadhaa... au naapa na yule ambaye nafsi yangu iko mikononi Mwake au Mgeuza Nyoyo.

2-Yamini Inayokubalika na isiyokubalika:

Yamini inakubalika kama itakuwa kwa maji na ya Allah Mtukuka kwa sababu Mtume ﷺ alikuwa anaapa kwa kutaja jina la Alah ambaye hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa kwa ibada ya haki ila yeye tu si mwingine, na hakuwa akiapa kwa kauli yake,

“Naapa kwa Yule Ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi Mwake.”

Na Jibril عليه السلام ameapa kwa Utukufu wa Allah akasema:

“Naapa kwa Utukufu Wako hakuna atakayesikia ila atauingia.”
(Tirmidhi)

Na Yamini haikubaliki bila majina ya Allah Aliyetukuka na Sifa zake, ni sawa kinachoapiwa kinatukuzwa kwa sheria kama vile al-Kaaba Tukufu Allah Alilinde na Mtume ﷺ au kisichotukuzwa.

Ni kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Anayeapa aape kwa Allah au anyamaze.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim na Ahmad).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Msiape ila kwa Allah na msiape ila muwe wakweli.” (Imepokewa na Abu Dawud na Nasai).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Atayemuapia asiyekuwa Allah basi huyo amemshirikisha Allah.”
(Ahmad).

Kauli yake Mtume ﷺ,

“Atayemuapia asiyekuwa Allah amekufuru.” (Tirmidhi na al-Hakim).

1-Vigawanyo vyake:

Yamini Inagawika Sehemu Tatu, Nazo ni:

a-Al-Ghamus (ya uongo):

Maana yake ni mtu kuapa huku anakusudia kudanganya, kama vile kusema: Wallahi nimenunua kitu kadha kwa khamsini, naye hakukinunua hivyo, au akasema: Wallahi nimefanya kadha, naye hakufanya. Na yamini hii imeitwa *Ghamus* kwa sababu inamzamisha mwenye yamini hiyo ndani ya dhambi, na yamini hii ndiyo iliyokusudiwa kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Atakayekula yamini hali yeye katika yamini hiyo anadanganya ili apate kwa yamini hiyo kumega mali ya mtu mwingine Muislamu basi mtu huyo atakutana na Allah hali ya kuwa amemkasirikia.”
(Imepokewa na Bukhari, Abu Dawud, Tirmidhi na Ibn Majah).

Na Hukumu ya Yamini al-Ghamus:

Ni kwamba kafara tu peke yake haitoshi bali pamoja na kafara mhusika atubie na kuomba maghfira (msamaha) kwani kosa hili ni kubwa sana. Hasa ikiwa yamini hiyo itamfikisha kwenye kumega haki ya mtu mwingine Muislamu kwa njia isiyo halali.

Minhajil Muslim

b-Laghwul-Yamini (ya upuuzi): hii ni ile ipitayo katika ulimi wa Muislamu bila ya kuikusudia, kama katika mazungumzo yake hujitokeza kwa wingi neno: Wallahi hapana, na ndio Wallalhi. Kufuatia kauli ya Mama Aisha رضي الله عنها

“Upuuzi katika yamini ni maneno anayozungumza mtu nyumbani mwake Wallahi hapana.” (Bukhari).

Miongoni mwa hizo ni Muislamu kuapa juu ya jambo fulani akilidhania liko hivyo ikaja ikabainika tofauti na alivyodhania.

Hukumu ya yamini hii:

Haina dhambi wala kafara kwa mhusika, kwa kauli yake Allah Aliyetukuka.

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَدْتُمُ الْأَيْمَانَ

“Mwenyezi Mungu hatakushikeni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini atakushikeni kwa mnavyo apa kweli kweli kwa makusudio...” (5:89)

c-Yamini iliyofungika: Hii ni yamini inayochukuliwa kwa kukusudiwa jambo la baadaye. Kama vile Muislamu akasema: “*Wallahi* nitafanya jambo kadhaa... au *Wallahi* sitalifanya...” hii ndio yamini atakayoadhibiwa atakayefanya kinyume chake kwa kauli ya Allah.

وَلَكِنْ يُؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَدْتُمُ الْأَيْمَانَ

“...lakini atakushikeni kwa mnavyo apa kweli kweli kwa makusudio...” (5:89)

Hukumu yake:

Akayekwenda kinyume na hivyo atapata dhambi na atawajibika atoe kafara, kama atatoa kafara dhambi ltaanguka dhidi yake na kumuondoa.

4) Kinachoondoa Kafara: Kafara itaanguka na dhambi kwa mwenye kula yamini kwa mambo mawili:

a) Kama atafanya lile alilokula yamini atalifanya, au akaliacha lile alilokula nalo yamini kuliacha, au kulifanya alilokula yamini kuliacha, au kuacha alichopa kuwa atalifanya lakini iwe kwa kusahau au kwa bahati mbaya au kwa kulazimishwa. Kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Atakayekula yamini akasema Inshaalahu hakwenda kinyume na yamini yake.” (Imepokewa na Tirmidhi, Nasai na Ahmad).

Na asipokwenda kinyume hana dhambi wala kafara.

5) Kupendekezwa kuhalifu yamini katika mambo ya kheri

Ikiwa Muislamu atakula yamini ya kuacha jambo la kheri ni sunna asilifanye, na atoe kafara la hiyo yamini yake, kwa kauli ya Allah Aiyetukuka.

وَلَا تَجْعَلُوا اللَّهَ عُرْضَةً لِأَيْمَانِكُمْ أَنْ تَبَرُّوا

“Wala msifanye jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio cha kuacha kufanya wema...” (2:224)

Kauli ya Mtume ﷺ

“Kama utakula yamini ukaona lililo bora kuliko hilo basi lifanye hilo bora na fanya kafara la yamini yako.” (Muslim).

6) Wajibu wa kuitekeleza yamini:

Muislamu anapomlia yamini Muislamu mwenzake kuwa atafanya kitu, basi ni wajibu kutekeleza kama alivyokula yamini, na asihalifu na kutoa kafara madamu kuna uwezekano wa kutekeleza yamini yake, na kuacha kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Kwa mwanamke aliye zawadiwa tende naye akala baadhi na baadhi akabakisha na akala kiapo mtoa tende kumuapia mpewa tende kuwa lazima zilizosalia azile naye akakataa kuzila, Mtume ﷺ, Akasema, Mkamilishie yamini yake kwani dhambi za yamini ziko juu ya mwenye kuhalifu yamini yake.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, Ahmad na Nasai).

7) Kiapo kulingana na nia ya mwenye kuapa:

Kinachozingatiwa katika kwenda kinyume na yamini na kutovunja nia na kusudio la mla yamini, kwa sababu matendo huthibitishwa na nia, na kila mtu atapata alichokusudia atayekula yamini kuwa hatolala juu ya ardhi akiwa anakusudia godoro, basi yamini hiyo itakuwa kulingana na nia yake, kwa hiyo hatokwenda kinyume kama hakulala juu ya godoro, atayekula yamini kuwa hatavaa katani hii nguo akavaa suruali ya katani hiyo, hakwenda kinyume na yamini yake kama kiapo chake amekusudia nguo tu. Kama si hivyo atakuwa amekwenda kinyume.

8) Kafara la Yamini:

Kafara la yamini ni mambo manne:

- a) Kulisha maskini kumi kwa kumpa kila mmoja kibaba cha ngano, au kukusanya wote katika chakula cha mchana au usiku wale mpaka washibe au kumpa kila mmoja mkate na mchuzi.
- b) Kuwavisha nguo inavyotosheleza katika sala, na kama atampa mtu mwanamke ampe kanzu na mtandio kwa sababu huo ndio uchache wa vazi au linalomtosheleza katika sala.
- c) Kumuacha huru mtumwa Muislamu.
- d) Kufunga siku tatu mfululizo kama ataweza, asipoweza kufufuliza atafunga mbali mbali. Hafungi ila baada ya kushindwa kulisha au kuvisha au kuacha huru mtumwa kwa kauli ya Allah Mtukufu:

فَكَفَّرْتُمُوهُ إِطْعَامَ عَشْرَةِ مَسْكِينٍ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعَمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ
كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ^ط فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ^ع ذَلِكَ كَفَّارَةٌ
أَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ^ع

“Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha wastani mnacho walisha ahali zenu, au kuwavisha, au kumkomboa mtumwa. Asiye pata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapo apa...” (5: 89).



Mada ya Pili:

Inahusu Nadhiri

1) Maana yake:

Nadhiri ni kujilazimisha Muislamu kufanya ibada kwa ajili ya Allah ambayo si wajibu juu yake ibada hiyo kabla ya nadhiri hiyo kama kusema: Ninajilazimisha kwa Allah kufunga siku moja au kuswali raka mbili.

2) Hukumu yake:

Hukumu ya *nadhiri* ni hii ifuatayo: Inaruhusiwa nadhiri isiyokuwa na masharti ambayo inawekwa kwa ajili ya Allah kama vile nadhiri ya kufunga au kuswali na kutoa sadaka, na itakuwa wajibu kuitekeleza. Na itakuwa karaha nadhiri yenye masharti kama vile kusema: Allah kama atamponyesha mgonjwa wangu nitafunga siku kadhaa au nitatoa sadaka kadhaa kwa kauli ya Ibnī ‘Umar رضي الله عنه Mtume ﷺ amekataza nadhiri na akasema,

“Yamini hairejeshi kitu, bali hutolewa kwa nadhiri mali ya bakhili.” (Bukhari na Muslim).

Na itakuwa haramu kama haitakuwa kwa ajili ya Allah Mtukufu kama vile kuwekea nadhiri makaburi ya mawalii au roho za watu wema, kama vile kusema: Ewe muheshimiwa mtukufu wangu ikiwa Allah atamponesha mgonjwa wangu, nitachinja kaburini kwako kitu kadhaa au nitakutolea sadaka kitu kadhaa kwa sababu kufanya hivi maana yake ni kumuabudu asiyestahiki ibada, na kufanya hivyo ni kumshirikisha Allah ushiriki ambao Allah ameharamisha kwa kauli yake:

✽ وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا

“Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote...” (4: 36).

3) Aina zake:

Nadhiri ina aina nyingi nazo ni:

a) **Ni ile inayotoka kwa mtu kwa kusema:** Wallah nitafunga siku tatu au kuwalisha masikini kumi, akitaka hivyo ili kujikurubisha kwa Allah (*Subhanahu wa Taala*). Hukumu ya Nadhiri hii ni kuitekeleza kwa kauli Yake Allah (*Subhanahu wa Taala*)

وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ

“...*Na timizeni ahadi ya Mwenyezi Mungu mnapo ahidi...*” (16:91).

Na kauli Yake:

وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ

“*Na watekeleze Nadhiri zao*” (22:29)

b) **Nadhiri isiyokuwa na masharti** na haikutaja kitakachotekelezwa kama vile Muislamu kusema: Ninajilazimisha kwa Allah nadhiri akawa hakuitaja nadhiri yenyewe. Na hukumu ya nadhiri hii ni wajibu kwa mwenye kuweka nadhiri aitekeleze na kutekeleza kwake ni kutoa kafara ya yamini kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“*Kafara la nadhiri asiyoitaja ni kafara ya yamini.*” (Tirmidhi).

Inasemekana katika nadhiri ya namna hii itamtosha chochote kile kinachoitwa nadhiri kama vile kuswali rakaa mbii au saumu ya siku moja.

c) **Nadhiri iliyowekwa sharti** na sharti lenyewe liko katika uwezo wa Allah' kama vile kauli ya Muislamu kama Allah atamponya mgonjwa wangu au kama atamrejsha mpotevu wangu nitalisha masikini kadhaa, au nitafunga siku kadhaa.

Hukumu ya aina hii ya nadhiri ingawa ina karaha lakini inapasa kuitekeleza, ikiwa Allah amemkidhia mahitaji yake inamlazimu kuitekeleza kwa kufanya alichokitaja miongoni mwa ibada kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Aliyeweka nadhiri kumtii Allah basi amtii.” (Bukhari).

Na ikiwa Allah hakumkidhia haja yake si wajibu kuitekeleza.

d) **Nadhiri iliyowekewa sharti** lililo katika uwezo wa kiumbe na nadhiri hii huwa nadhiri ya malumbano kama kusema ukifanya jambo fulani basi mimi nitafunga mwezi mzima, au kama litatokea jambo fulani basi mimi nitatoa katika mali yangu kitu kadhaa.

Hukumu ya nadhiri hii, mwenye kuweka nadhiri ana hiyari kufanya moja ya mambo mawili, kutekeleza nadhiri yake au kutoa kafara la yamini kwa sababu ni kufanya kinyume na kilichowekewa nadhiri kwa kauli ya Mtume ﷺ :

“Hakuna nadhiri katika hasira na kafara lake ni kafara la yamini.” (Imepokewa na Abu Dawud, Nasai na Ahmad).

Kwa sababu mara nyingi nadhiri ya malumbano inakuwa katika hasira na ina maana ya kumzuia anayeelezwa asifanye kitu aache.

e) **Nadhiri ya maasi**, nayo ni ile ya kuweka nadhiri ya tendo la haramu au kuacha wajibu kwa mfano akanadhiria kumpiga muumini, au kuacha kuswali.

Hukumu yake ni haramu kuitekeleza, kwa kauli ya Mtume ﷺ .

“Aliyeweka nadhiri kumtii Allah-amtii na mwenye kuweka nadhiri amuasi Allah- asimuasi.” (Imepokewa na Ahmad, Tirmidhi, Ibnu Majah na Abu Dawud).

Isipokuwa baadhi ya wanazuoni wanasema mtu huyu inamlazimu kutoa kafara la yamini kwa kauli ya Mtume ﷺ :

“Hakuna nadhiri katika maasi, na kafara lake ni kafara la yamini.” (Abu Dawud).

f) **Nadhiri ya asichokimiliki Muislamu** au asichoweza kukifanya. Kwa mfano: akaweka nadhiri kumwacha huru mtumwa wa fulani si wake au atatoa Sadaka kintari ya dhahabu.

Hukumu yake ni kutoa kafara kwa hadithi ya Mtume ﷺ:

“Hakuna nadhiri katika kitu asichokimiliki.” (Abdurrazzak na An-Nasai).

g) **Nadhiri ya kukiharamisha alichokihalalisha Allah Mtukufu:** kwa mfano, akatoa nadhiri kuharamisha chakula au kinywaji alichokihalalisha Allah.

Hukumu yake kitu hicho hakitakuwa haramu kwani hakuna atakayekiharamisha alichokihalalisha Allah isipokuwa mke, ataye toa nadhiri kumharamisha juu yake mkewe basi atakuwa haramu mpaka afanye kafara la nadhiri ama kisichokuwa mke anachotakiwa kufanya ni kafara la yamini.

Tanbihi:

1. Aliye toa nadhiri kutoa mali zake zote yamtosha kutoa thuluthi yake ikiwa nadhiri isiyokuwa na masharti, na ikiwa ni nadhiri ya malumbano itamtosha kutoa kafara la yamini tu.

2. Aliyetoa nadhiri kufanya ibada akafa kabla hajaitekeleza basi walii wake ndiye atayetekeleze kwa niaba yake, kufuatia hadithi sahihi kuwa mwanamke fulani alimwambia Ibn ‘Umar رضي الله عنه kuwa mama yake ameweka nadhiri kuswali katika *Masjid Quba* kisha akafa. Ibn ‘Umar رضي الله عنه akamuamuru mwanamke akaswali *Masjid Quba* kwa niaba ya mama yake.



Kuchinja, Kuwinda, Vyakula na Vinywaji

Mada ya Kwanza

Yahusu Kuchinja

1) Maana yake:

Kuchinja ni kuchinja kinachochinjwa katika wanyama halali kuliwa na kuchinja ni kukata chini ya shingo kwa yule anayechinjwa hapo.

2) Ufafanuzi:

Ufafanuzi wa anayechinjwa juu ya shingo na yule anayechinjwa chini ya shingo. Mbuji, kondoo na pia aina za ndege kama vile kuku na wengine wanachinjwa juu ya shingo sio chini Amesema Allah Mtukufu:

وَفَدَيْنَهُ بِذَبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١٧﴾

“Basi tukamtolea fidia kwa dhabihu mtukufu.” (37:107).

Na ng’ombe anachinjwa kwa kauli ya Allah:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَذَحُوا بَقَرَةً

“...Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mchinje ng’ombe...” (2: 67)

Inafaa kumchinja chini ya shingo kwani imethibitika hivyo kwa Mtume ﷺ kuwa ng’ombe ana sehemu mbili za kumchinja, mahala pa *dhabhi* na Mahala pa *Nahr*; ama ngamia anachinjwa chini ya shingo, *Nahri*, si juu yake, na Mtume ﷺ amechinja ngamia chini ya shingo–*Nahri* huku ngamia amesimama na huku mkono wake, mguu wake wa mbele wa kushoto umefungwa.

3) Maana ya *Nahri* na *Dhabhi*:

Dhabh kukata koo, mrija wa hewa, na mishipa mikuu miwili iliyo kulia na kushoto mwa shingo. Na *Nahri* ni kumtoboa ngamia katika liba yake, na liba ni mahala kinapokaa kidani shingoni na hapo ni mahala ambapo kisu kinafika kwenye moyo kwa kupitia hapo na mnyama anakufa haraka.

4) Namna ya *Dhabhi* na *Nahri*:

Dhabhi: mbuzi anaangushwa na kulazwa ubavu wa kushoto hali ameelekezwa kibla baada ya kuandaa chombo cha kuchinja kuwa kikali, kisha mchinjaji atasema: “*Bismillah, Allahu Akbaru*” na hapo mnyama atachinjwa, vitakatwa kwa mara moja koo, mfereji wa hewa na mishipa mikuu miwili kulia na kushoto mwa shingo ya mnyama.

Ama *Nahri* ni kumfunga ngamia mguu-mkono wa kushoto huku amesimama kisha anatobolewa na mchinjaji chini ya shingo yake mahali pana poka kidani huku anasema, “*Bismillah Allahu Akbaru*” na ataendelea na harakati za kutoboa mpaka roho yake inatoweka. Kwa kauli ya Ibni ‘Umar رضي الله عنه alipopita kwa mtu fulani amemlaza chini ngamia wake tayari kwa kumchinja:

“Msimamisha wima huku amefungwa ndio sunna ya Muhammad ﷺ” (Bukhari na Muslim).

5) Sharti za kuswihi kuchinja:

Ili kuchinja kuwe sahihi ni sharti yapatikane yafuatayo:-

a) Chombo cha kuchinja lazima kiwe kikali kinachorusa damu kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Kilicho mwaga damu, na likatajwa jina la Allah juu yake kula, kisiwe mfupa na ukucha.” (Bukhari na Muslim).

b) Bismillahi aseme: “*Bismillahi Allahu Akbaru au Bismillahi*” tu kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَلَا تَأْكُلُوا مِمَّا لَمْ يُذَكَّرْ اسْمُ اللَّهِ عَلَيْهِ

“Wala msile katika wale wasio somewa jina la Mwenyezi Mungu...” (6: 121).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Kiichomwagwa damu na likatajwa jina la Allah juu yake kuleni.” (Bukhari na Muslim).

c) Kukata koo chini ya koromeo pamoja na kukata mfereji wa hewa na mishipa mikuu miwili kulia na kushoto mwa shingo ya mnyama kwa pamoja.

d) Sifa ya mchinjaji kwamba awe Muislamu baleghe mwenye akili timamu au mtoto mpambanuzi na si vibaya kama atachinja mwanamke au Ahli kitabu, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حِلٌّ لَكُمْ

“Na chakula (mnyama) kilichochinjwa cha waliopewa kitabu ni halali kwenu.” (5:45)

Na limefasiriwa neno chakula chao kuwa ni vilivyochinjwa na wao.

e) Kama itashindikana kumchinja mnyama labda kwa kuangukia kisimani au kwa kucharuka itafaa kumchinja kwa kumjeruhi popote pale katika viungo vya mnyama huyo kwa silaha inayoweza kumwaga damu kwa kauli ya Mtume ﷺ alipocharuka ngamia na wenye ngamia walikuwa hawana farasi, mmoja wao akamrushia mshale ukamzuia:

“Hakika ya hawa wanyama wana unyama kama unyama wa wanyama pori atakayefanya katika hao kama hivyo basi mfanyeni hivi.” (Bukhari na Muslim)

Wanazuoni wakachukua kiasi (kigezo) kila mnyama aliyeshindikana kumchinja kwenye koo lake au chini ya shingo yake.

Tanbihi:

1. Kuchinjwa mtoto aliye tumboni mwa mama yake ni kule kuchinjwa mama yake, na vizuri kumla kama umbile lake limekamilika, na nywele zake zimeota. Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu huyo mtoto aliye tumboni akasema:

“Mkitaka kuleni kwani chinjo lake ni chinjo la mama yake”
(Imepokewa na Ahmad, Abu Dawud na Ibn Majah).

2. Kuacha Bismillahi kwa kusahau haidhuru katika kuchinja kwa vile umma wa Muhammad hauadhibiwi kwa kusahau kwa hadithi:

“Kwa umma wangu limeondolewa dhambi la kosa walilolifaya kwa bahati mbaya au kusahau na walilolazimishwa.”

Na kauli yake ﷺ,

“Kichinjwa cha Muislamu ni halali limetajwa jina la Allah au halikutajwa, kwa sababu likichinjwa halitatajwa isipokuwa jina lake.” (al Balhaqi).

3. Kuchinja sana mpaka kutenganisha kichwa cha mnyama ni ubaya lakini mnyama aliyechinjwa hivyo ataliwa bila ya karaha.

4. Mchinjaji kama alifanya kinyume kwa mfano akamchinja chini ya shingo mnyama anayechinjwa juu ya shingo, au akamchinja juu ya shingo anayechinjwa chini ya shingo, mnyama ataliwa pamoja na karaha.

5. Anayeumwa na aliyejinyonga, na aliyepegwa kwa kitu kizito, na aliyeanguka kutoka kwenye muinuko, aliyepegwa pembe na mwenzake na aliyeliwa na mnyama mkali kama atawahiwa akiwa hai kiasi cha kama atachinjwa roho yake itaondoka kwa kuchinjwa si kwa sababu ya ugonjwa na akachinjwa inaruhusiwa kuliwa, kwa kauli ya Allah:

إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ

“ila mkimdiriki kumchinja...” (5:3)

Minhajil Muslim

Yaani mumediriki uhai na mkauondoa kwa kuchinja.

6. Mchinjaji kama atainua mikono yake kabla hajamaliza kuchinja kisha akaurejesha baada ya kupita muda mrefu wanazuoni wamesema: Mnyama huyo haliwi isipokuwa chinjo lake kama limemalizika kwa mara ya kwanza.



Mada ya Pili

Inahusu Kuwinda

1) Maana yake:

Kiwindwa ni kinachowindwa miongoni mwa wanyamapori au wanyama wa majini yaani wanaoishi katika maji – bahari.

2) Hukumu yake:

Ni halali kuwinda kwa asiye katika ibada ya hija au umra, kwa kauli ya Allah Mtukufu,

وَإِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَبَّادُوا

“*Na mkisha toka Hija yenu basi windeni...*” (5:2).

Isipokuwa inakuwa karaha kama itakuwa kwa upuuzi na mchezo tu.

3) Aina yake:

Wanyama wako aina mbili: wanyama wa baharini, nao ni kila mnyama anayeishi baharini kama vile samaki, na wengineo miongoni mwa wanyama wa baharini.

Hukumu yake:

Ni halali kwa aliye na asiye katika ibada ya Hija au Umra, na hakuna aliyekuwa karaha isipokuwa mwanadamu wa majini na nguruwe maji, kwa sababu ya ushirikiano wa jina na wanadamu na nguruwe ambao ni haramu. Na wanyama wa bara, nao wana jinsi tofauti na hao watakuwa halali wake tu waliohalalishwa na sheria na watakuwa haramu walioharamishwa na sheria.

4) Chinjo la mnyama aliyewindwa.

Chinjo la mnyama wa baharini ni kufa kwake, ni kwamba haliwi akiwa hai, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Tumehalalishiwa mizoga miwili, samaki na nzige.” (al-Baihaq).

Ama wanyama wa bara ni kwamba kama atawahiwa akiwa hai lazima achinjwe, hairuhusiwi aliwe bila ya kumchinja. Kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Na uliyemuwinda kwa mbwa wako asiyefundishwa kuwinda na ukamuwahi kumchinja mle.” (Bukhari na Muslim).

Na kama utamuwahi ameshakufa inaruhusiwa kuliwa kama yatakamilika masharti yafuatayo:

a) Mwindaji kuwa anachokichinja ni halali kama vile kuwa Muislamu mwenye akili timamu aliyepambaukiwa.

b) Mwindaji ataje jina la Allah wakati anaporusha silaha au kumtuma mbwa, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Uliye muwinda mle na ulie muwinda kwa mbwa wako asiyefundishwa kuwinda na ukawahi kumchinja basi mle.” (Bukhari).

c) Na chombo cha kuwinda-kama ni kisichojeruhi kiwe kikali kinachotoboa ngozi, kama si kikali kama vile bakora na jiwe si halali kumla mnyama aliyewindwa kwa vitu hivyo kwa sababu mnyama huyo ni *Mauqudha* amepigwa au kuangukiwa na kitu kizito-isipokuwa kama atamuwahi angali hai akamchinja, kwa kauli ya Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu mi’radhi (kitu chenye ubapa kama vile panga sehemu hiyo badala ya sehemu yenye ukali).

“Kama atampiga kwa ubapa usimle kwani huyo ni Waqidh aliyepigwa au kuangukiwa na kitu kizito.” (Bukhari).

Akiwa mnyama kama vile mbwa au kipanga ni lazima awe amefundishwa kwa kauli ya Allah:

فَكُلُوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَادْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ وَأَنْقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٠٠﴾

“Basi kuleni walicho kukamatieni, na mkisomee jina la Mwenyezi Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu...” (5:4).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Na uliye muwinda kwa mbwa wako aliyefundishwa taja jina la Allah-kisha kula.” (Bukhari).

Tanbihi:

Alama ya mnyama aliyefundishwa na hasa mbwa; ni kuwa akiitwa anaitika na anapotumwa kukamata anatumika anapokatazwa anakatazika, na kwa mnyama asiye mbwa ili sharti la kukatazwa akakatazika si la lazima kwa sababu halipatikani.

d) Mbwa huyu asishirikiane katika kumkamata mnyama huyo na mbwa mwingine aliyefundishwa, kwa sababu haitaeleweka yupi aliyemkamata, yule aliyetamkiwa Bismillahi au mwingine kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Kama utamkuta pamoja na mbwa wako mbwa mwingine na huyo mnyama aliyewindwa ameuliwa basi usimle kwani hauelewi yupi aliyemuua.” (Ahmad).

e) Mbwa aliyewinda asiwe ameanza kumla mnyama huyo na mbwa mwingine aliyefundishwa, kwa sababu haitaeleweka yupi aliyemkamata, yule aliyetamkiwa Bismillahi au mwingine kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Isipokuwa kama huyo mbwa atamla huyo mnyama usimle kwani mimi naogopa pengine amejikamatia yeye mwenyewe.” (Bukhari na Muslim)

Kauli ya Allah:

“Na akasema kuleni alichowakamatia.”

Tanbihi.

1. Endapo mnyama aliyewindwa kapotea kisha muwindaji akamgundua akiwa na jeraha la mshale aliomrushia mathalani na akawa hana athari nyigine isipokua hiyo, mnyama huyo inaruhusiwa kumla, kwa muda wa kuwa hajapita zaidi ya siku tatu kwa kauli ya Mtume ﷺ kwa yule aliyemkuta mnyama wake baada ya siku tatu:

“Kula muda wa kuwa hajatoa harufu mbaya.” (Muslim).

2. Ikiwa mnyama amewindwa kisha akaangukia majini akafa, si halali kumla, kwasababu huwenda kilichomuua ni yale maji na si ile silaha.

3. Endapo mnyama aliyewindwa na mbwa mathalani katika kiungo katika viungo vyake, basi hiki kiungo kilicho katika si halali kuliwa kwani kimeingia chini ya kauli ya Mtume ﷺ.

“Na kilichokatwa kwa aliye hai ni mzoga.” (Tirmidhi).



Mada ya Tatu

Inahusu chakula na kinywaji chakula

1) Maana yake

Kinachokusudiwa kwa neno chakula ni kila kinacholiwa kama vile nafaka tende na nyama.

2) Hukumu yake:

Asili katika vyakula vingine ni uhalali, hiyo ni kutokana na jumla ya kauli ya Allah Mtukufu,

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا

“Yeye ndiye aliye kuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi...” (2:29).

Havitakuwa haramu hivyo ila kile kilichotolewa kwa dalili ya kitabu–Qur-aan au Sunnah au qiasi sahihi. Muweka sheria ameharamisha baadhi ya vyakula kwa sababu vinasababisha madhara kwenye mwili na huharibu akili ya mtu kama alivyowaharamishia chakula umma mwingine si kuwa huu wa Kiislamu kwa ajili ya mtihani. Amesema Allah Mtukufu:

فَيُظْلَمُ مِّنَ الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ طَيِّبَاتٍ أُحِلَّتْ لَهُمْ

“Basi kwa dhulma yao Mayahudi tuliwaharamishia vitu vizuri walivyo halalishiwa...” (4:160).

3) Aina ya vilivyoharamishwa:

a) Vilivyo haramishwa kwa dalili ya kitabu, navyo ni:

i) Chakula cha mwenzake si chake, hakimiliki kwa sura yoyote miongoni mwa sura za kumiliki ambazo zinamhalalishia kula, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ

“Wala msiliane mali zenu kwa baat’ili...” (2:188).

Kauli ya Mtume ﷺ,

“Asikae mmoja wenu mnyama wa mwengine isipokuwa kwa ruhusa yake.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim na Abu Dawud).

ii) Mzoga, mzoga ni yule aliyekufa hvi hivi sio kwa kuchinjwa miongoni mwa wanyama na katika jumla ya mizoga aliyejinyonga akafa, aliyepigwa kwa kitu kizito kisicho na ncha kali akafa, aliyeanguka kutoka sehemu iliyo juu, aliyepigwa kwa upembe na mnyama mwenzake na aliyeliwa na mnyama mkali.

iii) Damu inayochuruzika wakati wa kuchinja, pia damu ya wasio chinjwa inayochuruzika au isiyochuruzika chache au nyingi.

iv) Nyama ya nguruwe pia viungo yake vingine kama vile damu, shahamu na vinginevyo.

v) Kilichochinja juu ya kinachoabudiwa badala ya asiyekuwa Allah kama vile makaburi na vibandu katika vinavyoabudiwa kinyume cha Allah miongoni mwa alama au ishara zinazoashiria kuabudiwa asiyekuwa Allah, au kinachotumiwa kufikisha kwa Mungu:

Na hoja ya hivi sita ni kauli yake Allah (*Subhanahu wa Taala*),

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أَلْمَيْتَةُ وَالْدَّمُ وَلَحْمُ الْخِنزِيرِ وَمَا أُهْلِيَ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ
وَالْمُنْخَبِقَةُ وَالْمَوْقُودَةُ وَالْمُتَرَدِّبَةُ وَالنَّطِيجَةُ وَمَا أَكَلَ السَّبُعُ إِلَّا مَا
ذَكَيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ

“Mmeharimishiwa nyamafu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama aliye chinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na aliye kufa kwa kunyongeka koo, na aliye kufa kwa kupigwa, na aliye kufa kwa kuanguka, na aliye kufa kwa kupigwa pembe, aliye liwa na mnyama, ila mkimdiriki kumchinja. Na pia ni haramu kula nyama aliye chinjiwa masanamu...” (5:3)

Kwa hiyo vilivyotajwa hapo juu vimeharamishwa kwa kitabu kitukufu.

b) Vilivyo haramishwa kwa katazo la Mtume ﷺ navyo ni:

a) Punda wanaofugwa, kwa kauli ya Jabir رضي الله عنه, “Siku ya Khaibari Mtume ﷺ

“Amekataza nyama ya punda wanaofugwa na akaruhusu farasi.”
(Bukhari na Muslim).

ii) *Al Bighal*: (Ni mnyama anayezaliwa kwa dume la farasi na jike la punda-Nyumbu) ni haramu kwa kuchukulia kiasi (kielezo) kwa punda kwa hiyo yuko katika jumla ya waliokatazwa na kauli ya Allah Mtukufu:

وَالْخَيْلِ وَالْبِغَالِ وَالْحَمِيرِ لَتَرَكَبُوهَا

“Na farasi, na nyumbu, na punda ili muwapande...” (16: 8).

Kwa hiyo ni dalili inayothibitisha uharamu wa kumla mnyama huyo. Kama pataulizwa vipi alihalalishwa farasi? (Punda tu ndiye aliyekuwa haramu na farasi akawa halali) wakati dalili yenyewe ni moja? Jibu: Farasi ametoka kwa dalili nyingine nayo ni ruhusa ya Mtume ﷺ ya kumla farasi kama ilivyokuja katika hadithi ya Jabir iliyotangulia.

iii) Kila mnyama mkali aliye na meno ya chongole kama vile simba, chui, dubu, mbwa, chui, tembo, mbwa mwitu na pia komba, kingenge. (ni mnyama anaefanana na panya, adui mkubwa wa kuku), mbweha, kiende (ni mnyama mkubwa kuliko paka, ana mkia mrefu ana manyoya mengi na hupenda kuinua juu mkia wake) na wengine miongoni mwa wanyama walio na meno ya chongole anashambulia kwa meno hayo na mwenye kucha katika ndege kama vile kipanga, mwewe, kipanga

mkubwa (ndege jamii ya kipanga mwenye kucha zenye nguvu ana manyoya ya miguu ana mdomo mfupi na macho makali kwa kuona). *Shahni, Hida-a* (ni ndege anayebeba panya, kuku na vyakula vinginevyo), na bundi na wasiokuwa hao katika ndege anayewinda kwa kucha. Kwa kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنه,

“Mtume ﷺ amekataza kumla kila mnyama mweye meno ya chongole na ndege mwenye makucha.” (Imepokewa na Tirmidhi, Ahmad na Hakim).

iv) *Al-Jallalah*, ni mnyama anayekula najisi na mara nyingi anakuwa ni katika ngamia, ngo’ombe, mbuzi na kondoo na mfano wa hao ni kuku, kwa hadithi aliyoipokea Abu Dawud kutoka kwa Ibn ‘Umar kuwa Mtume ﷺ amekataza kunywa maziwa ya wanyama wanaokula najisi, pia kula nyama yao, haliwi mpaka azuiwe kula najisi kwa masiku kadhaa, nyama yake itakuwa nzuri na hayanywewi maziwa yake isipokuwa baada ya kumtenganisha na najisi kwa masiku maziwa yake yatakuwa mazuri.

c) Kinachoharamishwa kwa dalili ya kuzuia madhara nacho ni kifuatacho:

- i) Sumu ya aina yoyote kwa sababu ya madhara yaliyothibitika katika miili.
- ii) Mchanga, udongo, mawe na mkaa, kwa madhara yake na kutokuwa na faida.
- iii) Uchafu ambao nafsi huuchukia na kuikataa kama vile wadudu na vinginevyo kwa sababu uchafu unasababisha maradhi, na kuletea mwili matatizo.

d) Vilivyoharamishwa kwa ajili ya kujiepusha na najisi, navyo ni vifuatavo:

- i) Kila chakula au kinywaji kilichochanganyika na najisi, kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Kuhusu panya anayeangukia katika samli ikiwa imeganda mtupeni na kinachomzunguka, na kilichosalia kuleni, na ikiwa imeyayuka msiikaribie.” (Abu Dawud).

- ii) Kila kilichokuwa najisi kwa umbile lake kama vile kinyesi cha mwanadamu na wanyama, kwa kauli yake Allah Mtukufu:

وَكَمْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا فَجَاءَهَا بَأْسُنَا بَيِّنًا أَوْ هُمْ قَائِلُونَ ﴿٧﴾

“Na anawaharamishia uchafu.” (7:4).

4) Kinachoruhusiwa kwa mwenye dharura miongoni mwa vilivyoharamishwa:

Inahalalishwa kwa mwenye dharura –Mwenye njaa kali ikiwa kwa njaa hiyo anahofia kupoteza nafsi yake, kula miongoni mwa vilivyoharamishwa kisichokuwa sumu, kile kitakachobakisha uhai wake, ni sawa kiwe chakula cha mtu au mzoga, au nyama ya nguruwe au vinginevyo, kisha anachokula kisizidi kiwango cha kuhifadhi uhai wake, usipotee, na tendo hilo alichukie asione anafaidi. Kwa kauli ya Allah:

فَمَنْ أَضْطَرُّ فِي مَخْصَصَةٍ غَيْرِ مُتَجَانِفٍ لِإِثْمِهِ

“...Na mwenye kushurutishwa na njaa, bila ya kupendelea dhambi...” (5: 3).

Kinywaji:

1) Maana yake:

Kinachokusudiwa kwa neno kinywaji ni kila kinachonywewa katika aina ya vitu vinavyomiminika.

2) Hukumu yake:

a) Asili katika vinywewa ni kama asili ya vinavyoliwa nayo ni halali kwa kauli ya Allah Mtukufu:

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا

“Yeye ndiye aliye kuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi...” (2: 29)

Isipokuwa kile kilichotolewa na dalili, baadhi ya hivyo ni:

i) Pombe, kwa kauli ya Allah Mtukufu.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ
عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَأَجْتَنِبُوهُ

“Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shet’ani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa...” (5: 90)

Na kauli ya Mtume ﷺ :

“Allah ameilaani pombe na mywaji wake, mnyweshaji wake, muuzaji wake, mnunuzi wake, mkamuwaji wake, mkamuliwaji wake, mbebaji wake, mbebewa wake, na mla thamani yake.”
(Abu Dawud na Ahmad).

ii) Kila kinacholeweshwa katika aina ya vimiminika ni pombe kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Kila kinacholeweshwa ni pombe na kila pombe ni haramu.” (Muslim).

iii) Juisi mchanganyiko wa maji ya tende changa na tende mbivu au maji ya zabibu na tende mbovu katika chombo kimoja na yakatiwa maji katika kikamchanganyiko huo, mpaka kinakuwa kinywaji kitamu. Ni sawa mchanganyiko huo unaleweshwa au la. Kwa sababu Mtume ﷺ amekataza kufanya hivyo kwa kauli yake:

“Msiroweke tende changa na tende zilizoiva pamoja na msiroweke tende changa na mbichi na zabibu kwa pamoja lakini rowekeni kila moja mahali pake.” (Bukhari na Muslim).

Na alikataza kwa sababu mchanganyiko hauchelewi kuingia ulevi. Ili kufunga njia ya kufikia huko akakataza.

- iv) Mikojo ya wanyama haramu kuliwa, kwa sababu ya unajisi wake, ni najisi na ni haramu.
- v) Maziwa ya mnyama asiyeliwa ni haramu isipokuwa maziwa ya mwanadamu.
- vi) Kilichothibitika madhara yake mwilini, kama vile gesi na vinavyofanana nayo.
- vii) Na aina zote za vinavyovutwa kama vile tumbaku, bangi, na shisha, kwani baadhi yake vina madhara mwilini na vingine vina uraibu na vingine vina harufu mbaya, inayomkera anayekaa na mvutaji wake awe mwanadamu au malaika, na kinachokuwa hivyo kisheria ni haramu.
- viii) Kinachoruhusiwa katika hiyo kwa mwenye dharura, inaruhusiwa kwa mtu aliyekwama na tonge kooni kukikwamua kilicho mkwama kwa pombe maana hakupata kitu ingine ili kuokoa nafsi isiangamie, kama inavyoruhusiwa kwa mwenye kiu kali ambayo anahofia kufa kunywa kitakachoondoa kiu yake katika vinywaji vilivyo haramishwa, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

إِلَّا مَا أَضْطُرَّرْتُمْ إِلَيْهِ

“...isipo kuwa vile mnavyo lazimishwa?...” (6:119),



Jinai na Hukumu zake

Mada ya kwanza

Jinai ya Nafsi

1) Maana yake:

Jinai ya nafsi ni uadui kwa mwanaadamu kwa kutoa roho yake, au kuharibu baadhi ya viungo vyake, au kumsababishia jeraha mwilini mwake.

1) Hukumu yake:

Ni haramu kutoa roho ya mwanadamu bila haki au kuharibu kiungo miongoni mwa viungo vyake, au kusababisha madhara yoyote mwilini mwake. Hakuna kosa kubwa mno baada ya ukafiri zaidi ya kumuua Muislamu. Kwa kauli ya Allah:

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُتَعَمِّدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ

وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا ﴿٩٣﴾

“Na mwenye kumuua Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu humo atadumu, na Mwenyezi Mungu amemkasirikia, na amemlaani, na amemuandalia adhabu kubwa.” (4:93).

Na kauli yake ﷻ,

“Kosa la kwanza kuhukumiwa siku ya kiyama litahusu damu”
(Imepokewa na Bukhari, Nasai, Ibn Majah na Hakim)

“Muislamu ataendelea kuwa na nafasi katika dini yake madamu hajamwaga damu iliyokua haramu kuimwaga.” (Ahmad na Hakim).

2) Aina za jinai za nafsi ni tatu, nazo ni:

a) Makusudi:

Maana yake mfanya kosa kukusudia kumuua muumini au kumdhuru kwa chuma au fimbo au jiwe au akamsukuma kutaka kumyonga mahala pa juu mno, au akamzamisha ndani ya maji, au kumchoma moto au kumlisha sumu au kumsababishia uharibifu wa viungo vyake au jeraha katika mwili wake. Hukumu ya jinai hizi zakukusudia ni mtu kulipa kisasi, kwa kauli ya Allah (*Subhanahu wa Taala*):

وَكُتِبْنَا عَلَيْهِمْ فِيهَا أَنْ النَّفْسَ بِالنَّفْسِ وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ وَالْأَنْفَ بِالْأَنْفِ
وَالْأُذُنَ بِالْأُذُنِ وَالسِّنَّ بِالسِّنِّ وَالْجُرُوحَ قِصَاصًا

“Na humo tuliwaandikia ya kwamba roho kwa roho, na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na jino kwa jino, na kwa majaraha kisasi. Lakini atakaye samehe basi itakuwa ni kafara kwake. Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu..” (5:45).

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Aliyeuliwa Ndugu yake ana khiyari kufanya moja kati ya haya mawili, ima atadai fidia au kisasi.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim na Tirmidhi).

Na kauli ya Mtume ﷺ :

“Mwenye kuuliwa na wake au kujeruhiwa ana khiyari kufanya moja ya matatu: Ima kisasi au diya (fidiya) au asamehe, kwa malaika la nne mzuieni.” (Imepokewa na Ahmad, Abu Dawud na Ibn Majah).

b) Mfano wa Makusudi

Nao nikifanya kosa amekusudia jinai chini ya kuua, au kujeruhi kama vile alimpiga kwa fimbo nyepesi kwa kawaida haiui au kumpiga ngumi kwa mkono wake, au

Minhajil Muslim

akampiga kwa kichwa, au kumtupa katika maji machache au kumpigia kelele usoni mwake au kumtisha na akafa kwa hilo.

Hukumu ya jinai ya aina hii ni diya-fidia itakayotolewa kwa mchango wa ndugu wa muuaji na muuaji mwenyewe atoe kafara, kwa kauli ya Allah:

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُتَعَمِّدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ
وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا ﴿٩٣﴾

“Na mwenye kumuwa Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu humo atadumu, na Mwenyezi Mungu amemkasirikia, na amemlaani, na amemuandalia adhabu kubwa.” (4:93).

c) Kosa (Bahati Mbaya)

Kama vile Muislamu kufanya analoruhusiwa kufanya kisheria kama vile kulenga shabaha au kuwinda au kwa mfano anakata nyama ya mnyama silaha ikapea ikampata mtu akafa kwa silaha hiyo au kumjeruhi. Na hukumu ya aina hii ya jinai ni: kama hukumu ya aina ya pili, isipokuwa diya-(fidia) katika aina hii inakuwa nyepesi na mwenye kufanya kosa hili hana dhambi tofauti na ile aina ya pili kwani aina ile diya inakuwa nzito na mfanya kosa hilo ana dhambi.



Mada ya Pili

Hukumu za Jinai

1) Sharti za kuwajibika kisasi:

Kisasi hakiwajibiki katika kuua au katika viungo au majeraha isipokuwa kwa sharti zifuatazo:

a) Mwenye kuuliwa damu yake iwe haramu kumwagwa, ama akiwa mzinifu *muhsan*-au mtu ameritadi kuacha dini ya Kiislamu au kafiri akiuawa hakuna kisasi, kwa sababu hawa damu zao ni halali kumwagwa kwa mujibu wa sheria, kwa makosa waliyofanya.

b) Muuaji awe baleghe na mwenye akili timamu kama atakuwa chini ya baleghe mwendawazimu hakuna kisasi Kwa kukosekana majukumu kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Imenyanyuliwa kalamu- haiandiki dhambi –kwa watatu, mtoto mpaka anabaleghe, mwendawazimu mpaka apate akili, aliyelala mpaka aamke.”

c) Muuaji aliungana hadhi na mwenye kuuliwa katika dini, uungwana, na utumwa kwa sababu hauliwi Muislamu kwa kuua kafiri, wala muungwana kwa kuua mtumwa, kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Hauliwi Muislamu kwa kumuua kafiri.” (Ahmad na Tirmidhi).

Kwa sababu mtumwa anathaminiwa kwa hiyo atathaminiwa kwa thamani yake na kwa kauli ya ‘Ali رضي الله عنه,

“Katika sunna muungwana hauliwi kwa kuua mtumwa.”

Na katika hadithi ya Ibn ‘Abbas رضي الله عنه

“Mtu muungwana hauliwi kwa kumuua mtumwa.” (al Baihaq na Daraqutn).

d) Muuaji asiwe baba wa mwenye kuuwawa au mama, babu au bibi kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Mzazi hauliwi kwa kumuua mtoto.” (Ahmad na Tirmidhi).

2) Masharti ya Kutekeleza Kisasi:

Mwenye kisasi hawezi kukitekeleza ila baada ya kukamilika sharti zifuatazo:

a) Mwenye haki ya kisasi awe Baleghe na mwenye akili timamu, kama atakuwa hajabalegh au mwendawazimu atazuiliwa kufanya jambo hilo mpaka mtoto ana baleghe, au mwendawazimu kupata akili, kisha wana haki kutekeleza kisasi au watachukua diya-fidia au kusamehe na haya yamepokewa kutoka kwa maswahaba رضي الله عنه.

b) Ndugu wa marehemu wakubaliane juu ya kisasi, kama baadhi yao watasamehe basi hakuna kisasi, yule asiyesamehe atapata hisa yake katika diya.

c) Kuwe na usalama wakati wakutekeleza kisasi wa kuzidisha zaidi yaalivyofanya mhukumiwa, kama ni jeraha basi lisiwe zaidi ya lile na asiuliwe asiyeua, na asiuliwe mwanamke mjamzito mpaka ajifugue na mtoto wake aache ziwa, kwa kauli ya Mtume ﷺ kuhusu mwanamke aliyeya kwa makusudi;

“Hakuuliwa mpaka anazaa kilicho tumboni mwake kama mjamzito na mpaka anamlea mtoto wake.” (Ibn Majah).

d) Utekelezaji wa kisasi ufanywe kwa kuwepo mtawala (sultan) au naibu wake ili ipatikane hali ya usalama.

e) Iwe kwa silaha kali, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Hakuna kisasi ila kwa upanga.” (Ibn Majah).

3) Khiyari (kufanya uchaguzi) kati ya kisasi, Diya na kusamehe:

Ikithibitika kwa Muislamu haki ya kisasi atapewa hiari (atakuwa na chaguo) kati ya mambo haya matatu: Atekeleze kisasi, au achukue-fidia, au asamehe, kwa kauli ya Allah,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلِ ۗ أَحْرَ بِأَحْرٍ وَالْعَبْدُ
بِالْعَبْدِ وَالْأُنْثَىٰ بِالْأُنْثَىٰ ۗ فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ شَيْءٌ فَاتَّبِعْ بِالْمَعْرُوفِ
وَأَدِّ إِلَيْهِ بِإِحْسَنٍ ۗ

“Na anaye samehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema, na yeye alipe kwa ihsani. Huko ni kupunguziwa kuliko tokana na Mola wenu Mlezi, na ni rehema. Na atakaye vuka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu chungu.” (2:178).

Na kauli yake Allah:

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۗ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّهُ لَا
يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾

“Na malipo ya uovu ni uovu mfano wa huo. Lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye hawapendi wenye kudhulumu.” (42:40).

Na kauli yake Allah: :

“Mwenye kuuawa ndugu yake ana hiyari kufanya moja ya mawili ima apokee diya au atekeleze kisasi.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake ﷺ:

“Hatosamehe mja dhuluma yoyote isipokuwa Allah atamuongezea utukufu kwa msamaha huo.” (Ahmad).

Tanbihi:

a) Aliyekhiyari diya haki yake katika kisasi imeanguka, na kama ataitaka tena hapewi na kama ataichukua kwa nguvu akaua atauliwa, ama kama atateua kisasi anaweza kuacha kisasi na kuchukua diya.

b) Kama atakufa muuaji kabla ya kisasi kitachobakia ndugu wa aliyeuliwa ni diya tu kwa vile kisasi hakitawezekana kwa kufa muhusika, kwa sababu hairuhusiwi kumua asiyewa kwa vyovyote vile. Kwa kauli ya Allah:

وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لَوْلِيَّهِ سُلْطٰنًا فَلَا يُسْرِفُ فِي الْقَتْلِ ۗ
إِنَّهُ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣٣﴾

“...Na aliye uliwa kwa kudhulumiwa basi tumempa madaraka mrithi wake. Lakini asipite mpaka katika kuuwa. Kwani yeye anasaidiwa...” (17:33).

Kuzidisha katika kuua kumetafsiriwa kuwa ni kumuua asiyewa.

c) Kafara ya kuua ni wajibu juu ya kila aliyeua kwa bahati mbaya au kwa mfano wa makusudi, ni sawa aliyeuliwa awe ni mimba au mzee, muungwana au mtumwa, na kafara lake ni kuacha huru mtumwa muumini-Muislamu asipompata afunge miezi miwili mfululizo kwa kauli ya Allah Mtukufu:

فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ وَدِيَةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهَا إِلَّا أَنْ يَصَّدَّقُوا فَإِنْ كَانَ مِنْ قَوْمٍ
عَدُوٍّ لَكُمْ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ وَإِنْ كَانَ مِنْ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ
وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ فَدِيَةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهَا وَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ ۗ فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامٌ
شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ تَوْبَةً مِّنَ اللَّهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٣٤﴾

“...basi amkomboe mtumwa aliye Muumini, na atoe diya kuwapa jamaa za maiti, isipo kuwa waache wenyewe kuwa ni sadaka. Na akiwa ni jamaa wa maadui zenu, hali yeye ni Muumini, basi ni kumkomboa mtumwa aliye Muumini. Na akiwa ni miongoni wa watu ambao pana ahadi baina yenu na wao basi wapewe diya watu wake na akombolewe mtumwa Muumini. Na asiye pata, basi afunge miezi miwili mfululizo, kuwa ni toba kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima...” (4: 92).



Mada ya Tatu

Jinai ya viungo

1) Maana yake:

Jinai ya viungo maana yake ni mtu kumfanyia mwingine uadui kumdhuru jicho lake au mguu au mkono wake.

2) Hukumu yake:

Kama mfanya jinai amekusudia, na hakuwa baba wa muathirika, na muathirika anawiana na mtenda kosa katika Uislamu na uungwana basi atachukuliwa kisasi cha muathirika, kwa kukata alichokikata, na atajeruhiwa kama alivyojeruhi kwa kauli ya Allah mtukufu:

“...Na majeraha yana kisasi.”

Isipokuwa kama muathirika atakubali diya au msamaha

3). Masharti ya kisasi cha viungo:

Katika kutekeleza kisasi cha viungo kuna sharti zifuatazo:

- a) Kuwe kuna uhakika dhuluma haitendeki, kama kutakuwa na dhulma hakuna kisasi.
- b) Iwe hicho kisasi kinawezekana na kama hakiwezekani basi kitaachwa na kuchukuliwa diya.
- c) Kiungo kinachotakiwa; kukatwa kilingane na kilichokatwa katika jina na mahali, hakitakatwa kiungo cha kuliani kwa cha kushotoni wala haukatwi mkono kwa mguu, wala kidole cha asili kwa kidole cha ziada.
- d) Usawa wa viungo viwili: Maana yake kilichoharibiwa na kinachotakiwa kukatwa vilingane katika uzima na ukamilifu hautakatwa mkono uliopooza kwa mzima wala jicho lenye chongo kwa jicho zima.

e) Kama jeraha liko kichwani au usoni-mpasuko-*Shajjah*—halina kisasi isipokuwa kama halikufika kwenye mfupa na kila jeraha lisilowezezana kulitekeleza kwa hatari yake haina kisasi, kwa hiyo hakuna kisasi katika kuvunja mfupa wala katika jeraha lililofika ndani ya tumbo, bali kinacholazimika kutolewa katika tuliyoyataja ni diya (fidia).

Tanbihi:

1. Kitauwawa kikundi kwa kuua mtu mmoja, na vitakatwa viungo vya wengi kwa kukata kiungo cha mtu mmoja kama watashirikiana kwa pamoja watu hao katika jinai kwa kauli ya ‘Umar رضي الله عنه:

“Kama walishirikiana watu wa Sanaa (Yemen) kuua ningaliwaua wote kwa ushirika huo.” (Imam Malik katika Al-Muwaat)

Hayo ‘Umar رضي الله عنه aliyasema baada ya kuwaua watu saba waliomuua mtu mmoja katika watu wa sanaa.

2. Kudumu kwa kosa la jinai litadhaminiwa: Mtu kama amemfanyia kosa la jinai mwingine kwa kumkata kidole chake kisha jeraha halikupona mpaka mkono wote ukapooza, au akafa basi kitatekeleza kisasi au kutolewa diya kulingana na hali ilivyo.

Ama maendeleo ya kisasi hakuna dhamana kama mtu alikata mkono wa mwingine akahukumiwa kisasi akakatwa mkono wake na akafa kwa jeraha hilo la kisasi, huyo hana atachopata isipokuwa kama itafanyika dhuluma wakati wa kukeleza kisasi, kwa mfano silaha haikuwa kali au ilikuwa na sumu katika sura hii kudumu huku kutadhaminiwa.

3. Kisasi cha jeraha hakitatekelezwa kabla ya kupona jeraha hilo kwa katazo la Mtume ﷺ kutekeleza kisasi cha jeraha kabla ya kupona jeraha, kwa sababu hakuna dhamana ya kutoendelea jeraha kwenye viungo vingine vya mwili wa mtu huyo navyo vikaharibika, kwa hiyo mtu kama atalazimisha kisasi kabla hajapona, kisha jeraha likaendelea hatimaye jeraha likaathiri kiungo kingine hana malipo kwa vile amekwenda kinyume na katazo la Mtume ﷺ la kukataza kisasi kabla ya kupona jeraha.

Mada ya Nne:

Diya (Fidia):

1) Maana yake:

Diya ni mali inayotolewa kwa anayestahiki damu.

2) Hukumu yake:

Diya ni sheria, kwa kauli ya Allah Mtukufu,

وَدِيَّةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهَا إِلَّا أَنْ يَصَدَّقُوا

“...na atoe diya kuwapa jamaa za maiti, isipo kuwa waache wenyewe kuwa ni sadaka...” (4: 92)

Na kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Mwenye kuuawa ndugu yake ana khiyari kufanya moja ya mawili ima apewe diya au apewe kisasi.”

3) Diya inawajibika juu ya nani?

Inawajibika juu ya kila aliyewa mwanadamu moja kwa moja au kwa kusababisha kifo. Kama amemuua kwa makusudi basi diya itachukuliwa kutoka kwenye mali yake muuaji, na kama mauaji yanafanana na makusudi au kwa makosa basi diya itatolewa na ndugu wa muuaji, kwa hukumu ya Mtume ﷺ:

“Walipigana wanawake wawili mmoja akamrushia mwengine jiwe akamuua yeye na mtoto aliye tumboni mwake Mtume ﷺ akahukumu diya ya mama yule juu ya ndugu wa muuaji.” (Ibn Majah)

Na ‘akila’ hapa ni kundi la watatoa diya.

Ndugu wanaokusudiwa hapa ni wale aswaba wa mtuihumiwa kama vile baba zake, ndugu zake, watoto wa ndugu zake na watoto wa ami zake diya itagawanywa

juu yao kulingana na hali yao ya kiuchumi kwa muda wa miaka mitatu kila mwaka watatoa thuluthi ya diya mpaka ikamilike na kama wataweza kuitoa mara moja hakuna pingamizi.

4) Nani itamuanguka Diya

Itaanguka diya kwa baba aliyemuadhibu mwanawe akafa, au kiongozi wa nchi aliyempa adabu raia wake akafa, au mwalimu aliyempa adabu mwanafunzi wake akafa, na kuanguka huku ikiwa hiyo adhabu haikukiuka kiwango cha adhabu ya kawaida kwa kosa kama hilo.

5) Viwango vya Diya:

a) ‘Diya ya Nafsi’:

Kama mtolewa diya ni muungwana Muislamu diya yake ni ngamia mia moja, au (*mithkala*) alfu moja za dhahabu au dirhamu kumi na mbili alfu za fedha, au ng’ombe mia mbili, au mbuzi alfu mbili, na ikiwa ni kwa bahati mbaya haitiwi uzito (diya) kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Elewa aliyeuawa kwa bahati mbaya ya makusudi kwa kiboko, fimbo, na jiwe kuna diya nzito, ngamia mia moja kati ya hao arobaini wenye umri wa miaka tisa na wote wana mimba.”
(Imepokewa na Ahmad, Nasai na Daraqtuni)

Ikiwa uuaji ni wa makusudi basi itakuwa kulingana na matakwa ya wenye ndugu, kwa sababu wana haki ya kutaka zaidi ya diya kwa sababu wanamiliki kisasi kwa hiyo wanaweza wakataka zaidi ya diya. Dalili ya makadirio ya Diya yaliyotajwa (hapo nyuma) ni kauli ya Jabir رضي الله عنه:

“Mtume ﷺ amewajibisha juu ya wenye ngamia, ngamia mia moja na wenye ng’ombe, ng’ombe mia mbilia wenye mbuzi, mbuzi elfu mbili.” (Abu Dawud kwa sanadi dhaifu isipokuwa matendo ya Jamhuri yako pamoja na Hadith).

Na kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنه

“Mtu mmoja aliuawa na Mtume ﷺ akasema kuwa diya yake ni Dirham alfu kumi na mili.” (Imepokewa na Abu Dawud, Nasai, Ibn Majah na Tirmidh).

Pia barua aliyopelekewa ‘Amru Ibn Hazmi ambayo umma wa Kiislamu wameipokea wote kwa kukubali:

“Na wenye dhababu dinari alfu moja.” (Darimi na al-Baihaqi).

Lolote katika matano yaliyotajwa kama atayatekeleza italazimu ndugu wa marehemu kukubali. Kama anayetolewa diya ni mwanamke Muislamu muungwana basi diya yake ni nusu ya diya ya mwanamume Muislamu kufuatia Hadithi aliyopokea Malik katika Muwatta kutoka kwa Urwaah Ibn Zubair. Ilikuwa inasemwa: Mwanamke anamlipa diya mwanamume kama itafikia thuluthi ya diya ya Mwanamume basi mwanamke atatolewa nusu ya diya ya mwanamume.

Na ikiwa anayetolewa diya ni (*Dhimmiyyu*) Yahudi au Mnaswara au mwingine basi diya yake ni nusu ya diya ya Muislamu na diya ya wake zao ni nusu ya diya ya wanaume zao. Kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Diya ya kafiri ni nusu ya diya ya mwanamume.” (Tirmidhi).

Na akiwa anayetolewa diya ni mtumwa basi diya yake ni thamani yake iwe itakavyokuwa kwa sababu mtumwa ni kitu na kilichothaminiwa kwa hiyo kitachotolewa ni thamani yake. Na kama anayetolewa diya ni mimba awe mwanamume au mwanamke basi diya yake ni mtumwa mwanamume au mwanamke, kwa hukumu ya Mtume ﷺ kwa mimba. Mtumwa mwanamume au mwanamke, kama ilivyokuja katika Swahili, kama ni muungwana na akatoka tumboni hali amekufa ama kama atatoka tumboni mwa mama yake akiwa hai kisha akafa baada ya kuzaliwa basi kitathibitika kisasi au diya kamili.

Tanbihi:

Baadhi ya wanazuoni wamethaminisha diya ya mimba kwa moja ya kumi 1/10 ya diya ya mama yake, kwa hiyo Imam Malik ameithaminisha kwa Dinari Khamsini au Dirham mia sita.

b) Diya ya Viungo:

Itawajibika diya kamili katika viungo vifuatavyo:

i) Jinai iliyoondoa akili

ii) Jinai iliyoondoa kusikia kwa kumtoa masikio.

iii) Jinai iliyoondoa sauti kwa kukata ulimi au midomo.

iv) Jinai iliyopoteza uwezo wa kunusa harufu kwa kuikata pua yote.

v) Jinai iliyoondoa uwezo wa kuona kwa kuharibu macho mawili.

vi) Jinai iliyoondoa uwezo wa kuingilia kwa kukata dhakari au kuponda ponda hasuwa.

vii) Jinai iliyoondoa uwezo wa kusimama au kukaa kwa kuvunja mgongo.

Kwa dalili iliyokuja katika barua ya Amri Ibn Hazmi aliyoiandika Mtume ﷺ kwamba:

“Pua ikikatwa yote ni diya kamili. Ulimi diya kamili, midomo miwili diya kamili, mayai mawili diya kamili, dhakari diya kamili, mgongo diya kamili na macho mawili diya kamili.” (Imepokewa na Darimi, Daraqutni na al Baihaq)

Hukumu ya ‘Umar رضي الله عنه kwa mtu aliyempiga mwingine pigo lililompotezea uwezo wa kuona, kusikia, kuelewa na kuingilia kwa kutoa diya nne, na yule mtu hakufa.

Diya ya mwanamke ya viungo ni nusu ya diya ya mwanamume. Ama diya ya majeraha kama itafikia thamani yake thuluthi ya diya ya mwanamume basi itakuwa nusu ya diya ya mwanamume, na kamai takuwa chini ya thuluthi basi haina tofuati na mwanamume.

c) Inawajibika nusu Diya katika viungo vifuatavyo:

- i) Jicho mojawapo kati ya mawili.
- ii) Sikio moja kati ya mawili
- iii) Mkono mmoja.
- iv) Mguu mmoja.
- v) Mdomo mmoja
- vi) Tako moja.
- vii) Kope moja (Mfuniko wa jicho)
- viii) Ziwa mojawapo la mwanamke

Tanbihi:

Kwa kukata kidole kimoja diya yake ni ngamia kumi, kwa kauli ya Mtume ﷺ. Diya ya vidole vya mikono miwili au miguu miwili ni sawa na ngamia kumi kwa kila kidole: (Tirmidhi). Diya ya jino moja ni ngamia watano, kwa kauli ya Mtume ﷺ katika barua aliyomtumia Amri Ibn Hazmi:

“Na katika jino ngamia watano”

Diya ya Shijaji na Jeraha:

1 *Shijaji* (Kujeruhi kichwa au uso).

a) Maana yake:

Shijaji ni jeraha la kichwani au usoni, na majeraha yaliyo maarufu ya kichwa na uso kwa wanazuoni wa kale ni kumi, matano hukumu yake ufafanuzi umekuja wake kutoka kwa muweka sheria, na matano hakuna ufafanuzi wa adhabu yake maalum kutoka kwa muweka sheria kuhusu diya yake

b) Hukumu yake:

Hukumu ya majeraha matano nayo ni:

i) **Katika muwadhwiha:** (Ni jeraha linalouonesha mfupa na kuudhihirisha), na diya yake ni ngamia watano. Kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Katika Muwadhwiha ngamia watano.” (Imepokewa na Abu Dawud, Tirmidhi na An-Nasai).

ii) **Katika al-Haashima** (ni jeraha lililovunja mfupa), diya yake ni ngamia kumi. Kwa kauli ya Zaid Ibn Thabit رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ,

“Amewajibisha katika Al-Hashima ngamia kumi.” (al Baihaq na Daruqutny).

iii) **Katika al-Munaqqila:** (Hii ni jeraha lenye kuhamisha mfupa kutoka mahala pake), ni ngamia kumi na tano, kwa maelezo yaliyokuja katika barua ya Amr Ibn Hazm:

“Na katika Al-Munaqqillah ni ngamia kumi na tano” (Darimy).

iv) **Katika Al-Ma-amuma,** (Ni jeraha lililofika kwenye ngozi nyembamba inayofunika ubongo) ni thuluthi ya diya, kama ilivyo katika barua ya Amri Ibn Hazm:

“Katika Mamuma thuluthi ya diya.” (Darimy).

v) **Damigha:** (na hilo ni jeraha linalotoboa ngozi nyembamba inayofunika ubongo), na jeraha hilo ni kubwa kuliko Maamuma na hukumu yake ni ile ile ya Maamuma thuluthi ya diya. Ama yale matano ambayo ufafanuzi wa diya yake haujaja ni kutoka kwa muweka sheria ni:

i) **Al-Haariswah:** (jeraha lililo kwaruza ngozi kidogo bila ya kuichana na kutoa damu).

ii) **Daamiya:** jeraha linalochana ngozi na kutoa damu.

iii) **Al Baadhwia:** jeraha linalochana nyama.

iv) **Al-Mutalaahima:** Hili ni kubwa kuliko *Al Baadhwia*, kwa sababu hili linazama mno katika nyama.

v) **As-Simhaaq:** jeraha hakuna kilichosalia kufika kwenye mfupa isipokuwa ngozi nyembamba.

Hukumu ya majeraha haya matano kwa wanazuoni ni kuwa serikali itaangalia na kuona mwenye majeraha anakadiriwa kuwa ni mtumwa kisha anathaminiwa akiwa hana jeraha, halafu anathaminiwa akiwa majeruhi na baada ya kupona jeraha, na ile tofuati iliyo kati ya tathmini mbili, akiwa mzima na baada ya kupona majeraha kile kilochozidi akiwa mzima ndicho kitachokuwa *diya* yake. Kama ni sudusi basi atapewa sudusi ya *diya* yake, na akiwa ushuru (Moja ya kumi) basi atapewa ushuru ya diya yake, na hivi hivi katika majeraha yote hayo matano. Kilichokuwa rahisi kuliko yote haya, (na hasa kwa wakati tulionao), ni kufanya jeraha *al-Muwadhwiha* ndicho kigezo kwa vile ni jeraha linalouonesha mfupa bila ya kuuvunja, na diya yake ni ngamia watano. Kwa hiyo majeraha matano yatakisiwa (kigezo) kwa *al-Muwadhwiha* kilekitachokuwa kama humsi yake –moja ya tano $1.5 =$ basi kitakuwa ndio diya yake nayo ni ngamia mmoja na jeraha likiwa kubwa kama thuluthi yake basi itakuwa diya yake ni ngamia watatu. Na kigezo kitachukuliwa na daktari bingwa kama ilivyo majeraha mengine katika sehemu zingine za mwili.

1. Jeraha

a) Maana yake:

Jeraha ni lile lisilo kuwa kichwani na usoni katika sehemu zingine za mwili.

b) Hukumu yake:

Katika *al-Jaifa*: (Ni jeraha linalofika ndani ya mwili) – ni thuluthi ya diya kwa yaliyo katika barua ya ‘Amri Ibn Hazmi رضى الله عنه na:

“Katika Jaifa ni thuluthi ya diya.”

i) Na katika ubavu kama utavunjika na ukaungika ni ngamia mmoja.

ii) Katika kuvunja mfupa wa dhira au mfupa wa ugoko au kiwiko kama kitaungika ni ngamia wawili, kwani masahaba wamehukumu hivyo رضى الله عنه.

iii) Majeraha mengine yasiyotajwa hapa ni hukumu au yatachukuliwa kigezo kwa jeraha *muwadhiha* na kufanya hivyo ni rahisi zaidi.

c) Namna ya Kuithibitisha Jinai:

Kama jinai itakuwa chini ya nafsi – kuua itathibiti kwa moja ya mambo mawili. Ima kwa kukiri (kukubali mfanya kosa mwenyewe) au kwa ushahidi wa waadilifu wawili. Kama jinai ni ya kuua, basi litathibiti ima kwa kukiri muuaji mwenyewe, au ushahidi wa waadilifu wawili au kwa **Kasaama**, kama kutakuwa na uishahidi wa mazingira kama vile uadui wa wazi kati ya aliyeuliwa na wanaotuhumiwa. **Kasaama**: Maana yake kupatikana mtu aliyeuawa, ndugu wa marehemu wakadai kuwa mtu au watu fulani ndio waliomuua kutokana na uhasama unaofahamika kati ya wa muda mrefu, kwa hiyo dhana kubwa ikawahusisha na tukio kuwa aliyeuawa ameuliwa na yeye au wao kwasababu hizo. Au hakuna uadui kati ya aliyeuliwa na wanaotuhumiwa, bali ameshuhudia mtu mmoja tu, kwa vile ushahidi wa kuthibitisha mauaji haukubaliwi ila kwa mashahidi wawili na hapa ushahidi uliotolewa ni wa mtu mmoja tu, utachukuliwa sawa na ushahidi wa mazingira, kwa hiyo italazimika **Kasaama**, watachukua kiapo ndugu wa marehemu, warithi wake wanaume tu sio wanawake, yamini khamsini itagawanywa kati yao

kulingana na haki ya kurithi kwao kwa marehemu akithibitisha kuwa huyu au hawa wamemuua kama wataapa basi watastahiki damu ya ndugu yao, kwa hiyo watapitishiwa kisasi kwa ndugu yao, kwa hiyo watapitishwa kisasi kwa ndugu yao, au watapewa diya na kama baadhi ya ndugu watapinga yamini basi haki yao itaanguka na hapo watuhumiwa watakula yamini khamsini ya kupinga na watakataa kuhusika na damu hiyo. (Jamhuri wakiwamo Abu Hanifa, Shaafii na ‘Umar Ibni ‘Abdil-‘Aziz –wamesema, “Kisasi hakithibitika kusaama bali litathibiti diya tu, isipokuwa Maliki na Ahmad, wanasema kitathibiti kisasi”).

Pia aliyetuhumiwa kama hakuna ushahidi hata wa mazingira atakuwa hana madai dhidi yake kwa kiapo kimoja tu, kama ilivyokuja katika Hadithi sahihi kuwa Mtume ﷺ alipelekewa kesi ya mauaji akataka ifanyike kasaama, akawaambia wenye ndugu aliyeuawa:

“Je mtakula kiapo na muwe na haki na muuwaji wenu? Au mtu wenu? Wakasema vipi tutachukua kiapo hali hatukuwepo wala hatukuona? Akasema basi ajitakase kwenu mayahudi (watuhumiwa) kwa kula yamini khamsini? Wakasema: Vipitakubali yamini ya watu makafiri?” (Imepokewa na Bukhari, Tirmidhi na Abu Dawud).

Mtume ﷺ akamtolea diya kutoka kwake mwenyewe.



Kinahusu Adhabu

Mada ya Kwanza

‘Adhabu ya pombe’

1) Maana ya adhabu ya Pombe

Adhabu *Hadu* ni kuzuiliwa kukifanya alichokiharamisha Allah (*Subhanahu wa Taala*) kwa kupitia kupiga au kuuawa na adhabu *Hududu*) za Allah Mtukufu ni vile alivyoviharamisha ambavyo ameamuru viepukwe (vilindwe) visisogelewe.

Pombe *Khamru*, Ni kinywaji cha aina yoyote kinacholeweshwa, kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Kila kinacholeweshwa ni pombe, na kila pombe ni haramu” (Muslim).

2) Hukumu ya kunywa pombe:

Ni haramu kuywa pombe iwe chache au nyingi, kwa kauli ya Allah Mtukufu alipokataza pombe na kamari:

فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ ﴿٩١﴾

“...Basi je, mmeacha?” (5:91).

Na kauli yake,

فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾

“...Basi jiepusheni navyo...” (5: 90).

Na kauli ya Mtume ﷺ

“Allah amemlaani mnywa pombe na muuza pombe.” (Abu Dawud na al Hakim)

Minhajil Muslim

Na Mtume ﷺ kwa kutekeleza adhabu kwa mwenye kunywa kwa kumpiga viboko mbele ya msikiti, kama ilivyo katika Bukhari na Muslim.

3). Hekima ya Kuharamisha Pombe:

Hekima ya kuharamisha pombe ni kuulinda usalama wa Dini ya Muislamu, na akili yake na mwili wake pia mali yake.

4) Hukumu ya Mwenye Kunywa Pombe:

Hukumu ya mwenye kunywa pombe na ikathibiti kweli amekunywa kwa kukiri mwenyewe au kwa ushahidi wa waadilifu wawili, aadhibiwe kwa kupigwa viboko thamanini juu ya mgongo wake kama ni muungwana na kama ni mtumwa viboko arubaini kwa kauli ya Allah Mtukufu kuhusu wajakazi,

فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ مِنَ الْعَذَابِ

“...Na wanapo olewa kisha wakafanya uchafu basi adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu waliyo wekewa waungwana...” (4:25)

Na mtumwa amechukuliwa kama mjakazi.

5) Sharti za kuwajibika adhabu kwa mwenye kunywa pombe:

Sharti la kutekelezwa adhabu kwa mwenye kunywa pombe awe Muislamu, mwenye akili timamu, baleghe anayeelewa uharamu wa pombe, awe mzima si mgonjwa, isipokuwa huyu mgonjwa haitamuangukia adhabu bali atasubiriwa mpaka apone, akipona ataadhibiwa.

6) Kutokurudia adhabu kwa mwenye kunywa pombe:

Kama litajirudia tendo la kunywa pombe mara nyingi, kisha akaadhibiwa, basi huyo itamtosha adhabu moja kwa mara zote zilizopita na kama atakunywa baada ya kuadhibiwa, atapewa adhabu nyingine, hivi hivi kila akinywa ataadhibiwa.

7) Namna ya kutekeleza adhabu kwa aliyekunywa pombe:

Inatekelezwa adhabu kwa aliyekunywa pombe kwa kukalishwa juu ya ardhi, na atapigwa mgongoni kwa kiboko kilicho na ukubwa na unene wa wastani viboko thamanini na mwanamke sawa na mwanamume, isipokuwa mwanamke atakuwa amesitiriwa kwa nguo nyepesi itakayomuhifadhi na haimlindi na kipigo.

Tanbihi:

Mnywaji pombe hapewi adhabu kipindi cha baridi kali au joto kali bali atasubiriwa mpaka kipindi cha kupoa hali ya hewa na kuwa nzuri akatiwa mchana, pia hapewi adhabu huku amelewa, wala mgonjwa bali atasubiriwa apate akili na apone.



Mada ya Pili

Adhabu ya *Qadhfi*:

1) Maana yake:

Qadhfu maana yake ni shutuma kwa zinaa, kama vile mtu kumwambia mwingine, Wewe mzinifu, au aseme yeye amemuona anazini, au anafanya ovu kadha kama vile zinaa au kulawiti.

2) Hukumu yake:

Qadhfu ni dhambi kubwa miongoni mwa madhambi makubwa na mwenye kufanya kosa hili Allah amemwita fasiki, na ameuangusha uadilifu wake yaani si muadilifu na amewajibisha juu yake adhabu kwa kauli yake.

وَالَّذِينَ يَرْمُونَ الْمُحْصَنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا بِأَرْبَعَةِ شُهَدَاءَ فَاجْلِدُوهُمْ ثَمَانِينَ
جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا لَهُمْ شَهَادَةً أَبَدًا وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٤١﴾ إِلَّا الَّذِينَ
تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٤٢﴾

“Na wanao wasingizia wanawake mahashumu, kisha wasilete mashahidi wane, basi watandikeni bakora thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena. Na hao ndio wapotovu. Isipo kuwa wale walio tubu baada ya hayo na wakatengenea; kwani bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye kurehemu.” (24:4-5)

3) Adhabu yake:

Ni viboko themanini kwa kauli ya Allah Mtukufu:

“Wapigeni mijeledi –viboko–thamanini.”

Na Mtume  ametoa adhabu ya viboko themanini kwa watu wa (ifki-wale waliomsingia Mama 'Aisha).

4) Hekima ya Adhabu ya *Qadhfu*:

Nikulinda usalama na heshima ya Muislamu na kuulinda utukufu wa mwanadamu. Pia kulinda usafi wa jamii, kutosambaa zinaa na machafu kati ya Waislamu ilhali Waislamu ni wasafi na waadilifu.

5) Sharti za Kutekeleza adhabu ya *Qadhfu*:

Ili kutekeleza adhabu ya *Qadhfu* ni lazima masharti yafuatayo yakamilike:

- a) Mtoa shutuma –*Qadhfu* –awe Muislamu, baleghe mwenye akili timamu.
- b) Mshutumiwa asifahamike kati ya watu kuwa mzinifu.
- c) Mshutumiwa atakiwe kutoa adhabu hiyo kwa mtoa shutuma, kwa sababu adhabu hiyo ni haki yake akitaka kuitumia ataitumia na akitaka kusamehe atasamehe.
- d) Mshutumu asiwalete mashahidi wanne watakaoshuhudia ukweli wa madai yake, kama litakosekana sharti moja kati ya sharti tulizozitaja haitatekelezwa adhabu hiyo.



Mada ya Tatu:

Adhabu ya Zinaa

1) Maana yake:

Zinaa ni ingilio la haramu iwe ni tundu ya mbele au ya nyuma:

2) Hukumu yake:

Zinaa ni miongoni mwa madhambi makubwa baada ya ukafiri, ushirikina na kuua. Ni miongoni mwa madhambi makubwa kabisa kabisa, ameharamisha Allah Mtukufu, kwa Kauli Yake.

وَلَا تَقْرَبُوا الزَّوْجَ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا

“Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu na njia mbaya.”
(17:32).

Na kwa mwenye kulifanya kosa hilo Amemuwekea adhabu kali kwa Kauli Yake.

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ

“Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mtandikeni kila mmoja katika wao bakora mia...” (24:2).

Amesema miongoni mwa aliyoteremsha katika Qur-aan yakafutwa matamko na kubaki hukumu yake ni, “Na Mzee mwanamume na mzee mwanamke kama wazinzi wapigeni mawe kabisa ni adhabu. Kauli ya Mtume ﷺ

“Hazini mzinifu na hali ni Muumini.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim Abu Dawud na Tirmidhi).

Na amesema, alipoulizwa kuhusu dhambi lililo kuwa mno.

“Kuzini na mke wa jirani yako.” (Bukhari).

3) Hekima ya kuharamishwa ‘Zinaa’:

Miongoni mwa hekima za kuharamishwa zinaa ni kuulinda usafi wa jamii ya Kiislamu na kulinda heshima ya Waislamu, usafi wa nafsi zao na kuendeleza heshima na utukufu wao. Pia kulinda heshima ya vizazi vyao na usafi wa roho zao.

4) Adhabu ya Zinaa:

Inatofuatiana kulingana na tofauti ya muhusika. Kama mzinifu- si *Muhswan* ni yule ambaye hajawahi kuoza ndoa kisheria wala kukaa faragha ndani ya ndoa hiyo na mkewe huyo kumingilia katika ndoa hiyo, basi huyu atapigwa viboko mia moja, na atahamishiwa kwa mwaka mmoja mbali ya mji wake, na mzinifu mwanamke si *muhswan* ni sawa na mwanamume, isipokuwa uhamisho wake kama utasababisha uharibifu hatohamishwa. Kauli ya Allah Mtukufu:

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ

“Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mtandikeni kila mmoja katika wao bakora mia...”(24:2).

Ibn ‘Umar رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ,

“Ampiga viboko na amewahamisha. Na Abu Bakar ampiga viboko na amehamisha, na ‘Umar رضي الله عنه ampiga viboko na amehamisha”. (Bukhari).

Kama ni mtumwa atapigwa viboko hamsini na hahamishwi kwa vile kuhamishwa kutapoteza haki ya mwenye mtumwa kama vile kumuhudumia. Na mzinifu akiwa *Muhswan* mwanamume au mwanamke atapigwa kwa mawe mpaka, kufuatana na aya iliyokua inasomwa ikafutwa afe na kubaki hukumu,

“Mzee mwanamume na mzee mwanamke kama watazini wapigeni mawe ni adhabu kutoka kwa Allah na Allah ni Mshindi Mwenye Hekima”

“Na kwa amri ya Mtume ﷺ ya kupiga mawe, na ameitekeleza kwani amempiga mawe Alghaamidiyyah na Maaiiz رضي الله عنه; na amewapiga mawe mayahudi wawili Allah awalaani” (Imepokewa na Muslim, Ahmad na al Hakim).

5) Sharti la kutekeleza adhabu za zinaa:

Ili kutekeleza adhabu ya zinaa kwa wazunifu kuna masharti yafuatazo:

a) Mzunifu awe Muislamu baleghe mwenye akili timamu, na amefanya zinaa kwa hiari yake hakulazimishwa, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Imenyanyuliwa kalamu kwa watatu: Mtoto mdogo mpaka abaleghe, aliyelala mpaka aamke, na mwenda wazimu mpaka apate akili”

Na kauli ya Mtume ﷺ,

“Kumeondolewa kwa umma wangu kosa (bahati mbaya) kwa kusahau na kile walicho lazimishwa.” (Tabarani).

b) Lithibitishwe tendo la zinaa kwa uhakika, na hilo litafikiwa kwa kukubali mzunifu mwenyewe, akiwa katika hali ya kawaida kuwa amezini, au kwa kushuhudia mashahidi wanne waadilifu kuwa wao wamemuona akizini na wameiona tupu yake imo ndani ya tundu ya mwanamke aliyezini naye kama kilivyo kijiti cha kutilia wanja kiko ndani ya kidawati cha wanja, na kama ilivyo kamba iliyofungiwa ndoo ndani ya kisima, kwa kauli ya Allah Mtukufu.

وَأَلَّتِي يَأْتِينَ الْفَحِشَةَ مِنْ نِسَائِكُمْ فَاسْتَشِرُّوهُنَّ عَلَيْهِنَّ أَرْبَعَةٌ مِّنكُمْ ط

“Na ambao wanafanya uchafu miongoni mwa wanawake wenu, washuhudizieni watu wane katika nyinyi..” (4:15).

Na kauli ya Mtume ﷺ kwa Maiz:

“Umemuungilia: Akasema ndiyo, akasema kama kinavyopotea kijiti cha wanja ndani ya kichupa cha wanja na kamba ya ndoo ndani ya kisima...” (Abu Dawud)

Au kwa kutokeza mimba kama ataulizwa akashindwa kutoa ushahidi utaomuondolea adhabu kama kusema amebakwa au kaingiliwa kwa *shubha*, au bila ya kuelewa zinaa ni haramu. Kama atatoa maelezo yenye kuashiria wasi wasi na kukosa ufasaha wa kupatikana kwa mimba hiyo hatu adhibiwa, kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Ondoeni adhabu katika utata (shubha-kwa kukosa uwazi).”
(Ibni Adiyi).

Na kauli yake Mtume ﷺ:

“Kama ningalikuwa nina muadhibu-kupiga mawe mtu bila ya ushahidi ningalimpiga.” (Bukhari na Muslim).

Amezasema hayo kwa mke wa Al-Ajilani.

c) Mzinifu asirudi nyuma kukubali kwake. Kama atarudi kabla hajaadhibiwa kwa kusema Maelezo aliyoyatoa yalikuwa ya uwongo, na akasema sikuzini haadhibiwa kwa hadithi sahihi kwamba Maaizi alipigwa mawe akakimbia, lakini masahaba wakamfukuza na wakampiga mpaka akafa, akaelewa Mtume ﷺ tukio hilo akasema: **“kwa nini msimuache!”** Kama vile Mtume ﷺ tendo la kukimbia Maaizi amezingatia kuwa ni kurudi nyuma sikukiri kwake, na imepokewa kuwa,

“Maaizi alipokuwa anakimbia alikuwa anasema nirudisheni kwa Mtume wa Allah kwani jamaa zangu wameniuu, wamenidanganya, wameniambia Mtume haniui.” (Abu Dawud na Ahmad).

6-Namna ya kutekeleza adhabu Juu ya wazinifu:

Mzinifu atachimbiwa shimo katika ardhi litakaloishia kifuani kwake na atawekwa humo na atapigwa mawe mpaka kufa mbele ya kiongozi wa nchi au Naibu wake, na kikundi cha Waislamu idadi yao isiwe chini ya wanne, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَلِيَشْهَدَ عَذَابَهُمَا طَائِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٤﴾

“...Na lishuhudie adhabu yao kundi la Waumini.” (24:2).

Mwanamke ni sawa na mwanamume isipokuwa atafungwa nguo yake ili asiwe uchi. Tuliyoaeleza hapa yanahusu adhabu ya mawe, ama viboko kwa asiyekuwa *Muhswan*, itakuwa kama ilivyotekelezwa adhabu ya Qadhfu na kunywa pombe.

Tanbihi:

Adhabu ya Kulawiti ni kupigwa mawe mpaka kufa bila ya kutofuatisha kati ya *Muhswan* na asiyekuwa *Muhswan*. Kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Mtakayemkuta anafanya tendo la watu wa Liwati muueni mfanyaji na mfanywaji.” (Abu Dawud na Ahmad).

Namna ya kuwaua kumepokewa njia tofuati kutoka kwa masahaba kwani kuna baadhi yao wamewachoma moto, na wengine wamewapiga mawe na Ibnu ‘Abbas رضي الله عنه amesema kuhusu kuuliwa kwao: Itatafutwa nyumba iliyo ndefu zaidi jijini au kijijini hapo na watarushwa kutokea juu ya nyumba hiyo huku wameinamishwa kisha yatafuatia mawe.

Aliyemuingilia mnyama apewe adhabu ngumu kama vile viboko au kifungo kwa kulifanya tendo chafu, haramu kwa makubaliano ya wote na ili adhabu kali iwe rekebicho la tabia mbaya alizonazo, na zimepokewa athari kuwa atauliwa yeye pamoja na mnyama huyo isipokuwa athari hizo hazikuthibiti kwa kiwango cha kutumika kama hoja, kwa hiyo itatumika ile adhabu alioruhusiwa kadhi aitumie kwa kiwango cha kurekebisha tabia iliyoharibika. Mtwana na mjakazi kama atazini adhabu yao viboko tu, hata kama watakuwa *Muhswan* kwa kauli ya Allah Mtukufu.

فَأَنكِحُوهُمْ بِأَذْنِ أَهْلِهِمْ وَءَاتُوهُمْ بِأُجُورِهِمْ بِالْمَعْرُوفِ مُحْصَنَاتٍ غَيْرَ
مُسْفِحَاتٍ وَلَا مُتَّخِذَاتِ أَخْدَانٍ ۚ فَإِذَا أُحْصِنَ فَإِنَّ أَتَيْنَ بِفِجْشَةٍ
فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ مِنَ الْعَذَابِ ۚ

“...Na wanapo olewa kisha wakafanya uchafu basi adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu waliyo wekewa waungwana...”
(4:25).

Na ilipokuwa kifo hakigawiki ikalazimika adhabu ya viboko tu bila mawe.

Bwana anaweza kumuadhibu kwa viboko mtwana wake au mjakazi wake pia anaweza kukafikisha suala lao kwa kiongozi. Kwa kauli ya Ali رضي الله عنه: Mtume ﷺ alinituma kwenda kwa mjakazi aliyezini nimpe adhabu ya viboko nikamkuta yuko katika damu yake, nikamueleza Mtume ﷺ.

“Akasema akimaliza nifasi yake mpige viboko khamsini.” (Ahmad).

Na kauli ya Mtume ﷺ:

“Mjakazi wa mmoja wenu akizini na zinaa yake ikabainika basi na ampige adhabu asimlaumu na kumfedhehesha.” (Imepokewa na Bukhari, Tirmidhi na Daraqutni).



Mada ya Nne

Adhabu ya Wizi

1) Maana yake:

Wizi ni kuchukua mali iliyohifadhiwa, kwa kujificha kama vile mtu fulani ameingia dukani au ndani ya nyumba akachukua kutoka hapo nguo, au nafaka, au dhahabu au kinachofanana na hivyo.

2) Hukumu yake:

Wizi ni dhambi kubwa miongoni mwa madhambi makubwa, ameharamisha Allah kwa kauli yake:

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوا أَيْدِيَهُمَا جِزَاءً بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ

عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٣٨﴾

“Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikatani mikono yao, hayo ni malipo ya waliyo yachuma, ndiyo adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.” (5: 38).

Mtume ﷺ amemlaani aliyeiba,

“Amemlaani Allah mwizi anayeiba yai na kukatwa mkono wake.” (Imepokewa na Bukhari, Muslim, An-Nasai na Ibn Majah).

Amekataa kuwepo imani kwa mtu anayeiba, amesema

“Haibi mwizi wakati anaiba huku akiwa muumini.” (Imepokewa na Tirmidhi, An-Nasai, Ahmad na Darimy).

Amesema Mtume ﷺ alipokuwa anafafanua kuwa hiyo ni adhabu miongoni mwa adhabu za Allah inatekelezwa kwa yeyote.

“Naapa kwa yule nafsi yangu iko mkononi Mwake kama angeliiba Fatma binti Muhammad ningeliukata mkono wake.”
(Muslim).

3). Nini Kinachothibitisha Wizi:

Wizi unatibiti kwa moja ya mambo mawili. Mwizi kukubali bayana bila ya kutishwa au kupigwa kuwa ameiba. Au ka ushahidi wa waadilifu wawili kuwa yeye ameiba na kama atarudi katika kukubali hakatwi mkono isipokuwa atakilipa alichokiiba kwa sababu hiyo anaweza kufundishwa kukataa ili kulinda mkono wa Muislamu kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Ziondoeni adhabu kwa shubha kadri mnavyoweza.”

4) Sharti za kukata Mkono:

Ili iwajibike kukata mkono ni lazima yapatikane masharti yafuatayo:

a) Mwizi awe Muislamu Baleghe, mwenye akili timamu, kwa hadithi ya Mtume ﷺ:

“Imenyanyuliwa kalamu kwa watatu. Na miongoni mwao mwenda wazimu na mtoto mdogo.

b) Mwizi asiwe baba wa mwenye mali iliyoibwa, pia asiwe mtoto, mume au mke wa mwenye mali, kwa sababu hao wote kila mmoja anayo haki katika mali ya mwingine.

c) Kusiwe na uhusiano kwa aliyeibiwa kumiliki kwa mali hiyo wa karibu au wa mbali kwa mfano asiwe ameiba kitu alichokiweka rehani kutoka kwa aliyemuwekea au asiibe mshahara wake uliokutwa kwa muajiri wake.

d) Kilichoibwa kiwe mali halali, si pombe au zumari, na kifikie thamani yake robo dinari kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Mkono haukatwi isipokuwa katika robo dinari na zaidi.” (Muslim).

Minhajil Muslim

e) Mali iliyoibwa iwe katika ulinzi kama vile nyumba au duka au katika banda au sanduku na mfano wa hayo miongoni mwa vinayozingatiwa kuwa ni ulinzi.

f) Isichukuliwe mali kwa kupokonya yaani akapora kitu kilicho mbele ya mwenye chake akakimbia nacho.

Au kunyang'anya yaani kukichukua kwa nguvu, na isichukuliwe kwa kupora, yaani kuichukua, kama vile ngawira, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Hakuna kukata kwa mwizi wa kuaminiwa, wala mporaji, wala mpokonyaji.” (Timidhi na Ibnu Hibban).

5) Kinachomlazimu Mwizi:

Baada ya kuthibiti wizi kinachomlazimu mwizi haki mbili:

a) Kulipa mali iliyoibwa kama ikiwa mikononi mwake au kama uwezo anao na ikiwa mali iliyoibwa imepotea au imeharibika atadaiwa na mwenye mali.

b) Kukata, ikiwa ni haki ya Allah Mtukufu, kwanini miongoni mwa haki ya Alah Mtukufu. Kama hakuna kukata labda kwa sababu masharti ya kukata hayakukamilika, basi mali kulipwa ni lazima ilikuwa chache au uyingi, ni sawa mwizi awe tajiri au masikini.

6) Namna ya kukata:

Kikatwe kitanga cha mkono wa kulia wa mwizi katika kiwiko kufuatia kiraa ya Ibni Masuudi (*Faqtawau Aymaanahumaa*) mikono yao ya kulia. Kisha itamalizwa kwa kutiwa katika mafuta yaliyochemka ili kuiziba midomo ya mishipa na kuikata damu. Ni sunna kipande hicho kitundikwe shingoni mwake kwa kipindi kwa fundisho.

7) Kisichokatwa mkono kwa kukiiba:

Hairuhusiwi kukata mkono kwa kuiba mali isiyokuwa na ulinzi, wala mali isiyofikia thamani robo dinari, wala kwa kuiba matunda yangali mtini, au tende iko juu ya

mtende isipokuwa atalipishwa maradufu ya bei ya matunda kama atachukua kuondoka nayo, na atapewa adabu kwa kupigwa.

Ama kile anachokila tumboni mwake halipi kitu, kwa kauli ya Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu mbuzi anayeibwa malishoni mwake akasema:

“Atalipwa thamani yake mara dufu, na kupigwa kwa adhabu, na yule Aliyechukuliwa wakati wa mapumziko yake, adhabu yake atakatwa mkono kama kilichochukuliwa kinafikia thamani ya ngao. Na akaulizwa Ewe Mtume wa Allah na matunda jee na kilichochukuliwa bado iko katika maganda yake? Akasema aliyechukua kwa kinywa chake hakutengeneza bindo agharimu Kitu na alichochukua atakilipa maradufu na kipigo cha adhabu na aliyechukua kutoka kwenye vikaushio utakatwa mkono kilichochukuliwa thamani yake inafikia thamani ya ngao.” (Imepokewa na Ahmad, Nasai, Ibn Majah).

Tanbihi:

-Endapo mwenye mali amemsamehe mwizi na hakumpeleka kwenye vyombo vya dola hakuna haki ya kumkata mkono, na kama atampeleka basi ni wajibu kukatwa na maombi ya msamaha hayatakubaliwa tena baada ya hapo, kauli ya Mtume ﷺ:

“Kwa nini msamaha usiwe kabla hujafika naye kwangu.” (Ahmad na Malik)

Ameyasema hayo kwa aliyetaka kusamehe mwizi baada ya kuthibiti wizi wake na kufikishwa kwa Mtume ﷺ kwa kuhukumiwa.

-Ni haramu kufanya ombi la msamaha baada ya kufikishwa kwa hakimu. Kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Atakayeomba asamehewe katika adhabu katika huduud za Allah (Subhanahu wa Taala) basi Atakuwa amekwenda kinyume na amri zake”

Na kauli yake Mtume ﷺ kwa Usama رضي الله عنه.

Minhajil Muslim

“Unamuomba msamaha ili kuzuia kutekelezwa kwa adhabu ya Allah?” (Bukhari na Muslim).

Hukumu ya mtu anayeparamia kuta za nyumba za watu ili akawaue wenye nyumba au kuchukua mali zao sawa na wapiganaji.



Mada ya Tano

Adhabu ya Wapiganaji

1) Maana yake:

Wapiganaji ni kikundi cha Waislamu wameshika silaha mbele za watu wakazuia njia yao kwa kuwashambulia wapitaji na kuwaua, pia kuchukuwa mali zao kwa nguvu walizonazo.

2) Hukumu yao:

Hukumu za wapiganaji ni:

a) Waonywe na watakiwe kutubu. Kama watatubu toba yao itakubaliwa, na wakikataa watapigwa, kupigana nao kwa kuzingatiwa ni jihadi katika dini ya Allah Mtukufu atayeuliwa miongoni mwao hana hukumu hana kisasi wala fidia na atakayeuawa katika Waislamu kafa shahidi Kwa kauli ya Allah Mtukufu.

فَقَاتِلُوا الَّتِي تَبَغَىٰ حَتَّىٰ تَفِيءَ إِلَىٰ أَمْرِ اللَّهِ

“...basi lipingeni linalo dhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu...” (49: 9).

b) Atayekamatwa katika wapiganaji kabla hajaleta toba ataadhibiwa au kusulubiwa au kukatwa mikono mwili au miguu miwili au kuhamishwa kwa kauli ya Allah Mtukufu:

إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَنْ يُقَتَّلُوا

أَوْ يُصَلَّبُوا أَوْ تُقَطَّعَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِّنْ خَلْفٍ أَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْأَرْضِ

“Basi malipo ya wale wanao mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika nchi, ni kuuwawa, au kusalibiwa, au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kutolewa nchi.” (5:33)

“Na kama alivyofanya Mtume ﷺ kwa watu wa Urana ambao walichukua ngamia saba na wakamuua mchungu wake na wakakimbia.” (Bukhari na Muslim).

Kwa hiyo kiongozi ana hiyari katika adhabu zao hizi. Na baadhi ya wanazuoni wanaona kuwa watauliwa kama wataua, na watakatwa mikono na miguu tofauti kama watapora mali na watahamishwa au kufungwa kama hawakuu wala kupora mali mpaka watubu.

c) Kama wataleta toba kabla hawajakamatwa kama vile kwa hiyari yao wakaacha uharamia na wakajisalimisha wenyewe kwenye dola basi haki ya Allah kwao imeporomoka na zitasalia juu yao haki za waja watafikishwa mahakamani kwa roho za watu na mali zao. Walipe mali na kufidia roho mpaka hapo itakapopokelewa kutoka kwao diya au kusamehewa, kwa sababu hayo yote yanawezekana kwa kauli ya Allah Mtukufu.

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ قَبْلِ أَنْ تَقْدِرُوا عَلَيْهِمْ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٤﴾

“ Isipo kuwa wale walio tubu kabla hamjawatia nguvuni. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu..” (5:34).

Hakuna pingamizi kwa dola kuwalipia au kuwatolea gharama kama hawana kitu mkononi vyote walivyo vipora katika mali.



Mada ya Sita

Waasi

1) Maana ya Waasi:

Ni kikundi chenye silaha na nguvu kilichoasi mamlaka halali iliyopo ya dola kwa kutumia hoja au sababu zinazokubalika. Kama vile wamemdhania kiongozi wa nchi ni kafiri au dhalimu wakaungana pamoja wakafanya maasi dhidi ya dola hiyo.

2) Hukumu Zao:

Kiongozi afanye nao mawasiliano awaulize kosa walilonalo kwa kiongozi wao, na sababu ya maasi yao, kama wataeleza dhuluma yao na sababu ya wao wafanye maasi au kwa wengine kiogozo ataiondoa, na kama watadai utata (shubha) kiongozi atawafanulia atawaeleza haki iko wapi katika suala hilo. Na dalili yake kama watarudi kwenye haki itakubaliwa kurudi kwao, na kama watakataa basi watapigwa vita tena ni wajibu kwa Waislamu wote, kwa kauli yake Allah (*Subhanahu wa Taala*):

وَإِن طَآئِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ۚ فَإِن بَغْت إِحْدَاهُمَا عَلَى الْآخَرَىٰ فَاقْتُلُوا الَّتِي تَبَغَىٰ حَتَّىٰ تَفِيءَ إِلَىٰ أَمْرِ اللَّهِ ۚ فَإِن فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾

“Na ikiwa makundi mawili katika Waumini yanapigana, basi yapatanisheni. Na likiwa moja la hao linamdhulumu mwenzie, basi lipigeni linalo dhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na likirudi basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao hukumu kwa haki.” (49:9).

Hairuhusiwi kupigana nao kwa kutumia zana zenye kuteketeza kama vile ndege au mizinga, bali watapigwa kwa kile kitachovunja nguvu zao na kuwalazimisha

Minhajil Muslim

wajisalimishe tu. Hairuhusiwi kuwauwa watoto zao na wake zao, pia kuwanyang'anya mali zao.

Hairuhusiwi kummaliza kabisa majeruhi wao, pia mateka wao hauliwi wala anayekimbia miongoni mwao, kwa kauli ya 'Ally رَضِيَ اللهُ عَنْهُ : Siku ya vita vya Jamal:

“Asiuawe anayekimbia na asimalizwe majeruhi na atayefunga mlango wake yuko katika amani.” (Ameipokea Ibn Mansur).

Vita vikimalizika na wakashindwa hawafanyiwi kisasi na wala hawatakiwi chochote kisichokuwa toba, na kurudi kwenye haki, kwa kauli ya Allah Mtukufu.

فَإِنْ فَآءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾

“...Na likirudi basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao hukumu kwa haki.” (49: 9).

Tanbihi:

Kama vitapambana vikundi viwili katika waislamu kwa ubaguzi au mali au cheo bila ya tafsiri, basi vikundi hivyo vyote ni madhalimu na kila kimoja atakilipa alichokiharibu iwe roho au mali ya kundi lingine.



Mada ya Saba:

Anayeuliwa kwa adhabu

Murtaddi, aliyeacha Dini

1) Maana yake:

Murtadi ni mtu aliyetiacha dini ya Uislamu kwenda nyingine kama vile Ukristo au Uyahudi au hakujiunga na dini nyingine kama vile mpagani na mkomunisti akiwa na akili timamu kwa hiyari yake.

2) Hukumu yake:

Hukumu ya *Murtadi* atatakiwa arudi kwenye Uislamu kwa siku tatu na asiporudi atauliwa kwa upanga. Adhabu kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Mwenye kubadili dini yake muuani.” (Bukhari).

Na neno lake Mtume ﷺ:

“Si halali kumwaga damu ya mtu Muislamu isipokuwa kwa sababu moja ya tatu: mzinifu muhsan, nafsi kwa kuuawa na mwenye kuhamia dini yake na Kufarikiana na umoja wa Waislamu.” (Imepokewa na Nasai, Ibn Majah na Abu Dawud)

3) Hukumu yake Baada ya kuuliwa:

Kama atauliwa *Murtadi* haoshwi, haswaliwi, hazikwi katika makaburi ya Waislamu na wala harithiwi na alichokiacha katika mali kitakuwa *fayi* kwa Waislamu au na kutumiwa katika huduma za jamii kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَلَا تُصَلِّ عَلَى أَحَدٍ مِّنْهُمْ مَاتَ أَبَدًا وَلَا تَقُمْ عَلَى قَبْرِهِ ۗ إِنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ

وَرَسُولِهِ ۚ وَمَاتُوا وَهُمْ فَسِقُونَ ﴿٢٤٤﴾

“Wala usimsalie kabisa yeyote katika wao akifa, wala usisimame kaburini kwake. Hakika hao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakafa na hali ni wapotofu” (9:84).

Kauli ya Mtume ﷺ,

“Kafiri hamrithi Muislamu wala Muislamu hamrithi kafiri.”
(Imepokewa na Ahmad, Hakim na Daruqutni)

Waislamu hawana hitilafu juu ya hukumu tulizozitaja za Murtadi.

4) Kauli na Itikadi Zinazokufurisha:

Kila aliyemtukana Allah au kumtukana Mtume ﷺ miongoni mwa Mtume wake ﷺ au Malaika miongoni mwa malaika عليه السلام atakuwa amekufuru.

Kila anayepinga uumbaji wa Allah au uungu wake Allah Mtukufu au utume miongoni mwa Mitume au akadai kuwa kuna Mtume atakuja baada ya Mtume wa mwisho (Muhammad ﷺ), amekufuru. kama vile mwenye kupinga wajibu katika wajibu wa sheria au usio na hitilafu kama vile Swala au Zaka au Funga au Hija au kuwafanya wema baba na mama au Jihadi amekufuru. Na kila atayehalalisha haramu isio na hitilafu inayofahamika kwa vyovyote katika sheria, kama vile zinaa au kunywa pombe, au wizi au kuua au uchawi amekufuru.

Kila aliyepinga sura au Aya au Herufi katika Qur-aan amekufuru. Kila aliyepinga sifa miongoni mwa sifa za Allah Mtukufu kama vile uhai, kujua, kusikia, kuona, huruma, huyu amekufuru. Na kila anayeonesha dharau kwa dini au wajibu wa dini au Sunna yake au ameifanyia mzaha au ameidharau au msahafu ameutupa kwenye uchafu, au ameukanyaga kwa mguu wake ili kuidharau amekufuru. Na kila anayeamini kuwa hakuna kufufuliwa adhabu ya neema hakuna siku ya kiama au adhabu na neema ni maana tu si hakika amekufuru.

Na kila anayesema mawalii wa Allah ni bora kuliko Mitume au wajibu wa ibada kwa mawalii wengine haupo amekufuru. Dalili ya hayo yote ni makubaliano ya Waislamu wote baada ya kauli ya Allah Mtukufu:

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ؕ قُلْ أْبِاللَّهِ وَءَايَاتِهِ
وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِءُونَ ﴿٦٥﴾ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ ؕ

“Na ukiwauliza, wanasema: Sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu. Sema: Mlikuwa mkimfanyia maskhara Mwenyezi Mungu na Ishara zake na Mtume wake? Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu!....” (9:65-66),

Hakika aya hii yajulisha kuwa kila aoneshaye mashaka na dharau kwa Allah au Sifa zake au sheria yake au Mtume wake amekufuru.

5) Hukumu ya aliyekufuru kwa sababu zilizotajwa:

Atatakiwa alete toba kwa siku tatu kama ataleta toba kwa kauli yake au itikadi yake ni vema, asipokubali atapewa adhabu, na hukumu yake baada ya kuuliwa ni hukumu ya murtadi.

Wanazuoni wamemtoa mwenye kumtukana Allah au Mtume ﷺ wakekuwa huyu atauliwa wakati ule ule, haikubaliwi toba yake. Baadhi ya wanazuoni wameona atatakiwa alete toba na toba yake itakubaliwa, atatoa shahada kuwa hakuna mola anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wake ﷺ na Mjumbe wake, na amuombe msamaha Allah Mtukufu na atubu kwake.

Tanbihi:

Mwenye kutamka tamko la ukafiri kwa kulazimishwa chini ya kipigo au kufishwa, na moyo wake umetulia katika imani. Huyu hakuna athari yoyote juu yake kwa kauli ya Allah Mtukufu.

إِلَّا مَنْ أَكْرَهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيمَانِ وَلَئِنْ مِّنْ شَرَحٍ بِالْكَفْرِ صَدْرًا
فَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ مِّنَ اللَّهِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٦٦﴾

“... isipo kuwa aliye lazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetua juu ya Imani, lakini aliye kifungulia kifua chake kukataa - basi hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ipo juu yao, na wao watakata adhabu kubwa”.(16:106).

Zandiki

1) Maana yake:

Zandiki ni mtu anayedhihirisha Uislamu na anaficha ukafiri, kama vile anayepinga kufufuliwa au anakataa Utume wa Mtume wetu Muhammad ﷺ au haamini kuwa Qur-aan ni maneno ya Allah huyo hayatangazi au kuyasema bayana anaogopa au yeye ni mnyonge.

2) Hukumu yake:

Hukumu ya Zandiki inapogundulika na hali yake ikaeleweka atauliwa, na inasemekana atatakiwa alete toba na kufanya hivyo ni vizuri pia bora, kama atatubu basi, na kama hakutubu atauliwa na hukumu yake baada kuuliwa ni hukumu ya murtadi katika hukumu zilizosalia, kwamba haoshwi na haswaliwi.

‘Mchawi’

1) Maana yake:

Mchawi ni yule anayefanya uchawi na kuutumia.

2) Hukumu yake:

Hukumu ya mchawi yataangaliwa matendo yake, ikiwa matendo yake anayoyafanya au maneno anayoyasema yanamkufurisha, atauliwa kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Adhabu ya mchawi kupigwa kwa upanga.” (Imepokewa na Tirmidhi na Daruqutni).

Na kama anayoyafanya au kuyasema hayamkufurishi, atapewa adhabu nyingine na atatakiwa atubu, kama atatubu basi, na asipotubu atauliwa kwa sababu lazima atafanya au kusema la kumfanya awe kafiri, kwa kauli ya Allah.

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ^ط

*“...Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie:
Hakika sisi ni mthani; basi usikufuru...” (2:102)*

Na kauli Yake Allah,

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولَا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ^ط

*“...Na hakika wanajua kwamba aliye khiari haya hatakuwa
na fungu lolote katika Akhera....” (2:102)*

Mwenye Kuacha Swala

1) Maana yake:

Mwenye kuacha swala miongoni mwa waislamu, Swala tano ataona kwa kudharau au kuipinga.

2) Hukumu yake:

Hukumu ya mwenye kuacha swala ataamrisha kuswali na ataachiwa mpaka wakati wa swala utabaki wakati wa dharura, kiasi cha kutosha rakaa moja, kama ataswali ni vema asiposwali atauawa, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَإِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ وَنُفُصِلُ

الْأَيْدِي لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

“Basi wakitubu na wakashika Sala na wakatoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika Dini. Na tunazichambua Aya kwa watu wajuao.” (9:11).

Na kauli ya Mtume ﷺ :

“Nimeamrisha kupigana na watu mpaka washuhudie kuwa hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na Muhammad ni Mjumbe wa Allah, na watoe zaka, kama waafanya hivyo, wamezilinda damu zao na mali zao isipokuwa kwa haki ya Waislamu.” (Bukhari na Muslim).

Zinduzi:

-Kumchelewesha aliyeacha sala kiasi cha raka'a moja tu. Kisha akikataa kusali anauliwa adhabu. Ni madhehebu ya Maliki na kumchelewesha kwa siku tatu ni madhehebu ya Ahmad رضي الله عنه

-Aliyeacha Uislamu kwa kupinga kinachoeleweka katika dini kwa hali yoyote toba yake haikubaliwi isipokuwa akikubali alichokikataa na kutamka shahada mbili. Na kuomba msamaha kwa dhambi zake.

-Madhumuni ya Neno (*Haddun*) katika neno letu kuwa murtadi, zandiki na mchawi atauliwa (*“Haddu Ssahir Dwarbuhu Bi-Sayfi”*). Maana yake atauliwa kwa sheria kwa dhambi lake ambalo ni rida au uzandiki au uchawi haswaliwi na wala hazikwi katika makaburi ya Waislamu.



Mada ya Nane:

Inahusu 'Taazira'

1) Maana yake:

Taazira ni kutia adabu kwa kipigo au kutukana au kukata uhusiano naye au kuhamisha.

2) Hukumu yake:

Taazira ni wajibu au lazima katika maasi yote muweka sheria hakuziwekea adhabu wala kafara kama vile wizi ambapo kilichoibwa hakikufikia kiwango cha kukata, au kama vile kumshika au kumbusu mwanamke Ajnabiya au kumtukana Muislamu si kwa tamko la kumuhusisha na zinaa, au kumpiga Muislamu bila ya kumjeruhi au kuvunja kiungo.

3) Sheria zake:

Sheria za *Taazira* ni:-

a) Kama ni kupigwa basi isiwe zaidi ya viboko kumi kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Hapigwi yeyote zaidi ya viboko kumi ispokuwa adhabu miongoni mwa adhabu za Allah Mtukufu”. (Imepokewa na Muslim, Abu Dawud, Tirmidhi na Ibn Majah).

b) Hakimu ajitahidi katika *Taazira*, na kila hali ataiweka na kile kinacholingana nacho, na kama tusi litatosha katika kumkemea, mhalifu au kumpa, adhabu atatosheka na kumtukana. Na kama kutiwa ndani kwa mchana na usiku kunatosha basi hakimu atatosheka na hilo bila ya kuongeza muda huo, na ikiwa faini ndogo itatosha kumkemea basi atatosheka nayo bila ya faini kubwa n.k. Kwa sababu kilichokusudiwa katika *Taazira* ni malezi na mafunzo sio adhabu na mateso, Mtume ﷺ alimpa adabu Abu Dhari kwa kauli yake:

“Wewe ni mtu wa tabia za Kijahiliya” (Muslim na Tirmidhi).

Minhajil Muslim

Akasema:

“Mwambieni aliyeuza na kununua Msikitini. Allah asikupe faida katika biashara yako.” (Tirmidhi)

Na mwenye kutangaza kitu kilichopotea msikitini,

“Allah asikurudishie kwa sababu misikiti haikujengwa kwa hili”
(Muslim).

Pia ameamuru kuwatenga watu watatu walioacha kushiriki katika vita bila ya udhuru akawapa adhabu hiyo tu, akawaamuru makhanithi wawe mbali na mji wa madina. Na alimtia ndani mtu Fulani aliyetuhumiwa mchana na usiku, na akamgharimu mara mbili ya thamani ya kitu alichochukua nacho ni tende bado zingali mtini kwa wizi na mengi mengineyo katika aina za taazira zilizothibitika katika matendo yake Mtume ﷺ ambayo lengo na madhumuni yake ni kumfundisha Muislamu na kumlea.



Kinahusu Hukumu za Ukadhi na Ushahidi

Mada ya Kwanza

‘Ukadhi’

1. Maana yake:

Ukadhi ni ufafanuzi hukumu za sheria na kuzitekeleza.

2. Hukumu yake:

Ukadhi ni miongoni mwa faradhi kifaya kwa hiyo inamlazimu kiongozi wa nchi amuweke kadhi katika kila mji miongoni mwa miji iliyo katika utawala wake atayekuwa badala yake katika kufafanua sheria na kuwalazimisha raia kuitekeleza kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Si halali kwa watatu wakawa jangwani katika ardhi isipokuwa wamemteuwa mmoja wao kuwa kiongozi juu yao.” (Ahmad).

3. Hatari ya cheo cha Ukadhi:

Ni miongoni mwa vyeo vya hatari kubwa mno na cheo kikubwa kwa sababu ni kutekeleza sheria ya Allah kwa niaba ya Allah na ni ukhalifa wa Mtume wake na kwa sababu hiyo Mtume ﷺ akawatahadharisha na kazi ya ukadhi. Na akasema,:

“Atakayejaaliwa ukadhi miongoni mwa watu basi amechinjwa bila ya kisu.” (Ahmad na Ibn Majah)

Na akawazindua watu hatari yake na akasema Mtume ﷺ:

“Makadhi ni watatu, mmoja yuko Peponi na wawili wako Motoni, amma aliyekuwa peponi ni mtu aliyeijua haki na akahukumu kwa haki hiyo, na mtu haki ameifahamu akadhulumu— kaacha haki katika hukumu – basi huyo yuko Motoni, na mtu amehukumu kwa watu bla ya kujua anachokifanya basi huyo yuko Motoni.” (Abu Dawud na Hakim).

Na amemwambia Abdu-Rahmani:

“Ewe Abdur-Rahmani Ibni Samurah usiombe uongozi, kwa sababu kama utapewa uongozi bila kuomba utasaidiwa, na kama utapewa kwa kuomba utaachiwa.” (Bukhari na Muslim).

Na kauli yake:

“Watakuwa na pupa kubwa juu ya kutaka uongozi na kesho kiama yatakuwa majoto, neema ya mnyonyeshaji na ubaya wa muachisha ziwa.” (Bukhari).

4. Hapewi Ukadhi anayeuomba:

Hairuhusiwi kupewa cheo cha ukadhi aliyeuomba au mtu aliye na pupa ya kukipata cheo hicho, kwa sababu ukadhi ni jukumu zito mno na dhamana kubwa hawezi kuitaka isipokuwa anayeuona kuwa ni kitu chepesi rahisi na haki yake ni nyepesi, mtu kama huyu haaminiki kuwa atailinda haki ya ukadhi, hatoichezea, na kufanya hivyo ni uharibifu katika dini, nchi na watu, uharibifu usiovumilika. Kwa sababu hiyo, Mtume ﷺ amesema:

“Sisi Wallahi hatumpi madaraka haya yeyote aliyeuomba, na yeyote aliye na pupa nayo.” (Bukhari na Muslim).

Pia Mtume ﷺ amesema:

“Sisi hatumpi mtu kazi yetu aliyeiomba.”

5. Sharti za kupewa Ukadhi:

Hapewi Ukadhi isipokuwa ambaye zimekamilika sifa zifuatavyo: Uislamu, akili timamu, ubaleghe, uungwana, kukijua kitabu cha Allah na Sunna za Mtume wake, kuelewa atachokitumia katika hukumu, uadilifu, anasikia, anaona, anazungumza.

6. Adabu Za Kadhi:

Kadhi analazimika awe na adabu zifuatazo: mwenye nguvu bila ya ukatili, awe mpole bila ya udhaifu ili dhalimu asiwe na tamaa na kufanya atakavyo wala mwenye

haki asimuogope kwa ukali na ukatili wa kadhi huyo, awe mvumilivu bila ya kudharauliwa ili wahasimu wapumbavu wasije wakathubutu kumchezea na asiwe na papara awe mchunguzi bila ya kuchelewesha na kutokujali awe mwerevu, mwenye kuona mbali bila ya kujiona, wala kumdharau mwengine. Makazi yake yawe kati ya mji, yenye nafasi wahasimu wanaenea, wasibanwe, wasibanwe mashahidi.

Awe muadilifu katika kuwaangalia mahasimu kwa jicho moja, au kwa macho yote kukaa kwake, na kuingia kwake, asimpendelee mmoja kuliko mwingine kwa chochote, na wafike wataalamu na Fiqhi katika baraza lake, wanaokijua Kitabu na Sunnah na awatake ushauri kwa kinachomtatiza.

7. Anayolazimika kadhi Kujiepusha Nayo:

Analazimika Kadhi kujiepusha na mambo mengi na awe mbali nayo ni:-

a) Ajiepushe kutoa hukumu akiwa na hasira au anahisi kuwa anaathiriwa na ugonjwa au njaa au kiu au joto au baridi au uchovu au uvivu, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Asihukumu hakimu kati ya wawili hali ana hasira.” (Bukhari na Muslim).

b) Kutoa hukumu bila ya kufika mashahidi.

c) Asijipe haki mwenyewe au yule ambaye ushahidi wake haukubaliwi, kwao, kama vile mtoto, baba na mke.

d) Asikubali/asipokee rushwa juu ya hukumu, kwa kauli yake Mtume ﷺ.

“Laana ya Allah iwe juu ya mtoa rushwa na mtaka rushwa katika hukumu.” (Ahmad)

e) Asipokee zawadi kutoka kwa mtu ilhali kabla yeye hajawa hakimu alikuwa hampi zawadi kwa kauli ya Mtume ﷺ:

“Tunae mpa kazi na tukampa mshahara basi atachochukua baada ya hapo ni dhulma.” (Abu Dawud na Ibn Majah).

8) Madaraka ya Kadhi:

Madaraka ya Kadhi na vinavyoingia katika uwezo wa cheo chake ni yafuatayo:-

- a) Kuhukumu kati ya wahasimu wawili katika madai mbali mbali na kesi, kwa hukumu zenye kutekelezwa au suluhu itayoridhiwa na pande mbili, kama ushahidi utapingana au hoja haziko wazi au dhaifu.
- b) Kuwalazimisha madhalimu na kuwazidi nguvu na kuwasaidia wenye haki na wadhulumiwa na kufikisha haki kwa mwenyewe.
- c) Kutekeleza adhabu na hukumu katika kuua na majeraha.
- d) Kuziangalia Ndoa, Talaka Matumizi na Mengineyo.
- e) Kutunza mali za wasioruhusiwa kisheria kutumia mali zao au kutunza, kama vile mayatima, wendawazimu na waliopotea, au hawapo na waliozuluiwa mali zao.
- f) Kutunza huduma za jamii katika mji kama vile barabara, shule, hospitali n.k.
- h) Kuamuru mazuri na kuwalazimisha watu kuyatekeleza na kukataza maovu na kuyabadilisha na kuondoa athari yake katika nchi.
- i) Kuongoza sala za Ijumaa na za Idd.

9. Kadhi atahukumu kwa kutumia nini?

Chombo cha hukumu atachokitumia hakimu kufikisha haki kwa wenyewe ni vinne navyo ni:

- a) Kukiri kwa mdaiwa haki aliyodaiwa kwa kauli ya Mtume ﷺ

“Kama atakiri mpige mawe.” (Ameipokea Bukhari na Muslim)

- b) Ushahidi nao ni mashahidi kwa kauli ya Mtume Muhammad ﷺ

“Ushahidi ni juu ya mwenye kudaiwa na kiapo ni juu ya mwenye kupinga.”

Kwa mdaiwa kwa mwenye kupinga ni yamini (Al bain) ni sahihi kauli yake ﷺ,

“Mashahidi wako wawili au yamini yake.” (Muslim)

na uchache wa mashahidi ni wawili, wasipopatikana basi ni shahidi mmoja na kiapo na kwa kauli ya Ibn Abbas رضى الله عنه Mtume Muhammad ﷺ,

“Amehukumu kwa yamini na shahidi mmoja”(Muslim).

c) Yamini kwa kauli ya Mtume ﷺ,

“Ushahidi kwa mdai na yamini kwa mwenye kupinga”,

Mdai kama atashindwa kuleta ushahidi ataapa mdaiwa yamini moja, na itamvua madai.

d) Kukataa kula yamini. Ni kukataa mdaiwa kula kiapo ikiwa hakuapa. Kadhi atamsihi kwa kumwambia kama utakula kiapo nitakuachia na usipokula kiapo nitatoa hukumu dhidi yako, kama atakataa basi kadhi atatoa hukumu dhidi yake isipokuwa Imam Malik رضى الله عنه anaona katika hali ya kukataa kula yamini, yamini itarudishwa kwa mdai, na akila yamini atatoa hukumu kwa mdai, na hoja ya Imam Maliki ni tendo la Mtume ﷺ la kurudisha yamini kwa mdai katika *kasaama*). Nakufanya hivyo ni tahadhari kubwa kwa hukumu na kuvua dhima.

10) Namna ya kuhukumu na njia yake; kama watafika mahasimu wawili atawaweka mbele yake. Kisha atawauliza yupi mdai kati yenu? Na kama atanyamaza mpaka mmoja wao aanze kutoa maelezo yake si vibaya kama atamaliza kutoa madai yake kwa upembuzi na ufasaha atamwambia mdaiwa wasemaje kuhusu madai hayo na kama atayapinga atamwambia mdai leta ushahidi wako kama ataleta atatoa hukumu kwa mdai, na kama ataomba muda wa kuleta ushahidi atampa muda utaomuwezesha kuleta ushahidi asipoleta ushahidi atamwambia mdaiwa kula kiapo, kama atakula kiapo atamuachia na kama atakataa kula yamini atamsihi kwa kumwambia asipokula yamini atatoa hukumu dhidi yake, isipokuwa vizuri kuirejesha yamini kwa mdai kama atakula atampa haki na haya ni kufuatia hadithi aliyoipokea Muslim katika sahihi yake. Kutoka

kwa walii Ibn Hajr رضي الله عنه: kuwa watu wawili walipeleka malalamiko yao kwa Mtume ﷺ Hadhwaramiyyu na mwingine ni Kindiyyu akasema yule Hadhwaramiyyu: Ewe mjumbe wa Allah huyu amenishinda katika ardhi yangu na Kindiyyu akasema: hiyo ni ardhi yangu na iko mikononi mwangu na hana haki katika ardhi hiyo. Mtume ﷺ akasema kumwambia Hadhwarami:

“Je, unayo bayyinna? Akasema hapana, akasema wewe kula yamini yake. Akasema ewe Mtume huyu ni mtu ‘Aswi hajali kula yamini, haogopi kitu. Mtume ﷺ akasema wewe hauna haki kwake ila kiapo tu.”

Tanbihi:

- 1) Kadhi kama ataelewa uadilifu wa shahidi, atahukumu kwa ushahidi huo.
- 2) Kama atashitakiwa mwanamke mwenye hijabu, hakuwa anaejitokeza katika hadhara za watu asie na uwezo wa kuzungumza na wanamume na kufika katika mahakama halazimishwi kufika mahakamani, inamtosha kuweka wakili kwa niaba yake katika kuhudhuria mahakamani.
- 3) Hakimu asitoe hukumu kulingana na anavyofahamu bali ahukumu kulingana na ushahidi ili asituhumiwe katika uadilifu wake na utakatifu wake, kwa kauli ya Abubakari Swiddik رضي الله عنه.

“Kama nitamuona mtu imemuwajibikia adhabu katika adhabu za Allah nisingali muadhibu na wala nisingalimuitia yeyote mpaka awe pamoja nami mtu mwingine.” (Imam Ahmad).

- 4) Kama atadaiwa aliyepo atawajibika kufika mahakamani, haitolewi hukumu akiwa hayupo isipokuwa kama atawakilishwa na wakili. Na kama hayupo ataitwa na atatakiwa ahudhurie Mahakamani au atawakilisha.
- 5) Maandishi ya kadhi kwa kadhi mwingine yatakubaliwa na huyo kadhi mwingine ikiwa maandishi hayo si katika hudud—kama atawashuhudishia juu ya maandishi hayo mashahidi wawili.

6) Hayakubaliwi madai yasiofafanuliwa na mdai: kama kusema mimi na mdai kitu fulani, au nadhani fulani namdai kitu kadhaa –mpaka akitaje kitu hicho na awe na uhakika wa anachokidai kwa mdaiwa.

7) Hukumu ya kadhi katika dhahiri haihalalishi haramu ya uhakika wa jambo lenyewe na wala haiharamishi halali, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Si vingine mimi ni mwanadamu, nanyi mnaniletea malalamiko yenu huenda baadhi yenu wakawa mahodari mno kwa hoja kuliko wengine, nitakavyohukumu kulingana na nilichosikia nikampa haki ya mwingine chochote kile asikichukue kwani si kingine alichopewa bali ni kipande cha moto.” (Bukhari na Abu Dawud).

8) Ushahidi unapopingana na kukawa hakuna kinachousaidia kuliko mwingine, kinachogombewa kitagawanywa kati ya wawili wanaokigombea. Kwa hukumu ya Mtume ﷺ (Imepokewa na Al Baihaqi, Abu Dawud na al Hakimu).



Mada ya Pili

Ushahidi

1) Maana ya Ushahidi:

Ushahidi ni mtu kueleza ukweli wa alichokiona au kusikia.

2) Hukumu yake:

Kuchukua ushahidi kama ulivyo ni wajibu au faradhi-kifaya kwa yule anayelazimika kuchukua na kutoa kwa kauli ya Allah Mtukufu,

وَأَسْتَشْهِدُوا شَهِيدَيْنِ مِنْ رَجَالِكُمْ ۖ فَإِنْ لَمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَامْرَأَتَانِ
مِمَّنْ تَرْضَوْنَ مِنَ الشُّهَدَاءِ أَنْ تَضِلَّ إِحْدَاهُمَا فَتُذَكِّرَ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَى ۚ
وَلَا يَأْبَ الشُّهَدَاءُ إِذَا مَا دُعُوا ۚ وَلَا تَسْعَمُوا أَنْ تَكْتُبُوهُ صَغِيرًا أَوْ كَبِيرًا إِلَى
أَجَلِهِ ۚ ذَٰلِكُمْ أَقْسَطُ عِنْدَ اللَّهِ وَأَقْوَمُ لِلشَّهَادَةِ وَأَدْنَىٰ أَلَّا تَرْتَابُوا ۗ

“...Na mshuhudishe mashahidi wawili katika wanaume wenu. Ikiwa hapana wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili katika mnao waridhia kuwa mashahidi. Ili ikiwa mmoja wao akipotea, mmoja wao amkumbushe mwengine. Na mashahidi wasikatae waitwapo. Wala msipuuze kuliandika deni likiwa dogo au kubwa mpaka muda wake. Hayo ndiyo haki zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, na ndiyo sawa zaidi kwa ushahidi, na vyema zaidi ili msiwe na shaka...” (2:282)

Na kauli yake,

وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ ۚ وَمَنْ يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ قَلْبُهُ ۚ

“... Wala msifiche ushahidi. Na atakaye ficha basi hakika moyo wake ni wenye kutenda dhambi...” (2:283)

Na kauli ya Mtume ﷺ:

“Je, niwaeleze mbora wa mashahidi, ni yule anayetoa ushahidi wake kabla hajatakiwa.” (Muslim).

3) Sharti za Shahidi:

Shahidi anatakiwa awe Muislamu baleghe mwenye akili timamu muadilifu hana tuhuma, maana ya hana tuhuma asiwe miongoni mwa usiokubaliwa ushahidi wao kama vile wazazi wawili kwa baadhi yao, na kama vile mume au mke kwa mwenzake, au kama vile ushahidi uliompatia maslahi shahidi, au kumuondolea dhara, na kama vile ushahidi wa adui dhidi ya adui wake, kwa kauli ya Mtume ﷺ.

“Ushahidi wa asiyekuwa muaminifu mwanamume na mwanamke –kha-ina-, Wala mwenye uadui na ndugu yake, wala ushahidi wa mtumishi au anaepata mahitaji yake ya lazima kwa watu wa kaya fulani haukubaliwi.” (Ahmad na Abu Dawud)

4) Sheria za Ushahidi:

a) Haikubaliwi kwa shahidi kutoa ushahidi isipokuwa kwa alichokielewa kwa kuona au kusikia, kwa kauli ya Mtume ﷺ kwa aliyemuuliza kuhusu ushahidi:

“Jua unaliona? Akasema: basi kama unavyoliona Jua toa ushahidi au acha.” (Ibnu Adiyyi).

b) Utakubaliwa ushahidi wa mwingine kama shahidi hataweza kufika Mahakamani iwe kwa ugonjwa au hayupo, au amekufa, kwa sababu ya dharura, ikiwa hakimu hawezi kutoa hukumu bila ya ushahidi huo.

c) Shahidi utathibitishwa kukubalika kwake kwa ushahidi wa waadilifu wawili: kwamba yeye ni muadilifu anakubalika, ikiwa uadilifu wa shahidi hauko bayana! Na shahidi uadilifu wake ulio bayana hakimu hana haja ya kutaka uthibitisho huo.

d) Kama watu wawili watathibitisha uadilifu wa shahidi na wakatokea wawili wengine wakasema shahidi huyo si muadilifu itatangulizwa kauli ya wapinga uadilifu kwa tahadhari.

e) Shahidi muongo ni wajibu kutiwa adabu na kufundishwa adabu kwa kupewa adhabu itakayomkomesha kutorudia tena kosa hilo, na kuwa fundisho kwa yule nafsi yake inamshauri kufanya kama hivyo.

5) Aina za Ushahidi:

a) Ushahidi wa zinaa, ni lazima katika ushahidi huu wapatikane mashahidi wanne, kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَالَّتِي يَأْتِيَنَّ الْفَنَحِشَةَ مِنْ نِسَائِكُمْ فَاسْتَشْرِدُوا عَلَيْهِنَّ أَرْبَعَةً مِنْكُمْ

“Na ambao wanafanya uchafu miongoni mwa wanawake wenu, washuhudizieni watu wane katika nyinyi...” (4:15)

Haitatosha katika kuthibitisha zinaa chini ya mashahidi wanne.

b) Ushahidi usiokuwa wa zinaa, katika mambo yoyote yasiyokuwa zinaa wanatosha mashahidi wawili waadilifu.

c) Ushahidi wa mali utatosha katika ushahidi wa mali shahidi mmoja mwanamume na wanawake wawili kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَاسْتَشْرِدُوا شَهِدَيْنِ مِنْ رَجَالِكُمْ فَإِنْ لَمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَأَمْرَأَتَانِ
مِمَّن تَرْضَوْنَ مِنَ الشُّهَدَاءِ

“...Ikiwa hapana wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili katika mnao waridhia kuwa mashahidi...” (2:282).

d) Ushahidi wa hukumu unatosha shahidi mmoja na yamini kwa kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنه Mtume عليه السلام ametoa hukumu kwa yamini na shahidi mmoja).

e) Ushahidi wa mimba na hedhi na wasichokiona isipokuwa wanawake unatosha ushahidi wa wanawake wawili.



Mada ya Tatu

Inahusu Kukiri:

1) Maana yake:

Kukiri ni kukubali mtu kitu katika dhima yake cha mtu mwingine, kamavile akasema: hakika ya zaidi kwangu ana dirham khamsini alfu au kitu fulani, ni cha fulani

2) Kukiri kwa nani kunakokubaliwa?

Kukiri kunakokubaliwa ni kukiri kwa mtu baleghe mwenye akili timamu, ama mwendawazimu, wala mtoto mdogo chini ya baleghe hakukubaliwi kukiri kwao, wala aliyelazimishwa, kwa sababu hawana majukumu kisheria kwa kauli yake Mtume ﷺ, “*Imenyanyuliwa kalamu kwa watu watatu na ilishatangulia hadithi hii, na kwa kauli yake Mtume ﷺ na... alicholazimishwa.*”

3) Hukumu yake:

Kukiri ni kulazimika, kwa hiyo atayekiri kwa mtu kitu fulani na aliyekiri ilhali ni baleghe mwenye akili timamu na amekiri kwa hiyari yake basi alichokiri kitamlazimu, kwa kauli ya Mtume ﷺ: “*akikiri mpige mawe*” hapa, Mtume ﷺ amekufanya kukiri kwake kumethibitisha wajibu wa adhabu ya kupigwa mawe kwake.

4) Baadhi ya sheria za ‘Kukiri’

Katika kukiri kuna sheria nyingi baadhi yake ni:

Kukiri kwa muflisi-mfilisiwa au mzuiliwa katika mambo yanayohusu mali haimlazimu kwa sababu yeye tayari ameshakuwa mtuhumiwa kuwa atawahadaa wanaomdai, na yule wa pili mwenye kuzuiliwa – kukiri kwake kama kutatambuliwa anakuwa kama vile hakuzuiliwa kwa vile kukiri kunapingana na kuzuiliwa, kwa hiyo walichokikubali kitabaki katika dhamana zao na watakuja wakilipe baadaye kuondoka kipingamizi walichonacho.

Kukiri kwa mgonjwa mahututi, kwa anayestahiki kurithi hakukubaliwi isipokuwa kwa ushahidi, kwa sababu anatumia kupendelea, kwa mgonjwa mahututi anaposema mwanangu fulani nina kitu chake fulani. Hatokubaliwa kuhofia asiwe amependelea yeye kuliko watoto wake wengine, na dalili haya ni kauli ya Mtume.

“Hakuna wasia kwa mwenye kurithi.”

Hivyo neno la mgonjwa mwanangu fulani nina kitu chake fulani linafanana mno na kumuusia, na Mtume ﷺ anasema hakuna wasia kwa mwenye kurithi mpaka waidhinisha warithi (wengine) muda wa kuwa hakuna ushahidi unaothibitisha hayo aliyoyakubali kwa mrithi wake huyo, na hapo kukiri kwake kutakuwa sahihi.



Kinahusu Mtumwa

Mada ya Kwanza

Utumwa

1) Maana yake:

Utumwa ni umiliki na utumwa na *Raqyq*: Ni mtumwa aliyemilikiwa inatokana na neno ‘*Riqqah*’ kinyume cha uzito, kwa sababu mtumwa kwa bwana wake anakuwa mwepesi laini hawezi kuwa mzito juu ya bwana wake kwa utumwa alionao.

2) Hukumu yake:

Hukumu ya utumwa unaruhusiwa kwa kauli ya Allah Mtukufu:

وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ

“...na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia...” (4:36).

Na kauli ya Mtume ﷺ,

“Atayempiga kofi mtumwa wake au akampiga, kafara lake ni kumwacha huru.” (Muslim).

3) Historia na mwanzo wa Utumwa:

Umejulikana utumwa kati ya wanadamu tokea maelfu ya miaka iliyopita. Utumwa umepatikana katika mataifa ya kale ya ulimwengu, kama vile Wamisri, wachina, Wahindi, Wagiriki na Warumi. Na umetajwa katika vitabu vitakatifu kama vile Taurat na Injili, na Hajar mama wa Islali Ibni Ibrahim juu yao na juu ya Mtume ﷺ wetu ziteremke swala na salamu zilizo bora, alikuwa ni mjakazi aliyemtoa zawadi mfalme wa Misri kwa (Sara) mke wa Ibrahim, naye akamtoa zawadi kwa mumewe Ibrahim عليه السلام kamfanya mke akamzalia mtoto Ismail عليه السلام. Ama chanzo cha utumwa kinarudi katika sababu zifuatazo:

a) Vita, kundi la watu linapopigana na lengine, na likashinda, basi watoto na wanawake wa walioshindwa wanafanywa watumwa.

b) **Ufakiri:** Mara nyingi ufakiri umewafaya watu wauze watoto wao na kuwa watumwa kwa wengine.

c) **Kutumia nguvu** bara na bahari, kulikuwa na makundi makubwa ya watu yenye nguvu kutoka Ulaya yanakuja Afrika, na wanawachukuwa Waafrika kwa nguvu na kuwauza katika masoko ya utumwa Ulaya, kama walivyokuwa wanafanya maharamia wa baharini wa Ulaya walikuwa wanashambulia mashua zilizopita baharini na kuwachukua wasafiri walio humo, kama watawazidi nguvu wanakwenda kuwauza katika masoko ya watumwa huko Ulaya na wanakula thamani zao.

Uislamu ambayo ni dini ya Allah Mtukufu haukuziruhusu sababu hizi isipokuwa sababu moja tu nayo ni ile ya utumwa unaosababishwa na vita, kwa ajili ya kuhurumia ubinadamu kwa sababu mara nyingi wale wenye kushinda ushindi wao unawashauri kufanya uharibifu chini ya athari ya kupenda kuadhibu, kwa hiyo wanawauwa wanawake na watoto kwa ajili yakuwakomoa waume zao kwa hiyo Uislamu ukaruhusu kwa wafuasi wake katika kuwapa wanawake na watoto kuwa watumwa kwanza kuyalinda maisha yao, lakini pili ni utangulizi wa maisha yao bora na kuwa huru, ama askari wanaume Uislamu umempa kiongozi wa nchi uhuru wa kuteua kati ya kuwaachia bure bila ya kujifidia na kujifikia kwa mali au silaha au watu, amesema Allah Mtukufu:

فَإِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَخْنَتُمْهُمُ فَشُدُّوا الْوَتَانَ
فَأَمَّا مَنَّا بَعْدُ وَإِنَّمَا فِدَاءٌ حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا^٤

“...Basi mnapo wakuta walio kufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomoe, mpaka vita vipoe. Ndio hivyo...” (47: 4).

d) Ushirikiano Wake:

Hakuna tofauti kuba kati ya umma mbalimbali katika ushiriano wa waumwa na waungwana (mabwana) isipokuwa umma wa Kiislamu kwani mtumwa kwa hizo umma mbalimbali hakuwa zaidi ya chombo kilichodhalilishwa kwa huduma za kila kitu na kutumiwa katika kila mahitaji, ongezea anaachwa na njaa anapigwa na analazimishwa mzigo au kazi asizoziweza, bila ya sababu, kama ambavyo inawezekana kwa moto na kukawa viungo vyake kwa sababu walikuwa wanamulia mtumwa ni chombo kilicho na roho, ni kifaa chenye (roho na uhai).

Ama mtumwa katika Uislamu anapewa ushirikiano unaolingana na heshima ya binadamu, Waislamu wameharamisha na kupiga marufuku kumpiga mtumwa na kumuua kama ulivyoharamisha kumdhalilisha na kumtukana na ukaamuru afanyiwe wema na hisani na hizi hapa dalili zake zinatamka hivyo.

i) Kauli ya Allah Mtukufu:

وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ
وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ
لَا يُحِبُّ مَن كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٣٦﴾

“...Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wanao jifakhiri.” (4:36).

ii) Kauli ya Mtume Muhammad ﷺ kuhusu wao:

“Hao ni ndugu zenu na watumishi wenu Allah amewaweka mikononi mwenu, basi yule ndugu yake yuko mikononi mwake amlishe anachokula mwenyewe na amvishe anacho vaa mwenyewe na wala msiwalazimishe kinachowashinda na kama mtawalazimisha wasaidieni” (Muslim).

Na kauli yake Mtume ﷺ,

“Atayempiga kofi mtumwa wake au akampiga, kafara yake ni kumwacha huru.” (Muslim).

Mbali na haya Uislamu unalingania katika kuachwa huru watumwa na kuhamasisha hilo kwa haya yafuatayo:

(a) Uislamu umuamuru bwana kumwacha huru mtumwa aliye omba aachiwe huru, na kumsaidia kufika azma yake hiyo. Kwa kumpatia fungu la la mali, Allah Aliyetukuka Amesema:

مِمَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا وَءَاتُوهُمْ مِّنْ مَّالِ اللَّهِ
الَّذِي ءَاتَيْتُمْ وَلَا تُكْرَهُوا فَتَيْبَتِكُمْ عَلَى الْبِغَاءِ إِنْ أَرَدْنَ تَحَصُّنًا

“...Na wanao taka kuandikiwa uhuru katika wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki, basi waandikieni kama mkiona wema kwao. Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu aliyo kupeni. Wala msiwashurutishe vijakazi vyenu kufanya zina kwa ajili ya kutafuta pato la maisha ya dunia, ilhali wao wanataka kujihishimu...” (24: 33)

(c) Kuambukiza uhuru mpaka viungo vilivyosalia, kama atapewa uhuru baadhi ya watumwa. Muislamu kama ataiacha huru sehemu yake, kwa mtumwa washirika na wengine atalazimishwa aithamini hisa iliyosalia na atoe thamani hiyo kwa wenye hisa yao, na mtumwa wote atakuwa huru amesema Mtume Muhammad ﷺ,

“Mwenye kuacha huru hisa yake katika mtumwa na akawa ana miliki thamani ya mtumwa huyo atalazimishwa kutoa thamani iliyo salia na awape washirika wenzake hisa zao na mtumwa wakati wote atakuwa huru.” (Bukhari na Muslim).

(d) Kuruhusiwa mabwana kuwafanya wake wajakazi wawili iwezekane siku moja mjakazi huyo awe huru wanapopata kuzaa wajakazi hao na hao wanaowamiliki. Amesema Mtume ﷺ,

“Mjakazi yeyote aliyezaa na bwana wake basi huyo ni huru baada kufa bwana huyo.” (Ibnu Majah na Al-Hakim).

(e) Uislamu umeifanya kafara—la kosa-la mtu aliyempiga mtumwa wake ni kumwacha huru mtumwa huyo, amesema Mtume ﷺ.

“Atakae mpiga mtumwa wake ikiwa ni adhabu ya kosa ambalo hakulifanya au kampiga kofi basi kafara yake ni kumuacha huru mtumwa huyo.” (Imepokewa na Ahmad, Abu Dawud, Tirmidh na Ibn Majah).

(f) Anakua huru kwa kumilikiwa na ndugu yake maharim. Amesema Mtume Muhammad ﷺ.

“Atayemiliki ndugu aliye maharim basi – mmilikiwa yuko huru.” (Muslim).

Tanbihi:

Kama atasema msemaji kwa nini Uislamu Uislamu usilazimishe kuachwa huru watumwa?

Tunasema: Kuwa Uislamu umekuja ukakuta utumwa uko mikononi kwa watu, hivyo basi si sawa kwa sheria ya Allah Mtukufu yenye uadilifu ambayo imekuja ili kumlinda mwanadamu nafsi yake, heshima yake, mali yake na imani yake halafu sheria hiyo hiyo kulazimisha watu waache mali zao mara moja. Kadhalika haikuwa ni maslahi ya haraka haraka kwa watumwa wengi ambao ni wanawake na watoto na wanaume masikini wasiojiweza kuendesha maisha yao mara moja, kwa hali hiyo ilikuwa ni bora mwanzoni kuendelea kulishwa anachokula mwenye kuwamiliki na kuwavisha anachovaa na kumsaidia kazi itakayokuwa juu ya uwezo wake. Kwa wakati ule ilikuwa bora hivyo kwanza kisha kampeni ya kuwaacha huru ilikuja baadae kuwaacha huru.



Mada ya Pili

Hukumu za Utumwa

1) Kuacha Huru

a) Maana Yake: *Itki*

Ni kumucha huru mtumwa na kumkomboa na udhalili wa utumwa.

b) Hukumu Yake:

Hukumu ya kuacha huru mtumwa ni sunna, kwa kauli yake Allah Mtukufu:

فَكُّ رَقَبَةٍ ۖ أَوْ إِطْعَمٌ فِي يَوْمٍ ذِي مَسْغَبَةٍ

“Kumkomboa mtumwa; 14. Au kumlisha siku ya njaa.” (90:13)

Na kauli ya Mtume Muhammad ﷺ,

“Atayeiacha huru shingo ya mtumwa-mtumwa muumini Allah atamwacha huru na moto, kiungo cha mtumwa kwa kiungo cha muacha huru, hata mkono kwa mkono na mguu kwa mguu na tupu kwa tupu” (Bukhari na Muslim.)

c) Hekima Yake:

Hekima ya kuacha huru ni kumkomboa mwanadamu mwenye kulindwa na madhara ya utumwa ili ajimiliki mwenyewe na ajitawale na akamilike na aweze kufanya kazi kwa maslahi yake anavyotaka na kuamua yeye mwenyewe kwa khiyari yake.

d) Sheria Zake:

Sheria za kuacha huru mtumwa ni:

i) Kuacha huru unapatikana kwa tamko bayana la wazi kama kusema: wewe uko huru, au umeachwa huria au na kumpa uhuru, au imekuacha huru, pia

unapatikana kwa matamko yasiyo kuwa ya wazi lakini pamoja na kukusudia kuacha huru, kama vile njia yako imeiacha au sina utawala juu yako.

ii) Kunakubalika kuacha huru kama kutafanywa na mtu anayeruhusiwa kisheria kutumia mali yake, yaani baleghe mwenye akili timamu muangalifu, kama muacha huru atakuwa mwenda wazimu au dini ya baleghe na asiyekuwa muangalifu hakutakubaliwa kwa sababu hayo hataruhusiwa kutuma mali zao kisheria.

iii) Mtumwa kama atamilikiwa na watu wawili au zaidi mmoja wa washirika akaacha huru sehemu yake basi hisa ya waliosalia itathaminiwa na atatakiwa alipe kama uwezo huo anaona mtumwa wote atakuwa huru, kama uwezo huo hana basi itakuwa huru hisa yake tu. Kwa kauli ya Mtume Muhammad ﷺ.

“Atayeiacha huru hisa yake katika mtumwa wa ushirika na akawa anamiliki thamani ya mtumwa basi atatakiwa awalipe washirika wenzake hisa zao na mtumwa atakuwa huru, na kama uwezo hana basi itakuwa huru hisa yake tu.”

iv) Atayemwekea uhuru mtumwa kwa kupatikana masharti fulani, basi atakuwa huru kwa kupatikana masharti hayo, na lisipopakana hawi huru. Atayesema: wewe utakuwa huru kama Mke wangu atazaa mtoto basi atakuwa huru mara tu mke huyo atakapozaa.

v) Mwenye kumiliki mtumwa akamwacha huru baadhi ya mtumwa huyo basi atakuwa huru mtumwa wote kwani anaingia katika maana ya maelezo ya Mtume Muhammad ﷺ.

“Mwenye kuacha huru hisa yake katika mtumwa kutoka katika mali yake...” (Bukhari)

vi) Atayeacha huru mtumwa au watumwa wake akiwa katika ugonjwa ambao ndio ugonjwa aliofia basi watakuwa huru watumwa kwa kiwango cha theluthi ya mali atayoiacha, kwani tendo hilo linalofanana na wasia na wasia hauwi zaidi ya thuluthi).

(2) Tadbiri:

a) Maana Yake:

Tadbiri ni kuwekea upatikanaji wa uhuru baada ya kufa kwa bwana wake kama vile bwana akimwambia mtumwa wake: wewe utakuwa huru baada ya kufa kwangu, kwa hiyo bwana akifa mtumwa yuko huru.

b) Hukumu Yake:

Hukumu ya *Tadbiri* inakubalika isipokuwa kama bwana hana anachomiliki zaidi ya mtumwa huyo, kama alivyopokea Bukhari na Muslim kutoka kwa Jabir رضي الله عنه kwamba mtu fulani alimwacha huru mtumwa wake kwa *Tadbiri* akawa na mahitaji, Mtume عليه السلام Akasema:

“Nani atamnunua mtumwa huyo kwangu? Akamuuzua Nuam Ibni ‘Abdallah kwa Dirham mia nane akampa na akamwambia wewe una mahitaji zaidi.”

c) Hekima Yake:

Hekima ya *Tadbiri* ni huruma kwa Muislamu, kwani Muislamu anaweza akawa na mtumwa akataka kumwacha huru na akajikuta analazimika kuzipata huduma zake basi akasema nikifa uko huru, akajipatia thawabu za kuacha huru na kipindi cha uhai wake amefaidika na huduma zake.

d) Sheria Zake:

Sheria za *Tadbiri* ni:

i) *Tadbiri* inapatikana kwa tamko kama vile wewe uko baada yangu, au nimekuweka baada yangu au nikifa wewe uko huru, na mfano wa hayo..

ii) Aliyewekewa *Tadbiri* atakuwa huru katika theluthi ya mali, kama thamani yake sawa na theluthi atakuwa huru, kama thamani yake ni kubwa kuliko theluthi ya mali ya marehemu basi atakuwa huru kulingana na thamani ya theluthi ya mali iliyopo tuliyoieleza hapa ndio Madh-habi ya Jamhuri ya wanazuoni katika

masahaba na *taabiina* na maimamu kwa sababu tendo hili ni kujitolea kama ulivyo wasia: na wasia haukubaliki zaidi ya theluthi moja.

iii) *Tadbiri* kama atasiwekea sharti inakubalika, na sharti likikamilika atakuwa huru na lisipokamilika hawi huru, kwa kauli ya Mtume Muhammad ﷺ.

“*Waumini wako juu ya sharti zao.*” (Abu Dawud)

Kama bwana kwa mfano atasema: ikifa kwa ugonjwa huu basi wewe utakuwa huru, na akafa, amekuwa huru asipokufa hawi huru.

iv) Ina ruhusiwa kumuuzwa kwa sababu ya deni au haja. Kwa sababu Mtume ﷺ:

“*Amemuuza mtumwa wa mtu fulani alimuwekea Tadbiri alipomuona na mahitaji ya thamani ya mtumwa huyo*” (Bukhari na Muslim).

Na mama Aisha amemuuza mtumwa wake aliyemuwekea *Tadbiri* alipomroga.

v) Kama atawekwa *Tadbiri* mja mzito basi mtoto wake sawa na mwenyewe atakuwa huru na mama yake kwa kufa bwana anayemiliki huyu mama kwa kauli ya ‘Umar na Jabir رضي الله عنه: Mtoto wa aliyewekwa *Tadbiri* (sawa na mama yake) amezitaja mwenye almughni.

vi) Bwana anaweza kumingilia mudabbara-aliyewekewa *Tadbiri*—kwa sababu bado yuko katika miliki yake, na Allah Mtukufu Anasema:

إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٣٠﴾

“*Isipo kuwa kwa wake zao, au iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi.*” (70:30)

Na ruhusa ya kumingilia imepokewa kutoka kwa maswahaba wengi رضي الله عنه.

Aliyeweka *Tadbiri* kama atamuua bwana wake *Tadbiri* yake imebatilika, na hawi huru ili kumfanyia kinyume na lengo lake, pia isije ikafikia waliowekewa *Tadbiri* wanaharakisha vifo vya waliowawekea *Tadbiri*.

3) *al Mukaatab*, Muandikiwa

a) Maana Yake:

Muandikiwa ni mtumwa anayepata uhuru kwa bwana wake kwa mali atayoona mtumwa huyo kumpa bwana huyo kwa awamu maalum, na atamuandikia risiti maalumu, anapokamilisha awamu zake katika kipindi alichowekewa na atakuwa huru.

b) Hukumu ya Kuandika:

Kuandikia ni Sunna kwa kauli ya Allah Mtukufu.

وَالَّذِينَ يَبْتَغُونَ الْكِتَابَ مِمَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ فِيهِمْ خَيْرًا
وَأَتَوْهُمْ مِنْ مَالِ اللَّهِ الَّذِي آتَيْنَاكُمْ ؕ وَلَا تَكْرَهُوا فَتَيْبَتِكُمْ عَلَى الْبِغَاءِ إِنْ
أَرَدْنَ تَخَصُّصًا

“...Na wanao taka kuandikiwa uhuru katika wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki, basi waandikieni kama mkiona wema kwao. Na wapeni katika mali ya Mwenyezi Mungu aliyo kupeni. Wala msiwashurutishe vijakazi vyenu kufanya zina kwa ajili ya kutafuta pato la maisha ya dunia, ilhali wao wanataka kujihishimu...”(24:33)

Na kauli ya Mtume Muhammad ﷺ

“Atayemsaidia mwenye madeni au mpiganaji au muandikiwa katika kwa kuiekelea kulipa hisa zake Allah atampatia kivuli Siku isiyokuwa na kivuli ila chake.” (Ahmad na Hakim).

c) Sheria Zake:

Muandikiwa ana Sheria nyingi nazo ni:

i) Muandikiwa atakuwa huru anapotoa fungu la mwisho katika awamu zake.

ii) Muandikiwa bado ni mtumwa na yatamuhusu yote yanayomuhusu mtumwa kwa muda wa kubakia dirham moja kwa kauli ya maswahaba wengi, na kwa mapokezi ya 'Amru bin Shu'ayb kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake kuwa Mtume Muhammad ﷺ amesema:

"Muandikiwa ni mtumwa kwa muda wa kusalia Dirham." (Abu Daud na Baihaqi)

iii) Bwana analazimika amsaidie Muandikiwa wake. Kufikia uhuru kwa kumpa kitu fulani katika mali kama vile robo ya makubaliano au mfano wa hao, ukiwa ni mchango wake bwana katika kufiia uhuru wake kwa kauli ya Allah Mtukufu.

"Nawapeni baadhi ya mali ya Allah Mtukufu ambayo amewapeni."

Anaruhusiwa kumkabidhi fedha taslimu au kwa kumpunguzia kiwango alichokitaka kwa muandikiwa huyo.

iv) Endapo muandikiwa ataharakisha kwa mfano akitoa fungu lote mara moja au mbili bwana analazimika kukubali, isipokuwa kama kufanya hivyo kutasababisha dhara kwa bwana, haitamlazimu kwake kukubali, na haya yamepokewa kutoka kwa 'Umar' رضي الله عنه

v) Kama bwana atafariki kabla mtumwa hajamaliza alichotakiwa kutowa, basi ataendelea kuwa muandikiwa na kilichosalia atakikabidhi kwa warithi wa marehemu huyo, na kama atashindwa kutekeleza basi atarudi kuwa Mtumwa na atakuwa miliki ya warithi wa bwana wake.

vi) Bwana hamzuii Muandikiwa wake kusafiri na kufanya kazi, bali anaweza kuzuia kuoa au kuolewa kwa kauli ya Mtume Muhammad ﷺ.

“Mtumwa yeyote atakayeo bila ya ruhusa ya bwana wake huyo ni mzinifu.” (Ahmad).

vii) Bwana haruhusiwi kumingilia Muandikiwa wake, kwa sababu kumuandikia kumemzuwua kumtumia na kufaidika nae, na kuingiliani ni jumla ya manufaa yanayopatikana kwa kumwandikia. Na hii ndio Rai ya Jamhuri ya Maimamu رضي الله عنه

viii) Muandikiwa kama atashindwa kutekeleza fungu katika mafungu aliyotakiwa na muda wa fungu lingine ukafika na ameshindwa kutekeleza alichotakiwa, inafaa kwa bwana kumshindisha na kumrejsha kwenye utumwa kama alivyokuwa, kwa kauli ya Ali رضي الله عنه,

‘Harejeshwi muandikiwa katika utumwa mpaka zipite awamu mbili bila ya kuzilipa’.

ix) Mtoto wa muandikiwa anakuwa huru na mzazi wake kama atakamilisha alichotakiwa na akawa huru kama atashindwa basi atarudi kwenye utumwa pamoja na mtoto wake ni sawa awe yule aliyekuwa tumboni wakati ana andikiwa au baada ya kuandikiwa na haya ndiyo madh-habi ya jamhuri.

x) Kama muandikiwa atashindwa kuelekea na mkononi mwake mna mali basi mali hiyo ni ya bwana sawa na yeye isipokuwa ama amepata kutoka katika mfuko wa zaka analazimika awape mafaqiri na masikini kwani wao wana haki zaidi ya fungu hilo kuliko bwana tajiri.

4) **‘Ummul-Waladi’:**

a) Maana Yake:

‘Ummul Waladi’ ni mjakazi anayeingiliwa na bwana wake kwa ujakazi na akapata mtoto kwa bwana wake huyo mwanamme au mwanamke (Huyo mtoto).

b) Hukumu Ya Mjakazi Kufanywa Mke

Bwana anaruhusiwa mjakazi wake kumfanya mke na kama atapata naye mtoto huyo mjakazi atakuwa ‘Ummul Waladi’ –mama moto kwa kauli ya Allah Mtukufu.

إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٧٠﴾

“Isipo kuwa kwa wake zao, au iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi.” (70:30)

Mtume Muhammad ﷺ alimfanya mke Mariya Al-Qibtwiyyah akamzaa Ibrahim, Mtume ﷺ akasema:

“Amemwacha huru mwanawe.” Amepokea Ibnu Majah Daruqutni)

kama alivyokuwa Hajar–mama wa Ismail ni mjakazi wa Ibrahim aliyefanywa mke akamzalia Ismail عليه السلام

c) Hekima ya Mjakazi Kumfanya Mke:

Miongoni mwa hekima ya kufanya mjakazi mke:

- i) Kumuhurumia mjakazi kwa kumtekelezea mahitaji yake ya matamano.
- ii) Kumuandaa awe mama wa mtoto na akawa huru kwa kufa kwa bwana wake.
- iii) Kuingiliwa na bwana wake kunaweza kukampatia kupewa umuhimu na bwana wake kwa hiyo kumfanya awe msafi zaidi na kivazi kizuri zaidi, na kitanda safi zaidi na chakula safi zaidi na mengineyo.
- iv) Kumuhurumia Muislamu kwa sababu Muislamu anaweza kushinda kupata mahari ya mwanamke muungwana akaruhusiwa kumuingilia mjakazi ili kufanyia wepesi na huruma.

d) Sheria zaUmmul-Waladi

Ummul-Waladi ana hukumu nyingi nazo ni:-

- i) Ummul Waladi: sawa na mjakazi katika mambo yote kama vile huduma, kuingiliwa kuachwa huru mipaka ya uchi na kuuozesha isipokuwa hajuzu kumuuzua

kwa katazo lake Mtume Muhammad ﷺ kuwauza mama watoto, na kwa sababu kuuza kunapingana na uhuru wake unaosubiriwa kwa kufa bwana wake.

ii) Mama mtoto atakuwa huru kwa kufariki bwana wake, kwa kauli ya Mtume ﷺ mjakazi yeyote aliyezaa na bwana wake basi yuko huru kwa kufa bwana wake (huyo).

iii) Mjakazi atakuwa mama mtoto hata kama mtoto huyo alitoka tumboni mwa mama yake hali amekufa ilimradi amekamilika umbile, kwa kauli ya ‘Umar رضي الله عنه’ mjakazi akizaa na bwana wake yuko huru hata kama ikitoka mimba yenyewe.

iv) Hakuna totauti katika kuwa huru *Ummul-Waladi* kati ya mjakazi Muislamu na asiye Muislamu, atakuwa huru tu, isipokuwa baadhi ya wanazuoni anasema kafiri hawi huru, lakini kauli zilizokuja hazitenganishi kafiri na Muislamu na hiyo ndiyo rai ya Jamhuri.

v) Mjakazi anapokuwa huru kwa kufa bwana wake mali alizo nazo zitakuwa za warithi wa bwana kwa sababu *Ummul Waladi* kabla hajafa bwana wake alikuwa mtumwa, na pato la mjakazi ni la bwana wake.

vi) Bwana wake akifa atajitakasa kwa hedhi moja kwa vile ametoka katika umiliki kwa kuachwa huru.

5) ‘Alwalaau’:

a) Maana Yake:

Al-Walaau ni nguvu – uaswaba-sababu yake ni wema kwa kuacha huru.

b) Hukumu Yake

Walaau ni jambo la kisheria kwa kauli ya Allah Aliye Tukuka

“Ni ndugu zenu katika dini na ni waachwa huru wenu”

Na kauli yake Mtume ﷺ

“Walaa ni wa mwenye kuacha huru’

Na kauli ya Mtume ﷺ,

“Walaau ni mnofu kama mnofu wa kuzaliwa hauuzwi wala hautolewi hiba” (al Hakim na al Baihaqi)

c) Sheria Zake:

Sheria za Walaa-u:

i) Walaa-u ni haki ya muacha huru kwa sura yoyote ile katika sura za kuacha huru, ni sawa iwe kwa mukataba (kumuandika) ajikombee au kwa Tadbiri au kwa namna nyengine.

ii) Walaa-u hauuzwi wala hautolewi hiba kwa sababu walaa-u sawa na undugu na undugu hauuzwi wala kutolewa hiba kwa hali yoyote ile, amesema Mtume ﷺ. (Walaa-u ni mnofu kama mnofu wa kuzaliwa hauuzwi wala hautolewi hiba).

iii) Harithi kwa *walaa-u* isipokuwa *Almuutiq* (muacha huru), awe ni mwanamume au mwanamke, au aswaba wa muacha huru wanamume tu ila ya wanawake, kama ilivyofafanuliwa katika elimu ya mirathi na Allah ndiye anayejua, na njia yake ndio nyoofu na ya usawa na Allah ateremshe rehema juu ya Mtume wetu Muhammad ﷺ na aali zake na swahaba zake.

iv) Hana haki ya kupata mirathi kwa *walaa-u* isipokuwa aliyeacha huru ni sawa awe mwana mume au mwanamke au atapata mirathi aswaba wamuacha huru aliyetajwa hapo nyuma lakini asiwe mwanamke kama ilivyofafanuliwa katika somo la mirathi Na Allah Aliye Tukuka ndiye anayejua zaidi na njia yake ndiyo nyoofu na ya usawa na Allah ateremshe rehema juu ya Mtume wetu Muhammad ﷺ na aali zake na swahaba zake.



Maana ya Baadhi ya Maneno Yaliyotumika:

- Tamaathuli:** Ni namba mbili zilizofanana kama 2, 2, au 3, 3 na kadhalika
- Tadaakhul:** Ni namba mbili zilizotofautiana moja kubwa na nyingine ndogo na namba kubwa ina kubali kugawika kwa ndogo kama vile 2, 4 au 4, 8 na kadhalika.
- Tawafuq:** Namba mbili zilizotofautiana moja kubwa na nyingine na hakuna namba katika hizo inayokubali kugawa na pia haziafikiani kugawa kwa namba yeyote ile nje ya hizo, kama vile 3, 5 au 5, 7 na kadhalika
- Muwafaka:** Ni jawabu la namba tawafuq kwa mfano 6, 4: $6/2=3$ kwa hiyo (3) ni muwafaka ya (6) au $4/2=2$ kwa hiyo (2) ni muwafaka ya (4)
- Fardhi Kifaya:** Ni wajibu ambao kama utatekelezwa na baadhi ya Waislamu ijapokuwa ni Muislamu mmoja kama vile kuosha maiti au kumvisha sanda au kumswalia n.k. wajibu utaanguka (utakuwa umetekelezeka) kwa wote.
- Aswaba:** Ni mtu mwenye haki ya kurithi lakini hana fungu maalumu kama vile $\frac{1}{2}$ au $\frac{1}{4}$ na kadhalika bali anachukuwa kilichosalia baada ya kuchukua wenye hisa na kama hakuna mwenye hisa anachukuwa mali yote na kama hakuna kilichosalia basi hana kitu.
- Sahih:** Mwisho wa hadithi linapokuja kauli “*Sahih*” maana ya yake ni hadithi iliyopokewa na Muislamu mwadilifu mwenye udhibiti kamili na mnyororo wa wapokezi umeungana naye ameipokea kutokea kwa mtu mwenye sifa kama zake, haina ila wala *shudhudh*).

